# HATUA TATU ZA MAISHA YA KIROHO

UTANGULIZI WA UZIMA WA MBINGUNI

*Kwa kibali cha Askofu wa Morogoro*

*+ Telesphor Mkude*

*Morogoro, 29-6-2006*

*Inaruhusiwa kutumia na kunakili kwa njia yoyote ile*

*sehemu yoyote ya kitabu hiki,*

*mradi itajwe imechukuliwa wapi*

*na isiwe kwa lengo la biashara.*

*Toleo pepe la kitabu hiki na la vinginevyo*

*linapatikana katika tovuti*

*ya Utawa wa Ndugu Wadogo wa Afrika:*

*www.unwa.tk*

**R. GARRIGOU-LAGRANGE, O.P.**

# HATUA TATU

# ZA MAISHA YA KIROHO

UTANGULIZI

WA UZIMA WA MBINGUNI

*(TAFSIRI FUPI)*

**Ndugu Wadogo wa Afrika - S.L.P. 6083 - Morogoro**

***Barua pepe: unwa@unwa.tk***

**HATUA TATU ZA MAISHA YA KIROHO**

UTANGULIZI WA UZIMA WA MBINGUNI

Tafsiri hii fupi imeandaliwa na nd. Rikardo Maria, UNWA

Toleo asili ni:
*Les Trois Ages de la Vie Intérieure, Prélude de Celle du Ciel,*
Les Editions du Cerf, Paris 1939

## YALIYOMO

Utangulizi .......................................................................................................... 7

1. Chemchemi na lengo la maisha ya Kiroho....................................................11
1.1. Uzima wa neema, mwanzo wa uzima wa milele....................................................................11
1.2. Maisha ya Kiroho, maongezi ya ndani na Mungu ....................................................................16
1.3. Muundo wa Kiroho....................................................................................................................18
1.3.1 Maisha ya kimaumbile na yanayopita maumbile...................................18
1.3.2. Maadili ya Kimungu.............................................................................20
1.3.3. Maadili ya kiutu ..................................................................................22
1.3.4. Vipaji saba vya Roho Mtakatifu ..........................................................24
1.3.5. Neema za msaada na aina zake ........................................................28
1.4. Uwemo wa Utatu Mtakatifu ndani mwetu, chemchemi isiyoumbwa wa maisha ya Kiroho .32
1.5. Kristo Mkombozi anavyoathiri mwili wake wa fumbo ............................................................36
1.6. Athari ya Maria mshenga.........................................................................................................40
1.7. Ustawi wa uzima wa neema kwa njia ya stahili, sala na sacramenti......................................44
1.8. Ukamilifu wa Kikristo ni nini hasa? ..........................................................................................48
1.9. Ukuu wa ukamilifu wa Kikristo na heri nane ...........................................................................55
1.10. Ukamilifu na ushujaa .............................................................................................................59
1.11. Ukamilifu wa Kikristo na matakaso ya Kimungu.....................................................................62
1.12. Ukamilifu na amri ya kumpenda Mungu ................................................................................67
1.13. Ukamilifu na mashauri ya Kiinjili.............................................................................................70
1.14. Wajibu wa pekee wa mapadri na watawa wa kulenga ukamilifu...........................................73
1.15. Hatua tatu za maisha ya Kiroho kadiri ya mababu na walimu wakuu ...................................78
1.16. Somo la Kimungu ....................................................................................................................85
1.17. Uongozi wa Kiroho...................................................................................................................89
2. Utakaso wa wanaoanza...............................................................................................93
2.1. Hatua ya Kiroho ya wanaoanza ...............................................................................................93
2.2. Fikra za kidunia na ufishaji kadiri ya Injili.................................................................................96
2.3. Ufishaji kadiri ya mtume Paulo na sababu zinazofanya uwe wa lazima ...........................99
2.4. Dhambi za kuepwa: mizizi yake na matokeo yake...............................................................103
2.5. Kilema tawala, mdudu anayekula ndani kwa ndani ..................................................108
2.6. Maono ya kuratibiwa..............................................................................................................112
2.7. Kujitakasa upande wa hisi......................................................................................................114
2.8. Kujitakasa upande wa ubunifu na kumbukumbu....................................................................117
2.9. Kujitakasa upande wa akili ....................................................................................................120
2.10. Kujitakasa upande wa utashi ...............................................................................................124
2.11. Kupona kiburi .........................................................................................................................128
2.12. Kupona uzembe .....................................................................................................................132
2.13. Sakramenti ya kitubio ...........................................................................................................135
2.14. Kushiriki misa, chemchemi ya utakatifu................................................................................139
2.15. Komunyo takatifu .................................................................................................................142
2.16. Sala ya kuomba ...................................................................................................................147
2.17. Sala ya Kanisa......................................................................................................................150
2.18. Sala ya moyo ya wanaoanza inavyozidi kuwa sahili.............................................................152
2.19. Kufikia maisha ya sala na kudumu ndani yake ....................................................................156
2.20. Wachelewaji..........................................................................................................................159
3. Mwanga wa wanaoendelea ........................................................................... 163
3.1. Lugha ya walimu wa Kiroho na ile ya wanateolojia...............................................................163
3.2. Kuingia hatua ya mwanga......................................................................................................167
3.3. Uongofu wa pili kadiri ya walimu wengine ............................................................................170
3.4. Kutakaswa hisi na kuingia hatua ya mwanga.........................................................................174
3.5. La kufanya katika usiku wa hisi .............................................................................................178
3.6. Sifa kuu za hatua ya wanaoendelea ......................................................................................182
3.7. Jengo la Kiroho la wanaoendelea ..........................................................................................183
3.8. Busara na maisha ya Kiroho .................................................................................................186
3.9. Haki, aina zake na kuunda utashi ..........................................................................................189
3.10. Subira na upole....................................................................................................................191
3.11. Usafi wa moyo, thamani na matunda yake ..........................................................................194
3.12. Unyenyekevu wa wanaoendelea..........................................................................................197
3.13. Unyenyekevu wa Neno aliyefanyika mwili na ule wa kwetu unavyotakiwa kuwa............201
3.14. Roho ya ufukara ..................................................................................................................204
3.15. Ukuu wa utiifu.......................................................................................................................207
3.16. Usahili na unyofu .................................................................................................................210
3.17. Roho ya imani na ustawi wake.............................................................................................213
3.18. Tumaini kwa Mungu na hakika yake.....................................................................................217
3.19. Upendo wa kulingana na matakwa ya Mungu ......................................................................221
3.20. Upendo wa kidugu, mng'ao wa ule wa Mungu......................................................................225
3.21. Ari kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa watu ...........................................................230
3.22. Usikivu kwa Roho Mtakatifu .................................................................................................233
3.23. Upambanuzi wa roho ...........................................................................................................239
3.24. Sadaka ya misa na wanaoendelea.......................................................................................242
3.25. Komunyo ya wanaoendelea.................................................................................................245
3.26. Heshima ya wanaoendelea kwa bikira Maria .......................................................................248
3.27. Kitabu cha "Kumfuasa Yesu Kristo" kinawaelekeza wote njia ya mafumbo ........................251

3.28. Sala ya kumiminiwa ....................................................................................................253
3.29. Uzushi kuhusu sala ya kumiminiwa na kuhusu upendo safi ..........................................256
3.30. Ngazi za sala ya wanaoendelea .......................................................................259
3.31. Masuala yanayohusu sala ya kumiminiwa ......................................................................261
3.32. Yaliyo mapya katika sala ya kumiminiwa ........................................................................266
3.33. Ulinganifu na tofauti kati ya watakatifu Teresa wa Yesu na Yohane wa Msalaba ..........268
**4. Muungano wa waliokamilika ........................................................ 271**
4.1. Kuingia hatua ya muungano kupitia usiku wa roho ..........................................................271
4.1.1. Haja ya kutakaswa roho na utangulizi wa hatua ya muungano .......... 271
4.1.2. Ufafanuzi wa utakaso wa Kimungu wa roho ..................................... 275
4.1.3. Kinachosababisha roho kutakaswa .................................................. 278
4.1.4. Giza la mwanga mkali ...................................................................... 281
4.1.5. Maelekezo kwa usiku wa roho ........................................................... 284
4.1.6. Matokeo ya roho kutakaswa hasa upande wa maadili ya Kimungu .... 287
4.1.7. Hatua ya waliokamilika: muungano wao na Mungu ........................... 296
4.1.8. Aina mojawapo ya maisha makamilifu: njia ya utoto wa Kiroho ......... 301
4.2. Ushujaa wa maadili ..........................................................................................................304
4.2.1. Ushujaa wa maadili kwa jumla ........................................................... 304
4.2.2. Imani ya kishujaa inayozama katika mafumbo .................................. 307
4.2.3. Tumaini la kishujaa na kujiachilia kwa Mungu ................................... 309
4.2.4. Upendo wa kishujaa ......................................................................... 312
4.2.5. Ushujaa wa maadili ya kiutu .............................................................. 314
4.2.6. Upendo kwa Msulubiwa na kwa Maria katika hatua ya muungano ..... 318
4.3. Namna na ngazi za hatua ya muungano ………………………………………………320
4.3.1. Maisha kamili ya kitume na sala ya kumiminiwa ................................ 321
4.3.2. Maisha ya malipizi ............................................................................. 323
4.3.3. Roho Mtakatifu anavyomuathiri aliyekamilika .................................... 327
4.3.4. Muungano mkavu na ule wa kutoka nje ya nafsi ..................................... 330
4.3.5. Muungano unaotugeuza, utangulizi wa ule wa mbinguni ............................ 333
**5. Neema za pekee ........................................................................................ 341**
5.1. Karama ..........................................................................................................................341
5.2. Mafunuo na njozi ..........................................................................................................342
5.3. Maneno na miguso ya Kimungu ......................................................................................345
5.4. Madonda matakatifu na kudanganyika ............................................................................346
5.5. Tofauti kati ya matukio hayo ya Kimungu na yale yatokanayo na ugonjwa .....................349
5.6. Matukio ya kishetani .......................................................................................................351
**Hatima ....................................................................................................... 355**
**Namna ya kutumia kitabu hiki kwa mafungo matatu ya siku sita sita..........360**

# UTANGULIZI

## KITU KILICHO MUHIMU PEKE YAKE

Mtu akiacha kuongea na wenzake, mara anaanza kuwaza yanayomvutia zaidi. Mawazo hayo yanatofautiana hasa kadiri ya umri na uadilifu wa watu. Kwa mtu anayelenga ukweli na wema yanaelekea kugeuka maongezi na Mungu, naye mwenyewe, badala ya kujipendea katika yote (yaani kujifanya lengo la yote, ajue asijue) anamlenga Mungu katika kila jambo akimpenda na kuwapenda watu kwa ajili yake. Ndiyo maisha ya Kiroho, jambo bora na la lazima kuliko elimu, sanaa, fasihi, siasa na mengineyo: wale wasio na maisha ya Kiroho wakijihusisha na mambo hayo wanaonekana kutafuta humo ukweli na wema, lakini utafiti wao unaathiriwa na umimi kiasi kwamba tunapaswa kujiuliza kama utazaa matunda kwa uzima wa milele. Wengi wao hawainuki juu ya utendaji wa kibinadamu tu na wa njenje, wala hawaishi kwa jambo lililo bora kuliko wao, yaani kwa Mungu.

Maisha ya Kiroho, yaani kuishi na Mungu, ndiyo *kitu pekee cha lazima* kwa sababu kwa njia yake tu tunaelekea lengo letu kuu. Tusiutenganishe *wokovu* na safari ya utakatifu iliyo njia ya wokovu. *Mbinguni kutakuwa na watakatifu tu,* wawe wameingia mara baada ya kufa, au wawe wamehitaji kutakaswa toharani. Hakuna anayeingia mbinguni akiwa na doa lolote. Ili aweze kufurahia daima uso wa Mungu, yaani kumjua na kumpenda kama mwenyewe anavyojijua na kujipenda, ni lazima hatia yoyote hata ndogo iwe imefutwa, na adhabu aliyostahili iwe imetimizwa au kuondolewa. “Atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?” (Math 16:26). Ikiwa tuko tayari kupoteza vitu vingi ili kuokoa mwili, ambao kwa vyovyote utakuja kufa, kwa nini tusiwe tayari kupoteza vyote ili kuokoa roho inayotakiwa kuishi milele? Je, binadamu hapaswi kuipenda roho kuliko mwili wake?

## SUALA LA MAISHA YA KIROHO SIKU HIZI

Hayo tuliyoyasema ni ya kweli nyakati zote, lakini siku hizi yanahitaji kufikiriwa zaidi, kwa sababu kuna fujo: wengi wamejitenga na Mungu, wakijitahidi kupanga mbali naye maisha ya binafsi na ya jamii. Matatizo makuu yaliyowapata daima binadamu sasa yana sura mpya ya kutisha. Kwa kuwa Mungu ni mwanzo na mwisho wa yote, mtu akitaka kutenda bila yake anajikuta vilindini mwa unyonge mbaya kuliko utovu wa vyote. Anakuja kukabiliwa na rundo la masuala ambayo hayana jibu lolote asiporudia suala la msingi la fungamano na Mungu, akitambua kuwa yote yanadai azingatie dini kuliko chochote, asiweze kuepa kusimama ama upande wake ama dhidi yake.

Mtu asipotimiza wajibu wake kwa Mungu, aliye muumba na lengo lake kuu, *uzito wa maisha unasogea* upande mwingine. Lakini baada ya muda analazimika kutambua yote yamevurugika. Anajikuta akiabudu vingine, k.mf. sayansi au haki ya kijamii au kipeo chochote cha kibinadamu. Siku hizi bingwa anaabudu taratibu za sayansi na kuzijali kuliko ukweli wenyewe. Angefanya bidii hizohizo katika maisha ya Kiroho, angefikia mapema utakatifu. Kumbe hiyo ibada ya sayansi lengo lake ni utukufu wa mtu badala ya upendo wa Mungu. Vilevile siasa mara nyingi inajidanganya kuboresha maisha ya binadamu kwa kukataa haki za Mungu. Historia ya karne XX imetuonyesha hilo waziwazi.

*Mali haiwezi kuwa yote ya wengi kwa wakati mmoja:* ndiyo sababu watu na mataifa wanashindana, lengo kuu likiwekwa katika mali. Kumbe *mema ya Kiroho yanaweza kuwa yote ya wote kwa wakati mmoja:* tunaweza kuchanga ukweli uleule, uadilifu uleule na Mungu yuleyule bila ya kunyang'anyana. “Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa” (Math 6:33). Kukataa fundisho hilo ni kujitakia maangamizi: "Bwana asipoijenga nyumba waijengao wafanya kazi bure. Bwana asipoulinda mji yeye aulindaye akesha bure" (Zab 127:1).

Mtu akijali sayansi au siasa kuliko dini, na akijitafutia utukufu badala ya kumtafutia Mungu, maisha yatamfundisha mapema kuwa ameshika njia isiyofika mahali. “Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu, na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya” (Math 12:30).

Lakini dini haiwezi kuwa jibu *halisi* la masuala makuu ya leo isiposhikwa kwa dhati. Maisha ya Kiroho yanatakiwa yawe kweli muungano na Mungu ili dini idumu kuwa juu ya sayansi na siasa.

## LENGO NA TARATIBU

Lengo letu ni kuwaalika watu kwenye muungano na Mungu, wakiepa hatari mbili. Ya kwanza ni kwamba leo kutofautisha fani kumezidi hata kufanya wengi wakose mitazamo mipana inayohitajika ili kupima kwa busara mambo yoyote katika uhusiano na mengine. Basi, katika maisha ya Kiroho pia kuzingatia

madogomadogo kusitusahaulishe jumla ya yote, la sivyo tutasogea mbali na hekima ya Kikristo. Ya pili ni kwamba vitabu vingi vya dini na vya ibada vinakosa msingi imara katika imani na kurahisisha mno mafundisho ya Kiroho.

Maisha ya Kiroho ni *tawi la teolojia* linalohusu utekelezaji wake katika kuongoza watu waungane kwa dhati na Mungu, likifafanua muungano huo ni nini na njia za kuufikia ni zipi. Hivyo linafafanua taratibu za uzima wa neema kwa misingi ya teolojia likiilinganisha na mang'amuzi ya watakatifu. Linahitaji kuchambua mang'amuzi hayo kitaalamu, likibainisha taratibu zake kadiri ya saikolojia (k.mf. ukavu unaotakasa unavyohusiana na muungano na Mungu). Somo hilo ni la kiteolojia uchambuzi huo unapotegemea mafundisho ya imani pia. Ikiwa *elimunafsia* ni ya lazima kwa maadilidini, *ni ya lazima zaidi kwa maisha ya Kiroho* ambayo yanachunguza ndani ya mtu hatua zake hadi muungano kamili.

Katika ngazi ya chini, maadilidini yanatakiwa kuzungumzia sio tu madhambi ambayo tuyaepe, bali pia maadili ambayo tuwe nayo na usikivu katika kumfuata Roho Mtakatifu. Maisha ya Kiroho hayana upana wa maadilidini, lakini ni tawi la juu yake kwa jinsi linavyolenga kufikisha hadi *muungano wa dhati na Mungu:* kwa njia yake teolojia inarudi ilipoanzia na *kudumisha umoja wake.* Kwa hiyo linatakiwa kufuata *mwanga wa ufunuo* wa Kimungu uliomo katika Maandiko na Mapokeo, ambao peke yake unaweza kutujulisha uzima wa Kimungu na muungano na Mungu ambao unapita maumbile. Maisha ya Kiroho yanatumia mawazo ya maadilidini, lakini kuhusiana zaidi na ustawi wa uzima wa Kimungu rohoni. Utekelezaji wake, ambao ndio lengo la maisha ya Kiroho kupitia uongozi wa mtu mmojammoja, una pande mbili: juhudi na mafumbo. Upande wa *juhudi* maisha ya Kiroho yanazungumzia hasa namna ya kufisha vilema na kutekeleza maadili. Upande wa *mafumbo* yanazungumzia hasa usikivu kwa Roho Mtakatifu, neema ya kuzama katika mafumbo ya imani, na muungano unaotokana na neema hiyo, halafu karama ambazo pengine zinaongozana nayo.

Hapa tutaeleza yaliyo ya lazima tu, kwa kukwepa aina mbili za upotovu ambazo ni rahisi zitupate: moja kwa kuzingatia mafundisho ya imani na kupuuzia mang'amuzi, nyingine kwa kuzingatia mang'amuzi na kupuuzia mafundisho ya imani. Tunapaswa kuzungumzia maisha ya Kiroho kwa mwanga wa teolojia kuhusu neema inayotia utakatifu, maadili ya kumiminiwa na vipaji saba; la sivyo tungekusanya tu dalili za hali za Kiroho za juu, pasipo kuelewa kanuni za msingi za *ustawi wa uzima wa Kimungu* ambao haung'amuliki kwa kuwa si wa kimaumbile. Pia tungetia maanani mno uhaba wa watu wanaofikia muungano wa ndani na Mungu: hapo tungedhani walio wengi hawaitwi hata kwa mbali na kwa jumla wafikie hatua hiyo; tungesahau maneno ya Bwana yanayokumbushwa na walimu wa Kiroho kuhusu suala hilo: "Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache" (Math 22:14). Upande wa pili tunapaswa kuzingatia maelezo ya watakatifu kuhusu hatua mbalimbali za maisha ya Kiroho, tukiyaangaza kwa imani ili kutambua katika mang'amuzi yao yapi ni *ya pekee tu* na yapi ni *ya juu, lakini yanakusudiwa kuwa ya kawaida.* Upande huo hatari nyingine ni kudhani neema ya kuzama katika sala ni ya wengi, tukiichanganya na sala sahili ya mapendo ambayo ni utangulizi wake tu. Kufuatana na aina hizo mbili za upotovu, kuna makosa mawili ya kuepwa katika kuongoza watu: kuwaachisha njia ya juhudi mapema mno au baadaye mno.

Basi, tunapaswa kuchimba ukamilifu wa Kikristo ili kuona wazi lengo ambalo Mwokozi amewawekea watu tusilipunguze. Halafu kuchambua mang'amuzi ili tutofautishe yaliyo ya lazima na yaliyo ya ziada. Hatimaye kujumlisha hayo mawili ili kuona *yaliyo ya lazima au ya kufaa na ya kutamaniwa* kusudi tuufikie ukamilifu, na yale ambayo ni *ya pekee tu* na hayahitajiki kufikia utakatifu mkuu.

Kutokana na hatari hizo mbalimbali, kusoma maisha ya Kiroho kunadai ujuzi wa teolojia (hasa juu ya neema, maadili ya kumiminiwa, na vipaji vya Roho Mtakatifu kuhusiana na mafumbo makuu ya Utatu, umwilisho, ukombozi na ekaristi) pamoja na ujuzi wa walimu wa Kiroho, hasa wale ambao Kanisa limewataja kuwa viongozi katika masuala hayo.

### UPANDE WA JUHUDI NA ULE WA MAFUMBO: TOFAUTI NA UHUSIANO

Kadiri ya watakatifu Thoma wa Akwino, Yohane wa Msalaba na Fransisko wa Sales *upande wa juhudi* maisha ya Kiroho yanazungumzia hatua ya *utakaso* wa wanaoanza; hao, wakijua kwamba hawatakiwi kubaki nyuma na kupooza, wanajitahidi kutekeleza maadili, lakini *kwa namna ya kibinadamu,* yaani kwa nguvu zao zikisaidiwa na neema za kawaida. Kumbe *upande wa mafumbo* unaanza katika hatua ya *mwanga* ambapo wanaoendelea, wakiangazwa na Roho Mtakatifu, wanatenda mara nyingi na waziwazi kwa *vipaji vyake saba;* kwa uongozi maalumu wa huyo mlezi wa ndani wanatenda kwa namna *ipitayo maumbile* ambayo kabla ya hapo ilikuwa imefichika au kujitokeza mara mojamoja tu. Kwa walimu hao mambo yanayopatikana upande wa mafumbo ni *ya juu katika njia ya kawaida ya utakatifu,* ila si ya pekee hasa (kama njozi). Ni hivyo hata kwa wale wanaoitiwa utakatifu katika utendaji mwingi. Basi, kujua upande wa mafumbo hakufai tu kwa uongozi wa watu wachache wanaoitwa kufuata njia za pekee, bali kwa watu wote wanaolenga ukamilifu na muungano na Mungu katika maisha ya kila siku. Ujinga wa kiongozi wa Kiroho kuhusu mambo hayo unaweza ukazuia wale anaowaongoza: kwa kuwa hapaswi kudhani kila huzuni ya mtu aliyechoka kiakili ni takaso la Kimungu, lakini pia asidhani kuwa hilo likipatikana ni huzuni ya kinafsi tu.

Kutokana na hayo yote, ni wazi kwamba *upande wa juhudi unalenga upande wa mafumbo.* Vilevile upande wa mafumbo usipotanguliwa na juhudi za kufaa ni uongo mtupu. Tukitazama njia ya utakatifu

kuanzia *umbile letu,* mafundisho haya yataonekana yamezidisha. Lakini tukiitazama kuanzia *mafumbo yapitayo maumbile* (uwemo wa Utatu mtakatifu ndani mwetu, umwilisho ulioleta ukombozi na ekaristi), hapo tutaiona kwa hekima, yaani kutoka juu, badala ya kupima yote kutoka chini unavyofanya upumbavu. Ikiwa kweli Utatu mtakatifu unaishi ndani mwetu, ikiwa kweli Neno alifanyika mwili akafa kwa ajili yetu, yumo katika sakramenti kuu na kila siku anajitoa kwa ajili yetu, basi hapo *watakatifu tu,* wanaoishi kwa kujua na kama kung'amua mara nyingi mafumbo hayo, na kwa kuyapenda zaidi na zaidi katika giza na matatizo maishani, *ndio waliopo panapotakiwa.* Hapo *maisha ya muungano wa ndani na Mungu* yanaonekana kuwa peke yake *ya kawaida kweli.* Kabla hatujafikia maisha hayo, tuko bado kama watu waliosinzia, wasioishi vya kutosha kwa hazina ile kuu tuliyokabidhiwa na Mungu. Utakatifu ni muungano wa ndani na Mungu, yaani ukamilifu wa upendo kwake na kwa jirani. Ukamilifu huo unapatikana katika njia ya kawaida, kwa sababu amri ya upendo inayowapasa wote haina mipaka. Utakatifu huo hauhitaji elimu ya juu, wala utendaji mwingi wa nje, bali kuishi kwa ndani na Mungu kwa kutekeleza kwa namna bora maadili na vipaji vya Roho Mtakatifu vinavyoongozana nayo. Ndio *utangulizi wa kawaida wa uzima wa milele,* nao unafanyika duniani au toharani, mpaka roho *iwe imetakata kabisa* iweze kukaribishwa kwenye heri ya kumuona Mungu. Tukisema kuzama katika mafumbo ya imani ni sharti la kufikia utakatifu, maana yake ni kwamba pasipo hilo kwa kawaida hatufikii utakatifu.

# 1. **CHEMCHEMI NA LENGO LA MAISHA YA KIROHO**

Kwa kuwa maisha ya Kiroho ni namna ambayo mtu mwenye bidii anaishi kwa neema akizidi kujitambua, tutaongelea kwanza *uzima wa neema* ili kuuthamini kikamilifu. Halafu tutazingatia muundo wa Kiroho, hasa maadili ya kumiminiwa pamoja na vipaji vya Roho Mtakatifu, ambavyo vyote vinatokana na neema ya utakaso. Hayo yatatuongoza kuzungumzia *uwemo wa Utatu* katika kila mwadilifu, na *athari ya kudumu* ya *Bwana wetu Yesu Kristo,* aliye mshenga pekee, na ya *Maria* pamoja naye kwa mtu huyo. Ndizo chemchemi za maisha ya Kiroho tunazozikuta juu sana, kuliko chemchemi za mito zinazotoka kwenye vilele vya milima mirefu. Kwa kuwa zinatoka juu, maisha ya Kiroho yanaweza kumrudia Mungu aliye juu na kuungana naye kwa ndani.

Katika sehemu hii ya kwanza, kisha kuongelea chemchemi za maisha ya Kiroho, tutazungumzia lengo lake, yaani *ukamilifu wa Kikristo* na wajibu wa kuulenga, kila mmoja kadiri ya hali yake maishani. Lengo ni la kwanza katika kupanga, lakini la mwisho katika kutekeleza. Ndilo tulilo na hamu nalo toka mwanzo, ingawa tunaweza kulipata mwishoni tu. Ndiyo sababu Bwana alianza kuhubiri kwa kutuambia juu ya heri.

## 1.1. ***UZIMA WA NEEMA, MWANZO WA UZIMA WA MILELE***

Maisha ya Kiroho yanadai *hali ya neema inayotia utakatifu*, ambayo ni kinyume cha hali ya dhambi ya mauti. Kila mtu ana mojawapo kati ya hali hizo mbili, yaani ama anamuelekea Mungu kama lengo kuu, ama amepotoka mbali naye. Hakuna anayeweza kuwa na hali ya kimaumbile tu, kwa kuwa wote wanaitiwa lengo linalopita maumbile, yaani kumuona Mungu uso kwa uso na hivyo kumpenda kabisa. Ili tuwe na maisha ya Kiroho haitoshi tuwe na neema inayotia utakatifu, kama vile mtoto aliyebatizwa, bali ni lazima tupigane na yale yote yanayoweza kutuangusha dhambini, na tuwe na juhudi halisi za kumlenga Mungu.

Tungeng'amua kwa ndani hali ya neema, tungeona kwamba siyo tu mwanzo wa maisha matakatifu bali ni mbegu ya uzima wa milele pia. Ni lazima tusisitize mapema jambo hilo, kwamba "neema inayotia utakatifu ya mtu mmoja ni bora kuliko mema ya kimaumbile ya ulimwengu wote" (Mt. Thoma wa Akwino); kwa sababu neema hiyo ni mbegu ya uzima wa milele, ambao una ubora usio na kifani kuliko uzima wa kimaumbile wa kwetu na wa malaika. Ndilo linalotuonyesha vizuri kuliko yote thamani ya *neema inayotia utakatifu*, ambayo tunaipata katika ubatizo na kurudishiwa na kitubio ikiwa tumeipoteza. Ni muhimu tuthamini kweli neema hiyo ambayo Uprotestanti umeisahau, ukifuata wanafalsafa wengi wa karne XIV. Hatuwezi kujua thamani ya mbegu tusipojua kinachoweza kutokana nayo. Upande wa binadamu, tukitaka kuthamini roho ambayo imesinzia bado katika mtoto, ni lazima tujue nguvu ya roho ya mtu aliyekomaa. Vilevile hatuwezi kuthamini neema inayotia utakatifu tusipozingatia ustawi wake kamili katika uzima wa

milele.

Inafaa tuizingatie kwa mwanga wa maneno ya Bwana, ambayo ni "roho, tena ni uzima" (Yoh 6:63) na yana ladha bora kuliko maelezo yoyote ya teolojia. Lugha ya Injili inatuzamisha katika sala kuliko lugha ya kitaalamu hata ile yenye hakika ya juu. Hakuna cha kufaa kuliko kupumua hewa safi ya vilele hivyo vinavyobubujika maji hai. "Mafundisho ya Yesu Kristo yanapita mafundisho yoyote ya watakatifu na mtu aliye na roho yake anakuta humo mana iliyositirika. Lakini inatokea kuwa wengi, kwa kusikia Injili mara nyingi, hawaguswi inavyotakiwa, kwa sababu hawana roho yake. Mnataka kuelewa mpaka ndani na kufurahia maneno ya Yesu Kristo? *Mjitahidi kulinganisha maisha yenu yote na ya kwake*" (Kumfuasa Yesu Kristo I,1:2).

**UZIMA WA MILELE ULIOAHIDIWA NA MWOKOZI**

Neno "uzima wa milele" ni adimu katika Agano la Kale, ambamo yote yanaelekea ujio wa Mwokozi aliyeahidiwa. Kumbe katika mahubiri ya Yesu yote yanaelekea moja kwa moja *uzima wa milele*. Tukizingatia kwa makini maneno yake tutaona jinsi uzima huo ulivyo tofauti na *maisha yajayo* yaliyozungumziwa na wanafalsafa bora (k.mf. Plato) kama hali ya kimaumbile tu na isiyo ya hakika. Kumbe Mwokozi anaongea kwa hakika juu ya uzima wa milele, bora, usio na jana, leo na kesho, unaopita maumbile na usiopimika, kama ule wa ndani ya Mungu, kwa kuwa unashiriki umilele wake usiobadilika.

Yesu alifundisha kuwa "njia imesonga iendayo uzimani" (Math 7:14) na kuwa tukitaka kuupata ni lazima tuache dhambi na kushika "amri" za Mungu (taz. Math 19:17). Mara kadhaa alisema kuwa anayemwamini "yuna uzima wa milele" (Yoh 5:24; 6:40,47), maana yake anayemuamini kuwa Mwana wa Mungu kwa imani hai, inayoambatana na upendo na utekelezaji wa amri, ameanza kuwa na uzima wa milele. Ndivyo alivyotamka tangu aanze kuhubiri, "Heri walio maskini wa roho, maana *ufalme wa mbinguni ni wao*... Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao *watashibishwa*... Heri wenye moyo safi, maana hao *watamwona Mungu*" (Math 5:3,6,8). Uzima wa milele ni kushiba huko na kumuona Mungu katika ufalme wake. Kwa namna ya pekee, wanaoteswa kwa kufanya atakavyo Mungu wanaambiwa, "Furahini na kushangilia, kwa kuwa *thawabu yenu ni kubwa mbinguni*" (Math 5:12). Yesu akajieleza zaidi kabla ya mateso yake aliposema, "Baba... ulimpa Mwanao mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba *wote uliompa awape uzima wa milele. Na uzima wa milele ndio huu: wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (Yoh 17:1-3).

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, *tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo"* (1Yoh 3:2), yaani si kwa kuzingatia mng'ao wa sifa zake katika viumbe (vile vinavyoonekana, pamoja na roho za watakatifu zinazojitokeza katika maneno na matendo yao), bali *moja kwa moja* jinsi alivyo. "Wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule *tutaona uso kwa uso*; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule *nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana*" (1Kor 13:12). Mtume hakusema nitamjua ninavyojijua mpaka ndani; kwa sababu najifahamu kuliko wengine, lakini mimi pia sielewi yote niliyonayo ndani, k.mf. siwezi kupima uzito wote wa dhambi zangu. Mungu tu ananijua fika: yeye tu anaelewa kikamilifu siri za moyo wangu. Mbinguni *nitamjua anavyonijua*, moja kwa moja, pasipo kupitia kiumbe chochote au wazo lolote la kimaumbile, kwa sababu hakuna wazo la namna hiyo linaloweza kumchora Mungu na ukweli wake usio na mipaka, nuru angavu ya milele. Kila wazo la namna hiyo lina mipaka, linazingatia sifa mojawapo ya Mungu (k.mf. ukweli au wema). Mawazo hayo mbalimbali hayatoshi kutujulisha undani wa Mungu, umoja wake usiogawanyika kamwe. *Mawazo hayo* yanahusiana na *uzima wake wa ndani* kama vile rangi saba za upinde wa mvua zinavyohusiana na mwanga mweupe ambao zinatokana nao. Hapa chini sisi ni kama watu tulioona hizo rangi saba tu na sasa tunatamani kuona huo mwanga mweupe unaozisababisha. Kabla hatujaona *umungu* wenyewe hatuwezi kuona ulinganifu wa dhati wa sifa zake, hasa huruma isiyo na mipaka na haki isiyo na mipaka. Mawazo yetu ya kimaumbile kuhusu sifa za Mungu ni vipande tu vya sura nzima, ambavyo vinaleta picha ya Mungu isiyopendeza vya kutosha. Tukifikiria haki yake, inaonekana ni kali mno, na tukifikiria upendeleo wa huruma yake unaonekana kwenda kinyume cha haki. Tukitafakari zaidi tunakiri kuwa *ndani ya Mungu haki na huruma ni kitu kimoja, hazitofautiani kweli*. Huo ni ukweli ambao tunauungama kwa hakika, lakini hatujaona *ulinganifu wa dhati* wa sifa hizo, kwa kuwa unahitaji tutazame umungu jinsi ulivyo, moja kwa moja, pasipo kutumia mawazo yoyote ya kimaumbile.

Mtazamo huo ndio uzima wa milele. Nani anaweza kueleza ukuu usiopimika wa furaha na upendo utakaokuwemo ndani mwetu kutokana na mtazamo huo? Upendo wa Mungu wenye nguvu na wa moja kwa moja, hivi kwamba hakuna lolote litakaloweza kuupunguza; kwa upendo huo tutafurahia hasa kuwa Mungu ni Mungu, mtakatifu, mwenye haki na huruma pasipo mipaka, na tutaabudu mipango yote ya maongozi yake iliyolenga ufunuo wa wema wake. Tutazama katika heri yake, alivyosema Mwokozi, "Vema, mtumwa mwema na uaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; *ingia katika furaha ya bwana wako"* (Math 25:21,23). Tutamuona Mungu vile anavyojiona, ingawa hatutaweza kumaliza vilindi vya hali yake, vya upendo wake na vya uweza wake. Pia tutampenda anavyojipenda. Vilevile tutamuona Bwana wetu Yesu Kristo. Ndiyo heri ya milele yenyewe, mbali ya furaha ya ziada tutakayokuwa nayo kwa kuwaona na

kuwapenda Bikira Maria na watakatifu wote, hasa tuliowafahamu duniani.

## MBEGU YA UZIMA WA MILELE NDANI MWETU

Huo mtazamo wa moja kwa moja wa Mungu unapita uwezo wa kimaumbile wa akili yoyote ya malaika na ya binadamu, kwa kuwa ungehitaji *ulingane na ule wa Mungu*. Basi, akili ya kiumbe inaweza kupata mtazamo huo *kwa neema ya Mungu tu*, ambayo ni kama kupandikiza chipukizi la mti bora katika shina la mti mwitu ili uzae matunda mema. Malaika na binadamu hawawezi kumjua na kumpenda Mungu kwa namna inayopita maumbile yao kabla hawajapandikiziwa *neema inayotia utakatifu*, ambayo ni *kushiriki umungu*, yaani uzima wa ndani wa Mungu. Neema hiyo tu, ikipokewa rohoni mwetu kama zawadi isiyolipika, itatuwezesha *kutenda Kimungu*, yaani kumuona moja kwa moja vile anavyojiona, na kumpenda vile anavyojipenda. Kwa maneno mengine, kushirikishwa umungu kwa akili na utashi kunategemea *kushirikishwa umungu kwa roho yenyewe* iliyonavyo.

Neema hiyo ikikamilika isiweze kupotezwa inaitwa *utukufu*, ambao unazitia akili za watakatifu wa mbinguni *mwanga usio wa kimaumbile* unaowawezesha kumuona Mungu, na unautia utashi wao *upendo wa kumiminiwa* unaowawezesha kumpenda wasiachane naye kamwe. Kwa ubatizo tumeshapokea mbegu ya uzima wa milele, kwa kupokea neema inayotia utakatifu ambayo inaleta uzima huo na upendo wa kumiminiwa unaokusudiwa kudumu milele. "Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, 'Nipe maji ninywe', ungalimwomba yeye, *naye angalikupa maji yaliyo hai…* Yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele, bali *yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele*" (Yoh 4:10,14). "Atakayekunywa maji hai ya neema yanayotolewa na Mwokozi hatatamani mengine, ila atatamani kuyapokea hayohayo kwa wingi zaidi... Lakini, tofauti na maji ya kawaida yanayoelekea chini, yale ya Kiroho yanapanda juu. Ni maji hai ambayo hayaachani kamwe na chemchemi yake na yanabubujikia uzima wa milele ambao yanatustahilisha" (Mt. Thoma wa Akwino). Hayo maji hai yanatoka kwa Mungu, ndiyo sababu yanaweza kurudi juu kwake. "Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake" (Yoh 7:37-38). Anayemuamini Mwokozi, anaweza kuchota katika chemchemi ya maji hai, si kwa ajili yake tu bali pia kwa wokovu wa wengine. "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele" (Yoh 3:36). Hatakuwa nao baadaye tu, bali kwa namna fulani anao tayari, kwa kuwa uzima wa neema ni mwanzo wa uzima wa milele. *Kwa undani ni uzima uleule wa Kimungu*, ambao hapa chini umo ndani ya Mkristo kama mbegu na huko juu utachanua kikamilifu katika watakatifu. Ndiyo maana Bwana aliongeza, "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho" (Yoh 6:54). Ufalme wa Mungu umo ndani mwetu kama mbegu ya haradali, kama chachu itakayoumua donge lote, kama hazina iliyositirika shambani.

*Tunawezaje kujua* kama tumeshaupokea uzima huo unaokusudiwa kudumu milele? "Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini *kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu*. Yeye asiyependa, akaa katika mauti… Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa *mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini* Jina la Mwana wa Mungu" (1Yoh 3:14; 5:13). Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia: Mtu akilishika neno langu, *hataona mauti milele*" (Yoh 8:51). Kwa kuwa, liturujia inavyosema, "Ee Bwana, uzima wa waamini wako hauondolewi ila unageuzwa tu", tena unastawi kikamilifu mbinguni tu. Hakika uzima wa neema hapa duniani ni mbegu ya utukufu, hivi kwamba kiwango kidogo cha neema inayotia utakatifu ni bora kuliko mema ya kimaumbile ya ulimwengu wote na ya malaika pia, kwa sababu kinahusu hali ya juu, yaani *uzima wa ndani wa Mungu*; kwa hiyo ni bora kuliko miujiza pia na ishara nyingine za nje za ufunuo. Uzima uleule unaopita maumbile, ndio unaopatikana duniani katika waadilifu na mbinguni katika watakatifu. Ni pia upendo uleule wa kumiminiwa, isipokuwa tofauti mbili zinazohusu imani na tumaini: kwamba hapa chini tunamjua Mungu si kwa kumtazama mwangani, bali katika *giza* la imani ya kumiminiwa; halafu hapa chini, ingawa tunatumaini kuwa naye milele, tunaweza *kupotewa naye* kwa kosa letu.

Kwa mwanga huo tuelewe maisha yetu ya Kiroho yanavyotakiwa kuwa na kustawi yawe utangulizi wa kufaa kwa uzima wa milele. Ikiwa neema inayotia utakatifu, maadili ya kumiminiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu kwa mfumo wake vinaulenga uzima wa milele, je havikusudiwi kulenga pia muungano wa hali ya juu na Mungu?

## JAMBO MUHIMU LITOKANALO

Neema inayotia utakatifu na upendo, vinavyotuunganisha na Mungu katika maisha yake ya ndani, ni bora, tena sana, kuliko neema za pekee (k.mf. kusema kwa lugha ngeni) ambazo ni ishara tu za kazi za Mungu lakini hazituunganishi naye (taz. 1Kor 12:28-13:13). Hali ya kuzama katika mafumbo haitokani na neema hizo za pekee, bali ni tunda la imani tuliyomiminiwa, ikiangazwa na vipaji vya akili na vya hekima. Hivyo inatokana na neema inayotia utakatifu, ambayo inaitwa pia "neema ya maadili na vipaji" na tunaipata wote katika ubatizo. Kwa kuwa neema hiyo *kwa mfumo wake* inalenga uzima wa milele, *inalenga pia hali ile inayohitajika ili kupata mwanga wa utukufu.* Hali hiyo ni upendo kamili pamoja na *hamu kubwa ya kumuona Mungu* ambayo kwa kawaida inatokana na neema ya kuzama katika mafumbo. Basi, kuzama humo si

karama, bali ni *hali ya juu iliyopo katika njia ya kawaida* ya utakatifu, ingawa ni adimu kama ukamilifu ulivyo adimu. Kwa vile neema inayotia utakatifu inalenga uzima wa milele, inalenga pia kutuweka tayari kupata mwanga wa utukufu mara baada ya kufa bila ya kupitia toharani, ambako ni *adhabu* inayotokana na kosa lisilotakiwa pamoja na malipizi yasiyotosha. *Ingekuwa kawaida kutakaswa katika maisha haya kwa kujilimbikizia stahili* na kukua katika upendo, badala ya kutakaswa kisha kufa *pasipo stahili* yoyote. Utayari wa kupokea mwanga wa utukufu *mara baada ya kifo* unahitaji kwanza utakaso kamili unaolingana na ule wa roho zinazotoka toharani zenye hamu kubwa ya kumuona Mungu. Hamu hiyo imedhihirishwa na Mt. Paulo vizuri ajabu, "Katika nyumba hii twaugua, tukitamani sana kuvikwa kao letu litokalo mbinguni… twaugua, tukilemewa, si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa… Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya neno lilo hilo ni Mungu, aliyetupa arabuni ya Roho" (2Kor 5:2-5).

Tukitaka kujadili vilivyo maisha ya Kiroho, hatupaswi kusahau vilele hivyo ambavyo tunajulishwa na Maandiko na kuelezwa na walimu wakuu. Hasa katika masuala hayo tunatakiwa kuzingatia watu si walivyo tu, bali wanavyokusudiwa kuwa. Tupumue hewa bora ya vilele vya juu, badala ya kuishia katika hali ya wastani ya binadamu. Heri watu wanaojaribiwa hata wanakuta hewa ya kuwafaa upande wa Mungu tu na kumuonea hamu kuu.

## 1.2. ***MAISHA YA KIROHO, MAONGEZI YA NDANI NA MUNGU***

**MAONGEZI YA KILA MTU NA NAFSI YAKE**

Mtu anapoacha shughuli za nje na maongezi na wenzake, mara anaanza kuwaza kwa kuongea na nafsi yake, hata kama yuko katikati ya makelele ya jiji. Akiwa kijana anafikiria ya kesho; akiwa mzee anafikiria ya zamani, na mang'amuzi aliyonayo sasa yanamfanya apime tofauti watu na matukio. Akiwa na umimi anafuata tamaa au kiburi: hivyo ndani yake anapata huzuni tu. Ndiyo sababu anajaribu kujitoroka kwa kuzama katika mambo ya nje na anasa ili asahau utupu wa maisha yake yasiyo na maana. Kwa kufanya hivyo anakuja kujifahamu kwa namna ya chini tu na kujipenda visivyo. Sanasana anajifahamu upande wa hisi, alizonazo sawa na wanyama; hivyo ana aina hiyo ya furaha na uchungu kadiri ya mabadiliko ya hali ya hewa au ya biashara yake. Anavyovitamani na anavyovichukia ni vya aina hiyohiyo, na akipingwa anakasirika kutokana na jinsi anavyojipendea kwa ubinafsi. Kumbe anajifahamu kidogo tu upande wa roho, ambayo inafanana na malaika. Hata akiamini ukuu wa roho yenye akili na utashi haishi katika ngazi hiyo, hang'amui sehemu hiyo bora ya utu wake, wala haipendi vya kutosha. Angeijua angeona ndani yake sura ya Mungu na kuanza kujipenda kwa ajili ya Mungu, badala ya kujipendea tu. Hata akionyesha mara nyingi alivyo na uwezo wa kuelewa na kutenda kwa ujanja, akili yake inaelekea daima yaliyo ya chini kuliko yeye. Ingawa ameumbwa ili kumtazama Mungu, ukweli mkuu, anafuata udanganyifu hata kuutetea kwa kila njia. Ni kwamba maisha yasipofuata ubora wa mawazo, mawazo yatafuata uduni wa maisha: yote yanafungamana, hata misimamo mizuri aliyonayo inazidi kudhoofika. Hivyo maongezi ya ndani yake yanaelekea mauti na hayastahili kuitwa maisha ya Kiroho. Kwa kujipendea anajiona kiini cha yote, na kuelekeza watu na vitu kwake; lakini hiyo haiwezekani, ndiyo sababu mara nyingi anakata tamaa na kuchukizwa, havumiliki kwake wala kwa wengine. Mwishowe anajichukia pamoja na maisha, kwa kuwa alitamani mno mambo ya chini.

Akianza kutafuta uadilifu, hata kama hajapata neema ya utakaso, maongezi na nafsi yake yanakuwa tofauti: k.mf. anazingatia yanayohitajika ili aishi kwa haki na kutegemeza familia yake. Pengine mawazo hayo yanamhangaisha hata kumfanya atambue unyonge wake na haja ya kumtegemea Mungu badala ya kujiamini tu. Akiwa na dhambi ya mauti isiyo dhidi ya imani wala tumaini anaweza akawa na maadili hayo yanayodumu hata baada ya kupoteza upendo. Hapo anaweza akaangazwa na imani namna ipitayo maumbile akawaza uzima wa milele na kuutamani, ingawa si zaidi; tena pengine anajisikia msukumo wa kwenda kanisani.

Hatimaye, akija kujuta na kuondolewa makosa yake, anarudishiwa neema inayotia utakatifu na upendo kwa Mungu na kwa jirani. Kuanzia hapo, mawazo yake yanakuwa mengine. Anaanza kujipenda na kuwapenda watu si kwa ajili yake, bali *kwa ajili ya Mungu;* anaanza kuelewa anavyopaswa kusamehe na kupenda maadui, na kuwatakia uzima wa milele kama vile anavyojitakia. Hata hivyo mawazo yake yanaendelea kuchafuliwa na umimi, tamaa na kiburi. Kwake makosa hayo si tena ya mauti, lakini yakitokea mara nyingi yatamfanya arudie dhambi kubwa na mauti ya roho. Hapo atajaribu tena kujitoroka, kwa sababu haoni uzima ndani mwake.

Pamoja na hayo, *maongezi ya ndani mwake yanaanza tena* yasiweze kuzuiwa na chochote, wala na yeye mwenyewe. Roho ina haja inayodai kutimizwa. Mungu tu anaweza kufanya hivyo. Kwa hiyo njia pekee ni kumuendea yeye. *Roho inahitaji kuongea naye* kwa sababu lengo lake kuu ni *Mungu aliye hai*, hata isiweze kutulia nje ya Mungu.

**MAONGEZI YA NDANI NA MUNGU**

Katika maisha ya Kiroho maongezi ya mtu na nafsi yake yanainuliwa na kugeuka maongezi na Mungu. Ni

kwamba Roho Mtakatifu anazidi kuwaonyesha watu wenye mapenzi mema yale anayowadai na yale anayotaka kuwazawadia. Lo! Kama tungepokea kwa mikono miwili yale *yote* Mungu anayotaka kutupatia! Hatuonyeshwi hayo tusipojitahidi kuokoka katika vifungo vitokanavyo na dhambi, kufisha hatua kwa hatua "utu wa kale" na kuunda "*utu wa ndani"*, ambamo akili na utashi vitawale mwili wetu unaofanana na ule wa mnyama. "Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa *utu wa ndani;* lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu" (Rom 7:22-23). "Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini *utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku"* (2Kor 4:16). Nguvu za Kiroho zinafanywa upya mfululizo kwa njia ya neema tunazozipokea. "Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa *utu mpya, unaofanywa upya* upate ufahamu *sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba"* (Kol 3:9-10). Baba "awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, *kufanywa imara* kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, *katika utu wa ndani"* (Ef 3:16).

Ndivyo vilindi vya maisha ya Kiroho yanayolenga mfululizo kulitazama fumbo la Mungu na kulifanya chakula chake katika muungano naye wa ndani zaidi na zaidi. Mtume aliandika hayo kwa Wakristo wote, si kwa mmojammoja tu, akaongeza, "*Mfanywe wapya katika roho ya nia zenu*; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli… *mkaenende katika upendo*, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi; tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato" (Ef 4:23-24; 5:2).

Kwa kuzingatia maneno hayo ya Mungu tunaweza kufafanua maisha ya Kiroho kama *maisha ambayo yanapita maumbile na kutuelekeza na kutufikisha kwenye muungano na Mungu kwa njia ya kujikana na kusali.* Maisha hayo yana hatua ya kwanza inayotawaliwa na utakaso, ya pili inayotarajia mwanga mkubwa zaidi na zaidi, na mwisho wake ni muungano na Mungu. Ndivyo mapokeo yanavyofundisha, yakithibitisha uwepo wa hatua ya kutakaswa kwa wanaoanza, hatua ya kuangazwa kwa wanaoendelea, na hatua ya kuungana na Mungu kwa waliokamilika. Kadiri maisha ya ndani ya mtu yanavyozidi kuwa *maongezi na Mungu,* anakuja kung'amua sehemu bora ya nafsi yake na kumjua Mungu. Polepole mawazo ya nafsi yake aliyoifanya kuwa lengo la yote, yanaiachia nafasi kumbukumbu ya kudumu ya Mungu. Vivyo hivyo kujipendea kunaacha nafasi kwa upendo wa Mungu na wa watu kwa ajili yake. Maongezi ya ndani yanabadilika hata kusema, "Sisi, wenyeji wetu uko mbinguni" (Fil 3:20).

Kwa mtu mwenye neema inayotia utakatifu, maisha ni ya unyenyekevu, majikanio, imani, tumaini na upendo, pamoja na amani inayotokana na kuweka miguso na matakwa yote chini ya upendo wa Mungu atakayekuwa heri yake. Ili awe na maisha ya Kiroho haitoshi wala si lazima afanye utume mwingi wala kujua sana dini. Akianza tu kujikana na kusali kwa juhudi, anayo tayari maisha ya Kiroho ambayo yanatakiwa kustawi zaidi na zaidi. Katika maongezi hayo yanayoelekea kuwa ya kudumu tunasema kwa njia ya sala, ambayo ingekuwepo hata kama Mungu angemuumba mtu mmoja au malaika mmoja tu. Sala inaweza kuwa ya kuomba, ya kuabudu au ya kushukuru; lakini daima ni kuinua roho kwa Mungu. Naye anajibu akitukumbusha yale ambayo tuliambiwa katika Injili na yanatufaa kuitakasa nukta ya sasa hivi, "Huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yoh 14:26). Hivyo mtu anazidi kuwa mtoto wa Mungu kwa kumtambua kama Baba na kujifanya mdogo mbele yake. Anaelewa ni lazima arudi katika tumbo la Mungu ili kuzaliwa upya Kiroho kila siku zaidi, kwa mfano wa Neno kuzaliwa milele. Wenye heri wa mbinguni wanabaki daima katika tumbo hilo.

Watakatifu wanafuata njia hiyo, hata maongezi yao na Mungu hayana mwisho. Mt. Dominiko hakuweza kusema isipokuwa juu ya Mungu au na Mungu; ndiyo sababu alikuwa amejaa daima upendo kwa watu. Maongezi hayo na Mungu yanaundwa kwa njia ya Kristo mshenga: "Ulimi hauwezi kusema, / wala maandishi kufafanua, / aliyeng'amua tu anaweza kuamini / kumpenda Yesu ni nini" (Utenzi wa Jina Takatifu la Yesu).

## 1.3. *MUUNDO WA KIROHO*

Ili tuelewe mbegu ya uzima wa milele iliyomo ndani mwetu ni nini, tunatakiwa kuzingatia jinsi neema ya utakaso inavyoleta katika akili na utashi maadili ya kumiminiwa na vipaji saba vya Roho Mtakatifu. Maadili hayo na vipaji hivyo ndio utendaji wa muundo uleule wa Kiroho unaokusudiwa kustawi hadi tuingie mbinguni.

### 1.3.1. *MAISHA YA KIMAUMBILE NA YANAYOPITA MAUMBILE*

Kwanza tutofautishe ndani ya roho yetu yale yaliyo ya kwake kwa jinsi ilivyoumbwa, na yale ambayo ni zawadi tu ya Mungu. Hata malaika, ingawa ni roho tu, ana umbile la chini kuliko neema inayotia utakatifu. Basi, umbile la binadamu lina pande mbili tofauti: *wa kwanza unalingana na wanyama, ukiwa na hisi* za nje (milango ya fahamu) na za ndani (ubunifu na kumbukumbu) pamoja na uwezo wa kupatwa na maono mbalimbali (hasa pendo na chuki, hamu na hofu, furaha na huzuni, hasira).

Juu yake, katika umbile letu *upo upande mwingine unaolingana na malaika*, ingawa ndani mwao una nguvu na uzuri zaidi. Upande huo wa roho unapita mwili, maana hautegemei moja kwa moja, bali unaweza kudumu baada ya mwili kufa. Kutokana na umbile la roho upande huo wa juu tuna vipawa vya akili na utashi. *Akili* inajua sio tu sifa za viumbe zinazohisikana (rangi, sauti n.k.), bali undani wao na kweli

zisizobadilika kama vile: "Hakuna kinachotokea pasipo sababu, na hasa pasipo sababu kuu, yaani Mungu"; "tunapaswa kutenda mema na kuepa maovu"; "timiza wajibu wako, liwalo na liwe". Mnyama hataweza kamwe kujua kweli hizo. Kwa kuwa akili inaweza kujua sio tu yale yanayotupendeza au yanayotufaa bali pia maadili (k.mf. kwamba "ni afadhali kufa kuliko kusaliti"), basi *utashi* unaweza *kupenda uadilifu, kuutaka na kuutekeleza* kwa kutawala hisi na maono alivyonavyo mnyama pia. Kwa akili na utashi mtu anafanana na malaika, ingawa katika maisha haya akili yetu, tofauti na malaika, inazitegemea hisi katika kuanza kujua mambo. Akili na utashi vinaweza vikastawi, pasipo kufikia kujua na kupenda *maisha ya ndani ya Mungu*, ambayo ni ya ngazi ya juu kupita maumbile ya malaika na ya binadamu. Hao wanaweza kumjua kimaumbile Mungu kwa nje, kutokana na mng'ao wa sifa zake katika viumbe, lakini haiwezi kuumbwa akili yenye nguvu ya kuyajua yaliyo ya Mungu tu: "Ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na *mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu"* (1Kor 2:11).

Kumbe neema inayotia utakatifu inatuingiza katika hiyo hali ya juu ya ukweli na uzima *inayopita maumbile yoyote,* kwa kuwa *unashiriki maisha ya ndani ya Mungu;* ni hali ya Kimungu ambayo inatuandaa *kumuona milele anavyojiona na kumpenda anavyojipenda.* "Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho*"* (1Kor 2:9-10). Neema ya utakaso inayotuwezesha tuanze kuishi ndani ya Mungu, juu kuliko umbile la malaika, ni kama chipukizi la Kimungu lililopandikizwa ndani ya roho ili kuinua uzima wake na kuifanya izae si matunda ya kimaumbile, bali matendo yanayostahili uzima wa milele. Kupandikizwa huko kunapita miujiza inayojulikana na hisi. Kwa mfano, ufufuo unaurudishia mwili *uhai wa kimaumbile,* ndiyo sababu unaweza kujulikana na umbile letu; kumbe neema ya utakaso inaipatia roho *uzima usio wa kimaumbile,* ndiyo sababu hauwezi kuhakikishwa. Tangu sasa uzima huo wa neema unatutia *maadili ya kumiminiwa na vipaji saba vya Roho Mtakatifu.* Kama vile umbile la roho lina kipawa cha akili na vinginevyo, katika ngazi ipitayo maumbile neema ya utakaso inaleta rohoni maadili na vipaji hivyo ambavyo, pamoja na mzizi unaovisababisha, ndio muundo ambao tulijaliwa katika ubatizo na kurudishiwa na ondoleo la dhambi ikiwa tuliupoteza.

*Muundo huo wa Kiroho* unaweza kuonyeshwa na jedwali lifuatalo:

| | **MAADILI** | **VIPAJI** |
|---|---|---|
| **YA KIMUNGU** | Upendo | Hekima |
| | Imani | Akili |
| | Tumaini | Elimu |
| **YA KIUTU** | Busara | Shauri |
| | Haki | Ibada |
| | Nguvu | Nguvu |
| | Kiasi | Uchaji wa Mungu |

### 1.3.2. ***MAADILI YA KIMUNGU***

Maadili ya Kimungu ni maadili ya kumiminiwa yanayomhusu *Mungu mwenyewe* aliye lengo letu kuu. Tofauti na hayo, maadili ya kiutu yanahusu *njia* za kufikia lengo hilo.

Kati ya maadili ya Kimungu, *imani* inatuwezesha kusadiki *yale yote ambayo Mungu ametufunulia*, kwa kuwa ndiye ukweli wenyewe. Ni kama hisi ya Kiroho inayotuwezesha kusikia muziki safi wa Kimungu usiojulikana kwa njia nyingine yoyote. Kuna tofauti kubwa kati ya kusoma Injili kihistoria au kitaalamu na kuiamini kama Neno la Mungu, kwa kuwa *kusadiki ni tendo linalopita maumbile* yetu na ya malaika, likituingiza katika ulimwengu wa juu. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, *ni kipawa cha Mungu"* (Ef 2:8). Ndiyo msingi wa kufanywa waadilifu, kwa kuwa inatujulisha lengo lipitalo maumbile tunalopaswa kulikusudia. "Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki" (Mwa 15:6; Rom 4:3,9). "Walakini haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake; bali na kwa ajili yetu sisi tutakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu" (Rom 4:23-24). Sisi tutaokoka tu kwa imani hiyo ambayo ni zawadi ya Mungu. Kanisa lilitamka rasmi dhidi ya Wapelajiupande kwamba *hata mwanzo wa imani ni neema*. Imani hiyo *inapita kabisa maumbile*, si kama muujiza unaoonekana au kama utabiri wa tukio la kawaida tu (k.mf. mwisho wa vita); kwa sababu imani inamhusu *Mungu mwenyewe katika maisha yake ya ndani*, ambayo hayawezi kujulikana kimaumbile, tena kwa sababu tunasadiki kwa kutegemea *mamlaka ya Mungu aliyejifunua*, ambayo pia haiwezi kujulikana na maumbile. Imani inatufanya *tushike kwa namna ipitayo maumbile* na isiyoweza kukosa, *yale ambayo Mungu ametufunulia* kadiri tunavyofundishwa na Kanisa lililokabidhiwa

ufunuo huo.

"Tazama, msomi fulani anachimba mafundisho ya Kikatoliki bila ya kuyakataa kwa ukaidi, bali anakariri, Heri nyinyi mlio na imani; mimi pia ninapenda kuwa nayo lakini siwezi. Anasema ukweli: anataka asiweze (bado); kwa sababu kusoma na kuwa na nia njema hakufikii daima kujua ukweli, ili ionekane wazi kuwa *hakika ya akili si hakika kuu* inayotegemeza mafundisho ya Kikatoliki… Kinachotokea ndani mwetu tunapoamini ni *tukio la mwanga wa ndani unaopita umbile letu*... Mwongofu atawaambia, Nilisoma, nilitafakari, nilitaka nisifike; lakini siku fulani, siwezi kusema vipi, kwenye pembe ya njia, au nyumbani karibu na moto, sijui, sikuendelea kuwa yuleyule, nimesadiki... Kilichotokea ndani mwangu katika nukta ya kupata hakika kuu ni jambo tofauti kabisa na yale yote yaliyotangulia. Muwakumbuke wanafunzi wale wawili waliokwenda Emau" (H. Lacordaire).

Imani tunayomiminiwa ni kama uwezo wa kusikia ambao unapita maumbile na kutufanya tusikilize sauti ya Mungu kupitia manabii na Mwanae mwenyewe, kabla hatujakaribishwa kumuona uso kwa uso. Mtu anayesoma Injili bila ya imani, na mwingine mwenye imani, ni tofauti kama watu wawili wanaosikiliza wimbo fulani, lakini mmojawao ana karama ya muziki, mwingine hana. Wote wanasikia noti zote, lakini yule wa kwanza tu anaelewa undani na ujumbe wa wimbo ule. Vivyo hivyo mwamini tu, hata kama hajui kusoma, anashika Injili namna ipitayo maumbile kama *Neno la Mungu,* wakati msomi pamoja na elimu yake yote hawezi kuishika hivyo pasipo imani ya kumiminiwa. "Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake. Asiyemwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu amemshuhudia Mwanawe" (1Yoh 5:10). Miaka mia iliyopita mtu angeshangaa kuambiwa siku moja ataweza kusikia kwa redio muziki unaochezwa wakati huohuo katika nchi nyingine. Kwa imani ya kumiminiwa tunasikia muziki wa mbinguni, ambao baadhi ya nyimbo zake ni mafumbo ya Utatu, umwilisho, ukombozi, ekaristi na uzima wa milele. Kwa kusikiliza hayo tunaongozwa zaidi na zaidi kule unakotokea muziki huo bora.

Ili tuelekee kweli lengo hilo na kulifikia, tumepewa mabawa mawili, *tumaini* na *upendo*. Pasipo hayo tunaweza kuelekea tu tunapoelekezwa na akili yetu; kumbe tukiwa nayo tunarukia tunapoelekezwa na imani. Kama vile akili yetu pasipo mwanga wa imani haiwezi kujua lengo letu lipitalo maumbile, utashi wetu pia hauwezi kuelekea lengo hilo nguvu zake zisipozidishwa na kuinuliwa kwenye ngazi ya juu. *Kwa tumaini* tunatamani kumpata Mungu, na kusudi tumfikie tunategemea si nguvu za umbile letu, bali *msaada aliotuahidia,* yaani *yeye aliye tayari daima kusaidia*. *Upendo unatufanya tumpende Mungu* namna bora zaidi, isiyojitafutia faida; si tu ili tumpate hapo baadaye, bali *kwa ajili yake na kuliko tunavyojipenda*, kutokana na wema wake usio na mipaka, unaopendeza kuliko fadhili zake zote. Unatufanya tumpende hasa kama *rafiki* aliyetangulia kutupenda. Unamuelekezea vitendo vya maadili mengine yote ukiyahuisha na kuyafanya yaweze kustahili. Ndiyo nguvu yetu kuu ipitayo maumbile, *nguvu ya upendo* ambayo wakati wa dhuluma imeshinda vipingamizi vyote, hata katika viumbe dhaifu kama watakatifu Anyesi na Lusia. Hivyo mwenye mwanga wa imani anamuelekea Mungu kwa mabawa ya tumaini na upendo. Akitenda dhambi ya mauti, mara anapoteza neema inayotia utakatifu na upendo, kwa kuwa anajitenga na Mungu akiacha kumpenda kuliko nafsi yake. Hata hivyo huruma ya Mungu inamuachia imani na tumaini (mpaka atakapotenda dhambi dhidi ya maadili hayo) awe bado na mwanga wa kumuelekeza njia, na aweze bado kutegemea huruma isiyo na mipaka ili kuomba neema ya uongofu.

Kati ya maadili hayo ya Kimungu, upendo ndio la juu zaidi, nao utadumu milele pamoja na neema inayotia utakatifu, ambapo badala ya imani na tumaini mtu atakuwa na Mungu akimjua waziwazi, bila ya hofu ya kupotewa naye. *"Upendo haupungui neno wakati wowote;* bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika… Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo (1Kor 13:8,13). Ndio utendaji wa juu wa muundo wa Kiroho: maadili matatu ya Kimungu ambayo yanastawi pamoja, halafu maadili ya kiutu yanayoendana nayo.

### 1.3.3. ***MAADILI YA KIUTU***

Ili tuzielewe taratibu za muundo wa Kiroho, ni muhimu tujue vizuri maadili ya kiutu, yaliyo chini ya yale ya Kimungu. Jina linavyosema, ya kwanza, yanayopatikana kwa kurudiarudia vitendo vyake, yanajulikana na Wapagani pia kwa kuwa lengo lake linajulikana na akili. Baadhi ya vijana waliojitoa kwa Mungu hawayajali vya kutosha; kinyume chake wengine wenye umri mkubwa zaidi, kisha kutambua umuhimu wake hawajali tena vya kutosha maadili ya Kimungu, ambayo ni bora pasipo mfano, kwa kuwa ndiyo yanayotuunganisha na Mungu.

Basi tupande ngazi kwa ngazi hadi uadilifu unaopita maumbile. Tuone kwanza mtu mwenye dhambi ya mauti anavyoweza kuwa na *maadili ya bandia*, k.mf. kiasi cha mchoyo; yeye anakitekeleza si kwa kupenda uadilifu, bali kwa kupenda fedha. Vilevile akilipa madeni si kwa kutekeleza haki bali kwa kukwepa gharama za kesi.

Juu kuliko hayo maadili ya bandia, mtu mwenye dhambi ya mauti anaweza kuwa na *maadili halisi* ya kiutu aliyojipatia. Wako wengi wanaofuata kiasi ili kuishi akili inavyotaka, na kwa ajili hiyohiyo wanalipa madeni na kuwalea vizuri watoto wao. Lakini mtu akibaki katika dhambi ya mauti, ni dhaifu katika kutekeleza uadilifu,

hata ule wa kiutu. Maadili yake hayana msimamo, kwa kuwa utashi wake haumuelekei Mungu: badala ya kumpenda kupita yote, anajipenda kuliko Mungu. Halafu, maadili mengine yanayotakiwa kuyasaidia hayo hayapo, hivyo *yanakosa mshikamano*. Anayeendesha gari la kukokotwa na farasi kadhaa, anahitaji kila mmojawao awe amezoea kazi hiyo: vilevile adili moja haliendi bila ya lingine; yote yanahusiana na kuongozwa na busara. Basi, ili maadili ya kiutu *yawe imara* ni lazima yashikamane, na hiyo inadai mtu asibaki katika dhambi ya mauti, bali utashi wake ulenge kuishi na Mungu; ni lazima ampende kuliko nafsi yake, jambo lisilowezekana pasipo neema ya utakaso. Akiipata tu, maadili yote yanaweza kushikamana na kuwa imara; nayo chini ya upendo yanakuwa chanzo cha matendo yanayostahili uzima wa milele.

Maadili ya Kimungu yanatuinua na kuturekebisha kuhusu lengo lipitalo maumbile na kuhusu *njia zipitazo maumbile* zinazoweza kulifikia. Bila ya hayo, maadili ya kiutu hayatoshi: kuna *tofauti ya dhati* kati ya kiasi walichokieleza Wapagani na kile cha Kikristo (k.mf. kati ya ufukara wa mwanafalsafa na ule wa Kiinjili), kwa sababu *kanuni* na *lengo* ni tofauti. Cha kwanza kinataka mtu ale tu kipimo cha wastani *ili kufuata akili*, kutodhuru afya au kufikiri vizuri. Kumbe kiasi cha Kikristo kinamtaka ajipatie chakula *ili kuishi kama mtoto wa Mungu*, akielekea uzima wa milele; hivyo kinadai maisha magumu zaidi: kinadai mtu autese mwili wake "na kuutumikisha" (1Kor 9:27), kusudi asiwe tu raia mwadilifu wa nchi yake, bali pia mwenyeji "pamoja na watakatifu" na mtu "wa nyumbani mwake Mungu" (Ef 2:19).

Tofauti hiyohiyo ipo kati ya adili la ibada linalotakiwa kumpatia Muumba heshima anayostahili, na adili la ibada la Mkristo linalomtolea Mungu, asili ya neema, sadaka ya misa ipitayo maumbile. Kwa kuwa ni tofauti ya ngazi, aina ya kwanza inaweza kustawi mfululizo kwa kurudiarudia vitendo vyake, bila ya kufikia kiwango kidogo cha aina ya pili iliyoinuliwa na neema inayotia utakatifu. Kinachoongoza maadili hayo mawili yenye jina lilelile ni tofauti: upande mmoja ni akili ya binadamu tu, upande wa pili ni imani iliyomiminwa na Mungu.

Ni malengo mawili tofauti na nia mbili tofauti, ambapo busara haijui nia zipitazo maumbile, ila ikiangaziwa na imani inakuja kuzijua kwa kujua ukuu usio na mipaka wa lengo letu, yaani kumuona Mungu; hapo inakuja kujua uovu wa dhambi ya mauti, thamani ya neema inayotia utakatifu na ya neema za msaada ambazo ziombwe kila siku, na hazina ya sakramenti zilizowekwa kwa faida yetu. Vilevile kuna tofauti kubwa kati ya utaratibu ulioelezwa na mwanafalsafa Aristotle na unyenyekevu wa Kikristo unaozitegemea kweli za imani. Kuna tofauti kubwa kati ya ubikira wa wanawake waliokabidhiwa kuchochea daima moto wa miungu, na ule wa Mkristo aliyejiweka wakfu mwili na moyo kwa Mungu ili kumfuata Yesu kikamilifu zaidi.

Upendo unapoturekebisha tulenge uzima wa milele, unarekebisha maadili pia kuhusu njia zipitazo maumbile za kufikia wokovu. Walioendelea Kiroho wanaongozwa zaidi na kwa namna wazi na hiyo nia ipitayo maumbile, kumbe nia ya kibinadamu ndiyo inayozidi kuwaongoza wengine. Katika dhambi ya mauti mtu anajipenda kuliko Mungu na kwa umimi anaelekea kutotimiza hata wajibu wa kiutu.

Maadili ya kiutu yanainuka *katikati* ya pande mbili tofauti, ambazo mmoja umezidisha na mmoja una upungufu. Kwa mfano, adili la nguvu linainuka katikati ya woga (unaokimbia hatari bila ya sababu yenye msingi) na ushupavu (unaotaka kuvunjika kichwa bila ya sababu ya kutosha). Lakini, ebu! Hiyo katikati isieleweke vibaya. Wanaopenda anasa na watu vuguvugu wanataka kusimama katikati si kwa kupenda uadilifu, bali kusudi waepe matatizo ya vilema vinavyopingana pande hizo mbili. Hao wanachanganya hiyo katikati na ule *wastani* ambao haupatikani kama kilele *katikati ya vilema viwili vinavyopingana* bali *katikati ya uovu na uadilifu*. Wastani huo unakimbia uadilifu wa juu ukijisingizia kuwa "pengine yaliyo bora yanazuia yaliyo mema", ukiwa na maana ya kwamba, eti! *"Mara nyingi* au daima yaliyo bora yanazuia yaliyo mema". Kumbe hiyo *katikati* halisi ya uadilifu haisimami tu kati ya vilema viwili vinavyopingana, bali inainuka juu ya upotovu wa pande hizo mbili tofauti: busara halisi iko juu ya upumbavu na ya ujanja; ukarimu uko juu ya uroho na ya ubadhirifu; adili la ibada liko juu ya kudharau dini na ya ushirikina. Tena *hiyo katikati inaelekea kuinuka zaidi na zaidi,* pasipo kupotoka upande mmoja wala upande mwingine, *kadiri uadilifu unavyokua*, kwa kuwa inafuata kanuni ya juu na lengo la juu.

Hatimaye, tuzingatie Injili na walimu wa Kiroho walivyosisitiza *baadhi ya maadili ya kiutu ambayo yanahusiana zaidi na Mungu* na kulingana zaidi na maadili ya Kimungu: *ibada na toba* (zinazompatia Mungu heshima na malipizi anavyostahili), *upole* (ukiambatana na subira), *usafi kamili* (au ubikira) na *unyenyekevu* ambao ukituinamisha mbele ya Mungu unatuinua juu ya ufinyu wa moyo na ya kiburi na kutuelekeza tuzame katika mambo ya Mungu na kuungana naye. "Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu" (Math 11:29). Yesu tu, kwa jinsi alivyojengeka katika ukweli, aliweza kusema juu ya unyenyekevu wake pasipo kuupoteza papo hapo.

Maadili ya kiutu na yale ya Kimungu (ambayo yayaongoze ya kwanza) ni utendaji wa aina mbalimbali wenye kulingana vizuri ajabu, dhambi nyepesi isipokuja kuvuruga. Sehemu zote za muundo huo wa Kiroho zinakua pamoja kama vidole vya mkono mmoja. Kutokana na mshikamano uliopo maadili yote yanakua pamoja na upendo, hasa maadili ya kumiminiwa, kwa kuwa yale ya kujipatia pengine yanastawi kidogo zaidi yasipofanyiwa mazoezi. Hatuwezi kuwa na upendo mkubwa pasipo unyenyekevu mkubwa; ni kama tawi la juu la mti linalozidi kuinuka kadiri mzizi unavyozidi kupenya ardhi. Tunapaswa kukesha kitu chochote kisije kikaharibu ulinganifu huo, kama inavyowatokea wale ambao wanadumu katika neema inayotia utakatifu lakini wanajali elimudunia na mafungamano na watu kuliko ustawi wa imani, tumaini na upendo wa Mungu.

## 1.3.4. ***VIPAJI SABA VYA ROHO MTAKATIFU***

Kusudi tujue kweli muundo wa Kiroho, haitoshi tuyajue maadili. Ni lazima tuzingatie pia vipaji vya Roho Mtakatifu, pasipo kusahau namna mbalimbali za kupata msaada wa Mungu.

**USHUHUDA WA MAANDIKO MATAKATIFU**

Ufunuo kuhusu vipaji vya Roho Mtakatifu unapatikana hasa katika dondoo la Isaya 11:2 ambalo linamhusu kwanza Masiya, halafu kwa kumshiriki yeye linawahusu waadilifu wote ambao Yesu aliahidi kuwapelekea Roho Mtakatifu: "Roho ya Bwana atakaa juu yake, *roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na* ya *kumcha Bwana"*. Kipaji cha ibada hakitajwi katika lugha asili ya Kiyahudi, bali katika tafsiri za Septuaginta na Vulgata. Halafu, Isaya 11:3 kwa Kiyahudi inataja tena "kumcha Bwana", ambapo katika Agano la Kale "kumcha Bwana" na "ibada" ni maneno mawili yenye maana karibu ileile. Hivyo kuanzia karne III mapokeo yanashika idadi ya vipaji saba.

Katika kitabu cha Hekima tunasoma: "*Naliomba, nikapewa ufahamu; nalimwita Mungu, nikajiliwa na roho ya Hekima.* Naliichagua kuliko fimbo za enzi na viti vya enzi, wala mali sikudhani kuwa ni kitu ikilinganishwa nayo; wala sikuifananisha na kito cha thamani, mradi dhahabu yote ya nchi ni kama mchanga kidogo mbele yake, na fedha itahesabiwa kama udongo. Naliipenda kupita afya njema na uzuri wa sura, hata zaidi ya nuru nikataka kuwa nayo, kwa maana mwangaza wake haufifii kamwe. Na pamoja nayo nikajiliwa na mema yote jamii… ingawa sijajua ya kama yeye ndiye aliyeyazaa… Maana yeye amekuwa hazina kwa wanadamu isiyowaishia; nao wale waitumiao hujipatia urafiki na Mungu… na *tangu kizazi hata kizazi huwaingilia roho takatifu*, huwafanya wanadamu kuwa rafiki za Mungu na manabii" (Hek 7:7-11,12,14,27).

Ufunuo wa Agano la Kale umetimilizwa na Mwokozi: "Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami *nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;* ndiye Roho wa kweli… anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu… huyo *Roho Mtakatifu*, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, *atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia"* (Yoh 14:15-17,26). Yohane, akitaka kuwakinga waamini dhidi ya wazushi, akaongeza, "Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu… Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama *mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote,* tena ni kweli wala si uongo" (1Yoh 2:20,27).

Katika Maandiko yapo pia madondoo kuhusu kipaji kimojakimoja.

**USHUHUDA WA MAPOKEO**

Mababu wa Kanisa waliyafafanua mara nyingi maneno hayo na kutamka wazi kuwa vipaji saba vya Roho Mtakatifu vimo ndani ya waadilifu wote. "Hivyo vipaji vya Roho Mtakatifu kwetu ni kama chemchemi ya Kimungu tunapochota ujuzi hai wa amri za maisha ya Kikristo, na kwa njia yake tunaweza kujua pia kama Roho Mtakatifu anakaa ndani mwetu" (Katekisimu ya Mtaguso wa Trento). Ushuhuda muhimu wa Mapokeo kuhusu vipaji saba unapatikana katika liturujia ya Pentekoste: "Wape waamini wako, / wenye tumaini kwako, / paji zako zote saba" (sekwensya "Uje Roho Mtakatifu"). "Mtoa wa vipaji saba... / tia nuru akilini / na upendo mioyoni" (utenzi "Uje Roho Muumbaji").

Ushuhuda huo ulielezwa vizuri na Leo XIII, "*Mwadilifu* anayeishi kwa neema inayotia utakatifu na kutenda kwa njia ya maadili kama kwa vipawa mbalimbali, *anahitaji kabisa vipaji saba*, ambavyo vinaitwa kikamilifu zaidi vipaji vya Roho Mtakatifu. *Kwa vipaji hivyo roho ya mtu inainuliwa na kuwezeshwa kutii kwa urahisi na mapema zaidi miangaza na misukumo ya Roho Mtakatifu.* Vipaji hivyo vina nguvu kubwa hata kumwongoza mtu kwenye utakatifu mkuu; ni bora hivi hata kudumu mbinguni pia, ingawa kwa kiwango cha juu zaidi. Kwa njia yake roho inaongozwa na *kuhimizwa kujipatia heri za Kiinjili, ambazo ni maua yanayochanua kwa wakati wake, dalili tangulizi za heri ya milele... Kwa kuwa vipaji ni vikubwa hivyo* navyo vinaonyesha wema mkuu wa Roho Mtakatifu kwetu, *vinatudai tumuonyeshe heshima na utiifu mkuu kabisa*. Tutafikia kwa urahisi hatua hiyo tukijitahidi zaidi na zaidi kumjua, kumpenda na kumuomba... *Tunapaswa kumpenda Roho Mtakatifu kwa kuwa ni Mungu... tena kwa kuwa ni upendo wenyewe, asili, wa milele, kwa sababu hakuna kinachopendeza kuliko upendo...* Yeye atatujalia kwa wingi zawadi zake za kimbingu, hasa kwa sababu utovu wa shukrani unafunga mikono ya mfadhili, lakini moyo wa shukrani unaifungua tena... *Tunapaswa kumuomba mfululizo na kwa tumaini kubwa atuangaze zaidi na zaidi na kuwasha ndani mwetu moto wa upendo wake,* ili kwa kutegemea imani na upendo tutembee kwa ari kuelekea tuzo la milele, kwa kuwa *ndiye amana ya urithi wetu"*.

**MAELEZO YA MT. THOMA WA AKWINO**

Mwalimu huyo wa Kanisa alifundisha hasa matatu: 1° kwamba vipaji ni misimamo ya kudumu, lakini tofauti na maadili; 2° kwamba ni vya lazima kwa wokovu; 3° kwamba vinashikamana na upendo na kukua pamoja nao.

1° "Ili kutofautisha vipaji na maadili mbalimbali tunapaswa kufuata lugha ya Biblia inayoviita si vipaji bali roho" kusudi tuelewe kuwa vinapatikana ndani mwetu kwa *uvuvio wa Mungu* au msukumo kutoka juu wa Roho Mtakatifu. Ni lazima tuzingatie kwamba binadamu ana *mambo mawili yanayomuongoza*: moja limo

ndani mwake, yaani akili, lingine liko nje, yaani Mungu. “Ni wazi kwamba chochote kinachosukumika kinatakiwa *kulingana* na lile linalokisukuma; na *ukamilifu wake* ni *urahisi wa kusukumwa* nalo. Basi, kadiri hilo lilivyo bora, ni lazima kinachosukumwa kiwe kikamilifu zaidi ili kupokea msukumo wake. Hatimaye ni wazi kwamba *maadili ya kiutu* yanamkamilisha mtu katika kujiongoza *kwa akili yake* katika maisha ya ndani na ya nje. Basi unahitajika ndani mwake ukamilifu wa juu ambao umuandae *kusukumwa Kimungu*, na namna hizo kamilifu zinaitwa vipaji siyo tu kwa kuwa tunamiminiwa na Mungu, bali pia kwa sababu kwa njia yake *mtu anawezeshwa kupokea mara uvuvio wa Kimungu,* alivyosema Isaya (50:5): ‘Bwana Mungu amenizibua sikio langu, wala sikuwa mkaidi, wala sikurudi nyuma’. Ndiyo sababu wengine wanasema vipaji vinamkamilisha binadamu vikimuandaa kutenda mambo bora kuliko ya maadili”.

Hapo tunaona kuwa vipaji vya Roho Mtakatifu si matendo wala si misukumo au misaada ya kupita ya neema, bali ni misimamo ya kudumu tunayomiminiwa, inayotuweka tayari kupokea uvuvio wa Mungu, kama vile tanga zinavyowezesha chombo kwenda kwa nguvu ya upepo. Kwa utayari huo wa kupokea misukumo vinatusaidia kutenda mambo yale bora ambayo ukamilifu wake unaonyesha kwamba yanategemea vipaji kuliko maadili.

Mfano huo ulitolewa na Bwana mwenyewe aliposema, “*Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho*” (Yoh 3:8). Hatujui vizuri upepo unaovuma umetokea wapi na utasikika mpaka wapi; vilevile hatujui vizuri uvuvio wa Kimungu unaanzia wapi, na utatufikishia ngazi gani ya ukamilifu tukiufuata kwa uaminifu. Tusiwe kama wanamaji wazembe wasiotweka tanga wakati wa kufaa.

Vipaji *vinatofautiana* na maadili kama wanavyotofautiana wanaoviongoza, yaani Roho Mtakatifu na akili iliyoangazwa na imani; hiyo ni miongozo na *kanuni tofauti*. Utendaji wa kibinadamu unafuata kanuni ya kibinadamu, utendaji upitao maumbile unafuata kanuni ya Kimungu, yaani uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hata busara iliyoinuliwa na upendo inatenda kwa kuzingatia mifuatano ya mawazo, tofauti na kipaji cha shauri kinachotuandaa kupokea uvuvio maalumu usioihitaji. Kwa mfano, tukiuliziwa siri fulani, busara inasita kuona namna ya kutunza siri hiyo bila ya kusema uongo, kumbe uvuvio wa Roho Mtakatifu unaondolea wasiwasi (taz. Math 10:19). Vilevile, imani *inaambatana* tu na kweli tulizofunuliwa, kumbe kipaji cha akili kinatuwezesha *kuona* vilindi vya kweli hizo, na kile cha hekima kinatuwezesha *kuonja* utamu wake.

2° *Vipaji vya Roho Mtakatifu ni vya lazima kwa wokovu wa milele.* “Maana Mungu humpenda yeye tu akaaye na Hekima” (Hek 7:28). “Miongoni mwa ndugu awatawalaye ana heshima, bali machoni pa Bwana ni wao wamchao” (YbS 10:20). Sasa kipaji bora ni hekima, na cha mwisho ni uchaji wa Mungu.

Maadili ya Kimungu yanajilinganisha na *namna ya kibinadamu* ya akili na utashi wetu, na hivyo yanatuacha katika hali isiyotosha kwa lengo letu kuu lipitalo maumbile, ambalo tunahitaji kulijua kwa namna hai, ya kuchimba na kuonja, na ambalo tunatakiwa kulilenga kwa ari zaidi. Imani hata ikiwa kubwa inaendelea kuwa na upungufu kwa sababu tatu za msingi: 1) yale inayoyaamini ni giza kwake, haiyaoni moja kwa moja, ila “kwa kioo kwa jinsi ya fumbo” (1Kor 13:12); 2) inayafikia kwa njia ya matamko mbalimbali ya Kanisa, kumbe Mungu ni sahili kabisa; 3) inayafikia kinadharia, kwa kukiri au kukanusha maneno fulanifulani, kumbe Mungu aliye hai anatakiwa kujulikana kama kwa mang'amuzi. Tumaini linashiriki upungufu wa imani, na vilevile upendo, kwa kuwa imani ndiyo inayoupatia la kupenda. Zaidi tena busara ina upungufu, kwa kuwa inahitaji kufuata mawazo, kutafuta sababu za kutenda, ili kuelekeza maadili ya kiutu; mara nyingi inasita isijue la kufanya, ikihitaji mwanga kutoka juu, k.mf. ili kushinda vishawishi visivyotambulikana au vikali na vya muda mrefu.

“Akili ya binadamu, hata baada ya kukamilishwa na maadili ya Kimungu, haiwezi kujua yale yote inayohitaji kuyajua, wala haiwezi kuepuka kila upotovu. Mungu tu aliye na ujuzi wote na enzi zote anaweza kufidia ujinga na upumbavu, ugumu wa moyo na kasoro nyinginezo tulizo nazo. Ili kutuondolea kasoro hizo tumejaliwa vipaji vya Roho Mtakatifu, vinavyotuwezesha kupokea vizuri uvuvio wa Kimungu... Kwa njia ya maadili ya Kimungu na ya kiutu, binadamu hajakamilika kuhusu lengo lake kuu linalopita maumbile asihitaji daima kusukumwa na Roho Mtakatifu kutoka juu”. Haja hiyo ni ya kudumu, ndiyo sababu vipaji ni misimamo ya kudumu tunayomiminiwa.

Sisi *tunatumia* vipaji kwa mfano wa utiifu, ili kupokea na kutekeleza vizuri agizo kutoka juu, lakini hatuwezi kuwa na uvuvio huo kila tunapotaka. Upande huo vipaji vinatufanya tusitende wenyewe, bali kwa Roho Mtakatifu. Hivyo ni wazi kuwa vipaji, kama vile utiifu, ni misimamo ya kudumu ya mwadilifu.

Tunaweza kuona vizuri zaidi tunavyovihitaji, tukizingatia jinsi kila kimoja kinavyokamilisha akili au utashi na hisi:

| | | | | **KIPAJI** | **ADILI** |
|---|---|---|---|---|---|
| Vipaji vinakamilisha | akili iliyoangazwa na imani | ili kupenya ukweli | | akili | imani |
| | | ili kuamua kuhusu | mambo ya Mungu | hekima | upendo |
| | | | mambo yetu | shauri | busara |
| | | | malimwengu | elimu | tumaini |

| | | | |
|---|---|---|---|
| utashi na hisi | ili tumuabudu Mungu ipasavyo | ibada | ibada |
| | ili tusiogope hatari | nguvu | nguvu |
| | ili tushinde tamaa mbaya | uchaji | kiasi |

3° Kwa kuwa vipaji ni vya lazima kwa wokovu, *vinashikamana na upendo*. Roho Mtakatifu haji ndani mwetu pasipo vipaji vyake, ambavyo vinaendana na upendo na kupotezwa pamoja nao kwa dhambi yoyote ya mauti. Basi, vipaji ni sehemu ya muundo wa Kiroho wa neema inayotia utakatifu, ambayo kwa sababu hiyo inaitwa "neema ya maadili na vipaji". Kama vile maadili ya kumiminiwa yanavyokua pamoja kwa mfano wa vidole vya mkono, vipaji pia vinakua pamoja. Hakuna mwenye *kiwango kikubwa cha upendo wa Mungu,* inavyotakiwa na ukamilifu, asiye na *vipaji vya Roho Mtakatifu kwa kiwango hichohicho*.

Tutauzungumzia mbele usikivu kwa Roho Mtakatifu, lakini tangu sasa tunaona thamani ya huo muundo wa Kiroho ambao ni *chanzo cha uzima wa milele.* Ni thamani kubwa kuliko ile ya macho, ya afya na ya akili kwa maana mwadilifu akipotewa navyo hapotewi na hazina hiyo ambayo kifo chenyewe hakiwezi kumnyang'anya. Ni thamani kubwa kuliko ile ya karama (kufanya miujiza n.k.) kwa kuwa hizo ni alama za nje tu ambazo zinaweza kuelekeza njia ya kumfikia Mungu, lakini haziwezi kutuunganisha naye inavyofanya neema ya utakaso.

## 1.3.5. *NEEMA ZA MSAADA NA AINA ZAKE*

Ili tuelewe zaidi utendaji wa muundo wa Kiroho, tuone neema za msaada zinavyohitajika ili tutekeleze maadili na vipaji.

### HAJA YA NEEMA ZA MSAADA

Hakuna kiumbe kinachotenda pasipo nguvu ya Mungu, aliye chanzo cha utendaji wote wa miili na wa roho: "Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu" (Mdo 17:28). Zaidi upande wa maisha yapitayo maumbile, ili tutende kwa maadili ya kumiminiwa na kwa vipaji, tunahitaji *msukumo wa Kimungu* unaoitwa *neema ya msaada*. Ni ukweli wa imani kwamba pasipo neema hiyo hatuwezi kujiandaa kuongoka, wala kudumu muda mrefu katika kutenda mema, hasa kudumu mpaka kufa katika neema inayotia utakatifu. Pasipo neema ya msaada hatuwezi kuzaa hata tendo dogo linalostahili wokovu, wala zaidi hatuwezi kuufikia ukamilifu. Kwa hiyo Yesu alisema, "Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote" (Yoh 15:5). "Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu" (2Kor 3:5). "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Fil 2:13), akisukuma hiari yetu bila ya kuilazimisha. Ndiye anayetujalia tujiandae kupokea neema ya utakaso na halafu kustahili uzima wa milele.

Ndiyo sababu tunapaswa kusali daima. *Haja ya kusali inatokana na haja ya kupata neema za msaada*. Mbali na neema ya kwanza tunayojaliwa pasipo kuiomba (kwa kuwa ndiyo chanzo cha sala), sala ndiyo njia *ya kawaida, ya hakika na ya jumla* ambayo Mungu anataka tupate neema tunazozihitaji. Bwana ametusisitizia, *"Ombeni,* nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa" (Math 7:7-8). Kuna haja hiyo hasa katika kishawishi: "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu" (Math 26:41). Tunaposali tunapaswa kuamini kuwa Mungu ndiye asili ya mema yote, kwa hiyo tegemeo lolote lisilo na msingi katika sala ni la kipumbavu tu.

*"Mungu haagizi kamwe yasiyowezekana*, bali akiagiza anatuambia tufanye tunayoyaweza, tuombe tusiyoyaweza, naye mwenyewe anatusaidia ili tuweze" (Mtaguso wa Trento); tena kwa neema anatusaidia kusali pia. Kuna neema kadhaa tusizoweza kuzipata isipokuwa kwa kusali.

Haitatosha kamwe kusisitiza jambo hilo, kwa kuwa wengi mwanzoni wamejaa mawazo ya kibinadamu tu, wakidhani wanaweza kufanya lolote kwa utashi na bidii, pasipo neema za msaada. Watang'amua mapema ukweli wa maneno ya Yesu na ya Mt. Paulo, na kwamba tunapaswa kuomba ili tushike vizuri zaidi na zaidi amri za Mungu, hasa ile kuu ya upendo.

### AINA ZA NEEMA ZA MSAADA

Neema za msaada zina namna nyingi tofauti ambazo inafaa kuzijua, kwa kukumbushwa wazi iwezekanavyo kweli kadhaa ambazo ni za hakika, ingawa zinatokeza fumbo mojawapo la imani ambalo kuliko mengine mengi lina mchanganyiko wa mwanga na giza kwetu.

Mara nyingi tunapewa *neema ya mwanga,* k.mf. wakati wa masomo ya misa tunaangaziwa kwa ndani maana yake. Hiyo inafuatwa na *neema ya mvuto,* yaani tunavutiwa na tendo fulani, k.mf. katika kuzingatia Mwokozi anavyotupenda, tunajisikia kumrudishia upendo. Neema ya namna hiyo inatenda katika utashi na kuusukuma upendo hata kujitoa kwa Mungu, tayari kupokea mateso yoyote na kufa kwa ajili yake. Hapo si neema ya mvuto tu, bali *neema ya nguvu* ambayo mara nyingi tunaipokea pasipo kuing'amua, lakini inatuwezesha kustahimili ukavu wa roho. Hata neema nyingine nyingi tunazozipokea hatuzitambui, kwa kuwa zinapita maumbile, hivyo zinapita njia zetu za kujua mambo.

Neema ya msaada inayogusa utashi inaweza kuuathiri kwa namna mbili: *kwa kuupendekezea jambo* ambalo liuvutie, na *kwa kuusukuma kwa ndani*. Bila ya shaka Mungu anaweza kuelekeza utashi wetu kwenye uadilifu kwa kuupendekezea jambo fulani, k.mf. heri ya milele, au ustawi wa upendo. Ndivyo mama anavyomvuta mtoto wake atende mema; hata malaika mlinzi anaweza kufanya hivyo kwa kututia mawazo mazuri. Lakini Mungu tu anaweza kuusukuma kwa ndani utashi wetu utende mema. Mungu yumo ndani mwetu kuliko nafsi yetu, akidumisha roho yetu, pamoja na akili na utashi alivyoviumba; ndiyo sababu anaweza kuvisukuma kwa ndani kadiri ya maelekeo ya maumbile aliyovipatia, si kwa kuvilazimisha bali kwa kuvitia nguvu mpya. Mama akitaka kumfundisha mtoto atembee anamsaidia sio tu kwa sauti, huku akimuonyesha kitu ambacho akifikie, bali pia kwa mikono akimuinua. Mungu anaweza kufanya hivyo upande wa roho, akiinua utashi wetu ufikie uadilifu. *Ndiye Muumba wa utashi,* aliyeuelekeza ulenge uadilifu, *naye peke yake anaweza kuusukuma kwa ndani kadiri ya elekeo hilo.* Ndivyo anavyotenda ndani mwetu akitufanya tutake na kutenda. Atafanya hivyo kadiri tutakavyomuomba kwa ukakamavu atustawishie upendo tunaopaswa kuwa nao kwake.

Neema ya msaada inaitwa *ya kutangulia* ikisababisha ndani mwetu wazo jema au mguso mwema, kabla hatujafanya lolote kusababishia kitu hicho. Tusipoikaidi Mungu atatuongezea neema *ya kuchangia* itakayousaidia utashi wetu kutekeleza tendo linalohitajika ili kutimiza mpango wetu mzuri.

Mungu anatusukuma, mara *kutenda kufuatana na uamuzi* tulioukata kwa utaratibu wa kibinadamu, mara *kutenda kwa uvuvio maalumu* kutoka juu, bila ya sisi kukata shauri kwa utaratibu huo. Mfano wa namna ya kwanza ni pale ninapoamua kwenda kusali rozari saa niliyozoea kufanya hivyo; hapo natenda kwa neema ya msaada ya kawaida inayoitwa *ya kushiriki tendo* kwa kuwa inashirikiana nami katika kutenda kwa kuamua kibinadamu. Mfano wa namna ya pili ni pale ambapo ghafla, wakati wa kazi nzito, najisikia kusali, nami nafanya hivyo mara: neema hiyo inaitwa *ya kutenda*, kwa kuwa inatenda ndani mwangu pasipo mimi kukata shauri, ingawa nakubali kwa hiari na kustahili tuzo. Kwa namna ya kwanza Mungu anatusukuma kutenda *namna ya kibinadamu ya maadili*. Kwa namna ya pili anatusukuma kutenda *namna ipitayo utu ya vipaji vya Roho Mtakatifu;* hapo chombo chetu kinakwenda si kwa kasia tu, bali kwa msukumo wa upepo: tunatendewa kuliko kutenda wenyewe, na kazi yetu hasa ni kukubali ile ya Mungu, kuacha Roho Mtakatifu atuongoze, kufuata mara na kwa juhudi uvuvio wake wowote. Lakini hata tukiwa na neema ya kushiriki tendo tu, kila tendo linalostahili tuzo ni *lote* la Mungu kama asili kuu, na *lote* la kwetu kama asili ya pili.

**UAMINIFU KWA NEEMA**

Ni muhimu tuwe waaminifu kwa neema, tena kuwa waaminifu zaidi na zaidi kwa neema ya msaada ya sasa hivi, ili tutimize wajibu wa dakika hiyo unaotudhihirishia matakwa ya Mungu kwetu. Tukumbuke maneno ya Mt. Augustino, "Aliyekuumba pasipo wewe, hatakufanya mwadilifu pasipo wewe" kwa kuwa lazima ukubali na kuzitii amri. Tunasaidiwa na Mungu si kusudi tusifanye chochote, bali kusudi tutende kwa kustahili wokovu. Yeye anatutolea mfululizo neema za msaada ili tutimize wajibu wa sasa hivi, kama vile hewa inavyoyafikia mapafu yetu tuweze kupumua kila nukta. Kama tunavyotakiwa kuingiza hewa inayosafisha damu, tunatakiwa pia kupokea kwa mikono miwili neema inayozifanya mpya nguvu zetu za Kiroho ili tumuelekee Mungu. Kama vile asiyepumua anakufa, vivyo hivyo roho isiyopokea neema inakufa kwa kukosa hewa yake.

"Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure" (2Kor 6:1). Tunapaswa kuiitikia na kushirikiana nayo kwa bidii. Ndio ukweli mwepesi ambao tukiutekeleza siku hadi siku utatufikisha kwenye utakatifu. Kwa hakika Mungu ndiye wa kwanza kupiga hatua kwetu kwa neema ya kutangulia, halafu anatusaidia kuikubali; anatuongoza katika njia zetu zote hadi saa ya kufa. Upande wetu tunapaswa kuwa waaminifu. Namna gani? Mosi kwa kupokea kwa furaha mianga ya kwanzakwanza; halafu kwa kufuata kwa makini maelekezo yake; hatimaye kwa kufanya juu chini kuyatekeleza, bila ya kujali gharama. Hapo tutashiriki kazi ya Mungu, na utendaji wetu utakuwa tunda la neema yake na papo hapo la hiari yetu.

Neema ya kwanza inayotutia wazo jema *inatosha* kufanya utashi ukubali kutenda kwa adilifu, kwa maana inatupa uwezo wa kulitekeleza. Lakini tukikaidi wazo hilo tunajinyima neema ya msaada ambayo *ingesababisha kwa hakika* tulikubali. Ukaidi unaangukia neema ya kutosha kama mvua ya mawe inavyonyeshea maua yanayotarajiwa kuzaa matunda mengi: maua yakiangamizwa, matunda hayataundwa kamwe. Neema ya hakika inatolewa kwetu katika ile ya kutosha kama tunda katika ua; ni lazima tusiangamize ua ili tupate tunda. Tusipoikaidi neema ya kutosha tutapewa ile ya hakika na kwa njia yake tutaendelea bila ya wasiwasi katika njia ya wokovu. Hivyo neema ya kutosha inatuzuia tusijisingizie, na ile ya hakika haituruhusu tujivunie; kwa njia yake tunasonga mbele kwa unyenyekevu na juhudi.

Ndilo fumbo la neema ambalo mwanga wake umo katika kweli mbili, wakati giza lake limo katika namna ya kuzilinganisha. Upande mmoja Mungu *haagizi kamwe yasiyowezekana* (angekuwa hana haki wala huruma), bali kwa upendo *anawawezesha kweli wote* watimize wajibu wao. Hakuna mtu mzima anayenyimwa neema ya lazima kwa wokovu asipoikataa kwa kukaidi mwaliko wa Mungu. Upande mwingine, *"kwa kuwa upendo wa Mungu kwetu ni asili ya mema yote, hakuna mtu anayeweza kuwa mwema kuliko mwingine asipopendwa zaidi na Mungu"* (Mt. Thoma wa Akwino). Kwa maana hiyo Yesu alisema kuhusu

wateule, “Hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu” (Yoh 10:29). “Ikiwa baadhi wanaokolewa ni kwa zawadi ya Mwokozi: ikiwa wengine wanapotea ni kwa kosa lao” (Mtaguso wa Quiercy wa mwaka 853). Kukaidi neema ni ovu linalotokana na sisi wenyewe tu; *kutoikaidi ni jema* linalotokana na Mungu, chemchemi ya mema yote. Ndiyo sura mbili za fumbo lilelile; kila moja ni la hakika, kama lile la kwamba wote wanaweza kuokoka, na lile la kwamba mtu akiwa bora kuliko mwenzake ni kwa sababu amependwa zaidi na Mungu. Lakini hakuna kiumbe anayeweza kuona hayo mawili yanavyolingana kabla hajamuona Mungu mbinguni, kwa sababu ni sawa na kuona jinsi haki isiyo na mipaka, huruma isiyo na mipaka, na hiari yake kuu *zinavyolingana katika ukuu wa Umungu*.

Tusikatae ukarimu wa Mungu ambaye ametujalia neema ya maadili na vipaji, tena kila siku anatuvuta kwake. Tusiridhike na maisha ya wastani na kuzaa matunda yasiyoiva, wakati Mwokozi wetu mwema alisema, “Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele” (Yoh 10:10) hadi kufurahia milele heri yake. Mungu ana moyo mkuu, basi tuwe nao sisi pia.

Uaminifu huo unahitajika kwanza ili *kutunza* uzima wa neema, na kukwepa dhambi ya mauti. Uzima huo una thamani isiyo na kifani, hata Mwokozi alikabili kifo ili kuturudishia. Tungejaliwa kuona wazi mng'ao wa ajabu wa neema inayotia utakatifu, tungejisahau. Uaminifu unahitajika pia ili tustahili na *kupata ustawi* wa uzima huo, unaotakiwa kukua mpaka tutakapoingia mbinguni, kwa sababu tunapohiji kuelekea umilele tunasonga mbele kwa kukua tu katika upendo wa Mungu.

Kwa hiyo tunahitaji *kutakasa matendo yetu yote, hata ya kawaida zaidi*, tukiyatenda kwa nia safi na kwa lengo lipitalo maumbile. Tungekuwa waaminifu saa zote, siku zetu zingejaa na kufurika matendo ya upendo kwa Mungu na kwa jirani, katika nafasi yoyote, ya furaha na ya uchungu, na kufikia jioni muungano wetu na Mungu ungekuwa wa dhati na imara zaidi. Kwa yeyote hakuna njia rahisi na ya hakika ya kupata utakatifu kuliko ile ya kuinua kila tendo juu ya maumbile, kwa kumtolea Mungu pamoja na Yesu, kwa utukufu wake na kwa wokovu wa watu.

## 1.4. *UWEMO WA UTATU MTAKATIFU NDANI MWETU, CHEMCHEMI ISIYOUMBWA YA MAISHA YA KIROHO*

Tuzingatie sasa chemchemi isiyoumbwa ya maisha ya Kiroho, yaani Utatu mtakatifu uliomo ndani ya waadilifu wote wa duniani, toharani na mbinguni.

### USHUHUDA WA MAANDIKO MATAKATIFU

*Mungu yumo katika viumbe vyote* kwa kuwa hana mipaka: “Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko” (Zab 139:7-8). “Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi… hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu” (Mdo 17:24-28). Kwa hakika, Mungu anaona vyote, anadumisha vyote, na kukiongoza kila kiumbe kitende jinsi inavyokifaa.

Lakini Maandiko yanasema pia juu ya uwemo wa pekee wa Mungu katika waadilifu. “Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi *tutakuja* kwake, na kufanya makao kwake” (Yoh 14:23). Hayatakuja tu mambo yaliyoumbwa (kama vile neema inayotia utakatifu, maadili ya kumiminiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu), bali watakaokuja ni walewale wanaopenda, Baba na Mwana wasiotenganika na Roho Mtakatifu, ambaye Bwana alimuahidi na kumtuma wazi kwenye Pentekoste: “Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili *akae nanyi hata milele…* Ndiye Roho wa kweli… anakaa kwenu, naye atakuwa *ndani yenu*…” (Yoh 14:15-17). Hao watakuja si kwa muda, bali *watafanya makao yao ndani ya mwadilifu* mpaka atakapodumu katika upendo. Maneno hayo hayakuwahusu mitume tu: “Mungu ni upendo, naye *akaaye katika pendo*, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake” (1Yoh 4:8). Huyo anaye Mungu moyoni mwake, lakini hasa Mungu anaye huyo ndani mwake akimdumishia sio tu uhai wa kimaumbile, bali pia ule mpya wa neema na upendo. “Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na *Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi*” (Rom 5:5). Hatukujaliwa tu upendo ulioumbwa, bali Roho Mtakatifu aliye Upendo-Nafsi. Hao wamo ndani mwetu, lakini tutafananishwa nao kikamilifu kwa kupokea tu mwanga wa utukufu. “Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?... Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe” (1Kor 3:16; 6:19). Hivyo Maandiko yanafundisha wazi kuwa Nafsi tatu za Mungu zinaishi katika waadilifu wote.

### USHUHUDA WA MAPOKEO

Mwanzoni mwa karne II, Mt. Inyasi wa Antiokia aliwaita Wakristo halisi “waleta Mungu” kwa sababu wanaye ndani mwao. Mt. Lusia alikiri ukweli huo mbele ya mahakimu, “Ndio, wale wote wanaoishi kwa usafi na imani ni mahekalu ya Roho Mtakatifu”. Mt. Atanasi alisema kuwa Nafsi tatu za Mungu zimo ndani mwetu. Mt. Bazili Mkuu alitamka kuwa Roho Mtakatifu kwa kukaa ndani mwetu anatufanya tuwe watu wa Kiroho zaidi na kufanana na Mwana Pekee. Mt. Sirili wa Aleksandria pia alisema juu ya muungano huo wa ndani kati

ya mwadilifu na Roho Mtakatifu. Upande wa magharibi, Mt. Ambrosi alifundisha kuwa tumempata katika ubatizo na zaidi katika kipaimara. Mt. Augustino alithibitisha kwa shuhuda za mababu waliomtangulia kwamba hatupewi neema tu, bali tunajaliwa Mungu mwenyewe, yaani Roho Mtakatifu.

Ukweli huo uliofunuliwa unawekwa na Ualimu wa Kanisa machoni petu tena. Mtaguso wa Trento umesema, "Anayetufanya waadilifu ni Mungu ambaye kwa huruma yake anatutakasa bure na kutufanya watakatifu, akitupaka mafuta na kututia mhuri wa Roho Mtakatifu tuliyeahidiwa ambaye ni dhamana ya urithi wetu (taz. Ef 1:13-14)". Leo XIII alifafanua zaidi, "Inafaa sana kukumbuka maelezo yaliyotolewa na walimu wa Kanisa kadiri ya mafundisho ya Maandiko matakatifu: Mungu yumo katika vitu vyote *kwa uwezo wake*, kwa sababu vyote viko chini yake; halafu *kwa uwepo wake*, kwa sababu vyote viko wazi mbele yake; tena *kwa undani wake*, kwa sababu yumo ndani ya viumbe vyote kama chanzo cha uwepo wao. Lakini katika binadamu Mungu hayumo tu kwa namna ile ambayo yumo katika vitu vyote, bali zaidi *kwa kujulikana na kupendwa naye*, kwa sababu umbile letu wenyewe linatufanya tupende, na kutamani na kufuata yaliyo mema. *Kwa neema yake Mungu anakaa katika roho adilifu kama hekaluni kwa namna ya ndani na ya pekee kabisa.* Ndipo kinapotokea kile kiungo cha upendo kinachofungamanisha roho na Mungu kuliko mtu na rafiki yake mkuu na kinachoifanya imfurahie kwa ukamilifu wote. Muungano huo wa ajabu, ambao unaitwa *uwemo ndani* na unatofautiana na hali ya wenye heri wa mbinguni kwa namna yake tu, unasababishwa kwa ukweli wote na uwemo wa Utatu mzima: 'tutakuja kwake, na kufanya makao kwake' (Yoh 14:23). Hata hivyo unasemwa kuwa ni hasa kazi ya Roho Mtakatifu, kwa kuwa tunaona alama za uwezo na za hekima ya Mungu hata katika mtu mwovu, lakini mwadilifu tu anashiriki *upendo*, ambao ni *sifa ya Roho Mtakatifu*... Wingi wa mema ya kimbingu unaosababishwa na uwemo wa Roho Mtakatifu katika roho adilifu unajitokeza kwa namna mbalimbali... Kati ya zawadi hizo zimo tahadhari za siri, na mialiko ya kifumbo ambavyo roho zinajaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu, na ambavyo visipokuwepo hatuwezi kujitahidi katika maadili, wala kuendelea, wala kufikia wokovu wa milele".

**UFAFANUZI WA TEOLOJIA KUHUSU FUMBO HILO**

"Mbali ya neema inayotia utakatifu hakuna linaloweza kuangaza jambo hilo, kwamba Nafsi ya Kimungu imo ndani mwetu kwa namna mpya... Ili *tuwe nayo* ni lazima tuweze *kuifurahia* na kuitumia. Sasa hatuwezi kufurahia Nafsi ya Kimungu isipokuwa kwa neema inayotia utakatifu na upendo" (Mt. Thoma wa Akwino). Pasipo hayo Mungu *hakai* ndani mwetu. Haitoshi kumjua kimaumbile (kama mwanafalsafa), wala kwa imani iliyokufa (kama Mkristo mwenye dhambi ya mauti). Ni lazima *tumjue kwa imani hai na vipaji vya Roho Mtakatifu* vinavyohusiana na upendo. Hiyo namna ya mwisho ya kumjua Mungu *inampata* si kama jambo la mbali lililochorwa tu kwetu, bali *kama jambo ambalo lipo*, tunalo na tunaweza *kulifurahia* tangu sasa. Ili Nafsi za Kimungu *zikae* ndani mwetu, inatakiwa *tuweze* kuzifahamu kama kwa *mang'amuzi ya kimapenzi*, ambayo msingi wake ni upendo tuliomiminiwa *unaotulinganisha* na maisha ya ndani ya Mungu.

Ili akae ndani mwetu si lazima tumjue hivyo *kila nukta*; inatosha *tuweze* kufanya hivyo kwa neema ya maadili na vipaji. Basi uwemo wa Utatu mtakatifu katika mtu mwadilifu unadumu hata usingizini mpaka atakapodumu katika neema inayotia utakatifu. Ila mara mojamoja inatutokea kumtambua Mungu kama kiini cha roho yetu na uhai wa maisha yetu: "Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, 'Aba!' yaani, 'Baba!' Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Rom 8:15-16). "Roho Mtakatifu anathibitishia roho yetu kwa kusababisha ndani mwetu *upendo kama wa mwana* kwa baba" (Mt. Thoma wa Akwino). Upendo huo ni ishara inayotutia hakika fulani ya kwamba tuna neema inayotia utakatifu.

Basi, kwa namna fulani Utatu mtakatifu unakaa katika roho adilifu vizuri kuliko Yesu anavyokaa katika maumbo ya ekaristi, kwa kuwa yeye yumo kweli katika maumbo hayo, lakini yenyewe hayamjui wala hayampendi. Kumbe Utatu mtakatifu umo ndani ya mwadilifu kama katika hekalu hai linaloujua na kuupenda (kwa kiasi tofautitofauti). Umo katika wenye heri wa mbinguni wanaoutazama moja kwa moja, hasa ndani ya roho ya Mwokozi ambayo Neno ameungana nayo katika Nafsi moja. Kuanzia dunia hii, katika mwanga/giza la imani, Utatu mtakatifu unakaa ndani mwetu, ingawa hatuuoni, ukizidi kutuuhisha hadi saa ya kuingia utukufu. Uwemo huo hautuondolei haja ya kukaribia ekaristi, kwa kuwa Utatu mtakatifu unakaa ndani ya Kristo kuliko unavyokaa ndani mwetu. Ikiwa ni faida kumkaribia mtakatifu wa Mungu, jinsi gani tutafaidika tukimkaribia Mwanae!

**YATOKANAYO KWA MAISHA YA KIROHO**

Ikiwa uwemo wa Utatu mtakatifu ndani mwetu *unatuwezesha kumjua Mungu kama kwa mang'amuzi*, maana yake ujuzi huo si jambo la pekee (kama njozi) bali lipo katika njia ya kawaida ya utakatifu. Ujuzi huo unatokana na *imani iliyoangazwa na vipaji vinavyohusiana na upendo*. Kama ni hivyo, unatakiwa kustawi kadiri upendo unavyostawi. Tutaona kuwa sala ya kumiminiwa, ambayo ni kuchanua kwa aina hiyo ya ujuzi/mang'amuzi, inaanza katika hatua ya mwanga na kukamilika katika hatua ya muungano. Ujuzi huo wa Mungu na wa wema wake utakua pamoja na ule wa unyonge wetu. Jambo lingine linalotokana na hayo tuliyosema ni kwamba upendo uliomo ndani mwetu unapostawi sana, *Nafsi za Kimungu zinakuwemo mwetu*

*kwa undani zaidi*, yaani kirafiki zaidi: ndivyo inavyotokea k.mf. wakati wa uongofu wa pili ambao ni mwanzo wa hatua ya mwanga. Hatimaye hao Watatu wamo ndani mwetu sio tu kusudi tuwafahamu na kuwapenda kwa namna ipitayo maumbile, bali wamo kama *asili ya vitendo vinavyopita maumbile,* kama Yesu alivyosema, "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi" (Yoh 5:17), hasa katika kiini cha roho.

Lakini kiutendaji tukumbuke kwamba kwa kawaida Mungu anajitoa kwa kiumbe kadiri huyo alivyo tayari kumpokea. Mtu akiwa safi zaidi, ndani mwake Nafsi za Kimungu zinakuwemo na kufanya kazi zaidi. Hapo *Mungu ni wetu nasi ni wake*, na tunatamani kuliko yote tuendelee katika upendo wake. "Hilo ni mojawapo kati ya mambo yanayotusukuma zaidi kuendelea Kiroho, kwa sababu linaifanya roho iwe daima na juhudi kwa maendeleo yake, iwe macho ili kuzaa mfululizo vitendo vyenye nguvu na motomoto zaidi na zaidi kuhusu maadili yote, ili kwa kukua katika neema, ustawi huo umlete upya Mungu ndani mwake… kwa ajili ya muungano wa ndani zaidi, wa kudumu zaidi na imara zaidi" (L. Chardon).

**TUNA WAJIBU GANI KWA MGENI WETU WA KIMUNGU?**

Mgeni huyo anatuambia, "Mwanangu, nipe moyo wako" (Mith 23:26). "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (Ufu 3:20). Mwadilifu anafanana na mbingu, kwa sababu Utatu mtakatifu umo ndani mwake, lakini bado ana giza mpaka atakapojaliwa kuuona waziwazi ndani mwake.

Kwa kifupi wajibu wetu kwake ni kama ifuatavyo: kumfikiria mara nyingi, kwa kujiambia, "Mungu anaishi ndani mwangu". Kumwekea wakfu siku zetu, tena kila saa, kwa kusema, "Kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu". Kukumbuka alivyo chemchemi ya mwanga, ya faraja na ya nguvu kwetu. Kumuomba kadiri ya neno la Bwana: "Wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi" (Math 6:6). Kumuabudu kwa kusema, "Moyo wangu wamwadhimisha Bwana, na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu" (Lk 1:46-47). Kumuamini, kumtumainia, kumpenda kwa upendo unaozidi kuwa safi, mkarimu, wenye nguvu. Kumpenda kwa kumuiga hasa katika wema: "Basi iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma" (Lk 6:36). "Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu" (Yoh 17:21).

Hayo yote yanatuonyesha kwamba *maisha ya Kiroho upande wa mafumbo* (ambapo mang'amuzi ya Mungu kuwemo ndani mwetu ni ya sasa hivi) si ya pekee, bali *ni ukamilifu wa kawaida. Watakatifu tu,* ambao wanayo kwa kiasi kikubwa, *wapo kweli wanapotakiwa*. Kabla hatujafikia muungano huo wa ndani na Mungu, sisi ni kama *tumesinziasinzia*: bado fumbo tamu la uwemo wake tunalijua kijuujuu, kumbe ndio uzima tele tuliokaribishwa; hatujamuabudu wala kumpenda Mungu inavyotakiwa, na pengine tunahesabu kile ambacho pekee ni cha lazima kana kwamba si muhimu kuliko vyote; vilevile hatujaelewa kwa undani ukuu wa zawadi tuliyopewa katika ekaristi, wala Mwili wa fumbo wa Kristo ni nini.

Roho Mtakatifu ndiye anayehuisha Mwili wa fumbo ambao Yesu ndiye kichwa chake. Kama vile roho nzima imo katika mwili wote na katika kila kiungo, nayo inafanya kazi bora kichwani, vivyo hivyo Roho Mtakatifu yumo mzima katika Mwili wote wa fumbo, naye anafanya kazi bora ndani ya Mwokozi na kwa njia yake kwetu pia. *Kiini cha uhai* kinachounganisha hivyo Mwili wa fumbo *kina nguvu ya kuunganisha* kuliko roho inavyounganisha mwili wake, na kuliko umoja wa familia au taifa fulani. Hivyo vinaunganishwa tu na namna fulani ya kutazama, kupima, kuhisi, kupenda, kutaka na kutenda. Roho anayeunganisha Mwili wa fumbo ana nguvu pasipo mfano, kwa kuwa ni Roho aletaye utakatifu, ni chemchemi ya maji hai yanayobubujikia uzima wa milele. Mto wa neema zote unaotokana naye unapanda juu tena umrudie Mungu kama ibada, sala, stahili na sadaka. Ndiyo mambo yapitayo maumbile tunayopaswa kuyajua zaidi na zaidi. *Upande wa mafumbo tu ndipo roho inapozinduka na kutambua zawadi ya Mungu ilivyo, kwa namna ile hai, ya ndani na angavu* tunayohitaji ili kumrudishia kikamilifu upendo alio nao kwetu.

## 1.5. *KRISTO MKOMBOZI ANAVYOATHIRI MWILI WAKE WA FUMBO*

Tumeona jinsi Utatu mtakatifu uliomo ndani ya kila mwadilifu ulivyo chemchemi isiyoumbwa ya maisha ya Kiroho. Lakini utakatifu wetu unategemea pia nguvu zinazomtoka mfululizo Kristo Mkombozi ambaye, kwa njia ya sakramenti na hata nje ya hizo, anatushirikisha neema alizotustahilia alipoishi duniani, na kwa namna ya pekee wakati wa mateso. Basi, tuongelee nguvu hizo zinazotuletea utakatifu hasa kwa njia ya sakramenti kuu kuliko zote.

**JINSI MWOKOZI ANAVYOTUSHIRIKISHA NEEMA ALIZOTUSTAHILIA**

Anafanya hivyo kama chombo hai kilichounganika moja kwa moja na umungu, chemchemi ya neema zote. "Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema" (Yoh 1:16). Mwenyewe ametuambia, "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi; akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana *pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote…* Ninyi

mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu" (Yoh 15:4-8).

Mt. Paulo alitoa mfano mwingine wa kushangaza, akisema Kristo ni *kama kichwa* kinachovishirikisha viungo vyote uhai wa roho; *Kanisa ndio mwili wa fumbo wa Kristo*, na Wakristo ndio viungo vya mwili huo. "Ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake" (1Kor 12:27). "Tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu mojamoja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo" (Ef 4:15-16).

Kufuatana na hayo, Mwokozi anatushirikisha nguvu hai za neema kama vile kichwa kinavyovishirikisha viungo vyake uhai ambao roho ndiyo asili yake. Ili tuelewe vizuri tunapaswa kutofautisha umungu na ubinadamu wa Kristo. Kama *Neno* yeye anakaa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu katika kiini cha roho yetu akiidumishia uzima wa kimaumbile na ule upitao maumbile; anaiongoza kufanya yale isiyoweza kufanya peke yake. *Ubinadamu* wa Mwokozi ndio chombo kilichounganika na umungu moja kwa moja ambacho tunashirikishwa neema zote; haukai rohoni mwetu, kwa kuwa mwili wake hauwezi kuwemo rohoni mwetu, ila uko mbinguni kwa namna ya mwili na umo katika ekaristi kwa namna ya sakramenti. Hata hivyo roho adilifu inapokea mfululizo nguvu za ubinadamu wa Yesu, kwa sababu kila neema inatolewa kwa njia yake tu. Kwa kuwa kila nukta tuna wajibu fulani, ubinadamu wake unatushirikisha neema ya msaada ya sasa hivi, kama vile hewa inavyoingizwa mfululizo mapafuni.

Mungu, asili ya neema, anatumia ubinadamu wa Mwokozi ili kutujalia neema, kama vile mwanamuziki bora anavyotumia ala ili kutushirikisha aliyonayo moyoni, au mwanafalsafa bora anavyotumia ufasaha wa lugha ili kutokeza mawazo yake. Ubinadamu wa Yesu ni chombo bora, chenye kujua na kutaka kutumika, kilichounganika moja kwa moja na umungu ili kutushirikisha neema zote tunazojaliwa, ambazo zote alitustahilia msalabani. Kwake zinatoka neema zote za mwanga, mvuto, faraja na ushujaa, tunazozihisi na tusizozihisi. Ni nguvu ya mfululizo ambayo anachangia kila tendo linalostahili wokovu kuliko mama bora anavyoweza kumsaidia mwanae anapomfundisha kusali. Utendaji huo wa Mwokozi unawashirikisha wasioamini mianga ya imani, na Wakristo wakosefu neema ya kujuta inayowaalika kwenye kitubio. Lakini nguvu hiyo inatumika hasa katika ekaristi, kwa kuwa sakramenti hiyo haina neema tu, bali inaye aliyetustahilia neema, tena ni sadaka yenye thamani isiyo na mipaka. Jambo hilo linatakiwa kusisitizwa, tunapoongea juu ya chemchemi ya maisha ya Kiroho.

### NGUVU YA KUTAKASA INAYOTOKA KWA MWOKOZI KATIKA EKARISTI

Ili tufaidike zaidi na kumshukuru Bwana ni afadhali tufuate maneno ya Injili, tukikumbuka *alivyotuahidia* kwanza ekaristi kwa upendo; *alivyotupatia* katika karamu ya mwisho, alipoweka upadri; *anavyoifanya upya* kila siku katika misa; anavyotaka kubaki kati yetu *kwa kudumisha uwemo wake halisi* katika sakramenti; hatimaye anavyojitoa kwetu katika *komunyo ya kila siku*, hadi ile ya mwisho tunayotumainia kuipokea kabla hatujafa. Ukarimu wote huo wa Kimungu unatokana na upendo na kulenga ustawi wa utakatifu wetu.

Maneno aliyotuahidia ekaristi (taz. Yoh 6:26-69) yanatuonyesha kwa namna bora hizo nguvu hai za Mwokozi zinazotakiwa kutufanyia kazi na jinsi sisi tunavyotakiwa kuzipokea. Baada ya kuzidisha mikate, alisema, "Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele, ambacho Mwana wa Adamu atawapa. Kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani Mungu... Baba yangu anawapa ninyi chakula cha kweli kitokacho mbinguni. Kwa maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima". Basi wakamuambia, "Bwana, sikuzote utupe chakula hiki". Yesu akawaambia, "*Mimi ndimi chakula cha uzima*... Lakini niliwaambia ya kwamba mmeniona wala hamwamini... Amin, amin, nawaambia: yeye aaminiye yuna uzima wa milele. Mimi ndimi chakula cha uzima. Baba zenu waliila mana jangwani; wakafa. *Hiki ni chakula kishukacho kutoka mbinguni, kwamba mtu akile wala asife*. Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. *Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu*... Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli... Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima". Kutokana na hayo, wengi wa wafuasi wake walirudi nyuma, wasiandamane naye tena. Basi, Yesu akawauliza wale kumi na wawili, "Je, ninyi nanyi mwataka kuondoka?" Simoni Petro akamjibu, "Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele". Ahadi hiyo ya ekaristi inadokeza yale yote ambayo sakramenti kuu inakusudiwa kuzaa ndani mwetu.

Simulizi la kuiweka linatuonyesha uzito wa ahadi hiyo: "Walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, *'Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu'*. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, *'Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi'"* (Math 26:26-28). Maneno ya ahadi yanaangazwa na hayo yaliyomtuza Mt. Petro kwa sababu alisema kwa imani, "Wewe unayo maneno ya uzima wa milele". Hakika karamuni Yesu alikuwa na neno lenye nguvu kuliko kawaida, neno *lenye kugeuza* dhati ya mkate kuwa mwili wake ili abaki kati yetu kisakramenti.

Papo hapo *aliweka upadri* ili kudumisha kisakramenti sadaka ya msalabani mpaka mwisho wa nyakati. Kwa kusema, "*Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu*" (Lk 22:19; 1Kor 11:24-25) aliwapa mitume uwezo wa kugeuza, wa kutolea sadaka ya ekaristi, ili watushirikishe matunda, stahili na malipizi yake mpaka mwisho wa dunia. Bwana wetu ndiye kuhani mkuu anayeendelea kujitoa, "maana yu hai sikuzote ili awaombee" (Eb 7:25). Anafanya hivyo hasa katika sadaka takatifu, ambayo ina thamani isiyo na mipaka, kutokana na kuhani mkuu anayeitoa, sadaka inayotolewa, na damu azizi inayomwagwa kisakramenti. Papo hapo Yesu anamtolea Baba yake ibada, dua, malipizi na shukrani zetu, yaani kwa jumla matendo yote ya Mwili wake wa fumbo yanayostahili wokovu.

Upendo wa Kristo umetupatia ekaristi si mara moja tu, bali *kila siku upya*. Angeweza kuamua misa iadhimishwe mara moja au mbili tu kwa mwaka mahali fulani patakatifu ambapo waamini waende kutoka nchi za mbali. Kumbe kila nukta misa kadhaa zinatolewa duniani kote. Hivyo analijalia Kanisa lake neema linazozihitaji kulingana na nyakati linazoishi, tuwe na nguvu ya kukabili hatari kubwa tulizonazo.

Kristo anarudi kila siku, kweli, kati yetu, si kwa muda wa saa moja, tunapoadhimisha sadaka ya ekaristi, bali kusudi *abaki nasi mfululizo* katika tabenakulo kama mwenzetu hapa uhamishoni, akitungojea kwa hamu ya kutusikiliza, na kumtolea daima Baba yake ibada yenye thamani isiyo na mipaka.

Hatimaye *komunyo* ni utimilifu wa kujitoa zawadi. Wema kwa jinsi ulivyo unaelekea kuenea; unavutia na kujishirikisha. Hiyo ni kweli hasa kwa wema mwangavu wa Mungu na Kristo wake. Katika komunyo Mwokozi anatuvuta kwake na kujitoa kwetu, sio sote kwa jumla, bali tukitaka kwa kila mmoja wetu, tena tukiwa waaminifu kwa ndani zaidi na zaidi. Anajitoa si kusudi alingane nasi bali sisi tuzidi kulingana naye. "Mkate ule tuumegao, *si ushirika wa mwili wa Kristo?*" (1Kor 10:16). Tunaupokea uhai wenyewe.

Ushirika huo unatakiwa kutuunganisha na Kristo zaidi na zaidi, ukikuza ndani mwetu unyenyekevu, imani, tumaini na hasa upendo, ili moyo wetu ulingane na ule wa Mwokozi aliyekufa kwa kutupenda. Kwa maana hiyo komunyo zetu zinatakiwa kuwa na upendo mwingi zaidi na zaidi, kwa kuwa kila mojawapo inatakiwa sio tu kutunza, bali kustawisha upendo wa Mungu ndani mwetu na hivyo kutuandaa kumpokea Bwana kesho yake kwa utashi motomoto zaidi (umotomoto wa hisi ni wa ziada tu: tunaweza kupokea vizuri ekaristi katika ukavu mkubwa wa hisi, kama ilivyokuwa bora sala ya Yesu bustanini). Inatakiwa kuwa kama mbio ya kumuendea Mungu ambayo izidi kuwa ya kasi kadiri tunavyomkaribia na kuvutiwa naye, kama vile vitu vinavyoanguka kwa kasi kadiri vinavyokaribia ardhi inayovivuta.

"Ninakuabudu Mungu wangu, / unayejificha altareni. / Ninakutolea moyo wangu, / usiofahamu siri yako... / Ewe Yesu nipe pendo lako, / tumaini kwako na imani. / Umeteswa nini, Bwana mwema, / kwa kunipa mkate wa uzima? / Yesu unifiche ndani yako, / ili nilionje pendo lako. / Yesu pelikane nitazame, / na kwa damu yako nitakase. / Tone moja ndilo linatosha, / na dunia yote yaokoka. / Ndani ya mafumbo Yesu yumo. / Atafumbuliwa kwangu lini? / Nikuone, Yesu, uso wako, / nishiriki nawe heri yako" (Mt. Thoma wa Akwino). Mtu akiishi hivyo ekaristi kila siku, atafikia urafiki wa ndani naye, na kuzama zaidi na zaidi katika fumbo kuu la altare, chemchemi ya neema mpya daima, ambamo vizazi vyote vinatakiwa kutuliza kiu yao na kupata nguvu ya kufikia mwisho wa safari ya kuelekea uzima wa milele. Nabii Eliya alipoishiwa nguvu alizipata upya kwa kula mkate kutoka mbinguni, akatembea mpaka mlima Horebu, unaomaanisha kilele cha ukamilifu. Kristo anatuambia kama alivyomuambia Mt. Augustino, "Ndimi mkate wa watu wazima... Kua, nawe utanila; lakini hutanigeuza ndani mwako, kama chakula cha mwili wako; bali wewe utageuzwa ndani mwangu". Anayemshiriki kweli Kristo anazidi kuunganishwa naye, hata akaishi kwa mawazo yake na kwa upendo wake na kuweza kusema, "Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida" (Fil 1:21), kwa kuwa ni mlango wa uzima usio na mwisho.

## KUUNGANA NA KRISTO ZAIDI NA ZAIDI NA UTAKATIFU

Mafundisho hayo kuhusu kuungana na Kristo zaidi na zaidi yatamfaidisha ajabu anayeamua kuyaishi.

Kwanza *ili tufie dhambi na matokeo yake* tukumbuke kwamba "tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake… ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena" (Rom 6:4-6); "hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake" (Gal 5:24). Ndiyo hatua ya kufia dhambi kwa ubatizo na toba.

Pili, *kwa mwanga wa imani na uvuvio wa Roho Mtakatifu, tunatakiwa kuvaa "utu mpya,* unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba... Basi... jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu… Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu" (Kol 3:10-14). Ndiyo hatua ya mwanga ya wanaomuiga Yesu kwa kujipatia misimamo yake, roho ya mafumbo yake: ya mateso, kifo na ufufuko. "Nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo" (Fil 3:8).

Tatu, *njia hiyo* waliyoifuata watakatifu wote *inafikisha hadi kuungana na Mwokozi kama kwa kudumu:* "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu" (Kol 3:1-3). Hapo amani yake itamtawala mtu anayependa kumuambia, "Bwana, nipe

nafsi yako, pokea nafsi yangu". Elekeo la roho yetu kwake linamjulisha hamu yetu, likimtolea udhaifu wetu, nia yetu njema, azimio letu la uaminifu, kiu yetu ya nafsi yake. Ndiyo hatua ya kuzama kwa upendo katika mafumbo, kama utangulizi wa heri ya kuonana na Mungu uso kwa uso.

Wengi wanadanganyika wataweza kufikia muungano naye pasipo *kumkimbilia mfululizo Bwana Yesu:* hao watafikia tu ujuzi wa mbali wa Mungu, si ule ujuzi mtamu ambao unaitwa hekima na ni kama kumng'amua Mungu na maongozi yake hata katika mambo madogo. Tusiache kamwe kwa makusudi kuzingatia ubinadamu wa Mwokozi katika sala: kwa kuwa ndiye njia ya kufikia umungu wake. Tufikirie mara nyingi utajiri wa Kiroho wa Yesu, wa akili, utashi na hisi zake, ili tuzidi kuelewa neno lake: "*Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima"* (Yoh 14:6).

## 1.6. *ATHARI YA MARIA MSHENGA*

Tunaposema juu ya misingi ya maisha ya Kiroho, hatuwezi kuzungumzia kazi ya Kristo mshenga juu ya mwili wake wa fumbo tusidokeze pia juu ya msaada wa mama Maria. Wakatoliki kadhaa hawaamini vya kutosha haja ya kumkimbilia Maria ili kuungana na Mwokozi kwa undani zaidi. Mt. Alois Maria wa Montfort aliwasema "walimu ambao wanamjua Mama wa Mungu kinadharia tu, kwa namna kavu, tasa na baridi; na wanaogopa heshima kwa Bikira mtakatifu itatumika vibaya hivi kwamba kwa kumheshimu mno Mama mtakatifu Bwana atachukizwa. Wakiongelea heshima kwa Maria ni kwa kuzuia namna zake zisizofaa kuliko kwa kuihimiza"; unaweza kudhani wanamuona ni kizuio kwa kufikia muungano na Mungu! Kumbe muungano huo unasaidiwa na heshima halisi na kubwa kwa Maria. Ni kiburi kutowajali wasaidizi tuliojaliwa kwa udhaifu wetu.

### TUELEWEJE USHENGA?

Mt. Thoma wa Akwino aliandika, "Kazi ya mshenga ni kuwasogeza karibu na kuwaunganisha wale ambao amewekwa katikati yao: kwa kuwa pande mbili zinaungana kwa njia ya mshenga. Basi, kuunganisha watu na Mungu ni kazi hasa ya Kristo, kwa kuwa ndiye aliyewapatanisha na Mungu alivyosema Mt. Paulo: 'Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake' (2Kor 5:19). Kwa hiyo mshenga kamili kati ya Mungu na watu ni Kristo tu, kwa kuwa kwa kifo chake amewapatanisha watu na Mungu. Hata Mt. Paulo aliposema: 'mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu' akaongeza, 'ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote' (1Tim 2:5-6). Lakini hakuna kinachozuia wengine wasiitwe kwa namna fulani washenga kati ya Mungu na watu kwa kuwa wanachangia muungano wa Mungu na watu kama wahudumu katika ugawaji". Kwa maana hiyo manabii na makuhani wa Agano la Kale wanaweza kuitwa washenga; kama vile mapadri wa Agano Jipya, walio wahudumu wa mshenga halisi. Mwalimu huyo akaongeza kuwa "*ni kwa ubinadamu wake* kwamba Kristo ni *mshenga*: kwa sababu ni kama binadamu kuwa yeye yupo kati ya pande mbili: chini ya Mungu kwa umbile, juu ya watu kwa ukuu wa neema na utukufu. Tena kama binadamu anawaunganisha watu na Mungu akiwatolea amri na zawadi za Mungu, na kutoa fidia na sala kwa ajili yao". Yesu alifidia na kustahili kama binadamu, ambaye fidia na stahili zake zilikuwa na thamani isiyo na mipaka kutokana na Nafsi yake ya Kimungu. Hapo tuna ushenga wa aina mbili, wa kushuka na wa kupanda, yaani wa kuwapa watu mwanga na neema ya Mungu na wa kumtolea Mungu ibada na malipizi anayostahili kwa ajili ya watu. Chini ya Kristo, hakuna kinachozuia uwepo wa *washenga washiriki*. Maria hakuteuliwa awe mhudumu, bali awe mshiriki wa pekee na wa dhati wa ukombozi wa wanadamu, "kadiri ya maneno, 'nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye' (Mwa 2:18)" (Mt. Alberto).

Kama *Mama wa Mungu* alikusudiwa kuwa *mshenga kwa wote na yote* kati ya Mungu na watu. Kwa kuwa ni kiumbe yuko chini sana kuliko Mungu na Kristo; lakini ameinuliwa juu ya watu wote kwa neema ya kuwa Mama wa Mungu, na kwa ukamilifu wa neema ambao alijaliwa tangu achukuliwe mimba hali amekingiwa dhambi ya asili, ukaongezeka moja kwa moja hadi kifo chake. Naye hakuteuliwa tu awe mshenga kutokana na umama wake wa Kimungu, bali kweli alikabidhiwa na kutekeleza kazi hiyo ambayo inamfaa kwa sababu: 1° alichangia sadaka ya msalabani kwa *malipizi* na *stahili* zake; 2° haachi *kutuombea, kutupatia* na kutugawia neema zote tunazopokea. Ndio ushenga wa kupanda na kushuka tunaopaswa kuuzingatia ili kuufaidi kila siku zaidi.

### MARIA MSHENGA KWA KUCHANGIA SADAKA YA MSALABANI

Maisha yake yote bikira Maria alichangia sadaka ya Mwanae hadi aliposema, "Imekwisha" (Yoh 19:30). Kwanza ilihitajika ridhaa yake, aliyoitoa alipopashwa habari na malaika, ili fumbo la umwilisho lifanyike, kana kwamba Mungu alisubiri kibali cha binadamu kwa sauti ya Maria. Hapo alichangia sadaka ya msalabani kwa kutupatia kuhani na kafara yake.

Aliichangia pia kwa kumleta hekaluni Mwanae, ambaye mzee Simeoni kwa mwanga wa kinabii alimuona ndiye wokovu ulioletwa na Mungu "tayari machoni pa watu wote; nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli" (Lk 2:31-32). Maria akiwa ameangaziwa kuliko yeye, alimtoa Mwanae na kuanza kuteseka pamoja naye, akitabiriwa kwamba mtoto amewekwa "kuwa ishara itakayonenewa. Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako" (Lk 2:34-35).

Hasa chini ya msalaba Maria alichangia sadaka ya Kristo, akiungana naye kwa undani usioelezeka. Baadhi ya watakatifu, hasa waliotiwa madonda ya Mwokozi, waliungana na mateso na stahili zake kwa namna ya pekee, lakini kidogo kuliko Maria aliyemtoa Mwanae kama mwenyewe alivyojitoa. Yesu angeweza kuzuia kwa urahisi ukatili wa watesi wake usimuue, lakini alitoa kwa hiari uzima wake: "Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena" (Yoh 10:18). Alijinyima haki ya kuishi, akijitoa mhanga kwa wokovu wetu. Maria alisimama "penye msalaba wake Yesu" (Yoh 19:25), akiungana naye kwa dhati katika kuteseka na kujitoa, "akijinyima haki zake za kimama kuhusu Mwanae kwa wokovu wa watu wote" (Benedikto XV). Alikubali kifodini cha Kristo na kukitoa kwa ajili yetu. Upendo wa Bikira ulipita ule wa watakatifu wote. Hivyo alionja kuliko wote uchungu wa Mwanae katika mwili na katika roho; *alisikitishwa na dhambi kadiri ya upendo wake: kwa Mungu,* anayechukizwa nayo; *kwa Mwanae,* aliyesulubiwa nayo; *kwa watu* wanaoangamizwa nayo.

Alichangia sadaka ya msalabani kama *malipizi* kwa kumtolea Mungu *kwa niaba yetu,* kwa uchungu mwingi na upendo mkuu, uhai wa Mwanae mpenzi, aliyemuabudu na kumpenda kuliko alivyojipenda. Saa hiyo *Mwokozi alikuwa akitulipia kwa msingi wa haki,* kwa matendo yake ya kibinadamu yaliyoshiriki thamani isiyo na mipaka ya nafsi yake ya Kimungu, yenye uwezo wa kufidia dhambi zote na zaidi tena. Upendo wake ulimpendeza Mungu kuliko anavyochukizwa na dhambi zote. Ndio kiini cha fumbo la ukombozi. Maria, akiungana na Mwanae, alitulipia *kwa msingi* si wa haki yenyewe, bali *wa urafiki wa ndani* uliomuunganisha na Mungu. Mwanae alipokuwa akifa msalabani kama mtu aliyeshindwa na kutupwa, Maria hakuacha hata kidogo kumuamini. Ndilo tendo kuu la imani; ndilo pia tendo kuu la upendo baada ya lile la Kristo mwenyewe. Tendo hilo limemfanya Maria *malkia wa mashahidi,* kwa kuwa sio tu shahidi kwa ajili ya Kristo, bali *pamoja naye,* hivi kwamba msalaba mmoja uliwatosha Mwana na Mama aliyesulubiwa kwa namna fulani kutokana na upendo wake kwa Kristo. Hivyo akawa *mkombozi mshiriki* kwa maana alikomboa binadamu pamoja naye, kwa njia yake na ndani mwake.

Kwa sababu hiyohiyo, yale yote ambayo Kristo msalabani alitustahilia kwa msingi wa haki, Maria alitustahilia kwa msingi wa upendo uliomuunganisha na Mungu. Kristo tu, akiwa ni kichwa cha binadamu wote, aliweza kustahili kwa haki tushirikishwe uhai wa Kimungu, lakini ilikuwa inafaa Mungu azingatie pia stahili za Maria aliyeungana naye katika kazi ya wokovu. Mapokeo yote ya mashariki na magharibi yanamuita Eva mpya, Mama wa wote upande wa roho, kama vile Eva alivyokuwa upande wa mwili. Basi *Mama wa Kiroho wa watu wote anatakiwa kuwapa uzima wa Kiroho*, ingawa si kama asili yake kuu. Msingi wa mafundisho hayo ni maneno ya Yesu kufani: "alipomwona mama yake, na yule mwanafunzi aliyempenda amesimama karibu, alimwambia mama yake, 'Mama, tazama mwanao'. Kisha akamwambia yule mwanafunzi, 'Tazama mama yako'. Na tangu saa ile mwanafunzi yule akamchukua nyumbani kwake" (Yoh 19:26-27). Maneno hayo yalimhusu kwanza Yohane, lakini mtume aliwakilisha watu wote waliokombolewa msalabani. Kwa kuwa Mungu anasema sio tu kwa maneno, bali pia kwa matukio na watu ambao mikononi mwake wanamaanisha yale anayoyataka. Kama vile neno la Yesu lilivyosababisha ndani ya Maria mapendo makubwa ya kimama kwa mwanafunzi mpendwa, vilevile hayo mapendo yakaenea kwa wote na kumfanya kweli mama yao wa Kiroho. Basi, ikiwa mama mwema kwa uadilifu wake anaweza kuwastahilia watoto wake neema nyingi, zaidi Maria kwa ukamilifu wa upendo wake anawastahilia watu wote, *ingawa si kwa msingi wa haki.*

Ndio ushenga wa kupanda wa Maria, ambao alitoa pamoja na Bwana sadaka ya msalabani kwa ajili yetu. Sasa tuzingatie ushenga wa kushuka ambao anatugawia zawadi za Mungu.

**MARIA ANAVYOTUPATIA NA KUTUGAWIA NEEMA ZOTE**

Kwa kuwa ni Mama wa watu wote, Maria anashughulikia wokovu wao, akiwaombea na kuwapatia neema wanazojaliwa. Ndiyo sababu Kanisa linamuelekea ili kupatiwa neema za kila aina, za kimwili na za Kiroho, zikiwa ni pamoja na zile za uongofu na kifo chema, zile zinazohitajiwa na mabikira watunze ubikira wao, na wachungaji kwa ajili ya utume wao, na wafiadini ili wadumu kukiri imani. Kwa namna fulani hata neema za sakramenti zinagawiwa kwa njia yake, kwa kuwa alitustahilia ameunganika na Bwana huko Kalivari, halafu kwa sala zake anatuandaa tuzipokee vema; pengine anatutumia padri tuweze kufaidi huduma hiyo. Imani ya Kanisa inasali mfululizo atuombee *"sasa na saa ya kufa kwetu";* kwa maneno hayo tunajiombea *neema ya sasa hivi*, ambayo ni tofauti kwa kila mtu na kwa kila nukta aliyonayo. Ikiwa sisi tunayatamka bila ya kuyazingatia, Maria hapana: anajua mahitaji yetu yote, anatuombea na kutupatia neema tunazojaliwa.

Msingi wa imani hiyo umo katika Maandiko na Mapokeo. Maria aligawa neema hata alipoishi duniani. Kwa njia yake Yesu alimtakasa Yohane mtangulizi wake, akaimarisha imani ya wanafunzi kwenye arusi ya Kana. Kwa njia yake Roho Mtakatifu alimiminwa juu ya mitume, alipokuwa akisali pamoja nao. Zaidi tena, baada ya kupalizwa mbinguni, akiwa Mama mwenye heri ya milele, anajua mahitaji ya wanae aliowaacha duniani. Basi, kwa upendo wake mkuu anatuombea, na kwa uwezo wake mkuu juu ya moyo wa Mwanae anatupatia neema zote tunazojaliwa, zile zote wanazozipata wasiofanya moyo wao kuwa mgumu. Ndiyo sababu alifananishwa na mfereji unaoleta maji ya neema, na shingo la Mwili wa Kristo linalounganisha kichwa na viungo.

Tutakaposema juu ya wanaoendelea tutaongelea heshima halisi kwa bikira Maria. Lakini tangu sasa tunaona umuhimu wa kufanya mara nyingi *sala ya washenga,* yaani kuanza kuongea na Maria kwa tumaini kubwa atuunganishe na Mwanae kwa dhati, halafu kwa njia ya Mwokozi tuinukie muungano na Mungu.

## 1.7. *USTAWI WA UZIMA WA NEEMA KWA NJIA YA STAHILI, SALA NA SAKRAMENTI*

Hatuwezi kuzungumzia chemchemi ya maisha ya Kiroho bila ya kusema juu ya ustawi wa upendo. Hakuna wokovu bila ya adili hilo la Kimungu, lililo kuu kuliko yote na linalotakiwa kuyaongoza na kuyahuisha mengine pia. Tena halitakiwi kubaki lilivyo, bali *kukua* ndani mwetu hadi siku ya kufa. Fundisho hilo linaweza, tena linapaswa kuangaza maisha ya Kiroho, kwa kuwa ni msingi wa himizo lolote la kusonga mbele kwa unyenyekevu na moyo mkuu, kwa kutamani muungano wa ndani na Mungu, kwa kujitahidi kuupata pamoja na kuuomba. Basi, tuone kwanza *kwa nini* upendo unatakiwa kustawi daima, halafu *jinsi* unavyostawi.

### UZIMA WA NEEMA NA UPENDO USTAWI NDANI MWETU HADI KUFA

Hata katika kiwango kidogo upendo halisi (ambao tuliupokea kwa ubatizo na kurudishiwa pengine kwa upatanisho) unampenda tayari Mungu Mwokozi kuliko yote, na kwa ajili yake unampenda jirani kama mtu mwenyewe anavyojipenda. Kiwango hicho cha upendo uliomiminwa rohoni kinapita bila ya kifani pendo la kimaumbile tunaloweza kuwa nalo kwa Muumba na kwa watu; *hakimbagui yeyote,* kwa kuwa ubaguzi huo ungekuwa dhambi ya mauti inayofuta upendo. Lakini upendo huo wa wanaoanza uko mbali na ushindi dhidi ya umimi wowote. Unaendana bado na kujipendea ambako kunasababisha si dhambi ya mauti, bali dhambi nyepesi nyingi na hivyo kunazuia upendo usiweze kutenda na kupamba vizuri.

Ni wazi kuwa upendo huo unatakiwa kustawi: "Hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana" (Fil 1:9). "Bwana awaongeze na kuwazidisha katika upendo, ninyi kwa ninyi, na kwa watu wote, kama vile sisi nasi tulivyo kwenu; apate kuifanya imara mioyo yenu iwe bila lawama katika utakatifu mbele za Mungu, Baba yetu" (1Thes 3:12-13). "Mwenye haki na azidi kufanya haki, na mtakatifu azidi kutakaswa" (Ufu 22:11). "Njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu" (Mith 4:18). Hapa duniani Mkristo ni *msafiri* anayemuelekea Mungu na kumkaribia kwa vitendo vya upendo kamili zaidi na zaidi, kwa "hatua za upendo" (Mt. Gregori Mkuu). Upendo wake unaweza na kupaswa kustawi mfululizo, la sivyo badala ya kusafiri atasimama kabla hajafika. Lengo la njia ni kutembea, si kulala.

Kila mtu anayeelekea uzima wa milele anatakiwa kukua katika upendo ili azidi kumkaribia Mungu: sio tu wanaoanza na wanaoendelea, bali hata waliokamilika. Tena hao wa mwisho wanapaswa kwenda *kasi zaidi* kadiri wanavyomkaribia na kuvutwa naye. Nguvu ya maisha yao ya Kiroho *inaongezeka* zaidi na zaidi, elekeo la roho yao linainuka zaidi na zaidi; kwao hakuna machweo: mwili tu unadhoofika kwa uzee.

Bwana alisema, *"Mimi nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu"* (Yoh 12:32). "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka" (Yoh 6:44). Mungu ndiye anayetufanya twende, anakotuvutia ni kwake: ndiye mwanzo na mwisho wa yote, ndiye wema mkuu unaovuta upendo kwa nguvu kadiri tunavyomkaribia. Ndiyo sababu katika maisha ya watakatifu, ustawi wa upendo miaka yao ya mwisho ni mkubwa sana; ingawa wanalemewa na uzee na udhaifu upande wa hisi (k.mf. kumbukumbu) wanang'amua ukweli wa maneno, "Ujana wako unarejezwa kama tai" (Zab 103:5). Maendeleo hayo ya kasi zaidi na zaidi yalikuwepo hasa katika bikira Maria, kwa kuwa ndani mwake hayakuzuiwa na chochote, tena yalikuwa ya haraka kadiri ilivyokuwa kubwa neema ya kwanza aliyojaliwa. Basi, upendo hautakiwi tu kustawi hadi kufa, bali kustawi zaidi na zaidi, kama vile kasi ya kitu kinachoanguka inavyozidi hadi kikafika ardhini.

Ikiwa ni hivyo, upendo unastawi *vipi* ndani mwetu? Kwa kuwa hata katika kiwango cha chini unampenda tayari Mungu na majirani wote, hauwezi *kuenea* zaidi: lakini unaweza *kuongezewa nguvu* na kutia mizizi ndani ya utashi wetu zaidi na zaidi. Upendo hauongezeki kwa wingi kama nafaka, bali unakua kwa ubora, kwa kuongezewa nguvu katika utashi, *ukizidi kuuelekeza* kwenye mema yapitayo maumbile na kuuepusha na maovu. Mfano wake ni elimu ya msomi ambayo haipati daima taarifa mpya, ila inazidi kuchimba na kuwa na hakika; vivyo hivyo upendo unastawi ndani mwetu, ukitufanya tuwapende kwa namna *kamili na safi zaidi na zaidi* Mungu kwa ajili yake mwenyewe na jirani kwa ajili ya Mungu. Tukielewa hayo, tutaona haja ya *kutakaswa* kila uchafu ili kudhihirisha jinsi maadili makuu yanavyolenga ukweli na wema wa Mungu. Basi, upendo kama joto, unastawi kwa ubora, kwa kupata nguvu zaidi na zaidi; na hiyo inafanyika kwa namna tatu: kwa stahili, kwa sala na kwa sakramenti.

### USTAWI WA UPENDO KWA NJIA YA STAHILI ZETU

Tendo linalotokana na upendo (au adili lolote linalohuishwa nao) linastahili tuzo lipitalo maumbile, hasa ustawi wa upendo wenyewe. Stahili hazisababishi ustawi huo, kwa kuwa upendo si *adili la kujipatia,* bali *la kumiminiwa.* Mungu tu anaweza kuutia ndani mwetu (kwa kuwa ni kushiriki uzima wake wa ndani), naye tu anaweza kuustawisha: "Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali *mwenye kukuza ni Mungu*. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali *Mungu akuzaye*… ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu" (1Kor 3:6-9).

Yeye "atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu" (2Kor 9:10). Ingawa matendo ya upendo hayawezi *kusababisha* ustawi wa adili hilo, *yanauchangia* kwa namna mbili, yaani kwa *kuustahili* na kwa *kutuandaa* tuupokee.

Stahili ni haki ya kupata tuzo; hailisababishi ila inalipata. Mwadilifu akitenda mema yapitayo maumbile anastahili upendo wake ustawi. Bwana kabla hajampa tuzo la mbinguni anampa lile la kukua katika upendo wake. Wazushi walioitwa Watulivu walidharau tuzo wakijidai eti! Hawajitafutii faida. Kumbe *kadiri mtu alivyo na upendo, anatamani tuzo hilo: kumpenda Mungu kwa nguvu na kwa usafi mkubwa zaidi na zaidi,* jambo lisilotenganika na ustawi wa maadili mengine ya kumiminiwa na wa vipaji vya Roho Mtakatifu.

Matendo ya upendo (na ya maadili yanayohuishwa nao) hayastahili tu ustawi huo, bali pia *yanaandaa* kuupokea, kama kwa kufungua na kupanua akili na utashi ili uzima wa Mungu uweze kuvipenya zaidi, na kwa kuvitakasa uviinue juu zaidi. Hiyo ni kweli hasa kwa matendo motomoto ya upendo. Tendo moja la namna hiyo linaathiri pengine maisha yote ya baadaye na kustahili ustawi mkubwa wa upendo, *likituandaa* kuupokea. Ni kana kwamba tunainuliwa hadi ghorofa ya juu, tunapopewa mtazamo mpya wa mambo ya Mungu na mvuto mkubwa zaidi kwa hayo. Tunaongezewa talanta, yaani Roho Mtakatifu anakuwemo ndani mwetu kwa namna mpya inayofanya kazi zaidi.

Kwa kawaida yeye anamsukuma mtu kulingana na kiwango cha maadili na vipaji alichonacho au kulingana na usikivu wake. Kama angemsukuma *atende kwa upungufu,* angekuwa amempa *bure* kiwango kikubwa cha maadili na vipaji. Basi, mwadilifu *asipozuia* kazi ya Mungu, atapokea neema kubwa zaidi na zaidi apande mbio kwake.

Wanateolojia kadhaa wamefundisha kuwa Mungu anatukuzwa na tendo moja la upendo la talanta kumi kuliko anavyotukuzwa na vitendo kumi vya upendo vya talanta mojamoja; vilevile *mwadilifu mmoja aliye mkamilifu anampendeza Mungu kuliko wengine wengi wanaobaki katika wastani.* Ubora ni muhimu kuliko wingi. Ndiyo sababu ukamilifu wa Maria unapita ule wa watakatifu wote, kama vile almasi moja ilivyo na thamani kuliko vito vingine vingi.

Basi, upendo unatakiwa kustawi kwa njia ya stahili zetu hadi tutakapokufa. Pamoja na adili hilo utakua pia utayari wetu wa kupokea ongezeko lingine. Moyo unapanuka zaidi na zaidi na ujazo wake wa Kimungu unaongezeka: "mioyo yetu imekunjuliwa… Basi, ili mlipe kadiri ile mliyopewa… nanyi pia mkunjuliwe mioyo" (2Kor 6:11,13).

Mara nyingi tunasahau tuko safarini kuelekea uzima wa milele, na tunajaribu kustarehe katika maisha haya kana kwamba yangedumu moja kwa moja. Mfano wake ni maabiria wa treni bora ambamo wanakula na kulala kama hotelini hata wakasahau wako safarini; pengine wakiangalia dirishani wanaona mandhari ikibadilika haraka na baadhi ya wenzao wakiteremka: hapo wanajisemea kuwa wao pia watawahi kufikia mwisho wa safari. Shida ni kwamba, ingawa tunaona wengi kufa, hatupati hakika ya ndani kuwa siku fulani itakuwa zamu yetu. Basi, tuishi kwa kukazia macho mwisho wa safari, kusudi tusipoteze tena muda tuliojaliwa, bali tuujaze iwezekanavyo matendo ya kustahili uzima wa milele.

## UZIMA WA NEEMA KUSTAWI KWA NJIA YA SALA

Ustawi wa upendo (pamoja na maadili mengine na vipaji) unapatikana si kwa njia ya stahili tu, bali kwa sala pia, kama Kanisa linavyoomba, "Ee Mungu Mwenyezi wa milele, utuzidishie imani, tumaini na upendo" (Jumapili ya 30 ya mwaka).

Tukumbuke tofauti iliyopo kati ya kuomba na kustahili: asiye na neema inayotia utakatifu hawezi kustahili (kwa kuwa neema hiyo ndiyo asili ya stahili yoyote ipitayo maumbile); lakini kwa neema ya msaada anaweza kujiombea (k.mf. neema ya uongofu) na akiomba kwa unyenyekevu, imani na udumifu, atapata. *Stahili* inahusu haki ya Mungu; kumbe *sala* inaelekea huruma ya Mungu ambayo mara nyingi inanyanyua walioanguka na kusikiliza ombi lao lisilostahili chochote. Mtu duni kuliko wote, aliyetumbukia vilindi ambamo hawezi kustahili tena, anaweza kulilia huruma ya Mungu: "Kilindi chapigia kelele kilindi" (Zab 42:7), yaani kilindi cha unyonge kinalilia kile cha huruma. Mkosefu akisihi kwa moyo wote anasikilizwa, roho yake inanyanyuliwa, na Mungu anatukuzwa. Nguvu ya sala haitegemei tu neema inayotia utakatifu iliyo ya lazima ili kustahili.

Tukishaongoka, tunaweza kustawishiwa uzima wa neema kwa stahili na kwa sala pia. Hiyo ikiwa na unyenyekevu, imani na udumifu, inatupatia ustawi wa maadili ya Kimungu tunaoomba katika maombi matatu ya kwanza ya Baba Yetu. Sala ya mwadilifu, anayependa kutafakari polepole na kujilisha kwa undani maombi hayo (hata kusimama pengine nusu saa kuzamia mojawapo kwa upendo), inastahili pamoja na kuomba neema: inampa haki ya kustawishiwa upendo ulioisababisha, na kwa nguvu ya ombi *inapata kuliko inavyostahili.* Tena, ikiwa motomoto kweli, *inapata mara.* Hapo tunaweza kuona matunda ya sala na jinsi inavyomvuta Mungu ajitoe kwetu kwa dhati, nasi tujitoe kwake. Hapo moyo unazidi kutanuka upokee neema kwa wingi zaidi; roho inajitenga na malimwengu na kumtamani zaidi Mungu, ambaye ndani yake inakuta yale yote yanayostahili kupendwa, tena kwa ngazi ya juu. Hakutatosha kamwe kuyaishi hayo katika sala ya moyo, k.mf. katika kimya kikubwa cha usiku, ambapo mtu yuko peke yake na Muumba na Mwokozi wake. Hapo anang'amua kuwa Mungu ni mwema kupita kiasi, na sala ni mwanzo wa uzima wa milele.

*Kwa kusali mwadilifu anaweza kupata neema kadhaa ambazo hawezi kuzistahili,* hasa ile ya kudumu mpaka mwisho. Hawezi kustahili zawadi hiyo kwa kuwa ni kudumu kwa hali ya neema iliyo chanzo kisichostahilika cha stahili. Lakini neema ya kifo chema inapatikana kwa sala nyenyekevu, yenye imani, ya kila siku. Kanisa linatualika kukariri kwa bidii, "Maria mtakatifu, Mama wa Mungu, utuombee sisi wakosefu, sasa na saa ya kufa kwetu. Amina". Vivyo hivyo tunaweza kumuomba Mungu neema ya kumjua kwa ndani zaidi na zaidi, yaani ya kuzama katika sala, ambayo matokeo yake ni kuungana naye kwa namna imara na yenye matunda mengi zaidi: "Neno moja nimelitaka kwa Bwana, nalo ndilo nitakalolitafuta: nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu. Niutazame uzuri wa Bwana na kutafakari hekaluni mwake" (Zab 27:4), yaani nione kila siku vizuri zaidi jinsi wema wake usivyo na mipaka kwa wale ambao wanamtafuta na kumpata.

**USTAWI WA UZIMA WA NEEMA KWA NJIA YA SAKRAMENTI**

Hatimaye upendo (pamoja na maadili mengine na vipaji) unastawi ndani mwetu kwa njia ya sakramenti, hasa ekaristi. Stahili na sala za mwadilifu zinapata zawadi za Mungu kulingana na imani na upendo alivyonavyo; kumbe sakramenti zinaleta neema kwa nguvu zake zenyewe katika wale wasioweka kizuio. Kwa kuwa ziliwekwa ili kutugawia stahili za Mwokozi, zenyewe zinasababisha neema bila ya kutegemea sala na stahili za yule anayeziadhimisha wala za yule anayezipokea. Padri mwovu, na hata mtu asiye Mkristo, anaweza kubatiza mradi awe na nia ya kufanya Kanisa linavyofanya.

Hata hivyo sakramenti zinaleta neema kwa kiasi tofauti kulingana na juhudi za yule anayezipokea. "Kila mmoja anapokea uadilifu kadiri Roho Mtakatifu anavyomtakia kulingana na utayari wake" (Mtaguso wa Trento). Moto unawaka wenyewe, lakini sisi tunafaidi joto lake kadiri tunavyoukaribia. Vivyo hivyo tunafaidika na sakramenti kadiri imani yetu ilivyo hai na utashi wetu ulivyo motomoto. Kwa msingi huo Mkristo anapoondolewa dhambi anapata neema kadiri ya majuto yake. "Inatokea kwamba nguvu ya majuto ya mwenye kuungama ni kubwa, sawa au pungufu kuliko kiwango cha neema alichokipoteza; hapo anapata tena neema kwa kiwango kikubwa, sawa au pungufu kuliko awali" (Mt. Thoma wa Akwino). Kwa mfano, aliyekuwa na talanta tano kabla hajazipoteza kwa dhambi ya mauti, akija kuwa na majuto kama ya talanta mbili, anapata tena neema, lakini kwa kiasi kidogo kuliko awali. Kinyume chake, kwa majuto makubwa anaweza kuipata kwa kiwango kikubwa zaidi. Hilo ni muhimu kwa wale wanaokuja kuanguka wakati wa kupanda mlima; wanaweza kuinuka kwa bidii na kuendelea na safari yao kuanzia pale walipoanguka. Lakini wakiinuka kwa kuchelewa na bila ya bidii wanajikuta chini, badala ya kuendelea tu kupanda.

Kwa msingi huohuo komunyo moja yenye bidii inafaa kuliko nyingi vuguvugu. Kadiri tunavyomkaribia Yesu ekaristi kwa imani hai, tumaini imara na upendo motomoto tunafaidi neema za mwanga, upendo na ushujaa za kututosha hata tukashirikisha wengine. Kinyume chake, tunda la komunyo ni dogo tukikaribia meza takatifu kwa namna ambayo inatosha tu tusikufuru. Hayo yatufikirishe tuking'amua kuwa hatuendelei kweli baada ya kukomunika kila siku kwa miaka kadhaa (ingawa ni kweli pia kwamba mtu akiendelea, anazidi kufahamu unyonge wake mwenyewe kadiri anavyokuja kujua ukuu wa Mungu). Tuwe na bidii za kutosha itutokee kama kwa watakatifu: kwamba kila komunyo iwe na upendo mkubwa na matunda mengi kuliko ile iliyotangulia. Kumbe mara nyingi uzembe na uvuguvugu vinazuia ustawi huo: kwa kuambatana na dhambi nyepesi fulani, tunda la komunyo linazidi kupungua, kama kasi ya jiwe lililorushwa hewani wima ambayo inazidi kupungua mpaka jiwe likaanguka tena ardhini. Mungu atuepushe!

## 1.8. *UKAMILIFU WA KIKRISTO NI NINI HASA?*

Baada ya kuongelea chemchemi za maisha ya Kiroho, tuzingatie lengo lake: si lengo kuu tulilokwishalizungumzia tukisema kuwa maisha hayo ni mwanzo wa uzima wa milele, bali lile linaloweza kufikiwa duniani, yaani ukamilifu wa Kikristo. Zamani watu wasiostaarabika waliona ukamilifu wa binadamu unategemea *nguvu.* Wanafalsafa wengi waliona unategemea *hekima.* Kumbe Injili imetuambia unapatikana hasa katika *upendo.* Tuzikumbuke kwa ufupi dhana mbili za kwanza, tukitambua sura zilizonazo siku hizi. Hivyo tutaweza kuthamini zaidi ukuu wa jibu la tatu, pia kwa sababu hizo mbili zina chembe za ukweli ambazo chini ya upendo zinapata thamani.

**DHANA DANGANYIFU NA PUNGUFU KUHUSU UKAMILIFU**

Makabila yasiyostaarabika yaliweka ukamilifu wa binadamu hasa katika *nguvu,* moyo, uhodari, tunavyoona katika hadithi zao. Pengine utaifa unaelekea kuwarudisha watu kwenye kipeo hicho kinachotukuza mambo magumu, ambayo yanahitaji nguvu nyingi na kuhatarisha uhai, k.mf. vitani. Mtazamo huo umechanganyikana na kiasi kikubwa cha kiburi, na pengine cha utovu wa haki. Hautoshi kumweka binadamu sawa mbele ya Mungu na ya jirani.

Kuna watu motomoto wanaosafisha dhana hiyo na kuihamisha upande wa roho wakijiona *askari wa Kristo* na kujali mno kifodini. Kumbe ubora wa kifo hicho hautegemei kuwa tendo la nguvu, bali kuwa ishara angavu ya upendo mkuu. Karne tatu za dhuluma za Kanisa la mwanzoni zilikuwa za uhodari, lakini hasa za upendo: ndio unaotofautisha wafiadini wa Kikristo na mashujaa wa Kipagani.

Kwa mtazamo unaofanana na huo kuna watu wanaoona ukamilifu umo hasa katika *ugumu wa maisha* (mafungo, makesha n.k.): huo unaweza kuhitajiwa na utawa unaokusudia zaidi sala na sadaka. Ila ugumu huo si *lengo* bali *njia* tu ya ustawi. Maisha makamilifu zaidi si yale magumu zaidi, bali yale yenye lengo bora na njia za kufaa zaidi kulifikia. Maisha ya Kiroho yanahusu uadilifu kuliko ugumu. Kwanza si kila tendo gumu ni adilifu: pengine ni juhudi ya ushupavu tu. Halafu *uadilifu* ni mgumu mara nyingi, lakini si daima: vitendo kadhaa vya upendo vinatendeka pasipo shida, kwa msukumo mkubwa wa roho, hata hivyo vina stahili kubwa kwa kuwa vinatokana na upendo mkubwa. Nguvu ni sifa muhimu ya askari, lakini je, ndio ukamilifu wa mtu kama mtu na wa Mkristo kama Mkristo? Nguvu inahitajika kwa ukamilifu, lakini juu yake kuna *haki* kuhusu wengine, kuna *busara* inayoongoza maadili yote ya kiutu, na hasa kuna *maadili yanayomlenga Mungu* moja kwa moja: imani, tumaini na upendo. Basi, hatuwezi kukubali kwamba ukamilifu umo hasa katika nguvu, kwa kuwa si ukamilifu wa akili yetu kuhusu ukweli mkuu, wala si ukamilifu wa utashi wetu kuhusu wema mkuu, ila ni adili linaloshinda hofu tu ili tuzidi kufuata njia nyofu hata kwenye shida na hatari.

Ikiwa ukamilifu haumo hasa katika nguvu, je, utapatikana katika *hekima?* Ndivyo walivyodhani wanafalsafa wengi, wakisema *binadamu* anatofautiana na viumbe vilivyo chini yake kwa *akili* aliyonayo; kwa hiyo ukamilifu wake ni hasa ule wa akili yake, yaani hekima au ujuzi mkuu. Hakika hekima *inahitajika kwa ukamilifu*, lakini si kweli kwamba kumjua Mungu kinadharia *kunafuatwa daima na upendo kwake.* Mwanafalsafa, hata kama ana akili na wazo sahihi kuhusu Mungu kama asili na lengo kuu la ulimwengu, anaweza akawa mwovu. Ukweli ni ukamilifu wa akili, lakini si ukamilifu wa mtu mzima, wala si jema pekee la binadamu. Elimu inaweza kuwepo pasipo upendo kwa Mungu na kwa jirani; hapo "huleta majivuno" (1Kor 8:1). Ukamilifu wa mtaalamu kama mtaalamu si ule wa binadamu kama binadamu, wala ule wa Mkristo kama Mkristo. Tusichanganye ukamilifu wa akili na ule wa mtu mzima unaohitaji kunyosha utashi kuhusu lengo kuu. Tofauti na sanaa na sayansi, uadilifu unadai *utashi unyoshwe:* hapo tu mtu ataitwa mtu mwema, sio tu mchoraji mzuri, mjenzi mzuri au mganga mzuri. Hatimaye hapa duniani kumpenda Mungu ni bora kuliko kumjua. Ujuzi unamvuta kwetu na kumlazimisha ndani ya mipaka ya mawazo yetu finyu; kumbe upendo wa Mungu unatuvuta kwake na kutufanya tupende ndani mwake hata yale tusiyoweza kuyajua sawasawa, kwa sababu tuna hakika ya kuwa maisha yake ya ndani yaliyofichika kwetu yanapendeza kupita kiasi.

Dhana ya kuwa hekima ndiyo ukamilifu inajitokeza leo katika wale wanaojali *elimu* kuliko yote. Hata baadhi ya Wakristo wanaelekea kudhani inawezekana kuufikia ukamilifu haraka kwa kusoma maandishi mengi ya watakatifu, bila ya kujitahidi zaidi kutekeleza maadili yao, wala kukumbuka vya kutosha kuwa *sala ya kuzama katika mafumbo inatakiwa kujaa upendo upitao maumbile na kujikana.* Tutaona mbele kuwa sala hiyo sio ukamilifu hasa, na kuwa huo umo katika kuungana na Mungu kwa upendo; ila kumtazama kwa upendo ni *njia iliyounganika na lengo hilo* kwa sababu kunatuandaa moja kwa moja tuungane naye. Hivyo tusilenge hasa sala hiyo, bali Mungu mwenyewe ambaye apendwe kuliko yote.

Basi, ukamilifu unahitaji kweli nguvu na hekima, lakini pia maadili yote ya Kimungu na ya kiutu, pamoja na vipaji saba vya Roho Mtakatifu. Je, ukamilifu umo katika jumla ya maadili? Ndiyo, mradi jumla hiyo iwe *imepangwa* vizuri kama muundo hai, na kati ya maadili liwepo moja lenye kuyatawala, kuyaongoza na kuyahuisha yote na kuelekeza juhudi zake zote kwenye lengo kuu. Kama ni hivyo, ukamilifu umo hasa katika adili hilo kuu ambalo mengine yote yanapaswa kulisaidia. Lenyewe ni lipi?

### UKAMILIFU KADIRI YA MAANDIKO MATAKATIFU

Bwana ametufundisha kwa namna mbalimbali kwamba amri inayotawala maagizo na mashauri yote ni ile ya upendo iliyotajwa tayari katika Agano la Kale: "Mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" (Kumb 6:5). "Umpende jirani yako kama nafsi yako. Mimi ndimi Bwana" (Law 19:18). Ndicho kipeo kikuu kuliko nguvu na hekima, chenye nguvu ya aina nyingine, na hekima ya kweli na ya juu zaidi. "Kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana na kusameheana… *Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu*" (Kol 3:12-14)". Upendo ndio *kifungo cha ukamilifu* kwa sababu ni adili bora ambalo linatuunganisha na Mungu na kudumu milele; ndio unaohuisha maadili yote yawe na stahili kwa kuyalengesha kwa Mungu mpendwa kuliko yote.

Mt. Paulo alikuwa na hakika kwamba upendo ni bora kuliko maadili mengine, vipaji vya Roho Mtakatifu na karama mbalimbali: "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu" (1Kor 13:1-3). Pasipo upendo karama hazisaidii kitu kwa uzima wa milele, kwa sababu nisipopenda sitekelezi amri ya kwanza ya Mungu, silinganishi matakwa yangu na ya kwake, napotoka mbali naye katika njia isiyoelekea moyo wake. Basi, katika wokovu "kama sina upendo, si kitu mimi", sistahili kitu ingawa ninaweza nikawasaidia wengine kuokoka kwa mahubiri na kwa miujiza.

Kwa maana hiyo Mt. Augustino alisema, *"Penda, halafu tenda lolote utakalo",* nalo litakustahilisha uzima

wa milele. Lakini uwe na upendo halisi, kwa sababu hakuna lililo baya kuliko *upendo wa bandia* (unaofumba macho usitimize wajibu wake dhidi ya maovu: huo ni udhaifu au miguso ya kibinadamu tu inayotaka kukubaliwa na upendo halisi na kuuambukiza). Kati ya mapambano makuu ya leo, mojawapo ni lile kati ya upendo halisi na upendo wa bandia, ambao unatukumbusha *Makristo wa uongo* wanaozungumziwa na Injili. *Uharibifu mbaya zaidi ni ule unaohusu yaliyo bora,* kama vile upendo ulio adili kuu. Kwa kuwa *yale yanayoonekana tu mema* ni ya hatari kadiri ya ubora wa mema halisi yanayoigizwa nayo (k.mf. kipeo cha wanaotaka kuunganisha madhehebu ya Kikristo kwa kupunguza kweli za imani). Ikiwa kwa upumbavu au woga wale wanaotakiwa kuwakilisha upendo halisi wanayakubali kwa namna moja au nyingine *yale yanayoficha upendo wa bandia,* yanaweza kutokea mabaya yasiyopimika, makubwa kuliko yale yanayoweza kusababishwa na watesi waliojitokeza wazi.

Tofauti na upendo wa bandia, ule halisi una maadili yote ndani yake na chini yake hivi kwamba yanaonekana kama namna au sura mbalimbali za upendo kwa Mungu na kwa jirani. "Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari, haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote; hutumaini yote, hustahimili yote" (1Kor 13:4-7). Imani itaachia nafasi kumuona Mungu, tumaini litaachia nafasi kuwa naye, lakini upendo utadumu milele.

Kwa upendo huo tunakuwa hekalu la Roho Mtakatifu. Kadiri tunavyompenda Mungu tunamfahamu na kama kumng'amua kwa ujuzi upitao maumbile unaoitwa hekima ya Kimungu. "Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani *mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu* pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo na kina; na kuujua *upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"* (Ef 3:17-19).

Mafundisho hayohayo tumepewa na Mt. Yohane: "Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake… Yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake" (1Yoh 4:16,21). Mt. Petro aliandika vilevile, "Zaidi ya yote iweni na juhudi nyingi katika kupendana, kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi" (1Pet 4:8). Alivyosema Yesu, "Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana" (Lk 7:47).

Kadiri ya mafundisho hayo, ukamilifu haumo *hasa* katika unyenyekevu, ufukara wala ibada, bali katika upendo unaofanya matendo ya maadili mengine yote yastahili. Ufukara sio ukamilifu, ila ni *njia* ya ukamilifu. Basi, njia haitafutwi kwa ajili yake, bali kwa ajili ya *lengo,* nayo ni bora si kadiri ya ukubwa wake, bali *kadiri inavyolingana na lengo,* kama vile daktari mzuri ni yule anayetoa matibabu yanayoponya, si anayetoa mengi zaidi. Ni vivyo hivyo kuhusu unyenyekevu unaotuinamisha mbele ya Mungu ili kupokea kwa mikono miwili msaada wake ambao utuinue hadi kwake. "Unyenyekevu ni adili la msingi kwa kuwa unaondoa kizuio kikuu, yaani kiburi, lakini umo chini ya maadili ya Kimungu yanayotuunganisha na Mungu" (Mt. Thoma wa Akwino). Hata adili la ibada, linalompatia Mungu heshima inayompasa, halistahili lisipohuishwa na upendo. Si adili la Kimungu kwa sababu halimhusu moja kwa moja yeye, ila *ibada* kwake. Tukisahau hayo tunaweza tukazingatia liturujia kuliko Mungu mwenyewe, mifano kuliko ukweli, namna ya kusali Baba Yetu kuliko maana yake: hapo utumishi wa Mungu ungepiku upendo wake.

## MAELEZO YA TEOLOJIA KUHUSU UKAMILIFU

"Kila kiumbe ni kamili kadiri kinavyofikia *lengo lake* ambalo ndio ukamilifu wake wa mwisho. Sasa, lengo kuu la maisha ya binadamu ni Mungu, na upendo ndio unaotuunganisha naye, kadiri ya neno la Mt. Yohane: 'Kila mtu aishiye katika upendo, anaishi katika muungano na Mungu, na Mungu anaishi katika muungano naye'. Basi, ukamilifu wa maisha ya Kikristo umo hasa katika upendo" (Mt. Thoma wa Akwino). Imani na tumaini haviwezi kuwa kiini cha ukamilifu, kwa sababu vinaweza kuwepo katika mtu ambaye kwa dhambi ya mauti amepotosha utashi wake mbali na Mungu. Vinabaki ndani mwake kama mzizi wa mti uliokatwa na ambao unaweza kuchipua tena.

Mt. Thoma akaongeza, "*Ukamilifu umo hasa katika upendo kwa Mungu, halafu katika upendo kwa jirani,* kwa kuwa ndio amri kuu za sheria ya Kimungu". Hatutaweza kamwe kusisitiza mno neno la Bwana: "Amri mpya nawapa: Mpendane. *Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.* Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yoh 13:34-35). Ndiyo dalili kuu ya ustawi wa upendo wa Mungu mioyoni mwetu: "Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa… Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini *kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu*. Yeye asiyependa, akaa katika mauti. Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji; nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake" (1Yoh 3:14-15).

Sasa tuzingatie mambo mawili yanayotofautisha ukamilifu wa duniani na ule wa mbinguni.

## HAPA DUNIANI "KUMPENDA MUNGU NI BORA KULIKO KUMJUA"

Tusisitize neno hilo la Mt. Thoma. Yeye alikubali kuwa akili ni bora kuliko utashi unaoongozwa nayo, kuwa ni kipawa cha kwanza cha binadamu kinachomtofautisha na mnyama, tena kuwa mbinguni heri yetu itatokana hasa na *akili kumuona Mungu moja kwa moja,* kwa kuwa ndiyo njia ya *kumpata* milele: kuzamisha

akili yetu katika vilindi vya maisha yake ya ndani yakiwa wazi tu. Mungu atajitoa moja kwa moja kwetu, nasi tutajitoa kwake; sisi tutakuwa naye kama mali yetu, nasi tutakuwa mali yake, kwa kuwa tutamfahamu kama anavyojifahamu na anavyotufahamu. *Upendo wenye heri* utakuwa matokeo ya huo mtazamo wa moja kwa moja wa umungu, tena *matokeo ya lazima,* kwa kuwa utashi wetu utavutwa moja kwa moja na uzuri wa Mungu. Tutaona wema wake mkuu kwa namna iliyo wazi hivi hata tusiweze kutompenda; hatutaweza kuona *kisingizio chochote* cha kusimamisha kwa nukta moja tu tendo hilo la upendo lililo juu kuliko hiari yetu, na ambalo halitapimwa na muda, bali na *umilele tulioshirikishwa,* ile nukta pekee isiyokwisha kamwe ya Mungu kuwepo pasipo badiliko. Upendo kwake na furaha ya kuwa naye kama mali yetu vitatokana kwa lazima na heri ya kumuona.

Hata hivyo mwalimu huyo alisema *ukamilifu wa Kikristo* hapa duniani umo *hasa katika upendo* ambao ni adili la utashi, badala ya kuwemo upande wa akili. Ni kwamba *kipawa fulani kinaweza kuwa bora kuliko kingine* kwa umbile lake, lakini *tendo fulani la hicho cha pili linaweza kuwa bora kuliko mojawapo la hicho cha kwanza.* Kwa mfano uwezo wa kuona ni bora kuliko ule wa kusikia, na upofu ni tatizo kubwa kuliko uziwi; lakini kusikiliza muziki bora kuna thamani kuliko kuona vitu vya kawaida. Vivyo hivyo, ingawa kwa umbile lake akili ni bora kuliko utashi, *hapa duniani kumpenda Mungu ni bora kuliko kumjua,* hivi kwamba mtakatifu ambaye hana elimu lakini ana upendo mkubwa kwa hakika ni mkamilifu kuliko mwanateolojia mkuu mwenye upendo mdogo. Jambo hilo, ambalo Wakristo wote wanalielewa kwa urahisi, tukilifikiria kwa makini tutaliona ni ukweli wa thamani unaoweza kuthibitishwa na madondoo mengi ya Biblia na ya walimu wa Kiroho.

*Huo ubora wa upendo hapa duniani unatokana na kwamba* "kazi ya akili yetu inafanyika kwa *kujichorea* ukweli uliojulikana, kumbe *utashi wetu unavutwa na upendo ukiendee kilichopendwa jinsi kilivyo.* Alivyosema mwanafalsafa, wema ulio lengo la utashi umo ndani ya vitu, kumbe ukweli umo hasa katika roho yetu" (Mt. Thoma wa Akwino). Kwa hiyo *tunapomjua Mungu, kwa namna fulani tunambana ndani ya mipaka ya mawazo yetu finyu ili tujichoree alivyo; kumbe tunapompenda, sisi ndio tunaovutwa naye na kuinuliwa kwake jinsi alivyo kweli.* Basi, duniani na toharani upendo kwa Mungu ni bora kuliko kumjua; unahitaji kumjua kwanza, lakini unapita ujuzi huo. Tena tokea hapa duniani *upendo wetu unamfikia Mungu na kuambatana naye moja kwa moja:* "Ujuzi wetu unainuka kwa Mungu kupitia viumbe, kumbe upendo wetu unawashukia viumbe kutoka kwa Mungu" (Mt. Thoma wa Akwino).

Hatimaye, sisi *tunapenda ndani ya Mungu hata yale tusiyoyajua*, kwa sababu tuna hakika ya kuwa ndiye wema wenyewe. Kwa maana hiyo *tunaweza kumpenda kuliko tunavyomfahamu;* tena ndani mwake tunapenda zaidi yale yaliyofichika, kwa kuwa tunaamini ndiyo maisha yake ya dhati yanayopita uwezo wowote wa kujua. Basi, hapa duniani upendo kwa Mungu unashinda ujuzi unaomhusu. Hilo ni ajabu linalotuonyesha ukuu wa upendo juu ya imani na tumaini, juu ya ujuzi wowote tunaoweza kuwa nao duniani, na hata juu ya tendo la kuzama katika sala, kwa kuwa hata hilo halimpati bado Mungu jinsi alivyo, na utamu ulilonalo unatokana na upendo unaoliongoza. Ndiyo sababu *upendo ni kifungo cha ukamilifu:* hakuna adili linalotuunganisha na Mungu kwa undani kuliko hili, wala pasipo hili.

Pamoja na mapokeo yote ya Kanisa tukariri kwamba ukamilifu wa Kikristo umo hasa katika *upendo wa vitendo ambao unatuunganisha na Mungu* katika ukavu kama katika faraja, na kuzaa kila aina ya vitendo vyema. Kwa usahihi zaidi ukamilifu haumo hasa katika adili lenyewe la upendo, bali katika utekelezaji wake ambao kwa waliokamilika ni wa kudumu. Kwa sababu lengo la adili ni kutekelezwa, na ukamilifu umo katika *muungano wa kudumu na Mungu.* Kumbe Watulivu walikataa utendaji wowote kwa kisingizio cha kumuachia Mungu tu kutenda; hali yao ya kutotenda ilikuwa ya kujitakia, si ya kujaliwa: hivyo walifuta juhudi wakasinziasinzia tu! Kinyume chao, ni wale wanaopindua mpangilio wa upendo wakidhani ukamilifu umo katika kuwasaidia watu, wakati upendo kwa Mungu ni wa juu kuliko ule kwa jirani ambao ni ishara na tunda lake tu. Wengine tena, wanaozingatia zaidi maisha ya Kiroho, wanazidisha matendo ya ibada badala ya kulenga sala sahili ya kimapenzi ambayo ni kama tendo moja tu linalodumu kwa muda fulani.

Basi upendo unatakiwa kushika nafasi ya kwanza rohoni mwetu, juu kuliko hamu ya ujuzi na ya maendeleo yoyote ya kibinadamu; hapo utazidisha nguvu zetu zote kwa kumtumikia Mungu na jirani.

**HAPA DUNIANI UPENDO HAUWEZI KUDUMU KAMA MBINGUNI**

Mungu tu anaweza kujipenda anavyostahili, kama vile mwenyewe tu anavyoweza kujifahamu kikamilifu; lakini watakatifu wa mbinguni, ingawa hawampendi anavyostahili, *wanampenda kwa nguvu zao zote, kwa upendo wa kudumu moja kwa moja.* Hiyo haiwezekani duniani, hasa kutokana na usingizi. Ukamilifu unaowezekana hapa ni ule *unaozuia yale yote yanayopinga upendo wa Mungu* (yaani dhambi ya mauti) *na yale yote yanayozuia upendo usimuelekee kikamilifu.* Waadilifu wanaoanza maisha ya Kiroho na wale wanaoendelea wanalenga huo muungano na Mungu ambao ni maalumu wa waliokamilika: kwao upendo *unazuia* sio tu *dhambi ya mauti* na *dhambi nyepesi za makusudi,* bali pia *kasoro za hiari,* k.mf. juhudi pungufu katika kumtumikia Mungu, na *mazoea ya kutenda kwa namna pungufu* (kulingana na talanta zao) *na ya kupokea sakramenti pasipo utashi kuitamani zaidi.*

Upendo wa waliokamilika kwa jirani *unaenea* si kwa wote jumla tu, bali ikipatikana nafasi kwa kila mmoja

wanaofungamana naye, hata adui. Tena ndani mwao upendo huo wa kidugu *una nguvu* hata ya kujitolea mali na uhai, kwa kuwa Bwana ametuambia, "Amri yangu ndiyo hii: Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi" (Yoh 15:12). Ndiyo sababu Mt. Paulo aliandika, "Nami kwa furaha nyingi nitatapanya, tena nitatapanywa kwa ajili ya roho zenu" (2Kor 12:15). Ili tufikie hatua hiyo vinahitajika: kazi kubwa juu ya nafsi zetu, juhudi halisi, moyo wa kujikana na kujikatalia hivi kwamba mapendo yetu yaache kuteremkia vitu vya dunia au ubinafsi, na badala yake yazidi kumuinukia Mungu kwa usafi na nguvu. *Roho ikiacha kushuka, inapanda kwa Mungu.* Hapa duniani haiwezi kubaki pale ilipo; sheria yake, kama ile ya moto, ni kupanda, si kushuka.

Hapa duniani upendo wa waliokamilika, ingawa haudumu moja kwa moja kama ule wa mbinguni, unatenda karibu mfululizo na kwa namna ya ajabu: "Upendo ni jambo kubwa sana; ni jema kushinda mema yote. Upendo peke yake hugeuza mazito kuwa mepesi, hubeba magumu kwa urahisi… Upendo una hamu ya kupaa, hautaki kuzuiwa na mambo ya chini… Upendo umetoka kwa Mungu, hauwezi kutulia isipokuwa kwa Mungu peke yake mbali na viumbe vyote. Mwenye upendo huenda kama kuruka, huenda mbio kwa furaha, yu huru, hazuiliki, hutoa yote kusudi apewe yote; katika mambo yote yeye hupata yote, kwa sababu humtegemea yule aliye juu kabisa, ndiye asili panapotokea mema yote… Mara nyingi upendo haujui kiasi, huchangamka kupita kiasi chochote… Upendo hukesha unapolala, hausinzii usingizi; unapochoka haupumziki… Kama moto unaoteketea, kama mwenge unaowaka huruka juu, hupenya kila mahali" (Kumfuasa Yesu Kristo III,5:3-5).

Ndiyo maisha ya watakatifu, na ndiyo wito wetu, kwa kuwa tunaitwa mbinguni, ambapo wapo watakatifu tu. Ili tufike huko tunapaswa kutakasa kila tendo la siku zetu, tukikumbuka kwamba juu ya mfululizo wa matukio ya kila siku (ya kupendeza na ya kuchukiza, yaliyotarajiwa na yasiyotarajiwa) kuna *mfululizo sambamba wa neema za msaada* tunazojaliwa nukta kwa nukta ili tufaidi upeo matukio hayo. Hapo tutayaona sio tu upande wa hisi au wa akili iliyopotoshwa na umimi, bali upande wa roho kwa imani. Yatakuwa mafundisho yanayotekeleza yale ya Injili, na polepole maongezi kati ya Bwana na sisi yataelekea kufululiza: ndiyo maisha halisi ya Kiroho na kama mwanzo wa uzima wa milele.

## 1.9. *UKUU WA UKAMILIFU WA KIKRISTO NA HERI NANE*

Hotuba ya mlimani ni muhtasari wa mafundisho aliyoyatoa Mwokozi ili kutimiliza sheria ya Musa na kusahihisha ufafanuzi wake usiofaa. Heri nane alizotangaza mwanzoni mwa hotuba hiyo zinaonyesha ukamilifu anaowaitia wote na zinajumlisha vizuri ajabu kipeo cha maisha ya Kikristo katika ukuu wake wote.

Neno la kwanza la Yesu ni kuahidi heri na kuelekeza njia za kuipata. Alianza na heri kwa sababu kila mtu kwa umbile lake anaitamani: ndiyo lengo ambalo wote, watake wasitake, wanalitafuta katika yote. Lakini mara nyingi wanatafuta heri pasipokuwepo, watakapokuta tu mahangaiko na unyonge. Tumsikilize Bwana ambaye anatuambia heri halisi ya kudumu na *lengo* la maisha yetu viko wapi, tena anatupatia *njia* za kuvipata. Lengo linaloelekezwa kwa majina mbalimbali ni ile heri ya milele ambayo waadilifu wanaanza kuionja hapa duniani: ni ufalme wa Mungu, nchi ya ahadi, faraja kamili, utimilifu wa hamu zote zilizo halali na takatifu, rehema kuu, kumuona Baba yetu. Njia zinakwenda kinyume cha maelekezo ya ulimwengu, kwa kuwa lengo ni tofauti mno.

Mpangilio wa heri nane *unaanzia chini kwenda juu* (kinyume na sala ya Baba Yetu ambayo kisha kuzingatia utukufu wa Mungu inateremkia mahitaji yetu). Heri tatu za kwanza ni zile *zinazopatikana katika kukwepa dhambi na kukombolewa:* katika ufukara uliopokewa kwa upendo wa Mungu, katika upole na katika machozi ya majuto. Heri mbili zinazofuata ni zile za *maisha ya utendaji* ya Kikristo: zinahusu kiu ya haki na utekelezaji wa huruma kwa jirani. Halafu zinakuja zile za *kuzama katika mafumbo ya Mungu:* usafi wa moyo unaotuandaa kumuona na amani inayotokana na hekima ya kweli. Heri ya mwisho na bora kuliko zote ni ile inayoziunganisha zilizotangulia hata wakati wa *kudhulumiwa* kwa ajili ya haki.

### HERI ZA UKOMBOZI KUTOKA DHAMBI

Hizo zinahusu hatua ya utakaso, ambayo ni maalumu kwa wanaoanza.

Wakati ulimwengu unasema heri inapatikana katika utajiri na heshima, Bwana amesema wazi, kwa hakika tulivu ya ukweli, *"Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao"* (Math 5:3). Kila heri ina *viwango* mbalimbali: heri walio mafukara bila ya kunung'unika, kwa uvumilivu, bila ya kijicho, hata wakikosa chakula, na wanaofanya kazi wakimtegemea Mungu tu. Heri waliobahatika zaidi, lakini hawana roho ya utajiri, fahari, kiburi, wala hawashikamani na mali. Heri zaidi walioacha vyote ili kumfuata Yesu, wakijifanya mafukara kwa hiari na kuishi kweli wito huo; hao watapata mara mia hapa duniani halafu uzima wa milele. Mafukara hao, kwa kuvuviwa *kipaji cha uchaji,* wanafuata njia nyembamba ambayo baadaye inakuwa barabara kuu ya mbinguni, ambapo roho inazidi kutanuka, wakati njia pana za ulimwengu zinaelekea maangamizi: "Ole wenu ninyi ambao mmeshiba sasa, kwa kuwa mtaona njaa" (Lk 6:25). Kinyume chake, ufukara wenye heri unatufungulia ufalme wa Mungu, ulio bora kuliko mali yoyote, yanavyoonyesha maisha ya Mt. Fransisko wa Asizi. Heri wanyenyekevu wa moyo, wasiojitwalia mema ya kimwili wala ya Kiroho, wala heshima wala upendo, na ambao wanatafuta ufalme wa Mungu tu.

Wakati tamaa ya utajiri inawatenganisha watu na kusababisha ugomvi, mashtaka, kesi, dhuluma na hata

vita kati ya mataifa, Yesu amesema, *"Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi"* (Math 5:5). Heri wasiowakasirikia ndugu zao, wasiotafuta kulipa kisasi wala kutawala wengine, wasiohukumu bila ya msingi, wasiomuona jirani kama adui wa kushindana naye, bali kama ndugu wa kusaidiwa. *Kipaji cha ibada* ndicho kinachotutia upole huo kwa mapendo ya kitoto kabisa kwa Mungu, Baba yetu sote. Walio wapole hawashikamani mno na mtazamo wao wala hawaoni haja ya kuapa kwa chochote kile. Ili tuwe wapole hivyo, hata kwa wanaotutendea kwa ukali, tunahitaji kuungana na Yesu aliyesema, "Mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo" (Math 11:29). Yeye hakuvunja "mwanzi uliopondeka" wala kuzima "utambi utokao moshi" (Math 12:20) hata alifananishwa na "mwanakondoo apelekwaye machinjoni" asifunue "kinywa chake" (Isa 53:7; Mdo 8:32). Upole huo si ule wa kulaumiwa usiomchukiza yeyote kwa sababu unaogopa, bali ni adili linalotegemea upendo mkubwa kwa Mungu na kwa jirani: unazidisha thamani ya huduma unayotoa, unaweza kusema lolote na kufanya mashauri yake yapokewe, na hata lawama kwa kuwa anayeambiwa anatambua vinatokana na upendo mkubwa. Heri walio wapole, maana watarithi nchi halisi ya ahadi, na tangu sasa wanajipatia kitakatifu mioyo ya wale wanaojiaminisha kwao.

Wakati ulimwengu unasema furaha imo katika anasa, Yesu amesema, *"Heri wenye huzuni, maana hao watafarijika"* (Math 5:4). Tajiri alijibiwa vilevile, "Wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa" (Lk 16:25). Heri wale ambao, kama Lazaro, wanateseka kwa subira, bila ya kufarijiwa na watu; ila Mungu anaona machozi yao. Wenye heri zaidi wanaolia juu ya dhambi zao, ambao kwa *kipaji cha elimu* wanang'amua kwamba dhambi ndiyo jambo baya kuliko yote, na wanajipatia msamaha kwa kulia machozi. Zaidi tena wana heri wanaolia kwa upendo wakizingatia huruma na hisani zisizo na mipaka za Mchungaji mwema aliyejitoa sadaka kwa kondoo zake. Hao wanapokea farajia isiyo na kifani kuanzia hapa duniani.

**HERI ZA MAISHA YA UTENDAJI YA KIKRISTO**

Furaha nyingine takatifu zimeandaliwa kwa mwadilifu ambaye, kisha kuopolewa maovuni, anajitahidi kutenda mema kwa moyo wote.

Mtu anayetawaliwa na kiburi anamuita mwenye heri yule anayeishi na kutenda anavyotaka, asiyekaa chini ya wengine bali anawashinda. Kumbe Yesu amesema, *"Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa"* (Math 5:6). Maana pana ya neno "haki" ni kumpatia Mungu yale anayostahili; hapo kwa upendo wake hata kiumbe anapatiwa anayostahili: kama malipo Mungu anajitoa kwetu. Ndio utaratibu kamili katika utiifu unaoongozwa na upendo unaopanua moyo. Wenye heri wanaotamani haki hiyo hadi kuwa na njaa na kiu nayo. Kwa namna fulani watashibishwa kuanzia hapa duniani, kwa kugeuka watakatifu. "Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe… mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake" (Yoh 7:37-38). Lakini ili tudumishe kiu hiyo hata katikati ya ukavu wa hisi, upinzani, vizuio, kukabili ukweli, ni lazima tupokee kwa mikono miwili *kipaji cha nguvu,* kinachotutia moyo katika matatizo tusishindwe wala tusikate tamaa. "Bwana anataka tuitamani haki hiyo hivi kwamba tusishibe kamwe hapa duniani, kama vile mroho asivyoshiba kamwe… Watashiba watakapomuona Mungu milele… na tangu sasa katika mema ya Kiroho… Watu wakiwa katika dhambi, hawasikii njaa ya Kiroho, lakini wanapoacha dhambi hapo wanaisikia" (Mt. Thoma wa Akwino).

Lakini njaa na kiu za haki hazitakiwi kuendana na ari chungu kuhusu wakosefu: *"Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema"* (Math 5:7). Katika maisha yetu, kama vile kwa Mungu, haki inapaswa kuungana daima na huruma. Hatuwezi kuwa wakamilifu tusipomsaidia mwenye uchungu au ugonjwa kama alivyofanya Msamaria mwema. Bwana atawalipa wanaojitolea bilauri ya maji kwa upendo wake, wanaokaribisha mezani pao mafukara, walemavu na vipofu. Mkristo anapaswa kufurahia zaidi "kutoa kuliko kupokea" (Mdo 20:35), tena kusamehe (kwa Kilatini "kutoa zaidi") waliomchukiza, kusahau dharau na kupatana na nduguye kabla hajatolea altareni sadaka yake. *Kipaji cha shauri* kinatuelekeza kwenye huruma, na kutufanya tutambue mateso ya wenzetu pamoja na dawa yake, yaani pengine neno la kuwainua na kuwafariji.

Kama utendaji wetu utafuata mara nyingi maadili hayo mawili ya haki na huruma, pamoja na vipaji vinavyohusiana nayo, tutajaa furaha takatifu tokea hapa duniani na kuwa tayari kuingizwa katika mafumbo ya Mungu.

**HERI ZA KUZAMA NDANI YA MUNGU NA KUUNGANA NAYE**

Baadhi ya wanafalsafa walidhani kuwa heri imo katika kujua ukweli, lakini hawakujali usafi wa moyo; kwa hiyo maisha yao yalikuwa yakipingana na mafundisho yao katika mambo kadhaa. Kumbe Yesu amesema, *"Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu"* (Math 5:8). Hakusema wana heri walio na akili sana pamoja na muda na njia ya kuistawisha, bali wenye moyo safi, hata kama kimaumbile akili yao ni ndogo kuliko ya wengine. Hao watamuona Mungu: ni kama maji safi ya ziwa ambamo uangavu wa anga unarudishwa, au kama kioo cha Kiroho ambamo sura ya Mungu inaonekana. Lakini usafi halisi wa moyo unadai kujifisha kwa bidii: "Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe… Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe" (Math 5:29-30). Tunapaswa kuangalia hasa tuwe na *nia*

*njema:* si kutoa sadaka mbele ya watu ili kuonekana nao, wala kusali ili kusifiwa nao, bali kutafuta tu tumpendeze Baba "aonaye sirini" (Math 6:4,6,18). Hapo tu yatatimia maneno ya Mwalimu: "Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru" (Math 6:22). Tokea hapa duniani Mkristo atamuona Mungu kwa namna fulani katika jirani yake, hata katika watu kadhaa ambao mwanzoni aliwaona wanampinga; atamuona katika Maandiko, katika maisha ya Kanisa, katika nafasi mbalimbali za maisha yake mwenyewe, hata katika majaribu, ambapo atajifunza maongozi ya Mungu. Ndipo sala ya kumiminiwa inapopatikana kwa msaada wa *kipaji cha akili,* tunapojiandaa kumuona Mungu na uzuri wake usiopimika; hapo hamu zetu zote zitatimia, nasi tutakuwa kama tumelewa na mto wa vitamu vya Kiroho.

Tangu hapa duniani huko kuzama ndani ya Mungu kunazaa matunda; kunaleta amani angavu, inavyotangaza heri ya saba: *"Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu"* (Math 5:9). Heri hiyo inahusiana na *kipaji cha hekima* kinachotufanya tuonje mafumbo ya milele, na kuona kwa namna fulani mambo yote ndani ya Mungu. Miangaza ya Roho Mtakatifu, ambayo kipaji hicho kinatusaidia kuipokea kwa mikono miwili, inatuonyesha polepole utaratibu mzuri ajabu wa maongozi ya Mungu, pengine palepale - na hasa palepale - tulipopatwa kwanza na mshtuko mkubwa katika matukio machungu yasiyotarajiwa ambayo Mungu aliyaruhusu kwa manufaa makubwa zaidi. Hatuwezi kung'amua hivyo anavyoongoza maisha yetu bila ya kufaidi amani kubwa ambayo ni utulivu wa utaratibu. Ili tusifadhaishwe na matukio hayo, bali tuyapokee yote mikononi mwa Mungu kama njia ya kumuendea, ni lazima kujiachilia kwa Roho Mtakatifu, anayetaka kutujalia hatua kwa hatua kutazama mambo ya Kimungu, ambako ni sharti la kuungana naye. Ndiyo sababu tumejaliwa kipaji cha hekima. Miangaza yake inatupatia amani angavu, sio tu kwa ajili yetu, bali kwa jirani pia; inatufanya *wenye amani;* inatusaidia kuwapa amani watu wasiotulia, kuwapenda maadui, kusema maneno ya upatanisho yanayomaliza ugomvi. Hiyo amani ambayo ulimwengu hauwezi kuitoa, ndiyo ishara ya *watoto halisi wa Mungu* ambao hawaachi kumfikiria Baba wa mbinguni.

Hatimaye, katika heri ya nane, Bwana ametuonyesha kwamba yale yote aliyoyasema yanathibitishwa hasa na majaribu yaliyovumiliwa kwa upendo: *"Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao"* (Math 5:10). Ndiyo hasa majaribu ya mwisho yaliyo masharti ya utakatifu. Halijasikika neno la kushangaza kama hilo: halituahidii heri milele tu, bali pia *wakati wa uchungu na dhuluma*. Ni heri isiyo ya kimaumbile hata kidogo, inaeleweka tu na wale walioangazwa na Mungu. Ndani yake kuna ngazi nyingi, kuanzia ile ya Mkristo anayeanza kuteseka kwa kuwa ametenda mema, ametii, ametoa mfano mzuri, hadi ile ya mfiadini. Heri hiyo inamhusu mwongofu anayepingwa tu katika mazingira yake; pia mtume ambaye kazi yake inazuiwa na walewale anaotaka waokoke, wasiokubali kumsamehe kwamba anawaeleza wazi kweli za Injili. Pengine makabila mazima yanapaswa kustahimili dhuluma za namna hiyo. Heri hiyo ni kamili kuliko zote kwa kuwa ni ya wale wanaofanana zaidi na Yesu msulubiwa. Kudumu wanyenyekevu, wapole na wenye huruma wakati wa dhuluma, hata kwa watesi wenyewe, na sio tu kuendelea kuwa na amani, bali kuwashirikisha wengine pia, ndio ukamilifu wa Kikristo. Si watakatifu wote walifia dini, lakini kwa viwango tofauti wote *walidhulumiwa kwa ajili ya haki* na kujua walau kidogo ule ushahidi wa moyoni uliomfanya Maria Mama wa huzuni. Yesu alisisitiza tuzo waliloahidiwa watu hao, "Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia, kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni" (Math 5:11-12). Kutokana na maneno hayo Mt. Inyasi wa Antiokia na wengineo walitamani kufia dini. Ndiyo sababu wakawa "chumvi ya dunia" na "nuru ya ulimwengu" (Math 5:13-14), na nyumba yao, iliyojengwa kwenye mwamba, ilistahimili dhoruba zote isianguke.

Heri hizo ni matendo bora ya maadili yaliyokamilishwa na vipaji, hivyo zinapita juhudi zetu na kutegemea mafumbo. Kwa maneno mengine, ukamilifu wa Kikristo ni mwanzo wa uzima wa milele, tutakapokuwa *wakamilifu kama Baba*, tukimuona na kumpenda kama mwenyewe anavyojiona na kujipenda. Mt. Teresa wa Yesu aliandika, "Vitabu kadhaa vinasema *tusijali mabaya yanayosemwa juu yetu, bali tuyafurahie* kuliko maneno ya sifa, tusijali sana heshima tunayopewa, tusishikamane na ukoo… na sijui mambo mangapi ya namna hiyo… Nionavyo mimi, *hayo ni zawadi za Mungu tu, ni mema yanayopita maumbile",* yaani yanapita uwezo wa juhudi zetu katika kutekeleza maadili; ni matunda yanayozaliwa na usikivu mkubwa kwa Roho Mtakatifu. "Tukipenda heshima na tunu za kidunia, hata tukifanya sala, au afadhali niseme tukitafakari miaka na miaka, hatutaendelea kweli kamwe. Kumbe *sala kamili inatukomboa kutoka kasoro hizo".* Maana yake pasipo sala ya kumiminiwa hatuwezi kamwe kuufikia ukamilifu.

Ndivyo ilivyoandikwa katika Kumfuasa Yesu Kristo, "Utakapofaulu *kujidharau kabisa,* uwe na hakika kwamba umepata kuonja amani yote inayowezekana hapa duniani" (III,25:3). Kwa sababu hiyohiyo, mwanafunzi anaomba *kumiminiwa sala,* "Mungu wangu, nahitaji sana neema kubwa zaidi, ikinipasa kufikia hali njema nisiweze kuzuiwa tena na kiumbe chochote… Mtu mmoja aliyekuwa na pupa ya kuruka ili afike kwako, alisema, Nani atanipa mabawa kama ndege nipate kuruka na kufika mustarehe? Mtu asiyevunja vifungo vinavyomfunga pamoja na viumbe, hatapata nafasi ya kumfikiri Mungu na mambo yake. *Ndiyo maana hatuoni watu wengi wa kuzama ndani ya Mungu, kwa kuwa wenye kujitenga kabisa na mambo mapotevu ya dunia au hata na viumbe vyote huwa wachache.* Kufanya hivi hutaka neema kubwa sana, yenye kuinua roho na kuivuta hata ipae juu ya hali yake. Lakini kama mtu hapandi vile rohoni mwake kwa

kujitenga na viumbe vyote aambatane na Mungu tu, yote ayajuayo na yote awezayo hayana maana” (III,31:1-2).

Ustawi huo kamili wa muundo wa Kiroho, yaani wa neema ya maadili na vipaji, unaonyeshwa katika heri nane si kinadharia tu, bali katika utekelezaji wake.

## 1.10. *UKAMILIFU NA USHUJAA*

Ili tutimilize tuliyoyasema kuhusu ukamilifu wa Kikristo, tunapaswa kuona kama unadai upendo mkubwa na ushujaa katika maadili yote.

### UKAMILIFU WA KIKRISTO UNADAI UPENDO MKUBWA

Baadhi ya wanateolojia walijiuliza kama ukamilifu unadai upendo mkubwa au unaweza kupatikana pasipo kiwango kikubwa cha adili hilo. Jibu la hakika ni kwamba, kama vile utu uzima unadai nguvu za mwili nyingi kuliko za mtoto (ingawa kwa nadra watoto wenye afya wana nguvu kuliko watu wazima kadhaa), hata hali ya waliokamilika inadai upendo mkubwa kuliko ule wa wanaoanza (ingawa mwanzoni mwa maisha ya Kiroho, wanaoitiwa utakatifu mkuu, wanaweza wakawa tayari na upendo mkubwa kuliko baadhi ya wazee waliokamilika). Kanisa linafundisha hivyo kwa kuwa ukamilifu unapatikana tu baada ya *kutekeleza maadili kwa muda mrefu,* na kwa utekelezaji huo maadili yanastawi zaidi na zaidi. Ikiwa mwanzoni “upendo wa kiwango cha chini *unaweza* kushinda vishawishi vyote” (Mt. Thoma wa Akwino), baadaye unavishinda *kweli* na kuzidi kuwa na nguvu. Haiwezekani kumfikiria Mkristo mkamilifu, aliye juu kuliko wanaoanza na wanaoendelea, asiye na upendo mkubwa, ingawa kupima kiwango kinachotakiwa ni kazi ya Mungu tu. Mfano wake ni utu uzima, ambao kwa kawaida unadai nguvu za mwili nyingi kuliko zile za utoto, lakini bila ya kipimo maalumu.

Fundisho hilo msingi wake mwingine ni kwamba *upendo unastawi kwa nguvu* kuliko kwa uenezi. *Viwango vitatu* vya upendo vinavyowafaa wanaoanza, wanaoendelea na waliokamilika, *ni viwango vya nguvu* ya adili hilo, ambalo linazidi kuzuia dhambi nyepesi na kututenganisha na malimwengu ili tuambatane na Mungu. Hata hivyo mtu mmoja anaweza akakwepa dhambi hizo kuliko mwingine mwenye kiwango kilekile cha upendo, kwa sababu kwa wakati huo ana juhudi nyingi zaidi au halazimiki kupambana zaidi na tabia yake, uchovu na upinzani. Mt. Teresa wa Yesu alipokuwa nje ya monasteri katika nafasi zisizotazamiwa ilimtokea kutenda dhambi nyepesi nyingi zaidi, lakini pia kujipatia stahili nyingi zaidi kutokana na majaribu aliyoyashinda. Ni kama mtu ambaye akipanda mlima mrefu, inamtokea kuanguka kuliko anapotembea mahali tambarare, lakini ana stahili ya kutenda kazi ngumu ya kupanda.

Basi, ukamilifu unadai upendo mkubwa unaopatikana tu kwa kushinda kwanza vishawishi vingi na kujipatia stahili nyingi. *“Ukamilifu umo katika kumpenda kikamilifu Mungu na kujidharau...* Kuna watu wanaoridhika na aina yoyote ya kukusanya mawazo na ya kuongoka; wengine wanaishia katika kutekeleza maadili kwa ukamilifu mkubwa au mdogo, na kuwa waaminifu katika sala na kujinyima. Wanachokosa ni kujishusha, kuwa mafukara au kujikana na kuwa safi Kiroho… *Wanakwepa msalaba ambao ungewalinganisha na Bwana wetu Yesu Kristo.* Wanajifanya lengo ndani ya Mungu, jambo ambalo ni kinyume kabisa cha upendo… Ningependa kuwa na uwezo wa kuwathibitishia watu wote wa Kiroho ukweli huu: kwamba njia ya Mungu haimo katika kuzidisha mawazo, mbinu na maonjo, ingawa kwa namna fulani wanaoanza wanahitaji vitu hivyo. Lakini jambo moja tu ni la lazima kabisa, yaani kuweza kujikana moja kwa moja, kwa ndani na kwa nje, kujitoa mhanga kwa Yesu Kristo kama sadaka kamili ya kuteketezwa. Katika zoezi hilo tu tutayakuta mengine yote na mengi zaidi tena. Kumbe, tukipuuzia zoezi hilo, ambalo ni muhtasari na mzizi wa maadili, tutakuta tu vitu visivyo muhimu, na maendeleo yatakwama, hata tukiwa na mawazo na neema za kimalaika… Mtu wa Kiroho akifaulu kujiangamiza, yaani kutekeleza unyenyekevu kamili, hapo muungano wake na Mungu utatimia, nao ndio hali bora tena kuu tunayoweza kuifikia katika maisha haya” (Mt. Yohane wa Msalaba).

Mafundisho hayo yanalingana na yale ya Mt. Thoma wa Akwino alipoeleza ukamilifu kuwa “hali ya wale ambao wanalenga hasa kuambatana na Mungu na kumfurahia, na ambao wanatamani kufa ili kuishi na Kristo”, wakikabili magumu kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa watu. Basi, pasipo juhudi kubwa haiwezekani kufikia upendo mkubwa, hata kwa miaka ya kukomunika kila siku na kutenda mema mapungufu. Kwa njia hizo tunaweza kujidumisha katika neema inayotia utakatifu au kuinuka mapema baada ya kutenda dhambi ya mauti, lakini hatutafikia kamwe upendo mkubwa.

### UKAMILIFU UNADAI USHUJAA KATIKA MAADILI YOTE

Ikiwa upendo kwa nchi yetu unatudai ushujaa inapopatwa na hatari, bila ya shaka ukamilifu wa Kikristo unadai ushujaa katika maadili, walau upande wa nia. Kwa msaada wa Mungu, kila Mkristo anapaswa kuwa tayari auawe kwa ajili ya imani, kama atajikuta analazimika kuchagua aikane au kuteswa. Padri aliyewekwa wakfu awachunge watu anapaswa kuhatarisha uhai wake ili kuwaletea sakramenti wakiwa na shida kubwa nazo (k.mf. kwenda kuwaungamisha wenye tauni). Zaidi tena askofu, katika nafasi kadhaa anapaswa kutoa uhai wake kwa ajili ya kundi lake. Tunapaswa pia kuwapenda maadui wetu na kuwasaidia wakiwa na shida

kubwa. Ushujaa huo wa lazima kwa wokovu unadaiwa zaidi na ukamilifu.

Mkristo akiwa mwaminifu katika wajibu wowote wa kila siku, awe na hakika kwamba Bwana atamsaidia kulingana na ugumu wa wajibu mkubwa wa dharura: "Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia" (Lk 16:10). "Msifadhaike kwa kuwaza maneno yenu jinsi mtakavyojibu au kusema; kwa kuwa Roho Mtakatifu atawafundisha saa ileile yawapasayo kuyasema" (Lk 12:11-12). Vipaji vyake ni vya lazima kwa wokovu ili tupokee kwa dhati na kwa mikono miwili uvuvio wake wa pekee pale ambapo maadili hayatoshi, kutokana na nafasi kuwa ngumu zaidi. Lakini kuwa tayari rohoni kutekeleza maadili kwa ushujaa ni tofauti na *kuwa nayo kwa kiwango cha ushujaa.*

Katika sura ijayo tutaona kuwa ukamilifu unadai Mungu atakase hisi na roho ili kufuta kasoro za wanaoanza na za wanaoendelea. Mt. Yohane wa Msalaba alifafanua matakaso hayo yanavyowatokea wanasala wanaoitiwa ukamilifu mkuu kwa njia ya mkato; lakini mambo ya namna hiyo yanawatokea wengine pia ambao kwao matakaso hayo ya ndani yanaendana na huzuni na shida za utume. Mara nyingi katika majaribu hayo mtu anatakiwa kushinda kishujaa vishawishi dhidi ya usafi wa moyo na subira, halafu dhidi ya imani, tumaini na upendo. Hapo *unadaiwa ushujaa fulani katika maadili,* ambao baadaye unaweza na kutakiwa uongezeke.

Hatimaye, *upendo wa Kikristo,* kwa kuwa unalenga kutulinganisha na Mwokozi aliyesulubiwa kwa ajili yetu, *unatakiwa kulenga ushujaa katika maadili.* Hiyo inatokana na yale tuliyoyasema kwanza: tendo la kishujaa linalompasa Mkristo yeyote linalingana na *lengo* la upendo, yaani kumpenda Mungu kuliko yote. Kwa umbile lake, upendo huo unampenda kuliko uhai wa mwili, kwa hiyo unapaswa uwe tayari kuutoa. "Upendo wa Mungu unafanya tutende bila ya kikomo na kuvumilia bila ya kuchoka" (Mt. Bernardo) hasa katika tabu za ndani na za nje ambazo watumishi wa Mungu wanapaswa kustahimili kwa utakaso wao na kwa kuchangia pamoja na Yesu wokovu wa watu.

Mtu anaweza akapinga mafundisho hayo akisema eti! Yangekuwa kweli Wakristo wanaofikia ushujaa wangekuwa wengi zaidi. Mt. Thoma alijibu hoja ya namna hiyo kuhusu idadi ya wateule, "Jema linalolingana na umbile la binadamu wote kwa kawaida linafikiwa; lakini sivyo kuhusu jema linalopita umbile hilo". Ni adimu kudumu maisha yote katika neema inayotia utakatifu, bila ya kutenda dhambi ya mauti baada ya ubatizo. Hata hivyo kwa mfumo wake neema inayotia utakatifu *inalenga uzima wa milele, kwa hiyo idumu milele* isiangamizwe kamwe na dhambi ya mauti. Ila tumepokea hazina hiyo katika chungu cha udongo, hivyo tamaa na kiburi vinaweza kufanya tuipoteze. Wengi wanaishi kijuujuu tu wakifuata hisi, na wachache tu wanafuata akili nyofu; hata hivyo kwa umbile lao wana akili, nayo neema inatakiwa kuwafanya waishi Kimungu. Vivyo hivyo upendo ni mbegu ya uzima wa milele, hivyo kwa mfumo wake unalenga ushujaa ili kudumu mwaminifu kwa Mungu.

Utakatifu mkubwa unadhihirika hasa katika *ulinganifu wa maadili yote, hata yale yaliyo mbalimbali zaidi.* Kimaumbile mmoja anaelekea nguvu, lakini si upole; mwingine ni kinyume. Kwa namna fulani umbile linaelekea daima *upande mmoja,* hivi kwamba linahitaji kukamilishwa na maadili tofauti. Kuunganisha nguvu kubwa na upole kamili, kupenda motomoto ukweli na haki pamoja na kuhurumia waliopotoka, kunathibitisha muungano wa dhati na Mungu, kwa kuwa yaliyogawanyika katika ulimwengu huwa yameunganika katika ufalme wake, na hasa ndani mwake mwenyewe. Utakatifu ni mfano mzuri wa umoja wa sifa mbalimbali zisizo na mipaka ndani ya ukuu wa Umungu.

## 1.11. *UKAMILIFU WA KIKRISTO NA MATAKASO YA KIMUNGU*

Ukamilifu wa Kikristo umo *hasa katika upendo,* unaotuunganisha na Mungu na jirani, lakini unadai pia matendo ya maadili mengine na ya vipaji vya Roho Mtakatifu. Ni kama binadamu ambaye mwili ni sehemu ya utu wake, ingawa utu umo hasa katika roho inayomtofautisha na wanyama. Hata katika suala hilo watu walipotoka pande mbili. Watulivu walipuuzia maadili hayo na kufuta utekelezaji wa kujinyima na wa kuwatendea mema majirani. Kinyume chao, wengine walisisitiza matendo ya toba, ibada na huruma wasitambue vya kutosha ukuu wa upendo wa Mungu, na hivyo wakazingatia juhudi zao na utume wa njenje kuliko mafumbo.

Ukamilifu wa Kikristo unadai *matendo ya maadili mengine ambayo ni ya amri* na yanatakiwa kuhuishwa na upendo. Amri kuu inatudai tuzidi kukua katika maadili yote kama vile katika upendo. Kutokana na yale tuliyoyasema kuhusu muundo wa Kiroho, ukamilifu unadai maadili yote ya kumiminiwa na ya kujipatia, halafu vipaji saba vinavyohusiana na upendo hivi kwamba vinakua pamoja nao.

Upendo ndio *kiungo cha ukamilifu* huo wa maadili na vipaji, ambavyo ni kama fungu la maua la kumtolea Mungu; lakini upendo wa wanaoanza hautoshi kuunda ukamilifu, mpaka ukue. Kwa kawaida upendo wa waliokamilika unapaswa kuwa *mkubwa na motomoto* kuliko ule wa wanaoanza na wanaoendelea; unadai pia utekelezaji wa maadili yote na wa vipaji saba kwa kiwango kinacholingana na upendo. Mtu hawezi kuwa mkamilifu bila ya kupenya mafumbo ya imani kwa kipaji cha akili, wala kuyaonja kwa kile cha hekima (ingawa hicho kinaelekea zaidi sala hasa katika watakatifu kadhaa na utendaji katika wengine).

Ili tuifikie hatua ya waliokamilika tunahitaji *kujikana, kuwa wasikivu kwa Roho Mtakatifu* na *kupokea kwa mikono miwili misalaba* au matakaso yanayokusudiwa kufisha ndani mwetu umimi na kuhakikisha nafasi ya

kwanza ishikwe moja kwa moja na upendo wa Mungu wenye kuangaza na kuwaka zaidi na zaidi.

## MATAKASO YANAYODAIWA NA UKAMILIFU WA KIKRISTO

*"Kwa ajili yake (Kristo) nimepata hasara ya mambo yote* nikiyahesabu kuwa kama mavi *ili nipate Kristo;* tena nionekane katika yeye… ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na *ushirika wa mateso yake*, nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yoyote kuufikia ufufuo wa wafu. *Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu;* la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo, kwa ajili yake, nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu: nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu, katika Kristo Yesu. Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo… Lakini, hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo*"* (Fil 3:8-9,10-15,16). Ndio ukamilifu wa Kikristo kweli, si wa kifalsafa tu; nao tumependekezewa sisi sote tunaolishwa na Maandiko hayo hadi mwisho wa dunia.

Watu kadhaa walisema eti! Mt. Thoma wa Akwino alizungumzia kidogo tu matakaso ya Kiroho. Kumbe alifafanua maneno hayo kwa Wafilipi kuhusu *kushiriki mateso ya Kristo* kusudi tusipoteze misalaba yetu, tufanane naye na kuwaokoa watu pamoja naye (maana ulimwengu umejaa misalaba tasa, kama ule wa mhalifu wa pili aliyesulubiwa pamoja na Yesu: njia ya kuifanya ilete faida ni kuibeba kwa uvumilivu na upendo pamoja naye). Pia alifafanua mfano wa mzabibu wa kweli ambao Baba *anausafishia kila tawi lizaalo*: "Ili waadilifu wanaozaa matunda wazae kwa wingi zaidi, Mungu anapogolea ndani mwao yaliyo ya ziada; anawatakasa kwa kuwatumia tabu na kuruhusu washambuliwe na vishawishi ambavyo katikati yake wazidishe nguvu na juhudi. *Hapana duniani mtu safi kiasi kwamba asihitaji kutakaswa zaidi".* Ndiyo matakaso ya Kimungu yaliyokuja kuelezwa zaidi na Mt. Yohane wa Msalaba, mwalimu wa Kanisa aliyeyachimba kuliko wote. Katika mafundisho yake tunapata pia mwanga mkubwa ili kutofautisha hatua tatu za maisha ya Kiroho.

Basi, tuone yale yanayohitajika ili tufikie *kilele* cha ustawi wa *kawaida* wa upendo. Tunaposema kilele tusisahau neno kawaida; vilevile tunaposema kawaida tusisahau neno kilele. Mara nyingi tunaita "ya kawaida" yale ambayo wengi wanayafikia kweli, bila ya kujiuliza vya kutosha juu ya yale ambayo *wangeyafikia* kama wangekuwa waaminifu. Haifai kutamka eti! Muungano wa karibu mfululizo na Mungu uko *juu* kuliko kilele cha ustawi wa kawaida wa upendo, kwa sababu tu wengi hawaufikii. Tusichanganye *yanayotakiwa kuwa* na yale *yaliyopo* maishani, la sivyo tutasema uaminifu halisi hauwezekani, kwa kuwa walio wengi wanajali *faida* yao (k.mf. pesa na anasa) kuliko *uadilifu.*

Wengi wanafuata yale *yasiyo mabaya mno* badala ya kutimiza *wajibu* unaowadai juhudi kubwa katika mazingira ambamo yote yanawaelekeza kudidimia; wanafuata mkondo kadiri ya sera ya kujitahidi kidogo iwezekanavyo. Sio tu kwamba wanayavumilia *yasiyo mabaya mno,* bali *wanayatenda* na mara nyingi wanayaunga mkono ili wadumishe hali yao. Wanasiasa wengi wanajitetea kwamba wanafanya hivyo ili kuepa mabaya makubwa zaidi ambayo wengine wangeyafanya mahali pao kama wenyewe wangepotewa na wadhifa wao kwa kutowapendeza watu. Hivyo, badala ya kuwasaidia *kurudi juu* wanawasaidia *kudidimia,* wakijitahidi tu kupunguza kasi ya anguko. Kuna kitu cha namna hiyo katika maisha ya Kiroho pia.

Tukumbuke kwamba *sheria* ya ustawi wa upendo ni tofauti na ile ya utu wetu ulioanguka. Hata baada ya ubatizo tunaendelea kuwa na madonda yanayotuelekeza kudidimia, kumbe neema inayotuumba upya hatua kwa hatua inatufanya tupande daima. Tunapongojea uzima wa milele, maisha yetu yanatushangaza kwa jinsi yalivyo na mwanga na giza pamoja: "Kwa sababu *mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana"* (Gal 5:16-17). Upendo wa Kristo uliomo ndani mwetu haujashinda umimi wetu moja kwa moja, bali unahitaji bado kushindana nao kwa nguvu. Unahitajika utakaso mkubwa; sio tu ule tunaotakiwa kujipatia, bali ule tunaopatiwa na Mungu anapokuja kupogolea matawi ya mzabibu ili yazidi kuzaa.

"Ili tufikie nuru ya Kimungu na muungano kamili wa upendo na Mungu - nayasemea yanayowezekana duniani - roho inapaswa kupitia *usiku wenye giza…* Kwa kawaida, wateule wanapojitahidi kufikia hiyo *hali ya ukamilifu* wanakuta giza nene, na kupaswa kuteseka katika mwili na roho namna ambayo ujuzi wa kibinadamu hauwezi kueleza hata kidogo… Picha zake hazijulikani na mtu isipokuwa na wale waliyoyang'amua" (Mt. Yohane wa Msalaba). Tawi ambalo Mungu analisafisha si hai tu, bali anajitambua pia, na ili mtu aweze kujua kupogolewa ni nini anatakiwa kukupata mwenyewe. Kila mmoja anapaswa kubeba *msalaba wake,* lakini hajui msalaba ni nini kabla hajaubeba kwa upendo.

Bila ya tabu hatufikii kushinda *kikamilifu* umimi, tamaa, uzembe, hasira, wivu, kijicho, utovu wa haki, kujipendea, kujidai kipumbavu, *kujifanya lengo* hata la ibada, hamu kubwa mno ya kufarijika, kiburi upande wa akili na wa roho, yale yote yanayopingana na imani na tumaini kwa Mungu, ili tumpende *kikamilifu* "kwa moyo wote, kwa akili yote, kwa nguvu zote, kwa roho yote" na kumpenda jirani, hata adui, *tunavyojipenda.* Tunahitaji kwa wingi imani, subira na ustahimilivu ili kudumu katika upendo kwa vyovyote, yanapotimia maneno ya Mt. Paulo: "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa" (2Tim 3:12).

Kwa hiyo Mt. Yohane wa Msalaba, akielekeza njia inayofikisha kwa hakika na haraka zaidi *kwenye ukamilifu*, alisema hatuwezi kuufikia *Mungu asipotutakasa hisi* - ndiyo ishara ya kuingia hatua ya mwanga - na *asipotutakasa roho* - kwenye kizingiti cha hatua ya muungano. *Kujitakasa* hakutoshi: "Mtu, hata akiwa na juhudi namna gani, hawezi kufaulu kujitakasa kikamilifu: hawezi kabisa *kujiandaa kuungana na Mungu kwa upendo kamili.* Ni lazima Mungu *mwenyewe ashughulike* na kumtakasa kwa *moto ambao ni giza kwa roho…* Roho zinaanza kuingia katika huo usiku wa giza Mungu mwenyewe anapowakomboa polepole kutoka *hali ya wanaoanza*, ambapo wanatafakari katika njia ya Kiroho, ili awaingize katika *hali ya wanaoendelea*, ambayo ni ile ya wanasala. Wanapaswa kupitia njia hiyo ili wawe *wakamilifu,* maana yake wafikie muungano wa Kimungu".

Kwanza tunaachishwa faraja za kihisi, ambazo zinafaa kwa muda, lakini zikitafutwa zinakuwa kizuio. Ndiyo sababu tunahitaji kutakaswa hisi kwa ukavu na kuongozwa kwenye maisha ya Kiroho yasiyotegemea mno hisi, ubunifu na mifuatano ya mawazo. Hapo, ingawa pana giza la kusumbua, tunaangaziwa na *vipaji vya Roho Mtakatifu* ujuzi unaotuingiza kwa undani katika mambo ya Mungu, tuyapenye pengine kwa nukta moja kuliko kwa miezi au miaka ya kutafakari. Ili kushinda vishawishi dhidi ya usafi wa moyo au ya subira, vinavyotokea mara nyingi wakati wa usiku wa hisi, unahitajika pengine ushujaa mkubwa unaoleta faida baadaye. Katika usiku huo hisi zinatupwa kwenye giza na ukavu kwa sababu ya kutoweka kwa neema za kihisi ambazo mtu alikuwa anaziishia akizifurahia kwa umimi. Lakini katika giza hilo, akili na utashi vinaanza kupata mwanga wa uzima ambao unapita mifuatano ya mawazo na unaelekeza kumkazia Mungu macho ya upendo katika sala. "Basi, mtu ametoka na kuanza kupenya njia ya roho wanayoifuata wale *wanaoendelea,* njia inayoitwa *ya kuangazwa* au ya *kumiminiwa sala"* (Mt. Yohane wa Msalaba).

Baadaye utahitajika *utakaso mwingine wa kujaliwa* ili kuondolewa kasoro ambazo "*haziponyeki* kadiri hao wanaoendelea wanavyodhani ni mema ya Kiroho… Basi, anayetaka kusonga mbele kweli, *ni lazima apitie* utakaso wa usiku wa roho. Hapo tu ataweza kuona njia ya kufaa aungane na Mungu" (Mt. Yohane wa Msalaba). Utakaso huo wa roho unawapata walioendelea zaidi ambao wanatamani mema lakini wanadai wayafanye wao na kwa namna yao. Hao wanapaswa kutakaswa kila namna ya kushikilia kibinadamu mawazo na matendo yao, namna yao binafsi ya kuona, kutaka na kutenda. Utakaso huo ukivumiliwa vizuri, katikati ya vishawishi dhidi ya maadili ya Kimungu, unawazidishia mara mia imani, tumaini na upendo.

Jaribu hilo linajitokeza kwa namna tofauti katika maisha ya sala tu na katika yale ya kitume. Pia ni tofauti kadiri linavyolenga kumfikisha mtu mapema kwenye ukamilifu mkuu au linavyotokea mwishoni tu ili kumsaidia *kutakaswa* walau kiasi *kabla hajafa,* akistahili kwa *ustawi wa upendo,* si toharani asipoweza kustahili. Hivyo dogma ya purgatorio inathibitisha haja ya matakaso hayo.

Hapo *mchanganyiko wa mwanga na giza* ni mkubwa kuliko ule wa usiku wa hisi. Mtu anaonekana amekosa urahisi wa kusali na wa kutenda aliokuwa anaufurahia mno kutokana na mabaki ya kujipendea na kiburi. Lakini katika huo usiku wa roho unaonekana mwanga mkuu zaidi; polepole, katikati ya vishawishi dhidi ya imani, tumaini na upendo, zinajitokeza kama nyota kuu tatu sababu zenyewe za maadili hayo ambazo ni: ukweli asili wenye kufunua, huruma yenye kusaidia na wema mkuu wa Mungu. Mtu anafikia kumpenda kwa usafi mkubwa na kwa uwezo wake wote.

Tutayaeleza hayo kirefu mwanzoni mwa sehemu ya tatu na ya nne. Hapa yalihitajika tusije tukapunguza ukuu wa *ustawi kamili wa kawaida* wa maisha ya Kikristo. Tulivyokwishaona, kilele hicho kinachoweza kufikiwa duniani ni kile cha *heri nane za Kiinjili:* hizo (hasa zile za mwisho) zinapita juhudi na kupatikana upande wa mafumbo, kama hayo matakaso ya Kimungu.

**UKAMILIFU WA KIKRISTO NA SALA YA KUMIMINIWA**

Fundisho la kwamba ukamilifu unadai matakaso ya Kimungu ya hisi na roho lina mengi yanayotokana nalo. Kwanza, *sala ya kumiminiwa,* yaani kuzama katika mafumbo ya imani, imo katika njia ya kawaida ya utakatifu, kwa kuwa inaanza katika ukavu wa utakaso wa hisi. Ingekuwa kosa kubwa kuchanganya sala hiyo na faraja ambazo hazifuatani nayo daima. Usemi wa kuwa mizizi ya ujuzi ni michungu lakini matunda yake ni matamu unafaa kuhusu mizizi na matunda ya sala ya kumiminiwa. Pili, siku hizi hakuna tena mtu anayesema kuzama katika mafumbo ni karama tu, kama ile ya unabii au ile ya kusema kwa lugha ngeni. Wote wanakubaliana sala hiyo inahusiana na neema inayotia utakatifu, yaani neema ya maadili na vipaji. Hatimaye, tusipoweza kustahili neema ya kuzama katika sala, maana yake si kwamba ipo nje ya njia ya kawaida ya utakatifu. Mwadilifu hawezi kustahili vilevile neema ya kufa kitakatifu, ingawa ni ya lazima kwa uzima wa milele. Wala hawezi kustahili neema ya hakika inayomkinga dhidi ya dhambi ya mauti ili adumu katika neema inayotia utakatifu. Lakini zawadi hizo asizoweza *kuzistahili,* anaweza kuzipata kwa *sala* nyenyekevu, zenye tumaini na udumifu.

Tusichanganye maswali mawili yafuatayo: "Je, sala ya kumiminiwa ipo katika njia ya kawaida ya utakatifu? Je, waadilifu wote wanaweza kuifikia, bila ya kujali tofauti za mazingira, malezi na uongozi?" Kama vile isivyofaa kuchanganya haya yafuatayo: "Je, neema inayotia utakatifu ni mbegu ya uzima wa milele? Je, kati ya wale walioipokea kwa ubatizo au kati ya waliodumu nayo miaka kadhaa, wataokoka wote au walau wengi wao?" *Wanasala hasa ni wachache kwa sababu wachache tu wanajua kujitenga na viumbe*. Wengine

wanaweza wakawa na nia njema, lakini hawana juhudi zile zote zinazohitajika ili kufikia *ukamilifu.* Tena ili kuufikia ni muhimu kupata malezi mazuri na uongozi mzuri, ingawa Mungu anavifidia kwa watu kadhaa wenye juhudi nyingi. Tusisahau pia kwamba wito wa kuwa mwandani wake unaweza kuwa wa jumla na wa mbali tu, au maalumu na wa jirani. Tena huo wa pili unaweza kuwa wa kutosha au wa hakika. Hatimaye huo wa hakika unaweza kuhusu viwango vya chini au vile vya juu vya muungano na Mungu.

Hatutakiwi kupunguza ukuu wa *lengo* la kulifikia. Kuhusu *njia zake,* busara izipendekeze kulingana na hali mbalimbali walizonazo watu, na kadiri walivyo kati ya wanaoanza au wanaoendelea. Hivyo tunahakikisha ukuu wa lengo, na uongozi wa kufaa kulifikia.

## 1.12. ***UKAMILIFU NA AMRI YA KUMPENDA MUNGU***

Baada ya kuona ukamilifu umo hasa katika upendo, tujiulize kama ukamilifu huo ni shauri tu au amri inayowadai Wakristo wote kuulenga. Ni sawa na kujiuliza maana halisi na upana wa amri ya upendo.

### JE, AMRI KUU INA MIPAKA?

Baadhi ya watu wanadhani si lazima kuwa na upendo mkubwa ili kutimiza kikamilifu amri kuu; *kwao* ukamilifu haulengi amri hiyo, bali utekelezaji wa mashauri kadhaa yaliyo juu zaidi. Mt. Thoma wa Akwino alijibu kwamba wote *wanapaswa kulenga* ukamilifu, kila mmoja kadiri ya hali yake (k.mf. ndoa au utawa), ingawa hawadaiwi kuwa wakamilifu tayari. Amri kuu *inalazimisha wote kwa jumla kulenga* ukamilifu wa upendo, walau kwa kufuata *njia ya kawaida,* wakati nadhiri za kitawa zinawabana wale walioziweka waulenge kwa kufuata *njia ya pekee* ya wito wao. "Ukamilifu wa upendo, ambao unafanya maisha ya Kikristo yawe kamili, umo hasa katika kumpenda Mungu kwa moyo wote na jirani kama nafsi yetu. Kwa hiyo ukamilifu umo hasa katika kushika amri", si katika kutimiza nadhiri.

*Kimsingi* ukamilifu umo katika *upendo*; tusidhani huo *unaagizwa kwa kiwango fulani tu,* halafu unakuwa *shauri*. Amri hiyo inadai wazi ukamilifu: *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote".* Mipaka iko wapi? Vilevile: *"na jirani yako kama nafsi yako"* (Lk 10:27). Kila mmoja anajipenda iwezekanavyo, tena anapaswa kujitakia uzima wa milele si kwa kiwango cha chini tu, bali pasipo mpaka, kwa sababu hajui Mungu anataka kumfikishia wapi. Ni hivyo kwa kuwa *upendo ndio lengo la amri yoyote,* na katika utashi lengo halipo kwa kiwango fulani tu, bali katika ukamilifu wake, tofauti na njia za kulifikia. Lengo tunalitaka au hatulitaki; *hatuwezi kulitaka nusu.* Daktari hawezi kutaka mgonjwa apone nusu; anapima dawa, lakini *analenga afya pasipo kipimo.* "Kwa nini ukamilifu huo usiagizwe kwa binadamu, ingawa hakuna anayeweza kuwa nao katika maisha haya?" (Mt. Augustino). Maana yake, hata ukamilifu wa mbinguni unadaiwa na amri ya kumpenda Mungu si kama kitu cha kutimizwa mara moja, bali kama lengo ambalo *wote wajiwekee.*

Amri nyingine zilizo chini ya amri kuu, lengo lake ni kuondoa vile ambavyo *vinapinga* upendo na vinataka kuuangamiza; kumbe mashauri ya Kiinjili, lengo lake ni kusukumia mbali *vinavyoweza vikazuia* utekelezaji kamili wa upendo, ingawa haviupingi, k.mf. ndoa, shughuli za kidunia n.k. "Amri… na mashauri… vinashikwa vizuri vinapotimizwa ili kumpenda Mungu na kumpenda jirani kwa ajili ya Mungu, katika ulimwengu huu na ule ujao" (Mt. Augustino). "Ndiyo sababu katika Mafundisho ya Wazee, abati Musa alisema: Mafungo, makesha, kutafakari Maandiko, kwenda uchi na kukosa vitu si ukamilifu, bali *vifaa* au *njia* za ukamilifu; huo haumo ndani ya mambo hayo, ila kwa njia hizo unafikiwa kwa kasi na hakika zaidi" (Mt. Thoma wa Akwino). Ndiyo njia inayoelekea ukamilifu; lakini wenyewe ni kumfuata Yesu kwa upendo: "*Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini,* nawe utakuwa na hazina mbinguni, *kisha njoo unifuate*" (Math 19:21). Tunaweza kuwa mafukara kwa hiari kutokana na sababu isiyo ya kidini (k.mf. kwa kudharau utajiri kifalsafa) au kwa upendo wa Mungu; kwa vyovyote si sharti la ukamilifu. Huo umo hasa katika kutekeleza vizuri zaidi na zaidi amri kuu isiyo na mipaka. Wote *wanapaswa* walau kulenga ukamilifu huo: kwao *si afadhali tu,* bali ni wajibu sawa na ule wa kuelekea mbinguni, ambapo upendo wa Mungu utatawala kikamilifu, kisiwepo kitu kinachoweza tena kuupunguza.

### UPENDO WA MUNGU HAUPATIKANI KATIKATI

Fundisho la kuwa amri kuu haina mipaka kwa jinsi ilivyotolewa linathibitishwa kwa kuzingatia kuwa lengo tunalolizungumzia hapa si la katikati (kama vile malimwengu), bali ni lile kuu, yaani Mungu mwenyewe, aliye *wema usio na mipaka*. Ikiwa mgonjwa anajitakia afya pasipo kiwango, zaidi sisi tunapaswa kutamani upendo wa Mungu pasipo kiwango, kwa kuwa hatujui ni kipi ambacho Mungu anataka kutufikishia na kweli atatufikishia tukiwa waaminifu. *"Binadamu hawezi kamwe kumpenda Mungu anavyotakiwa kupendwa; kama vile hatutaweza kamwe kumuamini na kumtumainia tunavyopaswa"* (Mt. Thoma wa Akwino). Tofauti na maadili ya kiutu, lengo, sababu na kipimo halisi cha yale ya Kimungu ni Mungu mwenyewe, ukweli wake na wema wake usio na mipaka. Kwa hiyo hatuwezi kumuamini mno na kumtumainia mno; hatutaweza kamwe kumpenda anavyostahili. Hivyo tunazidi kuona amri kuu haina mipaka: inawadai wote hapa duniani waulenge upendo wa Mungu ulio safi na wenye nguvu zaidi na zaidi.

Tumaini linapatikana kati ya kukata tamaa ya wokovu na kuudai kipumbavu, lakini anayetarajia

kipumbavu kuokoka si kwamba anamtumainia mno Mungu, bali anabadili sababu ya kutumainia, akitumaini kile ambacho Mungu hawezi akaahidi, k.mf. msamaha pasipo majuto halisi. Vilevile kilema cha wepesi wa kuamini si katika kumuamini mno, bali katika kusadiki mambo yaliyobuniwa na binadamu kana kwamba yamefunuliwa na Mungu.

Kusahau kuwa katikati adilifu ni pia kilele, na kudhani maadili ya Kimungu yamo hasa katikati (kama maadili ya kiutu), ndiyo tabia ya *mtu wa wastani* anayejisingizia kuwa na kiasi. Mtu wa namna hiyo yupo kati ya uadilifu na uovu, tena anakaribia uovu kuliko uadilifu: "Mtu wa wastani kweli anapendezwa na kila kitu, lakini hapendezwi na chochote hata achangamke… Anachukia tamko lolote, kwa kuwa kila tamko linapinga tamko lingine tofauti. Kumbe ukijifanya kidogo rafiki na kidogo adui wa kila jambo, atakuona mwenye busara na kiasi. Mtu wa wastani anasema katika yote kuna mchanganyiko wa mema na mabaya, kwa hiyo tusiwe na msimamo mkali katika kupima mambo. Ukisisitiza ukweli kwa nguvu, mtu wa wastani atasema unajiamini mno. Mtu wa wastani anasikitika kuwa Ukristo una dogma; angependa ufundishe maadili tu; ukimuambia maadili ya Ukristo yanatokana na dogma zake kama matokeo na sababu yake, atakujibu umezidisha… Kama neno 'kuzidisha' lisingekuwepo, mtu wa wastani angelitunga… Kwa kawaida mtu wa wastani anaonekana mtaratibu; hawezi kuwa mnyenyekevu, la sivyo angeacha kuwa wa wastani. Mnyenyekevu anakataa uongo, hata ukitukuzwa na ulimwengu wote, naye anaupigia magoti ukweli… Mtu mwenye upendo hawezi kamwe kuwa wa wastani" (E. Hello).

**WAJIBU WA KUSONGA MBELE KUELEKEA UZIMA WA MILELE**

Sababu ya mwisho ya amri ya upendo kutokuwa na mipaka ni kwamba *tunaelekea uzima wa milele,* nasi tunasafiri vizuri kadiri tunavyokua katika upendo ambao *unatakiwa kustawi mfululizo* mpaka mwisho wa safari. Hilo si shauri tu, yaani jambo bora la hiari, bali *ni agizo, linatakiwa,* hivi kwamba mtu ambaye hapa duniani hataki kukua katika upendo anamchukiza Mungu. Njia ya uzima wa milele haikusudiwi kwa kusimama wala kulala, bali kwa kutembea tu. Kwa msafiri ambaye hajafikia mwisho wa lazima wa safari yake, kusonga mbele si shauri, ni sharti. Basi, tunapomuelekea Mungu, tunasonga mbele Kiroho, kwa kukua katika upendo: ndicho tunachotakiwa kuomba.

Ikiwa hivyo, tusipotimiza bado kikamilifu amri hiyo, je, *tunaivunja?* Jibu la hakika ni hapana, kwa kuwa "ili tuepe uvunjaji huo inatosha tushike kwa namna fulani sheria ya upendo kama wanavyofanya wanaoanza" (Mt. Thoma wa Akwino). Ni kweli kwamba upendo wa Mungu unaingia *wote kabisa* katika lengo la amri hiyo; hata ukamilifu wa mbinguni hauwekwi kando, kwa kuwa ndio lengo ambalo tulikusudie, lakini hatuivunji amri tukitimiza upendo kwa kiasi. Kiwango *cha chini* cha kumpenda Mungu ni kutopenda chochote *kuliko yeye, au kinyume chake au sawa naye;* asiye na kiwango hicho hatimizi amri. Kinyume na hicho, kuna kiwango cha upendo kisichoweza kufikiwa hapa duniani, nacho ni kumpenda Mungu *kwa kumlenga kweli mfululizo.* Hatuvunji amri kama hatujafikia ukamilifu huo, wala viwango vya katikati, mradi tuwe na kiwango cha chini. Lakini tukisimama katika kiwango hicho hatutimizi kikamilifu amri kuu.

Ni kosa kudhani eti! Upendo usiokamilika tu ni wa lazima, na viwango vyake vya juu ni vya shauri. Hivyo vinaagizwa walau kama lengo, hata ikiwa si kwa sasa hivi. Ni sawa na mtoto ambaye asipokua anavyotakiwa, hatabaki mtoto, bali atakuwa mbilikimo. Upande wa roho pia *sheria ya ukuaji* ina masharti makali: ikiwa mbegu ya Kimungu tuliyotiwa kwa ubatizo haistawi, ina hatari kubwa ya kusongwa na magugu. Hakika katika njia ya wokovu, watu walio tofauti na jinsi wanavyotakiwa kuwa si waliozama katika mafumbo, bali *wachelewaji na vuguvugu.*

Yapo matatu yatokanayo tutakayoyafafanua hapo mbele:

1° *Katika njia ya Mungu, asiyesonga mbele, anarudi nyuma:* kwa sababu kwetu ni sheria kusonga mbele mfululizo, na asiyefanya hivyo anakuwa *mchelewaji,* kama garimoshi linalosimama mno kwenye stesheni lisifuate ratiba.

2° Ustawi wa upendo unatakiwa kuwa wa kasi zaidi na zaidi kadiri tunavyomkaribia Mungu na kuvutwa naye. Ndivyo jiwe linavyoanguka kasi kadiri linavyokaribia ardhi na kuvutwa nayo.

3° Hatimaye, ikiwa ndio ukuu wa amri ya upendo, hatuwezi kuwa na wasiwasi wa kwamba *hatutazidi kupewa neema za msaada ili tulifikie lengo hilo,* kwa sababu Mungu haagizi kamwe yasiyowezekana. Anatupenda mno, kuliko tunavyoweza kudhani. Ni juu yetu kuitikia. Baada ya kumpenda *kwa moyo wote*, kwa hisia ya mapenzi, tumpende *kwa akili yote,* kwa upendo mtendaji, *kwa nguvu zote* saa ya kujaribiwa inapotufikia, na hatimaye *kwa roho yote,* iliyoachana na vurugu za hisi, ili tumuabudu "katika rono na kweli" (Yoh 4:23,24).

Kwa jumla fundisho hilo linatuonya tusitenganishe utakatifu na wokovu wa milele, kama wanavyofanya wanaosema, eti! Mimi sitakuwa mtakatifu kamwe; kwangu inatosha niokoke. Hilo ni kosa kubwa. Kugeuka watakatifu zaidi na zaidi ndiyo njia ya wokovu; mbinguni kutakuwa na watakatifu tu, na kwa maana hiyo kila mmojawetu anapaswa kulenga utakatifu.

## 1.13. *UKAMILIFU NA MASHAURI YA KIINJILI*

Tumeona kuwa waamini *wanapaswa* kulenga upendo kamili; kutokana na amri kuu, huo ni w*ajibu wa*

*wote,* kila mmoja kadiri ya hali yake maishani. Lakini hawawezi kuufikia wakiishi duniani kana kwamba ndiyo maskani ya milele, pasipo *roho ya mashauri ya Kiinjili,* ambayo ni kutoambatana na malimwengu. Kutokana na wito wa pekee, baadhi wana *wajibu maalumu* wa kulenga ukamilifu kufuatana na nadhiri za *kutekeleza mashauri* ya ufukara, useja na utiifu. Tuanze kuzungumzia utekelezaji huo kuhusiana na ukamilifu wa Kikristo na uponyaji wa madonda yetu ya rohoni.

**MASHAURI YA KIINJILI NA MADONDA YA ROHO**

Yesu alipomualika tajiri akauze vyote ili kumfuata katika ukamilifu, "yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi" (Math 19:22). Kutekeleza kwa vitendo mashauri ya Kiinjili si wajibu wala si sharti la kufikia ukamilifu tunaopaswa kuulenga, ila ni njia inayofaa kulifikia lengo hilo kwa hakika na kasi zaidi, tusije tukasimama tu. Katika huyo aliyeshindwa tunaona ni vigumu kuwa na roho ya kutoambatana na malimwengu tusipoitekeleza kwa vitendo. Anayeishi ulimwenguni yuko katika hatari ya kuzamia mahangaiko ya kujipatia nafasi nzuri au kuwatafutia ndugu zake, hata akasahau kwamba anapaswa kuelekea nchi nyingine, na kwamba ili aifikie anahitaji sio akili kuhusu shughuli za kidunia, bali msaada wa Mungu (ambao ajiombee) na tunda la neema (yaani stahili). Katika maisha ya kifamilia anaelekea kukwama katika mafungamano yanayomtimizia haja ya mapendo, hata akasahau wajibu wa kumpenda Mungu kuliko wote; mara nyingi upendo wake si mwali hai unaomuinukia Mungu ukihuisha mapendo mengine yote, bali ni kama makaa madogo yanayozidi kuzimika chini ya majivu: ndiyo sababu anaweza akatenda dhambi kwa urahisi, asifikirie anasaliti urafiki na Mungu. Hatimaye yuko katika hatari ya kufuata matakwa yake na, kisha kusali kifupi, kupanga maisha yake upande wa maumbile tu, akiathiriwa na umimi, mawazo ya kibinadamu na madai ya mazingira. Hapo anahangaikia masuala ya kidunia na pengine michezo, halafu yakitokea matatizo makubwa yanayohitaji nguvu nyingi za Kiroho anakuja kutambua imani yake ni haba mno: kwake kweli kuu za imani hazina nguvu kiutendaji, ziko mbali angani zisiingie ndani ya roho. Anakosa imani yenye vitendo inayoleta nuru ya mafumbo ya wokovu katika maisha ya kila siku.

Ndizo hatari zinazomkabili Mkristo asipozingatia mashauri ya Kiinjili kadiri anavyoweza. Akiteleza kwenye mteremko huo, anapotea na kuzidiwa na maradhi matatu yanayopingana moja kwa moja na hayo mashauri matatu: "Kila kilichomo duniani, yaani tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia" (1Yoh 2:16). Hayo ni madonda matatu yenye usaha yanayoziathiri roho na kuziua kwa kuzisogeza mbali na Mungu. Madonda hayo yameenea ulimwenguni kufuatana na dhambi ya mtu wa kwanza pamoja na dhambi zetu tulizozirudiarudia. Ili tuelewe ubaya wake tunapaswa kukumbuka hayo yanashika nafasi ya ule *ulinganifu uliokuwepo katika hali ya uadilifu wa asili* pande zote tatu.

Mtu alipoumbwa kulikuwa na ulinganifu kamili kati ya Mungu na roho, kati ya roho na mwili, kati ya mwili na vitu vya nje. Kulikuwa na *ulinganifu kati ya Mungu na roho,* kwa sababu roho imeumbwa ili kumjua, kumpenda na kumtumikia, na hivyo kupata uzima wa milele. Mtu wa kwanza, aliyeumbwa katika utakatifu na uadilifu, alikuwa mwanasala mwenye kuongea kirafiki na Mungu akijilisha hasa mambo ya Kimungu, akizingatia yote katika mwanga huo na kumtii. Kutokana na ulinganifu huo wa juu kulikuwa na ule *kati ya roho na mwili,* ulioumbwa ili utumikie roho. Roho ikiwa chini ya Mungu kikamilifu iliutawala mwili wake, huku maono na maelekeo ya hisi yakifuata kwa makini uongozi wa akili (yenye busara na imani) na msukumo wa utashi (uliohuishwa na upendo). Hatimaye kulikuwa na *ulinganifu kati ya mwili na vitu vya nje,* dunia ikizaa yenyewe pasipo haja ya kulimwa kwa jasho la uso; vilevile wanyama walikuwa wakimtii mtu aliyepewa kuwatawala, au walau hawakumdhuru.

Dhambi ilivuruga ulinganifu huo wote ikiangamiza ule wa juu: mtu aliasi sheria ya Mungu, na tangu hapo roho yake *inaelekea kiburi* na kukariri, "Sitatii". Imeacha kujilisha ukweli wa Kimungu ijitungie mawazo finyu, danganyifu, geugeu, na kujiongoza kwa kuiwekea mipaka mamlaka ya Mungu, badala ya kufuata maongozi yake ambayo tu yanafikishia uzima. Kwa kumkaidi Mungu, roho imepoteza utawala wake juu ya mwili na juu ya maono yake yaliyokusudiwa kutii akili na utashi. Tena mara nyingi imejifanya mtumwa wa mwili na hamu zake za kinyama: ndizo *tamaa mbaya za mwili.* Watu wasio na idadi wanasahau lengo lao la Kimungu na kushughulikia kutwa kucha mwili wao kama mungu wao. Maono yanaitawala roho hata isipotaka, kwa kuwa ndani yake pendo, wivu, hasira na chuki vinajitokeza vikipambana na kuipeleka huko na huko kama farasi wasiokubali lijamu wala hatamu. Hatimaye mwili, badala ya kufaidika na vitu vya nje, umekuwa mtumwa wa vitu hivyo: unajichosha ili kuvipata kwa wingi, unajizungushia fahari ya bure kwa hasara ya maskini wenye njaa, unajiona anahitaji vile vyote vinavyong'aa na kuthaminika: ndizo *tamaa za macho.* Kisha kujilimbikizia vitu, hangaiko la kuvidumisha na kuvizidisha tena linakuwa wazo kuu la umati wa watu ambao, kama watumwa wa shughuli hizo, hawana kamwe muda wa kusali na kusoma Injili ili kujilisha rohoni; wanajijenga duniani kana kwamba wataishi hapa milele yote, wasiwazie wokovu wao. Utumwa huo wa pande tatu ni kinyume cha utaratibu. Mwokozi alikuja kuurudisha ulinganifu wa asili pande zote tatu, na kwa ajili hiyo ametupatia mashauri matatu.

**MASHAURI YA KIINJILI NA KURUDIA ULINGANIFU WA ASILI**

Yesu katika ubinadamu wake ndiye kielelezo cha maadili yote, mfano bora wa utakatifu. Kutokana na

umoja wake na Nafsi ya Neno, utu wake uliwekwa wakfu kwa Mungu tangu achukuliwe mimba; ulipokea utakatifu wa kuzaliwa nao, usioumbwa. Haiwezekani kuwaza muungano na Mungu ulio wa ndani na wa kudumu kuliko huo unaounganisha utu na umungu katika Nafsi ya Neno aliyefanyika mwili. Kutokana nao utu wa Mwokozi umewekwa wakfu pamoja na vipawa vyake vyote na matendo yake yote, hata akili yake isiweze kudanganyika, utashi wake usiweze kufanya kosa na hisi zake safi zisiweze kuvurugwa na lolote. Matendo yake yote ni ya Mungu, yanatokana na Mungu na kumuelekea Mungu; utawala wa Aliye Juu hauwezi kutimia kikamilifu hivyo popote pengine. Kwa kuwa utu wa Yesu umewekwa wakfu namna hiyo bora, ukuu wake umemtenga na roho ya ulimwengu na yale yote yaliyo maovu au yasiyo mema tu, naye akatolewa kwa ulimwengu ili kuukomboa kutoka upofu wa tamaa na kiburi.

Kwa ukuu huo wa asili, Yesu alitenganika na mali, heshima, shughuli za kidunia: kielelezo cha ufukara, hakuwa na mahali "pa kujilaza kichwa chake" (Lk 9:58). Kwa ukuu huo, hakuambatana na furaha za dunia, alikuwa huru kuhusu madai ya familia ili aiunde nyingine ya kimataifa, yaani Kanisa: hivyo ni kielelezo cha useja mtakatifu, wenye uzazi wa Kiroho usio na mipaka. Hatimaye, kwa ukuu wake upitao maumbile, Yesu hakuambatana na matakwa yake yoyote: akiwa na umri wa miaka kumi na miwili alitamka, "imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu" (Lk 2:49), halafu "akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba" (Fil 2:8).

Kwa kuwa Mwokozi alitoka juu, hakuwa wa ulimwengu huu, bali alitolewa auokoe, ukuu wake wenyewe ulimtenga na mambo yote ya chini aweze kuufanyia kazi ulimwengu kutoka juu ili kazi hiyo ifike popote na ipenye zaidi, kama vile jua likifikia kilele cha mzunguko wake. Kwa kuwa huru kutoka vifungo vyote vya binadamu (mali, familia na mawazo finyu), Yesu aliweza kuwashughulikia binadamu wote akiwaletea uzima wa milele. Injili yake haizeeki, ni mpya daima, vile Mungu alivyo. Hivyo katika Bwana tunaona urekebisho wa ulinganifu wa asili pande zote tatu, urekebisho bora kuliko ukamilifu wa Adamu: "dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi" (Rom 5:20).

Urekebisho huo unatakiwa kuendelea katika Kanisa, linalopaswa kung'aa kwa utakatifu. Sifa yake hiyo inatakiwa kuwa ya ajabu na kuonekana, sio tu mara mojamoja katika watu shujaa (k.mf. wafiadini na watakatifu waliotangazwa rasmi), bali mfululizo katika familia za kitawa ambamo idadi kubwa ya watu inafuata shule ya utakatifu na kutamka hadharani nia ya kumfuata Bwana kwa kuungana na Mungu wasiambatane na malimwengu. Lakini kuna tofauti kubwa kati ya Bwana na watu hao, hata wakiwa na juhudi nyingi namna gani: yeye alitoka juu, hao wametoka chini, katika dhambi na udanganyifu, na wanapaswa kujitenga navyo zaidi na zaidi ili kujitoa kwa Mungu kwa ndani zaidi na zaidi. Mwokozi anawapendekezea waliopokea wito huo maalumu waishi sio tu kwa kufuata roho ya mashauri matatu ya Kiinjili, bali kwa kuyatekeleza kweli katika maisha ya pekee, akiwaahidia mara mia zaidi. Anawaalika *wajitenge pande tatu ili kuwekwa wakfu pande tatu* na hivyo kuhakikisha ustawi wa maadili hadi muungano na Mungu. Katika kutumia malimwengu anawashauri *wajibanie wasije wakavutwa kuzidisha.*

Anawaalika kutekeleza *ufukara,* kujitenga na matumizi huru na hata umilikaji wa vitu ili kuviweka wakfu kwa Mungu, visiwe tena vizuio, bali vyombo kwa safari ya kuelekea uzima wa milele. Anawaalika kuishi kwa *usafi kamili,* yaani kujinyima furaha za jinsia na kuuweka moyo wao wakfu kwa Mungu, usiwe tena kizuio, bali chombo kinachohuishwa na neema. Hatimaye anawaalika kuwa na *utiifu mtakatifu,* kujikomboa kutoka matakwa yao yoyote, yaliyojaa ugeugeu na ukaidi, ili utashi wao usiwe tena kizuio, bali chombo ambacho upendo unazidi kukifanya cha Kimungu ili kuungana na Mungu kwa undani na nguvu kila siku zaidi.

Utekelezaji wa maadili hayo matatu na wa nadhiri zake una shida, lakini unaondoa shida nyingine nyingi. Ndege anainua mabawa, lakini ni kweli zaidi kuwa mabawa yanamuinua ndege. Vilevile maadili ya kitawa na nadhiri zake vinamletea mtu wajibu wa pekee, lakini hasa vinamleta kwenye ukamilifu wa upendo kwa kasi na hakika zaidi.

Maadili ya ufukara, useja na utiifu yako chini ya *adili la ibada* ambalo linampa Mungu heshima inayotupasa, kwa hiyo ni kuu kuliko maadili mengine ya kiutu, likifuata mara yale ya Kimungu. Ndilo linalomtolea Mungu vitendo vya kitawa. Ili mtawa awe na msimamo wa kutorudi nyuma anajifunga kwa nadhiri, akiwajibika kutekeleza hayo matatu kwa mfano wa Bwana mpaka kufa: anajitoa pamoja naye kwa maisha mazima ya sadaka; na kwa kuwa anapaswa kutoa yote (vitu, mwili na moyo, matakwa) asijichukulie tena, jina la sadaka ya kuteketezwa linafaa kweli.

Sadaka hiyo itimizwe kwa dhati kila siku; hapo itatupatia mara mia zaidi. "Amin, nawaambieni: hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele" (Mk 10:29-30).

## 1.14. *WAJIBU WA PEKEE WA MAPADRI NA WATAWA WA KULENGA UKAMILIFU*

Baada ya kueleza Wakristo wote wanavyopaswa kulenga ukamilifu kutokana na amri kuu ya upendo, tuzungumzie wajibu wa pekee wa kufanya hivyo unaompasa kila padri, awe ameweka nadhiri za kitawa au sivyo, ili awe mhudumu mwadilifu wa Bwana. Tunataka kwanza kuonyesha jinsi adili la ibada linavyohitaji

kuhuishwa na upendo kwa Mungu ambao uwe safi na wa nguvu zaidi na zaidi.

**WAJIBU HUO KWA MTAWA**

Msingi wa wajibu huo ni nadhiri za kitawa, ambazo neema zake si za muda, bali za kudumu tukizidi kuwa waaminifu. "Wengine wako katika hali ya ukamilifu, si kwa kufanya tendo la upendo kamili, bali *kwa kujifunga* moja kwa moja, kwa fahari fulani, washike *kile kinachoelekeza kwenye ukamilifu…* Kwa kuwa watawa wanajifunga kwa nadhiri kujinyima malimwengu ambayo wangeruhusiwa kuyatumia kwa hiari; wanafanya hivyo ili kushughulikia mambo ya Mungu kwa urahisi zaidi… Vilevile maaskofu wanajifunga kushika mambo ya ukamilifu wanapokubali daraja ya uaskofu, kwa sababu mchungaji anapaswa kutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo zake" (Mt. Thoma wa Akwino).

Mtawa anatamka atalenga ukamilifu: "Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo, kwa ajili yake, nimeshikwa na Kristo Yesu" (Fil 3:12). Hatendi kosa la unafiki kwa kutokuwa bado mkamilifu, ila analifanya asipolenga ukamilifu kwa unyofu. Kwake wajibu huo wa pekee na ule wa kushika nadhiri zake na kanuni aliyoahidi ni mamoja. Lakini wajibu huo uzingatiwe daima katika uhusiano wake na ule wa jumla unaotokana na amri kuu ya upendo; hapo utawa hautatazamwa upande wa sheria tu, bali utaonekana katika upana wa maana yake ya Kiroho.

Kwa mtazamo huo tu utaeleweka uzito halisi wa neno la Mt. Thoma: "Kufanya tendo kwa nadhiri kunastahili kuliko kulifanya bila ya nadhiri". Si kwamba tuzidishe nadhiri ili kustahili zaidi, bali kwamba mtawa atekeleze nadhiri zake vizuri zaidi na zaidi, akizidi kuchimba sababu tatu alizozitoa mtakatifu huyo katika ufafanuzi wake:

1° *Nadhiri ni tendo la adili la ibada,* ambalo ni bora kuliko yale ya utiifu, ufukara na usafi wa moyo ambayo linamtolea Mungu yawe ibada.

2° Kwa nadhiri ya daima mtu anamtolea Mungu si tendo mojamoja, bali *uwezo wenyewe* wa kutenda, na kwa hakika ni afadhali kutoa mti na matunda yake kuliko kutoa matunda tu.

3° Kwa nadhiri utashi *unaimarishwa* katika kutenda mema, na kwa hakika kutenda kwa msimamo kunastahili zaidi, kama vile ni vibaya zaidi kutenda dhambi kwa utashi ulioimarika katika nia mbovu.

Tukiishi kwa roho hiyo tutaelewa kwa namna hai fundisho la kwamba, kwa kujifunga kushika mashauri matatu, yaliyo kiini cha utawa, mtu *anajitenga* na yale yanayoweza yakazuia mapendo yake yasimuelekee Mungu tu, halafu asipofuta uamuzi huo *anajitoa kwake kama sadaka ya kuteketezwa.* Hivyo hali yake ni ya kujitenga na ulimwengu na ya kuwekwa wakfu kwa Mungu.

Hasa mambo matatu yanaweza kuzuia mapendo yake yasimuelekee Mungu: tamaa za macho (yaani za vitu vinavyoonekana), tamaa za mwili na kiburi cha maisha (yaani kupenda kuwa huru tu). Mtawa anayakataa hayo matatu kwa nadhiri zake, akimtolea Mungu mali kwa ufukara, mwili na moyo kwa useja mtakatifu na matakwa yake kwa utiifu. Asipojitwalia tena chochote, bali akitekeleza vizuri, kwa upendo mkubwa zaidi na zaidi, maadili matatu yanayohusiana na nadhiri za kitawa, basi anamtolea kweli Mungu sadaka ile kamili inayostahili kuitwa ya kuteketezwa. Hapo maisha yake *yanatolewa kila siku pamoja na sadaka ya misa* kwa adili la ibada. Ni hivyo hasa kama mtawa anarudia mara nyingi ahadi zake kwa namna inayostahili kuliko alipozitoa kwa mara ya kwanza. Stahili zinakua ndani mwake pamoja na upendo na maadili mengine, hivyo hali yake ya kuwekwa wakfu kwa Mungu inazidi kuwa ya dhati na kamili.

Lengo la kujinyima pande tatu na kujitoa pande tatu ni kuungana na Mungu kila siku kwa ndani zaidi, kama utangulizi wa uzima wa milele. Mtawa anapaswa kuufikia muungano huo kwa kumuiga Yesu aliye "njia, na kweli, na uzima" (Yoh 14:6). Yeye, katika ubinadamu wake, *alitenganika* na roho ya ulimwengu *akaunganika na Mungu* vizuri iwezekanavyo. Mtawa anatamka hadharani nia ya kumfuata, lakini Yesu alitoka juu, kumbe mtawa ametoka duniani, palipotawaliwa na dhambi, hivyo anapaswa kujitenga zaidi na zaidi na mambo yote ya kidunia, kadiri ya maneno haya: "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na *uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu*. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu" (Kol 3:1-4). Mt. Thoma alifafanua hivi, "Msionje malimwengu kwa kuwa mmefia ulimwengu; uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo; mwenyewe amefichika kwetu, kwa kuwa yuko katika utukufu wa Mungu Baba yake, na hivyo uhai… tulionao kutoka kwake umefichika, kadiri ya maneno ya Maandiko matakatifu, 'Jinsi zilivyo nyingi fadhili zako ulizowawekea wakuchao; ulizowatendea wakukimbiliao mbele ya wanadamu!' (Zab 31:19). 'Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa' (Ufu 2:17)". Hiyo mana ya Kiroho, ambayo ile ya jangwani ilikuwa mfano wake tu, ndiyo chakula cha roho: kujaliwa kuzama katika mafumbo ya imani. Hivyo utekelezaji wa maadili unaandaa kumiminiwa sala; kwa namna ya pekee "ubikira unalenga ustawi wa roho katika maisha ya kuzamia sala" (Mt. Thoma wa Akwino). Hivyo maisha ya kitawa yanalenga utekelezaji kamili zaidi na zaidi wa amri ya upendo na undani wa muungano na Mungu.

Wajibu wa pekee alionao mtawa wa kulenga ukamilifu uzingatiwe daima kuhusiana na wajibu wa waamini kwa jumla unaotegemea amri kuu ya upendo. Amri hiyo inatawala mashauri ya Kiinjili, kwa kuwa hayo ni *njia* na *vyombo* tu kwa ajili ya kufikia ukamilifu wa upendo kwa kasi na hakika zaidi. Hivyo, maadili matatu

ya kitawa yanatekelezwa kikamilifu kwa maadili matatu ya Kimungu. Kati ya hayo linaundwa fungamano la ndani, hivi kwamba *tumaini la heri ni kama uhai wa ufukara mtakatifu* ambao unaachana na mali ya dunia na kutufanya tuzidi kumtumainia Mungu ili kupata ya milele; *upendo ndio uhai wa useja* unaojinyima pendo la chini ili kupata upendo wa juu kabisa: unapotekelezwa sawasawa unastawisha ndani mwetu upendo kwa Bwana na kwa watu; *imani ndiyo uhai wa utiifu* unaotekeleza maagizo ya wakubwa kana kwamba yamefunuliwa na Mungu: utekelezaji huo unakuza roho ya imani. Hivyo maisha ya kitawa yanafikisha kwenye sala ya kumiminiwa na muungano wa dhati na Mungu unaozidi kustawisha ule na jirani.

**WAJIBU WA PEKEE ALIONAO PADRI WA KULENGA UKAMILIFU**

Ikiwa bradha na sista wana wajibu wa pekee wa kulenga ukamilifu, zaidi tena anao padri, hata kama si mtawa. Utawa ni *hali ya kulenga ukamilifu;* maaskofu wako katika *hali ya kutekeleza ukamilifu;* ndiyo sababu inafaa wawe katika hatua ya muungano ya waliokamilika. Padri mwanajimbo anajiongezea stahili mpya akiingia utawani; kwa vyovyote anapaswa tayari alenge ukamilifu kutokana na sakramenti ya daraja na kazi zake takatifu. Wajibu huo maalumu si tofauti na ule wa kutimiza kitakatifu majukumu mbalimbali ya kipadri. Kutokana na amri kuu anapaswa kuyatimiza vizuri zaidi na zaidi, kadiri upendo unavyostawi hadi kufa kwake.

Upadirisho unadai, sio tu hali ya neema inayotia utakatifu na sifa maalumu, bali mwanzo wa ukamilifu, maisha bora kuliko yanayotakiwa kwa kuingia utawani. Kwa kuwa padri anapaswa kuwaangaza wengine, inafaa awe katika hatua ya mwanga. Upadirisho unatia alama isiyofutika inayomshirikisha moja kwa moja ukuhani wa Kristo, na neema ya sakramenti inayomwezesha kutimiza kazi za kipadri inavyomfaa mtumishi wake. Hiyo neema ya sakramenti inatimiliza neema inayotia utakatifu na kumpa padri haki ya kupokea misaada inayohitajika ili atimize huduma yake kitakatifu zaidi na zaidi. Ni sehemu ya sura ya Kiroho ya padri, ambaye azidi kuelewa ukuu na masharti ya upadri wake. Kwa hakika upadirisho ni bora kuliko nadhiri za kitawa, na wajibu maalumu wa kulenga ukamilifu unaotokana nao ni mkubwa kuliko ule unaotokana na nadhiri.

"Umekuwa padri, umepakwa mafuta ili umtolee Mungu sadaka ya misa. Fanya sasa kwa bidii, kwa uaminifu, kila wakati inapofaa. Uwe na mwenendo mzuri usio na hitilafu. Usidhani u huru kuliko watu wengine, bali umefungwa kifungo cha sheria, hata imekupasa kutafuta ukamilifu mkubwa zaidi. Ni lazima padri awe mtu aliyepambwa maadili yote, kusudi awape watu wengine mfano wa maisha mema. Mazoea yake siyo waliyozoea watu wa dunia, watu wa chini, bali yafuatana na malaika wa mbinguni; marafiki wake ndio watu watimilifu walioko duniani" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,5:2). Kazi za padri, kuhusiana na Mwokozi aliyemo katika ekaristi na katika Mwili wake wa fumbo, zinatuonyesha kuliko upadirisho wenyewe wajibu wake wa pekee wa kulenga ukamilifu.

Padri anapoadhimisha misa anamwakilisha Kristo aliyejitoa kwa ajili yetu. Anapaswa kuelewa ukuu wa kazi yake na kuzidi kuungana kwa dhati na *kuhani mkuu ambaye ni kafara pia.* Ni unafiki, au walau uzembe, kupanda altareni bila ya nia imara ya kupanda ngazi ya upendo. Mtumishi wa Kristo anapaswa aseme kila siku kitakatifu zaidi, "Huu ndio mwili wangu… Hiki ni kikombe cha damu yangu". Kila siku zaidi komunyo yake iwe motomoto kwa utashi kuwa tayari kumtumikia Mungu, kwa sababu ekaristi inatakiwa kukuza upendo ndani mwetu, si kuutunza tu. "Kwa ukuu wa kazi ambayo padri altareni ni mtumishi wa Kristo, unadaiwa utakatifu wa ndani ulio mkubwa kuliko ule unaodaiwa na utawa" (Mt. Thoma wa Akwino). Hivyo, mambo yakilingana, tendo dhidi ya utakatifu ni dhambi kubwa zaidi likitendwa na padri kuliko likitendwa na bradha. "Padri mwenye kumtolea Mungu sadaka ya misa, humsifu Mungu, huwafurahisha malaika, huthibitisha Kanisa, husaidia walio hai, hutuliza marehemu, hupewa mwenyewe neema zote" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,5:3).

Anapaswa pia kuadhimisha kwa makini na ibada halisi Sala ya Kanisa ambayo inatangulia na kufuata misa. Ni wimbo wa Bibi arusi wa Kristo kwa usiku na mchana, hivyo ni heshima kubwa kuhusika nao. Tusali hivyo tukizingatia nia kuu za Kanisa, kama vile kupatanisha ulimwengu kwa kueneza utawala wa Mungu.

Hatimaye padri ana wajibu wa pekee wa kulenga ukamilifu ili atimize vizuri kazi zake kwa ajili ya Mwili wa fumbo wa Kristo. "Hakuna kinachofaa zaidi kuwaongoza waamini kwenye ibada halisi kuliko mfano mwema wa padri. Macho ya watu yanamuelekea yeye, kama kioo cha ukamilifu wanaotakiwa kuiga. Kwa hiyo, basi, anatakiwa kupanga maisha yake, sura yake ya nje, mwenendo wake, matendo na maneno yake hivi kwamba adumishe daima uzito, utaratibu na tabia ya kidini anavyopaswa kuwa navyo" (Mtaguso wa Trento). Padri mwanajimbo halazimiki kuahidi ufukara, lakini anatakiwa kutoshikamana na vitu na kuwa radhi awape maskini; anatakiwa pia kumtii askofu wake na kuwa kama mtumishi wa waamini, bila ya kujali matatizo na pengine masingizio anayoweza akakabiliana nayo.

Haja ya ukamilifu huo ni wazi kuhusu mahubiri, maungamo na uongozi wa Kiroho. Ili mahubiri yawe hai na kuzaa matunda, ni lazima padri aseme "yaujazayo moyo wake" (Math 12:34). Tena yanatakiwa "kutokana na utimilifu wa sala ya kumiminiwa" (Mt. Thoma wa Akwino), na imani hai yenye kupenya na kuonja fumbo la Kristo, thamani isiyo na kifani ya misa, ya neema inayotia utakatifu na ya uzima wa milele. Padri anapaswa kuhubiri kama mwokozi wa roho, akifanya kazi mfululizo kwa wokovu wa wengi. Asiwe amepokea

upadri bure. Ni vilevile kuhusu huduma ya kitubio na uongozi wa Kiroho. Padri asipokuwa mwangavu na motomoto, huduma hiyo inaweza kumpotosha mwenyewe, badala ya kuokoa watu. Maisha yasipopanda juu, yanateremka chini; ili yasiteremke ni lazima yapande juu kama mwali wa moto. Hasa hapa asiyesonga mbele, anarudi nyuma. Hatimaye, wanaweza wakamuelekea padri watu ambao Mungu anawadai zaidi; ni lazima awape msaada wa hakika kwa kufuata njia nyofu ya utakatifu; haifai waende mbali naye pasipo kupata chochote.

M.H. Antoni Chevrier aliwafundisha mapadri aliowalea wawe daima na pango, Kalivari na tabenakulo machoni mwao. *Pango* liwakumbushe *ufukara;* padri anapaswa kuwa fukara katika nyumba, mavazi na chakula. Anapaswa kuwa mnyenyekevu kwa Mungu na kwa watu. Kadiri alivyo hivyo anamtukuza Mungu na kumfaa jirani. *Padri ni mtu asiye na kitu. Kalivari* imkumbushe haja ya *kujitoa sadaka,* kujifisha kuhusu mwili wake, roho yake, matakwa yake, heshima yake, familia yake na ulimwengu. Anapaswa kujitoa sadaka kwa kimya, kazi, malipizi, mateso na kifo. Kadiri padri alivyokwishakufa hivyo ana uzima ndani mwake na kuwashirikisha wengine. "*Padri ni msulubiwa.* Kwa mfano wa Mwalimu anapaswa kwa upendo kujitoa mwili, roho, muda, mali, afya, uhai; anapaswa kueneza uhai kwa imani yake, mafundisho yake, maneno yake, sala zake, juhudi zake, mifano yake. Anapaswa kuwa mkate mtamu. *Padri ni mtu wa kuliwa". Tabenakulo* imkumbushe *upendo* anaopaswa kuwa nao.

Ndicho kipeo cha upadri ambacho kila mmoja awe nacho: "Nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo" (Yoh 13:15).

## 1.15. *HATUA TATU ZA MAISHA YA KIROHO KADIRI YA MABABU NA WALIMU WAKUU*

Kisha kusema juu ya ukamilifu wa Kikristo, tuzungumzie hatua tatu za maisha ya Kiroho; hilo ni mojawapo katika masuala makuu ya fani hiyo. Hatua hizo zinaitwa za wanaoanza, wanaoendelea na waliokamilika; au za utakaso, mwanga na muungano. Tofauti na wanateolojia kadhaa wa karne za mwishomwisho, walimu wakuu wa maisha hayo waliamini *watu wowote wanaweza kutamani na kujiombea kwa unyenyekevu neema ya kuzama katika mafumbo ya imani,* ambayo yote yanadhihirisha wema wa Mungu usio na mipaka. Waliona hiyo sala ya kumiminiwa ni sharti la muungano wa dhati na Mungu ulio ukamilifu wa Kikristo. Kwa msingi huo walifafanua kila hatua ya maisha ya Kiroho.

**USHUHUDA WA MAANDIKO MATAKATIFU**

Tutataja madondoo machache tu yaliyo muhimu zaidi, baada ya yale mengi tuliyokwishatoa.

Katika Injili, hasa katika heri nane, tumeona ukuu wa ukamilifu wa Kikristo tusioweza kuupata tusipofisha yale yote yasiyofaa ndani mwetu, tusipobeba msalaba kwa uvumilivu, tusipomuomba Baba aliyefichika moyoni mwetu, tusipomsikiliza kwa makini Roho Mtakatifu kila anapotuangaza, ili kwa msaada wake wa pekee tuzame kwa upendo katika mafumbo ya wokovu na hivyo tuungane na Mungu. "*Iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu…*twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu... Mambo ambayo jicho halikuyaona, wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao… ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu" (1Kor 2:6-10). Ndiyo yanayotazamwa na waliokamilika wanaposali. "Kwa hiyo nampigia Baba magoti… *awajalieni,* kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, *kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, katika utu wa ndani.* Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani *mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu* pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua *upendo wake Kristo, upitao ufahamu* kwa jinsi ulivyo mwingi, *mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"* (Ef 3:14-19).

*Katika maisha ya mitume,* waliolelewa na Bwana mwenyewe, *kuna hatua tatu tofauti* zinazolingana na zile za maisha ya Kiroho. Hatua ya kwanza, ile ya wanaoanza, ilichukua *tangu waongoke hadi Mateso ya Bwana,* walipopitia shida kubwa hata Mt. Petro akamkana Mwalimu wake. Halafu akajuta, na ndio uongofu wake wa pili, katika ule utakaso wa Kimungu uliokuwa kama usiku wa giza na mateso. Kitu cha namna hiyo kiliwatokea mitume wengine pia walipojaliwa kughairi baada ya kukimbia. Hatua ya pili, ile ya wanaoendelea, ilichukua *kuanzia Mateso hadi Pentekoste.* Kipindi hicho walikuwa bado waoga, imani yao ilihitaji kuangazwa, tumaini lao lilihitaji kuimarishwa, na upendo wao haukuwa bado na ari uliyopaswa kuwa nayo. Hatua hiyo ilitimia kwa kuondolewa uwepo wa kimwili wa Bwana alipopaa mbinguni. Hapo walipaswa kuendelea kwa imani tupu, wakikabili dhuluma walizotabiriwa. Hatua ya tatu iliwaanzia *Pentekoste,* ambayo ikawa kwao kama uongofu wa tatu, *utakaso halisi wa Kimungu* na mageuzo yaliyowaingiza katika maisha makamilifu. Iliangaza akili yao na kuimarisha utashi wao ili wamhubiri popote Yesu msulubiwa. Sifa maalumu ya hatua hiyo ni kuzidi kuungana kwa ndani na Mungu, kujitoa sadaka kikamilifu hadi kufia dini. Hapo mbele tutazirudia hatua zao hizo ambazo kila moja inaanza na uongofu au mageuzo ya roho. Tukizitafakari zinaangaza kweli hatua tatu za maisha ya Kiroho.

**USHUHUDA WA MAPOKEO**

Maelekezo ya Maandiko yanathibitishwa na Mababu wa Kanisa. Tuone kwanza ushuhuda wa wale wa mashariki.

*Mt. Inyasi wa Antiokia* aliandika mara nyingi juu ya uwepo wa Kiroho wa Mwokozi ndani ya waamini, akawahimiza hivi, "Tufanye tendo letu lolote kwa kuzingatia kwamba Mungu anaishi ndani mwetu; hivyo tutakuwa mahekalu yake, naye atakuwa Mungu wetu mwenye kukaa ndani mwetu". Mwenyewe alitaka kuishi kwa kuungana na Kristo zaidi na zaidi, na kufa ili kuungana naye milele. Alitamani kusagwa na meno ya simba awe unga wa ngano wa Kristo, kama vile Yesu alivyosagwa awe mkate wetu wa ekaristi. Barua zake zimejaa ujuzi wa juu wa Kristo, imani hai yenye kupenya ambayo ni sala ya kumiminiwa na ambayo inafurika katika utume wenye matunda mengi kutokana na upendo mkubwa. Ili kufikia muungano huo wa dhati ni lazima *kujidharau* pamoja na yale yote ambayo hayafai na yanafisha uzima wa Kimungu ndani mwetu.

*Mt. Irenei* alisisitiza binadamu akubali kuundwa na Mungu kama udongo mikononi mwa mfinyanzi. Badala ya kupinga au kukwepa kazi hiyo, azidi kujionyesha mtulivu kwa Roho Mtakatifu katika sala na hivyo atafikia kupima mambo yote Kiroho na kuishi kwa upendo wa Mungu tu.

*Klementi wa Aleksandria* alieleza roho inavyopanda juu kupitia hali zifuatazo: kwanza uchaji wa Mungu, halafu imani na tumaini, hatimaye upendo na hekima. Waliokamilika wana amani na kutawaliwa na upendo; wamejaliwa hekima ya siri ya Mungu, ujuzi wa dini ambao unatokana na mwanga wa Roho Mtakatifu kwa roho sikivu na kugeuza maisha yao ya ndani kwa kuwafanya marafiki wa Mungu.

Sawa naye, mwanafunzi wake *Origenes* alisema mtu aliyekamilika anaishi hasa kwa upendo na kwa kawaida anapokea kwa Roho Mtakatifu hekima ya kumiminiwa, ujuzi wa dhati wa fumbo la Utatu mtakatifu. Kuhusu Injili ya Yohane aliandika, "Hakuna anayeweza kuelewa maana ya Injili kama hajaegama kifuani pa Yesu wala hajapokea kutoka kwake mama Maria awe mama yake pia". Neno ndiye anayejifunua kwa waliokamilika na kuwaunda kama alivyowaunda mitume. Mwenyewe alibainisha hatua tatu: ile ya wanaoanza, ambao ndani mwao maono yasiyofaa yanapungukiwa nguvu; ile ya wanaoendelea, ambao ndani mwao maono hayo yanaanza kuzimika kwa wingi wa neema; hatimaye ile ya waliokamilika. Alihimiza usikivu kwa Roho Mtakatifu, ambaye kwa njia yake tunaweza kumuendea Kristo na kupanda juu kwa Baba, katika sala ya kumiminiwa inayosaidiwa na upweke.

*Didimo Kipofu* alimualika kila Mkristo kuungana kikamilifu na Kristo, Bwana arusi wa roho iliyotakata.

*Mt. Bazili Mkuu* katika Kanuni zake alipanga maisha imara ya Kiroho yanayoandaa kwa sala ya kumiminiwa na muungano na Mungu. Ni sharti kutakata zaidi na zaidi: "Jicho la roho, kisha kuwa safi pasipo kivuli, linatazama mambo ya Mungu kwa mwanga ambao unatoka juu na kuijaza kwa wingi usiishibishe… Kisha kustahimili mapigano yenye tabu na kufaulu kuiokoa roho - iliyoambatana sana na mwili - katika mchanganyiko wa maono, roho inakuwa ya kufaa kwa kuongea na Mungu… Aliyefikia hali hiyo hatakiwi tena kukubali mvuke wa maono ya kidunia uchafue na kufunika kwa ushungi macho ya roho yake na hivyo kuifanya ikose sala ya kumiminiwa ya Kiroho na ya Kimungu".

*Mt. Gregori wa Nazienzi* alisema Mungu ni mwanga halisi tunaoweza kuupata tu tukiwa wenyewe mwanga na kutakata ili tupande kutoka uchaji wa Mungu kwenda hekima. Katika waandishi hao wote tunakuta majina haya matatu: utakaso, mwanga na muungano.

*Mt. Gregori wa Nisa* alionyesha tunavyopaswa kujitenga na viumbe na kuishi na Kristo ili tukaribishwe kutazama umungu na kuungana nao. Ushindi huo juu ya adui unapatikana kwa njia ya msalaba tu, na kwa kutakasa zaidi na zaidi akili katika mambo yote ya hisi. Ukamilifu unaifanya roho iwe bibi arusi wa Kristo.

Hata *Mt. Efrem* aliona kuwa sala ya kumiminiwa, tunayojaliwa kwa kuwa wasikivu kwa Roho Mtakatifu, ndiyo fadhili ya maisha makamilifu. "Tutakapokuwa tumeshinda maono yetu, na kuangamiza ndani mwetu mapenzi yoyote ya kimaumbile, na kuondoa kabisa rohoni mwetu hangaiko lolote lisilosaidia wokovu, hapo Roho Mtakatifu, kwa kuikuta roho yetu katika utulivu, na kuishirikisha akili yetu uwezo mpya, atatia mwanga mioyoni mwetu, kama inavyowashwa taa iliyo tayari na utambi na mafuta… Basi, kabla ya yote, tuandae roho zetu kupokea mwanga wa Kimungu, ili tustahili zawadi za Mungu".

Kwa *Denis* utakaso unaandaa kumjua Mungu kwa dhati; mwanga unashirikisha ujuzi huo; hatimaye utakatifu unafanya uchanue kikamilifu. Hatua ya muungano inahusu mafumbo na ni utangulizi wa uzima wa milele.

*Mt. Masimo Muungamadini* alibainisha hatua tatu za sala kuhusiana na hatua tatu za upendo. "Sala ya kawaida ni kama mkate: inawatia nguvu wanaoanza; ikiongezewa neema ya kuzama kidogo katika mafumbo, inakuwa kama mafuta tunayojipaka; hatimaye, tukizama kabisa ni kama divai tamu mno inayolevya wanaoinywa hata wakajisahau… Kuzama katika sala kunatokana na mwanga wa Roho Mtakatifu… Aliyetakata anaangazwa na kustahili kuingia ndani kabisa mwa hekalu na kufurahia muungano na Neno". Mwenyewe alionyesha majaribu makali ambayo wanasala wanapaswa kuyapitia ili kutakaswa moja kwa moja na kuthibitishwa katika upendo wa Mungu.

Hatimaye *Mt. Yohane wa Damasko* aliandika, "Aliyefikia kiwango cha juu kabisa cha upendo, kama kwa kutoka nje ya nafsi yake, anamvumbua Yule asiyeonekana, akiruka juu ya wingu lile la hisi linalozuia macho ya roho yasione. Akidumu katika amani, anamkazia macho Jua la Haki na kufurahia tamasha hilo asiloweza

kulikinai… Kufikia kumtazama Mungu, kisha kutekeleza kwa bidii maadili, ni hazina isiyonyang'anyika kamwe".

Basi, kadiri ya Mababu wa mashariki, huko kuzama katika mafumbo ya Kimungu ni kwenye njia ya utakatifu: mwanzo wake ni hatua ya wanaoendelea, halafu kunaendana kwa kawaida na upendo wa waliokamilika.

Mababu wa Kilatini wametuachia mafundisho hayohayo.

*Mt. Augustino* alitofautisha ngazi mbalimbali, akisisitiza vita dhidi ya dhambi (vilivyo kazi ngumu ya utakaso), vinavyofuatwa na mwanga kwa waliotakata, na hatimaye na muungano na Mungu. Halafu akaelekeza safari ya kupanda kwa Mungu kufuatana na vipaji vya Roho Mtakatifu: uchaji wa Mungu ndio kidato cha kwanza, na hekima ndiyo kilele. Katikati alibainisha vipindi viwili vya maandalizi yenye kutakasa. Alikiita kile cha mbali *maisha ya utendaji*, yaani utekelezaji wa maadili ya kiutu yanayohusiana na vipaji vya ibada, nguvu, elimu, shauri; halafu kile cha karibu *maisha ya kumiminiwa sala*, yaani utekelezaji bora wa maadili ya Kimungu na wa vipaji vya akili na hekima katika roho zilizo tulivu na sikivu kwa neema. Hapo imani ni chanzo cha kuzama katika mafumbo, na upendo motomoto unaunganisha kwa dhati na Mungu.

*Mt. Yohane Kasiano* alionyesha maisha ya Kiroho yanavyolenga kumtazama Mungu, ambako upendo wake unatekelezwa kikamilifu. Tunapaswa kujiandaa tufikie huko kwa kusali ili tusamehewe dhambi, kutekeleza maadili na kutamani upendo wa kuwaka zaidi. Hapo sala inakuwa "yote ya moto" kutokana na "kumtazama Mungu tu na kuwaka kwa upendo motomoto… Hivyo roho katika chungu cha udongo inaanza kuonja malimbuko ya utukufu inaotumainia mbinguni".

*Mt. Gregori Mkuu* alikubali kugawa maisha ya Kiroho katika ngazi tatu: mapambano na dhambi, maisha ya utendaji au utekelezaji wa maadili, na maisha ya kumiminiwa sala yanayohitajiwa na wahubiri wa Neno la Mungu na wale wanaotaka kuufikia ukamilifu. Kwake matendo yote yanakosa ukamilifu mpaka roho ziwe zimeangazwa na sala ya kumiminiwa kutoka juu. Ndiyo kikomo cha juhudi, tunda la neema maalumu na utekelezaji wa kipaji cha hekima. Ni hali ya kujaliwa kuzama katika mafumbo ambayo mtu ajiandae kuipokea kwa unyenyekevu, usafi wa moyo na kukusanya mawazo karibu mfululizo. Mwenyewe alionyesha matakaso machungu ambayo "yanakausha ndani mwetu kila pendo la kihisi" na kutuandaa tuzame katika sala na kuungana na Mungu, ambapo tunakuta nguvu kubwa katika majaribu na upendo motomoto.

## HATUA TATU ZA MAISHA YA KIROHO NA ZA MAISHA YA KIMWILI

Mt. Thoma wa Akwino amefananisha hatua tatu za maisha ya Kiroho na zile za maisha ya kimwili: utoto, ujana na utu uzima. Ni mfano unaostahili tuuzingatie pamoja na kuangalia vipindi vya mpito kati ya hatua moja na nyingine.

Inakubalika kuwa sehemu ya kwanza ya utoto inakwisha akili inapochangamka kwenye umri wa miaka saba hivi, halafu inafuata sehemu ya pili inayodumu mpaka ubalehe, kwenye miaka kumi na nne hivi. Ujana unaenea kati ya miaka hiyo na ishirini. Halafu unafuata utu uzima, ambamo tunatofautisha kipindi kinachotangulia ukomavu kamili na kile kinachoufuata kwenye miaka thelatini na tano hivi, kabla ya kuanza mteremko wa uzee.

Namna ya kuwaza inabadilika pamoja na mwili. Mtoto anafuata ubunifu na hisi; hajajua kupambanua na kupanga, na hata akili inapoanza kuchangamka inaendelea kutegemea mno hisi. Mtu anapobalehe anabadilika si upande wa mwili tu, bali pia wa nafsi, akili na maadili: haridhiki tena na ubunifu, bali anaanza kutafakari maisha na haja ya kujiandaa afanye kazi fulani. Kipindi hicho cha mpito, kinachoitwa pengine umri usio na shukrani, hakikosi matatizo; ndipo tabia adili inapoundika au inaharibika; pengine mtu anabaki nyuma, bila ya msimamo. Mfano huo unaangaza maisha ya Kiroho ambamo aliyeanza asipokuwa kwa wakati wake mtu anayeendelea, basi ama anaelekea maovu ama anabaki nyuma na kuwa vuguvugu, aina ya mbilikimo upande wa roho. "Kutotaka kusonga mbele ni kurudi nyuma" (Mt. Bernardo), kumbe kulenga ukamilifu moja kwa moja ni kuwa nao tayari kwa namna fulani.

Ikiwa ubalehe ni kipindi kigumu, vilevile ni kigumu kile cha uhuru wa kwanza kinachomuingiza kijana kwenye utu uzima. Akimaliza kukomaa kimwili anapaswa kuanza kushika nafasi yake katika jamii. Sawa na mwana mpotevu, wengi wanapita vibaya kipindi hicho, wakitafsiri uhuru wanaoachiwa kuwa idhini ya kutenda lolote. Kinyume chake, anayekomaa inavyotakiwa, anajihusisha na mambo yake binafsi, ya familia na ya jamii kwa namna bora kuliko kijana, akiyazingatia kwa upana zaidi. Inatokea karibu hivyo katika maisha ya Kiroho kwa mtu anayeendelea: namna yake ya kuwaza inainuka na kuwa ya Kiroho zaidi na zaidi, akiona vizuri mambo ya Mungu au maisha ya Kanisa kuhusiana na uzima wa milele.

Katika hatua tatu za maisha ya Kiroho "kuna viwango mbalimbali vya upendo kulingana na majukumu mbalimbali ambayo ustawi wa upendo unamdai mtu ayachukue. La kwanza ni *kukwepa dhambi* na kushinda mivuto ya tabia mbovu inayopingana na mivuto ya upendo: ndilo jukumu la *wanaoanza,* ambao ndani mwao upendo unatakiwa kulishwa na kutunzwa usije ukapotea. Hapo linakuja jukumu la pili: mtu anapaswa hasa *kukesha na kukua katika uadilifu,* jambo linalowafaa *wanaoendelea* ambao kazi yao hasa inalenga upendo uimarike kwa kustawi ndani mwao. Jukumu la tatu la mtu ni *kujitahidi hasa kuungana na Mungu na*

*kumfurahia:* ndilo linalowafaa *waliokamilika,* wanaotamani kwenda zao wakae na Kristo" (Mt. Thoma wa Akwino).

Kama kati ya utoto na ujana kuna kipindi kigumu cha ubalehe, vilevile kuna kipindi cha namna hiyo katika kuvuka toka hatua ya utakaso ya wanaoanza kwenda hatua ya mwanga ya wanaoendelea. Hapo mtu aliyeanza kwa bidii anakabili hatari ya kukwama katika kasoro kadhaa asizozitambua, hasa kwa kuishia faraja za kihisi katika sala. Basi anaachishwa hizo ili kuingizwa katika *njia ya Kiroho isiyotegemea hisi,* ambapo katika ukavu anaanza kumiminiwa sala ili asonge mbele.

Ndivyo alivyoeleza Mt. Yohane wa Msalaba, "Usiku au utakaso wa Kimungu wa hisi unampatia mtu usafi wake ukimvua upande wa hisi na kuulinganisha na upande wa roho… Ni jambo *la kawaida, linalowatokea wengi kati ya wanaoanza"*. Hapo wanakuja kutambua kwamba, ili wakue katika upendo, wanapaswa kuwa maskini rohoni, kujinyima aina zote za upuuzi, majivuno, kiburi na ulafi wa roho. "Hayo makao ya hisi yanapopata kutulia hivyo, kwa maono kuratibiwa, tamaa mbaya kuzimwa, hamu kutulizwa na kulala usingizi katika usiku wa utakaso, ndipo roho inapoweza kutoroka iwajibike katika njia ya Kiroho. Inaanza kuwa miongoni mwa *wanaoendelea,* na kujikuta katika hatua inayoitwa *ya mwanga*. Ndipo Mungu anapolisha na kuimarisha roho kadiri anavyopenda kwa *sala ya kumiminiwa,* pasipo roho kuichangia kwa mifuatano ya mawazo, kwa utendaji au kwa kushiriki katika kazi hiyo" (walau kwa kawaida).

Mbele zaidi alieleza kasoro maalumu za wanaoendelea: ushamba wa kimaumbile, haja ya kujitokeza, kujiamini kipumbavu na kiburi cha chinichini. Hizo zinaonyesha wanavyohitaji *utakaso wa Kimungu wa roho* ili kuingia *hatua ya waliokamilika.* Jaribu hilo ni kipindi kigumu kama kile kinachotokea katika maisha ya kawaida, kijana anapoanza kutumia uhuru, pengine kwa hasara yake mwenyewe.

Mt. Yohane wa Msalaba ametufafanulia *sheria za juu za uzima wa neema* zinazotimia kwa wale wanaosonga mbele kwa bidii wasigeuke nyuma. Tukisoma kwa makini maisha ya watumishi wa Mungu, tunaona katika matatizo yao utakaso huo wa kina wa hisi na wa roho ambao hatimaye uliweka utu wao wote *chini ya Mungu.* Mtakatifu huyo alieleza vizuri kuliko wote *vipindi hivyo viwili vigumu vya mpito kutoka hatua moja hadi nyingine,* alivyoviita kwa usahihi *matakaso ya Kimungu ya hisi na roho.* Hayo yanalingana na umbile la binadamu (lenye pande mbili, yaani mwili na roho), tena yanalingana na mfumo wa neema inayotia utakatifu, inayotakiwa kuhuisha zaidi na zaidi vipawa vyetu vyote na matendo yetu yote mpaka *undani wa nafsi uwe kweli wa Mungu tu kwa kutakata umimi wowote* (kujipendea kwa kujitambua au la).

Kwa ufupi ni kwamba katika wale wanaoanza, pamoja na *kiwango cha kwanza cha upendo,* yanaonekana *maadili chipukizi*. *Kujishinda* kwa ndani na kwa nje kunazidi kuwaepusha na dhambi nyepesi za makusudi, au kuwainua mara wakiangukia dhambi ya mauti. Sala yao ni *ya midomo* na ya *kutafakari kwa mifuatano ya mawazo* kunakoelekea kugeuka sala sahili ya mapendo. Ndani mwao *vipaji vya Roho Mtakatifu* vinafichikafichika bado: mara mojamoja wanapata miangaza yake ya pekee, lakini hawajawa tayari kufaidika nayo. Usikivu kwa Roho Mtakatifu unaendelea kuwa dhaifu; mtu anatambua zaidi utendaji wake mwenyewe na kulazimika mara nyingi kukiri umaskini wake katika *kipindi kigumu cha ukavu wa hisi, utakaso mchungu wa Kimungu* ambao unastahimiliwa vizuri au kiasi na unaashiria kuvukia hatua ya mwanga.

Katika wale wanaoendelea, pamoja na *kiwango cha pili cha upendo,* yanaonekana *maadili imara,* hasa upole, subira, unyenyekevu halisi zaidi unaoelekeza kuwa wema kwa jirani, na roho ya mashauri matatu ya Kiinjili. *Vipaji vya Roho Mtakatifu vinaanza kujitokeza,* hasa vitatu vya chini, yaani uchaji, elimu na ibada. Wanazidi kuwa wasikivu kwake na kufaidika na mianga ya ndani. Hapo wakijitahidi kweli, kwa kawaida *sala ya kumiminiwa* inaanza kwa tendo mojamoja la kuzama katika sala wakati wa kukusanya mawazo kwa hiari; halafu, wakiwa waaminifu, zinafuata polepole sala ya kujaliwa kukusanya mawazo, sala ya utulivu (ama mkavu ama wenye nderemo), ambapo ni wazi mchango wa kipaji cha ibada kinachowafanya walie, "Aba! Yaani, Baba!" (Rom 8:15; Gal 4:6). Ndipo maongezi na nafsi yao yanapogeuka kuwa maongezi na Mungu. Hapo *wanaanza kuona ndani mwao* kiburi kinachofichika, utovu wa wema kwa jirani, pengine ukali, utovu wa ari kwa wokovu wa watu wengi wanaopotea; kasoro hizo zote *zinahitaji utakaso mwingine wa Kimungu*, ule wa roho.

Katika wale waliokamilika, pamoja na kasoro kadhaa zisizo za hiari kabisa, tunashuhudia *kiwango cha tatu cha upendo na maadili ya hali ya juu* (pengine ya kishujaa): upole mkubwa, subira inayoyumbishwa kwa nadra tu, unyenyekevu mkuu ambao hauogopi dharau bali unapenda kudhalilishwa, imani kubwa inayofanya waone mambo yote kutoka juu, tumaini kubwa kwa Mungu, moyo mkuu unaolenga kutenda makuu ingawa yanaendana na vipingamizi, halafu kujiachilia kikamilifu katika matakwa ya Mungu ambayo hali yetu ya kesho na ya milele inayategemea. Roho ni kama *inatawaliwa* na Roho Mtakatifu anayeiongoza kutekeleza maadili kikamilifu zaidi. *Vipaji vya akili na hekima* vinaonekana *kwa namna wazi na mara nyingi* zaidi. Kwa kawaida ndipo inapopatikana sala ya kumiminiwa ya muungano. Hatimaye undani wa roho umetakata, na vipawa vyote vya umbile vipo moja kwa moja chini ya Mungu aliyemo katika hekalu la ndani kama utangulizi wa heri isiyo na mwisho kamwe.

Tunaweza kuonyesha hayo maendeleo ya Kiroho kwa jedwali lifuatalo, ambalo lisomwe kuanzia chini kwenda juu.

| VIWANGO VYA UPENDO | MAADILI | VIPAJI | MATAKASO | SALA | MAKAO YA MT. TERESA |
|---|---|---|---|---|---|
| WALIOKAMILIKA Hatua ya muungano Maisha ya mafumbo | Maadili ya juu na ya kishujaa: kiwango cha 3° cha upendo, unyenyekevu kamili, imani kubwa, kujiachilia kwa Mungu, subira inayoyumbishwa kwa nadra tu. | Vipaji vya juu kuonekana vizuri na mara nyingi zaidi. Mtu ni kama anatawaliwa na Roho Mtakatifu, akimuacha atende tu, lakini mwenyewe haachi kutekeleza maadili. | Utakaso wa Kimungu wa roho hasa chini ya kipaji cha akili (ambapo majaribu yanaongozana huku vipaji vya nguvu na shauri vikijitokeza): kuingia hatua ya muungano. | Sala za kumiminiwa ya muungano wa kawaida, ya muungano kamili (pengine kwa kutoka nje ya nafsi) na ya muungano unaotugeuza, chini ya kipaji cha hekima kinachostawi (fadhili zinaongozana). | 5°, 6° na 7° |
| WANAOENDELEA Hatua ya mwanga Kizingiti cha maisha ya sala hasa | Maadili imara: kiwango cha 2° cha upendo, utiifu, unyenyekevu mkubwa, roho ya mashauri ya Kiinjili. | Vipaji vya Roho Mtakatifu kuanza kuonekana, hasa vile vitatu vya chini (uchaji, elimu na ibada). Mtu anazidi kuwa msikivu na kufaidi mianga ya ndani. | Utakaso wa Kimungu wa hisi, hasa chini ya vipaji vya uchaji na elimu (majaribu yanaongozana): kuingia hatua ya mwanga. | Zinaanza sala za kumiminiwa: kuzama mara mojamoja katika mafumbo wakati wa kujikusanya kwa hiari; halafu sala ya kukusanyika kwa kujaliwa, na ya utulivu mkavu au wenye nderemo. Kipaji cha ibada. | 3° na 4° |
| WANAOANZA Hatua ya utakaso Maisha ya juhudi | Maadili chipukizi: kiwango cha 1° cha upendo, kiasi, usafi, subira, ngazi za kwanza za unyenyekevu. | Vipaji vya Roho Mtakatifu kufichikafichika: mianga ya mara mojamoja, ambayo mtu hajawa tayari kufaidika nayo. Anatambua hasa utendaji wake mwenyewe. | Utakaso wa hiari wa hisi na wa roho, yaani kujishinda kwa nje na kwa ndani. | Sala za kujipatia yaani za kujikusanya kwa hiari (sala ya midomo, tafakuri, halafu sala ya mapendo inayozidi kuwa sahili). | 1° na 2° |

## 1.16. ***SOMO LA KIMUNGU***

Kati ya njia kuu za utakatifu zilizotolewa kwa wote, mojawapo ni somo la Kiroho, hasa la Maandiko matakatifu. Katika sura hii tutalizungumzia, tukionyesha misimamo inayohitajika ili kufaidika nalo.

**MAANDIKO MATAKATIFU NA UZIMA WA ROHO**

Mara nyingi udanganyifu, uzushi na uhuni vinaambukizwa kupitia vitabu vibaya, kumbe "kusoma vitabu vitakatifu ni uzima wa roho" (Mt. Ambrosi). Mt. Jeromu alisimulia jinsi alivyovutiwa kusoma kwa juhudi Maandiko matakatifu. Alipoanza kutawa, akipenda bado vitabu vya kipagani, alijiona katika ndoto yuko mbele ya Mungu na kuulizwa kwa ukali yeye ni nani. Alipojieleza kuwa ni Mkristo, Hakimu mkuu akamjibu, "Mwongo wewe, u mfuasi wa Sisero; kwa sababu hazina yako ilipo, ndipo ulipo moyo wako pia". Mara akaagiza apigwe mijeledi. "Nilipoamka nilitambua haikuwa ndoto tu, bali kweli, kwa sababu mabegani nilikuwa na alama za mapigo niliyoyapata. Kuanzia hapo nimesoma Maandiko matakatifu kwa bidii nyingi kuliko nilivyokuwa nikisoma vitabu visivyo vya dini kwanza". Kutokana na hayo tunaelewa aliyomuandikia Eustoki, "Usingizi ukukute tu ukisoma, tena angalia sana usipatwe na usingizi juu ya kitabu tofauti na Maandiko matakatifu".

Katika kitabu gani tutaweza kuchota uzima kuliko katika kile kilichoandikwa na Mungu? Hasa *Injili,* maneno ya Mwokozi na matukio ya maisha yake yanatakiwa kuwa fundisho hai la kulizingatia daima. Yesu alijua kufanya mambo makuu yaeleweke kwa wote kutokana na usahili alioutumia. Tena neno lake halibaki nadharia tu, bali linaongoza mara kwenye unyenyekevu halisi, upendo wa Mungu na wa jirani. Katika kila neno tunahisi alitafuta tu utukufu wa Baba aliyemtuma na wokovu wa watu. Turudie daima maneno ya hotuba ya mlimani (taz. Math 5-7) na yale yaliyofuata karamu ya mwisho (taz. Yoh 13-17). Tukiyasoma kwa unyenyekevu, imani na upendo, tutakuta ndani yake neema inayotuongoza kuiga kila siku vizuri zaidi maadili ya Mwokozi na upendo wake wa kishujaa kwa msalaba. Pamoja na ekaristi, ndiyo lishe halisi ya watakatifu: Neno la Mungu tulililoletewa na Mwanae pekee, Neno aliyefanyika mwili. Chini ya herufi zake limefichika wazo

hai la Mungu, ambalo vipaji vya akili na hekima vinatuwezesha kulichimba na kulionja zaidi na zaidi.

Baada ya Injili hakuna kinachotulisha vizuri kuliko *Matendo ya Mitume* na *Nyaraka* zao. Ndiyo mafundisho ya Mwokozi ambayo wafuasi wake wa kwanza, walioagizwa kutulea katika shule yake, waliyatekeleza na kuyafafanua waamini walivyohitaji. Maisha ya kishujaa ya Kanisa la mwanzoni, uenezi wake kati ya matatizo makubwa, yale yote yanayoelezwa na *Matendo ya Mitume* ni fundisho la kumtumainia Mungu na kujiachilia kwake. Tutaona wapi kurasa za dhati na hai kuliko zile za *Nyaraka* kuhusu Nafsi na kazi za Kristo (taz. Kol 1), uangavu wa maisha ya Kanisa na ukuu wa upendo wa Mwokozi kwake (taz. Ef 1-3), kufanywa waadilifu kwa kumuamini Kristo (taz. Rom 1-11), ukuhani wa milele wa Yesu (taz. Eb 1-9)? Halafu tukizingatia maadili ya Nyaraka, tutaona wapi mahimizo ya nguvu zaidi kwa ajili ya upendo, uwajibikaji, udumifu, subira, utakatifu, pamoja na kanuni za hakika kuhusu namna ya kuwatendea wakubwa, watu wa hali moja, wadogo, tena watu dhaifu, wakosefu, walimu wa uongo? Tutaona wapi maelezo hai zaidi kuhusu wajibu wa Wakristo wote kwa Kanisa?

Katika Agano la Kale kila Mkristo anapaswa kuzijua hasa *Zaburi,* zinazodumu kuwa sala ya Kanisa.

Tukirudia kusoma mfululizo, kwa heshima na upendo, Maandiko matakatifu, tutakuta ndani yake mwanga na nguvu mpya daima. Mungu amelitia neno lake uweza usioisha, nasi tukisha kusoma vitabu vingi na kuvikinai karibu vyote, hatimaye tutairudia Injili kama utangulizi wa mwanga wa milele.

**MAANDISHI YA WATAKATIFU**

Baada ya Biblia, vitabu vya Kiroho vya watakatifu ndivyo vinavyotuangaza na kutuwasha zaidi. Ingawa havikuandikwa kwa uvuvio ule usioweza kukosea, hata hivyo vimeandikwa kwa mwanga na mpako wa Roho Mtakatifu.

Tujue vitabu bora vya watakatifu Bazili Mkuu, Yohane Krisostomo, Jeromu, Augustino, Yohane Kasiano, Leo Mkuu, halafu Denis na watakatifu Benedikto, Gregori Mkuu na Masimo Muungamadini.

Tujue pia yanayohusu maisha ya Kiroho katika maandishi ya watakatifu Anselmi na Bernardo, Richard wa Mt. Viktori, watakatifu Alberto Mkuu, Thoma wa Akwino na Bonaventura, M.H. Anjela wa Foligno, Yohane Tauler, M.H. Henri Suso, Mt. Katerina wa Siena, M.H. Yohane Ruysbroeck, pamoja na Thomas wa Kempis anayedhaniwa kuwa mtunzi wa *Kumfuasa Yesu Kristo.*

Kati ya waandishi wa karne zilizofuata, inafaa tusome vitabu vya Fransisko wa Osuna, Mt. Inyasi wa Loyola, Alois wa Blois, watakatifu Teresa wa Yesu na Yohane wa Msalaba, Alois wa Granada, Mt. Fransisko wa Sales, Alois Lallemant, Yohane Olier, watakatifu Visenti wa Paulo na Yohane Eudes, Yakobo B. Bossuet, Mt. Alois Maria wa Montfort, Petro Caussade na Mt. Alfonso Maria wa Liguori.

Hatuwataji waandishi wa karne za mwishomwisho, ambao walio muhimu zaidi kati yao wanajulikana na wote, hasa Mt. Teresa wa Mtoto Yesu.

**MAISHA YA WATAKATIFU**

Tuongeze kusoma maisha ya watakatifu, ambayo daima yanavutia na mara nyingi yanaweza kuigwa. Vitabu hivyo vinatueleza walivyotenda, katika nafasi pengine ngumu, wanaume na wanawake wenye umbile kama la kwetu, ambao mwanzoni walikuwa na kasoro na udhaifu sawa nasi, lakini polepole neema ikaja kushinda umbile kwa kuliponya, kuliinua na kulitia uzima mpya. Hasa ndani mwao tunaona maana halisi na uzito wote wa neno la Mt. Thoma wa Akwino: “Neema haiangamizi umbile, bali inalikamilisha”. Katika watakatifu, hasa kwenye hatua ya muungano, mema ya umbile na neema vinalingana kweli.

Katika maisha yao tuzingatie hasa yanayoweza kuigwa; mambo ya pekee tuyaone tu kama *ishara ya Kimungu* tuliyopewa ili tutoke usingizini na kutambua *yaliyo ya ndani na ya juu zaidi katika maisha ya Kikristo ya kawaida.* Kwa mfano, maumivu ya wenye madonda ya Yesu yatukumbushe Mateso ya Mwokozi yanapaswa kuwa nini kwetu na jinsi tunavyotakiwa kuimba vizuri zaidi kwenye Njia ya Msalaba, “Mama mtakatifu, fanya hivi, / choma kabisa moyoni mwangu / madonda ya Msulubiwa”. Neema ya watakatifu kadhaa kunywea donda la Moyo wa Yesu itukumbushe kila Komunyo inavyopaswa kuwa motomoto na bora kuliko ile iliyotangulia. Mifano ya watakatifu kuhusu unyenyekevu, subira, tumaini, upendo usiokoma, inatuvuta kuliko mafundisho ya kinadharia tutekeleze maadili: “Mawazo hayasukumi”.

Inafaa zaidi kusoma maisha ya watakatifu yaliyoandikwa na watakatifu, kama vile yale ya Mt. Fransisko wa Asizi yaliyoandikwa na Mt. Bonaventura; yale ya Mt. Katerina wa Siena yaliyoandikwa na kiongozi wake, M.H. Raimundi wa Capua; na yale ya akina Mt. Teresa waliyoyaandika wenyewe.

**MISIMAMO INAYOHITAJIKA ILI KUFAIDIKA NA MASOMO HAYO**

Sala iliyofanywa vizuri mwanzoni inatupatia neema ya msaada ya kusoma kwa *imani,* inayotuelekeza kumtafuta Mungu mwenyewe katika maandishi ya Kiroho, tukikwepa udadisi usio na maana, majivuno ya akili, elekeo la kuhukumu tunayoyasoma badala ya kufaidika nayo. Badala ya kuridhika na ujuzi tu, tuone *namna ya kutekeleza wenyewe,* tukiwa na *hamu hai tena nyofu ya ukamilifu.* Hapo, hata tukisoma yanayohusu “maadili madogomadogo” (Mt. Fransisko wa Sales) tutapata faida kubwa, kwa kuwa yote yanahusiana na adili kuu la upendo.

Waliosonga mbele katika njia ya ukamilifu, pengine inawafaa warudie kusoma yale yanayowafaa wanaoanza: wataona yote kwa mwanga wa juu zaidi na kushangaa yaliyofichika ndani yake; k.mf. katika mistari ya katekisimu ndogo inayohusu malengo ya kuwepo duniani: "kumjua, kumpenda na kumtumikia Mungu ili kupata uzima wa milele". Vilevile inafaa wanaoanza wachungulie ukuu wa ukamilifu wa Kikristo, mradi wasidai kuruka juu kabla hawajapewa neema hiyo. Kwa kuwa *lengo* la kulifikia ni la mwisho katika utekelezaji, lakini *ni la kwanza katika nia:* toka mwanzo ni lazima tutake kufikia utakatifu ule unaotuwezesha kuingia mbinguni mara baada ya kufa.

Ikiwa wanaoanza na wanaoendelea wana hamu kubwa ya utakatifu, watakuta katika Maandiko matakatifu na katika vitabu vya watakatifu yale yanayowafaa na watafundishwa na mlezi wa ndani. Lakini ni lazima *tusome polepole:* si kumeza vitabu, bali kupenyezwa na yale tunayoyasoma. Hapo masomo ya Kiroho yanageuka kuwa sala. Kwa Mt. Benedikto kusoma ni kidato cha kwanza katika ngazi ifuatayo ya kupanda juu: "Lectio (kusoma), cogitatio (kufikiri), studium (kuzingatia), meditatio (kutafakari), contemplatio (kutazama)".

Inafaa pia *turudie kusoma* baada ya miaka vitabu bora vilivyokwishatusaidia. Maisha ni mafupi: turidhike kusoma na kurudia kusoma yale ambayo kweli yana mhuri wa Mungu, bila ya kupoteza muda katika masomo yasiyo na uhai wala thamani. Ni afadhali kuchimba kitabu bora kimojawapo kuliko kusoma kijuujuu vile vyote vya waandishi wa Kiroho.

Halafu tusome kwa roho ya ibada, *"kwa kutafuta sio ujuzi tu, bali ladha hasa"* ya mambo ya Mungu (Mt. Bernardo). "Asomaye na afahamu" (Math 24:15), akimuomba Mungu mwanga ili aelewe vema. Wanafunzi wa Emau walikuwa hawajaelewa utabiri wa manabii mpaka Bwana alipofungua akili zao. Ndiyo sababu Mt. Bernardo alisema, "Sala ikatishe somo": hapo tu litakuwa lishe ya roho na kuelekeza kusali.

Hatimaye ni lazima *tuanze mara kutekeleza tuliyoyasoma:* "Kila asikiaye maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake *juu ya mwamba…* Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake *juu ya mchanga"* (Math 7:24,26). "Kwa sababu sio wale waisikiao sheria walio wenye haki mbele za Mungu, bali ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki" (Rom 2:13). "Iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu" (Yak 1:22).

Hapo somo litazaa matunda mema: "Nyingine zilianguka penye udongo mzuri; zikamea, zikazaa *moja kwa mia…* ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia" (Lk 8:8,15). Ndivyo lilivyokuwa somo alilolifanya Mt. Augustino aliposikia maneno haya: "Chukua na kusoma"; akafungua Nyaraka zilizokuwa mezani, akasoma, "Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo" (Rom 13:13-14). Kuanzia hapo akaongoka, akajitenga kwa muda fulani, akajiandikisha kwa ubatizo, matunda yakawa kweli mara mia yakawafaidisha wengi hadi leo.

## 1.17. ***UONGOZI WA KIROHO***

Kati ya misaada ya nje kwa utakatifu upo uongozi wa Kiroho. Kwanza tutasema unavyohitajika kwa jumla na kwa hatua tatu za maisha ya Kiroho; halafu sifa ambazo kiongozi awe nazo, na wajibu wa yule anayeongozwa.

### HAJA YA UONGOZI KWA JUMLA

Ingawa uongozi si wa lazima kwa utakatifu, ni njia ya kawaida ya maendeleo ya Kiroho. Bwana alipounda Kanisa lake alitaka waamini wawe chini ya Papa na maaskofu upande wa nje, na chini ya waungamishi upande wa ndani, hao wakiwaelekeza kutoanguka dhambini na kusonga mbele katika maadili. Mt. Paulo alipoongoka, Yesu hakumfunulia mwenyewe mipango yake, bali alimtuma Damasko kwa Anania, ajue kwa njia yake yatakayompasa kuyafanya (taz. Mdo 9:6).

"Fanya bidii sana na uangalifu mkubwa kabisa ili kumpata mtu ambaye aweze kukuongoza kwa hakika katika kazi uliyokusudia ya kuishi kitakatifu; umchague mtu anayeweza kuwaelekeza wenye mapenzi mema njia nyofu ya kumuendea Mungu… Ni kiburi kabisa kudhani huna haja na mashauri" (Mt. Bazili Mkuu). "Usijifanye mwalimu wako mwenyewe, la sivyo utapotea haraka sana" (Mt. Jeromu). "Kama vile kipofu asivyoweza kushika njia nyofu asipoongozwa na mtu, hakuna anayeweza kutembea bila ya kiongozi" (Mt. Augustino). Mt. Yohane Kasiano alifundisha kwamba anayetegemea akili yake hatafikia kamwe ukamilifu wala hataweza kukwepa hila za Ibilisi; njia bora ya kushinda vishawishi vya hatari ni kuvifunua kwa kiongozi mwenye busara na mwanga. Kweli, mara nyingi inatosha kuvifunua kwa anayehusika ili viishe.

"Anayejifanya kiongozi wake mwenyewe anajifanya mwanafunzi wa mpumbavu… Upande wangu natamka kuwa kwangu ni rahisi na ya hakika zaidi kuwaagiza wengi kuliko kujiongoza mimi tu" (Mt. Bernardo). Katika kuwaongoza wengine umimi wetu unatudanganya kidogo kuliko katika kujiongoza; na kama tungejua namna ya kutekeleza wenyewe yale tunayowaambia wengine, maendeleo yetu yangekuwa makubwa. "Bwana wetu, ambaye pasipo yeye hatuwezi kitu, hatamjalia kamwe neema yake yule ambaye, ingawa anaye mtu mwenye uwezo wa kumfundisha na kumuongoza, anapuuzia chombo hicho muhimu cha utakatifu, akidhani

anajitosheleza na kuweza kwa nguvu zake kutafuta na kuona yanayofaa kwa wokovu wa milele… Aliye na kiongozi ambaye anamtii katika yote na kikamilifu, atalifikia lengo lake kwa urahisi na haraka sana kuliko kama akifanya peke yake, hata kama ana akili sana na vitabu vyenye hekima kuhusu mambo ya Kiroho… Kwa jumla, wale wote waliofikia ukamilifu wamefuata njia ya utiifu, isipokuwa kama kwa fadhili au neema ya pekee Mungu alimfundisha mwenyewe mtu mmojammoja asiyekuwa na wa kumuongoza" (Mt. Visenti Ferrer).

Mt. Fransisko wa Sales alionyesha kuwa hatuwezi kuamua kwa haki katika kesi zetu wenyewe, kutokana na aina ya kujipendea "ya siri na isiyotambulikana ambayo tusipoona vizuri hatuwezi kuivumbua; na wale waliopatwa nayo hawaijui wasipoonyeshwa". Aliyekaa muda mrefu katika chumba ambacho milango na madirisha yake yamefungwa hatambui kuwa humo hewa imekuwa chafu kwa njia ya kupumua, kumbe anayeingia anatambua mara. Sisi sote tunakubali kwamba kiongozi anahitajika ili kupanda mlima mrefu; bila ya shaka anahitajika zaidi ili kupanda hadi kilele cha ukamilifu, hasa kwa sababu tunapaswa kukwepa hila za yule asiyetaka tupande. Mt. Alfonso Maria wa Liguori alitaja uongozi unahusika na nini zaidi: malipizi, upokeaji wa sakramenti, sala, utekelezaji wa maadili na namna ya kutenda kitakatifu kazi za kila siku.

Shuhuda hizo zote na nyinginezo zinaonyesha wazi haja ya uongozi kwa jumla. Tutaelewa zaidi kwa kuzingatia hatua tatu za maisha ya Kiroho, yaani mahitaji ya wanaoanza, wanaoendelea na waliokamilika.

### UONGOZI WA WANAOANZA

Uongozi wenye busara, uimara na moyo wa kibaba unahitajiwa hasa na wanaoanza, kama unavyofanywa na walezi utawani. Baadaye haja hiyo haisikiki tena vile, isipokuwa katika vipindi vigumu yanapotokea mabadiliko na unapotakiwa uamuzi muhimu.

Wanaoanza wanahitaji kukingwa dhidi ya marudio ya makosa na dhidi ya kasoro mbili zifuatazo zinazopingana. Baadhi wakipokea faraja za kihisi katika sala wanazidhania neema za juu, na kwa kiburi wangetaka *kuruka mara* na kufikia muungano wasipitie hatua za lazima. Hao wanahitaji kukumbushwa haja ya unyenyekevu na kusadikishwa kuwa safari ya ukamilifu ni kazi ya maisha yote: hatuwezi kuruka bila ya mabawa, na katika kujenga tunaanza na misingi. Lengo ni la kwanza kutamaniwa na kukusudiwa, lakini ni la mwisho kufikiwa; tena haifai kupuuzia njia duni za lazima kulifikia. Baadhi wana *kiburi cha siri katika kushika maisha magumu* na kujitosa *mno* katika malipizi hadi kuharibu afya. Baadaye, wakitaka kujitibu wanalegea na kwenda kinyume cha awali. Hao wanahitaji kujifunza kiasi cha Kikristo na kwamba maadili ya Kimungu hayatoshi pasipo maadili ya kiutu ili kutawala polepole hisi.

Uongozi unahitajika hasa katika *kipindi kirefu cha ukavu* ambapo kutafakari ni kwa shida, tena kuna vishawishi vikali pamoja na upinzani wa watu. Tutakavyoeleza, jaribu hilo linavusha kutoka hatua ya utakaso kwenda hatua ya mwanga mradi ziwepo dalili tatu ambazo kiongozi anatakiwa kuzitambua: 1) kutofurahia mambo ya Mungu wala ya dunia; 2) kuendelea kwa kawaida kumkumbuka Mungu, kutamani ukamilifu na kuogopa kutomtumikia; 3) kushindwa kutafakari kwa mpangilio na badala yake kuvutiwa na tendo la kumtazama tu Mungu. Katika kipindi hicho kigumu, kinachotakiwa kuleta uongofu wa pili, ni lazima kumsikiliza kiongozi wa kufaa ili kusonga mbele kwa bidii badala ya kubaki nyuma.

### UONGOZI WA WANAOENDELEA NA WA WALIOKAMILIKA

Kwa kawaida uongozi wa wanaoendelea unaweza kufanyika haraka zaidi, kwa sababu anayeongozwa ameshajua zaidi maisha ya Kiroho na mara nyingi anaweza kueleza kwa neno moja shauri analohitaji linahusu nini. Hapo kiongozi ni kama shahidi wa maendeleo yake; anatakiwa kutambua kazi ya mlezi wa ndani ili awe chombo chake na kuhakikisha usikivu wa mtu kwa Roho Mtakatifu, akipambanua ndani yake pumba na mchele, yaani kilema kikuu ambacho apambane nacho, na mvuto maalumu wa neema ambao aufuate. Inafaa tumkimbilie kiongozi hasa wakati wa mazoezi ya Kiroho ya kila mwaka ili kumueleza kwa unyofu wote undani wa roho tusije tukajidanganya kwa kuangukia kiburi kilichofichika na kujiamini kipumbavu.

Kwa wanaoendelea pia kuna vipindi vigumu vinavyohitaji uongozi bora, hasa wanapotakiwa *kuvukia hatua ya muungano.* Majaribu hayo yana namna mbalimbali, lakini kwa kawaida ni kunyimwa kwa muda mrefu faraja si za hisi tu, bali za roho pia. Hapo vinatokea mara nyingi vishawishi dhidi ya imani, tumaini na upendo na unahitajika kwa namna ya pekee msaada wa kiongozi mwenye mwanga na mang'amuzi. Hata mtu anayeweza kuongoza wengine katika hatua hiyo hawezi kujiongoza kwa sababu "hakuna tena mapito tayari" (Mt. Yohane wa Msalaba), hivyo anapaswa tu kufuata mwanga wa Roho Mtakatifu asiuchanganye na msukumo mwingine unaoweza ukafanana nao.

Waliokamilika pia wanajisikia haja ya msaada huo ili kuona *namna ya kulinganisha* msimamo wa *kujiachilia* mikononi mwa Mungu *na utendaji* ambao Bwana anawadai, ili kutekeleza vizuri msemo huu: "kuwajibika na kujiachilia". Wanajisikia haja ya kuongozwa ili kudumisha moyoni mwao upendo hai kwa msalaba pamoja na unyenyekevu mkubwa. Basi, ikiwa hao wanahitaji uongozi, zaidi tena wanauhitaji wanaoanza.

**SIFA ZA KIONGOZI NA WAJIBU WA ANAYEONGOZWA**

Kiongozi "awe amejaa *upendo, elimu na busara:* likikosekana mojawapo kati ya hayo matatu, kuna hatari" (Mt. Fransisko wa Sales). "Ni muhimu sana kiongozi awe na mwanga: yaani awe na *busara na mang'amuzi sana.* Ikiwa zaidi ya hayo ni *mwanateolojia* pia, basi ni kamili. Lakini isipowezekana kumuona mtu mwenye sifa hizo tatu pamoja, ni afadhali awe na zile mbili za kwanza, kwa sababu katika shida inawezekana kupata shauri la wasomi. Nionavyo mimi, hao wa mwisho, wasipojitahidi katika sala, hawafai sana kwa wanaoanza; lakini sitaki kushauri wasiwe na uhusiano nao… Elimu ni jambo kubwa… Mungu atuepushe na ibada za juujuu na zilizojaa upuuzi" (Mt. Teresa wa Yesu).

Upendo wa kiongozi umfanye asijitafutie faida na aongoze mioyo kwa Mungu, si kwake mwenyewe. Y. Tauler alisema viongozi wanaojivutia watu ni kama mbwa ambao katika uwindaji wanamla mnyama badala ya kumleta kwa bwana wao; hapo huyo anawapiga kweli. Wema wa kiongozi usigeuke udhaifu: awe imara, asiogope kusema ukweli. Vilevile asipoteze muda katika maongezi na maelezo ya bure, bali alenge moja kwa moja ustawi wa roho. Awe anajua njia, mafundisho ya walimu wa Kiroho na kwa kiasi fulani saikolojia. Ili awe chombo cha Roho Mtakatifu atambue mvuto wake maalumu ambao mtu aufuate na kilema kikuu ambacho akiepe. Kwa ajili hiyo ajiombee mwanga, hasa katika kesi ngumu, na akiwa mnyenyekevu atapokea neema za kufanyia kazi yake. Ataona namna ya kusukuma wengine na ya kupoza umotomoto wa wengine, akiwafundisha hao wa mwisho wasichanganye mapendo ya juujuu na upendo unaothibitishwa na matendo. Busara yake katika kuongoza watu wenye bidii ikwepe hatari mbili: ile ya kutaka kufikisha wote haraka na bila ya tofauti kwenye sala ya hali ya juu, na ile ya kupuuzia suala hilo. Haifai kukimbia mno wala kuchelewa; kwanza zipimwe *dalili tatu* tulizozitaja ili kuvuka kutoka tafakuri kwenda sala ya kumiminiwa. Kabla ya kufanya hivyo, inafaa na kutosha kukumbusha watu wawe waaminifu kwa mianga ya mlezi wa ndani mara inapojitokeza kulingana na wito wao.

Kuhusu wajibu wa mtu anayeongozwa, unatokana na yale tuliyoyasema: *amheshimu* kiongozi kama wakili wa Mungu, akiepa mambo mawili, yaani kumlaumu vikali na kuhusiana naye kirafiki mno. Heshima hiyo iendane na mapendo ya mtoto kwa mzazi, manyofu, ya Kiroho tu, yanayozuia wivu wowote na hamu ya kupendwa kwa namna ya pekee. Awe na tumaini la kitoto na *uwazi mkubwa* kwa kiongozi wake. "Muongee naye kwa unyofu na uaminifu mkuu, mkimfunulia wazi kabisa mema yenu na mabaya yenu, bila ya kudanganya wala kuficha" (Mt. Fransisko wa Sales). Hatimaye, anahitaji *utiifu* mkubwa ili kusikiliza na kufuata mashauri yanayotolewa, la sivyo atafuata matakwa yake mwenyewe badala ya yale ya Mungu. Bila ya shaka hakatazwi kujulisha shida kubwa iliyopo katika kutekeleza shauri fulani; lakini baada ya kufanya hivyo aweke mtazamo wake chini ya kiongozi. Hata akikosea, sisi tukimtii hatukosei, isipokuwa akitushauri kinyume cha imani au cha maadili; hapo tumuache mara.

Tusibadili kiongozi pasipo sababu nzito, hasa tukifanya hivyo kwa ugeugeu, kiburi, aibu ya kipumbavu au udadisi. Lakini tumbadili bila ya wasiwasi tukiona mitazamo yake ni ya kibinadamu mno, anatupenda kihisi mno, au hana elimu wala busara zinazohitajika. Nje ya nafasi hizo tudumu iwezekanavyo katika uongozi uleule ili tuzidi kufuata njia njema bila ya kubadilibadili. Tuyakumbuke maneno ya Mt. Ludoviko IX kwa mwanae: "Uungame mara nyingi na kuchagua waungamishi wenye elimu na uadilifu ambao wajue kukufundisha la kufanya na la kukwepa, halafu uache wakuonye na kukushauri kwa uhuru wote".

# 2. **UTAKASO WA WANAOANZA**

Inatupasa tuongee juu ya kila mojawapo ya hatua tatu za maisha ya Kiroho, kuanzia utakaso wa wanaoanza. Tutaona sifa maalumu za hatua hiyo, na kuongea kirefu juu ya utakaso wa roho, matumizi ya sakramenti na sala, na hatimaye juu ya utakaso wa Kimungu wa hisi ambao unaingiza katika hatua ya wanaoendelea. Tutasema pia juu ya kutumia neema vibaya: walioanza halafu wakawa vuguvugu na wachelewaji hawafikii kamwe hatua ya juu. Sehemu hii ni muhimu kwa sababu wengi wasioitekeleza wanabaki nyuma, kumbe wanaofaidika nayo wanasonga mbele kweli. La maana si kusoma vitabu vingi na kuwa na mawazo mengi, bali kuamini kwa dhati mawazo ya msingi na kuyatekeleza moja kwa moja. Ni ajabu kwamba watakatifu wengi hawakuwa na elimu, ila walipenywa na Injili mpaka ndani na kuitekeleza kwa bidii, pengine katika maisha ya kawaida. Hivyo walifikia hadi hekima ya juu iliyoonekana katika maneno

yao, na hadi upendo uliozaa matunda tele kwa wokovu wa watu.

## 2.1. *HATUA YA KIROHO YA WANAOANZA*

Mwenye neema inayotia utakatifu anayeanza kulenga upendo kamili, hali yake ya Kiroho inaweza kufafanuliwa kwa kuangalia anavyojifahamu na anavyomfahamu Mungu, anavyojipenda na anavyompenda Mungu.

### KUJIFAHAMU NA KUMFAHAMU MUNGU

Wanaoanza wanajifahamu kiasi; polepole tu wanatambua kasoro walizonazo, matokeo ya dhambi walizosamehewa na ya zile mpya wanazotenda kwa ujuzi na hiari zaidi. Hapo hawatakiwi kujitetea, bali kujirekebisha kwa bidii, naye Bwana anawafanya watambue unyonge wao na kuuzingatia kwa mwanga wa huruma yake inayowahimiza kusonga mbele. Kila siku wanatakiwa kujitafiti dhamiri na kujifunza namna ya *kujitawala* wasije wakafuata tu msukumo wa maono.

Hata hivyo wanajifahamu kijuujuu tu. Hawajatambua hazina waliyotiwa na ubatizo wala *umimi* ambao unadumu ndani mwao na kujitokeza mbele ya shida kubwa au lawama. Mara nyingi wanaona wengine wanavyojipendea wasikumbuke maneno ya Bwana, "Mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii?" (Math 7:3). Ndani mwao wana almasi iliyozungukwa na udongo, wasijue bado thamani yote ya almasi wala kasoro zote za udongo. Mungu anawapenda kuliko wanavyodhani, lakini kwa upendo unaodai wajikane ili kufikia uhuru halisi.

Polepole wanazidi *kumjua Mungu kwa namna inayotegemea bado viumbe* na mifano ya Injili, kwa kuwa hawajazoea mafumbo ya wokovu wala kuona yanavyong'ariza wema wa Mungu. Pengine wanauona kidogo wakitafakari mateso ya Mwokozi, lakini hawajaweza kupenya vilindi vya ukombozi. Wanatazama mambo ya Mungu kijuujuu; hawajafikia ukomavu wa Kiroho.

### KUMPENDA MUNGU MWANZONI

*Upendo wa Mungu walionao unalingana na hali hiyo.* Wanaoanza kwa bidii wanampenda kwa *kuchukia dhambi* (wanakwepa ile ya mauti na hata ile nyepesi ya makusudi), na kwa *kufisha* tamaa za mwili, za macho na kiburi. Hapo tunatambua wanaanza kumpenda kwa utashi wao.

Lakini wengi wanapuuzia kimatendo hiyo kazi ya lazima ya kufisha, hivyo wanafanana na watu wanaotaka kupanda mlima kuanzia katikati, si toka chini walipo. Hapo wanapanda kimawazo tu, wasipige hatua zinazohitajika; umotomoto wao utazimika upesi kama moto wa nyasi kavu. Wakidhani wanaelewa mambo ya Kiroho watayaacha baada ya kuyakaribia tu.

Kinyume chake, wanaotaka kuendelea kweli - bila ya kudai kwa kiburi cha siri watangulie neema wala kufanya malipizi makubwa pasipo ruhusa - mara nyingi wanatunukiwa *faraja za kihisi* katika kusali au kusoma mambo ya Mungu. Hivyo Bwana anataka *kujipatia hisi zao,* kwa sababu bado wanazitegemea: basi, neema ikizigusa inaziondoa kutoka mambo ya hatari na kuzivuta kwake na kwa Mama yake. Waandishi wa Kiroho walieleza haya *maziwa ya faraja* yanayotolewa katika hatua hiyo, kufuatana na Mt. Paulo: "Naliwanywesha maziwa, sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza" (1Kor 3:2). Lakini karibu wote *wanapendezwa na faraja hizo* kupita kiasi, kana kwamba zingekuwa lengo, si njia. Hapo wanaangukia aina ya ulafi wa roho, inayoendana na *haraka* na udadisi katika kusoma mambo ya Mungu, na aina ya kiburi kilichofichika, kinachowafanya watake kuyazungumzia kana kwamba ni walimu tayari. Hapo *mizizi saba ya dhambi* inajitokeza tena*,* si kwa namna ya kawaida, bali *kuhusu mambo ya Kiroho.* Hiyo yote inazuia ibada halisi.

*Utahitajika uongofu wa pili* katika utakaso wa Kimungu unaojitokeza kwa *ukavu wa hisi wa muda mrefu,* wanaponyang'anywa hizo faraja walizozipenda mno. Ikiwa hapo wana *hamu kubwa ya Mungu,* pamoja na hofu ya kumchukiza, basi ni ishara ya kuwa ndiye anayewatakasa hivyo, hasa wakiwa na shida katika kutafakari kwa mpangilio, pamoja na *elekeo la kumtazama tu* kwa upendo. Ndizo dalili tatu za kuinuliwa kwenye hatua ya mwanga ya wanaoendelea. Wakivumilia vizuri utakaso huo, hisi zao zitazidi kutawaliwa na roho. Hapo mara nyingi wanapaswa kushinda kwa bidii vishawishi dhidi ya usafi na subira, maadili yenye makao katika hisi yanayoimarika katika mapambano hayo. Wakati huo mgumu Bwana anawafanyia kazi akizidi kulima kwa haro alipolima katika uongofu wa kwanza; anang'oa mizizi mibaya, yaani mabaki ya dhambi; anawaonyesha ubatili wa malimwengu na wa kujitafutia heshima na vyeo. Polepole wanaanza maisha mapya, kama mtoto anapokuwa kijana.

Lakini *kipindi hicho kinavumiliwa vizuri au kiasi tu.* Wengi hawafanyi bidii za kutosha na wanaweza wakageuka *wachelewaji.* Wengine wanafuata kiaminifu neema ya Mungu na kuendelea.

Ndizo sifa kuu za hatua ya wanaoanza: ni rahisi kuona uhusiano wa mambo ambayo wayapitie ili maisha yao ya ndani yastawi na kuwa maongezi na Mungu.

### JUHUDI ZINAZOHITAJIWA NA WANAOANZA

Jambo lililo muhimu zaidi kuliona ni *juhudi wanazozihitaji toka mwanzo* waweze kuufikia muungano wa

dhati na Mungu.

Kadiri ya Mt. Katerina wa Siena, Mungu alisema, "Nyinyi nyote mmealikwa kwa jumla na kwa namna ya pekee na Ukweli wangu alipolia hekaluni kwa umotomoto wa hamu yake, 'Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe' (Yoh 7:37)… Hivyo nyinyi mmealikwa kwenye chemchemi ya maji hai ya neema. Basi inawafaa mumpitie yeye aliye daraja kwenu, na kudumu hivi kwamba mwiba wowote au upepo wa mbisho au ustawi au pingamizi au tabu nyingine ambayo iwapate visiwafanye muangalie nyuma. Mnapaswa kudumu mpaka mnipate mimi niwapaye maji hai kwa njia ya huyo Neno mpole na mpendevu Mwanangu pekee".

"Bwana anataka tuwe na njaa na kiu ya haki… hivi kwamba hamu yetu ikue zaidi na zaidi… Heri wenye hamu hiyo isiyotulizika; hao watapokea uzima wa milele, na hapo katikati mema ya Kiroho kwa wingi katika kutekeleza amri za Mungu, Mwalimu alivyosema: 'Chakula changu ndicho hiki: niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake' (Yoh 4:34)" (Mt. Thoma wa Akwino).

"'Haya, kila aonaye kiu, njoni majini' (Isa 55:1). Anawaita wenye kiu, kwa kuwa ndio wanaotamani kumtumikia Mungu. Bwana hapokei huduma ya kulazimishwa, bali 'humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu' (2Kor 9:7). Hamuiti mtu mmojammoja tu, bali wale wote wenye kiu, *akiwaalika kunywa kinywaji cha Kiroho kilicho hekima ya Kimungu,* kinachoweza kutimiza hamu zetu; na hekima hiyo ya Kimungu tunapenda kuwapa wengine baada ya kuiona wenyewe. Ndiyo sababu anatuambia, 'Aniaminiye mimi… mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake' (Yoh 7:38). Lakini ili kuifikia chemchemi hiyo isiyokwisha ni lazima kuwa na kiu ya uadilifu, na kutembea kwa bidii *kwenye njia* ya kujikana, njia *iliyo nyembamba* kwa hisi zetu, lakini kwa roho itakuwa pana kama Mungu mwenyewe ambaye inamuelekea. Kumbe njia pana mwanzoni kwa hisi inazidi kuwa nyembamba kwa roho na kufikisha kwenye moto wa Jahanamu" (Mt. Thoma wa Akwino).

"Mfikirie kuwa Bwana anaalika wote. Ndiye ukweli wenyewe, kwa hiyo hakuna wasiwasi. Kama karamu isingekuwa kwa wote, asingetuita sote, au katika kutualika asingesema, 'Nitawapa cha kunywa', ila, 'Njoni nyote, hamtapata hasara, nami nitawapa cha kunywa wale nitakaowataka'. Lakini kwa kuwa anasema bila ya tofauti, 'Njoni nyote', naona ni hakika kuwa wale wote wasiosimama njiani watapewa hayo maji hai. Aliyetuahidia atujalie tuyatafute inavyotakiwa: naomba hivyo kwa jina lake mwenyewe!… Mungu anataka *tunywe maji hayo ili kutakasa roho… Ghafla anaivuta kwake*, na kwa nukta moja anaifundisha kweli nyingi na kuiangaza kuhusu ubatili wa yote kuliko inavyoweza kujipatia kwa miaka mingi… Kuanza, tuanze vipi? Kilicho muhimu zaidi, tena muhimu kabisa, ni kukata *shauri imara,* kuamua kabisa kwamba *hatutasimama mpaka tuifikie chemchemi,* yatokee yoyote, yatupate yoyote, hata tukilaumiwa au kufa njiani chini ya uzito wa vizuio vingi, hata kama ulimwengu wote utaangamia" (Mt. Teresa wa Yesu).

Juhudi hizo wanazozizungumzia watakatifu ni adili la *moyo mkuu* linalofanya tutake kutekeleza maadili yote kwa ukuu halisi; kwa hiyo ni *pambo la maadili yote,* linayachangia yote. Mwenye moyo mkuu haogopi vipingamizi, lawama wala dharau kwa ajili ya ukamilifu wa Kikristo. Anajali ukweli kuliko maoni ya watu ambayo mara nyingi ni ya uongo. Ingawa moyo mkuu haueleweki daima na wale wanaopenda maisha rahisi, kwa ndani unadumu kuwa na thamani: ukiunganika na unyenyekevu unampendeza Mungu usiweze kukosa tuzo.

"Unyenyekevu unaamini hauwezi kitu ukizingatia umaskini wetu, udhaifu wetu… kinyume chake moyo mkuu unatusemesha sawa na Mt. Paulo: 'Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu' (Fil 4:13). Unyenyekevu unatufanya tusijiamini, na moyo mkuu unatufanya tumtegemee Mungu… Kuna watu wanaopendezwa na unyenyekevu wa bandia na wa kijinga unaowazuia wasizingatie ndani mwao mema waliyotiwa na Mungu. Wanakosea kabisa, kwa kuwa mema tuliyotiwa na Mungu yanatakiwa kutambuliwa… kwa utukufu wa wema wa Mungu aliyetujalia… Bila ya shaka unyenyekevu usiozaa moyo mkuu ni wa uongo… Moyo mkuu unatokana na kumtegemea Mungu, nao *unaanza kutekeleza kwa bidii maagizo yake yote…* hata kama ni magumu namna gani… ukijisemea, Nini itaweza kunizuia nisifikie lengo, wakati 'niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema' ndani mwangu 'ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu' (Fil 1:6)?" (Mt. Fransisko wa Sales).

Juhudi za wanaoanza zinatakiwa kuwa za namna hiyo: "Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu" (Lk 9:62).

## 2.2. *FIKRA ZA KIDUNIA NA UFISHAJI KADIRI YA INJILI*

Kisha kupata picha ya jumla ya hatua ya wanaoanza, tunatakiwa kuona kazi inayowapasa wasirudie dhambi. Lakini kwanza tuone mitazamo miwili mipotovu: upande mmoja fikra za kidunia za walio wengi, upande mwingine ugumu wa maisha usiotokana na upendo wa Mungu bali na kiburi.

### FIKRA ZA KIDUNIA KATIKA KUTENDA AU KUTOTENDA

Fikra hizo, ambazo zinakanusha roho ya imani katika mwenendo, zinafufuka daima kwa namna mbalimbali zikidharau ufishaji badala ya kuuona ni ukombozi unaochangia ustawi wa roho. Eti! Kwa nini kusema juu ya *ufishaji,* ikiwa Ukristo ni mafundisho ya uzima; juu ya *kujinyima,* ikiwa Ukristo unatakiwa kupenya utendaji wote wa binadamu; juu ya *utiifu,* ikiwa Ukristo unaleta uhuru? Mbona *umbile* letu ni jema,

linatokana na Mungu na kuelekea kumpenda kuliko vyote? Wanaosema hivyo wanasahau maneno ya Mwokozi: "Amin, amin, nawaambia: Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi. Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele" (Yoh 12:24-25).

Wanasema tena: kwa nini kupinga *maoni na matakwa yetu?* Eti! Ni kujifanya watumwa wasioweza kutenda wanavyotaka, na ni kupoteza uhusiano na ulimwengu tunaopaswa kuuboresha, sio kuudharau. Hawaelewi kwamba waandishi wa Kiroho kwa neno "matakwa yetu" walimaanisha yale yasiyolingana na ya Mungu. Fikra hizo, zikichanganya kiujanja ukweli na uongo, zinatumia hata maneno: "Neema haiangamizi umbile, bali inalikamilisha". Uhaba wa imani unayapotosha, kwa kuwa hapo Mt. Thoma wa Akwino alizungumzia *umbile lenyewe* lilivyoumbwa awali na Mungu, sio *umbile lililojeruhiwa na kuanguka,* jinsi lilivyo sasa kutokana na dhambi ya asili na dhambi zetu binafsi.

Dhana hizo hazichelewi kuonyesha matokeo yake: "kwa kuwa kila mti hutambulikana kwa matunda yake" (Lk 6:44). Hao mitume wa aina mpya, wakitaka kupendeza ulimwengu wanaufuata badala ya kuuongoa; wanapuuzia *matokeo ya dhambi ya asili na uovu mkuu wa dhambi ya mauti* iliyo chukizo kwa Mungu, sio tu dhara kwa binadamu. Wanapuuzia hasa uzito wa dhambi za roho: kutosadiki, kujiamini, kiburi. Wanaona kosa kubwa zaidi ni kutojihusisha na shughuli za jamii, hivyo maisha ya sala tu kwao ni ya bure. Mungu alijibu mwenyewe fikra hizo za Umarekani kwa utakatifu wa Teresa wa Mtoto Yesu na uenezi wa uangavu wake. Hao wanapuuzia tena *ukuu usiopimika wa lengo letu,* yaani Mungu asili ya neema. Hivyo badala ya kusema juu ya uzima wa milele, wanazungumzia maadili yanayohusika kidogo tu na dini, na hawaonyeshi upinzani wa moja kwa moja kati ya mbingu na moto. Hatimaye wanasahau kuwa *msalaba* ndio chombo kilichochaguliwa na Bwana ili kuuokoa ulimwengu.

Matokeo ya fikra hizo yanaonyesha kuwa asili yake ni ubinadamu tu, unaokanusha walau kimatendo yale yanayopita maumbile, na hivyo hauoni ufishaji umo katika kiini cha Ukristo, ni kitu kimoja na toba ambayo ni ya lazima kwa wote.

Kwa namna nyingine fikra hizo ziliwahi kujitokeza kati ya *Watulivu,* hasa M. Molinos aliyedai kwamba *"kutaka kutenda* kunamchukiza Mungu, anayetaka kutenda peke yake ndani mwetu". Mtu asipotenda tena, eti! Anajiangamiza ili Mungu tu aishi na kutawala ndani yake. Kwa msingi huo alidai mtu asimfikirie wala kumpenda, asifikirie mbingu wala moto, *asizingatie matendo yake wala kasoro zake,* asitamani ukamilifu wala wokovu, asimuombe Mungu chochote ila ajiachilie kwake atekeleze mwenyewe matakwa yake ndani ya mtu pasipo mchango wake. Hatimaye alisema, "Mtu hahitaji tena *kupinga vishawishi,* ila asivijali; *msalaba wa hiari wa kujifisha ni mzigo unaolemea na wa bure ambao tuutupe".* Eti! Vishawishi vinafaa daima, hata vinaposababisha maovu: vikija si lazima kutekeleza maadili yaliyo kinyume chake, bali kuvikubali tu, na hivyo kujitambua si kitu. Fikra hizo zinatumbukia uzembe tu.

Kinyume cha fikra hizo mara mojamoja unapatikana *ugumu wa maisha unaotokana na kiburi,* kama ule wa *Wajanseni,* waliosahau kuwa roho ya ufishaji wa Kikristo ni upendo wa Mungu. Mafundisho yao yalizidisha matokeo ya dhambi ya asili hata wakasema, "mtu anatakiwa kufanya malipizi maisha yake yote kwa dhambi ya asili". Walizuia watu wasikomunike wakisema hawastahili muungano huo na Bwana, isipokuwa wenye kumpenda Mungu kitakatifu. Walisahau kuwa huo upendo safi ni tunda la ekaristi, mradi mtu aipokee kwa bidii. Msimamo mkali kama huo hauleti kamwe ukombozi wala amani.

Kama kawaida tunapaswa kukwepa aina mbili za uongo zinazopingana; ukweli uko juu yake, kama kilele kirefu, na unaonekana katika kuzingatia upande mmoja ukuu wa lengo letu na wa upendo, na upande mwingine uzito wa dhambi na wa matokeo yake.

### UFISHAJI KADIRI YA INJILI

Mwokozi hakuja duniani afanye kazi ya kibinadamu ya kusaidia watu, bali kazi ya Kimungu ya kuwapenda hadi kuteketea ili kuwaokoa. Yeye ametufafanulia haja ya *kufia dhambi* ili tupokee kwa wingi uzima mpya, akituonyesha mfano wake kwa kufa msalabani. Kufia dhambi na kuishi kwa hali ya juu ni mambo yanayokumbukwa daima pamoja, chini ya upendo wa Mungu. Mwinjili amesema wazi kuwa Yesu aliwaelekea "wote" aliposema, "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha. Kwa kuwa yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza, au kujipoteza mwenyewe?" (Lk 9:23-25).

Katika hotuba ya mlimani Yesu alionyesha haja ya ufishaji kwa kusisitiza ukuu wa lengo letu lipitalo maumbile: "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni… Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (Math 5:20,48). Sababu ni kwamba Yesu ametuletea neema ambayo ni kushiriki uhai wa ndani wa Mungu, hivyo ni bora kuliko uhai wa kimaumbile hata wa malaika, lakini inadai *ufishaji wa yale yote yasiyoratibiwa ndani mwetu.* Bwana alisema wazi kuhusu ufishaji wa ndani na wa nje unaompasa Mkristo halisi pamoja na roho ambayo iuongoze.

Tunatakiwa kuepa iwezekanavyo *kinyongo* na chuki moyoni: "Ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku

ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako. Patana na mshitaki wako upesi" (Math 5:23-25). Tusimuone ni adui, bali ndugu, mtoto wa Mungu.

Tunapaswa kufisha *tamaa:* "Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe… Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee, wala mwili wako mzima usitupwe katika Jehanum" (Math 5:29-30). Bwana amesema kwa nguvu hivi kwamba watakatifu wanashauri kufunga, kukesha na kushika magumu mengine ambayo, yakitekelezwa kwa busara, utiifu na bidii, yanatumikisha mwili na kuhahikisha uhuru wa roho.

Tunapaswa kufisha *hamu ya kulipa kisasi,* "Mmesikia kwamba imenenwa: Jicho kwa jicho, na jino kwa jino; lakini mimi nawaambia: Msishindane na mtu mwovu" (Math 5:38-39). Yaani msilijibu tusi kwa ukali; mumkatalie hadi kuuawa anayetaka kuwakosesha, lakini mvumilie makosa yake bila ya chuki wala hasira. "Mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili" (Math 5:39). Yaani uwe tayari kukosewa haki kwa ustahimilivu; ndiyo subira inayoshinda hasira ya adui na pengine inamuongoa ilivyotokea katika dhuluma za Kanisa. Ulenge kumpatia Mungu roho ya ndugu mwenye hasira kuliko kutetea haki zako za kidunia. Ndio ukuu wa haki ya Kikristo inayotakiwa kuendana daima na upendo. Haifai wakamilifu wagombane na watu wasipotakiwa kutetea tunu za juu zaidi.

Mwokozi anatudai tena tufishe *umimi* unaotufanya tumkwepe anayetaka kutuomba kitu (taz. Math 5:42), *hukumu* zisizo na msingi (taz. Math 7:1), *kiburi cha roho na unafiki* (taz. Math 6:1-16).

Hatimaye ametuonyesha *roho ya ufishaji* iwe ya namna gani: "Wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso, ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi" (Math 6:17-18). Maana yake, jipake upendo, huruma na furaha ya Kiroho; takasa roho yako na kila elekeo la kujionyesha. Ukitenda mema hukatazwi kuonekana, ila usijionyeshe, usitake kuonekana, la sivyo unapoteza usafi wa nia inayotakiwa kumuendea Baba moja kwa moja. Roho ya ufishaji ni upendo unaoangaza watu ili kuwaokoa. Inawezekanaje *kuwa wapole kwa mtu mkali bila ya kujitawala?* Ni roho ya kumtolea Mungu tabu yoyote inayotupata isaidie kumkaribia na kuokoa watu, ili yote yachangie kufanikisha wema, hata vizuio tunavyovikuta njiani, kama vile Yesu alivyofanya msalaba wake kuwa chombo bora cha wokovu.

Hivyo tunaona ufishaji wa Kikristo ulivyo juu kuliko uzembe wa fikra za kidunia na kuliko maisha yaliyo magumu kwa kiburi. Ndio ufishaji tunaouona katika watu wenye sura ya Yesu msulubiwa: Mungu ni wa ajabu katika watakatifu wake!

## 2.3. *UFISHAJI KADIRI YA MTUME PAULO NA SABABU ZINAZOFANYA UWE WA LAZIMA*

Mafundisho ya Injili kuhusu ufishaji yamefafanuliwa na Mt. Paulo aliyesema, "Nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa" (1Kor 9:27). Zaidi ya kutamka haja hiyo, yeye ametuonyesha ni lazima tufishe yale yote yasiyoratibiwa ndani mwetu kwa sababu ya: 1) matokeo ya dhambi ya asili; 2) matokeo ya dhambi zetu binafsi; 3) ukuu usio na mipaka wa lengo letu lipitalo maumbile; 4) wajibu wetu wa kumfuata Bwana msulubiwa.

Kwa kuzingatia sababu hizo, zinazokanushwa na fikra za kidunia, tutaona ufishaji wa ndani na wa nje ni nini. Unahusiana na maadili mengi, kwa sababu kila moja linapingana na vilema vilivyo kinyume chake, na kwa namna ya pekee unahusiana na adili la toba, ambalo linalenga kuangamiza ndani mwetu matokeo ya dhambi kwa kuwa ni chukizo kwa Mungu, na ambalo linatakiwa litokane na upendo wake.

### MATOKEO YA DHAMBI YA ASILI

Kwanza Mt. Paulo alimlinganisha Yesu Kristo, asili ya wokovu wetu, na Adamu, asili ya uharibifu wetu: "Kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti… Kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki… na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi… kwa Yesu Kristo Bwana wetu" (Rom 5:12,19-21).

Kifo ni mojawapo kati ya matokeo ya dhambi ya asili, lakini Mt. Paulo alitaja pia tabia mbovu ya "utu wa kale", yaani utu jinsi ulivyozaliwa na Adamu, wenye umbile lililoanguka na kujeruhiwa. "Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho na nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli" (Ef 4:22-24). "Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba" (Kol 3:9-10). "Naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" (Rom 7:22-24).

Utu wa kale unakosa ule ulinganifu mzuri wa uadilifu wa asili ulioangamizwa na dhambi. Mtaguso wa Trento umetamka kwamba mtu wa kwanza kwa kosa lake *"amepoteza kwake na kwetu utakatifu na uadilifu*

*wa asili"* na kuturithisha umbile lisilo na neema na lililojeruhiwa. Pasipo kuzidisha kuhusu ubaya wa hali hiyo, tukiri kuwa tunapozaliwa utashi wetu haumuelekei Mungu bali uovu; akili yetu inaelekea udanganyifu; hisi zetu zinaelekea anasa na hasira, vyanzo vya dhambi za kila aina. Ndipo vinapotokea kiburi, kumsahau Mungu, umimi wa namna nyingi ambao haujitambui na unataka raha duniani, badala ya kulenga juu zaidi. "Maumbile yanajifanya daima lengo lake yenyewe, kumbe neema… inafanya yote kwa ajili ya Mungu tu" (Kumfuasa Yesu Kristo III,54).

Utu ulioanguka, sio tu kwamba *umevuliwa* neema na fadhili za asili, bali *umejeruhiwa* katika umbile lake. Hasa ni kwa sababu tunapozaliwa utashi wetu *haumuelekei Mungu,* lengo lake kuu. Tungezaliwa katika hali ya maumbile tu, utashi ungeweza kumuelekea au kutomuelekea kwa hiari. Kumbe katika hali tunayozaliwa nayo, kutokana na dhambi ya asili, tuko dhaifu katika kushika sheria ya kimaumbile, na pasipo neema hatuwezi kumpenda Mungu kuliko nafsi yetu. Vurugu za tabia mbovu, zinazoonekana wazi kutosha, ni "dalili inayothibitisha kwa kiasi kikubwa uwepo wa dhambi ya asili" (Mt. Thoma wa Akwino) uliofunuliwa na Mungu. Badala ya ulinganifu wa asili kati ya Mungu na roho, roho na mwili, mwili na vitu, zimezuka vurugu pande zote tatu.

Kwa stahili za Mwokozi ubatizo umetuondolea dhambi ya asili na kutupatia neema inayotia utakatifu na maadili ya kumiminiwa: kwa imani akili yetu imeangazwa Kimungu, na kwa tumaini na upendo utashi wetu umeelekezwa kwa Mungu. Lakini hata wabatizwa wanaodumu katika neema inayotia utakatifu, wanaendelea kuwa na *madonda* ambayo pengine yanatia uchungu na ambayo tumeachiwa kama fursa ya kupiga vita na kustahili taji. Mtaguso wa Trento umefundisha kuwa ndani ya waliobatizwa inabaki cheche ya tabia mbovu kusudi washindane nayo kwa neema ya Kristo, na kuwa wasipokubali cheche hiyo haiwezi kuwadhuru. "Utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena… Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake" (Rom 6:6,12).

Tusipoufisha "utu wa kale", tutaendelea kutawaliwa na maono yetu: wasiotambua ukweli huo ni kwamba ndani mwao neema haina nguvu; umimi unawatawala, hata kama silika yao ina maelekeo mazuri yanayodhaniwa kuwa maadili halisi, kumbe siyo. Hatuna haja ya kujuta dhambi ya asili tuliyorithi tu bila ya kuitaka, ila tujitahidi kufuta matokeo yake, hasa tabia mbovu inayotuelekeza kutenda dhambi. Kwa kazi hiyo ya kudumu, madonda tuliyoyazungumzia yanazidi kugeuka makovu kwa ustawi wa neema *ambayo inayaponya na kutuinua* kwenye uzima mpya. Kwa njia ya ufishaji neema haiangamizi umbile, bali inalirekebisha likubali zaidi na zaidi kufanyiwa kazi na Mungu.

**MATOKEO YA DHAMBI ZETU BINAFSI**

Ufishaji unahitajika pia kwa sababu dhambi ikirudiwarudiwa inazaa tabia mbaya inayoitwa kilema. Vilema ni mazoea ya kuona, kupima, kutaka na kutenda yanayojenga roho potovu isiyolingana na Mungu; vinaweza vikajitokeza katika mwili pia, hata ni haki kusema mtu wa makamo amesababisha sura yake iwe ilivyo.

Tukiungama dhambi zetu kwa majuto ya kutosha, ondoleo lake linaacha maelekeo kadhaa yanayoitwa *mabaki ya dhambi;* k.mf. aliyetawaliwa na ulevi, akiondolewa dhambi anabaki na kilema hicho hivi kwamba asipokwepa nafasi ataiangukia tena. Maelekeo hayo mabaya yanatakiwa kufishwa, hasa upande wa kutopendana: "Mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana! Basi nasema: Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." (Gal 5:15). Nafasi ya ufishaji ni pana kwa sababu ya vilema vingi ambavyo vinatokana na mizizi ya dhambi na pengine ni vibaya kuliko hiyo.

Tunapaswa kufanya malipizi kwa dhambi tulizokwishaondolewa, kusudi tusizirudie. Adili la toba halimfanyi tu mtu achukie dhambi kwa kuwa ni kinyume cha Mungu, bali pia aitolee *fidia* haki yake, kwa sababu kila dhambi inastahili adhabu, kama vile kila tendo linalotokana na upendo linavyostahili tuzo. Ndiyo maana katika kitubio tunapoondolewa dhambi tunaagizwa malipizi fulani ili tuondolewe adhabu ya muda ambayo kwa kawaida inadumu kutupasa: hivyo tunalipa walau sehemu ya deni letu. Kwa ajili hiyohiyo tunapaswa kuvumilia tabu za maisha, halafu subira isipotosha kututakasa itatubidi tupitie *toharani:* dogma hiyo inathibitisha haja ya ufishaji, kwa kutuonyesha tunavyopaswa kulipa deni lote, ama duniani ama kisha kufa. Ila majuto yaliyojaa upendo yanaweza yakafuta dhambi na adhabu pia, kama yalivyofanya yale machozi yaliyobarikiwa na Yesu akisema, "Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana" (Lk 7:47). Anayepinga ufishaji atakunywa uovu kama maji, akiziita dhambi nyepesi "mapungufu", na dhambi za mauti "udhaifu wa kibinadamu".

Halafu tusisahau tunapaswa kupambana na roho ya ulimwengu na shetani: "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho" (Ef 6:12). Ili tumshinde shetani, anayetushawishi kutenda kwanza makosa madogo, halafu yale makubwa, Bwana ametuambia tutumie *sala, mfungo na sadaka:* "Namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga" (Math 17:21). Hapo kishawishi kitakuwa nafasi ya kutekeleza imani, tumaini na upendo: tutajikuta tunahitaji kujitahidi na kustahili zaidi tusiridhike na matendo maadilifu mapungufu.

**UKUU WA LENGO LIPITALO MAUMBILE UNADAI UFISHAJI WA PEKEE**

Kwa kuwa tumeitiwa lengo lipitalo maumbile ambalo ukuu wake hauna mipaka - yaani Mungu mwenyewe katika maisha yake ya ndani - haitoshi tufuate akili adili, tukiweka maono chini yake. Tunapaswa kutenda daima kama *watoto wa Mungu,* tukiweka akili chini ya imani, hivi kwamba upendo wa Mungu uongoze matendo yetu yote. Kwa hiyo tunalazimika kutengana na yale yote ambayo ni ya kidunia tu au hayawezi kuwa njia ya kumuendea Mungu na ya kufikisha watu kwake. Tunapaswa kushinda *mahangaiko mbalimbali ya kimaumbile yasije yakatawala utendaji wetu kwa hasara ya uzima wa neema:* "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu… Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi" (Kol 3:1-3,5). "Muda ubakio si mwingi; basi tokea sasa wale walio na wake na wawe kama hawana; na wale waliao kama hawalii; na wale wafurahio kama hawafurahi; na wale wanunuao, kama hawana kitu. Na wale wautumiao ulimwengu huu, kama hawautumii sana; kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita" (1Kor 7:29-31). Tukitaka kweli kwenda kwa Mungu tusiweke makao yetu hapa, bali tutumie maisha haya ili kujipatia uzima wa milele. Lengo letu lipitalo maumbile linadai tujikanie yale yote yaliyo ya kibinadamu tu, hata kama ni halali, tusije tukakwamishwa nayo.

Kwa mfano, "adili la kujipatia la kiasi linadai kwamba katika kutumia vyakula tufuate kipimo cha akili, yaani kiasi kinachoepuka yanayoweza kudhuru afya na kazi za akili na utashi. Kumbe kiasi cha Kikristo kinafuata kipimo cha Kimungu na kudai mtu aupe mwili wake mazoezi magumu na kuutia katika nidhamu kamili kwa kujinyima na kwa njia nyingine za namna hiyo. Lengo lake si la kimaumbile tu, bali ni kutufanya raia pamoja na watu wa Mungu, na watu wa jamaa ya Mungu" (Mt. Thoma wa Akwino). Hayo ni ya kweli zaidi kwa walioshika utume: "Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari" (2Tim 2:4). Vilevile askari wa Kristo asizame katika malimwengu, la sivyo atakuwa kama chumvi iliyoharibika: hapo "itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu" (Math 5:13).

**HAJA YA KUMUIGA YESU MSULUBIWA**

Yesu ametuambia, "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate" (Lk 9:23). Tunapaswa kumfuata Yesu aliyekuja si kufundisha falsafa au elimujamii, bali kutuokoa kwa kufa msalabani. "Kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye. Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu" (Rom 8:17-18).

"Nadhani ya kuwa Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauawe; kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu… Hata saa hii ya sasa, tuna njaa na kiu, tu uchi, twapigwa ngumi, tena hatuna makao… tumefanywa kama takataka za dunia, na tama ya vitu vyote hata sasa" (1Kor 4:9,11,13). "Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; sikuzote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu… Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu" (2Kor 4:8-10,12). Maneno hayo yanachora ukweli wa maisha ya mitume kuanzia Pentekoste hadi kifodini chao: kisha kuchapwa viboko walitoka "katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo" (Mdo 5:41). Walibeba msalaba wakachapwa sura ya Yesu ili waendeleze ukombozi kwa njia alizozifuata yeye. Roho hiyohiyo ya kulingana na Kristo imeonekana katika watakatifu wote, nasi tunapaswa kujilisha kila siku mifano yao. Ulimwengu hauhitaji wataalamu tu, bali hasa watakatifu wanaoleta tena kati ya watu sura hai ya Mwokozi.

Hizo sababu nne za ufishaji zinaweza kujumlishwa katika mbili tu: chuki kwa dhambi na upendo kwa Mungu. Ndiyo roho inayotakiwa kuchochea ufishaji wa nje na wa ndani tutakaozidi kufafanua. Jibu halisi kwa fikra za kidunia ni *kumpenda Yesu msulubiwa;* upendo huo unatufanya tufanane naye na kuokoa watu pamoja naye, tukifuata njia zilezile za kwake. Hivyo ufishaji, badala ya kuangamiza umbile letu, unalikomboa na kulirekebisha. Unatuwezesha kuelewa maana nzito ya msemo huu: *kumtumikia Mungu ni kutawala.* Ni kutawala juu ya maono, juu ya roho ya ulimwengu, juu ya mawazo yake ya uongo, juu ya mifano yake, juu ya shetani na juu ya uovu wake. Ni kutawala pamoja na Mungu kwa kushiriki zaidi na zaidi uzima wake wa ndani, kufuatana na sheria hii: *maisha yasiposhuka chini, yanapanda juu.* Mtu hawezi kuishi bila ya upendo, na akijinyima kila pendo la chini linaloelekeza kwenye mauti, anazidi kufungua roho yake impende Mungu na watu ndani mwake.

## 2.4. *DHAMBI ZA KUEPWA: MIZIZI YAKE NA MATOKEO YAKE*

Baada ya kusema juu ya haja ya ufishaji kwa jumla, inafaa tueleze kuhusu dhambi ambazo ni muhimu zaidi tuziepe, pamoja na mizizi yake na matokeo yake. Mafundisho ya Mt. Thoma wa Akwino yanatuwezesha kujitafiti vizuri, hasa tukimuomba Roho Mtakatifu tuone zaidi madoa ya roho zetu anavyoyaona Bwana. Hapo

vipaji vya elimu na shauri vinaweza vikakamilisha yale yanayosemwa na busara ya Kikristo, inayostawisha ndani mwetu dhamiri nyofu na ya hakika.

**ASILI YA MIZIZI YA DHAMBI**

Mizizi ya dhambi, yaani *majivuno, uzembe, kijicho, hasira, uroho, utovu wa kiasi na uzinifu,* si dhambi kuu kuliko zote; lakini ndivyo vilema tunavyovielekea kwanza na ndivyo vinavyotusogeza zaidi mbali na Mungu na kututumbukiza katika makosa makubwa zaidi, k.mf. uzushi, uasi wa dini, kukata tamaa na kumchukia Mungu. Mtu hafikii uovu mkubwa mara moja, bali polepole, akiteleza kwenye mteremko.

Ni muhimu tutafiti kwanza asili yenyewe ya mizizi saba ya dhambi. Yote inatokana na *kujipendea,* yaani umimi unaotuzuia tusimpende Mungu kuliko yote. "Kujipendea ni chanzo cha kila dhambi" (Mt. Thoma wa Akwino). *"Mapendo mawili yamejenga miji miwili:* kujipenda hadi kumdharau Mungu kumejenga mji wa Babuloni; kumbe kumpenda Mungu hadi kujidharau kumejenga mji wa Mungu" (Mt. Augustino).

Tunampa kisogo kwa sababu tu tunataka kitu kinyume na sheria yake kutokana na kujipendea. Basi, tunatakiwa kufisha hiyo asili ya dhambi yoyote ili tuwe na *upendo safi wa nafsi yetu:* ndio tendo la pili la upendo, ambalo tunajipenda kwa ajili ya Mungu, ili kumtukuza sasa na milele. Mwenye dhambi ya mauti anajipenda kuliko yote na kuliko Mungu. Kumbe mwadilifu anampenda Mungu kuliko nafsi yake, halafu anapaswa kujipenda ndani ya Mungu na kwa ajili ya Mungu; anapaswa kuupenda mwili wake ili usaidie roho, badala ya kuzuia uhai wake wa juu; anapaswa kuipenda roho yake ili aishi milele kwa uzima wa Kimungu; anapaswa kupenda akili yake na utashi wake ili vizidi kuishi kwa mwanga na upendo wa Mungu.

Kujipendea ndio chanzo cha mambo yale matatu yanayotokeza wazi roho ya ulimwengu kuhusu mwili, mali na roho. Dhambi za mwili *zinatia aibu* kuliko zile za roho, kwa kuwa zinatushusha kwenye ngazi ya wanyama; lakini zile za roho (k.mf. kiburi), ambazo peke yake zinapatikana ndani ya mashetani, ni *mbaya zaidi,* kwa kuwa zinapingana na Mungu na kutusogeza mbali naye zaidi.

*Tamaa za mwili* ni kupenda pasipo utaratibu vile vinavyoonekana kufaa kudumishia uhai wetu binafsi na wa ubinadamu kwa jumla; katika pendo hilo lisiloratibiwa vinatokana *utovu wa kiasi na uzinifu.* Hivyo uchu unaweza ukawa mungu wa bandia na kutupofusha zaidi na zaidi.

*Tamaa za macho* ni kupenda pasipo utaratibu vile vyote vinavyopendeza macho: umaridadi, utajiri, hasa pesa inayowezesha kujipatia chochote. Ndipo unapotokea *uroho* ambao tunaifanya hazina yetu iwe mungu wetu tukiiabudu na kuitolea sadaka muda, nguvu, familia, hata uzima wa milele.

*Kiburi cha maisha* ni kupenda pasipo utaratibu ukuu wetu, yale yote yanayoweza kutukuza, hata kama ni magumu. Anayefuata hicho kiburi, mwisho wake anajiabudu kama alivyofanya shetani. Ndipo zinapoweza zikatokea aina zote za dhambi, halafu upotovu wa milele. Kiburi si mmojawapo tu kati ya mizizi ya dhambi, bali ni asili inayochipua hasa vilema vinne vifuatavyo: *majivuno, uzembe, kijicho na hasira.* Majivuno ni kupenda pasipo utaratibu sifa na heshima. Uzembe unahuzunikia kazi ya kulenga utakatifu kwa sababu inadai juhudi na kujikana. Kijicho kinatufanya tusikitikie mema ya wenzetu, kwa kuwa yanaonekana kuzuia ukuu wetu. Hasira (isipokuwa ya haki) ni hali isiyoratibiwa inayotufanya tuyapinge kwa nguvu yale yasiyotupendeza. Vilema hivyo - hasa uzembe, kijicho na hasira - vinazaa huzuni mbaya inayogandamiza roho, kinyume cha amani na furaha zinazotokana na upendo.

Mbegu hizo zote za mauti tunapaswa kuzifisha, si kuziratibu tu: kwanza umimi, unaozaa hayo matatu yanayosababisha mizizi saba ya dhambi: "Kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi" (Rom 8:13). Ukweli huo unaonekana wazi katika maisha ya watakatifu, ambapo neema inakuja kutawala mielekeo yote ya umbile lililoanguka ili kuliponya na kulishirikisha uhai bora zaidi. Haja hiyo ni wazi kwa roho ya Kikristo, na utekelezaji wake wenye bidii unaandaa kutakaswa na Mungu kwa ndani zaidi ili kuangamiza viini vya kifo vilivyobaki bado katika hisi, akili na utashi.

**MATOKEO YA MIZIZI SABA YA DHAMBI**

Mizizi ya dhambi inaitwa hivyo kwa kuwa ni chanzo cha vilema vingine. Hivyo *majivuno* yanazaa ukaidi, majigambo, unafiki, mashindano, kupenda mapyamapya, kushikilia mno rai fulani. Hayo yanaweza yakafikisha kwenye maanguko mabaya zaidi na uasi wa dini. *Uzembe au ukinaifu kuhusu mambo ya Kiroho* unapingana moja kwa moja na upendo wa Mungu na kuzaa uovu wa moyo, kinyongo au ukali kwa jirani, kukosa nia ya kutekeleza wajibu, kukata tamaa, usingizi wa roho, kusahau amri na kutafuta yaliyokatazwa. Wakiteleza kwenye mteremko huo wa kiburi, majivuno na uzembe, wengi wamepoteza wito wao. *Kijicho* kinazaa chuki, masengenyo, masingizio, furaha kwa mabaya yanayowapata wengine na huzuni kwa mafanikio yao. *Utovu wa kiasi* na *uzinifu* vinazaa upofu wa roho, ugumu wa moyo, kushikilia maisha haya hata kupotewa na tumaini la uzima wa milele, kujipendea hata kumchukia Mungu, hatimaye kutotubu wakati wa kufa.

Mara nyingi mizizi hiyo ni dhambi za mauti, ila ni nyepesi ikiwa jambo husika ni dogo au hiari inapolichagua si kamili. Inaweza kupatikana katika namna ya chini, kama inavyowatokea wengi wenye dhambi za mauti, lakini inaweza pia kuwemo ndani ya watu wenye neema inayotia utakatifu kama namna za

upotovu wa maisha ya Kiroho: k.mf. kiburi kuhusu maisha ya Kiroho kinatufanya tuwakwepe wanaotukosoa, hata kama wana haki na mamlaka ya kufanya hivyo, halafu tuwe na kinyongo nao; ulafi kuhusu maisha ya Kiroho unaweza ukatutamanisha faraja za kihisi katika sala, hata tuzitafute kuliko Mungu. Hiyo miwili pamoja inasababisha njozi za bandia n.k.

Tofauti na maadili, vilema havishikamani, hivyo tunaweza kuwa na kimoja pasipo vingine, tena vingine havipatani. Hata hivyo tunapaswa kutekeleza maadili mengi, kama arubaini, na kukumbuka karibu kila moja kati ya hayo ni kilele kati ya vilema viwili vinavyopingana. Tena, kasoro nyingine zinafanana na maadili kwa namna fulani: basi, ni muhimu tuwe na upambanuzi ili kuvitofautisha, la sivyo katika kinanda cha maadili tutatoa noti ambazo hazitakiwi, tukidhani uzembe ni unyenyekevu, ukali ni haki, udhaifu ni huruma.

### KUTAFITI DHAMIRI

Orodha hiyo ya matunda mabovu ya kujipendea inatuelekeza kujitafiti na kukubali upana wote wa ufishaji unaohitajika tukitaka kuishi kwa undani uzima halisi. Kwa kuwa ukweli wa miguso yetu haueleweki kwa urahisi, tunapaswa kufanya utafiti wa makini. Kazi hiyo, badala ya kuondoa mawazo yetu yasimuelekee Mungu, inaturudisha kwake mfululizo. Tunapaswa kuomba mwanga wake ili kujiona kidogo anavyotuona yeye au tutakavyojiona siku ya hukumu. Kila jioni tunapaswa kutafiti kwa unyenyekevu na majuto makosa tuliyoyafanya kwa mawazo, maneno, matendo na kutotimiza wajibu. Lakini tusizidishe kwa kutafuta makosa madogo mno hata tukahangaishwa na kusahaulishwa mambo muhimu zaidi. Lengo si kuorodhesha kikamilifu makosa, bali ni kuona kwa unyofu chanzo chake ndani mwetu. Ili kuponya upele, hatuwazi kuponya vijipu kimojakimoja, bali kusafisha damu. Tusisimame mno kujitazama hata kuacha kumkazia macho Mungu. Kinyume chake tujiulize mbele yake: anatuona vipi? Ndivyo tunavyoona masharti matakatifu ya dhamiri ya Kikristo, yanayopita ya mwanafalsafa yeyote. Tusitenganishe kamwe makosa na huruma isiyo na mipaka, bali tuyaone katika mwanga wa wema wa Mungu ulio tayari daima kusaidia. Hivyo utafiti hautasababisha tukate tamaa, bali utazidisha tumaini letu kwake.

Kuona makosa yetu kunatuonyesha pia *thamani ya maadili* yaliyo kinyume chake. Tunathamini haki hasa tunapoonja uchungu wa kukosewa haki. Ubaya wa uzinifu utuonyeshe thamani ya usafi wa moyo; vurugu za hasira na kijicho zitufanye tuthamini upole na upendo halisi; uharibifu unaotokana na uzembe uchochee ndani mwetu hamu ya juhudi na furaha ya Kiroho; upotovu wa kiburi ututambulishe hekima na ukuu wa unyenyekevu halisi.

Tumuombe Bwana atutie *chuki takatifu kwa dhambi,* kwa kuwa dhambi inatuondolea wema mkuu wa Mungu aliyetujaza fadhili za ajabu na anayetuahidia nyingine za thamani zaidi tukidumu kuwa waaminifu. Kwa namna fulani chuki hiyo ni upande wa pili wa upendo kwa Mungu. Haiwezekani kupenda ukweli pasipo kuchukia uongo, wala kumpenda Mungu pasipo kuchukia yanayotusogeza mbali naye. Watakatifu wanyenyekevu na wapole wana chuki takatifu kwa uovu iliyo na nguvu sawa na upendo wao kwa Mungu. Tujiombee chuki hiyo dhidi ya kiburi na vinginevyo ili upendo halisi kwa Mungu na kwa watu uzidi kustawi ndani mwetu. Njia ya kushinda kiburi ni kuzingatia mara nyingi Mwokozi alivyodhalilishwa, pamoja na kujiombea unyenyekevu. Ili kuzima kijicho tumuombee jirani yale tunayojitakia. Tujifunze pia kuzuia mara hasira ikipanda kwa kusogea mbali na kile kinachoisababisha, pamoja na kuzoea kutenda na kusema kwa upole. Ufishaji huo ni wa lazima. Ili tuendelee kuelekea ukamilifu, tufikirie malipizi ya watakatifu, tukizingatia kuwa sisi pia tunatakiwa kufia dhambi zaidi na zaidi kwa ustawi wa maadili yote, hasa upendo.

## NYONGEZA: DHAMBI ZA UJINGA, UDHAIFU NA UOVU

Kwa ufupi, dhambi ya ujinga ni ile inayotokana na ujinga wa kujitakia na wenye kosa. Dhambi ya udhaifu ni ile inayotokana na maono yenye nguvu ambayo yanapunguza hiari na kuvuta utashi ukubali. Dhambi ya uovu ni ile inayotendwa kwa makusudi mazima, na mara nyingi bila ya maono wala ujinga. Tusidhani dhambi ya uovu tu inaweza kuwa ya mauti: dhana hiyo inatokana na upotovu wa dhamiri na kuchangia kuuzidisha.

### DHAMBI ZA UJINGA

Ujinga usioshindikana si dhambi; ila ujinga wa hiari kuhusu mambo tunayoweza au tunaopaswa kuyajua ni dhambi kadiri ya ukubwa wa wajibu ambao mtu hautimizi. Kwa sababu alifanya uzembe, ujinga huo hauwezi kumtetea, ila unapunguza kosa lake; kumbe unamtetea asipoweza kuachana nao kwa kuwajibika. Haukubaliki kuhusu mambo makuu ya sheria ya kimaumbile, k.mf. "ni lazima kutenda mema na kukwepa maovu"; "usimtende mwenzako usiyopenda kutendwa"; "usiue"; "usiibe"; "umuabudu Mungu mmoja tu". Kwa sababu walau katika utaratibu wa ulimwengu mtu anahisi kwa urahisi uwepo wa Mungu, mratibu wake; na kisha kuhisi hivyo anatakiwa kujitahidi kujua zaidi na kuomba mwanga wa juu. Ni vilevile kwa Mprotestanti aliyehisi kuwa Kanisa Katoliki ndilo la kweli: asipojitahidi kusoma na kuomba mwanga wa Mungu anatenda dhambi dhidi ya imani, kwa kuwa hataki kushika njia za lazima ili kuifikia.

Wenye moyo wa ibada mara nyingi hawafanyi bidii za kutosha ili kukwepa dhambi za ujinga, wakizitenda kwa kutozingatia --kadiri wanavyoweza na wanavyopaswa - majukumu yao ya kidini au ya hali yao, au haki na sifa za watu wanaohusiana nao. Tunapaswa kuchukua jukumu la mema yote tusiyoyatenda ingawa

yanatupasa, na ambayo tungeyatenda kama tungekuwa na juhudi kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa watu.

**DHAMBI ZA UDHAIFU**

Roho ni dhaifu inaposhindwa na nguvu za maono yanayofanya akili iyaone kuwa yanafaa, na utashi uyakubali kinyume cha sheria ya Mungu. Tutofautishe *maono yanayotangulia* kibali cha utashi, na *maono yanayokifuata.* Yanayotangulia yanapunguza kosa kwa kupunguza hiari katika kupima na kuchagua la kutenda, hasa kwa watu wepesi kuguswa. Kinyume chake maono yanayofuata ni dalili ya kuwa dhambi ni ya hiari, kwa kuwa utashi wenyewe unachochea maono, k.mf. mtu akitaka kukasirika ili kuonyesha hana nia njema na mwingine.

Dhambi ya udhaifu ni ile ambayo utashi unashindwa na nguvu ya maono yanayotangulia, na kwa hiyo uzito wake umepungua; lakini si kwamba haiwezi kamwe kuwa ya mauti. Hakika ni ya mauti ikihusu jambo kubwa, pamoja na kujua na kutaka, k.mf. mtu anapoua kwa hasira. Hasa mwanzoni anaweza kujizuia na kujiombea msaada wa Mungu: asipofanya hivyo, maono yanakuwa ya hiari. Dhambi ya udhaifu, hata ikiwa ya mauti, inaweza kusamehewa kwa urahisi kuliko nyingine.

Wenye moyo wa ibada nao wanatakiwa kujihadhari wasije wakapatwa na makosa makubwa kutokana na kijicho kisichozuiliwa, k.mf. kuhukumu bila ya msingi kwamba wengine wana dhambi kubwa, au kusema na kutenda kwa namna inayosababisha mafarakano makubwa, kinyume cha haki na upendo.

**DHAMBI ZA UOVU**

Anayetenda dhambi kwa uovu, akijua na kutaka, ni kwamba *anakusudia* jambo lililo baya kwa roho (k.mf. kupotewa na urafiki wa Mungu) ili kupata jema la kidunia. Si kwamba kila dhambi ya uovu ni ya kumkufuru Roho Mtakatifu: hiyo ni kati ya dhambi za uovu zilizo kubwa zaidi, na inafanyika mtu anapodharau yale yanayoweza kumuokoa au anaposikitikia kwa makusudi neema na maendeleo ya Kiroho ya jirani kutokana na kijicho.

Ni wazi kuwa dhambi ya uovu ni kubwa kuliko zile za ujinga na za udhaifu (ingawa hizo pia zinaweza kuwa za mauti): ndiyo sababu sheria za binadamu zinaadhibu vikali mauaji yaliyopangwa kuliko yale yanayotokana na maono. Uzito mkubwa wa dhambi za uovu unatokana na kwamba utashi unahusika kuliko unavyohusika na dhambi nyingine, bila ya kutetewa kiasi na ujinga wala maono yenye nguvu; mara nyingi zinasababishwa na kilema kinachotokana na marudio ya makosa.

Katika suala hilo tunaweza kudanganyika kwa namna mbili tofauti. Baadhi wanadhani dhambi ya uovu tu inaweza kuwa ya mauti, wasione uzito wa dhambi kadhaa za ujinga wa kujitakia, na za udhaifu zenye jambo kubwa, ujuzi wa kutosha na nia kamili. Kumbe wengine hawaoni uzito wa dhambi kadhaa za uovu zilizotendwa bila ya ono lolote, kama kwa utulivu wa nafsi: wale ambao kwa namna hiyo wanapinga dini ya kweli na kuzuia watu wanyofu wasijue ukweli wa Mungu, wanaweza kutenda dhambi kubwa kuliko mtu ambaye anamkufuru Mungu au kuua kwa hasira. Tunapaswa kuzingatia hasa akili na utashi, vilivyo sehemu zetu za juu. Kosa ni zito kadiri lilivyo la hiari, linavyotendwa kwa kujua na linavyotokana na kujipendea ambako pengine hatima yake ni kumdharau Mungu. Kinyume chake, tendo adilifu linastahili kadiri lilivyo la hiari na linavyotokana na upendo mkubwa kwa Mungu na kwa jirani. Kwa msingi huo, mtu anayesali kwa kushikamana mno na faraja za kihisi anastahili kidogo kuliko yule anayedumu kusali pasipo faraja yoyote, katika ukavu wa mfululizo; lakini huyo akitoka hali hiyo, stahili zake hazipungui ikiwa sala yake inatokana na upendo uleule ambao sasa una mwangwi katika hisi zake. Basi, ikiwa tendo baya la makusudi mazima (k.mf. agano na shetani) lina matokeo ya kutisha, tendo jema ambalo linatendwa kwa makusudi mazima na kurudiwa mara nyingi (k.mf. kujitoa kwa Mungu) linaweza kuwa na matokeo mema makubwa, kwa sababu Roho Mtakatifu anaweza kututakasa kuliko shetani anavyoweza kutupoteza. Tena yumo ndani mwetu kuliko tulivyo sisi wenyewe, naye anaweza kutuelekeza kwa nguvu na upole tutende yaliyo ya hiari na stahili, ya ndani na ya juu zaidi.

## 2.5. ***KILEMA TAWALA: MDUDU ANAYEKULA NDANI KWA NDANI***

Baada ya kusema juu ya dhambi ambazo tuziepe, pamoja na mizizi na matokeo yake ambavyo tuvifishe, tuseme kwa namna ya pekee juu ya kilema kinachotawala ndani ya kila mmoja wetu.

**KILEMA TAWALA NI KIPI?**

Ni kile kinachoelekea kutawala vingine pamoja na namna yetu ya kuona, kupima, kuhisi, kutaka na kutenda. Kinahusiana na tabia ya nafsi, ambayo ni kawaida yake *kuelekea upande mmoja.* Kuna tabia ambazo zinaelekea uzembe, ulafi na uzinifu; nyingine zinaelekea hasira na kiburi. Ndiyo sababu zinahitaji kukamilishwa na maadili mbalimbali, yanayotuwezesha kutenda kadiri ya akili na imani katika nafasi na kwa watu tofauti. Hatupandi wote upande mmoja kuelekea kilele cha ukamilifu; wenye tabia ya ulegevu wanatakiwa kupata nguvu kwa sala, neema na maadili; kumbe walio na nguvu kimaumbile wanatakiwa kujifanya wapole kwa msaada wa neema.

Kabla tabia haijabadilika hivyo hatua kwa hatua, kilema tawala cha kila mmoja kinajitokeza mara nyingi. Ndicho *adui yetu wa ndani* anayeweza kuangamiza kazi ya neema: ni kama ufa katika ukuta unaoonekana imara, kumbe sio, hivi kwamba tikisiko la nguvu linaweza kuubomoa. Kilema tawala ni cha hatari zaidi kwa sababu mara nyingi kinaathiri sifa yetu bora, yaani elekeo jema la umbile letu linalokusudiwa kustawishwa na kuinuliwa na neema. Mmoja anaelekea kimaumbile kuwa mpole, lakini ikiwa kilema chake tawala (pengine ni uzembe) kinaugeuza upole kuwa udhaifu unaoruhusuruhusu maovu yatendeke tu, atafikia hatua ya kukosa nguvu yoyote. Kinyume chake mwingine anaelekea kimaumbile kuwa hodari, lakini akikubali kutawaliwa na hasira, nguvu yake itatumika kwa ukatili na kusababisha vurugu za kila aina, k.mf. kugombana badala ya kushirikiana na wenzake katika shamba la Bwana.

Pamoja na kilema tawala ndani ya kila mmojawetu mna *mvuto maalumu wa neema* ambao kwa kawaida unaanza kukamilisha yaliyo bora katika umbile letu, halafu unakuja kuenea kwa yasiyo bora. Adui yetu analenga kustawisha zaidi na zaidi kilema tawala kiusonge mvuto maalumu wa neema ndani yetu. Hivyo tunaweza kuhisi hasara ambayo huenda ikatupata tusipokesha kushinda kilema hicho, ambacho ni kama mdudu anayekula tunda zuri ndani kwa ndani.

**TUNAWEZAJE KUTAMBUA KILEMA KINACHOTUTAWALA?**

Ni muhimu kukitambua tusijidanganye. Ujuzi huo unahitajika zaidi kwa sababu adui yetu anakijua fika na kukitumia ili kuvuruga ndani mwetu na kandokando yetu. Katika ngome ya maisha ya Kiroho, inayolindwa na maadili mbalimbali, kilema tawala ni kama *sehemu dhaifu* isiyolindwa. Basi, tukitambuaje? Kwa wanaoanza ni rahisi wakiwa wanyofu. Ila baadaye kinaelekea kufichama na kujidai ni adili: kiburi kinajidai ni moyo mkuu, na uzembe unajidai ni unyenyekevu. Hata hivyo ni lazima tukifichue ili tupambane nacho, la sivyo hatutakuwa na maisha halisi ya Kiroho.

Kwanza tunapaswa *kumuomba Mungu atuangazie:* "Bwana, unijulishe vizuio ambavyo, kwa kujua au kutojua, ninazuia kazi yako ndani yangu; halafu unipe nguvu ya kuviondoa, na nisipofanya hivyo kwa bidii, tafadhali uviondoe mwenyewe, hata kama itanipasa kuteseka. Sitaki kingine isipokuwa wewe, Bwana, ambaye peke yako ni wa lazima kwangu. Unijalie maisha yangu hapa duniani yawe kama mwanzo wa uzima wa milele". Baada ya kuomba hivyo kwa unyofu, tunapaswa kujitafiti kwa makini kwa *kujiuliza* mahangaiko yetu ya kawaida tunapoamka au kubaki pweke yanaelekea wapi. Mawazo na matamanio yetu yanaelekea wapi? Katika kufanya hivyo tukumbuke kuwa kilema kinachotawala kwa urahisi maono yetu yote kinajidai ni adili na kutuzuia tusitubu, ilivyomtokea Yuda asiyejua wala kutaka kutawala uroho. Tunapaswa pia kujiuliza juu ya *chanzo* cha kawaida cha huzuni na furaha yetu, sababu kuu ya matendo yetu, asili ya kawaida ya dhambi zetu, hasa zile ambazo zinajirudiarudia au kudumu muda fulani kama kwa kupinga neema. Tunapaswa kujiuliza tena *kiongozi* wetu wa Kiroho anawaza nini kuhusu kilema chetu tawala. Pengine ameshakitambua na kujaribu kusema nasi juu ya hicho, lakini tukajitetea. Hiyo ni rahisi kwa sababu kilema tawala kinachochea maono yote, na kujibu kwa dharau, hasira au utovu wa subira, kwa kuwa hakitaki kutambulikana na kupingwa. Hivyo jirani akitukosoa kuhusu hicho, pengine tunajibu, "Naweza kuwa na vilema vyote, isipokuwa hicho". Tunaweza kutambua kilema tawala hata kwa kuzingatia *vishawishi* ambavyo adui anasababisha mara nyingi zaidi ndani mwetu, kwa sababu ni kawaida yake kutushambulia hasa upande huo dhaifu. Hatimaye, tunapowaka juhudi kweli, *mianga ya Roho Mtakatifu* inatuomba sadaka hasa katika hicho.

Tukifuata kwa unyofu njia hizo, haitakuwa vigumu kutambua adui wa ndani anayetufanya watumwa: ni kama gereza tunalotembea nalo popote tuendapo. "Amin, amin, nawaambia: Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi" (Yoh 8:34). Kwa hiyo tunatakiwa kutamani ukombozi. Ni neema kubwa kukutana na mtakatifu atuambiaye, "Tazama kilema kinachokutawala na tazama pia mvuto maalumu wa neema ambao uufuate kwa bidii ili kufikia muungano na Mungu". Ndivyo Bwana alivyowaita "Boanerge, maana yake, wana wa ngurumo" (Mk 3:17) vijana Yakobo na Yohane waliotaka kuamuru "moto ushuke kutoka mbinguni, uwaangamize" Wasamaria waliokataa kumpokea Yesu; lakini yeye "akawageukia, akawakanya. Akasema, Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo. Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa" (Lk 9:53-55). Kwa kumfuata Mwokozi hao Boanerge wakawa wapole, hata Yohane mwishoni mwa maisha yake alikuwa hajui kusema lingine isipokuwa, "Wapenzi, na tupendane" (1Yoh 4:7). Akiulizwa kwa nini anarudiarudia hilohilo, alikuwa akijibu, "Ndiyo amri ya Bwana: ukiishika, umemaliza kazi". Katika hatua hiyo, ari yake ilikuwa imegeuka ya Kiroho na kuendana na upole.

**TUNAWEZAJE KUPAMBANA NA KILEMA TAWALA?**

Ni lazima tupambane nacho kwa kuwa ndicho adui mkuu wa ndani, ambacho kikishindwa, vishawishi vitakuwa fursa za maendeleo kuliko hatari. Ila hatuwezi kusema kilema hicho kimeshindwa kabla hayajapatikana maendeleo halisi ya Kiroho, kabla hatujafikia ari halisi ya kudumu, yaani kabla utashi haujawa tayari kumtumikia Mungu daima. Kwa mapambano hayo tufuate njia kuu tatu: sala, utafiti na adhabu. Tusali kwa unyofu, "Bwana, unionyeshe kizuio kikuu cha utakatifu wangu, kinachonizuia nisifaidike na neema zako na matatizo yanayoweza kuchangia ustawi wa roho yangu". "Bwana, uniondolee yale yote

yanayonizuia nisifike kwako; unijalie yale yote yanayoweza kunifikisha kwako; ujichukulie nafsi yangu, na kujipatia kabisa mwenyewe” (Mt. Nikola wa Flue). “Bwana, unichome moto hapa duniani, na kunikausha hapa duniani, ili unihurumie milele” (Mt. Ludoviko Bertrand). Sala hiyo haitusamehe utafiti, bali inatuelekeza kuufanya. Tena inafaa, hasa kwa wanaoanza, tuandike kila wiki tumeshindwa mara ngapi na kilema tawala. Tukihesabu mapato na matumizi ya fedha, tujue zaidi mapato na hasara upande wa uzima wa milele. Inafaa pia tujipangie adhabu kwa kila tutakapoangukia kilema hicho ili turekebishe kosa, tutoe fidia inayostahili na tuwe macho zaidi siku za mbele.

Kabla hatujashinda kilema chetu tawala, yale tunayodhani ni maadili yetu, mara nyingi ni maelekeo mazuri ya umbile tu; chemchemi ya neema haijafunguka vya kutosha juu yetu kwa sababu bado tunajipendea mno tusiishi kwa ajili ya Mungu kweli.

Hatimaye tushinde hali ya kukata tamaa inayotufanya tudhani kilema tawala kisiweze kung’olewa kwa neema ya Mungu. Katika jambo hilo mapambano ya kudumu na ya nguvu ni ya lazima kuliko ushindi, kwa sababu tukijisamehe kupambana, tunaacha maisha ya Kiroho. Hatutakiwi kamwe kupatana na kasoro zetu, la sivyo hatuwezi kulenga ukamilifu unaotupasa, wala kuwa na furaha ya ndani na amani, kwa kuwa hiyo inatokana na moyo wa kujitoa sadaka unaofisha ndani mwetu yale yote yasiyoratibiwa. Kwa njia hiyo tu upendo unafaulu kushinda kilema tawala na kushika nafasi ya kwanza rohoni mwetu. Ufishaji wa kilema tawala unatuweka huru na kuhakikisha mvuto maalumu wa neema utawale ndani mwetu. Hivyo polepole tunafikia *kuwa wenyewe* kupita umbile letu, pasipo kasoro zetu. Si suala la kuiga sifa za wengine wala la kuganda wote namna moja, kwa kuwa binadamu ni mbalimbali kama maua. Lakini hatutakiwi kutawaliwa na tabia, bali kuirekebisha kwa kudumisha yaliyo mema ndani yake na *kuyatia chapa ya maadili,* hasa yale ya Kimungu. Hapo, badala ya kujifanya kiini cha yote - kama tukitawaliwa na kilema fulani - tunajisikia *kuelekeza yote kwa Mungu,* kumfikiria karibu mfululizo, kuishi kwa ajili yake tu, na kuwavuta kwake wale wote wanaotujia.

Ili tujifahamu zaidi, inafaa tubadili pengine utaratibu wa kutafiti dhamiri, kwa kufuata mara amri za Mungu na za Kanisa, mara maadili ya Kimungu na ya kiutu, mara dhambi zinazopingana nayo, kadiri ya majedwali yafuatayo:

- Kujipendea
  - kiburi
    - kwake
      - MAJIVUNO yanazaa ukaidi, majigambo, unafiki, mashindano, kupenda mapyamapya, kushikilia mno rai fulani.
      - UZEMBE unazaa uovu wa moyo, kinyongo, kukosa nia ya kutekeleza wajibu, kukata tamaa, usingizi wa roho, kusahau amri, kutafuta yaliyokatazwa.
    - kwa jirani
      - KIJICHO kinazaa chuki, masengenyo, masingizio, furaha kwa mabaya yanayowapata wengine, huzuni kwa mafanikio ya wengine.
      - HASIRA inazaa mabishano, milipuko, matusi, ugomvi, kukufuru majina matakatifu.
  - 
    - ya macho
      - UROHO unazaa kutoaminika, utapeli, ujanja, viapo vya uongo, mafadhaiko, uchoyo, ugumu wa moyo.

| | | |
|---|---|---|
| tamaa ya mwili | | ULEVI NA ULAFI unazaa michezo kwa wakati usiofaa, porojo, machafu, mazungumzo yasiyo na maana, upumbavu.<br>UZINIFU unazaa upofu wa roho, kutozingatia mambo, kutenda bila ya kufikiri, ugeugeu, kumdharau Mungu, kushikilia maisha haya hata kupotewa na tumaini la uzima wa milele. |

| **MAADILI** | **VILEMA VINAVYOPINGANA NAYO** |
|---|---|
| **Ya Kimungu** | |
| UPENDO kwa Mungu na kipaji cha hekima | Ukinaifu wa mambo ya Kiroho |
| UPENDO kwa jirani na huruma | Kijicho, mashindano, vikwazo |
| TUMAINI na kipaji cha uchaji | Kukata tamaa, kujiamini kipumbavu |
| IMANI na vipaji vya akili na elimu | Kutoamini, kukufuru, upofu, ujinga wa kujitakia |
| **Ya kiutu** | |
| BUSARA, usikivu na kipaji cha shauri | Upumbavu, ulegevu, ujanja |
| HAKI, ibada, toba, utiifu, shukrani, unyofu, uaminifu, ukarimu na kipaji cha ibada | Udhalimu, utovu wa ibada, ushirikina, unafiki, uongo |
| NGUVU, moyo mkuu, subira, udumifu na kipaji cha nguvu | Ushupavu, kutowajibika, woga |
| KIASI, usafi wa moyo, upole na unyenyekevu | Utovu wa kiasi, uzinifu, hasira, kiburi, udadisi |

## 2.6. *MAONO YA KURATIBIWA*

Maisha ya Kiroho hayawezekani tusipojitahidi mfululizo turatibu maono yetu, kama vile tunavyotumia nidhamu ili kumlea kijana.

**MTAZAMO WA ELIMUNAFSIA**

Ono ni "badiliko la hisi linalotokana na kukabili jema au baya la kihisi na linaloendana na tukio la kimwili katika muundo wake, k.mf. pigo la moyo" (Mt. Thoma wa Akwino). Mabadiliko ya utashi ni ya roho tu, kumbe ono linaendana daima na tukio la kimwili kwa sababu hisi zinaendana na viungo. Maono yamo hata katika wanyama. La kwanza na la msingi ni pendo la kihisi; kutokana nalo kuna hamu, furaha, tumaini na ujasiri, au chuki kwa kilicho kinyume chake, kukipinga, huzuni, kukata tamaa, hofu na hasira. Hivyo ono si hai, kali na tawala daima.

**MTAZAMO WA MAADILI**

Watetezi wa anasa wanasema maono yote ni maadilifu, kama ustawi wa umbile letu; kinyume chake wengine wanayahukumu kwa kuwa yanapingana na akili na kuvuruga roho. Kumbe kwa yenyewe si maadilifu wala maovu, ila *yanakuwa maadilifu kadiri yanavyochochewa au kuratibiwa na akili na utashi* yaelekee lengo adilifu. La sivyo yanakuwa maovu kwa kutolingana na akili nyofu na kulenga yasiyokubalika. Bwana alikusudia kuonyesha hasira takatifu alipofukuza wafanyabiashara hekaluni na kupindua meza zao. Vivyo hivyo bustanini alikusudia kuwa na "huzuni nyingi kiasi cha kufa" (Mk 14:34) ili tuelewe huzuni inayotupasa kuhusu dhambi zetu.

Tendo linastahili zaidi likitumia maono kulifikia lengo adilifu, kwa kuwa Mungu ametujalia hisi vile alivyotujalia kumbukumbu, ubunifu na mikono ili tuvitumie kutendea mema. Kwa msingi huo, "haiwezekani kutenda chema kikubwa pasipo maono" (B. Pascal), yaani pasipo hisi kuwaka ari ya upendo. Kinyume chake, maono yasiyoratibiwa yanakuwa vilema: pendo la kihisi linakuwa ulafi na uzinifu, chuki ya kihisi inakuwa wivu na kijicho, hofu inakuwa woga na kutotimiza wajibu. Hapo, badala ya kuwa nguvu kwa ajili ya kutenda mema, yanakuwa nguvu kwa ajili ya kutenda maovu.

**MTAZAMO WA MAISHA YA KIROHO**

Kutokana na hayo, maono hayatakiwi kung'olewa, bali kuratibiwa kusudi tusiwe baridi kama watu walioganda, wala wakali kama mito iliyofurika. Hapo hisi zetu hazitafanana na zile za mnyama, bali zitalingana na hadhi yetu kama viumbe vyenye akili na kama watoto wa Mungu. Tufikirie hisi za Yesu zilivyokuwa kutokana na usafi wa moyo, subira na udumifu hata msalabani. Hapo tutaona jinsi hisi zetu zinavyotakiwa kuwa zaidi na zaidi chini ya akili iliyoangazwa na imani, chini ya utashi uliohuishwa na upendo, na jinsi mwanga na moto hai wa Roho vinavyotakiwa kuenea katika maono yetu ili kuyatakasa na kuyatumia kwa kumtumikia Mungu na jirani. "Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao" (Rom 12:15). Watakatifu wana uwezo mkubwa ajabu wa kushiriki maono ya wenzao. Pengine wao tu wanajua neno la kuwatia moyo wenye huzuni.

Kwa hiyo tunapaswa kuratibu maono kulingana na lengo na hali. Katika nafasi ngumu tunaweza kuonja huzuni, hofu au hasira kubwa bila ya kutenda dhambi. Musa alipoona Waisraeli wanaabudu ndama wa dhahabu alikasirika na kuwaadhibu vikali (taz. Kut 32:19-20); kinyume chake kuhani Eli alilaumiwa kwa kutokasirikia ulaghai wa wanae (taz. 1Sam 3:11-14). Katika kupanda farasi ni lazima kutumia mara hatamu mara kiboko; vilevile ni lazima pengine kuyazuia maono, pengine kuyachochea ili kujishtua dhidi ya uzembe, aibu na woga. Ni kazi ngumu kumtawala farasi mwenye nguvu, na vilevile kuratibu tabia zenye uwezo wa kutenda makuu. Lakini jinsi inavyopendeza, baada ya miaka 10 au 15 ya mapambano na nafsi yetu, kuona tabia imebadilika na kutiwa chapa ya Kikristo!

Hasa mwanzoni mwa maisha ya Kiroho tuepe kutenda bila ya kufikiria vya kutosha, wanavyofanya wengi. Hiyo ni dhambi dhidi ya busara na ya kipaji cha shauri, na inafikisha kuhukumu bila ya msingi: ni kama mtu anayeshuka ngazi haraka mno hata akaanguka, jambo ambalo lisingetokea kama angeteremka taratibu. Tunatakiwa kuzingatia kwanza lengo la kulifikia hadi kazi ya kuitenda, pasipo kupuuzia yaliyopo katikati, yaani *kumbukumbu* ya yaliyopita*, uzingatifu* wa hali ya sasa, *uwezo wa kutabiri* vizuio vinavyoweza vikatokea, *usikivu* wa kufuata mashauri muhimu. Ni lazima tuchukue muda ili kuamua polepole kabla hatujatenda, halafu itatupasa pengine kutenda mara moja. Lakini tukitenda kwa msukumo wa utashi au maono, pasipo kupitia hayo tutayumba na kuanguka.

Haraka hiyo inatokana na kwamba *utendaji wa kimaumbile unashika nafasi ya utendaji wa Kimungu;* tunatenda kwa kuhemka, pasipo kufikiria, wala kuomba mwanga, wala kushauriwa na kiongozi wa Kiroho. Hiyo haraka ya kimaumbile inasababisha matendo ambayo yanakosa busara na hivyo yana matokeo ya kusikitisha. Mara nyingi inatokana na kuzingatia tu lengo la mara moja bila ya kuona linavyohusiana na lengo kuu linalotupasa: hapo kwa kuona tu lengo la kibinadamu tunalikusudia kibinadamu kwa utendaji wa kimaumbile, pasipo kuomba vya kutosha msaada wa Mungu.

Haraka tunayozungumzia inaweza ikawafanya vijana wenye juhudi watake kufikia ukamilifu mapema kuliko neema inavyowajalia, wakiruka vituo, wasizingatie hatua za katikati wala haja ya kuratibu maono. Inawatokea kama wanafunzi ambao mwanzoni mwa masomo wanajitahidi kutokana na upya wa mambo; lakini udadisi ukiisha, au juhudi zikihitajika zaidi, unafuata uzembe. Wanaingia hatari ya kudanganyika, halafu udanganyifu ukiisha, wanatumbukia uzembe na kuacha nia ya kutimiza wajibu. Hatuwezi kufikia mara uwiano mzuri wa uadilifu. Tunapaswa kutembea kasi, lakini pia kutopiga "*hatua kubwa nje ya njia"* (Mt. Augustino). Matokeo ya haraka hiyo ni kupoteza utulivu wa ndani na kupatwa na mafadhaiko na mahangaiko ambayo hayazai kitu ila yanafanana kijuujuu na utendaji wa kufaa. Dawa ni *kujiweka chini ya Mungu* na kulinganisha matakwa yetu na ya kwake. Hatutaridhika zaidi na nafsi zetu, ila tutaona amani kubwa, na mara kwa mara furaha halisi ndani ya Mungu.

Ili turatibu maono tunapaswa kuangalia na kupinga: upande mmoja umotomoto wa tabia unaoendana na kujiamini mno, upande mwingine uzembe na uvivu ambavyo vinaleta madhara makubwa zaidi katika maisha ya Kiroho. Kuhusu kazi hiyo ya polepole lakini ya kudumu moja kwa moja, tujitafiti kila siku, na kuona umuhimu wa kujiratibu katika mwenendo au, kwa kusema vizuri zaidi, umuhimu wa kudumu waaminifu kwa neema ambayo tusipokuwa nayo hatuwezi kufanya kitu upande wa wokovu. Hapo ujasiri utasaidia adili la nguvu kutawala hofu ya kihisi. Vilevile upole utairatibu hasira itokane tu na ari ambayo ina subira bila ya kupotewa na umotomoto wake: hiyo ni dalili ya utakatifu.

## 2.7. *KUJITAKASA UPANDE WA HISI*

Tulipoeleza ufishaji kwa jumla, tumeona ni wa lazima kwa sababu nne. Sasa tuone utekelezaji wake kuanzia hisi zetu, kwa kuzungumzia ufishaji wa tamaa za mwili na wa hasira.

**KWELI ZA KUZINGATIWA**

Tukumbuke kwanza haja ya kushika amri, hasa ile kuu ya upendo, kwa kukwepa kila dhambi ya mauti, halafu polepole hata zile nyepesi za makusudi. Ingawa hatuwezi kukwepa mfululizo dhambi zote nyepesi - tusipojaliwa msaada wa pekee kama bikira Maria - tunaweza kukwepa kila mojawapo. Tuzidi pia kukwepa matendo mapungufu, ambayo ni mema kiasi tu. Jambo jema kiasi si baya, lakini linaonyesha hatuna bidii

zinazotakiwa katika utumishi wa Mungu. *Katika maadili hatupaswi kusimama katika ngazi ya chini,* bali kulenga juu; hasa vipaji vya Roho Mtakatifu vinatufanya tujitahidi zaidi ili kuendelea kwa kasi. Lakini juhudi hizo pia zina ngazi nyingi, kadiri tunavyotaka kupanda mlima wa ukamilifu kwa njia rahisi ya mzunguko, au kwa njia ya mkato inayofika haraka na juu zaidi.

Halafu tukumbuke kuwa mizizi ya dhambi inaelekeza kutenda dhambi nyingine ambazo mara nyingi ni kubwa zaidi. Hatuwezi kamwe kumuomba mno Mungu atuangazie ubaya wa dhambi na kutupatia majuto kamili. Hayo na upendo wa kidugu ni dalili kuu za maendeleo.

Tukumbuke pia kuwa dhambi nyepesi, hasa ikirudiwarudiwa, inaelekeza kutenda ya mauti, kwa sababu anayetenda kwa urahisi dhambi nyepesi anapotewa na nia safi, hivyo nafasi ikipatikana anafikia hatua ya kutenda ya mauti. Kwa hiyo dhambi nyepesi iko kwenye mteremko wa kutisha; ni kama ukuta unaotuzuia tusifikie muungano na Mungu. Vilevile matendo mapungufu, yaani uhaba wa juhudi, yanatuelekeza kutenda dhambi nyepesi; ingawa yanastahili, yanatuelekeza kuteremka, kwa maana hayapingani inavyotakiwa na maelekeo yanayoweza kutuangusha. “Mara nyingi *subira ya bandia* ni utovu tu wa juhudi katika njia ya maendeleo; kwa baadhi ya watu hatua ni za polepole kiasi kwamba labda Mungu mwenyewe atahukumu kwamba wamekuwa na subira nyingi mno!” (Mt. Yohane wa Msalaba).

**KUFISHA TAMAA ZA MWILI**

Nje ya ndoa, furaha za kijinsia *zilizokusudiwa* ni dhambi za mauti. Jambo hilo halina udogo, kwa sababu kulikubali kunatuelekeza kukubali lingine kubwa zaidi; ni kuingiza kidole mashineni, matokeo yake mkono mzima utashikwa nayo. Ni mzizi wa dhambi unaozaa kutozingatia mambo, ugeugeu, upofu wa roho, kujipendea hata kumdharau Mungu na kukata tamaa ya wokovu. Kuufisha ni kuhakikisha uhuru wa roho kuishi maisha yake bora isilemewe na mwili. Kwa ajili hiyo Kanisa limeagiza siku za kufunga na kujinyima nyama. Kuna magumu mengine pia tunayoweza kuyakusudia badala ya starehe. Waanzilishi wa mashirika wamepanga magumu ya pekee, kama kukesha na kujipiga viboko, zoezi ambalo linakinga na makosa, linadumisha upendo kwa maisha magumu, linatoa fidia kwa mapungufu na kuwafungua wengine waliojifunga. Utawani taratibu za sala na sadaka ni kama ganda la mti: ukiliondoa lote, utomvu hauwezi kupanda juu tena, hivyo mti unakauka. Tukilegeza taratibu hizo, tutalegeza roho pia zisiwe na nguvu zinazohitajika ili kupiga mbio katika njia ya ukamilifu.

Uzinifu unashindwa kwa kukimbia nafasi za hatari kuliko kwa kuzikabili ambako kungetufanya tufikirie mno jambo la kuvutia. Tukwepe iwezekanavyo yanayochochea ashiki hata tusipoikusudia, hasa kama kuna hatari kubwa ya kuikubali. Kwa hiyo inawafaa wengi wakwepe vitabu (k.mf. vya uganga) vinavyoweza vikawa vya hatari kwa udhaifu wao, hasa wakivisoma kwa udadisi, si kwa wajibu. Tukeshe pia kuhusu mapendo yanayoweza kugeuka ya kihisi na kupoteza amani ya moyo wetu. “Mapendo ambayo asili yake ni hisi kuliko ibada yakikumbukwa hayaongezi kumbukumbu ya Mungu wala upendo wake, bali matokeo yake ni lawama ya dhamiri” (Mt. Yohane wa Msalaba). Tusizoeane mno na viumbe ili tufurahie urafiki na Bwana. Aina nyingine za urafiki ni tauni halisi, nazo polepole zinapoteza juhudi za Kiroho, taratibu za kijumuia, pengine zinazaa mafarakano makubwa, hata kuhatarisha wokovu wa milele. “Kateni, vunjeni, pasueni; haitoshi kufumua aina hizo za urafiki kichaa, mnapaswa kuzing’oa pasipo huruma; haitoshi kufungua vifungo, tunapaswa kuvivunja na kuvikata” (Mt. Fransisko wa Sales). Ili tufaulu zaidi tunapaswa kufikiria mengine na kuzama katika wajibu. “Huwa tunaanza na upendo mwadilifu, lakini tusipoangalia utachanganyikana na mapendo ya juujuu, halafu ya kihisi, hatimaye ya kimwili” (Mt. Fransisko wa Sales). Katika urafiki wenye mchanganyiko huo, ikiwa upande wa roho unatawala, tunaweza kuudumisha pamoja na kuutakasa zaidi na zaidi kwa kuchunguza hisi na moyo; lakini upande wa hisi ukitawala, ni lazima kuusimamisha kwa muda mrefu kwa kuacha fungamano lolote lisilo la lazima. Hapo ufishaji wa moyo unahitajika sawa na ule wa mwili na wa hisi.

Hatimaye katika sala tusitafute faraja za kihisi kwa *ulafi wa roho.* Ulafi wa kawaida unazaa michezo kwa wakati usiofaa, porojo, mazungumzo yasiyo na maana, upumbavu na uchafu; ulafi wa roho, ambao matokeo yake yanafanana na hayo, unapatikana mara nyingi kwa wanaoanza: “Wanatamani furaha ya roho kuliko usafi wake na ibada halisi” (Mt. Yohane wa Msalaba). Kumbe faraja ni za ziada: zinafaa mradi tusizame ndani yake; tukizipenda mno, Mungu anatuondolea ili atujaribu. “Inawezekanaje mtu asielewe kuwa matokeo ya komunyo katika hisi si muhimu hata kidogo? Mara nyingi Mungu mwenyewe anawanyima furaha yoyote ya kihisi wale wanaopokea komunyo awalazimishe kumzingatia kwa macho ya imani” (Mt. Yohane wa Msalaba). Anayempenda Mungu si kwa ajili yake, bali kwa ajili ya faraja za kihisi anazozipokea au kuzitarajia, hayuko sawa kwa kuwa anapindua utaratibu: kwanza anajipendea, halafu anampenda Mungu kama anavyoweza akapenda tunda. Anayatumia vibaya yaliyo matakatifu zaidi na kukaribisha vishawishi vya kila aina: furaha za kihisi zikikusudiwa zinachochea maono yaliyosinzia ndani mwetu na kutufanya tuteleze kwenye genge la tamaa.

Uzinifu wa roho ni ashiki zisizokusudiwa zinazowapata wanaoanza wakati wa sala ya moyo au wa kupokea sakramenti. Kwa kawaida zinatokana na furaha ya ndani inayofurika katika hisi zisizotawaliwa au kutakaswa

vya kutosha. Pengine zinatokana na shetani anayetaka kuvuruga na kuhangaisha mtu aache sala. Pengine hofu yenyewe ya ashiki kurudia inaweza ikazisababisha, na walio wepesi kuguswa moyo wanazipata kutokana na maono mbalimbali. Hizo zote si dhambi kama utashi haujazikubali, bali unazipinga. Lakini zisichanganywe na ashiki zinazochochewa ingawa bila ya makusudi mazima (k.mf. kwa ujirani mkubwa mno na mtu unaoathiri urafiki wa Kiroho).

Upotovu ulio mbaya zaidi ni ule ambao unaathiri na kughushi yaliyo bora, kama vile sala ya bandia na upendo wa bandia. Kwa hiyo tunaonywa, "Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu" (1Yoh 4:1). Kusudi tusijidanganye tunahitaji unyenyekevu na usafi wa moyo. Tunaweza kujumlisha mafundisho kuhusu ufishaji wa tamaa katika maneno haya: "Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu" (Math 5:8).

**KUFISHA HASIRA**

Ufishaji mwingine unaosisitizwa na Injili unahusu hasira, vurugu ya pili ya hisi zetu. Kufisha hasira kunatupatia upole: si ule wa kuzaliwa nayo, wala ule unaoruhusu lolote kwa kukosa msimamo, bali *adili la upole* ambalo ni nguvu kubwa ya kujitawala, kudumisha roho katika utulivu wa Mungu, na kuwatendea mema wanaotukasirikia. Huo ufishaji wa hasira ni wa lazima kadiri matokeo yake yalivyo mazito kwa kuwa inaweza kufikishia madhambi mengine, hata kulikufuru jina la Mungu. Kinyume chake, upole ndio ua linalotunza matunda ya upendo, kwa kuwa unafanya yapokewe mashauri na hata maonyo yake. Kumbe yakifanywa kwa ukali hayazai kitu.

Mt. Yohane wa Msalaba alitaja *ari chungu* kati ya kasoro za wanaoanza, kwa kuwa wanaponyimwa faraja, mara wanakosa uvumilivu. "Ladha ya mambo ya Kiroho inapokuja kukosekana, umbile lao linavurugika; wanashikwa na huzuni, wanatimiza wajibu pasipo adabu, wanakasirika kwa mambo madogo sana na pengine haiwezekani kuwavumilia… Wanafanana na mtoto mchanga asiyeridhika kwa kuwa muda wa kuachishwa ziwa umefika". Pengine wanatumbukia uzembe. Mara nyingine "wanalaumu kasoro za wengine, wakisukumwa na ari isiyo na kiasi. Wanawasema na kusukumwa kuwaonya kwa ukali… kana kwamba wenyewe tu ni waadilifu… Wengine, wakiona kasoro zao wenyewe, wanasahau unyenyekevu na kujikasirikia, na huo utovu wa subira unaonyesha wazi kwamba walidai kugeuka watakatifu kwa mkupuo mmoja… Kwa wengine, ambao wamezoea kupanga makuu na kuweka maazimio ya kishujaa, lakini kwa kweli wana kiburi kuliko unyenyekevu, uponyaji wa hasira na upatikanaji wa upole wa Kiroho hauwezi kufanyika nje ya usiku wa giza" yaani utakaso wa Kimungu wa hisi.

Kujitakasa upande wa hisi kunatakiwa kufuta vurugu hizo mbili (tamaa na hasira). Lakini hakuwezi kuzifuta kabisa; unahitajika utakaso mkubwa zaidi: ule unaotokana na Mungu mwenyewe anapotia hisi katika ukavu wa muda mrefu ambapo anatutia mwanga wa kipaji cha elimu, yaani elimu ya ubatili wa malimwengu yote iliyo neema ya Kiroho tu. Utakaso huo ni namna mojawapo ya msalaba unaoleta wokovu ambao tuubebe ili kufikia maisha ya Kiroho kweli, ambayo yanatawala hisi na kutuunganisha na Mungu.

## 2.8. *KUJITAKASA UPANDE WA UBUNIFU NA KUMBUKUMBU*

Tuliyoyasema kuhusu kujitakasa upande wa hisi yameshatuonyesha kuwa ufishaji wa nje si ule muhimu zaidi, ingawa mtu akitaka kuupuzuia atapuuzia pia ule wa ndani na hatimaye atapotewa kabisa na roho ya kujikana. Hasa akikataa ufishaji kwa makusudi atatumbukia fikra za kidunia tu zilizo kinyume cha imani, inavyotukia mara nyingi. Tukitaka kujipatia yale yote yanayotupendeza, katika chakula na starehe, pasipo kuzingatia kiasi cha Kikristo, tunaacha kulenga ukamilifu na kukumbuka wajibu wetu. Lakini ufishaji wa nje wa mwili na hisi hauzai vya kutosha usipoendana na ufishaji wa ndani wa ubunifu na kumbukumbu, tunaotaka kuzungumzia sasa, na wa akili na utashi, tutakaozungumzia baadaye.

**KUJITAKASA UPANDE WA UBUNIFU**

Ubunifu ni uwezo wa kufaa kwa kuwa roho iliyounganika na mwili haiwazi pasipo taswira; ndiyo sababu Bwana alisema kwa mifano ili kuinua umati toka mfano wa kihisi hadi wazo la Kiroho. Lakini ubunifu unatakiwa kuongozwa na akili iliyoangazwa na imani, la sivyo unakuwa kama kichaa wa nyumbani, ukitusogeza mbali na mambo ya Mungu na kutuelekeza kwenye mambo ya bure ambayo hayajengi kitu, au hayapo au yamekataza pia. Walau unatuhamishia ulimwengu wa ndoto za mchana, inapozaliwa miguso ya juujuu ambayo ni kinyume cha ibada halisi inayoelekea yasiyoonekana, bila ya kusimama katika picha za kihisi zinazoyamaanisha: *kadiri tunavyokaribia muungano na Mungu hatutegemei picha.*

Hasa wakati wa uchovu hatuwezi kuondoa upesi taswira za bure na za hatari, lakini kwa msaada wa neema tunaweza kuacha kuzizingatia kwa roho, halafu polepole kupunguza idadi yake na mvuto wake. Hata waliokamilika wanasumbuliwa na mitawanyiko kadhaa ya mawazo isiyo ya hiari na inayotokana pengine na shetani. Lakini mtu akiendelea anazidi kujikomboa kutoka mitawanyiko hiyo na hatimaye anamtazama Mungu *karibu pasipo kuzingatia taswira* zinazoendana na tendo hilo la imani lenye kupenya na kuonja. Ni kama tunapoandikia peni bila ya kuzingatia aina yake, au tunapoongea na mtu bila ya kuangalia mtindo na rangi ya mavazi yake. Polepole ubunifu unaacha kuvuruga kazi ya akili, na hatimaye *unatumiwa nayo*

kufafanulia pengine maisha ya Kiroho kwa mifano mizuri ajabu. Mifano iwe na kiasi isije ikajivutia akili za watu, badala ya kuzivuta kwenye wazo inalolieleza kwa namna yake. Mfano ni kwa ajili ya wazo tu, nalo ni kwa ajili ya ufafanuzi wa ukweli. Hapo akili inatumia mfano pasipo kuishia ndani yake, kama vile mwadilifu anavyovaa nguo bila ya kuzitia maanani.

Lakini *ulinganifu* huo wa vipawa mbalimbali haupatikani pasipo *kuratibu* ubunifu na hivyo polepole kurudisha utaratibu uliokuwepo katika uadilifu wa asili ambapo sehemu ya juu ya roho ikimtii Mungu *ilikuwa inatawala ubunifu* na maono. Kwa misingi hiyo, tunapaswa kuondoa mara taswira za hatari, masomo yasiyo na faida, na ndoto za mchana ambazo zinapoteza muda wa thamani na kutuingiza katika udanganyifu wa kila aina, ambapo adui atucheke ili kutuangamiza. Tunapaswa kuwajibika kila nukta, kufanya vizuri tunachokifanya, tukielekeza utekelezaji wa wajibu kwa Mungu ili tumpende kuliko yote. Hivyo polepole akili na utashi vitatawala; na ubunifu ukitawaliwa utaona katika uzuri wa liturujia lishe ya maisha ya ndani.

**KUJITAKASA UPANDE WA KUMBUKUMBU**

Tuseme sasa kuhusu ufishaji wa kumbukumbu, inayotukumbusha mara nyingi mambo ambayo ni afadhali kuyasahau. Kumbukumbu yetu inahitaji kutakaswa kwa sababu, baada ya dhambi ya asili na ya dhambi zetu binafsi, imejaa kumbukumbu zisizo na maana na pengine za hatari. Tunakumbuka hasa tulivyokosewa, maneno makali ambayo aliyeyasema pengine ameyajuta na kuyaombea msamaha. Hatukumbuki hivyo mema tuliyotendewa, na pengine neno kali linatusahaulisha fungu la misaada tuliyopatiwa miaka na miaka. Lakini kosa kuu la kumbukumbu yetu ni *kumsahau Mungu.* Mara nyingi, badala ya kukumbuka yaliyo muhimu zaidi, inasahau *kitu kile ambacho pekee ni cha lazima.* "Je, mwanamwali aweza kusahau mapambo yake, au bibi arusi mavazi yake? Lakini watu wangu wamenisahau mimi kwa muda wa siku zisizo na hesabu" (Yer 2:32). "Wakayasahau matendo yake kwa haraka… Wakamsahau Mungu, mwokozi wao, aliyetenda makuu katika Misri" (Zab 106:13,21). Maandiko yanasema mara nyingi kuwa hasa katika tabu tunapaswa kukumbuka rehema za Mungu na kuomba msaada wake. Tukimsahau na kupuuzia fadhili zake kuu (k.mf. umwilisho uliotukomboa) tunakosa *shukrani* na kupoteza muda huu unaotakiwa kulenga uzima wa milele.

Kumsahau Mungu kunaifanya kumbukumbu yetu *izamie nyakati hizi* isione *zinavyohusiana na umilele* na fadhili na ahadi za Mungu. Kasoro hiyo inaifanya ione yote katika mfululizo wa mambo yanayopita, isione nukta ya sasa inavyohusiana na ile pekee isiyo na mwisho, yaani isione namna ya Kimungu ya kuishi nukta hiyo istahili uzima wa milele. Kumsahau Mungu kunatuacha tuone mambo *pasipo maana yake,* kumbe kumtazama Mungu ni *kuona toka juu mambo yapitayo* yanavyohusiana naye *asiyepita kamwe.* Kuzama katika muda ni kusahau maana ya muda, yaani uhusiano wake na uzima wa milele. "Katika mambo yako yote uukumbuke mwisho wako, hivyo hutakosa kamwe hata hatima" (YbS 7:36).

Kwa adili gani tunapaswa kuondoa kosa hilo kubwa? Mt. Yohane wa Msalaba, aliyefundisha kuwa tumaini ni kubwa kadiri kumbukumbu isivyo na habari za malimwengu, amejibu, "Kumbukumbu inayomsahau Mungu inatakiwa kuponywa na *tumaini la heri ya milele,* kama vile akili inavyotakiwa kutakaswa na ustawi wa imani, halafu utashi na ustawi wa upendo". Kama vile mababu na manabii wa Agano la Kale walivyoishi kwa kumtazamia Masiya aliyeahidiwa, sisi tuishi kila siku zaidi kwa kutumainia heri ya milele.

Kitabu cha Kumfuasa Yesu Kristo kinasema mara nyingi kuhusu utakaso wa kumbukumbu unaoandaa kumtazama Mungu, kinapozungumzia kutafakari kifo (I,23), kukumbuka fadhili za Mungu (III,22), uhuru wa moyo unaopatikana kwa sala kuliko kwa kusoma (III,26), kuvisahau viumbe ili kumuona Muumba wao (III,31), kukwepa mahangaiko katika shughuli (III,39) na elimudunia isivyo na faida (III,43): "Nahitaji kupaa juu ya viumbe vyote, kuacha kabisa nafsi yangu, kuangalia mambo ya Mungu na kufahamu kwamba wewe Muumba hufanani na kiumbe chochote… Lo! Moyo wa binadamu mjinga kama nini! Unafikiria mambo ya sasa tu, hauangalii ya mbele. Basi, yafaa ujitengeneze kwa mambo yote sawa kama ungalikufa leo hii… Hizi ni siku za kufaa. Kwa nini huzitumii vizuri zaidi basi, upate kustahili neema ya kuishi milele?… Jifunze kufia dunia, upate kuwa hai pamoja na Yesu siku ile. Jifunze sasa kudharau yote, siku ile upate kufika huru kwa Kristo… Usifikiri kitu ila usalama wako; usisumbukie lolote, isipokuwa ya Mungu… Mwanangu, usishindwe na maneno mazuri ya watu hata yakiwa na utaalamu mkubwa. Ufalme wa Mungu haupo katika maneno, bali katika fadhila. Sikiliza maneno yangu: huwasha moyo, huangaza akili, huleta majuto ya dhambi, hutuliza kwa namna nyingi... Ukiisha kusoma na kujua mengi, bado ni lazima urudie neno hili lililo msingi wa elimu: kwamba ndimi nimfundishaye binadamu; ndimi niwapaye wanafunzi wangu hekima kubwa kuliko ile wanayoweza kufundishwa na mwalimu yeyote… Chochote kisichokuwa Mungu si kitu; na sharti kidhaniwe vile".

Mafundisho hayo yaliendelezwa na Mt. Yohane wa Msalaba kuhusu kutozingatia kumbukumbu ya neema za pekee ambazo kwa namna fulani ni za nje; kuzikumbuka kwa kujipongeza kunazuia muungano na Mungu. Tumaini linatuinua kumpenda kuliko ujuzi wa neema za pekee: "Kusudi tuishi kwa tumaini safi kamili kwa Mungu, hatutakiwi kusimama kwenye fahamu, sura na taswira maalumu. Tulivyokwishaeleza, kila zinapojitokeza tunapaswa mara kumuelekezea Mungu roho tupu kuhusu hizo, kwa mruko wa mapenzi yenye hisani. Hatutakiwi kuyafikiria wala kuyazingatia isipokuwa kadiri kumbukumbu yake inavyohusiana na majukumu". Ndio utakaso halisi wa kumbukumbu inayohangaikia mengi yasiyo na faida au ni ya hatari.

Hivyo polepole roho itainuka kumfikiria Mungu na fadhili zake. Kumbe mara nyingi tunaingia kanisani ili kuomba neema inayohitajika haraka, tukisahau kumshukuru Mungu kwa fadhili kuu ya ekaristi inayodai asante ya pekee, kwa kuwa ndiyo ukumbusho wa ahadi za uzima wa milele.

## 2.9. ***KUJITAKASA UPANDE WA AKILI***

Vipawa vya juu vya binadamu, alivyonavyo sawa na malaika, ni akili na utashi. Hivyo pia vinahitaji kutakaswa na kuratibiwa, kwa kuwa vimevurugwa na dhambi ya asili na dhambi zetu binafsi. Mtazamo wa kwanza wa akili ya mtoto aliyebatizwa ni mnyofu, na vilevile mtazamo wa mtu anayeanza kuitikia wito kwa bidii. Lakini baadaye mtazamo huo unapotewa na unyofu kutokana na wingi wa mambo yanayozingatiwa kwa moyo usio safi. Hapo unahitajika utakaso mkali ili kurudia unyofu wa awali unaoshika mandhari ya maisha kwa jumla usiishie katika madogomadogo. Wana heri wazee wale ambao, baada ya majaribu na mang'amuzi mengi wanafikia unyofu huo wa hali ya juu wa hekima halisi waliowahi kuuchungulia kwa mbali. Kwa maana hiyo imesemwa, "Maisha mazuri ni wazo la ujanani lililotekelezwa katika utu uzima".

### HAJA YA UTAKASO HUO KUTOKANA NA KASORO ZA AKILI YETU

Akili imejeruhiwa na dhambi ya asili; donda hilo linaitwa *ujinga,* maana badala ya kuelekea mara ukweli, na hasa ukweli mkuu, akili inapata shida kuufikia: inaelekea kuzama katika malimwengu bila ya kuinukia sababu zake; inaelekea kwa *udadisi* mambo yanayopita, kumbe ina uvivu katika kutafuta lengo letu kuu na njia za kulifikia. Matokeo yake, *inadanganyika kwa urahisi,* inatiwa giza na mawazo yasiyo na msingi yanayotokana na maono yasiyoratibiwa, hata inaweza ikafikia upofu wa roho. Tofauti na walivyodhani Waprotestanti wa kwanza na Wajanseni, dhambi ya asili haikufanya akili isiweze kujua ukweli, bali kwa juhudi za kudumu, pasipo msaada wa ufunuo wa Mungu, inaweza ikajua kweli kadhaa za msingi, k.mf. uwepo wa Mungu. Lakini Mtaguso wa Kwanza wa Vatikano ulivyofundisha, wanaoweza juhudi hizo ni wachache, nao pia hawafikii hatua hiyo kabla ya muda mrefu, tena hawafaulu kujikomboa kutoka udanganyifu wote. Kwa ufunuo wa Mungu ndipo kweli za kimaumbile kuhusu dini zinapoweza kujulikana na wote upesi, kwa hakika na pasipo mchanganyiko wa makosa. Baada ya ubatizo donda la ujinga linaelekea kuwa kovu, lakini linaanza kutona tena kwa dhambi zetu binafsi, hasa udadisi na kiburi cha roho.

*Udadisi* ni kasoro inayotuelekeza kuwa na hamu ya harakaharaka ya kusoma na kuzingatia mambo yasiyo muhimu, tukipuuzia yale ya Mungu na ya wokovu wa milele. Udadisi huo unatokana na uzembe na kutupotezea muda mwingi. Watu kadhaa wenye elimu ndogo walioshiba kweli za Injili wanapima mambo vizuri. Kumbe wengine, badala ya kujipatia kwa ndani kweli kuu za Ukristo, wanapoteza muda mwingi kukusanya taarifa ambazo hazina faida au walau zinasaidia kidogo kupima mambo: *kwa kulimbikiza* taarifa bila ya mpango, badala ya kuunda roho, wanaizima kama tunapozidisha kuni motoni. Hapo hawaoni tena *mwanga wa mawazo makuu* ambayo peke yake yanaweza kupanga taarifa hizo na kuwainua kwa Mungu, asili na lengo la vyote. Mt. Thoma wa Akwino, akifafanua maneno: "Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga" (1Kor 8:1), aliandika, "Hapa mtume hamkubali anayejua mengi, asipojua namna ya kujua. Namna ya kujua ni kujua utaratibu, juhudi na lengo vinavyompasa: utaratibu, ili kukipa kipaumbele kinachochangia zaidi wokovu; juhudi, ili kukitamani zaidi kile kinachozaa zaidi upendo; lengo, yaani kwa kujijenga mwenyewe na jirani, si kwa majivuno na udadisi". Adili la kusoma linapinga upande mmoja udadisi wa bure, upande mwingine uvivu wa akili, limuongoze mtu kusoma yale anayotakiwa kuyasoma, kwa namna na kwa wakati wake, tena kwa lengo adilifu na lipitalo maumbile. Udadisi huo wa kishamba ni *kinyume cha kuzama ndani ya Mungu,* ambako kunapima yote kwa kumzingatia yeye. Unaweza kufikisha hadi *upumbavu wa roho* uliozungumziwa na Maandiko: "Hekima ya dunia hii ni upuzi mbele ya Mungu" (1Kor 3:19). Upumbavu huo ni dhambi, unapingana na kipaji cha hekima, na unatokana hasa na uzinifu. Hapo mtu anapima kijuujuu mambo yote, hata yaliyo makuu, kwa kuyazingatia upande wa chini, k.mf. kufuatana na tamaa au kiburi chake.

*Kiburi cha roho* ni vurugu kubwa kuliko udadisi; kinafanya tuiamini akili yetu hata tusikubali mashauri, hasa ya wakubwa wetu, wala kujitafutia mwanga kwa kuzingatia kwa makini na unyofu maneno ya wapinzani wetu. Hivyo tunakuja kukosa wazi busara, na matokeo yake tutalazimika kuyalipa kwa uchungu. Tunafikia kubishana kwa ukali, kushikilia mno msimamo fulani, kudhihaki na kukataa katakata yale yote yasiyolingana na rai yetu. Zaidi tena tunaweza tukafikia kuwakatalia wengine uhuru tunaodai kwa maoni yetu, kutokubali miongozo ya Papa, pia kupunguza na kupuuzia dogma tukijisingizia tunataka kuzifafanua vizuri kuliko zamani. Ni hatari *kushikilia mno* msimamo fulani na kukataa mashauri ya maana: pengine tabia hiyo wanayo watu waliopotoka baada ya kushika maisha ya Kiroho; hapo wana ari chungu inayotaka kulazimisha wote wafuate maoni yao, kana kwamba wao tu wanaye Roho Mtakatifu. Wamejaa kiburi cha roho, wanakosa upendo kwa kisingizio cha kurekebisha yote kandokando yao; wanaweza wakawa maadui wa amani na kusababisha mafarakano makubwa.

Hatimaye kasoro hizo, hasa kiburi, zinaweza zikatufikisha kwenye *upofu wa akili* ambao ni kinyume cha kuzamia mambo ya Mungu. "Ole wenu viongozi vipofu… wanafiki, kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa

kuyafanya, wala yale mengine msiyaache. Viongozi vipofu, wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia" (Math 23:16,23-24). Kadiri ya nabii Isaya (taz. 6:9-10), Yesu na Mt. Paulo, upofu huo ni adhabu ya Mungu anayewanyima mwanga wale wasiotaka kuupokea.

Kuna wakosefu ambao kwa kurudiarudia makosa wamekuwa hawatambui tena matakwa ya Mungu ingawa yameonyeshwa wazi, wala hawatambui kuwa mabaya yanayowapata ni adhabu zake, kwa hiyo hawaongoki. Wanayaeleza hayo na matatizo ya kimataifa kwa kutoa sababu za kibinadamu (k.mf. uchumi) wasitambue kuwa sababu kuu ni ya Kiroho, yaani kwamba wengi, badala ya kumfanya Mungu kuwa lengo kuu la maisha yao, wanalenga mali ambazo zinafitinisha kwa sababu haziwezi kuwa zote za wote kwa wakati mmoja.

Upofu huo unamfanya mkosefu apende mali kuliko mema ya milele, asisikie sauti ya Mungu inayomuita. Upofu wa roho ni adhabu yake, lakini ni dhambi pia ambayo tunaacha kwa makusudi kuzingatia kweli za Kimungu tukipendelea tamaa au kiburi chetu. Sawa na upumbavu wa roho, unatuzuia tusione ujirani wa kifo na hukumu, unatuondolea uwezo wa kuona ndani na unatuacha katika hali ya kutoelewa mambo ya juu: k.mf. ukuu wa amri wa upendo, thamani ya damu ya Mwokozi iliyomwagwa kwa ajili yetu na ya misa inayohudhurisha sadaka ya msalabani. "Kama mwizi anapoiba pesa angepotewa na jicho, wote wangesema ameadhibiwa na Mungu. Kumbe wewe umepotewa na jicho la roho, lakini unadhani Mungu hajakuadhibu" (Mt. Augustino).

Tunashangaa kuona Wakristo wenye elimudunia kubwa kuhusu sanaa au sayansi ambao hawajui vya kutosha kweli za dini, tena wanazichanganya na makosa mengi na maoni yasiyo na msingi: kukosa hivyo uwiano wa elimudunia na elimudini kunawafanya *wabilikimo upande wa roho.* Wengine wanaojua zaidi mambo ya imani, historia na sheria za Kanisa, wanaonyesha elekeo ambalo linakwenda *kinyume cha hekima* na kuwafanya walione Kanisa *kwa nje tu,* kama mtu anayetazama vioo vya rangi upande wa nje wa jengo, badala ya kuviona upande wa ndani kwa msaada wa mwanga kutoka nje.

Upumbavu huo unatuzuia hasa tusipokee ujumbe wa Mungu anayesema kupitia matukio makuu ya leo, tunapoona maelekeo mawili ya kimataifa kushindana moja kwa moja. Upande mmoja ufalme wa Kristo unataka kuwavuta wote kwa Mungu aliye uzima wenyewe; upande mwingine elekeo la kuwavuta wote kwenye mali, anasa na kiburi, hivi kwamba mfano wa mwana mpotevu unatimia kwa mataifa mazima. "Mvutano huo unazidi kuwa mkali mpaka utakaposababisha kitambaa kuchanika... Siku moja ushujaa wa Kikristo utakuwa ututuzi pekee wa matatizo ya maisha. Hapo, kwa kuwa Mungu analinganisha neema zake na mahitaji, asimjaribu mtu kuliko uwezo wake, *tutaona kwa hakika utakatifu kuchanua kwa wingi wakati utakaokuwa mbaya kuliko zote za historia ya binadamu"* (Y. Maritain). Juhudi kuu za uovu zitafanyika wakati wa ushindi wa mwisho wa Kristo. Katika mashindano hayo tukimbilie sala na sadaka hata kuliko masomo na utume.

**TUJITAKASE VIPI UPANDE WA AKILI?**

Ili turekebishe vurugu hiyo tuliyonayo wote, ingawa kwa kiasi tofauti, tunapaswa kujitakasa kwa *ustawi wa imani:* "Imani ndiyo chanzo cha utakaso wa moyo ili kujikomboa kutoka udanganyifu, halafu imani iliyo hai kwa upendo inakamilisha utakaso huo" (Mt. Thoma wa Akwino). Ni lazima akili inayoongoza utashi itakaswe, la sivyo mzizi wa utashi huwa umepotoka na kuchanganyikana na udanganyifu. Utakaso huo unategemea imani, inayotufanya kwanza *tushike* kweli zilizofunuliwa (kwa sababu ya mamlaka ya Mungu aliyezifunua), halafu tuzingatie na *kupima* yote kadiri ya kweli hizo. Hiyo inamtokea hata mkosefu mwenye imani, lakini hasa mwadilifu kwa kuwa ana vipaji vya Roho Mtakatifu. Hatutakiwi *kushikilia* tu kweli za imani, bali *kwa njia yake kupima* yote ambayo tuyawaze, tuyaseme, tuyatende au tuyaepe maishani mwetu. Ndiyo kuamua kwa imani na si kwa fikra za kidunia.

*Imani, ingawa ni giza, inatuangaza.* Ni giza kwa kuwa inatufanya tushike mafumbo tusiyoyaona; lakini mafumbo hayo, yanayohusu maisha ya ndani ya Mungu, yanatuangazia akili tuone wema wake kwetu. Mwanga huo wa safari yetu ni *chombo cha muungano na Mungu* unayemtambulisha kwetu kwa hakika na kwa namna ipitayo maumbile. Mwanga huo ni wa juu kuliko hakika yoyote tunayoweza kuipata duniani. Yaliyo wazi kwa hisi zetu si ya Kiroho, kwa hiyo si Mungu; yaliyo wazi kwa akili yetu yanaweza kuwa mawazo ya kweli juu ya Mungu, lakini si juu ya maisha yake ya ndani yanayopita maumbile yoyote. Ili tuyaone tunahitaji kufa na kujaliwa heri ya mbinguni; lakini imani inatufikisha kwenye maisha hayo tangu sasa katika giza.

Mtu akipenda *njozi* kuliko imani ya kumiminiwa anadanganyika kwa kupenda yaliyo ya nje, yanayofikiwa na hisi, yaliyo taswira tu kuliko ukweli wenyewe upitao maumbile. Hivyo hata kama njozi zake ni za kweli anasogea mbali na hali ya kumzamia Mungu. Imani, ingawa ni giza, inatuangaza, kama vile usiku kwa giza lake unavyotuwezesha kuona nyota na ukuu wa anga. Ajabu! Katika giza la usiku tunaona mbali kuliko mchana, tunapozuiwa na mwanga wa jua! Vilevile hisi na akili zetu zinaona maumbile, kumbe imani inatufumbulia ukuu upitao maumbile, tutakaouona wazi milele. "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana" (Eb 11:1). "Mambo yale ambayo ukweli wake haujaonekana kwetu, imani inatupa undani wake, kwa kuwa yenyewe ndiyo undani wake" (Mt. Yohane

Krisostomo). “Imani ni adili la akili, ambalo uzima wa milele unaanza ndani mwetu, ukifanya akili ikubali yasiyoonekana” (Mt. Thoma wa Akwino).

Basi, ili tuishi kwa imani, tuzingatie yote kwa mwanga huo: kwanza Mungu, halafu sisi wenyewe, wenzetu wowote na matukio ya kupendeza au ya kusikitisha. Tusiyazingatie upande wa hisi au wa akili, bali upande wa imani kwa kuyaona kwa macho ya Mungu, kidogo anavyoyaona yeye. Hivyo ni wazi haja ya kuitakasa roho kutoka *udadisi,* tusipende tena kusoma yasiyo muhimu kuliko kutafakari Injili na yale yanayoweza kulisha roho. Badala ya kusoma mengi ili kujuajua yote na kuyazungumzia, tusome kwa unyenyekevu yaliyo bora ili kuyachimba na kuyatekeleza na kuwafaidisha wengine pia. “Wapo wanaotaka kujua ili wajue tu, na huo ni udadisi; wengine wanataka ili wajulikane, na hayo ni majivuno; wengine wanataka ili wauze ujuzi, na hiyo ni biashara mbaya; wengine wanataka ili wajengeke, na hiyo ni busara; wengine wanataka ili wajenge wenzao, na huo ni upendo” (Mt. Bernardo). “Elimu ikiwa peke yake, pasipo upendo, inavimbisha kwa kiburi. Muunganishe elimu na upendo, hapo elimu itafaa” (Mt. Thoma wa Akwino).

Ni wazi pia haja ya kutopima mambo kwa haraka inayosababisha udanganyifu mwingi; tena zaidi haja ya kutoshikilia maoni yetu, bali kuyarekebisha kwa kusikiliza Kanisa, kiongozi wa Kiroho, na Roho Mtakatifu anayetaka kuwa mlezi wetu wa ndani. Hapo *kuzingatia madogomadogo kusingetusahaulisha ujumla,* inavyotokea mara nyingi, kama vile kuona mti kwa jirani mno kunavyotuzuia tusione msitu. Wanaokwazwa na mabaya yanayotokea, na kusema hayaeleweki, wanazingatia mno kwa uchungu madogomadogo ya tabu na kusahau ujumla wa mpango wa Mungu ambamo yote yanalenga faida ya wanaompenda. Kumbe mtazamo wa jumla ukiwa safi ni wa juu tayari. Hivyo mtoto akitazama nyota anahisi ukuu wa Mungu. Baadaye akichimba sayansi huenda akasahau mtazamo wa jumla, ambao akili inapaswa kuurudia ili kuona undani wake. Elimu kidogo inasogeza mbali na dini, kumbe elimu ya juu inarudisha kwake.

Kuna watu wawili walio sahili hasa: mtoto ambaye hajaanza kujua uovu, na mzee mtakatifu aliyeusahau kwa kuushinda mfululizo; kwa hiyo mzee anampenda mtoto na kupendwa naye. Upande wa sala, mtazamo wa kwanza ni ule wa mtoto mbele ya pango la Noeli; mtazamo wa dhati ni ule wa mwanasala mwishoni mwa maisha yake. Kwa mtawa, mtazamo wa kwanza ulio mnyofu na wenye kupenya ni ule alionao anapoitikia wito wa Mungu; mara nyingi mtazamo huo ni wa juu kuliko mambo mengi atakayoyazingatia baadaye. Heri watakaourudia, wakitazama kwa hekima undani wa maisha yao yote.

Vivyo hivyo, matokeo makuu yaliyokusudiwa na Mungu ili kuwaangaza na kuwaokoa wanyofu, kama yale ya Lurdi, yanawaelea kwa urahisi wenye moyo safi, wanaoona upesi asili yake ya Kimungu, maana na uzito wake. Tukiacha mtazamo huo na kuzingatia madogomadogo tunaweza tukashindwa kuelewa chochote. Hatimaye elimu ya juu ikiendana na unyenyekevu, inarudisha kwenye mtazamo wa kwanza na kuuthibitisha ili kutambua kazi ya Mungu na faida ya roho. Baada ya kusoma miaka mingi falsafa na teolojia, mtu anarudi kwa furaha kwenye imani nyofu ya Abrahamu, Isaka na Yakobo, kwenye maneno ya Zaburi na mifano ya Injili. Ndio utakaso unaoandaa akili kuzama katika mafumbo. “Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru” (Math 6:22).

## 2.10. *KUJITAKASA UPANDE WA UTASHI*

Sasa tuseme juu ya kutakasa na kuunda utashi, kipawa cha juu kinachotuelekeza kwenye mema yaliyojulikana na akili. Kwa kuwa unalenga mema yoyote, unaweza kuinuka umpende Mungu aliye wema mkuu. Kila kipawa cha binadamu kinaelekea jambo maalumu lililo jema kwake (k.mf. macho yanaelekea vinavyoonekana), lakini *utashi unaelekea mema ya mtu mzima* na kuelekeza vipawa vingine vyote vitekeleze kazi yake (k.mf. akili itafute ukweli): ndiyo sababu utashi ukiwa mwadilifu, basi mtu ni mwema. Kinyume chake, utashi usipokuwa mnyofu unavyotakiwa, usipoelekea yaliyo mema kweli kwa mtu mzima, huyo anaweza akawa mwanasayansi mzuri, lakini si mtu mwema: ana umimi, na maadili anayoonekana kuwa nayo yanatokana hasa na kiburi, hofu ya kusumbuliwa n.k. Hiari ya utashi inafanya yawe na stahili si matendo yake maalumu tu, bali pia yale ya vipawa vingine vyote. Kwa hiyo kuratibu utashi ni kuratibu mtu mzima. Basi, tuone kasoro na upotovu vilivyomo ndani mwake kutokana na dhambi ya asili na dhambi zetu binafsi.

**KASORO KUU YA UTASHI: UMIMI**

*Nguvu ya utashi* kwa kutenda na kuongoza kazi za vipawa vingine *inatokana na usikivu wake kwa Mungu,* na ulinganifu wake na matakwa yake, kwa kuwa hapo nguvu ya Mungu inaufikia. Ndilo wazo kuu linaloongoza suala zima. Tunaona maana yake yote tukikumbuka kuwa katika uadilifu wa asili, utashi ulipokuwa chini ya Mungu kwa upendo na utiifu, uliweza kuzuia vurugu yoyote ya hisi: maono yalikuwa chini ya utashi uliohuishwa na upendo. Lakini baada ya dhambi ya asili tunazaliwa huku utashi wetu haumuelekei Mungu, nao ni dhaifu kwa kutekeleza wajibu wowote, hata wa kimaumbile tu. Tunazaliwa huku *utashi wetu unaelekea kujipendea.* Ndilo donda la *uovu* linalojitokeza mara nyingi kwa umimi mkubwa unaochanganyikana na kila tendo letu na ambao tunapaswa kujihadhari nao. Kwa hiyo utashi, kisha kuwa dhaifu kwa kutomtii Mungu, hauna tena mamlaka kamili juu ya hisi, bali unaweza tu kuzibembeleza zikubali kuutii. Baada ya ubatizo uliotuzaa upya donda hilo linaelekea kupona sawa na mengine; lakini linaanza tena

kutoneshwa na dhambi zetu binafsi.

Kasoro kuu ya utashi ni kujipendea kwa kusahau upendo unaotupasa kwa Mungu na kwa jirani: *ndiyo asili ya dhambi zote. Matakwa yetu* yasiyolingana na yale ya Mungu ni hatari kwa kuwa yanaweza kupotosha mambo yote: hata yaliyo bora yanakuwa mabaya yakitokana na matakwa yetu, kwa kuwa yanajifanya lengo badala ya Mungu. Bwana akiyaona katika mfungo, sadaka n.k. anavikataa kama vitendo vya dini vilivyofanywa ili kujionyesha. Matakwa yetu yanatokana na umimi, ambao ni kama kansa ya utashi inayouharibu zaidi na zaidi. Utashi unahitaji kutakaswa na kuundwa Kikristo: ndiyo matokeo ya ustawi wa upendo "unaounganisha binadamu na Mungu, *ili mtu asiishi kwa ajili yake bali kwa ajili ya Mungu*" (Mt. Thoma wa Akwino).

"Yafaa ujue sana kwamba kujipendea kuna hasara inayopita hasara zote za ulimwengu. Upendacho na kufurahiwa nacho, ndicho kinachokunasa. Upendo wako ukiwa safi na kunyoka sawa, ukiongoka vema, hutaweza kufungwa mapingu na kiumbe chochote. Basi, usitamani jambo liwezalo kukupinga na kupunguza uhuru wa moyo wako. Kwa nini hujiweki mikononi mwangu kwa moyo wako wote, wewe pamoja na yote uliyo nayo, na pupa zako zote? Ni ajabu kweli! Kwa nini kupata majonzi ya bure? Kwa nini kuhangaika kwa tabu isiyo na maana? Simama thabiti katika hali ninayotaka mimi, hutapata hasara. Ukizidi kutamani leo mambo haya na kesho mambo mengine, au ukitaka kwenda mara huku mara kwingine, vile upendavyo mwenyewe, hutatulia kamwe; hutakuwa bila ya tabu hata siku moja. Kwa sababu kila jambo lina shida yake; kila mahali pana mtu atakayekusumbua" (Kumfuasa Yesu Kristo III,27:1-2).

"Maumbile ya mtu yana werevu, huwavuta wengi katika mitego, huwanasa. Kila mtu anaelekea kujipendea… Hitilafu zetu hazitaki kukomeshwa, wala kuzuiwa, wala kushindwa, wala kuamriwa, wala kutii… Maelekeo yetu ndiyo kujitafutia raha na kuangalia njia ya kujipatia faida kwa watu wengine… tunapenda sana kupokea sifa na heshima… tunaogopa kupata haya na dharau… tunapenda uvivu na kupumzisha mwili… tunataka mambo ya ajabu yenye kung'ara, hatutaki yale hafifu yasiyo na thamani… tunathamini sana malimwengu, tunafurahia faida ya kidunia, tunakasirika tunapopata hasara, tunashika hamaki tunapokosewa kidogo… Maumbile yetu ni kupenda mali, hutamani kupata, sio kutoa. Kwa maumbile yetu tunapenda kuweka vitu viwe mali yetu… Maumbile yetu huelekea viumbe na mwili na upuuzi na maongezi mengi… hujivunia cheo au asili maalumu, huwabembeleza watu wakuu, huwasifu wenye mali, huwakubali watu walio na tabia ileile… yanalalamika upesi kwenye masumbuko na ukosefu wa vitu… hutamani kutambua mambo ya siri na kusikia mapya. Hupenda kuonekana mbele za watu na kusikia matamu mengi nafsini mwake. Hupenda kujulikana na kutenda mambo ya ajabu yanayovutia sifa za watu… Kadiri maumbile ya mtu yanavyovunjwa na kuzuiwa, neema huongezwa. Na kwa msaada wa neema hiyo binadamu hugeuka polepole kuwa mtu mpya kwa mfano wake Mungu" (Kumfuasa Yesu Kristo III,54:1-8).

Kadiri ya Mt. Katerina wa Siena, kujipendea *"kunatia giza na kupunguza upana wa mandhari ya akili,* ambayo hatimaye inaona na kutambua tu kwa mwanga wa bandia wa jema danganyifu, wa aina ya furaha ambayo pendo linashikamana nayo… Kujipendea kumetia sumu katika ulimwengu na katika mwili wa fumbo wa Kanisa, na kulijaza bustani la Bibi arusi magugu yenye kunuka". Kunatufanya *tuwakosee haki Mungu,* kwa kutompatia utukufu unaompasa, *na majirani,* kwa kutowapatia mema wanayoyahitaji. Hatimaye kujipendea, kwa kupindua katika utashi wetu utaratibu uliowekwa na Mungu, kunatufikisha hadi *kufadhaika, kukata tamaa, kugombana, kufarakana na kukosa amani,* ambayo ni utulivu wa utaratibu, kwa hiyo unapatikana tu katika wale wanaompenda Mungu kuliko nafsi yao na kuliko yote.

**UTAKASO WA UTASHI KWA USTAWI WA UPENDO WA MUNGU**

Tutawezaje kuurudishia utashi, ambao umedhoofika na kulemaa kwa kiasi fulani, *nguvu* ya kushinda uzembe na kiburi, ambacho ni udhaifu uliofichika nyuma ya kinyago cha nguvu? Tukikumbuka uadilifu wa asili, tunapaswa kuutiisha zaidi na zaidi utashi wetu kwa ule wa Mungu: hapo atazidi kutujalia neema tuendelee katika njia ya ukamilifu. Tuuunde kwa ustawi wa maadili yanayotarajiwa kuwemo ndani yake: adili la *haki* linalompatia kila mmoja yale anayostahili; adili la *ibada* linalompatia Mungu heshima inayotupasa kwake; adili la *toba* linalofidia chukizo la dhambi; adili la *utiifu* kwa wakubwa; adili la *ukweli* na uaminifu; hasa adili la *upendo* kwa Mungu na kwa jirani.

Katika utekelezaji wa maadili yote, kuyatii matakwa ya Mungu kunadai *tukatae matakwa yetu* yasiyolingana nayo. *Roho ya sadaka* tu, kwa kufisha ndani mwetu umimi, inaweza kuhakikishia upendo wa Mungu ushike nafasi ya kwanza na kutupa amani. Amani ya ndani haipatikani pasipo roho ya sadaka, ambayo tuwe tayari kuacha yote ili kutimiza matakwa ya Mungu: *"Ee Mungu, moyo wangu u thabiti"* (Zab 108:1). Tuseme kila siku aliyoyasema Mt. Paulo alipoongoka, "Nifanye nini, Bwana?" (Mdo 22:10).

Kwa watu kadhaa utakaso huo ni *mgumu zaidi,* kutokana na marudiorudio ya makosa, tena kwa wote hauwezekani pasipo neema ya Mungu, kwa kuwa upendo wake tu unaweza kushinda na kufisha umimi. Upendo huo ukistawi, magumu yanakuwa rahisi: "Kwa maana *nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi"* (Math 11:30). Utawani kazi hiyo inarahisishwa na utiifu, unaonyosha na kuimarisha utashi kwa kuulinganisha kila siku zaidi na matakwa ya Mungu yanayojulikana kwa njia ya katiba na maagizo ya wakubwa.

Ili tufaulu kutakasa na kuimarisha utashi, ni lazima *tutende kadiri ya misimamo ya imani ya Kikristo,* badala ya kufuata ugeugeu wa roho yetu inayobadilika kadiri ya hali na rai za umma. Kisha kutafakari mbele ya Mungu na kumuomba neema, *tutende kwa uthabiti* kadiri ya wajibu wetu na ya matakwa yake. Nguvu halisi ya utashi ni tulivu, kwa hiyo ni dumifu pia, haikati tamaa kwa kushindwa kwa muda wala kwa donda lolote. Kushindwa tunashindwa tu tukiacha mapambano. Naye anayemfanyia kazi Bwana, anamtegemea badala ya kujitegemea.

Kimsingi, utashi imara ni ule usiojijenga juu ya kiburi, bali juu ya Mungu na neema yake inayotupasa kuiomba kila siku kwa tumaini nyenyekevu. Tukidumu kuomba hivyo neema za lazima kwa utakatifu na wokovu, hakika tutajaliwa tulivyoahidiwa, *"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa"* (Math 7:7). Sala ndiyo nguvu yetu katika udhaifu: *"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu"* (Fil 4:13). Ndivyo anavyopaswa kusema hasa anayefia dini. Hapo utashi una nguvu ya Kimungu: "Wewe, Bwana, nguvu zangu, nakupenda sana" (Zab 18:1). Kwa neema utashi wa mtu unashiriki uweza usio na mipaka wa Mungu na *unajikomboa* kutoka umimi, kutoka mvuto wa yale yote ambayo yanausogeza mbali na Mungu na kuuzuia usiwe mali yake tu. *Kujikana na roho ya sadaka ndiyo njia pekee ya kuungana naye,* kwa upendo wake kushinda umimi. Anayejichukia kitakatifu hivyo anaokoka milele na kupata tangu hapa duniani amani na muungano na Mungu ambavyo ni mwonjo halisi wa uzima wa milele. Ndiyo malezi halisi ya utashi.

**KUTOAMBATANA NA CHOCHOTE**

Mt. Yohane wa Msalaba ametuachia mafundisho bora kuhusu kukataa kikamilifu matakwa yetu, akielekeza njia *nyofu zaidi* ya kufikia ukamilifu, na akionyesha jinsi ugumu wa *njia nyembamba* unavyofikisha kwenye utamu wa muungano na Mungu. Tukikumbuka ukuu wa lengo, hatutadhani anatudai mno. Aliyepania kupanda mlima mrefu, hasimami akipata shida; anajua zinahitajika juhudi, kwa hiyo anajikaza na kusonga mbele moja kwa moja. Ndivyo anavyopaswa kufanya aliyepania kufikia kilele cha ukamilifu. Hapa tunafupisha mafundisho hayo kuhusu kutoambatana na yale yote yasiyo Mungu wala matakwa yake.

Tusiambatane na mema ya nje, *mali na heshima:* "mali izidipo msiiangalie sana moyoni" (Zab 62:10). Tusiambatane na *mema ya mwili,* uzuri na afya: ni upotovu kuyathamini kuliko muungano na Mungu. Hayo yote yatapita kama maua. Kumbe tunajali afya kuliko tunavyodhani; kuondolewa moja kwa moja ni sadaka kubwa kwetu, lakini ni sadaka tunayoweza kudaiwa. *Tusijipongeze kwa maadili* tuliyonayo: ni majivuno na pengine dharau kwa jirani. Tuthamini maadili si kama mali yetu, bali kadiri yanavyofikisha kwa Mungu. Tukipata *faraja* katika sala tusiambatane nazo, la sivyo tutafuata kiburi cha roho na kuzigeuza kuwa kizuio badala ya msaada kwa kumuendea Mungu; tutasimama kwa umimi katika kiumbe na kuigeuza njia kuwa lengo. Si kila kinachong'aa ni dhahabu, hivyo tunapaswa kuwa macho. "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa" (Math 6:33), yaani yoyote yanayofaa kwa roho na kwa mwili, hata matatizo ambayo yanatuondolea udanganyifu na kuturudisha kwenye njia yenyewe. Hatimaye, tukijaliwa *neema za pekee* tusiambatane nazo, kwa kuwa, *"Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao"* (1Kor 13:1). *"Msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni"* (Lk 10:20).

Kuhusu kipaji cha kuhubiri, Mt. Yohane wa Msalaba aliandika, "Sikanushi kuwa mtindo wa hali ya juu, ujuzi mkubwa wa mafundisho, lugha bora na vitendo vya kupendeza vinaweza kuwa na matokeo makubwa, mradi vyote viwe vinahuishwa na roho ya ibada sana, la sivyo itabaki nini? Hisi zimeridhika, na akili vilevile, lakini utashi haujapenywa na moto wala utomvu. Badala ya kuwa tayari kwa lolote, unajikuta mwoga na dhaifu kama kwanza, ingawa yamesemwa mambo mazuri ajabu, tena kwa ufasaha kamili… Maneno hayo yote mazuri yanayeyuka na kusahaulika, kwa sababu hakuna kilichowasha utashi". Ni lazima mhubiri atakase nia yake ili neno liweze kuzaa matunda ya kudumu milele; aishi kwa sadaka na *kujikana* ili upendo wa Mungu na wa jirani uhakikishiwe nafasi ya kwanza ndani yake.

Tunda la utakaso huo wa utashi ni *amani,* ambayo si furaha daima, ila inaelekea zaidi na zaidi kuwa ya dhati na ya juu, na kuenea hata kwa watu wasiotulia ikiwafanya wamjue na kumpenda Mungu.

Kiutekelezaji, kila mmoja ajiulize: *je, roho ya kujikana inastawi au kufifia ndani mwangu?* Ikiwa majikanio ya nje yamekwisha, maana yake hata ya ndani yametoweka, hatulengi tena ukamilifu, tumekuwa chumvi isiyo na ladha. Tumuombe Bwana atujulishe tunavyozuia kazi yake ndani yetu, pengine bila ya kujitambua; halafu atupe nguvu ya kuondoa vizuio hivyo, na tukiwa walegevu katika kuviondoa, aviondoe mwenyewe. Hapo tutapokea misalaba mingi, lakini yenyewe itatubeba kuliko sisi tunavyoibeba, kama vile ndege anavyoinuliwa na mabawa kuliko kuyainua. Ndiyo njia halisi ya kuingia ufalme wa Mungu.

## 2.11. *KUPONA KIBURI*

Ili tukamilishe tuliyoyasema juu ya kujitakasa, tunapaswa kuzungumzia uponyaji wa maradhi mawili ya roho yanayotuua kwa hakika, yaani kiburi na uzembe.

**MFUMO HALISI WA KIBURI**

"Chanzo cha kiburi ni dhambi; yeye aishikaye atafurika machukizo" (YbS 10:13), kwa kuwa kinazuia kiumbe asimnyenyekee wala kumtii Mungu. Dhambi ya asili ilikuwa ya kiburi: kutaka kujua "mema na mabaya" (Mwa 3:5) ili kujiongoza badala ya kutii. Wengi wanadanganyika, kimawazo au walau kimatendo, kuhusu mfumo wa kiburi, na hivyo wanakubali unyenyekevu wa bandia, ambao ni kiburi kilichofichika, cha hatari kuliko kile cha wazi kinachokuja kutia aibu. Ni kwamba kiburi hakipingani tu na *unyenyekevu,* bali pia na *moyo mkuu* ambao mara nyingi unachanganywa nacho. Pengine tunahitaji kipaji cha shauri ili tusidhani moyo mkuu wa wengine ni kiburi, wala utovu wetu wa moyo ni unyenyekevu halisi.

Kiburi ni *hamu isiyoratibiwa ya ukuu:* mwenye kiburi anataka kuonekana bora kuliko alivyo kuhusu vitu (k.mf. nguvu ya mwili) au mema ya juu (k.mf. akili au maendeleo ya Kiroho). Katika maisha yake kuna uongo: anazingatia mno sifa zake na kasoro za wengine ili kujipandisha juu yao. Kupenda hivyo ukuu ni kinyume cha utaratibu wa akili, cha sheria ya Mungu na cha unyenyekevu wa kiumbe asiye kamili mbele ya Mungu. Ni tofauti na hamu halali ya kutenda makuu kulingana na wito wetu. Basi, kiburi ni "hamu ya ukuu mwovu" (Mt. Augustino); kinamfanya mtu amuige Mungu kinyume, asivumilie kuwa sawa na wenzake, bali atake kuwaweka chini yake, badala ya kuishi nao chini ya matakwa ya Mungu. Kwa hiyo kinapingana na unyenyekevu kuliko kinavyopingana na moyo mkuu, ingawa maadili hayo mawili yanafungamana na kukamilishana. Kumbe kiburi na utovu wa moyo ni vilema vinavyopingana.

Kiburi ni kama kitambaa kinachofumba macho ya roho yasione ukweli, hasa ukuu wa Mungu na ubora wa watu kadhaa. Kinatuzuia tusikubali kufundishwa au kuongozwa nao bila ya kubishabisha. *Hivyo kiburi kinapotosha maisha yetu,* kama springi inayokunjuliwa. Kinatuzuia tusimuombe mwanga Mungu, hivyo yeye anatuficha ukweli. Hakuna kitu kinachotuzuia kuliko kiburi cha roho tusizame katika mafumbo. Hivyo kinatuondolea ujuzi halisi wa Mungu katika sala hasa ambayo unyenyekevu unatuandaa kumiminiwa. "Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga" (Math 11:25).

**NAMNA MBALIMBALI ZA KIBURI**

Mt. Gregori Mkuu aliorodhesha ngazi za kiburi: kudhani tumejipatia wenyewe yale tuliyojaliwa na Mungu; kudhani tumestahili yale tuliyozawadiwa; kujivunia mambo tusiyonayo (k.mf. elimu kubwa); kutaka upendeleo na kudharau wengine.

Kwa nadra mtu anapotoshwa na kiburi hata kukanusha uwepo wa Mungu, kukataa katakata kumtii au kupinga mamlaka ya Kanisa kwa uzushi. Kwa kawaida *kimawazo* tunajua kuwa Mungu peke yake ni mkuu na anastahili utiifu wetu. Lakini *kimatendo* tunajithamini mno kana kwamba tungekuwa asili ya sifa njema tulizonazo; tunajipongeza kwa hizo tukisahau tunavyomtegemea Mungu kama asili ya mema yote; tunaziona kubwa kuliko zilivyo; tunafumbia macho kasoro zetu hata tukaziona ni sifa njema. Kwa mfano tunadhani tuna mawazo mapana kwa sababu tunapuuzia majukumu madogomadogo ya kila siku; hivyo tunasahau kwamba ni lazima tuanze kuwa waaminifu katika madogo tuweze kuwa waaminifu katika makubwa pia, kwa vile siku inaundwa na saa kadhaa, saa inaundwa na dakika kadhaa, nayo dakika inaundwa na sekunde kadhaa.

Hayo yote yanatufanya tujipendee na kuwashusha wengine, tukijiona bora kuliko wao hata kama kwa kweli ni kinyume. Dhambi hizo za kiburi, ambazo mara nyingi ni nyepesi, zinakuwa za mauti zikitufikisha kutenda namna inayostahili lawama kubwa.

Mt. Bernardo aliorodhesha matokeo kumi na mawili ya kiburi kikija kustawi: kudadisi, kunena kijuujuu, kufurahi usipofaa, kujivunia yasiyo kweli, kupenda upekee, kuringa, kujiamini kipumbavu, kutokubali makosa, kuficha dhambi kwenye kitubio, kuasi, kujiachia kutenda lolote, kuzoea dhambi hadi kumdharau Mungu.

Tunaweza kutofautisha aina za kiburi kwa kuzingatia mtu anajikuza kwa kitu gani: k.mf. asili yake, utajiri wake, mwili wake, elimu yake au roho ya ibada anayodhani kuwa nayo.

Kiburi cha akili kinafanya wasomi kadhaa wakatae ufafanuzi rasmi wa dogma, au kuzipunguza au kuzipotosha; wengine washikilie mno maoni yao wasikubali kusikia hoja muhimu za maoni tofauti; hatimaye wengine, ingawa wanashika ukweli, wanafurahia hivi uimara wa hakika zao na elimu waliojipatia hata wasiwe tayari kupokea kwa unyenyekevu mwanga mkuu wa Mungu katika sala. "Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi" (1Kor 4:8). Mtu *aliyejaa umimi* atapokeaje zawadi za juu ambazo Mungu anaweza na kutaka kumjalia kwa faida yake na kwa wokovu wa watu?

Kiburi cha roho si kizuio kidogo zaidi. Mt. Yohane wa Msalaba alikizungumzia hivi kuhusu wanaoanza, "Kutokana na hali yao ya kukosa ukamilifu, umotomoto wao wenyewe unakuwa chemchemi isiyotambulikana ya kiburi, kwa maana wanaridhika na matendo yao na kujithamini sana. Ndiyo sababu katika maongezi tunawasikia pengine kutokeza majivuno ya kuchukiza wakianza kujadili masuala ya Kiroho… Wanafurahi zaidi kufundisha kuliko kujifunza; moyoni wanahukumu wale wote wanaoelewa ibada namna tofauti na wao… hata inaonekana kumsikia Farisayo yule aliyedhani kumsifu Mungu kwa kujivunia matendo yake na kumdharau

mtozaushuru… Wanaona kibanzi jichoni mwa ndugu yao lakini si boriti jichoni mwao wenyewe. Ikitokea kwamba viongozi wao wa Kiroho hawakubali roho yao wala mwenendo wao… wanatamka kuwa viongozi hao hawaelewi roho yao tena si watu wa Mungu. Wanajifanya wa pekee kwa jinsi wanavyojitokeza kwa nje kwa kutenda, kupiga kite na kukaa namna za ajabuajabu. Wengi wao wanajitafutia upendeleo na urafiki wa ndani wa muungamishi, jambo linalosababisha wivu na mahangaiko. Wanaweza hata kufikia hatua ya kutothubutu tena kuungama kwa unyofu dhambi zao wakiogopa kupunguza heshima wanayopewa, hivyo wanajitetea badala ya kujishtaki. Pia wana muungamishi maalumu kwa dhambi mbaya, wakati yule wa kawaida anatumiwa tu kumuelezea yaliyo mema. Kutokana na kiburi cha roho, wengine wanaoanza wakianguka huwa wanachukia na kusikitika mno, wanajikasirikia wakidhani kabisa wangepaswa kuwa watakatifu tayari”.

**KASORO ZINAZOTOKANA NA KIBURI**

Kasoro kuu zinazotokana na kiburi ni kujiamini, kutamani vyeo na kujivuna.

*Kujiamini kipumbavu* ni hamu na taraja isiyoratibiwa ya kutenda mambo makuu kuliko nguvu tulizonazo. Tunadhani kwamba tunaweza kusoma na kujibu masuala magumu, hivyo tunayatolea msimamo harakaharaka. Tunadhani kwamba tuna mwanga wa kutosha tujiongoze bila ya shauri la kiongozi wa Kiroho. Badala ya kujenga juu ya unyenyekevu, kujikana na kutekeleza wajibu wa kila nukta hata katika madogo, tunasema juu ya juhudi za kitume au tunatamani kufikia mara ngazi za juu za sala, bila ya kupitia zile za kati, tukisahau kwamba tupo mwanzoni tu na kwamba utashi wetu bado ni dhaifu na umejaa umimi.

Ndipo panapotokea *kutamani vyeo.* Kwa kuwa tunajiamini mno na kujiona bora kuliko wengine, tunataka *kuwatawala,* kwa kuwalazimisha wafuate mafundisho yetu au kwa kuwaongoza. Tunajitafutia vyeo tusivyostahili kwa ajili ya ukuu wetu, si kwa utukufu wa Mungu na faida ya wengine. Jinsi zilivyo nyingi njama na mbinu za siri zinazotokana na tabia hiyo katika mazingira yoyote!

Kiburi kinazaa *majivuno,* yaani kutaka heshima *kwa ajili yetu sisi* badala ya kuielekeza kwa Mungu aliye asili ya mema yote; tena mara nyingi tunaitaka kwa mambo yasiyo na maana (k.mf. kuonyesha elimu kwa kutia maanani mno mambo madogo tunayojua na kudai wengine wawe na msimamo uleule). Majivuno yanazaa kasoro nyingi: *majigambo* ya kuchekesha; *unafiki* unaoficha kilema kwa kinyago cha adili; *ubishi* unaotetea rai fulani kwa mashindano na ukali, ukisababisha daima ugomvi; pia *ukaidi* na lawama kwa wakubwa.

Ni rahisi kuona matokeo ya kutisha ya kiburi kisiposhindwa: mafarakano, chuki na vita vingapi vimezaliwa nacho? Ndicho adui mkuu wa ukamilifu, kwa sababu ni asili ya kasoro zisizohesabika na kinatukosesha neema nyingi: “Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu” (Mith 3:34; Yak 4:6; 1Pet 5:5). Mafarisayo waliokuwa wakisali na kufunga na kutoa sadaka ili waonekane na watu, Bwana alisema juu yao, “wamekwisha kupata thawabu yao” (Math 6:3,5,16). Maisha yanayotawaliwa na kiburi ni tasa, na yanatabiriwa maangamizi yasiporekebishwa mapema.

**TUPONEJE KIBURI?**

Dawa kuu ya kiburi ni kutambua kimatendo ukuu wa Mungu, aliye asili ya mema yote ya kimaumbile na yapitayo maumbile: “Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?” (1Kor 4:7). “Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu watoka kwa Mungu” (2Kor 3:5). “Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema” (Fil 2:13). Mema si mali yetu, bali yanakusudiwa kumtukuza Mungu, asili yake.

Dawa ya kiburi ni kujikumbusha kuwa sisi si kitu, *tumeumbwa* kwa upendo wa bure wa Mungu anayetudumisha kwa hiari, la sivyo tungerudia *utovu wa vyote.* Halafu tukiwa na neema, ni kwa sababu Yesu Kristo ametukomboa kwa damu yake.

Dawa ya kiburi ni pia kujikumbusha kwamba ndani mwetu tuna jambo la chini kuliko hali ya kutokuwepo, yaani *vurugu ya dhambi* na matokeo yake. Tukiwa wakosefu, tunastahili *dharau* na aibu yoyote; ndivyo watakatifu walivyoona, vizuri kuliko sisi.

Hatimaye, tunawezaje kujikuza kwa *stahili zetu* kana kwamba zingetokana nasi tu? Pasipo neema inayotia utakatifu na neema za msaada tusingeweza kutenda lolote la kustahili. *“Mungu akituza stahili zetu anatuza zawadi zake”* (Mt. Augustino).

Hakika hiyo isibaki nadharia tu, bali iongoze matendo yetu. “Mtu mwenye kujijua vema anajidharau wala hapendezwi na sifa za watu… Ukitaka kujua kitu kinachofaa kufunzwa vema, usipende kujulikana, ila uvumilie dharau… Hata ungemuona mtu kutenda dhambi kwa wazi, au kufanya makosa makubwa, si lazima ujione mwema kumshinda yeye; kwa sababu hujui utasimama wima siku ngapi. Sisi sote tu dhaifu; lakini wewe sema hakuna mtu dhaifu kuliko ulivyo… Usione haya kuwatumikia watu wote kwa ajili ya Yesu Kristo, ukaonekane maskini hapa duniani… usitegemee elimu yako… ila uitumainie neema ya Mungu, *mwenye kusaidia wadogo, na kuwashusha wenye kiburi…* Usijione mwema kushinda wengine; kwa kuwa labda Mungu anayejua binadamu kwa ndani kabisa, atakuona wewe mwovu kuliko wao… mara nyingi hapendezwi na mambo yanayopendeza binadamu… Mtu mnyenyekevu ana raha siku zote, bali moyo wa mtu wa majivuno

una wivu na hasira nyingi… Mungu humtunza mtu mnyenyekevu, humuokoa, humpenda, humtuliza. Mungu humuelekea mnyenyekevu, humpa neema nyingi… Mtu mnyenyekevu hufumbuliwa na Mungu mambo yaliyositirika, huvutwa naye, hualikwa naye" (Kumfuasa Yesu Kristo I,2:1-4; I,7:1-3; II,2:2).

Ili tufikie unyenyekevu huo tunahitaji utakaso wa ndani. Ule tunaojipatia hautoshi, mpaka *tutakaswe* na mwanga wa vipaji vya Roho Mtakatifu unaotuondolea kitambaa cha kiburi tuone vizuri undani wetu wa udhaifu na unyonge, pamoja na faida ya aibu na matatizo, hata tuseme, *"Ilikuwa vema kwangu kuwa naliteswa, nipate kujifunza amri zako"* (Zab 119:71). *"Inatufaa kuvumilia upinzani watu wakitudhania vibaya, hata tunapotaka kutenda mema. Mambo hayo yanasaidia unyenyekevu na kutukinga na majivuno"* (Kumfuasa Yesu Kristo I,12:1). Katika matatizo ndipo tunapoweza kujifahamu na kujua tunavyohitaji msaada wa Mungu.

Baada ya kutakaswa hivyo, kiburi na matokeo yake vitajitokeza kidogo zaidi na zaidi. Badala ya kuwaonea *kijicho* wenye sifa kubwa kuliko sisi, tutajiambia kuwa mkono unatakiwa kufurahi kwamba jicho linaona na hivyo kuufaidisha mkono pia. "Kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho" (1Kor 12:26). Basi, katika mwili wa fumbo wa Kanisa, tunapaswa *kufurahia kitakatifu* sifa njema za jirani; hata tusipokuwa nazo, tunafaidika nazo. Tena tunapaswa kufurahia yale yote yanayoweza kuchangia utukufu wa Mungu na wokovu wa watu. Hapo tunarudishiwa unyofu wa kupenya mambo, ambao polepole unatuingiza katika uzima wa ndani wa Mungu.

## 2.12. *KUPONA UZEMBE*

Kati ya mizizi ya dhambi, mmojawapo unapingana moja kwa moja na upendo wa Mungu na furaha inayotokana na bidii katika kumtumikia: kilema hicho kinaitwa uzembe. Ni lazima tukizungumzie ili kukamilisha yale tuliyoyasema kuhusu kujitakasa upande wa utashi.

### UZEMBE NDIO NINI?

Uvivu kwa jumla ni kosa la kuchukia kazi na juhudi, kupoteza muda au walau kutenda kwa ulegevu ambao ni kinyume cha moyo mkuu. Si ule ugumu wa kutenda unaotokana na afya mbaya, bali ni msimamo mbaya wa utashi na wa hisi ambao unaogopa na kukataa jitihada, unataka kukwepa tabu ili kufurahia *utamu wa kukaa tu* bila ya kufanya chochote. Mvivu ni mnyonyaji anayekula jasho la wengine; ni mtulivu akiachwa bila ya kazi, lakini anachukia wanaotaka aifanye. Kilema hicho kinaanza na uzembe katika kazi, halafu kinazidi kusogea mbali na utendaji wowote wa maana.

Ukihusu wajibu wa dini unaitwa *uzembe*: ni huzuni mbaya, ukinaifu wa mambo ya Kiroho unaosababisha yafanywe kwa ulegevu, yafupishwe au yaachwe kwa visingizio mbalimbali. Ndio chanzo cha uvuguvugu. Huzuni hiyo, kinyume cha ile ya majuto, inatulemea kwa kuwa roho yetu inashindwa kuitikia ipasavyo. Hapo tunafikia hatua ya kukubali ukinaifu kwa mambo ya Kiroho, kwa kuwa yanadai juhudi na kazi nyingi juu yetu wenyewe. Roho ya ibada, yaani utayari wa utashi katika kumtumikia Mungu, inatuinua, kumbe uzembe unatufanya tuone nira ya Bwana haibebeki, tukakimbie mwanga wake unaotukumbusha wajibu wetu. *"Kwa macho mabovu ni chukizo mwanga unaoyapendeza yale mazima"* (Mt. Augustino).

Huzuni hiyo, ambayo kwa kiasi kikubwa ni ya kujitakia, si ule ukavu ambao unapatikana katika majaribu ya Kimungu na kuendana na sikitiko halisi la makosa, uchaji wa Mungu kuhusu uwezekano wa kumchukiza, hamu ya ukamilifu na haja ya upweke, umakinifu na sala ya mtazamo mnyofu. Utakaso wa Kimungu wa hisi unatufanya "tusipate ladha wala faraja katika mambo ya Kimungu wala katika kiumbe chochote… ila kwa kawaida tunaendelea kumkumbuka Mungu, tukiogopa hatumtumikii kwa sababu hatuonji ladha katika mambo yake… Ndipo tunapoona kwamba kutohisi chochote na kuwa wakavu hakutokani na ulegevu na uvuguvugu, kwa sababu sifa maalumu ya uvuguvugu ni kutojali kabisa rohoni mambo ya Mungu… umelegea katika utashi na akili, wala haujali suala la kumtumikia Mungu. Kinyume chake, ukavu unaotakasa una *ari ya kudumu* ndani yake; hautulii bali unasikitika kwa kuwa haujitahidi inavyotakiwa katika kumtumikia Mungu" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Kwa maneno mengine, jaribu hilo la Kimungu linatufanya tukose yaliyo ya ziada tu katika roho ya ibada, siyo kiini chake, ambacho ni nia ya kumtumikia Mungu kwa bidii. Kumbe uzembe ni *kupungukiwa kiini chenyewe cha roho ya ibada* kutokana na ulegevu wenye kosa. Katika jaribu hilo la Kimungu tunasikitikia mtawanyo wa mawazo katika sala na kujitahidi kuupunguza. Kumbe katika uzembe tunaupokea, hata mawazo ya bure yakaenea karibu muda wote wa sala kwa kuwa ndivyo tunavyojitakia kwa kiasi kikubwa. Tunafuta utafiti wa dhamiri kwa kuwa unachosha; hatutambui tena makosa yetu na tunazidi kutumbukia uvuguvugu; polepole tabia mbovu tatu zinapata nguvu na kuzaa maovu.

Ukinaifu kwa mambo ya Kiroho ni mbaya, tena ni dhambi kadiri inavyotokana na utashi kwa njia ya ulegevu. "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana… Pendo na lisiwe na unafiki; lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema… kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana; kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu" (Rom 12:1,9,11-12).

"Wanaougua uzembe wanakinai hata mambo bora ya Kiroho; wanayaepa kwa sababu hayawapi faraja

yoyote ya kihisi… Hivyo kwa uzembe hawafuati njia ya ukamilifu, ambapo ni lazima kujikana kwa upendo wa Mungu. Wakivutwa na yanayowapendeza, wanapendelea matakwa yao kuliko ya Mungu. Wangemtaka Bwana akubali madai yao, kwa sababu kinachowasikitisha ni kupaswa kupokea kwa mikono miwili yale yanayompendeza Mungu; wanapoyakubali ni shingo upande… *Wanamshusha Mungu mpaka kwao, badala ya kujiinua hadi kwa Mungu.* Wakinyimwa faraja, wanashughulikia ukamilifu wao kwa uvuguvugu na ulegevu tu. *Wanaukimbia msalaba ingawa ndio chemchemi ya furaha za Kiroho zilizo safi na imara zaidi…* Wakiingia katika njia nyembamba, ambayo Yesu Kristo alisema ndiyo inayoongoza kwenye uzima, wanaona tabu na huzuni tu" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Pengine wanaoacha sala wanajitetea, "Tunapaswa kujinyima utamu wa sala na kukabili ugumu wa masomo au wa kazi". Maneno hayo yakitamkwa na mtu mwenye bidii yana maana hii: "Tunapaswa kujinyima utamu wa sala, hasa faraja za kihisi, na kukabili ugumu wa masomo au kazi ya lazima kwa wokovu wa watu". Kumbe yakitamkwa na mtu anayetaka kuficha uzembe wake hayana maana, kwa kuwa yeye hajinyimi utamu wowote wa sala, kwa sababu hausikii, na anajisingizia kuzuiwa na kazi ambazo kwa kweli ni za juujuu tu na zinampendeza. Mara nyingi uzembe unasababishwa na utendaji mwingi wa kibinadamu tu, usiofanywa kitakatifu, ambapo mtu anajitafutia furaha badala ya Mungu na ya faida ya watu. Hata masomo yasiyoongozwa na upendo wa Mungu na wa jirani ni tasa Kiroho. Hatimaye ni kwamba mara nyingi sala ni kavu: ndiyo sababu ni vigumu kuwaongoza watu wadumu katika maisha halisi ya sala kuliko kuwavuta wasome na kusema juu yake.

**UZITO WA KILEMA HICHO NA MATOKEO YAKE**

Uzembe ukifikia hatua ya kuweka pembeni jukumu la lazima kwa utakatifu na wokovu (k.mf. misa ya Jumapili) ni dhambi ya mauti; ukiacha matendo ya dini yasiyo muhimu hivyo, ni dhambi nyepesi tu, lakini tusipopambana na ulegevu huo, utatuzidi na kutuingiza katika uvuguvugu. Polepole maelekeo mabaya yatachipuka tena na kutaka kutawala, yakijitokeza kwa dhambi nyepesi nyingi za makusudi, zinazoelekeza kutenda dhambi kubwa zaidi. Sawa na upungufu wa damu, ambao ni chanzo cha maradhi ya hatari, uzembe ni mzizi wa dhambi nyingine, kwa sababu "hakuna mtu anayeweza kudumu muda mrefu katika huzuni pasipo furaha yoyote" (Aristotle). Basi, anayekosa furaha ya Kiroho kutokana na uzembe wake, hachelewi kutafuta furaha za chini zaidi.

Matokeo yake ni ya kutisha: *uovu wa moyo,* si tena udhaifu tu; *kinyongo* kwa jirani; *kukosa nia* ya kutekeleza wajibu; *kukata tamaa; usingizi wa roho* unaofikia kusahau amri; hatimaye kutawanyika katika *kutafuta yasiyo halali,* hali inayojitokeza kwa kuzama katika mambo ya nje, kwa njia ya udadisi, usemaji, mahangaiko, ugeugeu na utendaji mwingi usiozaa chochote. Hivyo mtu anaufikia upofu wa roho na udhaifu mkubwa zaidi na zaidi upande wa utashi. Kwa kuteleza kwenye genge hilo wengi wamesahau ukuu wa wito wa Kikristo, na ahadi walizomtolea Mungu.

**TUPONEJE UZEMBE?**

"Tunapaswa daima kukimbia dhambi, lakini kuhusu kishawishi kinachoelekeza kwake, pengine ni vema kukikimbia, pengine ni afadhali kupambana nacho. Tunapaswa kukikimbia ikiwa kukizingatia kunazidisha hatari; ndivyo tunavyopaswa kukimbia kishawishi cha uzinifu… Kinyume chake tunapaswa kupambana nacho ikiwa kulizingatia jambo linalokisababisha kunaondoa hatari inayotokana na kuliona kijuujuu tu. Ndivyo ilivyo kwa uzembe, kwa sababu *kadiri tunavyofikiria mema ya Kiroho tunapendezwa nayo,* na ukinaifu unaotokana na kuyajua kijuujuu tu unakuja kutoweka" (Mt. Thoma wa Akwino).

Basi, tushinde uzembe kwa upendo wa Mungu, kwa utayari wa utashi kumtumikia hata hisi zikiwa kavu. Tuzingatie mema ya milele tuliyoahidiwa. Ili kujipatia roho hiyo ya imani pamoja na juhudi kubwa ya upendo kwa Mungu, *tujifunge kutoa kila siku sadaka fulani katika mambo yale yanayotushinda zaidi* (k.mf. kuamka saa iliyopangwa au kujiweka tayari kutumikia wote). Hatua ya kwanza ndiyo ngumu. Baada ya kujitahidi wiki moja, jambo limeshakuwa rahisi zaidi.

Dawa mojawapo ni *unyofu wa dhati kuhusu nafsi yetu na kwa muungamishi,* utafiti makini wa dhamiri kila siku, *utekelezaji wa mfululizo wa wajibu wetu, uaminifu* katika sala na katika kumtolea Mungu matendo yote. Maadamu hatuna mengi yanayostahili, tumtolee mara nyingi damu azizi ya Yesu na sadaka inayodumu katika moyo wake wa Kimungu.

Hasa sadaka fulani kila siku itafaa kuyarudishia maisha ya Kiroho nguvu na ubora: polepole juhudi halisi itarudi hata pasipo umotomoto wa hisi, ambao tukubali kupungukiwa nao kama malipizi ya makosa yaliyopita. Ni vema pia kupanga matumizi ya kidini ya saa za siku (kwa kuadhimisha vipindi vya liturujia au rozari n.k.) na ya siku za wiki (kufuatana na mafumbo ya imani yaliyo kanuni ya maisha yetu). Hivyo, badala ya kupoteza muda unaokimbia, tutarudi kufaidika nao na kujipatia uzima wa milele. Polepole tutaona tena furaha ya Kiroho aliyozungumzia Mt. Paulo, "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini. Upole wenu na ujulikane na watu wote. Bwana yu karibu. Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Fil 4:4-7).

## 2.13. ***SAKRAMENTI YA KITUBIO***

Tumeona utakaso wa roho unavyopatikana kwa kufisha hisi, matakwa na maoni yetu. Tutaona unavyotokana na sala pia; lakini Mungu ametuandalia njia nyingine nyepesi na zenye nguvu za kututakasa, yaani sakramenti, ambazo zinatenda zenyewe na, tukiwa tayari kwa imani na upendo, zinasababisha neema kubwa kuliko zile tunazoweza kuzipata nje ya sakramenti. Lakini kiasi cha neema kinachosababishwa nazo kinatofautiana: zinakuwa nyingi kadiri misimamo ya wale wanaozipokea ilivyo kamili; na tofauti kati ya wanaopokea sakramenti ileile ni kubwa kuliko tunavyodhani. Sakramenti ya kitubio ni mojawapo kati ya njia bora za utakatifu; basi, tunapaswa kuipokea vema, si kwa mazoea tu, jambo linalopunguza matunda yake. Kwa hiyo ni muhimu kujua namna ya kujiandaa na ya kuungama vizuri pamoja na matunda yake.

**TUJIANDAE VIPI KWA MAUNGAMO?**

Tunapaswa kutafiti dhamiri zetu na kuchochea majuto yetu.

Utafiti wa dhamiri unadai uangalifu mkubwa kadiri makosa ya mtu yalivyo mengi, na ujuzi wake wa hali ya ndani ulivyo mdogo. Lakini wanaotafiti makosa yao kila jioni hawakuti shida kujifahamu vema na hivyo kujihimiza wafanye bidii zote ili kujirekebisha. Watu wa Mungu ambao wanaungama mara nyingi na kujitahidi wajikinge na dhambi nyepesi za makusudi, utafiti wao wa dhamiri unahitaji muda mfupi tu. Wanapaswa kujiuliza: wiki hii kitu gani hakistahili kuandikwa na Mungu katika *kitabu cha uzima?* Katika nini nimekuwa *wa Mungu,* na katika nini nimekuwa *wangu tu* kwa kushindwa na hali ya nafsi, umimi, kiburi n.k.? Tukizingatia hivyo mambo kutoka juu pamoja na kuomba mwanga, tutajaliwa mara nyingi kuona maisha yetu mpaka ndani.

Hapa tutofautishe dhambi za mauti, zile nyepesi ambazo ni za makusudi kwa kiasi kikubwa au kidogo, na makosa ya udhaifu.

Ikiwa mtu anayelenga ukamilifu anatenda *dhambi ya mauti* katika kitambo cha udhaifu, aiungame kwa unyofu na wazi toka mwanzo wa maungamo, bila ya kujaribu kuificha kwa kuitaja katikati ya wingi wa dhambi nyepesi. Ni lazima aeleze idadi, aina na sababu zake, na hasa *ajute* kwa nia imara ya kukwepa siku za mbele sio dhambi zenyewe tu, bali pia nafasi na sababu zake. Kisha kusamehewa, atunze hamu ya *kufidia* kwa maisha magumu na upendo. Dhambi moja ya mauti ikibaki peke yake, na kuungamwa mara na kufidiwa, inaathiri kidogo tu, hivi kwamba mtu anaweza kuendelea kupanda juu kuanzia pale alipoanguka, asilazimike kuanza na moja.

Kumbe *dhambi nyepesi za makusudi* ni kizuio kikubwa cha ukamilifu, hasa zikijirudiarudia kwa kuwa tumeambatana nazo. Ni maradhi halisi yanayodhoofisha roho. Bwana alimuambia Mt. Getruda, "Usiache dhambi izeeke ndani mwako": dhambi nyepesi ya makusudi ni kama sumu ambayo isipotapikwa inaathiri mwili polepole, pasipo kuuua mara. Kwa mfano tusitunze *kwa hiari* kinyongo, wala kushikilia maoni na matakwa yetu, wala mazoea ya kusengenya au kuhukumu pasipo msingi, wala mapendo ya kibinadamu yanayoweza kuwa mtego kwetu na kutuondolea uhuru na juhudi za roho kumuelekea Mungu. Tukimnyima sadaka hizo anazotudai, hatuwezi kutarajia toka kwake neema zinazofikisha kwenye ukamilifu. Basi tuungame wazi dhambi nyepesi *za makusudi,* hasa zile zinazotutia aibu zaidi. Tutafute sababu zake na kukusudia kuziepa; la sivyo ukamilifu umeacha kuwa lengo halisi kwetu. Hilo ni jambo la msingi.

Kuna dhambi nyingine tunazozitenda *kwa hiari kiasi,* bila ya kufikiria zaidi, zinazochangiwa na mishtuko na misukumo ya nafsi, ingawa utashi umeambatana nazo. Zikitokea mara nyingi ni ishara ya kwamba tunapambana kwa ulegevu, pasipo nia ya kuondoa vizuio vyote.

Kuhusu *makosa ya udhaifu,* utashi unahusika nayo kidogo: unayaelekea kwa muda mfupi, halafu unajilaumu. Makosa hayo hatuwezi kuyaepa yote (walau mfululizo); ila tunaweza kupunguza idadi yake. Si kizuio kikubwa kwa ukamilifu, kwa kuwa yanarekebishwa mapema. Lakini inafaa kuyataja kwenye kitubio ili usafi wa roho ukamilike.

*Matendo mapungufu* yanatofautiana nayo kwa kuwa ni *upungufu tu wa juhudi* za kumtumikia Mungu. Lakini, ikiwa kinadharia ni rahisi kubainisha, kiutekelezaji ni vigumu kusema upungufu wa juhudi unaishia wapi na dhambi ya uzembe inaanzia wapi. Tena, anayelenga kweli ukamilifu, *hatakiwi kulegeza mwendo, sio tu kukwepa asirudi nyuma tu.* Zaidi ya hayo, matendo mapungufu yanatuelekeza kutenda dhambi nyepesi kwa kuwa hatupambani na maelekeo ya umimi kwa nguvu zinazotakiwa.

**TUUNGAMEJE?**

Maungamo yafanywe kwa imani kubwa, tukikumbuka padri yupo mahali pa Bwana. Ni *hakimu* (kwa kuwa sakramenti hiyo inatolewa kama hukumu: *"nakuondolea"),* lakini pia ni *baba wa Kiroho* na *mganga* anayeonyesha kwa wema dawa, mradi tumueleze vizuri maradhi yanayotusumbua. Kwa hiyo haitoshi *tujishtaki* kijuujuu kwa namna isiyomfumbulia kitu, k.mf. "nimetawanya mawazo wakati wa sala". Bali tuseme, "nimetawanya mawazo hasa kwa uzembe wakati wa ibada fulani: nimeianza vibaya, pasipo kujikusanya kwanza, au sikupambana na mawazo yaliyotokana na kinyongo au mapendo ya kibinadamu au masomo". Ni vema tukumbuke maazimio tuliyowahi kuyaweka, halafu kusema kama hatujayatimiza sawasawa.

Hasa tuchochee *majuto* yetu na kuweka *azimio la kufaa* ambalo litokane nayo. Kwa ajili hiyo, tufikirie sababu za kutubu. Tuombe neema ya kuelewa vema kuwa dhambi, hata nyepesi, ni chukizo kwa Mungu, kwa kuwa inapinga matakwa yake; ni pia *utovu wa shukrani* kwa Baba aliye mwema kuliko wote (utovu mbaya kadiri alivyotujalia neema) ambao tunamnyima furaha ya ziada inayotupasa kumpatia. Makosa yetu yamefanya kichungu zaidi kikombe ambacho Bwana alipewa katika mateso, naye anaweza kutuambia, "Aliyetukana si adui; kama ndivyo, ningevumilia. Aliyejitukuza juu yangu siye anichukiaye; kama ndivyo, ningejificha asinione. Bali ni wewe, mtu mwenzangu, rafiki yangu, niliyejuana nawe sana. Tulipeana shauri tamu" (Zab 55:12-14). Ndiyo sababu halisi ya kutubu upande wa Mungu.

Upande wetu ipo nyingine: dhambi nyepesi, ingawa haipunguzi upendo, inauondolea umotomoto, uhuru wa kutenda na uenezi. Inafanya urafiki na Mungu usiwe wa ndani na mtendaji zaidi. Kupoteza urafiki na mtakatifu ni hasara kubwa; lakini kupoteza *urafiki wa ndani na Mwokozi* hakuna kifani. Halafu dhambi nyepesi, hasa ya makusudi, inaotesha upya maelekeo mabaya na hivyo kutuandaa tutende dhambi ya mauti; na katika mambo kadhaa, mvuto wa anasa unatuvusha haraka mipaka kati ya dhambi nyepesi na ya mauti.

Kitubio kikiadhimishwa hivyo, kwa nguvu ya maondoleo na kwa mashauri ya padri, kitakuwa chombo kikubwa kwa utakatifu. M.H. Anjela wa Foligno alipotambua dhambi zake kwa mara ya kwanza alishikwa na hofu kubwa kwa wazo la maangamizi ya milele aliyostahili, akalia machozi mengi, lakini kwa aibu hakuziungama, na hata hivyo akasogea meza ya Bwana: "Nikiwa na dhambi zangu niliupokea Mwili wa Yesu Kristo. Lakini usiku na mchana dhamiri yangu haikuacha kamwe kulalamika. Nikamuomba Mt. Fransisko anikutanishe na muungamishi wa kunifaa, ili aweze kunielewa, nami niweze kujifunua kwake… Nikaungama inavyotakiwa na kuondolewa dhambi. Sikuona upendo kabisa, ila uchungu, aibu na sikitiko. Nikadumu kufanya malipizi niliyopewa nikijitahidi kulipa haki, huku najikuta sina kabisa faraja, ila nimejaa uchungu. Halafu nikaanza kuzingatia huruma ya Mungu na kuifahamu hiyo iliyonitoa motoni na kunijalia neema ninayosimulia. Nikapata mwanga wake wa kwanza; uchungu na machozi vikazidi maradufu. Nikajiachia kufanya malipizi makali… Kwa mwanga huo ndani mwangu nikaona nina dhambi tu, nikatambua kwa hakika nimestahili moto wa milele… Faraja yangu pekee ilikuwa kulia machozi. Mwanga mpya ukanionyesha kwa undani ukuu wa dhambi zangu. Ndipo nilipoelewa kwamba, kwa kumchukiza Muumba nilivichukiza viumbe vyote pia. Kwa maombezi ya bikira Maria na ya watakatifu wote nikaiitia huruma ya Mungu; nikijisikia mfu nikaomba uhai huku nimepiga magoti… Ghafla ikanitokea nijisikie kufikiwa na huruma ya viumbe vyote na watakatifu wote. Hapo nikapokea zawadi, yaani moto mkali wa upendo na uwezo wa kusali jinsi nisivyowahi kamwe… Nikajaliwa ujuzi mkubwa wa jinsi Yesu Kristo alivyokufa kwa dhambi zangu. Nikang'amua ukatili wa dhambi zangu, *nikatambua kuwa aliyemsulubisha ni mimi mwenyewe.* Ila nilikuwa sijapata kuelewa ukuu usio na mipaka wa faida ya msalaba… Halafu Bwana, kwa wema wake, akanitokea mara nyingi, katika usingizi na katika kukesha, akiwa daima msalabani na kuniambia, *Tazama, tazama madonda yangu!* Alikuwa akihesabu mapigo ya mijeledi na kuendelea kuniambia, *Ni kwa ajili yako, kwa ajili yako, kwa ajili yako…* Nikawasihi bikira Maria na mtume Yohane waniombee nipate mateso ya Yesu Kristo, walau yale waliyojaliwa kushirikishwa. Wakanipatia fadhili hiyo, hata siku fulani Mt. Yohane akanishirikisha kiasi kwamba siku hiyo ikawa mojawapo kati ya zile za kutisha zaidi za maisha yangu… Mungu akaandika *Baba Yetu* moyoni mwangu kwa msisitizo mkubwa wa wema wake na wa unyonge wangu hata siwezi kutamka silabi moja". Kwa majuto hayo Anjela alishika njia ya utakatifu. Neema kubwa alizojaliwa zituvute kuzingatia misaada ambayo Bwana anatutolea kila siku, na makuu yaliyomo katika maisha ya Kikristo ya kawaida.

**MATUNDA YA KITUBIO**

Ni matunda ya maadili ya unyenyekevu na toba, na hasa ya maondoleo. Tendo gani la *unyenyekevu* ni halisi na la lazima kuliko lile la kukiri kwa unyofu makosa tuliyotenda? Ndiyo dawa ya kiburi, kilicho asili ya dhambi zote. Ndiyo sababu uzushi, ambao ni tunda la kiburi, umefuta kitubio. Dhambi za kiburi zinaanza kufidiwa tayari na maungamo manyenyekevu. Tendo la *toba,* yaani majuto, linalaumu na kukataa dhambi iliyotendwa kwa kuwa inamchukiza Mungu. Hivyo mtu anamrudia Bwana wake, ambaye alimuacha kwa dhambi ya mauti, au walau alisogea mbali naye kwa dhambi nyepesi. Anamkaribia tena na kujitupa kwa upendo na tumaini mikononi mwa huruma yake. Hasa kwa maondoleo *damu ya Mwokozi* inamwagwa kisakramenti juu ya roho yetu. Mprotestanti, kama ametenda dhambi zisizomuacha atulie, hapati kamwe faraja ya kumsikia mtumishi wa Mungu akimuambia kwa niaba yake, *"Nakuondolea dhambi zako".* Hapati faraja ya kuona anavyohusika na neno la Mwokozi kwa mitume wake, *"Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa"* (Yoh 20:23). Kumbe katika sakramenti damu azizi ni kama dawa bora ambayo, ikiunganisha nguvu yake na unyenyekevu na toba, inaondolea dhambi, na kuchangia uponyaji kamili wa roho. "Kwa njia ya kitubio hampati tu maondoleo ya dhambi nyepesi, bali pia nguvu kubwa ya kuziepa siku za mbele, mwanga mkali kwa kuzitambua, na wingi wa neema kwa kufidia hasara zote zilizosababishwa nazo" (Mt. Fransisko wa Sales).

Lakini matokeo ya maondoleo *yanalingana daima na ubora wa misimamo* ambayo sakramenti inapokewa, kwa kuwa kati ya watu wanaoungama Mungu anang'amua tofauti ambazo hakuna anayeweza kuzihisi. Kuna viwango vingi vya unyenyekevu, majuto na upendo wa Mungu, kama viwango vya joto la mwali. Hiyo ni

kweli pia kuhusu *malipizi ya sakramenti,* ambayo yana thamani kuliko mengine kwa kuwa matokeo yake yanategemea sakramenti, lakini kipimo chake kinategemea juhudi katika kuyafanya, hivyo yanatuondolea kwa kiasi tofauti adhabu tuliyostahili kwa dhambi tulizoondolewa. Kwa hiyo tusiahirishe malipizi, bali tuwahi kuyafanya na kumshukuru Mungu kwa maondoleo. Damu ya Yesu imetiririka rohoni mwetu ili kuitakasa; tumuombe tudumu mpaka kufa katika hali ya neema. Watakatifu tu wanajua thamani ya damu yake. Jinsi ilivyo kubwa neema ya kuangaziwa vilindi vya fumbo la ukombozi!

Hatimaye inafaa tujishtaki walau kwa jumla kuhusu *dhambi za zamani,* kwa kuzifikiria zile kubwa zaidi, ili tuzidi kuzijuta na kusudi stahili za Yesu, zikihusishwa na dhambi hizo zilizokwishaondolewa, zipunguze adhabu ya muda ambayo kwa kawaida inatupasa bado. *"Ni nani awezaye kuyatambua makosa yake? Unitakase na mambo ya siri"* (Zab 19:12), ambayo yanategemea hiari kiasi, kutokana na uzembe wangu katika kujua na kutaka yale yanayonipasa niyajue na kuyataka.

Bwana alimuambia Mt. Veronika Giuliani, "Utaendelea katika ukamilifu kadiri utakavyochuma matunda ya sakramenti hii". Mt. Fransisko wa Sales ametushauri, "Muwe makini sana… kusikiliza rohoni mwenu maneno ya maondoleo ambayo Mwokozi wa roho zenu anatamka kutoka juu mbinguni wakati uleule ambao mtumishi wake anawaondolea hapa duniani kwa niaba yake… Hakuna tabia ngumu kiasi kwamba isiweze kutawaliwa na kurekebishwa, kwanza kwa neema ya Mungu, halafu kwa juhudi na bidii. Katika hayo mfuate maagizo na mwenendo wa kiongozi aliyejaa ari na busara". Mtakatifu huyo aling'amua kuwa majuto halisi hayakatishi tamaa kamwe, bali ni huzuni takatifu ambayo inaweka roho tayari kwa bidii, na kuinua moyo kwa sala na tumaini, hata uruke kwa ari: "katika ukubwa wa uchungu wake inazaa daima utamu wa faraja isiyo na kifani". Ikiwa huzuni ya majuto ina *utamu* huo, ni kwa sababu inatokana na *upendo.* Kadiri tunavyoona uchungu kwa makosa yetu, tuna hakika ya kumpenda Mungu. Katika huzuni hiyo yanapatikana matunda ya Roho Mtakatifu: "upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" (Gal 5:22-23).

## 2.14. ***KUSHIRIKI MISA, CHEMCHEMI YA UTAKATIFU***

Utakatifu unapatikana katika kuungana na Mungu kwa undani zaidi na zaidi kwa njia ya imani, tumaini na upendo. Kutokana na ukweli huo, chombo kikuu kimojawapo ni kushiriki misa, tendo bora la adili la ibada na la liturujia ya Kikristo. Misa inatakiwa kuwa kila asubuhi *chemchemi kuu* ya neema zinazohitajika mchana kutwa, chemchemi ya mwanga na joto upande wa roho, kwa mfano wa pambazuko la jua ambalo, baada ya usiku na usingizi ulio mfano wa kifo, ni kana kwamba linavirudishia uhai vyote vinavyoamka duniani. Tungeelewa kwa undani thamani ya misa tungeona inavyotengeneza upya na kudumisha na kustawisha uzima wa Mungu ndani mwetu. Kumbe mara nyingi mazoea ya kushiriki sadaka takatifu kwa imani haba yanafanya tendo hilo liwe la kawaida, tusipate matunda yale yote yanayotarajiwa. Hilo liwe *tendo kuu la siku yetu yoyote,* hivi kwamba matendo mengine yote yawe *ya kulisindikiza tu,* hasa sala nyingine na sadaka ndogondogo tunazopaswa kumtolea Bwana mfululizo.

### MOYO WA KRISTO KUJITOA KWA KUDUMU

Ubora wa misa unatokana na kwamba kwa dhati ni sadaka ileile ya msalabani, kwa sababu *kuhani yuleyule* ndiye anayeendelea kujitoa kwa njia ya watumishi wake, na *kafara ileile* ndiyo inayotolewa kwa kuwepo kweli altareni. Tofauti ni namna ya kuitoa tu: huko Kalivari ilitolewa kwa kupokea ukatili, kumbe katika misa *inatolewa kisakramenti* kwa njia ya mageuzo mawili yanayotenganisha Mwili na Damu ya Mwokozi, ingawa si kimwili.

Sadaka hiyo ni *ishara* ya Yesu kujitoa moyoni, na ni ukumbusho wa sadaka aliyoitoa Kalivari kwa kupokea ukatili. Sadaka hiyo ya Neno wa Mungu aliyefanyika mwili, ingawa inatolewa kisakramenti tu, ina *uzito* mkubwa kuliko ile ya mwanakondoo wa Pasaka na nyingine zote za Agano la Kale. Kwa kuwa ishara ina thamani kulingana na ukuu wa jambo inaloashiria: bendera inayotukumbusha nchi yetu, hata kama imeshonwa kwa kitambaa cha kawaida, kwetu ina thamani kuliko vitambaa vyovyote vile. Sadaka za Agano la Kale zilikuwa mifano ya mbali ya ile ya msalabani, kumbe ekaristi inatokeza kule *kujitoa kwa ndani* kunakodumu katika moyo wa Kristo. Kiini hicho cha misa kina *thamani isiyo na mipaka* kutokana na Nafsi ya Kimungu ya Neno aliyefanyika mwili, aliye kuhani mkuu na kafara.

"Mnapomuona altareni mtumishi wa Mungu akiinua hostia takatifu kuelekea mbinguni, msidhani mtu huyo ndiye kuhani halisi, bali mkiinua mawazo yenu juu kuliko yanayogusa hisi, mzingatie mkono wa Yesu Kristo unaojinyosha bila ya kuonekana" (Mt. Yohane Krisostomo). Padri tunayemuona hawezi kupenya fumbo hilo mpaka ndani, lakini juu yake vipo akili na utashi wa Yesu, kuhani mkuu. Ikiwa mtumishi si daima anavyotakiwa kuwa, kuhani mkuu ni mtakatifu tu. Ikiwa mtumishi, hata kama ni mwema, anaweza akapitiwa kidogo au akazingatia taratibu za ibada kuliko maana yake, juu yake yupo asiyepitiwa, naye anamtolea Mungu kwa ujuzi kamili ibada ya fidia, dua na shukrani ambayo ina thamani na upana pasipo mipaka.

Huku kujitoa kwa kudumu ni *mwendelezo* wa Yesu kujitoa sadaka maisha yake yote, kuanzia alipoingia ulimwenguni na hasa msalabani. Alipokuwa duniani sadaka hiyo ilikuwa na stahili; sasa inaendelea pasipo stahili, kama *ibada ya fidia na dua* ili kutugawia stahili za msalabani. Baada ya ulimwengu kwisha, hakutakuwa tena na misa wala sadaka halisi, ila utimilifu wake: Kristo ataendelea kujitoa kwa ndani kwa

Baba si kama fidia na dua, bali kama *ibada na shukrani.* Wimbo wa "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu" unatufanya tuhisi kidogo ibada ya milele. Tungejaliwa kuona moja kwa moja upendo unaomfanya Kristo ajitoe kwa kudumu tungeshangaa mno! "Sina dhana tupu, bali hakika kabisa ya kwamba roho ingeona na kutazama kwa dhati kiasi fulani cha uangavu wa ndani wa sakramenti ya altare, ingewaka moto kabisa, kwa kuona upendo wa Mungu. Naona kwamba wanaotoa sadaka au kuihudhuria wanatakiwa kutafakari kwa dhati ukweli mkuu wa fumbo takatifu mno, ambalo tuzame ndani yake na kutulia tusigeuke" (M.H. Anjela wa Foligno).

**MATOKEO YA SADAKA YA MISA NA MISIMAMO YETU YA NDANI**

Yesu Kristo kujitoa kwa dhati, ambako ndiko kiini cha sadaka ya ekaristi, kuna *malengo yaleyale* na matokeo yaleyale ya sadaka ya msalabani, lakini ni lazima tutofautishe matokeo yanayomhusu Mungu na yale yanayotuhusu sisi. Matokeo ya misa yanayomhusu Mungu moja kwa moja yanapatikana daima *kwa hakika na kikamilifu* pasipo haja ya mchango wetu, hata akiadhimisha padri asiyestahili, kwa kuwa sadaka hiyo inampendeza Mungu kuliko dhambi zote pamoja zinavyomchukiza. Kumbe matokeo *yanayotuhusu wenyewe* yanapatikana tu *kadiri ya misimamo yetu ya ndani.*

Hivyo misa kama sadaka ya *upatanisho* inawapatia wakosefu wasiokaidi (hasa wale wanaoihudhuria au wale ambao inatolewa kwa ajili yao) neema inayowafanya watubu na kuamua waungame, kama sadaka ya msalabani ilivyomsababishia mwizi mwema. Misa kama sadaka ya *fidia* inawaondolea waliotubu, kadiri misimamo yao ilivyo kamili, walau sehemu ya *adhabu za muda* zinazowapasa kutokana na dhambi. Ndiyo sababu inatolewa kwa kukomboa roho za toharani. Hatimaye misa kama sadaka ya *dua* inatupatia neema zote tunazohitaji kwa utakatifu. Ndiyo sala kuu ya Kristo aliye hai daima, sala ambayo haikomi bali inaongozana na ile ya Bibi arusi wake. Matokeo yake yanalingana na ari yetu, hivyo anayejiunga nayo vizuri ana hakika ya kupata neema kwa wingi kwa ajili yake na ya wapendwa wake.

Ndiyo sababu watakatifu, waliojaa vipaji vya Roho Mtakatifu, walikuwa wakijikokota kuihudhuria misa hata wasipojiweza kwa ugonjwa. Wengine walikuwa wakitokwa na machozi ya upendo au kujisahau wakati wa misa. Wengine walimuona Bwana mwenyewe badala ya padri. Wengine waliona damu kufurika kutoka kikombeni na kutiririkia mikono ya padri na hekalu, wakati malaika wanaikinga kwa vikombe vya dhahabu ili kuifikisha popote walipo wenye kuhitaji wokovu.

**TUNAVYOWEZA KUJIUNGA NA SADAKA YA EKARISTI**

Maneno ya Mt. Thoma wa Akwino kuhusu sala ya midomo yanafaa kwa jambo hilo pia: "Unaweza kuelekea ama maneno ili kuyatamka vema, ama maana ya maneno, ama lengo la sala, yaani Mungu na jambo tunaloliomba… Uzingatifu huo wa mwisho, ambao hata watu wanyofu wasio na elimu wanaweza kuwa nao, pengine ni mkubwa hivi hata roho ni kana kwamba inainuliwa kwa Mungu na kusahau mengine yote". Vilevile kuna namna mbalimbali za kushiriki misa kwa imani, tumaini na upendo. Tunaweza kuzingatia sala za liturujia, ambazo ni nzuri ajabu na katika usahili wake zinatokeza mawazo makuu. Tunaweza kuzingatia Pasaka ya Bwana, ambayo misa ni ukumbusho wake hai, tukijiona chini ya msalaba pamoja na Maria na Yohane. Tunaweza pia kumtolea Mungu, pamoja na Yesu, malengo manne ya sadaka, yaani ibada, fidia, dua na shukrani. Tunaweza kufaidika na misa mradi tusali, hasa tukijisikia kuvutwa na upendo safi wa nguvu, kidogo kama Mt. Yohane alipoegemea moyoni pa Yesu.

Kwa vyovyote tusisitize tunavyopaswa *kuungana kwa dhati na Mwokozi katika kujitoa,* tukimtoa kwa Baba yake na *kujitoa wenyewe* kila siku vizuri zaidi, hasa kwa tabu na matatizo, anavyosema padri wakati wa matoleo, "Ee Bwana, utupokee sisi tunaokunyenyekea na kutubu moyoni". Katika Kumfuasa Yesu Kristo, Bwana anasema, "Kwa ajili ya dhambi zako nimejitoa kwa Mungu Baba kwa hiari yangu, nikinyosha mikono msalabani na mwili uchi… Vivyo hivyo inafaa na wewe ujitoe kwangu kwa hiari yako kama sadaka safi na takatifu, kila siku katika misa, kwa nguvu zako zote… Siombi zawadi yako, nakutaka mwenyewe tu" (IV,8:1-2). Halafu mfuasi anajibu, "Bwana wangu, katika unyofu wa moyo najiweka leo mikononi mwako niwe wako siku zote, nikutumikie, niwe sadaka ya utukufu wako daima. Unipokee nikijitoa pamoja na mwili wako mtakatifu" (IV,9:1).

Kutembelea sakramenti kuu kutukumbushe misa na kuwa katika tabenakulo, hata kama hakuna sadaka halisi (kwa sababu inakwisha pamoja na misa), Yesu yumo kweli akiendelea kuabudu, kutuombea na kushukuru. Kila saa tuungane naye katika kazi hiyo. Kwenye tabenakulo tunyamaze ili tumsikilize, tujisahau ili tuzame ndani mwake.

## 2.15. *KOMUNYO TAKATIFU*

Anayelenga ukamilifu wa Kikristo anatakiwa kuishi zaidi na zaidi kwa ekaristi, sio tu kwa kuhudhuria misa, bali hasa kwa kuipokea mara nyingi, hata kila siku. Kwa ajili hiyo tuseme juu ya mkate wa uzima na juu ya masharti ya kuupokea vema, halafu motomoto.

**EKARISTI NDIYO MKATE HAI KUTOKA MBINGUNI**

Bwana hakuweza kujitoa kwa wokovu wa wote jumla kuliko alivyojitoa msalabani, na sasa hawezi kujitoa kwa kila mmojawetu kuliko anavyojitoa katika ekaristi. Akijua mahitaji yetu, alituahidia, "Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe… Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu… Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake" (Yoh 6:35,51,55-56).

Ekaristi ndiyo sakramenti kuu, kwa sababu ndani mwake haimo neema tu, bali yumo aliyetustahilia neema. Ndiyo sakramenti ya upendo, kwa kuwa ni tunda la upendo unaojitoa, na tokeo lake kuu ni kustawisha ndani mwetu upendo wa Mungu na wa watu. Kuipokea kunaitwa "komunyo" (= ushirika) yaani muungano wa ndani na Mungu na watu *unaolisha* roho na kuihuisha Kimungu zaidi na zaidi; kwa namna fulani *unaifanya iwe ya Kimungu* kwa kustawisha neema inayotia utakatifu.

Kila kiumbe hai kinahitaji lishe: mimea inajilisha rutuba ya ardhi; wanyama wanajilisha mimea au viumbe vingine; binadamu analisha mwili wake kwa vyakula vya kufaa, na anatakiwa kulisha akili yake kwa ukweli, hasa wa Kimungu, tena utashi wake kwa matakwa ya Mungu anayopaswa kuyatekeleza kila siku ili kufikia uzima wa milele. Kwa maneno mengine, anatakiwa kujilisha imani, tumaini na upendo; matendo ya maadili hayo yanamstahilisha *ustawi* wa uzima upitao maumbile. Lakini Mwokozi anamtolea chakula kingine, cha Kimungu zaidi: anajitoa kuwa chakula alivyomuambia Mt. Augustino, "ndimi chakula cha wenye nguvu; kua unile. Lakini hutanigeuza ndani mwako unavyogeuza chakula cha mwili wako; kinyume chake wewe utageuzwa ndani mwangu". Katika ushirika huo Mwokozi hapati faida yoyote, ila mwamini anapata kuhuishwa Kimungu. Maadili ya Yesu yanamuingia awe kiungo hai zaidi cha mwili wake wa fumbo. Hasa Yesu aliyemo katika ekaristi anamfanya ampende Mungu kwa usafi na nguvu zaidi.

"Matokeo yale ambayo mateso ya Kristo yalisababisha ulimwenguni, sakramenti hii inayasababisha ndani ya kila mmojawetu… Kama vile chakula cha kawaida kinavyotegemeza uhai wa mwili na kuuongeza na kuuburudisha na kupendeza kwa ladha, ekaristi inasababisha matokeo ya namna hiyo rohoni" (Mt. Thoma wa Akwino). Kwanza *inategemeza:* mtu ambaye upande wa mwili hajilishi au anajilisha vibaya anadhoofika; inatokea vilevile upande wa roho asipokula mkate upitao maumbile anaopewa na Bwana kama chakula bora cha kila siku. Kama vile chakula cha kawaida *kinavyoburudisha* mwili kwa kufidia ulichopoteza kwa ugumu wa kazi, ekaristi inafidia nguvu zilizopungua kutokana na uzembe wetu: inatuondolea dhambi nyepesi na kuturudishia ari iliyopotea kwa dhambi hizo, pia inatukinga na dhambi ya mauti. Chakula cha kawaida *kinakuza* uhai wa mtoto anayetakiwa kuwa mtu mzima. Upande wa roho, tunapaswa kukua daima katika upendo hadi kufa kwetu: hivyo tu tunazidi kuelekea uzima wa milele. Mkate wa ekaristi unatuletea neema mpya daima kwa ajili ya ustawi huo; ndani ya watakatifu, kila siku imani inakuwa angavu na hai zaidi, tumaini linakuwa imara na upendo safi na motomoto zaidi na zaidi. Polepole, badala ya kuvumilia tu mateso wanakuja kuthamini na kupenda msalaba. Kwa komunyo maadili yanakua pamoja hata kufikia ushujaa, na vipaji vya Roho Mtakatifu vinastawi pamoja nayo. Hatimaye, kama vile chakula cha kawaida *kinavyonoga,* mkate wa ekaristi ni mtamu kwa mtu mwaminifu anayechota ndani yake faraja na hisi ya kuwa na afya.

"Kwa kutegemea wema wako na huruma yako kubwa, Ee Bwana wangu, nathubutu kukujongea; mimi mgonjwa nakujia wewe Mwokozi wangu, mimi mwenye njaa na kiu nakutafuta asili ya uzima… mimi niliye kiumbe nakujia Muumba, katika majonzi nakujia wewe mtuliza wangu mwema… Ukijitolea kwangu imenitosha; kama hupo sipati kutulia. Siwezi kukaa mbali nawe; sina uhai nisipokuona" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,2:1; IV,3:2). *"Jambo la ajabu! Mtu maskini, mtumishi na mnyonge anamla Bwana!"* (Mt. Thoma wa Akwino). Kumbe mara nyingi mazoea yanatuzuia tusizingatie uangavu wa Kimungu wa zawadi hiyo isiyo na kifani!

**MASHARTI YA KUPOKEA VEMA**

Masharti hayo yanatajwa katika hati ambayo Mt. Pius X aliwahimiza waamini wote kupokea ekaristi mara nyingi: "Tunapaswa kujitahidi tutangulize maandalizi mema kabla hatujapokea, halafu kutoa shukrani kwa namna ya kufaa, kulingana na uwezo na hali ya kila mmoja". Kadiri yake sharti la kwanza ni *nia nyofu:* "anayeikaribia meza takatifu asiende kwa mazoea tu, kwa majivuno au kwa sababu nyingine ya kibinadamu, bali atake kumtimizia Mungu hamu yake, kuungana naye kwa dhati kwa njia ya upendo, na kuponya maradhi yake na kasoro zake kwa dawa hiyo ya Kimungu". Mtu akiwa na nia nyingine pamoja na hiyo ya kwanza (k.mf. hamu ya kusifiwa) komunyo inabaki njema, lakini matunda yanapungua. Komunyo moja motomoto ina faida kuliko nyingi vuguvugu.

**MASHARTI YA KOMUNYO MOTOMOTO**

Mt. Katerina wa Siena alitumia mfano wa watu wanaotafuta mwanga kwa mishumaa yenye ukubwa tofauti, ambayo mkubwa unaangaza kuliko mdogo. Inatokea vilevile kwa sakramenti hii, ambayo matunda yake yanalingana na *hamu takatifu* ya kila anayeikaribia. Hamu hiyo inajitokeza hasa kwa *kukomoa*

*mshikamano wowote na dhambi nyepesi.* Mshikamano huo unastahili lawama ndogo kwa Wakristo wenye ujuzi mdogo kuliko kwa wale waliopokea zaidi. Ikiwa huo uzembe na utovu wa shukrani unaongezeka, unafanya komunyo ilete faida ndogo zaidi na zaidi. Ili hiyo iwe motomoto *tusishikamane na matendo mapungufu,* yaani kutenda bila ya ukamilifu, kutopambana kwa nguvu na kasoro zetu, na kujitafutia maburudiko halali yasiyo ya lazima (k.mf. kinywaji). Kujinyima hayo kunampendeza Mungu, naye Mkristo kwa kujifanya mkarimu zaidi anazidi kujaliwa neema katika komunyo. Kielelezo chetu ni Mwokozi *aliyejitoa sadaka* hadi msalabani, nasi tunapaswa kuufanyia kazi wokovu wetu na wa wenzetu kwa njia zilezile za Yesu.

Kujitenga na dhambi nyepesi na matendo mapungufu ni msimamo wa kutotenda; misimamo *ya kutenda* ni: unyenyekevu *(Bwana, sistahili),* heshima kwa ekaristi, imani hai, hamu ya kumpokea Bwana, ambayo yote inajumlishwa katika neno moja: *kuwa na njaa ya ekaristi.* Tukiwa na njaa, kila chakula ni kitamu; tukiwa na njaa ya ekaristi kwa kuamini ndiyo chakula cha lazima kwa roho yetu, komunyo italeta matunda mengi. Ikiwa njaa imetuishia, tunapaswa "kufanya mazoezi" ili kuipata tena; upande wa roho mazoezi ni kumtolea Mungu *kila siku sadaka fulani,* hasa kujikana badala ya kujipendea katika yote. Polepole umimi utatoweka, na *upendo utatawala* bila ya pingamizi; tutaacha kuhangaikia mambo madogo yanayotuhusu ili tuzingatie zaidi utukufu wa Mungu na wokovu wa watu. Hapo njaa ya ekaristi itaturudia.

Kwa walio dhaifu tunatafuta chakula cha kufaa kuwarudishia nguvu. Basi, tutafute pia kinachofaa zaidi kutengeneza upya nguvu za roho. Hisi zetu zinazoelekea tamaa na uvivu zinahitaji kuhuishwa kwa kugusa mwili safi wa Kristo uliostahimili mateso makali kwa upendo. Roho yetu, inayoelekea kiburi, upumbavu, kutojali na kusahau kweli kuu, inahitaji kuangazwa na mguso wa akili angavu ya Mwokozi. Utashi wetu unakosa nguvu, ni baridi kwa kupungukiwa upendo; nani anaweza kuurudishia moto unaohitajika kama si mguso wa moyo wa Yesu ulio tanuri ya upendo, ambao utashi wake mwadilifu daima ni chemchemi ya stahili zisizopimika? "Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema" (Yoh 1:16). Tunahitaji huo *muungano na Mwokozi* ulio tokeo kuu la komunyo.

*Matunda ya komunyo motomoto* yanalingana na ubora wa misimamo yetu. "Kwa maana yeyote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele" (Math 13:12). Mfano wa matokeo ya komunyo motomoto ni Eliya alipoishiwa nguvu katika kukimbia dhuluma; malaika akamuonyesha "mkate umeokwa juu ya makaa, na gudulia la maji, kichwani pake. Akala, akanywa, akajinyosha tena. Malaika wa Bwana akamwendea mara ya pili, akamgusa, akasema, 'Inuka, ule, maana safari hii ni kubwa mno kwako'. Akainuka, akala, akanywa, akaenda katika nguvu za chakula hicho siku arobaini mchana na usiku, hata akafika Horebu, mlima wa Mungu" (1Fal 19:6-8). Tukumbuke kwamba *kila komunyo inatakiwa kuwa bora kuliko iliyotangulia,* kwa kuwa kila moja inakusudiwa *kustawisha* upendo, na hivyo kutuandaa kumpokea Bwana kesho yake kwa upendo mkubwa zaidi. Ndiyo *sheria ya kuongeza kasi* inayotakiwa kutimia hasa kwa komunyo ya kila siku, tunavyoona katika watakatifu, ambao miaka yao ya mwisho ilikuwa na maendeleo ya kasi kuliko ile ya nyuma; ilitimia hasa kwa Maria, kielelezo cha ibada kwa ekaristi. Mungu atujalie tufanane nao.

"Nani anaweza kuikaribia chemchemi ya utamu kwa unyenyekevu, asionje utamu walau kidogo? Nani ajongee moto unaowaka mno, asisikie joto hata kidogo? Basi, ndiwe chemchemi iliyojaa utamu siku zote kabisa; ndiwe moto unaowaka daima, bila ya kufifia" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,4:3). Hiyo chemchemi ya neema ni bora hivi kwamba inastahili kupatiwa sifa za maji yanayoburudisha na papo hapo za moto uwakao. Yaliyotenganika upande wa viumbe yameunganika katika ekaristi. Tukienda kumpokea Yesu tumfikirie mtume Yohane aliyeegemea moyoni pake, na Mt. Katerina wa Siena aliyejaliwa kunywa kwa wingi katika donda la moyo huo ulio wazi daima ili kutuonyesha upendo wake. Tumuombe pia bikira Maria atushirikishe upendo aliokuwa nao katika kuipokea ekaristi kwa mikono ya Mt. Yohane.

## UTAFITI: KOMUNYO ZISIZO NA SHUKRANI

### KAMA TU UNGALIJUA ZAWADI YA MUNGU!

Waamini walio wengi wanatoka kanisani *mara* baada ya misa ambapo walipokea sakramenti. Mara nyingi lilitolewa kwa faida fundisho la Mt. Filipo Neri aliyetuma watumishi wawili wenye mishumaa kumsindikiza mama aliyetaka kufanya hivyo. Lakini wengi wanazoea vibaya kwa urahisi, hivyo kuna *komunyo nyingi, lakini washiriki halisi wachache.* Kama hakutakuwa na watu wenye ari ya kwenda kinyume cha mkondo huo, utaangamiza roho yote ya ibada.

Je, shukrani si wajibu kwa mtu aliyepokea fadhili? Je, haitakiwi kulingana na fadhili yenyewe? Basi, tuseme nini kuhusu utovu wa shukrani kwa Bwana ambaye fadhili zake zina thamani isiyopimika? Yesu alimshukuru Baba mara nyingi kwa fadhili zake, hasa kwa umwilisho, kwa kuwafumbulia watu wadogo mafumbo yake, naye hakomi kumshukuru katika misa na huko mbinguni. Kisha kuwaponya wakoma kumi, alipoona mmoja tu amerudi kushukuru, aliuliza, "Hawakutakaswa wote kumi? Wale kenda wa wapi?" (Lk 17:17). Katika ekaristi tunajaliwa fadhili kubwa kuliko muujiza wa kuponywa mwili: tunampokea aliyetustahilia wokovu, pamoja na ustawi wa uzima wa Kimungu na wa upendo.

Basi, kama kuna kitu kinachodai *shukrani za pekee* ndicho *ekaristi,* ambayo Yesu amependa kubaki kweli kati yetu ili kuendelea kisakramenti kujitoa sadaka na kulisha roho zetu kuliko chakula bora chochote.

Hatulishwi mafundisho ya mtakatifu fulani, bali ubinadamu wa Yesu Kristo uliojaa ukamilifu wa neema kwa kuungana na Neno katika Nafsi ya Kimungu. Fadhili isiyo na kipimo inadai shukrani inayolingana nayo. Kwa kuwa hatuwezi kumtolea Mungu shukrani ya namna hiyo, tumuombe bikira Maria atusaidie tushiriki shukrani aliyomtolea Mungu chini ya msalaba, baada ya neno "Yametimia".

Yesu anabaki kweli ndani mwetu mpaka maumbo ya sakramenti yanapodumu, yaani kama robo saa baada ya kupokea. Tunawezaje kushindwa kuongea naye muda huo mfupi? Tunashindwaje kuona kosa la kutoshukuru? Hatusemi juu ya watu wenye roho ya ibada wanaolazimika kutoka ili kutimiza wajibu halisi fulani. "Kisha kukomunika, siwezi kabisa kutoka kanisani. Muda uliopangwa na jumuia kwa kushukuru nauona mfupi hivi hata napaswa kujilazimisha kuifuata mezani" (M. T. Couderc). Bwana anatuita, anajitoa kwetu kwa upendo mkuu, nasi tusiwe na neno la kumuambia bali tuone vigumu kumsikiliza kidogo! Shukrani baada ya komunyo ndiyo fursa bora ya maisha ya Kiroho. Kiini cha misa ni mageuzo, lakini sisi tunaishiriki kwa njia ya komunyo, ambapo uwepo muungano wa roho takatifu ya Yesu na roho yetu; muungano wa akili yake iliyoangazwa na utukufu na akili yetu ambayo mara nyingi imejaa giza; muungano wa utashi wake wenye kusimama daima upande wa uadilifu na utashi wetu geugeu, usio na hakika; hatimaye muungano wa hisi zake safi na hisi zetu zinazovurugika mara nyingi.

*Yesu anasema na wale wanaomsikiliza,* wasiotawanya mawazo kwa hiari, yaani sio tu kwa makusudi mazima, bali pia kwa ulegevu katika kuzingatia, kutaka na kutenda yanayowapasa. Uzembe huo unasababisha dhambi nyingi za kutotimiza wajibu zisizozingatiwa katika kutafiti dhamiri. Wengi wanaoshindwa kuona dhambi yoyote ndani mwao, kwa sababu *hawajatenda* ya mauti, wamejaa dhambi za kutotimiza wajibu, na makosa ya uzembe ambao kwa kiasi fulani ni wa hiari. Tusipuuzie wajibu wa kushukuru: komunyo zisizo makini zinaweza kuzaa matunda gani?

Wapo mapadri wengi ambao hawatoi shukrani baada ya misa, au badala yake wanatimiza wajibu wa kusali Sala ya Kanisa, hivi kwamba ndani mwao haibaki roho ya ibada ya kuweza kuhuisha liturujia wanazotakiwa kuziongoza. Padri asiyeishi vya kutosha kwa uzima wa Kimungu, atawezaje kuwashirikisha wengine? Atawezaje kuwatimizia mahitaji makubwa ya Kiroho watu ambao wakimuomba msaada wanarudi mikono mitupu na kwa masikitiko? Pengine watu wenye njaa na kiu ya Mungu, ambao wamejaliwa mengi na kujitoa kati ya matatizo makubwa, wanajibiwa, "Usihangaike! Unafanya zaidi kuliko unavyopaswa!" Iko wapi ari ya upendo ya Mwokozi: "Nimekuja kutupa moto duniani, na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi?" (Lk 12:49). "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yoh 10:10). Mtu fulani aliyekuwa akijilaumu kwa kutofikiria vya kutosha mchana juu ya komunyo ya asubuhi, akajibiwa, "Mbona hatufikirii hata mlo tuliopata saa chache zilizopita?" Ndio jibu la fikra za kidunia zisizoona umbali mkubwa uliopo kati ya mkate wa ekaristi na ule wa kawaida. Jibu hilo linatokeza hali iliyo kinyume cha kuzamia fumbo hilo na inayotokana na uzembe katika kupokea fadhili bora za Mungu.

Hayo yanaweza kufikisha mbali, na kusahaulisha kuwa kila Mkristo anatakiwa kulenga upendo kamili; padri na mtawa wanaweza wakasahau wajibu wao wa pekee wa kulenga ukamilifu, ili kutimiza kila siku kitakatifu zaidi huduma yao na kuungana na Bwana zaidi na zaidi. Tukiona muungano na Mungu si jambo la kwanza, hatuelekei tena ukamilifu, hatupimi mambo kwa busara na hekima, bali tunateleza kwa uzembe kwenye mteremko wa upumbavu wa roho. Uzembe katika kushukuru unakuwa uzembe katika kuabudu, kuombea na kufidia. Hivyo tunasahau malengo ya sadaka, na tunafuatilia mambo yasiyo na thamani ya Kiroho yasipohuishwa na muungano na Mungu. Uzembe katika kushukuru baada ya komunyo unatokana na kutojua vya kutosha ukuu wa zawadi ya Mungu: "Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, 'Nipe maji ninywe'…" (Yoh 4:10). Tumuombe kwa unyenyekevu na ari atujalie roho kubwa ya imani, ambayo tuzamie fumbo hilo kwa vipaji vya akili na hekima: ndio chanzo cha shukrani iliyo motomoto kadiri tunavyojua ukuu wa zawadi tuliyojaliwa.

## 2.16. *SALA YA KUOMBA*

Kisha kusema juu ya utakaso kwa njia ya sakramenti, tuseme juu ya utakaso wa wanaoanza kwa njia ya sala, tukianzia mawazo makuu yanayohusika.

**JE, TUNASADIKI VYA KUTOSHA NGUVU YA SALA?**

Suala la nguvu ya sala linawahusu wote, hata wenye dhambi ya mauti, kwa sababu hawawezi kustahili lakini wanaweza kusali. Ombaomba alichonacho ni ufukara wake tu, lakini ndicho kinacholitia nguvu ombi lake; mtu akiomba kwa moyo wote, huruma inamuinamia. "Kwa kweli na haki umeyaleta hayo yote juu yetu kwa sababu ya dhambi zetu… Usituache kabisa, kwa ajili ya jina lako" (Dan 3:29,34). Zaburi zimejaa maombi ya namna hiyo.

Je, tunaisadiki nguvu ya sala? Kishawishi kinapotaka kutuangusha, au tunapokosa mwanga, au msalaba unapobebeka kwa shida, je, tunakimbilia sala alivyotuambia Bwana? Haitutokei kuitilia shaka, kimatendo kama si kinadharia? Ingawa tunajua ahadi ya Mwokozi, pengine tunadhani tumesali tusisikilizwe. Tunaona nguvu ya mashine, ya jeshi na ya pesa, lakini hatusadiki vya kutosha nguvu ya sala, kwa sababu hatujui vizuri inatokea wapi na tunasahau inaelekea wapi.

**CHEMCHEMI YA NGUVU YA SALA**

Asili ya mito iko juu, katika maji ya mvua: huo ni mfano wa sala ambayo nguvu yake inatokea juu vilevile. Pengine tunashawishika kudhani sala asili yake ni sisi ambao kwa njia yake tunajaribu kuvuta matakwa ya Mungu upande wetu kwa kumbembeleza. Papo hapo dhana hiyo inagongana na hakika ya kwamba hakuna anayeweza kubadili matakwa ya Mungu wala kuyavuta upande huu au huu. Mungu ni wema unaotaka kujitoa tu, ni huruma iliyo tayari daima kusaidia, lakini pia ni yule asiyebadilika hata kidogo, wala utashi wake haubadiliki milele. *"Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu"* (Mal 3:6). Kwa maongozi yake, utaratibu wa viumbe na wa matukio umeshapangwa tangu milele: "Mungu si mtu, aseme uongo; wala si mwanadamu, ajute" (Hes 23:19). Mbingu na dunia "zitaharibika, bali wewe utadumu, naam hizi zitachakaa kama nguo; na kama mavazi utazibadilisha, nazo zitabadilika. Lakini wewe u yeye yule, na miaka yako haitakoma" (Zab 102:26-27). "Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeukageuka" (Yak 1:17). Kama ni hivyo basi, je, tukubali kuwa sala haiwezi kitu na hivyo hata tukisali vizuri yatatukia yanayotakiwa kutukia?

Neno la Injili linabaki palepale, na maisha ya Kiroho yanapaswa kupenywa nalo zaidi na zaidi. "Amin, amin nawaambia: Mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa jina langu" (Yoh 16:23). Ni kwamba sala haina asili ndani mwetu, wala si juhudi ya kumfanya Mungu abadili mipango yake. Tukisema hivyo ni kibinadamu tu. Kwa kweli matakwa ya Mungu hayabadiliki hata kidogo, lakini ndiyo asili ya hakika ya nguvu ya sala. Hilo ni jepesi kueleweka, ingawa ndani yake limo fumbo la neema. Kwanza tusisitize kuwa *sala halisi inapata kwa hakika inachokiomba kwa sababu Mungu asiyeweza kukanusha aliyosema ameamua iwe hivyo.*

Kujichorea picha ya Mungu asiyetaka wala kujua tangu milele sala zetu ni dhana ya kitoto sawa na ile ya kuamini Mungu anaweza kubadili mipango yake ajilinganishe na matakwa yetu. Tangu milele maongozi yake yamekwishapangwa yote: sio tu *yatakayotokea,* bali pia *namna* ambayo yatokee, na *sababu* zitakazofanya yatokee. Kwa ajili ya mavuno Bwana ameandaa mbegu, mvua na jua. Vilevile upande wa roho ameandaa neema zinazohitajika kwa utakatifu na wokovu. Katika ngazi zote, kwa ajili ya matokeo fulani Mungu ameandaa sababu zitakazofanya yapatikane. Basi, sala ni sababu iliyokusudiwa naye ituletee zawadi zake, hasa Roho Mtakatifu: ndiye paji lenyewe ambalo tumeandaliwa na kupaswa kuliomba.

Uhai wa viumbe vyote ni zawadi ya Mungu, lakini binadamu tu anaweza kujitambua hawezi kuishi kimaumbile wala Kimungu pasipo zawadi hiyo. Basi, si ajabu kwamba Mungu amepanga binadamu ajiombee zawadi. Hapa pia yeye amekusudia kwanza tokeo la mwisho, halafu njia au sababu zitakazoliwezesha. Kisha kuamua kutoa, amepanga tusali ili kupokea, kama baba aliyepanga kuwafadhili wanae lakini ameona afadhali waombe fadhili hiyo. Zawadi ya Mungu ndiyo tokeo; sala ndiyo sababu itakayoliwezesha. "Watu wanapaswa kujiandaa kwa sala wapokee yale ambayo Mwenyezi Mungu amepanga kuwapatia tangu milele" (Mt. Gregori Mkuu). Hivyo ni lazima tuombe misaada tunayohitaji ili kutenda mema na kudumu mpaka mwisho, kama ilivyo lazima tupande mbegu ili kuvuna. Wapo wanaosema, eti! "Tusali tusisali, yatatukia yaliyopangwa". Tuwajibu, "Huo ni upumbavu sawa na kusema tutavuna iwe tumepanda au la". Maongozi ya Mungu yanatofautiana na imani potofu hiyo kwa kuheshimu hiari ya binadamu. Bila ya shaka tunahitaji neema ya msaada ili kusali, lakini hiyo *inatolewa kwa wote,* yaani wanaikosa wale tu wanaoikataa.

Tofauti na mbegu, ambazo zinaweza zikashindwa kuzaa, sala halisi, dumifu, nyenyekevu na yenye tumaini ambayo mtu anajiombea misaada ya lazima kwa wokovu haipotei kamwe. "Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (Lk 11:10-13).

Basi, tuamini sala: siyo nguvu ya kibinadamu yenye asili ndani mwetu, bali chemchemi ya nguvu yake imo ndani ya Mungu na ya stahili zisizo na mwisho za Mwokozi. Inashuka toka mpango wa milele wa upendo na kupanda juu hadi huruma ya Mungu. Hivyo *tunainua utashi wetu hadi utashi wake ili tutake pamoja naye yale aliyopanga tangu milele atupatie.* Sala, badala ya kutaka kumuinamisha Mungu kwetu, ni "kuinua roho kwa Mungu" (Mt. Yohane wa Damasko).

Kama ni hivyo, kinyume cha kupinda maongozi yake, *sala inayachangia.* Badala ya kutaka mmoja, tunataka wawili pamoja. Kwa mfano, maombi yetu mengi kwa uongofu wa mtu yakisikilizwa, tuseme, Mungu ndiye aliyemuongoa, lakini ametujalia tushiriki kazi yake hiyo, akipanga tangu milele tuombe hata neema hiyo itolewe. Namna hiyohiyo *tunachangia* wokovu wetu tukijiombea neema za lazima kuupata, ambazo *baadhi yake* (k.mf. kufa katika neema inayotia utakatifu) *hazistahiliki* ila zinapatikana kwa sala. Hivyo neema ya kukingiwa dhambi ya mauti haistahiliki (la sivyo tungestahili chanzo cha stahili, yaani kudumu katika neema inayotia utakatifu), lakini tunaweza kuipata kwa sala. Hata neema ya kuzamia sala, ingawa haistahiliki, inapatikana kwa kuomba. "Mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa" (Yak 1:5). Pia neema ya uongofu kwa mtu anayeonekana kuikataa, tunaweza kutumaini tutaipata kadiri tulivyo wengi na tunavyodumu kuiomba.

**TUOMBE NINI HASA?**

Mungu amepanga sala iwe njia ya kufikia utakatifu na wokovu, hivyo ina nafasi katika maisha ya roho, kama vile joto upande wa mwili. Basi, lengo la roho ni uzima wa milele, na mema yanayotufikisha huko ni ya aina mbili: yale ya Kiroho yanayohusika moja kwa moja, na yale ya kimwili yanayoweza yakachangia wokovu kadiri yanavyobaki chini ya yale ya Kiroho.

*Mema ya Kiroho* ni: neema inayotia utakatifu na za msaada, maadili, vipaji saba vya Roho Mtakatifu na stahili zinazotokana navyo. Sala inaweza yote ili kumpatia mkosefu neema ya uongofu, na mwadilifu neema ya kudumu katika wajibu wake. Sala hiyohiyo inaweza yote ili kutupatia imani hai zaidi, tumaini imara zaidi, upendo motomoto zaidi, uaminifu mkubwa zaidi kwa wito wetu. Tunavyoelekezwa na *Baba Yetu* tuombe kabla ya yote kwamba jina la Mungu litukuzwe kwa njia ya imani yenye kung'aa; kwamba ufalme wake ufike, inavyotarajiwa na tumaini, na kwamba atakalo lifanyike kwa upendo ulio safi na wa nguvu zaidi na zaidi. Sala inaweza pia kutupatia mkate wa kila siku kadiri unavyohitajika au unavyofaa kwa wokovu wetu, hasa mkate wa ekaristi pamoja na misimamo ya kufaa ili kuupokea vema. Inatupatia tena msamaha wa makosa yetu na kutuandaa tusamehe jirani; inatukinga na kishawishi au kutupa nguvu tukishinde. Lakini, ili sala iweze kupata hayo yote ni lazima itimize masharti tuliyoorodhesha: iwe nyofu, nyenyekevu (anayeomba ni maskini); ijae tumaini kwa wema usio na mipaka ambao hatutakiwi kuwa na shaka nao; idumu ili kutokeza hamu kubwa ya moyo. Ndivyo ilivyokuwa sala ya mama Mkananayo aliyeambiwa, "Na iwe kwako kama utakavyo" (Math 15:28).

Hata kama Bwana anatuacha tupambane na matatizo makubwa tuliyoomba atuepushe nayo, tusidhani hatusikilizi. Kwamba tu *tunaendelea kusali,* maana yake Aliye juu anatusaidia, kwa sababu pasipo neema mpya za msaada tusingeendelea kusali. Anatuacha tupambane na matatizo ili tujifunze kupiga vita, tutambue kuwa hivyo vinatuletea faida, kuwa neema tuliyojaliwa inatosha tuendelee kupambana ambako nguvu ya Bwana inayochochea ya kwetu inajitokeza wazi zaidi: *"Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu"* (2Kor 12:9). Ndivyo tunavyohakikisha katika kutakaswa hisi na roho, tunapopaswa kuomba mfululizo neema ya hakika ambayo peke yake inaweza kutukinga na udhaifu wowote.

Kuhusu *mema ya kimwili,* sala inaweza kutupatia yale yote yanayokusudiwa kutusaidia kwa namna moja au nyingine kuelekea uzima wa milele: chakula, afya, nguvu, mafanikio. Sala inaweza kuyapata, mradi tuombe kabla na juu ya yote kwamba tumpende Mungu zaidi na zaidi: *"Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa"* (Math 6:33). Tusipopata mema hayo ya kimwili ni kwa sababu hayatufai kwa wokovu, lakini kama sala imefanyika vizuri tutapata neema nyingine muhimu zaidi. *"Bwana yu karibu na wote wamwitao, wote wamwitao kwa uaminifu"* (Zab 145:18). Sala ya kuomba ikiinua kweli roho kwa Mungu, inaandaa kufanya sala bora zaidi ya kuabudu, ya kufidia, ya kushukuru na hatimaye ya kuungana naye.

## 2.17. *SALA YA KANISA*

Mojawapo kati ya njia kuu za kuungana na Mungu ni Sala ya Kanisa ambayo kila siku inaendana na misa takatifu. Misa ndiyo sala kuu ya Kristo inayoendelea hadi mwisho wa dunia, ambapo kwa huduma ya mapadri wake tendo la Mungu-mtu kupenda na kujitoa linapaa mfululizo toka moyo wake wa kikuhani kama ibada, fidia, dua na shukrani za thamani isiyo na mipaka. Liturujia ya Vipindi ndiyo sala kuu ya Bibi arusi wa Kristo, ambayo haitakiwi kukoma duniani, kama vile misa isivyokoma kamwe. Kwa waliojaliwa heshima ya kuishiriki, inatarajiwa kuwa shule nzuri ajabu ya sala hasa, ya kujitoa na ya utakatifu. Lakini ikipotewa na roho yake na kubaki na mwili tu, isizame katika mafumbo, badala ya kuwa mruko, mwinuko na pumziko la mtu kwa Mungu, inakuwa mzigo na uchoshi usiozaa tena matunda yake bora.

**LITURUJIA ILIYOLIPULIWA**

*Haraka* ndiyo kifo cha ibada, kwa kuwa inaizuia isiwe na undani. Hapo maneno yanatamkwa vibaya, pasipo mdundo wala kipimo. Antifona na tenzi hazieleweki, ingawa mara nyingi ni nzuri kama nini. Masomo yanafanyika pasipo kuzingatia vituo, kama mambo yasiyo na maana, kumbe ndiyo mng'ao wa hekima ya Mungu. Kwa kisingizio cha kuokoa muda (labda dakika tano zitakazotumika kwa upuuzi) unapotezwa muda ulio bora, ule uliotolewa kwa Mungu. "Kama tajiri angesema na mtumishi wake vile wengi wanavyosema na Mungu wakisali Liturujia ya Vipindi, mtumishi angedhani tajiri amerukwa na akili kwa jinsi anavyoropoka" (Ch. wa Condren). Liturujia iliyolipuliwa inafanana na *mashine:* sehemu zake zimepangwa moja karibu na nyingine pasipo kufungamanishwa na uhai. Maneno yanafuatana tu, bila ya kutokeza maana ya Kimungu, hivi kwamba anayetaka kuielewa na kuifuata anapaswa kujichosha kwa kuwa anazuiwa badala ya kusaidiwa kusali.

Pengine zinakumbushwa taratibu za liturujia, lakini hizo peke yake hazitoshi. Ugonjwa ni wa ndani zaidi, hivi kwamba ni lazima tung'oe mizizi yake. Dawa ya kufaa kweli, inayowezesha kufaidika na nyingine pia, ni *roho ya sala,* kama vile roho inavyohitajika kumrudishia uhai maiti. Kwa mtu asiyesali peke yake pia, Sala ya Kanisa ni kazi ya mwili, ibada ya nje tu. Kwa kukosa mazoea ya kujikusanya, anashambuliwa na mawazo

yasiyohusika na liturujia: kazi, masomo, shughuli na pengine upuuzi tu. Hata wanasala wanapatwa nayo, lakini kwake ni hali ya kawaida ya uzembe, na ndani yake mtawanyo wa mawazo haubaki katika ubunifu bali unaenea katika akili na utashi. Katika hali hiyo atawezaje kufurahia maneno ya Mungu, maandishi bora ya mababu na maisha ya watakatifu tunayoyapitia kila siku? Uzuri huo wote hauzingatii, kwake ni kama vitu visivyo na rangi wala ladha. Ubora wa ushairi wa Mtungazaburi na milio ya moyo wake vinaonekana vya kawaida na vya kukinaisha. Siku fulani, wakati wa kuimba Zaburi kwa pamoja, Mt. Bernardo aliona juu ya kila mtawa malaika mlinzi akiandika maneno yake, lakini kwa namna tofauti: kwa herufi ya dhahabu, ya fedha, ya wino au ya maji tu; tena mwingine alishika peni asiandike.

**LITURUJIA YA KUZAMA NDANI YAKE**

Kinachofanya liturujia iwe ya kuzama ndani yake ndicho roho ya sala, au walau hamu ya kuwa nayo ambayo inaitafuta na hatimaye itaipata. Kuzama katika mafumbo ndiyo njia pekee ya kuona katika liturujia mwanga, amani, *furaha ya ukweli*. Hiyo roho ya sala inachotwa hasa katika sala ya moyo na inapotea tukiwa na haraka ya kumaliza sala kana kwamba isingekuwa pumzi ya roho, fungamano na Mungu na uhai wetu. Ndiyo roho ambayo ilizaa Zaburi na inahitajika ili kuzielewa na kuzishika maishani: "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu" (Zab 42:1).

Liturujia ikiwa na roho hiyo ni hai, haihitaji kukumbushwa mfululizo taratibu zake, kwa sababu hizo zinalingana na maelekeo yetu ya ndani. Hapo, bila ya kwenda polepole mno, maneno yanatamkwa vizuri, vituo vinazingatiwa, antifona zinafurahiwa, na tunajilisha kweli ujumbe wa matini. Msomaji anajiandaa mapema asije akasoma kwa shida na namna isiyoeleweka; katika matamshi anakwepa kujitokeza mno binafsi. Kisha kusali Zaburi tunajisikia kuirefusha kwa kitambo cha sala ya moyo, kama walivyofanya watawa wa zamani ambao mara nyingi walipata hapo mianga mikuu walioitafuta kwanza kwa saa na saa za juhudi. Hapo tunaelewa kuwa sala ya moyo ndiyo roho ya Sala ya Kanisa, ambayo upande wake ndiyo lishe bora ya sala ya moyo, kwa kuwa ndiyo Neno la Mungu lililopangwa na kufafanuliwa kadiri ya mzunguko wa mwaka wa liturujia, yaani kadiri ya wakati halisi unaolingana na uzima wa milele.

Hapo kweli sala ni kuzidi kumuinulia Mungu roho ambayo inawaka na kumalizika kitakatifu kama mshumaa altareni. Ni heri kwetu kushiriki Sala ya Kanisa ikiadhimishwa hivyo: hapo tunahisi uhai halisi wa Kanisa, tunatambua wimbo wake mnyofu na papo hapo wa fahari ambao unatangulia na kufuata maneno bora ya Bwana arusi, yale ya mageuzo katika ekaristi. Hapo tunasahau huzuni za duniani na masharti ya kinafiki ya maisha ya jamii. Sala ya namna hiyo inavuta miito mizuri, wakati liturujia iliyolipuliwa inaisogeza mbali. Mungu atujalie idumu usiku na mchana katika nyumba za kitawa, kwa sababu sala hai haitakiwi kukoma, na sala ya usiku ina neema za pekee kwa kuzama katika mafumbo, kutokana na kimya kikuu kilichopo na kwa sababu nyingine nyingi. Sala hiyo ndiyo pumziko takatifu ambalo watu wanalihitaji baada ya kupatwa na uchovu, mahangaiko na fujo ulimwenguni. Ni pumziko ndani ya Mungu lililojaa uhai na linalofanana kidogo na pumziko lake ambaye anao *kwa mara moja* uhai wote usio na mwisho katika nukta ile isiyopita kamwe na iliyo kipimo cha utendaji mkuu na cha utulivu mkuu katika upendo.

Sala ya Kanisa ambayo inaandaa na kutimiliza misa ni njia kuu ya kuinuka juu ya mawazo ya kibinadamu hadi kuzama katika mafumbo, kumtazama tu Mungu na kuungana naye. Hata mtu anayesoma kirefu teolojia anahitaji kujiinua juu kuliko ujuzi wa vitabu, kukusanya mawazo mpaka ndani, kupokea nuru ya Mungu katika sala. La sivyo anadumaa, hawezi kuwashirikisha watu nuru ya kutosha, kazi yake haina uhai, mawazo yake hayapandi juu inavyotakiwa yaone mandhari yote, na polepole yanaacha kuvutia. Ni lazima aone mara nyingi mafumbo anayoyasoma yanavyojitokeza kwa namna hai na angavu katika maneno ya Mungu ambayo liturujia inatufanya tuyaonje na kuyapenda: Neno lake tunalokumbushwa hivyo katika sala linahusiana na vitabu vya teolojia kama vile duara nyofu inavyohusiana na umbo la pembe nyingi lililomo ndani mwake. Pengine ni lazima kusahau pembe zote za umbo hilo na kufurahia kitakatifu uzuri wa duara tu.

Hatimaye Sala ya Kanisa ni kanuni ya hakika dhidi ya udanganyifu wa binafsi: inatuponya mapendo ya juujuu kwa kutukumbusha mfululizo kweli kuu kwa lugha ya Maandiko. Wanaojiamini kipumbavu inawakumbusha ukuu wa haki ya Mungu, kumbe wanaomuogopa mno inawakumbusha huruma isiyo na mipaka na thamani ya mateso ya Mwokozi. Inawainua wanaofuata miguso na hisi tu hadi vilele vya imani na upendo halisi. Inatukumbusha hatua zote za maisha ya Kiroho, zikiwa ni pamoja na mafumbo ya furaha, mwanga, uchungu na utukufu. Hivyo inatupatia furaha halisi ambayo inapanua moyo na kutuandaa kwa sala ya kimya zaidi, yaani sala ya moyo.

## *2.18. **SALA YA MOYO YA WANAOANZA INAVYOZIDI KUWA SAHILI***

Tumeona kuwa sala ni kuinua roho kwa Mungu na kuwa maombi yanatakiwa kuendana na ibada, fidia na shukrani. Lakini tunajisikia haja ya sala ya ndani zaidi, ambapo tujikusanye na kuwasiliana na Utatu mtakatifu uliomo ndani mwetu tuweze kupokea ile nuru ya uzima ambayo peke yake itatuwezesha kupenya na kuonja mafumbo ya wokovu, halafu kurekebisha tabia yetu izidi kulingana na ile ya Yesu aliyetualika kupata raha nafsini mwetu kwa kujifunza upole na unyenyekevu wake.

**SALA YA MOYO NDIYO NINI? TUZIONEJE MBINU ZA KUTAFAKARI?**

"Wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi" (Math 6:6). "Sala ya moyo ni urafiki na Mungu, ni kukaa mara nyingi peke yetu na yule ambaye tunajua anatupenda" (Mt. Teresa wa Yesu). Ni sala ya kujiotea ambayo Wakristo wanyofu na safi waliijua daima. Mkulima aliyeulizwa na Mt. Yohane Maria Vianney kuhusu namna yake ya kusali, aliieleza vizuri ajabu, "Namtazama Bwana wetu katika tabenakulo, naye ananitazama mimi". Sala hiyo ilikuwepo daima kwa wanadini wanyenyekevu wenye kumtamani Mungu: "Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu, Mungu aliye hai, lini nitakapokuja nionekane mbele za Mungu?" (Zab 42:2).

Hakuna jambo sahili kuliko sala! Mara nyingi inanyang'anywa sifa hiyo kwa kupendekezewa mbinu ngumu ambazo zinamdai mtu azizingatie kuliko Mungu. Haifai kutia maanani mbinu kuliko lengo, au mpangilio wa mawazo kuliko ukweli. Mbinu ni nzuri ili kuuendea ukweli, mradi ifikishe huko na kusahaulika. Mbinu ngumu mno inasababisha itikio hasi, tena kupita kiasi: waliochoshwa na ugumu huo wanajiachia kufuata ndoto za mchana, pasipo roho halisi ya ibada. Mbinu ya kufanyia sala ya moyo inafaa, hasa mwanzoni, ili kukwepa mtawanyo wa mawazo. Lakini iwe sahili, la sivyo itazuia badala ya kusaidia. *Ielekeze tu njia ya kuinuka kwa Mungu,* ikionyesha matendo ya lazima ya mwendo huo. Kwa namna ya pekee tukumbuke kwamba *sala inategemea hasa neema ya Mungu* na kwamba tunajiandaa kuipokea kwa unyenyekevu kuliko kwa mbinu zetu.

**MATENDO YA LAZIMA KATIKA SALA YA MOYO**

Kwanza sala si kazi ya akili tu, kama kusoma. Kuna watu wadadisi wa mambo ya dini ambao hawawi watu wa sala kwa kuwa kinachowasukuma ni *hamu ya kujua kuliko upendo wa Mungu.* Katika udadisi wao wanapata furaha kubwa kuliko zile za hisi, lakini inatokana na ujuzi, kumbe upendo ndio unaokusudiwa kufikisha akili imjue katika sala ili kumpenda zaidi na zaidi. Mara nyingi furaha inayotokana na hamu ya kujua inazidisha kiburi na kujipendea, hivyo inalenga *umimi* wao wasijitambue. Masomo yanaweza yakafanyika pasipo neema inayotia utakatifu, nayo hayachangii kila mara kuistawisha. Kinyume chake, sala *inatakiwa itokane na upendo wa Mungu na kuishia ndani yake.* Kutokana na upendo alionao kwa Mungu mtu anajitahidi kumtazama katika sala, na mtazamo huo wa wema na uzuri wake unazidisha upendo. "Upendo unafuata ujuzi na kwa kupenda utajitahidi kutafuta ukweli na kuuvaa… Kadiri tunavyomfahamu hivyo Mungu tunampenda, na kadiri tunavyompenda tunamfahamu… Upendo na ujuzi vinalishana" (Mt. Katerina wa Siena). Halafu *hapa duniani "kumpenda Mungu ni bora kuliko kumjua"* (Mt. Thoma wa Akwino), hata kuliko imani. Basi, katika sala tunapaswa kuinuka kwa Mungu kwa mabawa mawili ya akili na utashi tukisaidiwa na upepo wa neema: hilo ni tendo la kujua na kupenda lipitalo maumbile.

Ikiwa ni hivyo, ni rahisi kusema matendo ya lazima ya sala ni yapi: inatakiwa kuandaliwa na *tendo la unyenyekevu,* na kutokana na *maadili matatu ya Kimungu* ambayo yanatuunganisha na Mungu, yanahuisha adili la *ibada* na kutupatia *mianga na minong'ono ya Roho Mtakatifu.* Mwenye bidii anaruka kama ndege kwa nguvu ya mabawa yake, lakini upepo wa Roho Mtakatifu unategemeza kazi hiyo na mara nyingi unamfikisha juu kuliko anapoweza kufikia kwa maadili yake tu. Si bure kwamba vipaji vya Roho Mtakatifu vinapatikana katika waadilifu wote. Pengine sala ya moyo inageuzwa kuwa zoezi la kutafakari kwa kutumia hasa *busara* inayopanga la kufanya, badala ya kutumia *maadili matatu* yanayomhusu Mungu mwenyewe. Tuliachie nafasi azimio (litokanalo na imani inayoongoza busara toka juu) lakini tusigeuze sala ya moyo kuwa uchunguzi wa dhamiri wala upangaji wa matendo: ni muhimu tudumishe ukuu wa maadili ya Kimungu, hasa upendo.

Basi, tuzingatie hayo matendo ya lazima. Mara nyingi katika waliokamilika yanafanyika kwa pamoja na mfululizo, lakini tukitaka kuyafafanua tunalazimika kuyaorodhesha moja baada ya lingine, yanavyojitokeza katika wanaoanza.

Kwa kawaida, kwanza kuna *tendo la unyenyekevu,* kwa sababu inafaa tujikumbushe sisi tunaotaka kuongea na Mungu ni nani. Tuzingatie maneno ya Bwana kwa Mt. Katerina wa Siena: "Mimi ndimi niliye; *wewe ndiwe usiye".* Peke yetu sisi si kitu, tena dhambi zetu ni vurugu mbaya kuliko utovu wa vyote. Kwa kawaida tendo hilo liendane na mengine ya *kujuta* na *kuabudu* (kama lile la kupiga goti tukiingia kanisani) ambayo yanaondoa kiburi, kizuio kikuu cha neema. Unyenyekevu halisi, badala ya kutukatisha tamaa, unatukumbusha kwamba katika chombo cha udongo tunatunza hazina ya thamani: neema inayotia utakatifu na Utatu mtakatifu. Sala ikianza hivyo haitatokana na mapendo ya juujuu, bali na uhai wa neema ulio bora kuliko miguso yetu.

Linafuata *tendo la imani* la dhati na la muda mrefu kidogo kuhusu ukweli mmojawapo wa msingi: Mungu na sifa zake, Bwana na mafumbo ya maisha yake, au kuhusu wito wetu, lengo la milele, dhambi, shughuli zinazotupasa tuzitende kitakatifu zaidi na zaidi. Mambo hayo yanatakiwa kujirudiarudia akilini mwetu. Mara nyingi liturujia ndiyo inayotupendekezea la kuzingatia: kama ni fumbo fulani la Mwokozi, inafaa tuanze upande wa hisi, halafu tuendelee upande wa roho, kwa kuzingatia thamani yake isiyo na mipaka na kutulia katika mtazamo huo wa imani. Mara nyingi yanatosha maneno machache ya Injili au ya liturujia ambayo kwa walioendelea ni kama chembe za ubani katika moto wa upendo. Si lazima kutafakari muda mrefu; tendo

nyofu la imani ni bora kuliko mifuatano ya mawazo, nalo linazidi kuwa mtazamo mnyofu ambao unaendana na mshangao na upendo na kuzama katika sala. Imani hiyo tuliyomiminiwa, bora kuliko falsafa na teolojia, inatufanya tuyashike katika giza lakini kwa hakika na kwa namna ipitayo maumbile mafumbo yale ambayo wateule wanayatazama wazi mbinguni. Ndiyo mwanga wa kwanza wa maisha ya Kiroho: "Nasadiki kwa Mungu mmoja…". Pengine *Nasadiki* inakuwa kama *Naona,* kana kwamba tungeona kwa mbali chemchemi ya maji hai tunayoitamani.

Mtazamo huo wa imani unazaa *tendo la tumaini.* Tunatamani heri, uzima wa milele, amani iliyoahidiwa kwa wafuasi wa Yesu. Lakini hatuwezi kulifikia lengo hilo lipitalo maumbile kwa nguvu za umbile letu. Hapo tunakimbilia wema wa Mungu wenye misaada isiyo na mwisho. Kisha kusema, Nasadiki, mtu anakuja kusema, *Natamani, natumaini.* Baada ya kuona chemchemi hiyo, tunatamani kuifikia tunywe kwa wingi.

Tumaini linaandaa *tendo la upendo.* "Mtu akitumaini kupata fadhili ya Mungu, anaelekea kufikiria kuwa mfadhili wake ni mwema. Ndiyo sababu tumaini linatuandaa kumpenda Mungu kwa ajili yake mwenyewe" (Mt. Thoma wa Akwino), kwa kuwa ni wema usio na mipaka. Hivyo ndani yetu linajiotea tendo la upendo, kwanza kwa namna ya *mapenzi,* ambamo hisi zinafaa zikisaidia tu utashi unaohuishwa na upendo, mradi zibaki chini ya huo; lakini si za lazima, tena zinatoweka wakati wa ukavu. Kuliko miguso ya juujuu yanahitajika mapenzi matulivu lakini ya kina, ya hakika na yenye matunda yanayosema, "Mungu wangu, sitaki kuongopa tena kwamba nakupenda. Unijalie nikupende kwa moyo wote na kukupendeza katika yote". Upendo huo unatakiwa kuwa *wa vitendo*: "Nataka kulinganisha matakwa yangu na ya kwako, kushika amri zako, kuvunja chochote kinachonifanya mtumwa wa dhambi. Wewe unataka kutoa tu; nami nataka kupokea unavyotaka nipokee, katika majaribu na katika faraja, uwe unanishirikisha matendo yako ya furaha na ya mwanga au yale ya uchungu, kwa kuwa yote yanafikisha kwenye utukufu. Leo naazimia kuwa mwaminifu katika jambo hili nililolizembea mara nyingi". Tunaweza pia kutafakari polepole Baba Yetu.

Kwenye kilele hicho cha sala, tunda la imani, tumaini na upendo, maadili hayo yanaelekea kuungana katika *mtazamo wa upendo* mwaminifu na mkarimu ulio chanzo cha kuzama ndani ya Mungu na ndani ya ubinadamu wa Mwokozi, kama msanii anapotazama viumbe na kama mama anapomtazama mtoto wake. Sala hiyo ya kumiminiwa inaanza kupenya na kuonja mafumbo ya wokovu, inatuingiza polepole katika urafiki wa ndani na Kristo, inazidi kulinganisha moyo wetu na wa kwake, kwa sababu, tutambue tusitambue, tunaelekea daima kuwaiga wale tunaowapenda kwa dhati. Kuna tabia ngumu ambazo zinaweza kurekebika tu kwa sala ya kumtazama Bwana kwa upendo.

**SALA YA USAHILI**

Kadiri ya ustawi wa roho matendo tuliyoyaorodhesha (unyenyekevu, imani, tumaini na upendo) yanaelekezwa na vipaji vya Roho Mtakatifu kuungana katika mtazamo wa upendo motomoto. Ndiyo sababu mbinu izidi kuuachia nafasi usikivu kwa Roho Mtakatifu anayevuma anakotaka. Hivyo sala inaelekea kuwa *ushirika wa Kiroho wa kudumu.* Mwanasala anasema mengi kwa maneno machache, ambayo anayakariri kwa namna iliyo mpya daima. Ni kama *pumzi ya roho* ambayo anaingiza ukweli na wema wa Mungu kwa njia ya imani na tumaini na kutoa upendo. Yale yote anayoyapokea kwa Mungu, anamrudishia kama ibada na upendo. Kwa hiyo kuomba neema ya kuzama katika sala ni kuomba ushungi wa kiburi unaofunika macho ya roho uanguke ili *tupenye na kuonja mafumbo ya wokovu.*

"Ukamilifu wa maisha haya ndio kuungana na wema mkuu; basi, kadiri usahili ulivyo mkubwa, muungano unakamilika. Ndiyo sababu neema inahimiza kwa ndani wale wanaotaka kuwa wakamilifu wajifanye sahili zaidi ili hatimaye wawezeshwe kufurahia kilicho muhimu peke yake… Tafakuri ni njema sana kwa wakati wake na inafaa sana mwanzoni mwa maisha ya Kiroho. Ila hatutakiwi kuishia kwake, kwa sababu roho, kutokana na uaminifu wake katika kujitakasa na kukusanya mawazo, *inapokea kwa kawaida sala* safi na ya ndani zaidi, inayoweza kuitwa ya *usahili,* ambayo ni kumtazama tu Mungu, au Yesu Kristo au fumbo lake mojawapo. Hapo mtu, akiacha mifuatano ya mawazo, anatumia mtazamo mtamu unaomdumisha katika hali ya amani, uangalifu na usikivu kwa vitendo na miguso ya Kimungu anayoshirikishwa na Roho Mtakatifu. Anafanya kidogo lakini anapokea sana… Kwa kuwa anazidi kukaribia ile chemchemi ya nuru yote, ya neema zote na ya maadili yote, anajaliwa zaidi na zaidi… Usahili huo wa kweli unatufanya tuishi kwa kujifia mfululizo na kwa kutoshikamana na chochote, kwa sababu unatuelekeza kwa Mungu kwa unyofu kamili, pasipo kusimama kwa kiumbe chochote. Lakini neema hiyo ya usahili *haipatikani kwa juhudi za akili* bali *kwa usafi mkubwa wa moyo,* kwa kujifisha kweli na *kujidharau. Anayekwepa kuteseka, kujinyenyekeza na kujifia hataipata kamwe.* Ndiyo sababu ni wachache wanaoendelea katika njia hiyo, kwa kuwa karibu hakuna mtu anayetaka kuachana na nafsi yake, *jambo ambalo tusipokuwa nalo tunapata hasara zisizopimika na kukosa mema yasiyoelezeka…* Mtu aliyeangazwa anathamini na kupenda kwa dhati mpango wa Mungu anayeruhusu adhulumiwe na viumbe na kulemewa na vishawishi na upweke… Baada ya kutakaswa kwa *tohara ya mateso,* ambayo ni lazima kuipitia, vitakuja *mwanga,* pumziko, furaha kwa kuungana kwa ndani na Mungu" (Y. B. Bossuet). Mateso hayo ya lazima kabla ya hatua ya mwanga ndiyo kutakaswa hisi.

## 2.19. ***KUFIKIA MAISHA YA SALA NA KUDUMU NDANI YAKE***

### TUNAWEZAJE KUYAFIKIA?

Kwa kuwa sala inaitegemea neema, tunajiandaa kwa *unyenyekevu* kuliko kwa matendo mengine*:* "Amin, nawaambia: Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Math 18:3), hasa katika undani wa ufalme huo kwa maisha ya sala. Wanyenyekevu wa moyo wanafundishwa na Mungu mwenyewe. Wakipenda kuwa si kitu, tena wakikubali dharau hata kuzifurahia, watapiga hatua kubwa katika sala na kujazwa mema mengi kuliko yale yote waliyoyatamani.

Baada ya unyenyekevu, tunajiandaa kwa *ufishaji,* yaani roho na matendo ya kujitenga na viumbe pamoja na umimi wetu. Tukihangaikia shughuli au kuvurugwa na mapendo ya kibinadamu mno, wivu, kumbukumbu ya makosa tuliyotendewa, na hukumu zisizo za haki dhidi ya jirani, hatutaweza kuongea na Bwana. Ikiwa mchana tunawasema wakubwa wetu na kutowasikiliza, jioni hatutaona uwepo wake katika sala. Maelekeo yote yasiyofaa yafishwe ili *upendo utawale* rohoni mwetu na kujiinua kwa Mungu katika tabu na faraja vilevile.

Ili tuyafikie maisha ya sala tunatakiwa *kuinua mara nyingi moyo wetu kwa Mungu,* kuongea naye kuhusu lolote, kama tunavyoongea na mtu anayetuongoza kupanda mlima. Tukifanya hivyo, tutakaposimama ili kuongea naye kwa dhati zaidi, tutakuwa na neno la kumuambia na hasa tutajua kusikiliza minong'ono yake kwa sababu tumezoeana naye kitakatifu.

Hatimaye tunapaswa *kuwa na kimya rohoni,* kunyamazisha maono yasiyoratibiwa ili kumsikiliza mlezi wa ndani anayesema kwa sauti ya chini, kama mtu na rafiki yake. Ikiwa kwa kawaida tunajijali mno, tunajifanya lengo la kazi, masomo na utendaji wowote, tutawezaje kuonja utamu wa mafumbo ya Utatu mtakatifu uliomo ndani mwetu, umwilisho ulioleta ukombozi, na ekaristi? Ni lazima fujo za hisi zikome: ndiyo sababu Bwana anazijaribu vikali (katika usiku wa hisi) ili zinyamaze na kuitii roho.

Kazi hizo zote zinaitwa *maandalizi ya mbali ya sala.* Ni muhimu kuliko maandalizi ya jirani (yaani kuchagua la kuzingatia katika sala) kwa kuwa lengo la hayo ya mwisho ni kuchochea tu huo moto wa upendo ambao hautakiwi kamwe kuzimika ndani mwetu bali kulishwa kwa bidii ya kutimiza kiaminifu wajibu wa kila nukta. Upande huo inafaa tushauri *sala wakati wa kazi,* yaani kujichagulia kama robo saa wakati wa kazi ya akili au ya mwili, si kwa kuisimamisha, bali kuifanya kitakatifu zaidi. Zoezi hilo litatuletea faida kubwa: tutaacha kujifanya lengo la kazi zetu, *tukifuata umbile tu* na umimi *katika utendaji,* na tutaanza kuutakasa tukidumisha muungano na Mungu, tukiweka nguvu zetu zote katika kumtumikia badala ya kujiridhisha nao. Hivyo kwa bidii na unyofu tutakuja kulingana na matakwa ya Mungu, na kumkumbuka karibu mfululizo. Jambo hilo litafanya maandalizi ya jirani kwa sala yasihitajike sana, kwa kuwa tutajikuta tayari na kumuelekea Mungu kama jiwe linavyoelekea ardhi likiachwa hewani. Hivyo tutafikia maisha ya sala ambayo yatakuwa kama pumzi ya roho yetu.

### TUNAWEZAJE KUDUMU KATIKA MAISHA YA SALA?

Faida ya udumifu ni kubwa, kumbe tusipodumu tunaweza tukapoteza yote. Kudumu si rahisi: ni lazima tupambane na nafsi yetu, uzembe na shetani anayetuelekeza kukata tamaa. Wengi wanarudi nyuma wanapoachishwa faraja walizojaliwa kwanza; hata wanaoendelea wanaweza wakarudi nyuma. Mt. Katerina wa Genoa, baada ya miaka mitano ya uchungu, aliacha maisha ya Kiroho kwa miaka mitano mpaka Mungu alipomvuta tena kwa nguvu wakati wa kitubio. Hapo kwa miaka kumi na nne ya malipizi makali akatoa fidia kamili akasema, "Ningerudi nyuma ningekubali kung'olewa macho, tena ningeona hata hilo si kitu". Maneno kama hayo yanasisitiza fundisho la kwamba ni afadhali kupofuka kuliko kupoteza neema inayotia utakatifu au hata kurudi nyuma katika njia ya milele. Hilo ni wazi kwa mtu anayeelewa thamani ya uzima wa milele kulingana na maisha haya yanayopita.

Kuna watu waliopambana muda mrefu halafu wakakata tamaa wakiwa wameikaribia chemchemi. Hapo, pasipo sala, hawana tena nguvu ya kubeba kwa moyo msalaba wao, na wanajiachia kuishi kijuujuu na kuingia hatari ya kupotea. Kuna watu wenye akili nyingi na tabia kali wasioweza kubaki katika wastani: ama watakuwa wa Mungu katika njia ya utakatifu ama watajiabudu, kwa mfano wa malaika ambaye ama ni mtakatifu ama ni mwovu tu. Hasa kwao ni muhimu wadumu katika maisha ya sala yanayoweza kuwatia roho ya kitoto, la sivyo watapuuzia maisha ya Kiroho na kutumia nguvu zao zote kwa kiburi wajifanye lengo la kazi na masomo yao.

Basi, ili kudumu katika sala, yanahitajika mawili: kumtumainia Bwana anayewaalika wote kwenye maji hai ya sala, na kukubali kwa unyenyekevu atuongoze kwenye njia aliyotuchagulia.

Kwanza tunapaswa kumtumainia. Ni kukosa tumaini kusema, baada ya muda mrefu wa ukavu, "Sala si kwa ajili yangu", au, "Mimi sifai kusali". Kwa msingi huo tungeweza kusema vilevile, "Kupokea ekaristi mara nyingi si kwa ajili yangu, ila ni kwa watakatifu wachache tu". Kumbe Bwana anawaita wote kwenye urafiki wake wa ndani. Anajifananisha na mchungaji mwema anayewaongoza kondoo zake kwenye malisho ya milele, yaani Neno la Mungu. Katikati ya malisho hayo kuna chemchemi ya maji yaliyo hai ambayo Yesu alimzungumzia mwanamke Msamaria tena mkosefu. Chemchemi hiyo ndiyo Roho Mtakatifu tunayepewa

pamoja na upendo unaotuunganisha naye. Tumepewa awe mlezi wa ndani na mfariji wetu ambaye atupenyeze na kuonjesha maana ya ndani ya Injili. "Huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yoh 14:26). Ahadi hiyo ilitimizwa siku ya Pentekoste, na kwa kila mmojawetu kwa kiasi chake siku ya kipaimara. Mt. Yohane aliwaandikia waamini wa kawaida, "Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua nyote… Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake" (1Yoh 2:20,27). Roho Mtakatifu hakai ndani mwetu ili kupumzika bali afanye kazi kwa vipaji vyake. Basi, tusipoelewa vizuri minong'ono yake ni kwa sababu tunajisikiliza mno na kutokuwa na hamu ya kutosha ya ufalme wa Mungu kutia mizizi ndani mwetu.

Pili, tukubali kuongozwa kwenye njia aliyotuchagulia. Njia ya unyenyekevu na kuambatana na matakwa ya Mungu ni ya lazima; sisi sote tunapaswa kusali kama mtozaushuru. Lakini katika njia hiyo sehemu ina kivuli, sehemu inapigwa na jua; sehemu ni tambarare, sehemu ina mipando mirefu ya kuchosha inayofikisha juu inapofurahiwa mandhari nzuri ajabu. Mchungaji mwema anawaongoza kondoo zake anapoona ni afadhali. Anawaongoza wengine kwa mifano; wengine kwa mifuatano ya mawazo. Anawajalia wengine katika giza la imani wahisi kwa unyofu na undani mapana ya hekima; anawaacha wengine mahali pagumu kwa muda mrefu ili kuwazoesha: kwa miaka mingi Mt. Teresa wa Yesu alilazimika kutafakari kwa msaada wa kitabu, na muda huo alikuwa akiuona mrefu mno. Bwana anawainua akina Maria kuliko akina Marta kwenye sala ya kumiminiwa, lakini hao wa kwanza wanakuta humo mateso ya ndani ambayo wa pili hawayajui, nao pia, wakiwa waaminifu, watayafikia maji yaliyo hai na kuburudika wanavyotamani.

Kama hatufurahii malimwengu bali juhudi zetu zinaelekea maendeleo ya Kiroho, hapo *ukavu* wa muda mrefu unafaa kwa kuwa hautokani na uvuguvugu. Kama vile moto unavyokausha ukuni kabla ya kuuwasha, ukavu huo ni wa lazima kwa *kukausha hisi zetu* zinazoleta vurugu, ili hatimaye zitulie chini ya roho, na upendo safi na wa nguvu ustawi juu ya maono. Hapo, tukiwa waaminifu, tutaanza polepole kumtazama Mungu katika *kioo cha vitu vinavyoonekana* au cha mifano ya Injili. Pengine tutamtazama katika *kioo cha mafumbo ya wokovu,* k.mf. tukitumia rozari. Hatimaye tutamtazama *mwenyewe* katika giza la imani kwa kuzingatia wema wake usio na mipaka unaotushirikisha mema yetu yote; tutaanza kumfikiria daima akiwa ndani mwetu na kuhusisha yote naye. Hapo katika matukio yoyote, hata yale yasiyotarajiwa na ya tabu, tutakumbuka utukufu wa Mungu na kuchungulia wema mkuu ambao yote yanatakiwa kuulenga. Ndiyo maisha ya sala ambayo kwa namna fulani yanawezesha kuona yote ndani ya Mungu na ni utangulizi wa kawaida wa uzima wa milele.

## 2.20. *WACHELEWAJI*

Mwanzoni mwa sehemu ya tatu tutaongea juu ya uongofu wa pili ambao kwa bidii kubwa walau kiasi tunavuka kutoka hatua ya utakaso ya wanaoanza kuingia ile ya mwanga ya wanaoendelea. Lakini wengine kwa uzembe hawavuki kamwe: ni wachelewaji, ni kama watoto wenye matatizo wasiovuka vizuri ubalehe, na hivyo, ingawa hawabaki watoto, hawafikii kamwe ukomavu wa mtu mzima. Inasikitisha kuwa wachelewaji hao, wasiopangika kati ya wanaoanza wala kati ya wanaoendelea, ni idadi kubwa. Wengi wao waliwahi kumtumikia Mungu kwa uaminifu; kumbe sasa wanakaribia kutojali kitu. Kwa hakika wametumia vibaya neema za Mungu, la sivyo angeendeleza ndani mwao kazi aliyoianza, kwa sababu hawanyimi msaada wanaofanya wanavyoweza ili kuupata. Kwa kawaida zinatajwa sababu mbili za hali hiyo ya uvuguvugu: uzembe katika mambo madogo ya utumishi wa Mungu, na kumnyima sadaka anazoziomba.

**UZEMBE KATIKA MAMBO MADOGO**

Uzembe huo unaonekana mwepesi, kumbe unaweza ukawa na matokeo mazito. Kama vile matone ya maji yanavyochimba polepole mwamba, na kama vile matone ya mvua yanavyoleta uhai katika ardhi kavu, ndivyo matendo mema yakirudiwarudiwa yanavyozaa zoea jema (adili la kujipatia) na kulidumisha na kulistawisha; yakitokana na adili la Kimungu, yanapata listawi. Toka alfajiri hadi usiku maadili madogo yanaunda stahili zetu. Katika utumishi wa Mungu mambo yanayoonekana madogo ni makubwa kwa kuwa yanahusiana naye, tena kwa kuwa tunatakiwa kuyatenda kwa maadili yapitayo maumbile ya imani, tumaini na upendo. Hapo tungemkumbuka daima *Mungu* na kuishi kwa ajili yake, tukiongozwa na Roho wake, badala ya kuishi kimaumbile, kufuatana na umimi. Polepole ndani mwetu ari kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa watu ingekua.

Kuzembea mambo madogo ya utumishi huo kunasababisha mapema uzembe katika yale makubwa na kumfanya padri au mtawa, k.mf. asali Sala ya Kanisa pasipo roho ya ibada, asijiandae vya kutosha kwa misa, aiadhimishe kwa kulipua au kuihudhuria pasipo uangalifu unaotakiwa. Hatimaye kwa kufuata mteremko huo anakuwa ofisa tu wa Mungu, akishughulikia mambo matakatifu kwa uzembe, na kuzingatia yale yanayompatia sifa kama mwalimu, mwandishi, mhubiri au mtendaji. *Polepole umuhimu wa maisha unahama* kutoka sadaka ya misa kwenda utendaji wa binafsi *anapotafuta mambo yake* badala ya lengo halisi lipitalo maumbile, hata anasahau *wokovu wa watu* na yale unayoyoadai. Usahaulifu huo unasababisha asizae

kitu. Anayepuuzia madogo kwa kawaida atafikia hatua ya kupuuzia makubwa pia: hapo atawezaje kukabili magumu anayoweza kudaiwa?

**KUKATAA SADAKA ZINAZODAIWA**

Sababu ya pili ya uvuguvugu ni kumnyima Bwana sadaka anazoomba. Wengi wanajisikia kuitwa waishi kikamilifu zaidi, kwa kulenga sala hasa na kutekeleza unyenyekevu ambao usipokuwepo hapana maadili halisi. Lakini wanakataa ama moja kwa moja ama kwa kujisingizia. Hawataki kusikiliza maneno yanayokaririwa katika mwaliko, "Ingekuwa heri leo msikie sauti yake: Msifanye migumu mioyo yenu" (Zab 95:7-8). Wengi wanaoshughulikia kitu kinachowatambulisha wanajisemea mara kadhaa, "Kwa kweli, jambo la kwanza lingekuwa niwe *mtu wa sala: kutenda lolote la nje ni bure* nisipoungana na Mungu". Lakini ingewabidi wajikane ili kumlenga Mungu badala ya umimi. Wakikataa kutoa sadaka hiyo, wanabaki nyuma, huenda wakachelewa moja kwa moja. Hapo wanapoteza ari na kuangukia uvuguvugu yaani, pamoja na kuzembea kwa kawaida, kuambatana na dhambi fulani nyepesi (yaani kuwa tayari kuitenda kwa makusudi ikipatikana nafasi), hatimaye kuwa na nia imara ya kudumu katika hali hiyo.

**ELEKEO LA KUCHEKA WATU**

Sababu nyingine tena zinaweza kusababisha uvuguvugu: *kutojali dhamiri* (k.mf. kwa kusema uongo usiomdhuru jirani); *uzembe* ambao hatimaye unamfanya mtu aache kupambana na kasoro zake na kilema tawala. Hivyo anafikia kupuuzia ukamilifu asiulenge tena kweli. Anasahau kwamba labda ameahidi kuulenga kwa njia ya mashauri ya Kiinjili; anasahau hasa ukuu wa amri ya upendo.

Kati ya sababu za uvuguvugu tutambue hasa elekeo la kucheka watu, lililo kilema kinyume cha haki. Kumfanya mtu achekwe ni kudhihirisha kwamba hatumheshimu; inaweza kuwa dhambi ya mauti ikihusu mambo au watu wanaostahili heshima kubwa (mambo matakatifu, wazazi, wakubwa, watu waadilifu). Dhihaka hizo zinaweza kuwa nzito kwa matokeo yake, kwa kuwapotosha walio dhaifu wasitende mema. "Mimi ni mtu wa kuchekwa na jirani yake, ni mtu niliyemwita Mungu, naye akanijibu" (Ayu 12:4). Dhihaka za kutisha toka juu zinakuja kuadhibu zile za hapa chini: "Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka" (Zab 2:4).

Anayedhihaki ni mchelewaji anayechelewesha wengine na hivyo anakuwa chombo cha shetani bila ya kujitambua. Msimamo wake ni kinyume cha unyofu wa Kiinjili na cha sala ya kumiminiwa. Asiyetaka kutumia wema anamfanya mwadilifu achekwe, kwa kusisitiza kasoro zake na kuchafua sifa zake njema. Kwa nini? Kwa sababu anajiona hana maadili kama mwenzake, lakini hataki kuungama alivyo nyuma kuliko yeye. Basi, kwa chuki anapunguza thamani halisi ya jirani na haja ya uadilifu wenyewe. Anaweza akawadhuru walio dhaifu kwa kuwatia woga, na anapopotea anaweza akachangia upotovu wao.

**MATOKEO MABAYA YA HALI HIYO**

Wachelewaji wanaweza wakafikia upofu wa roho na ugumu wa moyo, hivi kwamba ni vigumu kuwafanya wajirekebishe. "Mtaona kwa urahisi zaidi umati wa watu wa ulimwenguni kuacha vilema na kushika maadili, kuliko kuona mtawa mmoja ameacha maisha vuguvugu kwenda maisha ya bidii" (Mt. Bernardo). Kadiri mchelewaji alivyowahi kufika juu, anguko lake linastahili lawama na uongofu wake unakuwa wa shida; kwa kuwa anafikia hatua ya kudhani hali yake inaridhisha, hana tena hamu ya kupanda juu zaidi. Mtu asipoitambua *saa ya kutembelewa na Bwana,* pengine hiyo haitarudi kabla hajaomba sana. Wachelewaji wako hatarini: tuwakabidhi kwa bikira Maria awaombee neema ya kufufua hamu ya ukamilifu.

"Kuna aina nne za watawa: wengine wakamilifu; wengine waovu, wenye kiburi, wanaojiamini, wanaofuata hisi zao, maadui wa taratibu; wengine vuguvugu, waoga, wasiojali, wazembe; hatimaye wengine waadilifu ambao wanalenga ukamilifu, ingawa labda hawataufikia kamwe.

Hata mashirika matakatifu zaidi yanaweza yakawa na aina hizo nne za watu, kama yale yaliyolegea; ila katika shirika lililoanguka kutoka juhudi zake za awali, umati unaundwa na watawa vuguvugu, halafu kati ya wanaobaki kuna waovu kadhaa, idadi ndogo ya watu wanaofanyia kazi ukamilifu, na wachache sana waliokamilika. Kumbe katika shirika ambapo taratibu zinashikwa bado, umati ni wa watu wanaolenga ukamilifu, halafu kati ya wanaobaki kuna wakamilifu kadhaa, idadi ndogo ya watawa vuguvugu na wachache sana walio waovu.

Hapa tunaweza kuona jambo muhimu: kwamba shirika la kitawa linaelekea kurudi nyuma idadi ya walio vuguvugu inapoanza kuwa sawa na ile ya wenye juhudi, yaani ya wale wanaojitahidi kila siku kupiga hatua mpya katika sala, mkusanyo wa mawazo, ufishaji, usafi wa dhamiri na unyenyekevu. Kwa kuwa wasio na juhudi hizo, hata wakijihadhari na dhambi ya mauti, wanatakiwa kuhesabiwa vuguvugu na wanaambukiza wengine wengi, wakidhuru sana shirika lote. Hao wako hatarini ama mwa kutodumu katika wito ama mwa kutumbukia katika kiburi cha ndani na katika maovu makubwa mno. Wajibu wa viongozi katika nyumba za kitawa ni kufanya kwamba, kwa mifano yao bora na kwa maonyo, maongezi ya ana kwa ana na sala, wale wote walio chini yao wadumu kati ya wenye juhudi wanaolenga ukamilifu, la sivyo wataadhibiwa wenyewe namna ya kutisha.

Kuna mambo manne ambayo yanaharibu maisha ya Kiroho na ni misingi ya misimamo mibaya inayopenya jumuia takatifu: 1) kudanganywa na mvuto wa akili na wa sifa za kibinadamu tu; 2) kujitafutia marafiki kwa malengo ya kibinadamu; 3) kutenda kisiasa kwa kufuata busara ya kibinadamu tu, yaani kutumia ujanja ulio kinyume cha unyofu wa Kiinjili; 4) kujitafutia mapumziko mengi mno katika burudani za ziada, au maongezi na masomo yanayoridhisha umbile tu" (A. Lallemant).

Yatokanayo ni kutamani vyeo, kutaka sifa upande wa elimu na kujitafutia starehe: mambo yanayopingana wazi na maendeleo ya Kiroho. Tuzingatie umuhimu wa kukesha ili *utendaji ubaki chini ya maadili ya Kimungu.* Hayo na matendo yake ni bora kuliko utendaji wowote wa kimaumbile. Kukanusha ukweli huo ni uzushi. Lakini haitoshi kuukiri kinadharia tu, halafu kimatendo kutia maanani k.mf. masomo kuliko maisha ya imani, tumaini na upendo; au kulipua misa ili kuokoa muda kwa ajili ya kazi ambayo haitaweza kuzaa isipohuishwa na *roho*. Ili kukwepa hatari hiyo tukumbuke mara nyingi kuwa Mungu kwa huruma yake anatujalia mfululizo neema tutekeleze vizuri zaidi amri kuu, yaani tulenge upendo kamili: maisha yetu yatakapotua tutahukumiwa juu ya ukweli wa upendo wetu.

**UMIMI ULIOMO NDANI MWETU**

Kadiri ya Y. Tauler, kwa kuwa dhambi yoyote na laana ya milele zinatokana na umimi, inatufaa kuujua kuliko kujua ulimwengu wote. Dalili yake ni *kujifanya lengo la yote, badala ya kumlenga Mungu.* Ukionyesha upendo, ni wa bandia tu. Unadhani una wema na kujivunia matendo yake, hasa yenye *sura ya uadilifu* na utakatifu; unaridhika nayo na kudai ni ya kwake. Ingawa haupendi maadili halisi unajitafutia sifa zinazotokana nayo. *Unaona makosa yake kuwa si kitu,* na unajitahidi kuonekana safi, ingawa sivyo. Pengine unadhani kuwa na ari, ndiyo sababu *unakaripia vikali makosa ya jirani:* "Ungeona dhambi zake, ungesahau zile za wengine, hata zikiwa kubwa sana". Kila unapolaumiwa hautaki kunyoshwa wala *haukomi kujitetea*, ukisema, "Hata wengine wana kasoro zao; upande wangu nimetenda daima kwa nia njema, na kama nimekosa ni kwa ujinga au kwa udhaifu". Unaamini kuwa unamlenga Mungu katika yote, kumbe umejifanya lengo la yote na kuishi kwa kujionyesha tu, badala ya kuwa mwema kweli. Hivyo unajifanya lengo la sala pia: katika faraja unajielekezea Mungu na zawadi zake ili kujiridhisha. Ukija kukosa kinachompendeza, mara unakitafuta kingine ili kustarehe na kukielekeza kwake. "Mpaka utakapojifanya lengo, na kutenda kwa ajili yako, na kudai malipo ya matendo yako, na kutovumilia wengine wakujue jinsi ulivyo kweli, basi ujue kwa hakika unajidanganya vibaya sana. Unapomdharau mtu kwa kasoro zake na kutaka kupendelewa kuliko wasioishi kadiri ya mitazamo yako, basi hujajifahamu, kwa kuwa hujajua ubaya uliomo ndani mwako". Ndicho kinachozuia tusizae matunda ya uzima wa milele. Tunahitaji kujifahamu mpaka ndani ili kumjua Mungu na kumpenda kweli. Kwa ajili hiyo ni lazima tukeshe hisi za nje na za ndani zisitawanyike kwa kufuata viumbe. "Tunapaswa kujijengea chumba moyoni mwetu ili kukikimbilia na kuishi humo kadiri iwezekanavyo, bila ya kujulikana na ulimwengu, tusije tukaondolewa katika kumtazama Mungu. Tusisahau hata kidogo maisha na mateso ya Mwokozi". Kumkazia macho kutazaa hamu ya kufanana naye. Tutakapojikuta hatufanani tutamuomba Roho Mtakatifu atuonyeshe zaidi ubaya wa dhambi na matokeo yake. Tutajishusha kwa unyofu na kutumainia huruma ya Mungu ituinue. Kadiri tutakavyowahi kuufisha umimi, sura yake ndani mwetu itakuwa nzuri na hai, tutamlenga katika yote na kumpenda kwa vitendo.

# 3. **MWANGA WA WANAOENDELEA**

Katika sehemu ya kwanza tumeongelea misingi ya maisha ya Kiroho. Katika sehemu ya pili tumeongelea utakaso wa wanaoanza. Sasa tunatakiwa kusema juu ya wanaoendelea, yaani juu ya hatua ya mwanga ambayo ni mwendelezo wa ile ya utakaso, lakini inadai mwendo wa kasi zaidi. Tukisafiri njia ileile moja, tunaweza tukaona mandhari mbalimbali: sehemu tambarare na mpando pengine mkali; tena tunaweza tukaipitia njia hiyo usiku au mchana, kukiwa na jua au mvua. Ni vivyo hivyo upande wa roho. Halafu tukisafiri kwa garimoshi hatuwezi kuharakisha tusisimame vituoni, wala kusimama kirefu. Hata katika njia ya Mungu kutaka kuwahi mno kunahatarisha maendeleo halisi ya hatua kwa hatua, lakini kusimama mno kunachelewesha, jambo baya vilevile kwa sababu kutosonga mbele ni kurudi nyuma. Basi, tutaeleza hatua ya mwanga kwa mpango ufuatao:

*1) kuingia hatua hiyo:* kumeitwa uongofu wa pili au, kwa usahihi zaidi, kutakaswa hisi;

*2) sifa kuu za hatua ya wanaoendelea;*
*3) ustawi wa maadili ya kiutu;*
*4) ustawi wa maadili ya Kimungu;*
*5) vipaji vya Roho Mtakatifu katika wanaoendelea,* usikivu wao kwake na umakinifu wa kudumu zaidi;
*6) ongezeko la mwanga rohoni kwa njia ya ekaristi;*
*7) sala ya kumiminiwa ya wanaoendelea* na hatua zake;
*8) kasoro za wanaoendelea;* haja ya kutakaswa roho ili waingie hatua ya muungano.

Tutafuata mpangilio huo kwa sababu inafaa tuzingatie ustawi wa *maadili na vipaji* kabla ya maendeleo ya *vitendo vyake,* ili kuonyesha vitendo bora vilivyo lengo la ustawi huo. Tena inafaa kufuata *njia hiyo ya kupanda,* tukizingatia kwanza ustawi wa maadili ya kiutu, halafu ule wa maadili ya Kimungu, halafu ule wa vipaji vinavyokamilisha maadili, hatimaye neema za mwanga, upendo na nguvu tunazotolewa kila siku katika ekaristi. Hivyo tutavumbua kuwa kwa kawaida sala ya wanaoendelea ni ya kumiminiwa. Kama tungeeleza kwanza sala, labda tungeieleza *jinsi ilivyo* katika watu ambao wanaonekana tu kuendelea, kumbe hawaendelei vya kutosha, badala ya kuieleza *inavyotakiwa kuwa* katika hatua hiyo ya mbele.

Kabla hatujaanza kufuata mpangilio huo, tukabili suala lililo muhimu kwa wakati huu, yaani kulinganisha lugha ya walimu wa Kiroho na ile tofauti kiasi ya wanateolojia.

## 3.1. *LUGHA YA WALIMU WA KIROHO NA ILE YA WANATEOLOJIA*

Lugha ya maisha ya Kiroho, yenye msingi katika Biblia, imepata muundo maalumu kwa njia ya walimu wa Kiroho. Polepole misamiati waliyoitumia kutokana na mang'amuzi yao imepenya teolojia ya maisha ya Kiroho, lakini inahitaji kulinganishwa na ile ya teolojia ya kawaida ili kukwepa makosa kadhaa, kama yale aliyoyaangukia Eckart akitamka kwa maana ya kifalsafa maneno yaliyo kweli kwa maana ya Kiroho tu.

### SUALA LA LUGHA YA WALIMU WA KIROHO

Lugha ya walimu wa Kiroho inaonekana na wanateolojia wengi kuwa inatumia mno mifano, tena inapita kiasi. Shida ni kwamba pengine mwenye akili anadai kumsahihisha anayemzidi akili, kama vile kinda angedai kumfundisha tai namna ya kuruka! Wanateolojia hao hawaelewi kuwa "lugha ya Kiroho haina budi kutofautiana na ile ya falsafa; humo mifano ya kuzidisha inatumika si kama pambo la usemi, bali ni namna inayotakiwa kabisa ili kumaanisha mambo kwa usahihi, kwa sababu kazi yake ni kutokeza mang'amuzi, tena mang'amuzi ya hali ya juu, yaliyo magumu kutokezwa kuliko mengine yote… Akili inavuka toka misamiati ya aina moja hadi ya aina nyingine, kama vile kutoka Kilatini kwenda Kichina au Kiarabu. Lakini haiwezi kutumia sarufi ya lugha mojawapo kwa nyingine" (Y. Maritain).

Kwa mfano, Mt. Yohane wa Msalaba anaeleza hali ya kuzama katika sala kuwa ni *kutotenda,* kumbe Mt. Thoma wa Akwino anaiita *"utendaji bora kuliko wowote".* Wa pili anatazama upande wa falsafa, wa kwanza upande wa mang'amuzi ya mafumbo, ambamo *kusimama kwa utendaji wa kibinadamu* kunaonekana kama kutotenda. Vilevile, neno *"maumbile",* maana yake katika falsafa ni ya kinadharia: ni jinsi yalivyokusudiwa na Muumba, pasipo ubaya; kumbe maana ya Kiroho inategemea mang'amuzi ya dhambi ya asili, yaani kwamba madonda yaliyotokana nayo hayajapona kikamilifu hata ndani ya Wakristo, yakiathiri umbile na kujitokeza kama umimi mkubwa unaozidishwa na dhambi za binafsi. Hivyo mafundisho ya lugha hizo mbili hayapingani.

### MISINGI YA KITEOLOJIA YA LUGHA YA WALIMU WA KIROHO

Kila fani ina misamiati yake maalumu isiyoeleweka vizuri kwa wasioijua. Maneno yanatokeza mawazo, kama vile mawazo yanavyotokeza ukweli wa mambo. Mawazo ya sayansi ni sahihi kuliko yale ya kawaida, hivyo pengine yanadai misamiati mipya kuyatokeza. Ikiwa hivyo kwa sayansi, kwa nini isiwe hivyo kwa maisha ya Kiroho?

Teolojia ikitetea lugha ya walimu wa Kiroho inafundisha kwamba tunaweza kusema juu ya Mungu na juu ya maisha ya Kiroho kwa kutumia ama maneno yenye *maana halisi* ama *mifano.* Hivyo tunasema kwa maana halisi, "Mungu ni mwema na mwenye hekima: ndiye wema na hekima yenyewe". Kwa kuwa hizo sifa hazina kasoro, Mungu anazo kuliko viumbe. Kumbe kwa mfano tu tunaweza kusema, "Mungu anaghadhibika": kwa kuwa hasira ni ono la hisi, haiwezi kuwemo ndani ya Mungu aliye roho tu; hivyo "ghadhabu ya Mungu" ni mfano tu wa haki yake.

Tuongeze kwamba kati ya maneno yenye maana halisi yanayotumika kumhusu Mungu, yale *ya kukanusha* (k.mf. "asiyebadilika") *ni sahihi kuliko yale ya kukiri,* kwa sababu *sisi tunajua zaidi Mungu asivyo kuliko alivyo.* Yaani tunajua vizuri kwamba hana mwili, wala mwendo, wala mipaka; kumbe hatuwezi kujua *namna* ambayo sifa za Kimungu zimo ndani mwake na zilivyo kitu kimoja tu katika *ukuu wa Umungu* ambao uko wazi kwa wenye heri wa mbinguni tu, wanaouona moja kwa moja. Ndiyo sababu waliozama katika mafumbo wakimzungumzia Mungu wanatumia zaidi maneno ya kukanusha (k.mf. "asiyeeleweka"), tena wanasema kumtazama hivyo ni bora kuliko kuelewa, kwa sababu kwa namna yake kunafikia juu zaidi, hadi ukuu wa Umungu na maisha yake ya ndani.

Halafu, kati ya majina ya kukiri yanayotumika kwa maana halisi, *yale yasiyobainisha na yale ya kawaida*

ndiyo yanayomtokeza Mungu vizuri zaidi. Kwa hiyo jina YHWH ndilo lake kuliko yote, kwa kuwa fumbo la jina lenyewe linadokeza bahari isiyo na mipaka ya Umungu. Kinyume chake, majina yaliyo wazi (k.mf. "Mwenye akili") hayatokezi inavyofaa ukuu wa Mungu. Ndiyo sababu waliozama katika mafumbo wanasema sala ya kumiminiwa *si wazi* wala haielezeki, hata hivyo ni bora kuliko maneno wazi ya njozi.

Hatimaye, *maneno ya mifano* yanahitajika panapokosekana yale yenye maana halisi. Ndiyo sababu waliozama katika mafumbo wanasema juu ya kuposwa na kuolewa Kiroho ili kumaanisha muungano na Mungu ambao unaigeuza roho. Haja ya kutumia mifano ya namna hiyo inatokana na sisi kujua mambo ya Kiroho kwa njia tu ya vitu vinavyoonekana, pamoja na ugumu wa kupata maneno ya kufaa kuyatokeza.

**MISAMIATI MUHIMU ZAIDI YA WALIMU WA KIROHO**

Misamiati ya kawaida ya Maandiko matakatifu na ya teolojia yanaweza yakatosha kufundishia maisha ya Kiroho; lakini walimu wa maisha hayo, ili kuepa sentensi ndefu mno, walitumia misamiati maalumu au kuipa maana mpya ile ya zamani, kiasi kwamba haisemi ukweli ikitumika upande wa falsafa au wa teolojia ya kawaida. Kwa mfano, wakisisitiza udogo wa kiumbe chochote, ambao mwanateolojia angeutokeza kwa sentensi tano, wanatamka kifupi, *"kiumbe si kitu".* Usemi huo si uongo, isipokuwa tukiuelewa kwa maana halisi ya maneno (hapo ungesema Mungu hajaumba chochote; lakini hilo halihitaji maelezo). Kwa mtazamo wake mwanateolojia angeuongezea msemo huo walau *"peke yake"* aweze kuukubali.

*Misamiati ya kupinganisha* inatokeza jambo kuu kwa njia ya matokeo yake ndani mwetu yaliyo kama kinyume chake. Kwa mfano, "giza kuu" maana yake ni "mwanga usiofikiwa anamokaa Mungu" ambao unatupofusha macho. Vilevile hekima ya Mungu inaitwa "upumbavu" kwa kuwa ndivyo inavyoonekana na wapumbavu: "upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu" (1Kor 1:25).

*Misamiati ya kuzidisha* inataka kudokeza ukuu usio na mipaka wa Mungu (k.mf. "wema mkuu") au udogo wa kiumbe mbele yake. *Misamiati hiyo haipiti ukweli, bali dhana za watu,* kwa kuwa Mungu ni mkuu kuliko tunavyoweza kuwaza, na adhabu zake zinapita ubunifu wetu. Katika maandishi ya kibinadamu, pengine vipimo vinazidishwa ili kumgusa msomaji (k.mf. kwa kusema mtu mrefu ni jitu). Kumbe waliozama katika mafumbo wanatumia misamiati ya kuzidisha kwa sababu wanashindwa kueleza kwa namna tofauti ukuu wa Kimungu; kuzidisha kwao hakuna kosa wala udanganyifu. Mfano wa aina hiyo ni maneno ya Yesu: "Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe… Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe…" (Math 5:29-30). Si suala la kujikata, ila ni usemi unaofaa kuonyesha ukuu wa hatari na haja ya kuikwepa haraka.

Mt. Yohane wa Msalaba alipochora ukurasa wa kwanza wa kitabu chake "Kupanda Mlima Karmeli" aliandika juu ya mapito membamba ya ukamilifu, "kutokuwa na chochote, chochote, chochote, chochote". Ingawa anaonekana kudai mtu ajikane mno, kusudi lake ni kumpandisha kwa njia ya mkato. Juu ya hayo aliandika, "Kwa kuwa sitaki tena kitu kwa kujipendea, napewa vyote pasipo kuvitafuta". Hapo mbele akaeleza, "Kujitenga na viumbe kunaleta furaha na faraja kuliko kutamani kwa moyo kuvimiliki… Mtu akijitenga na vitu anakuja kuvifahamu wazi zaidi, upande wa maumbile na upitao maumbile, na hivyo anavifurahia sana kuliko yule anayeambatana navyo. Anavifurahia kadiri ya ukweli wake, si kadiri ya udanganyifu wake. Hisi zinafikia maumbo tu ya vitu, kumbe roho inapenya ukweli na thamani yake. Kwa sababu hiyo, furaha za hisi zinaitia giza akili yetu… Kuikataa na kuitakasa furaha hiyo kunaiwezesha akili ione vizuri, kama vile hewa inavyong'aa moshi ukiondoka. Aliyejitenga na viumbe anavifurahia vyote kama kwa kuvimiliki, kumbe yule anayetafuta tu kuvimiliki anavikinai bila ya kukifurahia hata kimoja". Mt. Paulo aliwahi kusema, "… kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote" (2Kor 6:10). Mt. Fransisko wa Asizi alifurahia mandhari nzuri za mkoa wake kuliko wenye maeneo yale ambao mawazo yao yote yalilenga tu kuyazalisha iwezekanavyo.

Basi, misamiati hiyo inatuamsha kutoka lepe la usingizi na kutuonyesha lililo muhimu peke yake.

**KULINGANISHA LUGHA YA WALIMU WA KIROHO NA ILE YA WANATEOLOJIA**

Kila mojawapo ina stahili zake. Kwa teolojia inafaa zaidi lugha ya kinadharia, sahihi, inayotumia misamiati kwa maana halisi tu. Lakini kwa kuongoza watu wajikane kwa bidii ili kuungana na Mungu, misamiati ya walimu wa Kiroho inafaa zaidi kwa sababu ni hai, ya kuvutia, mifupi na inaeleweka kimaisha. Haitokezi tu mawazo, bali mang'amuzi na upendo motomoto wa Mungu. Inaepa mizunguko ya maneno na mibainisho inayoweza ikazuia mruko wa upendo huo. Kinyume chake inatuongoza tumtafute Mungu mwenyewe ikitukumbusha kuwa hata kama *ukweli* wa mawazo umo akilini mwetu, *wema* unaolengwa na utashi uko nje ya roho yetu, umo ndani ya Mungu; tena inatufanya tufikirie kwamba yale ambayo ndani ya Mungu hayaeleweki wala hayasemeki, ndiyo mema makuu yanayoweza kupendwa motomoto hata yasipojulikana wazi.

Tofauti ya lugha hizo mbili inaonekana katika kulinganisha maneno yafuatayo ya Yesu na ufafanuzi wake wa kiteolojia: "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele" (Yoh 12:25). Ufafanuzi wa maneno hayo mafupi, hai na ya kimaisha ni

kama ifuatavyo: anayejipenda *kinyume* cha upendo wa Mungu atajipoteza; lakini hatajipoteza akijipenda kimaumbile, yaani kwa pendo lililo *tofauti* na upendo wa Mungu lisiwe kinyume chake; zaidi tena hatajipoteza akijipenda kwa pendo lililomo *ndani* ya upendo wa Mungu. Kubainisha aina hizo tatu za kujipenda ni jambo la lazima kwa teolojia, lakini ni kazi ya akili inayochunguza mambo, kumbe maneno ya Yesu yanatufanya mara tupende kwa bidii.

**IPI LUGHA BORA KATI YA HIZO MBILI?**

Lugha bora ni ile inayotokeza wazo la juu zaidi. Sasa, sala ya kumiminiwa, ingawa si wazi, ni ya juu kuliko nadharia. Basi, lugha ya wanaotushirikisha yale waliyomiminiwa katika sala ni bora kuliko ile ya wanateolojia. Inafaa kwamba baadhi ya wanaozama katika mafumbo ni pia wanashairi hodari waweze kutujulisha vizuri mang'amuzi yao ya ndani, jambo ambalo si la lazima kwa wanateolojia. "Ingawa tunajua kidogo sana mambo ya juu kabisa, kile kidogo tunachokijua kinatosha kutufanya tukipende na kukitamani kuliko ujuzi sahihi kabisa wa mambo ya chini ambao tunaweza tukawa nao" (Mt. Thoma wa Akwino). Hivyo, wazo la kufaa kuhusu Utatu, hata lisipokuwa la wazi, lina thamani kuliko hakika zote za hisabati, kutokana na ubora wa jambo husika. Vilevile sala ya kumiminiwa inang'amua uwepo wa Mungu, jambo bora kuliko tunalolizingatia kwa teolojia; tena namna yake ya kujua ni bora zaidi.

Tuliyoyasema yanathibitishwa na kwamba lugha ya Bwana ndiyo bora; sasa ile ya walimu wa Kiroho inalingana nayo kuliko ile ya wanateolojia. Lugha hiyo inadumisha imani na upendo kwa Mungu, yaani roho yenyewe ya teolojia. Upande mwingine, lugha ya falsafa na teolojia ni ya lazima kwa kufafanua ukweli uliofunuliwa dhidi ya udanganyifu unaoweza ukaupotosha. Ndiyo sababu walimu wa Kiroho waliwaheshimu wanateolojia bora, kumbe waliojidai tu kuzama katika sala waliwapuuzia. Basi, anayeongoza watu Kiroho anatakiwa kujua lugha hizo mbili na kuweza kuzifafanua moja kwa njia ya nyingine. Hatuwezi kusema mtu anaelewa lugha ya walimu wa Kiroho asipoweza kuifafanua kiteolojia, wala kusema anaelewa ukuu wa teolojia asipojua inavyohusiana na maisha ya Kiroho.

## 3.2. **KUINGIA HATUA YA MWANGA**

Mara nyingi Maandiko yanawakumbusha waadilifu haja ya kumuongokea Mungu zaidi. Mwokozi aliwaambia waliomfuata tangu mwanzo, "Amin, nawaambia: *Msipoongoka na kuwa kama vitoto,* hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Math 18:3), katika urafiki wa ndani na Mungu. Aliwahimiza watambue unyonge wao na jinsi wanavyomtegemea Baba wa mbinguni. Kwa namna ya pekee alisema na Mt. Petro kuhusu uongofu wake wa pili wakati wa mateso, "Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe *utakapoongoka* waimarishe ndugu zako" (Lk 22:31-32).

Liturujia inapokariri maneno juu ya uongofu haiwalengi tu wenye dhambi ya mauti wanaohitaji kuacha uovu waingie uadilifu, bali wengine pia ambao, pamoja na neema inayotia utakatifu, wana kasoro nyingi, hivyo wanahitaji kuongoka toka maisha ya Kikristo ya wastani kuingia maisha yenye juhudi: *"Nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote,* na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea. *Rarueni mioyo yenu,* wala si mavazi yenu, *mkamrudie Bwana,* Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma, si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya" (Yoe 2:12-13). Maneno ya namna hiyo yanamuelea mtu kadiri alivyoendelea Kiroho: ingawa ana neema inayotia utakatifu tangu miaka mingi, anajisikia kuhitaji uongofu kamili ili undani wenyewe wa utashi wake umuelekee Mungu tu. Aliyekwisha kulima anarudia ili plau iingie zaidi ardhini na kupindua udongo uzae iwezekanavyo. Kwa mtazamo huo walimu wa Kiroho wamesisitiza haja ya uongofu wa pili ili kuingia hatua ya mwanga ya wanaoendelea. Tutaeleza mafundisho yao tukianzia yale ya A. Lallemant.

**UONGOFU WA PILI KATIKA MAISHA YA WATAKATIFU**

"Kwa kawaida katika maisha ya walio wengi kati ya watakatifu na ya watawa wanaofikia ukamilifu, uongofu unatokea mara mbili: kwanza wanapojiweka wakfu kumtumikia Mungu, pili wanapojitoa kabisa kwa ukamilifu… Uongofu huo wa pili hautokei katika maisha ya watawa wote kwa sababu ya uzembe wao… Basi, tujipe moyo upya tusijihurumie katika juhudi za kumtumikia Mungu… Polepole juhudi zitakuwa tamu zaidi na matatizo yatapungua kwa sababu, kadiri moyo wetu utakavyozidi kutakata, tutapokea neema kwa wingi zaidi na zaidi".

Katika maisha ya watakatifu kuna kipindi cha tabu, kigumu kuvukwa, ambacho kinaingiza katika maisha ya juu zaidi na kuitwa "usiku wa hisi", kikifuatwa na kingine kinachoitwa "usiku wa roho". Ikiwa katikati ya vipindi hivyo unaonekana tayari ushujaa wa maadili (ambao unakuwa wazi zaidi baada ya kile cha pili), maana yake mtumishi wa Mungu amevuka vizuri hayo mahandaki yenye giza; hapo tabu hizo, badala ya kukanusha utakatifu wake, zinauthibitisha.

**HAJA YA UONGOFU WA PILI**

Uwepo wa haja hiyo ni wazi kwa sababu wanaoanza wanajipendea hata baada ya miaka ya juhudi.

“Sababu ya kuchelewa sana kufikia ukamilifu, au kutoufikia kamwe, ni kwamba katika mambo karibu yote tunafuata tu maumbile na busara ya kibinadamu. Tunakubali kidogo sana, au karibu hatukubali kabisa kuongozwa na Roho Mtakatifu, ambaye sifa yake ni kuangaza, kuelekeza na kutia moyo. Watawa walio wengi, hata walio wema na waadilifu, wanapojiongoza na wanapoongoza wengine, wanafuata tu akili na busara ya kibinadamu, ambayo wengi wao wanayo sana. Hiyo ni nzuri, lakini haitoshi kuufikia ukamilifu wa Kikristo” ambao unapita maumbile na kudai tutumie mara nyingi kipaji cha shauri.

“Kwa desturi watu hao wanaongozwa na mitazamo ya kawaida ya watu wanaoishi nao; kumbe hao, hata kama hawavunji taratibu zilizopangwa, wako mbali sana na ukamilifu, kwa sababu idadi ya waliokamilika ni ndogo sana. Basi nao pia hawafikii kamwe vilele vikuu vya roho: wanaishi kama umati unavyoishi, na namna yao ya kuongoza wengine ina kasoro kubwa. Roho Mtakatifu anavumilia muda fulani, akisubiri wajirudi na, kisha kutambua rohoni mwao kazi tofauti za neema na za maumbile, wajiweke tayari kufuata uongozi wake. Lakini wakipoteza muda na fadhili anavyowajalia, hatimaye anawaacha peke yao katika giza la ujinga kuhusu hali yao ya ndani”.

“Wokovu wa mtawa unafungamana moja kwa moja na ukamilifu wake, hivi kwamba akiacha juhudi za kuendelea Kiroho, anapiga hatua kuelekea maangamizi yake na kupotea milele. Asipofikia hapo ni kwa sababu Mungu, akitaka kumuokoa, anamkinga kwa huruma kabla hajatumbukia shimoni. Walimu wote wa Kiroho wanakubaliana kwamba, kutosonga mbele ni sawa na kurudi nyuma. Lakini watawa kadhaa, kwa kuwa wameshaendelea kiasi fulani, wanaishi pengine muda mrefu kidogo kabla hawajatambua kuwa wanarudi nyuma, kwa sababu hilo linatokea polepole”.

“Kati ya watawa tunaweza kubainisha aina tatu tofauti. Wa kwanza ni wale wasiozikatalia kitu hisi zao. Wakiwa na baridi, wanaota moto. Wakiwa na njaa, wanakula. Wakipata wazo la kujiburudisha, wanafanya hivyo bila ya wasiwasi, wakilenga daima kujiridhisha hata wasijue kimaisha maana ya kujikatalia. Kazi zao wanazifanya kiofisi, pasipo roho, ladha wala tunda. Hao wako hatarini… Aina ya pili ya watawa inakwepa kufikia kiasi hicho ikijikatalia raha inazoziona kuwa si za lazima; lakini hao pia wanadanganyika kufuata kinachoonekana chema. Wanafanya mpango unaowapendeza, halafu wanatafuta visingizio vya uadilifu ili kupamba chaguo lao na kutetea mwenendo wao. Kazi zao wanazifanya kiaminifu kwa nje, lakini bila ya kujitahidi kwa ndani na kukusanya mawazo, wakiziacha hisi zao huru mno na kupuuzia utunzaji wa moyo. Watawa hao wamejaa matendo mapungufu na dhambi nyepesi… Aina ya tatu ni ya waliokamilika, ambao wameachana na tamaa yoyote, hawapendelei chochote, wanaridhika na yote na kutafuta tu matakwa ya Mungu. Hao wanafaulu kuunganisha utimilifu wa kushika taratibu za nje na juhudi kwa maisha ya ndani, wakikesha kwa kutunza moyo, wanadumisha amani ya roho na kutekeleza umakinifu kadiri utiifu unavyoruhusu. Watawa hao wanajaliwa fadhili tatu kubwa za Nafsi tatu za Utatu Mtakatifu: toka kwa Baba, nguvu ambayo karibu haishindiki katika utendaji, mateso na vishawishi; kwa Mwana, miali na miangaza ya ukweli inayong’aa mfululizo rohoni mwao; kwa Roho Mtakatifu, bidii, utamu na faraja za kushangaza”.

Haja ya uongofu wa pili inatokana na mabaki yote ya umimi, ambao mara nyingi hautambulikani, lakini unachanganyikana na matendo yetu. Kwa wengi inatokana pia na kwamba hawataki kuonekana wajinga, wasitofautishe vya kutosha ujinga na ule unyofu wa hali ya juu unaotakiwa kustawi ndani mwao. Hivyo wanakuwa wanyofu na wakweli kidogo kuliko awali mbele ya Mungu, ya wakubwa wao na ya nafsi yao. Kwa kisingizio cha kutumia busara wanazingatia tu vipengele vidogo vya mambo makuu na kupuuzia wajibu wa kila siku katika mengi. Polepole, wakiacha unyofu wa mtazamo wa awali unaotakiwa kukamilika katika sala ya kumiminiwa, wanaangukia fujo ya mawazo yanayojidai kuwa ya hekima. Wanasahau kimatendo ukuu wa maadili ya Kimungu na umuhimu wa unyenyekevu.

“Utawani kuna ulimwengu mdogo, ambao mambo yake ni: kujali vipawa vya kimaumbile, kutamani kazi, nyadhifa na vyeo muhimu, kupenda na kutafuta ufanisi na sifa, raha na maisha ya starehe. Ndiyo mambo ambayo shetani anaundia tamasha lake la wanasesere ili kutuvuta na kutudanganya. Yeye anajua kuchezea vizuri mambo hayo yote mbele ya macho yetu hata tukasimama kuyatazama na kuchanganyikiwa nayo, tukipendelea madanganyifu hayo kuliko mema halisi ya kudumu”. Mara ngapi vipawa vya kibinadamu vinaheshimiwa kuliko maadili yapitayo maumbile! *“Sala tu inaweza kutukinga dhidi ya udanganyifu huo.* Yenyewe inatufundisha kupima mambo kwa hekima, yaani kuyatazama kwa mwanga wa ukweli, unaoondoa ono lake la bandia na mivuto yake midanganyifu”.

“Kwa siku moja tu tunatenda zaidi ya matendo mia ya kiburi” karibu bila ya kujitambua; lakini “maangamizi ya roho asili yake ni kuzidisha dhambi nyepesi, kunakosababisha kupungua kwa mianga na miongozo ya Kimungu, kwa neema na faraja za ndani, kwa bidii na moyo katika kupinga mashambulizi ya shetani”. Vipaji vya Roho Mtakatifu vinazuiwa na mshikamano wetu na dhambi nyepesi, vinakuwa kama tanga zilizokunjwa badala ya kupepea. Haitoshi tuelekeze baadaye nia yetu kwa Mungu ikiwa tendo letu ni la kimaumbile tu, na moyo wetu haujatolewa kweli kwake. Kujitoa kijuujuu hakutoshi, unahitajika uongofu mpya na halisi hata moyo umlenge kikamilifu.

Matunda ya uongofu wa pili yanaelezwa na padri huyo katika mawaidha yake kwa wahubiri, “Wengine wanajichosha kabisa kusoma ili kutoa hotuba nzuri, na hata hivyo hawachumi karibu tunda lolote. Sababu gani? Ni kwamba kuhubiri ni kazi ipitayo maumbile kama vile lengo lake, yaani wokovu wa roho, na ni lazima

chombo kilingane na lengo… Wahubiri wengi wana elimu ya kutosha, lakini si roho ya ibada na utakatifu vya kutosha. Njia halisi ya kupata elimu ya watakatifu na kuwa na mawazo ya juu… si kukimbilia vitabu, bali unyenyekevu wa ndani, usafi wa moyo, umakinifu na sala… Mtu anapofikia usafi kamili wa moyo, Mungu mwenyewe anamfundisha, mara kwa mpako wa faraja za Kiroho na wa nderemo za ndani, mara kwa mianga mitamu na ya kupendeza, ambavyo vinafundisha kuigusa mioyo ya wasikilizaji kuliko vinavyoweza kufanya masomo na mbinu nyingine za kibinadamu… Lakini hatufaulu kwa urahisi kuvua kiburi chetu na kujiachilia kwa Mungu... Mtu mwenye maisha ya Kiroho kweli atagusa mioyo kwa neno moja tu lililohuishwa na Roho wa Mungu, kuliko mwingine kwa hotuba nzima aliyoiandaa kwa kazi ngumu na kwa kumaliza nguvu zote za akili yake".

## 3.3. *UONGOFU WA PILI KADIRI YA WALIMU WENGINE*

Mafundisho hayo yaliwahi kutolewa kwa namna nyingine na Mt. Katerina wa Siena, M.H. Henri Suso na Y. Tauler, wote watatu Wadominiko wa karne XIV.

### YALIYOANDIKWA NA MT. KATERINA KUHUSU JAMBO HILO

Kadiri ya Mt. Katerina, Mungu alimuambia kuhusu upendo usiokamilika, "Kati ya wale ambao wamekuwa watumishi wangu wa ndani, baadhi wananitumikia kwa imani, pasipo hofu ya kitumwa: kinachowafanya waaminifu katika utumishi wangu si hofu ya adhabu tu, bali ni upendo. Lakini upendo huo haujakamilika, kwa kuwa katika kunitumikia wanajitafutia faida, yaani kile ambacho ndani mwangu kinawaridhisha na kuwapendeza. Upungufu huohuo umo katika upendo wao kwa jirani. Je, unajua dalili inayodhihirisha upungufu wa upendo wao? Ni kwamba wanaponyimwa faraja walizokuwa wakizipata ndani mwangu, upendo huo hauwatoshi tena, unafifia usiendelee kusimama. Unafifia, na mara nyingi unapoa zaidi na zaidi kwangu, ninapowaondolea faraja za Kiroho na kuruhusu badala yake wapatwe na mapambano na matatizo ili niwazoeshe katika uadilifu na kuwaondolea upungufu huo. Natenda hivyo kusudi tu niwasukume kwenye ukamilifu, na kuwafundisha wajifahamu vizuri na kujihakikishia kwamba wao si kitu, wala kwa wenyewe hawana neema yoyote… Kwa upendo wa namna hiyo usio kamili, ndivyo Mt. Petro alivyompenda Yesu mwema na mpole, Mwanangu pekee, alipofurahia kwa raha kabisa utamu wa urafiki wake wa ndani kwenye mlima Tabori... Lakini ulipofika wakati wa tabu, moyo wote ukatoweka. Si tu kwamba hakuwa na moyo wa kuteseka kwa ajili yake, bali alipopatwa na kitisho cha kwanza hofu ya kitumwa kabisa ikaja kushinda uaminifu wake, hata akamkana akila kiapo kwamba eti! Hajawahi kumfahamu… Ukamilifu wowote na adili lolote vinatokana na upendo, nao upendo unalishwa na unyenyekevu, ambao tena asili yake ni kujifahamu na kujichukia kitakatifu… Basi mtu anatakiwa ajizoeshe kung'oa takwa lake lolote… na kujifungia upwekeni ili kulia, kama alivyofanya Mt. Petro pamoja na wanafunzi wengine… Hata hivyo uchungu wa Petro ulikuwa haujakamilika, ukabaki hivyo siku arubaini zote na hata baada ya Bwana Kupaa, yaani mpaka Pentekoste iliyomaanisha kwa Petro na mitume wengine kuingia hatua ya waliokamilika".

Katika hali hiyo ya kumpenda Bwana kimamluki bado, mara nyingi maongozi yake yanatuachia sisi pia kosa fulani la wazi ili kutunyenyekesha na kutulazimisha kujirudi kama Mt. Petro pale Bwana alipogeuka "akamtazama": basi, "akatoka nje akalia kwa majonzi" (Lk 22:61-62). Tuna sababu za kutosha tukahisi kwa umotomoto wa majuto yake hakurudishiwa tu kiwango cha neema alichopoteza, bali cha juu zaidi. Bwana aliacha aanguke kusudi aponywe kosa la kujiamini kipumbavu, awe mnyenyekevu zaidi na kumtegemea yeye tu. Kisha kuaibika na kulia kwa kosa lake akawa bora kuliko alipopanda Tabori hajafahamu udhaifu wake: alijinyenyekeza, akamshukuru Mungu kwa huruma yake isiyo na mipaka akaendelea hadi kifodini.

Uongofu wa pili unaweza ukatokea pasipo kosa kubwa, k.mf. katika nafasi ya kuonewa au kusingiziwa ambayo, kwa neema ya Mungu, inachochea *njaa na kiu ya haki* badala ya mawazo ya kulipa kisasi. Katika nafasi ya namna hiyo, msamaha wa dhati unamvutia mtu neema nyingi zinazomuingiza kwenye hatua ya juu ya maisha ya Kiroho. Hapo anapata *hisi mpya* kuhusu mambo ya Mungu na *juhudi* asiyowahi kuwa nayo. Mtazamo wa ndani zaidi unaweza ukatokana pia na kufiwa mtu mpendwa, kufilisika, kushindwa vibaya na mengine yote yanayoonyesha ubatili wa malimwengu na umuhimu wa kile ambacho *pekee ni cha lazima.*

Mt. Katerina alisisitiza haja ya kumuendea Baba kwa kumpitia Yesu msulubiwa: tuache kujifanya lengo la yote tukamtafute Mungu kweli tukifuata njia ya kujikana inayoleta amani ya ndani.

### UONGOFU WA PILI KADIRI YA M.H. HENRI SUSO NA TAULER

M.H. Henri Suso alifundisha mengi kuhusu uongofu wa pili, alioung'amua baada ya miaka michache ya kuishi utawani kwa uzembe fulani. Ni muhimu hasa aliyoyasema juu ya watawa wanaozingatia mno masomo au taratibu za nje. Kwa mwanga wa Mungu aliona "aina hizo mbili za watu kuzunguka kandokando ya msalaba wa Mwokozi wasiweze kumfikia", kwa sababu wanajifanya lengo la masomo au la utekelezaji wa taratibu za nje, na wanahukumiana pasipo upendo. Hapo akaelewa alivyopaswa kuzidi kujikana na kuwa tayari kupokea kwa upendo yale yote atakayotaka Mungu, pamoja na kutekeleza upendo mkubwa wa kidugu.

Y. Tauler aliyafananisha makundi hayo mawili na walimu wa sheria na Mafarisayo: "Walimu wa sheria

walikuwa wasomi wanaojali sana ujuzi wao, kama vile upande wao Mafarisayo walivyojali sana ibada zao. Katika misimamo hiyo hakitatoka kamwe chochote chema. Ingawa ni adimu sana watu wasiokwama walau kiasi katika aina mojawapo au zote mbili za matope hayo, wengine wamekwama kuliko wenzao. Kwa jina la walimu wa sheria tuwaelewe… wanaodhani kujua mambo makuu. Ndipo wanapoweka utukufu wao wakitamka sentensi nzito wakati undani wao, unaotakiwa kububujika ukweli, unabaki tupu na mkavu. Upande wao Mafarisayo ni watu wa ibada wanaojiona bora na kujidhania kuwa kitu, wakishika sana ibada zao zote na taratibu zao kwa kudhani nje ya hizo hakuna jema lolote, na kwa kudai wasifiwe na kuheshimiwa kwa hizo. Undani wa roho yao umejaa lawama kwa wale wote wasiofanya sawa nao". Tukikumbuka maneno ya Injili kuhusu sala ya Farisayo na ya mtozaushuru, tutaelewa haja yao ya kuongoka kwa ndani zaidi.

Y. Tauler alifafanua pia *kiu ya Mungu* ambayo inatokana na uvuvio wa Roho Mtakatifu, na kuendana na *ukinaifu kwa viumbe vyote* (yaani kwa fujo, uongo na ubatili wote vilivyonavyo), na *mapambano* dhidi ya maelekeo yasiyoratibiwa ya hisi. Jaribu hilo linafuatwa na kipindi cha pumziko na furaha, halafu mfululizo wa pili wa majaribu ambayo hatua ya waliokamilika inaanza. Ndiyo kazi ya Mungu hasa: kutakasa kwanza hisi, halafu roho, ili mtu aungane naye kwa dhati. Mwanzoni mwa uongofu wa pili Mungu anamwinda, naye pia anamtafuta, lakini kwa mapambano na mahangaiko. Hali hiyo inajitokeza kwa *hamu kubwa ya Mungu na ya ukamilifu,* na kwa *mapambano* "kwa sababu mwili hutamani ukishindana na roho, na roho kushindana na mwili" (Gal 5:17). Ndipo linapotokea hata fadhaiko la mtu kujiuliza kama ataweza kamwe kulifikia lengo analolitamani. "*Mtu anapojikuta amezama katika hangaiko hilo* na anapotambua Mungu anavyomwinda rohoni mwake, *hapo bila ya shaka Yesu atafika na kuingia ndani mwake.* Lakini asipotambua anavyowindwa wala asipohangaika hivyo, Yesu hafiki. Wasiokubali kushikwa na uwindaji huo na fadhaiko hilo, hawawi kamwe wema kweli. Wanabaki walivyo, hawarudi ndani mwao, na matokeo yake hawajui yanayotukia". Tukipaswa kutaabika tupate digrii, hatupaswi kutaabika kidogo zaidi tuufikie ukamilifu. Kuna watu wanaodhani kuwa na hali hiyo, kumbe ni shida za nafsi; lakini pia si adimu watu ambao kweli wana hangaiko hilo, ila wakimkimbilia padri wapate mwanga wanajibiwa, "Usihangaike bure. Tulia tu: matakaso yanayozungumziwa na vitabu fulanifulani ni ya nadra na ya pekee". Baada ya jibu hilo mtu haoni zaidi, tena anajisikia hajaeleweka.

Basi, anayewindwa hivyo afanye "vile tu alivyofanya mwanamke Mkananayo: kumuendea Yesu na kumpazia sauti, yaani hamu kubwa, kwa kusema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi! Lo, wanangu! Mungu kufukuza au kuwinda roho hivyo kunasababisha *mlio wa dua wenye nguvu kubwa ajabu…* kama kutoka vilindi visivyopimika. Huo unapita kabisa maumbile, kwa kuwa ni Roho Mtakatifu mwenyewe anayetakiwa kuutoa ndani mwetu, alivyosema Mt. Paulo, 'Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa' (Rom 8:26)". Hivyo mtu, ingawa anabaki mkavu, anaingia maisha ya kuzama katika mafumbo kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu anayeanza hapo kutokeza kazi yake. Baada ya mlio huo, pengine Mungu anatenda kama Yesu kwa mwanamke huyo, akijifanya hasikii au hataki kusikiliza. Ndipo tunapopaswa kusisitiza, kama mama huyo alivyofanya vizuri ajabu kwa mwanga wa Mungu, aliyekuwa akimtafuta hata kwa makatalio na matusi ya bandia: "*Jinsi hamu ya ndani ya roho inavyotakiwa kuwa kubwa na kali zaidi hapo!…* Hata kama Mungu akikataa mkate, hata akikanusha hali yetu ya kuwa wana… tunatakiwa kumjibu kama vile Mkananayo, *'Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao'* (Math 15:27). Wanangu, tungefaulu hivyo kupenya undani wa ukweli… hapo Mungu au kiumbe chochote asingeweza kuwakanyaga nyinyi, kuwadhalilisha au kuwazamisha chini kiasi ambacho *wenyewe msingejizamisha zaidi…* mkitegemezwa na tumaini kamili, na juhudi kubwa zaidi na zaidi". Ndivyo alivyofanya Daudi akitukanwa na Shimei (taz. 2Sam 16:5-14). "Ndio, wanangu, yote yanategemea jambo hilo, na atakayefikia hapo atafaulu kabisa. *Njia hizo tu zinafikisha kweli kwa Mungu, pasipo kituo katikati.* Lakini kwa bahati mbaya wengi wanaona haiwezekani kufikia kiwango hicho cha kujishusha moja kwa moja na kubaki chini kwa udumifu, kwa hakika halisi na kamili kama alivyofanya mama huyo. Ndiyo sababu akajibiwa, '*Mama, imani yako ni kubwa! Na iwe kwako kama utakavy'o* (Math 15:28). Hakika jibu hilohilo watapewa wale wote watakaopatikana na misimamo hiyohiyo kwenye njia hiyo".

Y. Tauler alisimulia habari za msichana ambaye alijidhania kuwa mbali na Mungu, hata hivyo alijiachia daima katika matakwa yake matakatifu, limtokee lolote lile. Hapo "akainuliwa juu sana kuliko mshenga yeyote na kuvutwa kabisa ndani ya kilindi cha Mungu… Injili inavyofundisha, *'Nenda ukaketi mahali pa nyuma'* (Lk 14:10) *ndipo utakapopelekwa mbele zaidi.* Lakini, 'Kila ajikwezaye atadhiliwa' (Lk 14:11). Uyatamani yale Mungu aliyoyataka tangu milele, upakubali mahali pale ambapo matakwa yake mapendevu yameamua pawe pako". Pengine anataka katika mazingira yetu tuwe kama mzizi mdogo uliofichika ardhini, si ua linaloonekana na wote. Hata hivyo, kazi ya mzizi mdogo unaofyonza rutuba ya ardhi kwa kulisha mti ni kati ya zile za kufaa zaidi: heri wanaoshika nafasi hiyo vizuri! "Wanangu, ndivyo tunavyomuendea Mungu: kwa kujikana kabisa, kwa kila namna na katika yale yote tuliyonayo. Mtu anayeweza kupata *tone moja tu la hiyo roho ya kujikana*, anayepokea cheche yake moja tu, anajikuta tayari na *kufikishwa karibu na Mungu* kuliko kwa kuvua nguo ili kumpa jirani, au kwa kula mawe na miba kama umbile lingemruhusu. *Nukta fupi ya kuishi kwa msimamo huo ingetufaa kuliko miaka arubaini ya vitendo vya kujichagulia".*

## 3.4. ***KUTAKASWA HISI NA KUINGIA HATUA YA MWANGA***

Uongofu wa pili, ambao tunaingia hatua ya mwanga, unaitwa na Mt. Yohane wa Msalaba "kutakaswa hisi" au "usiku wa hisi". Ni muhimu tuone mafundisho yake katika sura hii na ile ijayo.

**HAJA YA KUTAKASWA HIVYO**

*"Kutakaswa hisi ni jambo la kawaida, linalowatukia wanaoanza walio wengi".* Baada ya jaribu hilo *"wanaoendelea wapo katika hatua ya mwanga,* ambapo Mungu analisha na kuimarisha roho… pasipo hiyo kuchangia kwa kazi au mawazo yoyote" ya makusudi. Inachotakiwa kufanya daima ni kuondoa vipingamizi na kuwa aminifu kwa neema. Madondoo hayo yanaonyesha katika hatua gani ya maisha ya Kiroho jaribu tunalolizungumzia linatukia kwa kawaida.

Haja ya utakaso huo inatokana na kasoro za wanaoanza, zinazojumlishwa katika tatu: kiburi cha roho, ulafi wa roho na uzembe wa roho, ambamo tunakuta mabaki ya mizizi saba ya dhambi kama aina za upotovu wa maisha ya Kiroho. *Ulafi wa roho* ni kushikamana mno na faraja za kihisi ambazo pengine Mungu anajalia wakati wa sala, au ni kujifanya lengo la utume au la kazi nyingine. Kwa kawaida *uzembe* unatokana na kwamba, mtu asiporidhishwa alivyotaka kwa ulafi wa roho au aina nyingine ya umimi, anakosa subira na kukinai kazi ngumu ya kulenga utakatifu. Mara nyingi *kiburi cha roho* kinajitokeza ulafi wa roho au aina nyingine ya umimi vikipata vilivyotaka, au mambo yakienda mtu anavyotaka; hapo akitegemea ukamilifu wake, anahukumu vikali wengine, na kujifanya mwalimu: kumbe bado ni mwanafunzi maskini. Kiburi hicho kinasababisha unafiki fulani, jambo linaloonyesha kuwa yuko mbali na ukamilifu.

Pamoja na kasoro hizo anazo nyingine nyingi: *udadisi* unaopotosha adili la kupenda ukweli, *kujiamini* ambako anajithamini mno na kukasirika asipothaminiwa vile, *wivu na kijicho* vinavyosababisha masengenyo, njama na mashindano yanayodhuru jamii. Katika utume kasoro ya kawaida zaidi ni *juhudi za kibinadamu tu* ambazo anajifanya lengo, k.mf. kwa kuvuta watu kwake au kwenye kundi lake badala ya kuwavuta kwa Bwana. Hatimaye anafikiwa na majaribu, kushindwa au ajali; hapo anavunjika moyo, analalamika, anakunja uso, na *kukosa hamu ya kujitahidi*, mambo yanayotaka kuonekana kama unyenyekevu. Hayo yote yanaonyesha haja ya kutakaswa mpaka ndani.

Baadhi ya kasoro hizo zinaweza kurekebishwa kwa ufishaji tunaopaswa kujifanyia kwa nje na hasa kwa ndani; lakini huo hautoshi kung'oa mizizi iliyopenya akili, utashi n.k. "Mtu, kadiri ya nguvu zake, ajitahidi kujitakasa na kujikamilisha; hivyo atastahili neema ya kushughulikiwa na Mungu ambaye atamtakasa kutoka unyonge ule wote asioweza kuurekebisha peke yake. Kwa juhudi zake zote hataweza kamwe kufikia hatua ya kutakata kabisa kwa nguvu zake; zaidi tena hataweza kujiweka tayari kuungana na Mungu katika upendo kamili. Ni lazima Mungu mwenyewe aingilie kati na kumtakasa katika huo moto usioeleweka kwake, kwa namna tutakayosema. Ni lazima kwamba, sawa na daktari bora, atie chuma cha moto kwenye madonda yetu ili kukausha usaha na kansa". Kwa maneno mengine ni lazima *msalaba* unaoletwa na Mungu ili kututakasa utimilize kazi ya ufishaji tunayojifanyia. Msalaba ndio unaofikisha kwenye mwanga wa uzima.

**HISI ZINAVYOTAKASWA**

Hali hiyo inabainishwa na dalili tatu: *"Dalili ya kwanza ni kutoona faraja za kihisi katika mambo ya Mungu wala katika malimwengu…* Bwana akitaka kutakasa hisi hatuachi tufurahie lolote. Ni dalili ya hakika kiasi kuwa ukavu huo na ukinaifu huo havitokani na makosa wala matendo mapungufu tuliyoyafanya hivi karibuni. La sivyo, umbile lingesikia mvuto au elekeo fulani kwa mambo yasiyo ya Mungu… Lakini, kwa kuwa ukinaifu kwa mambo ya mbinguni na ya duniani unaweza ukatokana na ugonjwa wa mwili au wa nafsi unaosababisha mtu asifurahie lolote, basi inahitajika dalili nyingine.

*Dalili ya pili* ya kutakaswa hisi ni *kumkumbuka Mungu kwa juhudi na kuhangaika kwa kutomtumikia* na kwa kurudi nyuma machoni pake, kwa sababu hatufurahii tena mambo ya Kimungu… Hangaiko la kutomtumikia Mungu likibaki ndani mwetu linaonyesha kuwa hali hiyo haitokani na uvuguvugu… Pengine inachanganyikana na shida ya nafsi; hata hivyo ukavu hautakosa kutakasa, ukiwa na hamu kubwa ya kumtumikia Mungu. Basi, mpaka hamu hiyo itakapodumu, hata kama hisi zina huzuni, mahangaiko na udhaifu katika utendaji kwa sababu hazivutiwi, roho inaendelea kuwa tayari na yenye nguvu…

*Asili ya ukavu huo ni kwamba Mungu anaihamishia roho mema na nguvu vya hisi,* na kwa kuwa hisi na umbile haviwezi kufyonza mema ya Kiroho, basi vinabaki na njaa, ukavu na utupu. Hakika hisi haziwezi kupokea yaliyo ya Kiroho tu. Upande wa roho, inayopata polepole lishe hiyo, inaimarika na kukesha na kuwa macho zaidi kuliko awali isimchukize Mungu. Isipofurahia toka mwanzo ladha na furaha ya Kiroho bali inaona ukavu na ukinaifu, ni kwa sababu ya upya wa badiliko… Kinywa cha roho hakijawa tayari wala kuzoea ladha mpya iliyo nyororo mno, kitakavyofanya hatua kwa hatua tu". Kipindi hicho cha mpito kimefananishwa vizuri na watoto wanaoachishwa maziwa ili wapewe chakula kizito zaidi. Wanalilia ladha ya maziwa waliyonyimwa mpaka wazoee chakula kipya wanachopewa.

"Kiini cha lishe hiyo ni *mwanzo wa kuzama katika mafumbo kwenye giza*, ambako ni kukavu kwa hisi na kunabaki kumefichika na kwa siri hata kwa mhusika. Kwa kawaida anayeng'amua ukavu na utupu huo upande wa hisi anajisikia kutamani upweke na utulivu, asiweze kuwaza wala kutaka lolote maalumu. Kisha

kufikia hatua hiyo, kama watu wa Kiroho wangejua kutulia tu… wangesikia *wororo wa lishe hiyo ya ndani* huku wamesahau yote… Lishe hiyo ni nyororo hivi kwamba kwa kawaida mtu akitaka kuionja, haionji kabisa… kama vile hewa isivyoshikika kwa mkono kufumbwa… Hapo mtu akitaka kutenda kwa uwezo wake anazuia kazi ya Mungu badala ya kuisaidia. Kazi ya Mungu inafanyika rohoni, wakati ukavu unapotawala hisi”. Hayo ni *maendeleo ya kawaida* ya maisha ya Kiroho, si jambo la pekee: mtu, ambaye alikuwa akitafakari kwa kupanga mawazo, anajisikia haja ya kutazama mambo ya Mungu kwa namna sahili, ya dhati, hai na ya kimapenzi zaidi; walau kwa kawaida hawezi tena kutafakari hivyo. Ni kama inavyomtokea mtoto aliyeanza kusoma hadithi: ukimnyang’anya hizo na kumrudisha kusoma alfabeti au silabisilabi, hawezi kwa sababu ameshapita hatua hiyo kwa kujifunza kusoma mfululizo. Maisha yanasonga mbele, hatuwezi kuyarudisha yalivyokuwa miaka iliyopita; ni vivyo hivyo upande wa roho.

“Ndipo inapotokea *dalili ya tatu* inayohakikisha ni hatua ya kutakaswa hisi. Ndiyo kushindwa kutafakari au kupanga mawazo kama awali kwa msaada wa ubunifu. Juhudi za kufanya hivyo hazizai lolote. Sababu ni kwamba *Mungu anaanza kujishirikisha kwa mtu,* si tena kwa njia ya hisi, wala kwa mifuatano ya mawazo ambayo inakumbuka na kupanga ujuzi, bali *kwa njia ya roho tu*, pasipo mifuatano ya mawazo, yaani Mungu anajishirikisha *kwa tendo sahili la kuzama katika mafumbo”.* Kisha kuingia hatua hiyo mtu *anazidi kushindwa kutafakari kwa uwezo wake,* ingawa pengine mwanzoni hali hiyo si ya mfululizo. “Katika hali hiyo Mungu anajishirikisha kwa mtu ambaye anabaki bila ya kutenda, kama vile mwanga unavyomfikia mwenye macho wazi asitende lolote kwa lengo la kuupokea. Basi, kwa mtu kuupokea hivyo *mwanga wa kumiminiwa* upitao maumbile ni kuelewa yote akibaki bila ya kutenda”.

Hivyo hali hiyo inajitokeza kwa dalili mbili mbaya (*ukavu wa hisi* na *shida kubwa ya kutafakari* kwa mpango), lakini iliyo muhimu na njema ni *mwanzo wa sala ya kumiminiwa pamoja na hamu kubwa ya Mungu* inayotokana nao. Ukavu na shida ya kutafakari vinatokana na kwamba neema inatwaa namna mpya, ya Kiroho tu, juu ya hisi na ya mifuatano ya mawazo inayotumia ubunifu. Bwana anaonekana kunyang’anya kitu (faraja za hisi), kumbe anatoa zawadi ya thamani zaidi: mwanzo wa sala ya kumiminiwa na upendo ulio wa Kiroho, safi na imara zaidi.

**SABABU ZA HALI HIYO**

Teolojia inaeleza hali hiyo ni *utakaso maalumu ambao unatendwa na Mungu* na kusababisha *mwanzo wa sala ya kumiminiwa,* ambao tena unasababisha *hamu kubwa ya Mungu;* tunaelewa hivyo kwa kuwa hatuwezi kutamani kwa nguvu lile lisilotuvuta. Hamu hiyo kubwa ya Mungu na ya ukamilifu inaeleza *hofu ya kurudi nyuma* (uchaji wa Mungu unaomtawala mtoto wake). Hatimaye *ukavu wa hisi* unaeleweka kwa kuwa neema inayotolewa hapo si ya kihisi bali ya juu: ni *uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu,* anayezidi kutokeza kazi yake kwa njia ya vipaji vyake.

*Kipaji cha elimu* kinaeleza dalili ya kwanza (kukosa faraja yoyote katika malimwengu na katika mambo ya Mungu yaliyofikiwa na hisi), kwa kuwa kinatufanya tung’amue *utupu wa viumbe,* yaani kasoro zilizomo ndani ya hivyo na ndani mwetu wenyewe. Ndiyo sababu kinahusiana na heri ya machozi yanayotokana na kujua uzito wa dhambi na ubatili wa viumbe: “Ubatili mtupu, ubatili mtupu, mambo yote ni ubatili” (Mhu 1:2; 12:8), isipokuwa kumpenda na kumtumikia Mungu.

Dalili ya pili inaonyesha kuwa katika hali hiyo vinajitokeza *vipaji vya uchaji na nguvu* pia. Tunakuta kwa namna wazi *uchaji wa Mungu* ambao ni kuogopa dhambi, si adhabu; uchaji huo unastawi pamoja na upendo, wakati hofu ya adhabu inapozidi kupungua. Kwa kipaji hicho mtu anashinda vishawishi vikali dhidi ya usafi wa moyo na ya subira, vinavyoendana mara nyingi na kutakaswa hisi. Kipaji hicho kinahusiana na heri ya maskini, wasiojidai walimu, bali wanaanza kupenda unyenyekevu wa maisha yaliyofichika ili wafanane zaidi na Bwana.

Katika hamu kubwa ya kumtumikia Mungu kwa vyovyote, inayodumu wakati wa ukavu, vishawishi na matatizo, kinajitokeza *kipaji cha nguvu* kinachohusiana na heri ya njaa na kiu ya haki ambayo Bwana anaisababisha na kuishibisha ndani mwetu. Katika hali ngumu, kipaji hicho kinakuja kusaidia maadili ya subira na ustahimilivu, umotomoto wa roho usije ukazimika kama ule wa hisi. “Kwa kipaji hicho mtu anataka kushinda kizuio chochote na kupita faraja yoyote, ili kumpata anayempenda” (M.H. Yohane Ruysbroeck). Ndio wakati wa kuelewa kwamba, “Ukiuchukua msalaba wako kwa radhi, utakuchukua wewe, utakuongoza mpaka mwisho unaotamani, yaani mwisho wa mateso yote; lakini siyo hapa duniani… Mara nyingine mtu hupata nguvu sana kwa kupenda masumbuko na pingamizi kwa ajili ya kutaka kufuata mfano wa Yesu msalabani. Hata mwisho asingependa tena kukosa mateso… Hiyo neema ina nguvu ya ajabu juu ya mwili dhaifu wa binadamu; inamwezesha kupokea kwa furaha na upendo mambo yote aliyozoea kuogopa na kuepa siku zote” (Kumfuasa Yesu Kristo II,12:5-8).

Hatimaye dalili ya tatu (shida kubwa zaidi na zaidi katika kutafakari) inatokeza *kipaji cha akili:* mwanzo wa sala ya kumiminiwa, ulio wa juu kuliko mifuatano ya mawazo inayotumia ubunifu, unaikata. Hapo mtu anapatwa na mtawanyo wa mawazo pasipo kuusababisha: ni kwamba ubunifu usipokuwa na kazi maalumu unatawanyika kwa kiasi fulani, wakati akili na utashi vinapozidi kuzama katika mafumbo. Ubunifu hautawanyiki hivyo tunaposoma au kutangaza Neno, la sivyo tungekwama. Kumbe unatawanyika inapoanza

sala ya kumiminiwa, ambayo haitegemei mifuatano ya mawazo wala kutumia mlolongo wa picha akilini, hivyo ubunifu unabaki hauna kazi kwa kuwa hauwezi kujihusisha na jambo la Kiroho tu ambalo akili inalielekea kwa namna isiyo wazi. Mt. Yohane wa Msalaba alieleza huo "mwanzo wa sala ya kumiminiwa wenye giza na ukavu" ambapo Mungu anamlisha mtu, akimtakasa na kumjalia aache mifano na apenye maana ya matamko rasmi ya imani, ili kuufikia usahili mkuu ulio sifa ya mtu wa sala hasa. "Mwali wa kwanza wa kipaji cha akili unaumba rohoni *usahili"* (M.H. Yohane Ruysbroeck) unaoshiriki ule wa Mungu. "Kipaji cha akili kinafanya kazi ya kutakasa; kinatakasa roho kwa kuiinua juu ya picha za kihisi na juu ya udanganyifu" (Mt. Thoma wa Akwino). Hivyo kinatukinga na upotovu na kutufanya tusiishie maneno ya Injili bali tuifikie roho yake; kinaanza kutupenyeza vilindi vya mafumbo ya imani yanayotokezwa na matamko yake rasmi, ambayo yanakuwa hivyo kituo cha kwanza, si cha mwisho, cha ujuzi wetu. Kipaji cha akili kitafanya kazi hiyo hasa katika usiku wa roho, lakini kinaitokeza tangu wakati huu katika *tendo la imani la kupenya* linaloitwa *la kumiminiwa* kwa sababu haliwezi kufanyika pasipo uvuvio maalumu. Kwa njia hiyo yanaanza kutokea aliyoyaonyesha Mt. Thoma: "Ili mtu afikie *usahili* wa sala ya kumiminiwa, ni lazima akombolewe kutoka aina mbili za kukosa usahili, yaani ile inayotokana na *tofauti za vitu…* na ile ya *mifuatano ya mawazo:* hiyo inatokea vitendo vyake vinapounganika *kutazama tu* ukweli".

Tunaweza kufupisha yaliyosemwa kwa jedwali lifuatalo:

| DALILI ZA KUTAKASWA HISI KADIRI YA MT. YOHANE WA MSALABA | UFAFANUZI WA TEOLOJIA KUHUSIANA NA VIPAJI SABA |
|---|---|
| 1° *ukavu wa hisi,* kukosa faraja katika mambo ya Mungu na malimwengu | *uvuvio wa kipaji cha elimu* kinachoonyesha ubatili wa viumbe na uzito wa dhambi; ndipo yanapotokea machozi ya majuto halisi |
| 2° *hamu kubwa ya kumtumikia Mungu,* kiu ya haki na hofu ya dhambi;<br>kupinga vishawishi | *uvuvio wa kipaji cha nguvu* kinachodumisha njaa na kiu ya haki wakati wa matatizo;<br>*na wa kipaji cha uchaji* ili kupinga vishawishi |
| 3° *shida kubwa ya kutafakari kwa mpango,* mvuto wa kumtazama tu Mungu kwa upendo | *uvuvio wa kipaji cha akili,* mwanzo wa sala ya kumiminiwa |

Hali hiyo inatofautiana na uchovu wa nafsi kwa dalili ya pili na ya tatu. Hasa hamu kubwa ya Mungu na ya ukamilifu inaitofautisha na uchovu wa nafsi tu unaoweza ukawepo pamoja nayo.

## 3.5. *LA KUFANYA KATIKA USIKU WA HISI*

Ni vema usiku na mchana vipokezane katika maisha ya Kiroho kama katika maisha ya dunia; mradi tujue la kufanya katika vipindi hivyo tofauti, hasa giza likidumu muda mrefu kama katika kipindi tunachokiongelea.

### KANUNI NNE ZA UONGOZI KATIKA HALI HIYO

Kwanza, Mt. Yohane wa Msalaba aliandika kwamba, hasa waliopo katika kipindi hicho cha mpito, *"wanahitaji kiongozi anayeelewa hali yao,* la sivyo watarudi nyuma, watapotea njia, wataangukia uvuguvugu au walau watachelewa kuendelea, waking'ang'ania kabisa kudumisha mbinu yao ya kutafakari na ya kupanga mawazo, au wakidai waonje faraja na kuridhisha vionjo vyao". Wakati huo ni lazima wamuombe shauri kiongozi mwenye mwanga, kutokana na matatizo yanayozuka kisha kunyang'anywa faraja za kihisi, pamoja na ugumu wa kutafakari unaozidi kuwa mkubwa na vishawishi dhidi ya usafi wa moyo na subira ambavyo mara nyingi shetani anavizusha ili kumuondoa mtu katika sala.

Pili, "wanatakiwa kujipa moyo wakidumu kwa uvumilivu; wasihangaikie mateso yanayowapata, bali *wamtumainie Mungu.* Yeye hawaachi kamwe wale wanaomtafuta kwa moyo sahili na mnyofu; *atawajalia neema za lazima kwa kufuata njia mpya* na pengine atawainua kwenye nuru safi angavu ya upendo, akiwapitisha siku za mbele katika usiku wa pili, ule wa roho, kama ataona wanastahili". Hakuna sababu ya kuvunjika moyo katika huo ukavu na utovu wa uwezo, sembuse ya kuacha sala kama kitu kisicho na faida. Kinyume chake, sala ina manufaa zaidi tukidumu kwa unyenyekevu na kujikana na kumtumainia Mungu. Ukavu wa hisi wa muda mrefu, pamoja na kuzidi kushindwa kutafakari, ni *dalili ya uhai mpya wa juu zaidi.* Kiongozi mwenye elimu na mang'amuzi, badala ya kusikitikia hali hiyo, anaifurahia. Kwa kuwa mtu anajikuta na haja yenye heri ya kutoridhika na vitendo vidogo vya imani, tumaini na upendo. Matendo *mapungufu* ya maadili hayo hayamtoshi tena; yanahitajika *matendo ya juu na yenye kustahili zaidi.* Tunakaribia pambazuko

la hatua ya mwanga, inayostahili tuvuke kwa bidii usiku wenye giza unaoitangulia. Tunatakiwa kumtumainia Mungu anapotufanyia kazi chungu ya kututakasa mabaki ya mizizi saba ya dhambi yanayoathiri maisha ya Kiroho: je, tumkimbie daktari wa meno mara anapoanza kututia uchungu ili atuponye? Tusipotakaswa duniani kwa kustahili, tutakaswa toharani pasipo stahili.

Tatu, tusipoweza kutafakari tena kwa mifuatano ya mawazo, *"tunapaswa kuridhika na mtazamo mtulivu wa kimapenzi kwa Mungu".* Kufanya juu chini ili turudi kutafakari kwa mifuatano ya mawazo ni kwenda kinyume cha mkondo wa neema badala ya kuufuata, hivyo ni kujichosha pasipo faida yoyote, ni kushuka tena, badala ya kukubali Mungu atuinue. Lakini inapowezekana, shida katika kutafakari zisipozidi ila zinajitokeza mara kadhaa tu, inafaa kurudia tafakuri sahili ya kimapenzi.

Nne, wenye ukavu wa muda mrefu wanaotaka faraja fulani, *"waepe wasiwasi wowote, hamu kubwa au tamaa ya kuhisi uwepo wa Mungu ili kuridhisha mwonjo wao.* Kwa sababu madai hayo yote yanamvuruga tu mtu, yanamuondoa katika utulivu wenye amani, katika pumziko tamu la sala ya kumiminiwa anayoipata wakati huo… Ni kama mtu aliyepozi ili kuchorwa picha: akigeukageuka huku na huku kadiri anavyopenda, mchoraji anayechanganywa hivyo atawezaje kumaliza kazi yake? Kadiri mtu atakavyotafuta ladha na ujuzi wa kumridhisha, ataonja utupu usioweza kujazwa kamwe kwa njia hiyo". Kwa maneno mengine, kutenda kimaumbile kwa kujifanya lengo, kinyume cha vipaji vya Roho Mtakatifu, unazuia uvuvio wake mwororo. *Tusitafute kuhisi zawadi ya Mungu* katika sala, bali tuipokee kwa mikono miwili katika giza la imani na bila ya kukusudia faida. Baadaye furaha ya Kiroho itakuja kuungana na tendo la kumiminiwa la kusali na la kumpenda Mungu, lakini hatupaswi kuitafuta, ila kumtafuta Mungu mwenyewe, aliye bora kuliko zawadi zake.

Mtu aliyefikia kipindi hicho cha mpito akifuata kiaminifu hayo tuliyoyasema, basi, "utendaji wa akili na utashi unapokoma, hauvurugi tena mwanzo wa *sala ya kumiminiwa* na Mungu. Yeye anamhuisha kwa wingi mkubwa zaidi wa amani, na kumuandaa kuwaka moto wa *upendo* ambao unaletwa na sala hiyo ya kumiminiwa yenye giza na ya fumbo na ambao unaenea rohoni. Kwa kuwa sala hasa ni mmiminiko tu ambao Mungu anautia kwa siri, kwa amani na kwa upendo, tusipouzuia unaiwasha roho kwa upendo". Hapo "mtu anatakiwa kuridhika na mtazamo wa upendo na utulivu kwa Mungu", pamoja na ujuzi wa jumla wa wema wake usio na mipaka, kama vile mtoto mwema anapomuona tena mama yake mpendevu baada ya kumsubiri miezi. Hapimi mapendo yao kama anavyofanya mwanasaikolojia, ila anaridhika na mtazamo wa upendo, utulivu na undani ambao, katika usahili wake, unapenya kuliko utafiti wowote wa elimunafsia. Huo mwanzo wa sala ya kumiminiwa iliyounganika na upendo, tayari ni utekelezaji bora wa maadili ya Kimungu na ya vipaji vya Roho Mtakatifu, ni *tendo la kumiminiwa la imani yenye kupenya* ambapo, katika kimya cha sala, tunapata maana halisi ya yale tuliyoyasoma na tuliyoyatafakari mara nyingi katika Injili. Ndivyo inavyoanza kwa kawaida sala ya kumiminiwa, roho inapoinuliwa kwa Mungu juu kuliko hisi, ubunifu na mifuatano ya mawazo.

Hata hivyo, "anayeanza kumiminiwa sala hajaenda mbali na tafakuri ya mpango kiasi kwamba asiweze kuirudia pengine" asipojikuta chini ya uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu. Mt. Teresa wa Yesu alisema pia juu ya haja ya kukimbilia tafakuri sahili mwanzoni mwa sala ya utulivu: inafaa, basi, kuanza sala kwa kutafakari polepole Baba Yetu au kwa kuongea kitoto na mama Maria ili atufikishe kwenye urafiki wa ndani na Mwanae. Ni vema kukumbuka alivyojitoa mhanga kwa ajili yetu na anavyozidi kujitoa sadaka katika misa. Mtu anayefuata kwa uaminifu njia hiyo, atapokea mara kadhaa mwanga wa ndani utakaomuonyesha maana halisi ya mateso na ya ekaristi. Hivyo maisha ya Kiroho yanazidi kuwa sahili kadiri yanavyoinuka juu: ndilo sharti la kuangaza na kuzaa sana.

**MAJARIBU AMBAYO KWA KAWAIDA YANAENDANA NA USIKU WA HISI**

Kwa kawaida wakati wa kutakaswa hivyo kwa uchungu, vinaongezeka vishawishi dhidi ya usafi wa moyo na subira vinavyoruhusiwa na Mungu ili kuchochea itikio la nguvu la maadili hayo yenye makao katika hisi. Itikio hilo linakusudiwa kuyaimarisha, kuyafanya yatie mizizi mirefu na hivyo yazidi kutakasa hisi na kuzitiisha chini ya akili iliyoangazwa na imani. Kwa sababu hiyohiyo, katika usiku wa roho vitakuwepo vishawishi hasa dhidi ya maadili ya Kimungu yenye makao upande wa juu wa nafsi. Kwa wengi majaribu hayo si makali kama kwa wengine ambao yanawadokezea kwamba, wakiwa waaminifu, Mungu atawafikishia ukamilifu wa juu. Mapambano hayo yakieleweka hivyo yanaonekana muhimu na mazuri kweli: pasipo hayo tungeridhika na juhudi ndogo kuliko maadili tuliyo nayo.

"Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kuliko mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" (1Kor 10:13). "Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo… Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya, watapanda juu kwa mbawa kama tai" (Isa 40:29,31). Jaribu linatufunulia unyonge wetu na haja ya kupata neema ya Mungu, linatulazimisha kuiomba na kumtegemea yeye, sio sisi tena, kama anavyofanya baharia katika dhoruba. "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu bila kupungukiwa na neno"

(Yak 1:2-4).

Tena wakati huo tunaweza tukapotewa na mema kadhaa ya kidunia tuliyoyategemea mno (k.mf. mali, heshima au urafiki); hapo Mungu anaomba kwa ajili yake mapendo hayo makubwa tusiyowahi kupanga tumpe. Pengine anaruhusu ugonjwa tujifunze kuteseka na kwamba peke yetu hatuwezi kitu, bali tunahitaji neema zake kwa ajili ya mwili na ya roho vilevile.

**MATOKEO YA KUTAKASWA HISI**

Tukistahimili vema majaribu hayo, yatazaa matunda ya thamani, hasa ujuzi hai na wa dhati wa Mungu na wa nafsi yetu. "Mtu anayekosa faraja anapojikuta katika hali ya kudumu ya tabu, ukavu na ukiwa, *anaanza kumiliki kweli adili bora la lazima la kujifahamu.* Hapo anaelewa kuwa peke yake hafanyi, wala hawezi kufanya kitu, hivyo hajithamini kwa lolote wala hajiridhii kwa lolote. Hapo Mungu anamthamini zaidi". Akijifahamu hivyo anahisi zaidi ukuu wa Mungu, wema wake usio na mipaka, thamani ya stahili za Yesu na ya ekaristi sadaka na chakula. "Hivyo katika giza la usiku wa hisi unazuka mwanga unaomuangaza juu ya unyonge wake na juu ya ukuu usio na mipaka wa Mungu".

Mt. Katerina wa Siena alisema kuwa ujuzi wa Mungu na wa unyonge wetu ni kama nukta ya juu na ya chini ya duara inayozidi kupanuka. Ujuzi huo wa kumiminiwa kuhusu unyonge wetu ndio mwanzo wa unyenyekevu halisi, unaotufanya tutamani kutojulikana na kuhesabika si kitu ili Mungu awe yote. Upande wake, ujuzi wa kumiminiwa wa wema usio na mipaka wa Mungu, unasababisha *upendo mkubwa, wenye bidii na usiojitafutia faida,* kwa Mungu na kwa watu ndani mwake, tena tumaini kubwa katika sala.

"Hapo upendo wa Mungu unakua, kwa sababu mtu hatendi tena kwa *kuridhisha hisi, bali kwa Mungu tu…* Mara nyingi sana, asipotarajia kabisa na anapozingirwa zaidi na ukavu pande zote, Mungu anamshirikisha ghafla utamu fulani wa Kiroho, upendo safi kabisa, mianga ya akili miororo sana; na kila fadhili ya namna hiyo ina thamani na nguvu kubwa kuliko yale yote aliyoyaonja kabla ya hapo. Lakini ni kweli kwamba mwanzoni hawazi hivyo, kwa kuwa hiyo kazi ya Kiroho ya Mungu, wakati huo ni nyororo sana, hivyo haijulikani na hisi" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Hapo tunatembea katika *mchanganyiko maalumu wa mwanga na giza.* Tunainuka juu ya *giza la chini* linalotokana na viumbe, udanganyifu na dhambi; na tunaingia katika *giza la juu* linalotokana na mwanga ulio mkali mno kwa macho yetu dhaifu: ndio uzima wa Mungu ambao mwanga wake haufikiwi na hisi wala akili peke yake. Lakini kati ya hayo mawili upo mwali wa Roho Mtakatifu, mwanzo halisi wa hatua ya mwanga. Ukiangazwa na mwali huo, upendo uliokuwa wa kimapenzi tu unakuwa na bidii za kutenda na kwa roho ya sadaka unazidi kujinyakulia nafasi ya kwanza ndani mwetu, na kutujaza amani ya kuwashirikisha wengine. "Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima" (Yoh 8:12).

Hatimaye tuangalie kuwa kutakaswa hisi kunajitokeza na *kunavumiliwa kwa kiasi tofauti.* Kwa wasiofanya bidii zaidi "mara nyingi usiku wa ukavu wa hisi unasimamishwa. Unajitokeza na kutoweka mara kadhaa; pengine kutafakari kwa mpango hakuwezekani, pengine ni rahisi… Hao hawamalizi kamwe kuziachisha ziwa hisi zao, waache kabisa kuzingatia na kufikiria lolote; *wana neema hiyo kwa kwikwi tu… Kwa kuwa wanakwepa uchungu unaotakasa, Mungu haendelei kuwatakasa; wanataka kuwa wakamilifu bila ya kukubali kuongozwa kwenye njia ya majaribu yenye kukamilisha*".

## 3.6. ***SIFA KUU ZA HATUA YA WANAOENDELEA***

Hali ya wanaoendelea inatakiwa kuelezwa kwa kusisitiza ujuzi na upendo wao kwa Mungu, na kwa kuzingatia tofauti zilizopo kati ya hatua hiyo na ile iliyotangulia, kama kati ya utoto na ujana.

**UJUZI WA MUNGU KATIKA HATUA HIYO**

Katika hatua iliyotangulia sanasana mtu alikuwa anamjua Mungu kupitia *kioo cha vinavyoonekana* (viumbe, mifano ya Injili na vitendo vya ibada), pamoja na kujifahamu kijuujuu tu. Kumbe anayeendelea amepata kujifahamu zaidi akipitia kipindi kirefu cha ukavu. Kwa kufahamu hivyo unyonge wake, amekuja kumfahamu Mungu pia kama kwa mang'amuzi kupitia *mafumbo ya wokovu* aliyoyazoea. Akiwa mwaminifu, katika mafumbo hayo anavipita vile vinavyoonekana, ashike vile vya Kiroho, hasa thamani isiyo na mipaka ya stahili za Yesu. Kwake rozari si kukariri tu Salamu Maria, bali ni sala hai na shule ya kuzama katika mafumbo. Akiishi vizuri zaidi na zaidi rozari yake, atafikia kumtazama Kristo katika sala. Chini ya Yesu na Maria atazidi kuingia fumbo la ushirika wa watakatifu, na kuchochewa *hamu ya utukufu wa Mungu na ya wokovu wa watu,* pamoja na kutiwa *upendo kwa msalaba,* nguvu ya kuubeba, na pengine mwonjo fulani wa uzima wa milele kwa njia ya tumaini. Zaidi na zaidi atapenya na kuonja mafumbo ya imani na kuyaona katika uhusiano na maisha ya kila siku. Kadiri ya uaminifu wake atajaliwa kipaji cha akili kinachofanya imani ichungulie uzuri sahili na wa hali ya juu wa mafumbo hayo.

Ndiyo sababu hatua hiyo inastahili kuitwa *ya mwanga.* Katika ile iliyotangulia Bwana alijipatia hisi zetu kwa kuzijalia faraja, lakini kwa kuwa tulishikamana nazo mno ilitubidi tuachishwe hizo ili kupewa chakula cha Kiroho na cha nguvu zaidi. Sasa *Bwana anajipatia akili yetu* kwa kuihuisha, akiiangazia anavyoweza yeye tu na kuifanya izidi kuwa sikivu kwake ili ishike ukweli wa Kimungu. Mara nyingi mianga hiyo haitambulikani,

lakini inazidi kutujulisha *roho ya Injili,* juu ya mahangaiko na fujo ya elimu ya kibinadamu tu. Inatufanya tutamani *usahili mkuu wa mtazamo wa upendo* unaotulia katika moyo wa Yesu aliye njia, ukweli na uzima. Hapo pana ujuzi wa Mungu na wa nafsi yetu ulio tofauti na ule unaopatikana kwa kusoma vitabu. Hivyo ni vya lazima kwa kufafanua Biblia, kutetea mafundisho ya Kanisa, kulinganisha maelezo ya wanateolojia. Lakini *tusiishie* maneno yake, bali hayo yawe *mwanzo wa safari* ya kung'amua fumbo lenyewe. Kwa imani tunazo tayari kweli tunazohitaji kuzijua; hivyo badala ya kujitafutia taarifa nyingi za kandokando tuziishi kweli hizo kwa kupokea kwa mikono miwili uvuvio wa Roho Mtakatifu. Si bure kwamba waadilifu wote wana vipaji saba, ambavyo kati yake kile cha akili kinakusudiwa kuwafanya wapenye maana na uzito wa matamko ya imani. Basi, inatokea kuwa wenye moyo safi na mnyofu wanayaona hayo kimaisha kuliko wanateolojia walioridhika na elimu waliyopata kwa kusoma.

Kinachoweza kuzuia tusizame katika mafumbo ni kujidai tunajua mengi, kumbe tunapaswa bado kujifunza mengi Kiroho. Kusoma vitabu hakutaweza kamwe kushika nafasi ya sala; ndiyo sababu walimu wa Kanisa walisema wamejifunza katika sala kuliko katika vitabu bora. Hivyo vinafafanua maneno, kumbe sala ya dhati inaipata ile roho inayoyahuisha, inaupata mwanga wa ndani unaoweza ukaangazia ghafla mawazo yaliyokaririwa bila ya kutambua yanavyohusu mengi katika maisha. Kwa mfano, "Una nini usichokipokea?" (1Kor 4:7) ndiyo msingi wa unyenyekevu, shukrani na upendo kwa Mungu ambaye alitangulia kutupenda na ndiye asili ya uhai, ya wokovu, ya neema na ya kudumu mpaka mwisho. Ndiyo namna ya kumjua anayohitaji mtu anayeendelea.

**UPENDO KWA MUNGU NA KWA WATU KATIKA HATUA HIYO**

Mianga hiyo inatufanya tusimpende Mungu kwa kukimbia tu dhambi za mauti na zile nyepesi za makusudi (kama katika hatua iliyotangulia), bali *kwa kuiga maadili ya Bwana* (hasa upole na unyenyekevu) na kukwepa matendo mapungufu. Hapo, kwa wingi mkubwa zaidi na zaidi wa mianga ya ndani, tutapokea mara kadhaa hamu kubwa ya utukufu wa Mungu na ya wokovu wa watu, na urahisi mkubwa zaidi katika sala (si adimu sala ya kumiminiwa ya utulivu ambapo kwa kitambo utashi unatwaliwa na mvuto wa Mungu) na katika utume (kwa kufundisha, kuongoza na kuratibu mipango). Baadaye tutahitaji kutakaswa roho ili kikome kiburi chote kinachotokana na urahisi huo wa kusali na kutenda. Safari ni ndefu bado, lakini wakati huo roho inastawi, maadili yanakomaa na kutokeza upendo kwa Mungu na kwa watu usioishia miguso, bali ni wa matendo na ukweli.

Basi, kuanzia sasa tutasema juu ya maadili hayo, tukisisitiza yale ya kiutu yanayohusiana zaidi na yale ya Kimungu, yale yanayohusu mashauri ya Kiinjili na yale yaliyotajwa na Yesu; hivyo tutaongozwa kueleza ustawi wa maadili ya Kimungu na wa vipaji vya Roho Mtakatifu unavyotakiwa kuwa katika hatua ya mwanga. Tutapanda juu kuelekea muungano na Mungu, yaani tutaona mambo kadiri ya safari ya mtu anayeendelea kutekeleza lengo lake.

## 3.7. *JENGO LA KIROHO LA WANAOENDELEA*

Ili tueleze ustawi wa maadili unaotakiwa katika hatua ya mwanga, inafaa tukumbuke mfano wa jengo la Kiroho, ambamo ni rahisi kutambua mafundisho mengi ya Yesu na ya Mt. Paulo yalivyoelezwa na Mt. Augustino na Mt. Thoma wa Akwino waliposema juu ya uhusiano wa maadili na vipaji vya Roho Mtakatifu.

Kwanza Bwana alituambia tunavyopaswa kujenga si kwenye mchanga, bali *kwenye mwamba,* halafu Mt. Paulo akaongeza kuwa *mwamba ndiye Kristo,* ambaye yote yajengeke juu yake.

Basi, ili kupandisha jengo hilo tunapaswa kuchimba misingi hadi tukute mwamba wenyewe. Uchimbaji huo wa kina unamaanisha *unyenyekevu* ambao ni wa msingi kwa kuwa unakomesha kiburi, asili ya dhambi zote. Haitoshi tuchimbe juujuu tu; tukimruhusu, Bwana mwenyewe atafanya kazi hiyo kwa kututumia mambo yanayotuaibisha.

Tunavyoona katika mchoro, *nguzo ya* kwanza ya jengo lote ni *imani,* kwa kuwa maadili mengine ya Kimungu yanaitegemea. Mbele yake ipo *nguzo ya tumaini* linalotufanya tumtamani Mungu na uzima wa milele tukitegemea msaada wake ili kuufikia. Juu ya nguzo hizo mbili linapanda *paa la upendo,* ulio adili bora; sehemu yake inayoelekea mbinguni inamaanisha upendo kwa Mungu, ile inayorudi nchini inamaanisha upendo wa kidugu unaotufanya tumpende jirani kwa ajili ya Mungu. Juu ya paa upo msalaba unaotukumbusha kuwa upendo wetu unatokana na stahili za Kristo na mateso yake.

Kila adili la Kimungu linahusiana na kipaji kimojawapo cha Roho Mtakatifu kilichochorwa kama taa. Kwenye nguzo ya imani unapatikana *mwanga wa kipaji cha akili,* kinachofanya imani ipenye Neno la Mungu: k.mf. tukitaka kuchanganyikiwa na kishawishi, tunahisi kwamba Mungu ndiye lengo letu kuu, na kwamba tunatakiwa kudumu waaminifu kwake.

Kwenye nguzo ya tumaini upo *mwanga wa kipaji cha elimu* ambacho tunajua mambo yanavyotokana na viumbe vyenye kasoro. Ndiyo sababu kinatuonyesha ubatili wa malimwengu na wa misaada ya kibinadamu katika kumlenga Mungu. Kwa maana hiyo kipaji hicho kinachokamilisha imani, kinakamilisha tumaini pia kwa kutufanya tutamani zaidi uzima wa milele na kutegemea msaada wa Mungu ili kuufikia. Tumaini linasaidiwa pia na kipaji cha uchaji kinachotukinga na kosa la kujiamini kipumbavu.

Kwenye paa, linalomaanisha upendo, inaning'inia taa ya *kipaji cha hekima* ambayo inaangaza jengo lote na kutuonyesha yote yanavyotokana na Mungu, yaani na upendo wake au walau ruhusa yake inayokusudia jema kubwa zaidi (ambalo tutaliona kwa hakika mbinguni, lakini pengine kuanzia duniani).

Katika jengo hilo anakaa Roho Mtakatifu pamoja na Baba na Mwana ili kujulikana na kupendwa.

Ili kuliingia jengo ni lazima kupitia *mlango* ambao *una bawaba nne,* yaani maadili ya busara, haki, nguvu na kiasi. Pasipo hayo tunabaki nje, kwenye magugu ya umimi na ya maelekeo yasiyoratibiwa. Bawaba mbili za juu zinamaanisha busara na haki zilizopo upande wa juu wa roho, na bawaba mbili za chini zinamaanisha nguvu na kiasi zilizopo upande wa hisi.

Kila bawaba ina ncha tatu zinazomaanisha maadili muhimu zaidi kati ya yale yanayohusiana nayo. Hivyo *busara* inategemeza *utabiri* (wa matokeo ya matendo)*, uchunguzi* (wa hali tunapopaswa kutenda), na *udumifu* (tusije tukaacha kwa sababu ya magumu yanayokabili tuliyoyaazimia mbele ya Mungu baada ya kufikiri: kutodumu ni namna ya kukosa busara).


*Haki* inategemeza maadili mengi; tutaje yanayomhusu Mungu: *ibada* inayompatia heshima inayotupasa, *toba* inayompa fidia ya makosa yanayomchukiza, na *utiifu* ambao tunatekeleza amri zake na za wawakilishi wake (wa Kiroho na wa kidunia).

*Nguvu* inatudumisha kwenye njia njema kati ya hatari kubwa, badala ya kushindwa na hofu: vilevile inategemeza maadili mengine, hasa *subira* inayovumilia matatizo, *moyo mkuu* unaolenga kutenda makuu pasipo kukatishwa tamaa, na *ustahimilivu* unaotudumisha muda mrefu katika shida zinazojirudiarudia kila siku, pengine miaka na miaka.

Hatimaye *kiasi* kinachoratibu hisi zetu, kinategemeza *usafi wa moyo, upole* unaoratibu hasira, na *ufukara wa Kiinjili* unaotufanya tutumie malimwengu bila ya kushikamana nayo.

Kila adili-bawaba linahusiana na kipaji kimojawapo cha Roho Mtakatifu, kilichochorwa kama kito cha kupambia mlango. Busara inahusiana na *kipaji cha shauri* kinachotuangaza busara yenyewe inaposita. Haki inahusiana na *kipaji cha ibada* kinachotusaidia katika ukavu wa muda mrefu kwa kututia upendo wa kitoto kwa Mungu. Nguvu inahusiana na *kipaji cha nguvu* kilicho wazi katika wafiadini. Kiasi kinahusiana na *kipaji cha uchaji wa Mungu* kinachotufanya tushinde vishawishi vichafu: "Mwili wangu unatetemeka kwa kukucha wewe" (Zab 119:120).

**HUMU ANAKAA MUNGU, AKIJULIKANA NA KUPENDWA**




Hayo tuliyoyasema yanaweza yakaonekana kukosa usahili wa mambo ya Mungu, lakini tutauona tena kwa neno lifuatalo. Ikiwa mtu au jumuia fulani msingi na paa vya jengo lake ni kama vinavyotakiwa kuwa (yaani tunakuta *unyenyekevu mkubwa* na *upendo halisi wa kidugu,* ulio dalili kuu ya maendeleo katika kumpenda Mungu), basi yote yanakwenda sawa, kwa sababu hapo Mungu anafidia kwa vipaji vyake upungufu wa ubinadamu, na anakumbusha mfululizo wajibu akitoa neema ya kuutekeleza vema. "Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu" (Mith 3:34; Yak 4:6; 1Pet 5:5) na hawaachi kamwe wanaoshika amri ya upendo: "Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yoh 13:34-35).

## 3.8. *BUSARA NA MAISHA YA KIROHO*

Tuanze kusema juu ya maadili ya kiutu yanayotumikia upendo, adili kuu kuliko yote, na juu ya jinsi yanavyohusiana na maisha ya Kiroho, tukionyesha yanavyotakiwa kustawi kwenye hatua ya mwanga.

Maadili ya Kimungu yanamhusu Mungu aliye lengo letu kuu na kutufanya tumsadiki, tumtumainie na kumpenda kuliko yote, kumbe maadili ya kiutu yanahusu njia za kulifikia lengo hilo. Maadili ya kiutu yanaingiza unyofu wa akili katika utashi na hisi: chini ya busara, polepole haki inakuja kutawala utashi, na nguvu na kiasi zinakuja kutawala hisi. Zaidi tena, yakiwa chini ya imani, yanaingiza katika utashi na hisi *mwanga wa neema,* yaani *kanuni ya maisha ya wana wa Mungu.* Kwa mfano, adili la kiasi likiongozwa na busara tu halizingatii mafumbo ya imani (jinsi tulivyoinuliwa kwenye uhai upitao maumbile, tulivyoathiriwa na dhambi ya asili, uzito wa dhambi ya mauti, thamani ya upendo na urafiki na Mungu, ukuu wa wito wa kuwa wakamilifu kama Baba wa mbinguni). Kumbe likiongozwa na imani pia, linazingatia hayo yote na kulenga sio tu tuishi kadiri ya akili, bali kama wana wa Mungu.

Tukianzia na busara, Bwana aliitaja mara kadhaa, kwa kuwa inahitajiwa na wote ili wajiongoze vizuri, lakini inawafaa hasa wanaotakiwa kushauri au kuongoza wengine. Lakini tuielewe vema, tusije tukaichanganya na vilema vinavyofanana nayo. Basi, tutasema kwanza juu ya kasoro za kuepwa, halafu juu ya adili la busara, na hatimaye juu ya kipaji cha shauri kinachokuja kulisaidia.

### KASORO ZA KUEPWA

Tunatambua zaidi thamani ya adili fulani tukizingatia madhara ya vilema vinavyopingana nalo, ambayo mara nyingi ni ya wazi. Injili inaonyesha matokeo ya kutofikiria yakilinganisha wanawali wenye busara na

wale wapumbavu (taz. Math 25:1-13). Mt. Paulo alisifu busara ya wazee, hasa waliowekwa juu ya jumuia za Kikristo, akiongeza tusiwe "watu wa kujivunia akili" (Rom 12:16) kwa sababu Mungu ataharibu "hekima yao wenye hekima" na kukataa "akili zao wenye akili" (1Kor 1:19) wanaotegemea uwezo na ujanja wao. Yesu alisali, "Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga" (Math 11:25).

Basi, tuepe kasoro mbili zinazopingana: upande mmoja *kutofikiria,* uzembe katika kuzingatia la kufanya, uamuzi wa harakaharaka; upande mwingine *busara ya bandia, "nia ya mwili"* (Rom 8:6), ambayo si adili, ina malengo ya kidunia tu, na mbinu nyingi za kujipatia faida: kwa kufanya hivyo wajanja hawataingia ufalme wa mbinguni.

**BUSARA NA KUJITAWALA**

Inafafanuliwa kama *akili nyofu inayoongoza matendo.* Inaitwa *dreva wa maadili ya kiutu*, kwa kuwa linaratibu matendo ya haki, nguvu na kiasi na maadili mengine yanayotokana nayo, ikipanga kipimo cha kufuata, bila ya kuzidisha wala kupunguza. Lakini ili ipime vizuri *inahitaji* maadili hayo mbalimbali *yawepo* tayari, kama vile dreva wa gari la kukokotwa anavyohitaji farasi waliozoeshwa vizuri. Adili dreva na mengine yanahusiana pande zote na kustawi pamoja. Hakuna mtu anayeweza kuwa na busara asipokuwa na haki, nguvu, kiasi, uaminifu na utaratibu kulingana nayo, kwa sababu "kila mmoja anapima la kufanya kwa kufuata misimamo ya ndani ya utashi wake na hisi zake" (Mt. Thoma wa Akwino): mwenye kiburi anaona ni jema lile linalopendeza kiburi chake, kumbe mwadilifu anapenda kutenda mema bila ya kujulikana. Basi, "uamuzi wa busara ni wa kweli kiutendaji kadiri unavyolingana na unyofu wa utashi" (Mt. Thoma wa Akwino). Tena, busara haitakiwi tu kupima vizuri, bali pia *kuagiza* kwa nguvu matendo maadilifu; lakini haiwezi kufanya hivyo utashi usiponyoshwa na maadili hayo. Unyofu huo ni mzuri; kumbe mara nyingi siasa inazingatia *faida* tu, badala ya *uadilifu,* ikiacha yatendeke maovu makubwa bila ya kutetea haki za wanyonge hata kupatwa na matokeo ya kutisha. Kwa kufidia maovu hayo yanahitajika maisha matakatifu ya watu kadhaa ambao kwa ajili yao Mungu anaweza akatumia huruma kama kwa wale kumi "wenye haki" (Mwa 19:16-33).

Basi, aliyetenda dhambi ya mauti dhidi ya adili lolote, hawezi kuwa na busara yenye msimamo, kwa sababu utashi wake umepotoka kuhusu lengo kuu. Ni lazima tumpende Mungu kuliko nafsi yetu ili busara iwe na msimamo na kushikamana na maadili mengine ya kiutu. Hapo itatushauri mengi yanayojulikana na akili, itatukinga na matendo yasiyofikiriwa, itatawala silika yetu, itatuambia tusifuate ndoto za mchana wala tamaa za hisi, itatukumbusha wajibu wa kupokea mashauri ya watu wenye mwanga na mang'amuzi kuliko sisi, na wa kutii wanaotuongoza.

Adili hilo, kubwa kuliko yale yote linayoyaongoza, haliishii *kutuzuia tusitende* (hasa makuu) kwa kuogopa usumbufu na ugumu. Hiyo ni "busara" ya wasio na moyo wanaoyumbayumba daima kati ya mema na mabaya, watu vuguvugu wanaojitetea kwa kusisitiza wazo lao kuu, kwamba "tusizidishe". Kumbe, adili la busara *linaelekeza kutenda* namna na wakati wa kufaa, bila ya kusahau lengo lipitalo maumbile, wala ari kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa watu.

Mwanzoni mwa malezi maadili ya unyenyekevu, usafi wa moyo na uvumilivu yanasisitizwa kuliko busara, kwa sababu yanamuelekeza aliye nayo aamue vizuri kuhusu maisha ya Kiroho. Lakini baadaye, anapoanza kujiongoza katika mengi na kushauri wengine, anatakiwa kuzingatia madai ya busara asiamue harakaharaka. Hapo tunazidi kuelewa *ukuu wa adili la Kikristo la busara* linalokuja *mara chini ya yale ya Kimungu* na kuingiza mwanga wa maadili hayo katika yale ya kiutu.

Basi, busara ya Kikristo inatakiwa kustawi pamoja na upendo, na *mitazamo yake ipitayo maumbile inatakiwa kushinda zaidi na zaidi mitazamo ya "akili ya chini"* (Mt. Augustino). Lakini busara hiyo ya juu ni ya nadra. Zinafika nyakati, kama za dhuluma, ambapo upungufu wa mitazamo ya kawaida unaonekana wazi. Busara halisi haisahau kamwe ukuu wa lengo tunalopaswa kulielekea, bali inapima kila tendo kulingana na uzima wa milele, si kulingana na desturi za mazingira tunamoishi. Inakumbuka daima kile ambacho peke yake ni cha lazima. Ikisaidiwa na kipaji cha shauri, inakuwa upambanuzi mtakatifu unaopima yote kwa kipimo cha Mungu.

**UPAMBANUZI MTAKATIFU NA KIPAJI CHA SHAURI**

Upambanuzi wa Kikristo unadai kwanza imani kubwa. Busara hairatibu matendo ya maadili ya Kimungu, kwa kuwa ni makuu zaidi na kanuni yake ni Mungu mwenyewe: hayategemei kilele kilicho katikati ya vilema viwili vinavyopingana mabondeni na ambacho kinaonyeshwa na busara. Hata hivyo *utekelezaji* wa maadili ya Kimungu haufanyiki pasipo busara ambayo ionyeshe, k.mf. lini inafaa kusema juu ya imani, ama kutekeleza tendo hili au hili la upendo. Basi, busara ya Kikristo pamoja na upendo vinashikamanisha maadili yote.

Busara hiyo ikiangazwa na *uvuvio maalumu wa kipaji cha shauri,* kinachohusiana nayo, inapatana na unyofu wa njiwa alivyodai Bwana. Unyofu huo kamili si ujinga, unatunza siri zisizotakiwa kutobolewa usiongope kamwe. Kipaji cha shauri kinasaidia busara hasa katika *nafasi ngumu* zisizotarajiwa, ili kulinganisha katika neno au tendo moja maadili yanayoonekana kupingana, k.mf. usemakweli na uaminifu

wa kutunza siri.

Kipaji hicho *kinahusiana na heri ya wenye huruma* kwa sababu mbili. Kwanza, tunatakiwa kuwa na huruma tuweze kushauri vilivyo wanaohitaji msaada huo, tuwainue kwa nguvu na upole bila ya kuwachukiza. Pili, busara inaposita kati ya ukali wa haki na haja ya kutosahau kamwe huruma, kipaji cha shauri kwa kawaida kinatuelekeza kwenye huruma ambayo itamuinua mkosefu na kumrudisha katika utaratibu wa haki, arekebishe alichoharibu kwa kujuta kwa dhati kuliko kwa kuvumilia adhabu pasipo upendo.

Tutaona zaidi ukuu wa busara ya Kikristo tutakapozungumzia unyofu unaotakiwa kuendana nayo daima. Tangu sasa tunaelewa umuhimu wa maneno ya Yesu: "Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote" (Math 24:45-47). Hayo yanahusu kwa namna ya pekee wale ambao wanatakiwa kuongoza wengine, na ambao watapata tuzo kuu: "Walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele" (Dan 12:3).

## 3.9. *HAKI, AINA ZAKE NA KUUNDA UTASHI*

Kati ya maadili-bawaba manne, lile la haki mara nyingi halizingatiwi vya kutosha na wale wanaofuata maisha ya Kiroho: wanajali aina mbalimbali za kiasi, mpango wa busara katika maisha, na upendo kwa jirani, lakini pengine wanapuuzia madai kadhaa ya haki. Tukitekeleza aina zake mbalimbali, tutaunda utashi wetu kwa namna bora. Kwa kuwa adili la haki limo ndani ya utashi ili kuukomboa na umimi, kama vile busara imo ndani ya akili ili kuizuia isipime mambo kijuujuu, na kama vile nguvu na kiasi vimo katika hisi ili kuzikinga na hofu na tamaa zisizoratibiwa.

Utashi ukikosa maadili yanayotarajiwa kuwemo ndani yake una upungufu mkubwa; kinyume chake, ukiwa nayo una nguvu mara kumi zaidi. Humo zinatakiwa kupatikana aina nne za haki, na juu yake maadili ya ibada, tumaini na upendo. Ndivyo utashi na *tabia* vinavyoundwa ili Mkristo aonekane na kuwa kweli mwenye akili nyofu na hasa mtoto wa Mungu. Basi, tutasema juu ya aina mbalimbali za haki tunazozivunja namna nyingi tunaposahau kimatendo kwamba hatutakiwi kuwatendea wengine tusivyopenda kutendewa. Mara nyingi tunafikiria tu *haki katika mabadilishano* (aina ya chini inayoratibu mabadilishano), bila ya kuzingatia vya kutosha *haki katika ugawaji* (inayoratibu kazi ya viongozi ya kugawa faida na mizigo kulingana na stahili, hitaji na umuhimu wa kila mtu) na hasa aina ya juu ya haki inayolenga moja kwa moja ustawi wa jamii nzima kwa kutunga na kutekeleza sheria na maagizo mengine (ndiyo *haki ya kisheria*). Juu tena upo *usawa,* ambao unazingatia si maneno tu ya sheria, bali roho yake, tena si ya sheria za nchi tu, bali ya zile zote zinazoratibu mwenendo wa Mkristo. Tungezingatia aina hizo nne za haki zinazotupasa, tungekwepa mashindano mengi kati ya watu binafsi, matabaka na makundi mbalimbali yanayotakiwa kufanya kazi ileile moja chini ya Mungu.

### HAKI KATIKA MABADILISHANO, HAKI KATIKA UGAWAJI NA MAISHA YA KIROHO

Tunatambua majukumu yetu kuhusu haki tukifikiria kasoro za kuepwa, kwa sababu uchungu unaotupata tukikosewa haki unatufanya tung'amue thamani yake. Basi, matendo dhidi ya haki katika mabadilishano ni uuaji, wizi, dhuluma, riba ipitayo kiasi, masingizio, shuhuda za uongo mahakamani, lakini pia matusi ya hasira, dharau, shutuma na lawama zisizo na msingi, masengenyo, minong'ono ya kutia shaka juu ya wengine, porojo zinazopunguza heshima wanazostahili, na usahaulifu wa kwamba jirani anahitaji sifa njema ili atende mema (kiasi kwamba waliokamilika wanapaswa kujitetea, si kwa ajili yao, bali kusudi waweze kuwatendea mema wengine). Ni ushujaa wa bandia kumcheka asiyeweza kujitetea au asiyekuwepo. Tukivunja haki katika mabadilishano kwa namna yoyote kati ya hizo, tunapaswa *kurudisha* au kufidia madhara tuliyosababisha.

Kasoro inayopingana na haki katika ugawaji ni *ubaguzi.* Ni halali kumpa mmoja kuliko mwingine, ila ni dhambi kufanya hivyo kwa kumnyima huyo wa pili *kitu anachokistahili,* k.mf. tukijali utajiri wa watu hata kuwanyima maskini heshima au misaada ya Kiroho wanayohitaji. Dhambi hiyo ni kubwa katika mambo ya roho kuliko katika malimwengu. Tuangalie upande huo tusije tukawakosea marafiki wa Mungu aliojichagulia kati ya watu duni. Pengine tunawakosea haki watumishi wake wavumilivu tukijua watastahimili yote wasilalamike. Kumbe ni wajibu, tuzo na furaha kuuhisi utakatifu unaotupitia karibu chini ya sura nyenyekevu.

### HAKI YA KISHERIA, USAWA NA KUUNDA TABIA

Juu kuliko haki katika mabadilishano na katika ugawaji, ipo haki ya kisheria (au ya kijamii) ambayo haihusu tu haki za watu binafsi bali *ustawi wa jamii* (yaani nchi, Kanisa na makundi yaliyomo ndani yake); inaelekeza *kujifunza* na kushika kikamilifu sheria za jamii husika. Kwa Mkatoliki ni kujifunza pia miongozo ya Papa kuhusu masuala ya kisasa. Kutofanya hivyo ni kosa linaloleta madhara makubwa kwa wote. Haki ya kijamii inatufanya *tuhisi na kujali ustawi wa jamii* ikituondolea ubinafsi na kutuelekeza tujitahidi kwa faida ya wote, tukijikana na kujinyima muda, starehe na maridhisho kadiri inavyohitajika. Kwa kuwa jamii inatupatia mengi, tunapaswa kujitolea kwa ajili yake. La sivyo *tunainyonya* badala ya kuichangia iendelee. Kila jamii ina

wanyonyaji wake ambao, kama baadhi ya vijidudu na vijimea, wanaweza wakasababisha hata kifo chake. Ili tushinde kilema hicho tunapaswa kutimiza wajibu wa kisheria, kujitolea kwa ustawi wa jamii, bila ya kusahau ulivyo muhimu kuliko ule wa binafsi. Upande huo, kupenda sheria za utawa na za Kanisa ni adili kubwa linalokinga dhidi ya vurugu nyingi. Kwa msingi huo mashirika yanastawi katika sala na utume; lakini kanuni ikipuuzwa, sala na utume vinadumaa. Ndiyo sababu Mungu alitokeza mara kadhaa watakatifu waliofufua juhudi za mwanzoni.

Hatimaye, juu ya haki ya kijamii upo usawa (kwa Kigiriki "epi dikaion" = juu ya haki) ambao hauzingatii tu maneno ya sheria, bali hasa lengo la yule aliyeitunga. Kwa kuwa unazingatia *roho ya sheria,* hauitafsiri vikali mno bali kwa akili ya juu, kwa namna ya pekee katika nafasi maalumu ambapo haifai kuitekeleza ilivyoandikwa isije ikatimia mithali ya Kilatini inayosema, "summum jus summa injuria" (= ukali wa sheria ni utovu mkubwa wa haki). Mtungasheria anazingatia yanayotokea kawaida, ingawa sheria anayoitunga haitaweza kutekelezwa na mtu fulani katika nafasi za pekee, ngumu na chungu. Kwa mfano, kitu kilichowekezwa kinatakiwa kurudishwa kwa mmiliki, lakini haifai tumrudishie tukijua atakitumia vibaya (kama vile silaha katika hasira). Usawa, unaotukinga na Ufarisayo, ndio aina ya haki iliyo bora na inayolingana zaidi na hekima. Haudharau sheria, ila unapima utekelezaji wake mmojawapo kwa kulenga juu kuliko maneno ya sheria, kwenye mahitaji halisi ya jamii na heshima anayostahili binadamu. Jambo hilo muhimu linakuja kueleweka tu baada ya kuishi miaka mingi. Basi, usawa unafanana na upendo ambao uko juu zaidi tena.

**HAKI NA UPENDO**

Kisha kujua ukuu wa haki na aina zake, tunaweza kuona wazi zaidi uhusiano wake na upendo unaotakiwa kuihuisha kutoka juu. Maadili hayo mawili yanaratibu mafungamano ya watu, ila yanatofautiana kwa kuwa haki inatudai *tumpe kila mmoja anachostahili* na tumuache *atumie haki yake.* Kumbe kwa upendo tunampenda Mungu kuliko yote, na *kwa ajili yake tunampenda jirani kama nafsi yetu.* Hivyo haki inamtazama jirani kama *mtu mwingine*, wakati upendo unamtazama kama *mimi mwingine.* Adili la haki linaheshimu stahili za mtu, kumbe upendo unatoa zaidi, kutokana na kumpenda Mungu na mtoto wake. Hivyo tunaelewa kwamba "*amani ni tunda la haki si moja kwa moja,* ila kwa sababu haki inaondoa vinavyozuia amani. Lakini *amani ni moja kwa moja tunda la upendo,* kwa kuwa upendo unazaa amani kwa umbile lake. Kwa sababu upendo ni *nguvu inayounganisha;* na amani ndiyo muungano wa mioyo na matakwa" (Mt. Thoma wa Akwino).

**MAADILI YANAYOTEGEMEA HAKI KATIKA MAISHA YA KIKRISTO**

Haki inayohuishwa na upendo inafuatana na maadili mengine ya kufanana nayo. Mojawapo ni bora kuliko haki yenyewe, yaani adili la *ibada* ambalo linampatia Mungu heshima inayotakiwa kwa ndani na nje, utiifu, sala na sadaka ya kuabudu, ya kufidia, ya kudua, ya kushukuru; pia linatukumbusha tuwaheshimu watakatifu na kwa namna ya pekee Mama wa Mungu. Hilo lifuatane na *toba* ili kufidia makosa dhidi ya Mungu. Haki inategemeza pia *heshima ya kitoto* kwa wazazi na nchi*, heshima* kwa watu kulingana na stahili, umri na cheo chao, *utiifu* kwa wakubwa, *shukrani kwa misaada,* uangalifu wa *kuadhibu kwa haki* inapofaa (pamoja na kutumia huruma), hatimaye *usemakweli* katika maneno na mwenendo. Inatukumbusha kuwa *urafiki una haki na wajibu* wa namna yake, ingawa hauwezi kudai kitu mahakamani. Pia, kuna wajibu wa *upendevu,* unaopingana na ulaghai na mabishano ya bure vilevile. Hatimaye kuna wajibu wa *ukarimu,* unaokwepa kwa pamoja uroho na ubadhirifu.

Hayo yote ni muhimu, lakini hata wanaofuata maisha ya Kiroho hawayafikirii vya kutosha, hivyo wanajipendea kuliko kuwajali wenzao. Pengine kwa kisingizio cha upendo, ari chungu inavunja upendo na haki kwa kuhukumu bila ya msingi, kusengenya na kutia shaka juu ya jirani. Kinyume chake, tungeyatimiza kwa bidii tuliyoyazungumzia, utashi ungenyoshwa na kuimarishwa na kuandaliwa uishi kwa maadili ya juu zaidi, yaani tumaini na upendo, yanayotakiwa kutuunganisha na Mungu na kudumisha muungano huo katika nafasi mbalimbali za maisha, hasa zile ngumu na zisizotarajiwa. Kuwa Wakristo hata katika matendo madogo, ndiyo heri halisi ya wanaomfuata Yesu.

Adili la haki, ambalo ni la pili kati ya maadili-bawaba, ni bora kuliko nguvu na kiasi, hata kuliko ubikira. Ukuu wake unajitokeza hasa katika tamko la Yesu alipolizungumzia katika maana ya juu ambamo yote tuliyoyasema yamo, tena kwa namna bora iwezekanavyo: "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa" (Math 5:6).

## 3.10. ***SUBIRA NA UPOLE***

Nyakati hizi ngumu inafaa tuyakumbuke maneno ya Bwana kuhusu adili la nguvu linalohitajika tusiogope tishio lolote wala kuzuiwa na pingamizi lolote kwenye njia ya wokovu. Tutasema hasa juu ya subira iliyo namna ya kawaida zaidi ya kutekeleza nguvu katika matatizo. "Kwa subira yenu mtaziponya nafsi zenu" (Lk 21:19).

## SUBIRA NA USTAHIMILIVU, NGUZO ZA MAISHA YA KIROHO

Subira ni adili ambalo linategemea nguvu na kuzuia mtu asiache kufuata akili iliyoangazwa na imani akishindwa na matatizo na huzuni; linamfanya avumilie mabaya asivurugwe nayo. *Asiye na subira, hata akiwa mkali, ni dhaifu tu:* kwa kweli anapofoka ameshindwa kiadili. Kinyume chake, mwenye subira anavumilia baya lisiloepukika ili aendelee kupanda kwa Mungu. Hiyo ni tofauti na ugumu wa wale wanaovumilia mapingamizi mradi wafikie matamanio ya kiburi chao. Kwa adili hilo mtu anatawala dhoruba za hisi zilizopatwa na huzuni. Wafiadini wanajitawala na kuwa huru kwa namna bora. Katika subira tunakuta sehemu ya tendo kuu la adili la nguvu: *kuvumilia tabu bila ya kushindwa nazo.* Kuvumilia kwa muda mrefu kinachopingana na umbile ni kugumu na kustahili kuliko kumshambulia adui kwa muda mfupi wa ari. Basi, ikiwa nguvu inavumilia mapigo yanayomuua askari vitani na hasa mfiadini, adili la subira linavumilia matatizo ya maishani bila ya kuyajali. Hivyo linalinda maadili mengine dhidi ya vurugu na kutegemeza jengo la Kiroho. Lakini ili subira iwe na msimamo ni lazima mtu awe na neema inayotia utakatifu, yaani upendo unaomjali Mungu kuliko yote na kwa vyovyote: "Upendo huvumilia" (1Kor 13:4).

Matatizo yakidumu muda mrefu mfululizo, inavyomtokea mtu anayepaswa kuishi na mkorofi, linahitajika adili ambalo linafanana na subira na kuitwa *ustahimilivu,* kutokana na urefu wa majaribu, mateso na dharau. Ili tutekeleze adili hilo Kikristo tukumbuke mara nyingi subira ya Mwokozi msalabani, inayopita wazo lolote la kibinadamu. "Bwana awaongoze mioyo yenu mkapate pendo la Mungu, na saburi ya Kristo" (2Thes 3:5). Kwa upendo wetu alivumilia mateso ya mwili makali mno, pamoja na yale ya roho yaliyomjia kutoka kwa watu wake na hata kwa kujisikia amelaaniwa na Mungu kwa niaba ya dhambi alizozibeba. "Kumbukeni mara nyingi kuwa Bwana wetu ametuokoa kwa kuteseka na kuvumilia, na kuwa vivyo hivyo sisi tunapaswa kuufikia uzima wa milele kwa njia ya mateso na huzuni, kwa kuvumilia dharau, upinzani na masikitiko kwa upole mkubwa iwezekanavyo… Wapo wanaokubali tu mateso yanayoleta heshima, k.mf. kujeruhiwa vitani… Aliye mvumilivu kweli na mtumishi wa Mungu anavumilia vilevile tabu zinazoleta aibu ya kusemwa, kulaumiwa na kutendwa vibaya na watu wema, marafiki, ndugu… Upinzani unaotoka kwa watu wema unavumilika vibaya zaidi, lakini unatokea mara nyingi sana" (Mt. Fransisko wa Sales). Tabu zilizovumiliwa vizuri ndizo matofali yanayojenga wokovu wetu, fungu la wana wa Mungu hapa duniani na *dalili ya uteule,* kwa kuwa "imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi" (Mdo 14:22). Pengine tendo moja la subira kubwa kufani linatosha kutupatanisha na Mungu. Tujifunze kuteseka kwa utulivu, pasipo manung'uniko. Watakaoshiriki zaidi mateso ya Yesu watatukuzwa zaidi pamoja naye.

## UPOLE WA KIMUNGU NA MATUNDA YAKE

Upole unaotakiwa kuendana na subira unatofautiana nayo kwa kuwa tokeo lake maalumu ni *kuzuia vurugu za hasira,* si kuvumilia tabu. Adili la upole ni tofauti na silika ya upole kwa sababu linaratibu kwa mwanga wa akili (na wa imani) hisi zilizotikiswa na hasira. Adili hilo ni bora kuliko tabia hiyo ya kisaikolojia, kama vile usafi wa moyo ulivyo bora kuliko elekeo la haya, na adili la huruma kuliko ulaini wa moyo. Mara nyingi tabia ya upole inajitokeza kwa watu wanaopendeza, lakini inaendana na ukali kidogo kwa wasiopendeza. Kumbe adili la upole linaondoa ukali na uchungu kwa wote na katika nafasi yoyote. Tena linaingiza utulivu fulani hata unapotakiwa ukali: kwa kuwa linategemea adili la kiasi, linapenda kutozidisha.

Upole huo unakusudiwa kutawala si maneno na mwenendo tu, bali moyo pia, la sivyo ni wa bandia. Ukisababishwa na lengo lipitalo maumbile na ukitekelezwa hata kwa watu wakali, upole ni "*ua la upendo"* (Mt. Fransisko wa Sales). Katika mmea ua ndiyo sehemu ya kuvutia zaidi, na ingawa ni dhaifu lina kazi muhimu ya kutunza tunda linaloundika ndani yake. Vivyo hivyo upole ndio unaovutia zaidi katika utekelezaji wa upendo. Ndiyo sura yake ambayo inajitokeza katika macho, tabasamu, mwenendo na maneno, ikizidisha thamani ya huduma inayotolewa. Pia unatunza matunda ya upendo na ari, kwa kufanya mashauri na maonyo yapokewe vizuri. Tunaweza tukawa na ari kwa jirani, lakini tusipotumia upole hatutaonyesha tunawapenda, na nia zetu njema zitashindikana kwa sababu tutaonekana kusema kwa hasira kuliko kwa busara na hekima.

Upendo unastahili kwa namna ya pekee unapotumiwa kwa wanaotutesa; hapo kwa hakika si wa kimaumbile, bali unatoka kwa Mungu na pengine unamgusa aliyetukasirikia bure. Sala ya Mt. Stefano (taz. Mdo 7:60) ilimvutia Saulo neema ya uongofu, na upole unawaondolea silaha wakatili. "Hakuna kinachoweza kumtuliza tembo aliyekasirika kuliko sura ya mwanakondoo, na hakuna kinachozuia nguvu ya mzinga kuliko sufu" (Mt. Fransisko wa Sales). Pengine upole wa Kikristo unaogeuza shavu la pili unamtuliza mwenye hasira walau kidogokidogo.

"Ni afadhali kuunda watubu kwa kutumia upole kuliko kuunda wanafiki kwa kutumia ukali… Mjitahidi kutekeleza upole mnyenyekevu unaowapasa kwa wote, kwa kuwa ndio adili bora alilotusisitizia Bwana wetu. Ikiwatokea kukosa dhidi yake, msifadhaike, bali kwa tumaini kubwa muinuke tena na kuendelea na safari kwa amani na upole kama awali" (Mt. Fransisko wa Sales). Tunashika nzi wengi zaidi kwa tone la asali kuliko kwa pipa la siki. Inahitajika ari, lakini yenye upole na subira. Basi, tuepe *ari chungu* ya kukaripia daima ambayo inasababishwa na kiburi na iliharibu marekebisho mengi utawani. Dhidi yake Mt. Yohane wa Msalaba alisema, "Pasipokuwa na upendo wa kutosha, mpatie upendo, nanyi mtavuna upendo".

*Heri ya upole* inahusiana na *kipaji cha ibada* ambacho kinatutia mvuto wa upendo wa kitoto kwa Mungu

tuzidi kumuona kama Baba mpendwa; hivyo kinatufanya tuone watu kuwa ndugu, watoto wa Baba yuleyule, si watu tusiohusiana nao wala wapinzani. Kipaji hicho kinatusemesha kwa dhati zaidi na zaidi, "Baba yetu uliye mbinguni…", tukitamani ufalme wake uimarike ndani yetu na ya ndugu zetu; hamu hiyo inasababisha upole unaong'aa kwa jirani.

Ili tutekeleze vizuri adili hilo, tunapaswa kulizingatia lilivyo ndani ya Bwana, upole upitao maumbile ambao umetokana na ari ya kuokoa watu bila ya kuipunguza, kama alivyotabiriwa, "Hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima" (Isa 42:2-3). Alipobatizwa alishukiwa na Roho Mtakatifu kwa sura ya njiwa, akatambulishwa kuwa "Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yoh 1:29). Hatimaye msalabani akawasamehe watesi wake kwa kuwaombea. Ndio upole katika tendo kuu la nguvu; tabasamu ya Msulubiwa ndiyo sura bora ya wema hapa duniani. Upole wa namna hiyo ni moja ya dalili zinazobainisha zaidi mashahidi wa kweli. Watu wengine wanayafia mawazo yao, na kiburi kinawafanya wavumilie mateso; ndani mwao haupatikani *ulinganifu wa maadili yanayoonekana kupingana*. Kumbe wafiadini ni wapole hata kwa watesi na wanawaombea; sasa kusahau mateso yao wenyewe ili kufikiria wokovu wa watesi ni dalili ya upendo mkuu unaolinganisha maadili yote ndani yake.

Tumuombe Bwana adili hilo pamoja na unyenyekevu wa moyo; tumuombe kwenye komunyo, katika ule muungano wa dhati wa roho yetu na yake, wa akili yetu na yake, wa moyo wetu na wake uliofurika upendo. Tumuombe mara nyingi, halafu tukipata nafasi tuyatekeleze maadili hayo kwa bidii. Hapo yatatimia maneno yake: "Mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi *mtapata raha nafsini mwenu"* (Math 11:29). Wakati wa ukinaifu na mahangaiko tung'amue raha hiyo kwa kusamehe kabisa waliotukosea. Kwa msaada wa neema tutarudi mahali petu mbele ya Bwana na ya jirani, kwenye utulivu wa utaratibu tuliopangiwa na kwenye amani ya dhamiri nyofu iliyounganika na Mungu wake. Katika upendo tutaona amani itokayo kwa Mungu, tofauti na ile ya nje tu inayopatikana ulimwenguni kwa kukubaliana na maadui wa Mungu na maelekeo yetu mabaya, kwa kutengana na waadilifu na kusambaratika kwa ndani: hiyo ni amani ya mauti inayoendana na uwozo. Kumbe amani aliyotuachia Bwana ni ya dhati na inadai tupambane mfululizo na tabia zetu mbovu, na ulimwengu na shetani: "Sikuja kuleta amani, bali upanga" (Math 10:34). Hakika, hatuwezi kuwa wanyenyekevu na wapole kwa wote tusipotumia nguvu juu yetu. Lakini, hata kama upendo wake una masharti makali, tunang'amua ukweli wa maneno yake: "nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi" (Math 11:30). Uzito wa mzigo huo unapungua kadiri yanavyostawi maadili ambayo ni namna za upendo. "Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari, haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote; hutumaini yote, hustahimili yote" (1Kor 13:4-7). Upole huo wa Kimungu unaandaa kuzama katika sala, ni utangulizi wa heri isiyo na mwisho.

## 3.11. *USAFI WA MOYO, THAMANI NA MATUNDA YAKE*

Tuzingatie sasa adili la kiasi, hasa aina yake muhimu zaidi, yaani usafi wa moyo. Kwanza tutauzingatia kwa jumla, unavyotakiwa katika hali yoyote ya maisha, hata katika ndoa. Halafu tutaona unavyozaa Kiroho, hasa ukitekelezwa kwa namna bora, yaani katika ubikira. Juu yake, Yesu alisema, "Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee" (Math 19:12). Mtaguso wa Trento umetamka rasmi kwamba hali ya useja mtakatifu ni bora kuliko ile ya ndoa, kama Mt. Paulo alivyofundisha wazi (taz. 1Kor 7:25,38,40).

### LENGO LA USAFI WA MOYO

Ingawa haya inastahili sifa, si adili bali elekeo jema la umbile tu. Kumbe usafi wa moyo ni adili linaloingiza mwanga wa akili nyofu na wa neema katika hisi zinazovurugika. Ubikira ni adili kubwa zaidi kwa kuwa unamtolea Mungu utimilifu wa mwili na moyo na kumwekea wakfu maisha yote; ni zawadi azizi ambayo inalitia Kanisa uangavu wa pekee na kulipamba kwa sifa ya utakatifu.

Tunaona thamani ya usafi wa moyo (katika ndoa pia) hasa tukifikiria vurugu ambazo zinatokana na tamaa za mwili, na kusababisha hata talaka, aibu kwa familia nzima, utovu wa raha kwa wanandoa na kwa watoto wao. Ili kutukinga nazo, Bwana alisema, "Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe… Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee, wala mwili wako mzima usitupwe katika Jehanum" (Math 5:29-30). Usafi unapotezwa kwa hisi, kwa mawazo, kwa tamaa. Haukubali aina yoyote ya ashiki iliyokatazwa; kinyume chake unapunguza hata zile halali ambazo hazihitajiki: unatuelekeza kutoambatana nazo. "Kukwepa hasira ni rahisi kuliko kuiratibu; vivyo hivyo kujinyima kabisa ashiki ni rahisi kuliko kuwa na kiasi ndani yake" (Mt. Fransisko wa Sales).

Lengo lake liwe upendo wa Mungu, kwa kuwa usafi wa moyo na wa mwili ni kujinyima mapenzi yoyote haramu kwa ajili yake. Unazuia maisha ya moyo yasiteremke, ili yaweze kuinuka kwa Mungu kama mwali hai na safi wa moto mkali zaidi na zaidi. Usafi wa viungo ni kama ganda la ule wa moyo ambao ndio wa thamani zaidi. Hauwezekani pasipo *aina mbili za ufishaji:* ule *wa mwili na hisi,* hasa mbele ya hatari, na ule *wa moyo,* unaojikatalia mapenzi yoyote yasiyoratibiwa: hayo yana madhara na utelezi kwenye mteremko wa kutisha. Kasi ya kwenda chini inaweza ikaongezeka kuliko tulivyodhani, halafu kupanda juu tena ni kugumu. Mara

nyingi mtu anajitengenezea minyororo ambayo baadaye hana moyo wa kuivunja. Ulimwengu ukisema, “Mapenzi ya kibinadamu yana haki zake”, tujibu, “Hayataweza kamwe kuwa na haki dhidi ya upendo wa Mungu, aliye wema mkuu na asili ya mapenzi yoyote halali”.

*Ili tudumishe adili hilo tunapaswa kuambatana daima na Yesu msulubiwa.* “Mtu anapoanza kutamani kitu pasipo utaratibu, mara anakosa utulivu… Amani halisi ya moyo inapatikana kwa kupinga maono, si kwa kuyafuata. Amani hiyo ni tuzo la mtu mwenye juhudi na maisha ya Kiroho… Anayepotewa na Yesu anapata hasara kubwa kuliko kama angepoteza ulimwengu wote. Anayempata, amevumbua hazina isiyo na mwisho, kuu kuliko mema yote… Pendeni marafiki na maadui ndani mwake na kwa ajili yake, na kumuomba kwa ajili ya wote ili wamjue na kumpenda” (Kumfuasa Yesu Kristo I,6:1-2; II,8:2-4). “Yesu, tumaini la wanaotubu, / jinsi ulivyo mpole kwa waombao! / Jinsi ulivyo mwema kwa wanaokutafuta! / Lakini hasa u nini kwa wanaokupata!” (Utenzi wa Jina Takatifu la Yesu). Ili tuufikie urafiki huo wa ndani na Kristo, ni lazima tutekeleze mfululizo unyenyekevu na usafi wa moyo pasipo kuyataja kamwe au kwa nadra tu.

**ADILI HILO LINAVYOZAA KIROHO**

Usafi kamili unatufanya tuishi mwilini kwa namna ya Kiroho iliyo utangulizi wa uzima wa milele. Kwa namna fulani unatufanya tufanane na malaika na kuwa huru kuhusu vyote vinavyoonekana. Tena unafanya mwili uzidi kufanana na roho, na roho izidi kufanana na Mungu.

*Mwili ukiishi kwa ajili ya roho tu, unaelekea kufanana nayo.* Roho *si ya kimwili,* inaonekana na Mungu na malaika tu; ni *sahili* kwa kuwa haina sehemu; ni *nzuri* kama mawazo na matendo maadilifu*,* hasa ikiwa na nia njema daima; ni *tulivu* maana haipatwi na badiliko lolote la mwili; *haiharibiki* kwa sababu haitegemei mwili unaokufa. Basi, kwa usafi, mwili pia, kwa namna fulani, unakuwa wa Kiroho na kuruhusu roho ionekane kwa njia yake, hasa katika macho: yale ya mtakatifu yanaonyesha nini? Kwa adili hilo mwili unakuwa sahili: mwenendo wa kahaba una fujo, ule wa bikira ni sahili. Kutokana na usafi, mwili unakuwa mzuri, kwa sababu kila kilicho safi ni kizuri, kama anga lisilo na mawingu na kama almasi inayopitisha mwanga. Kwa usafi mwili unakuwa mtulivu: vilema vinauharibu kabla ya wakati, kumbe ubikira unautunza. Miili ya Bwana na ya bikira Maria haikuoza kaburini, na mara kadhaa masalia ya watakatifu hayaozi, hata kwa muda fulani yanaendelea kunukia.

Ikiwa ni kweli kwamba usafi kamili unaufanya mwili ufanane na roho, ni kweli zaidi kwamba *unaifanya roho ifanane na Mungu.* Sifa tatu maalumu za Nafsi za Kimungu ni uweza, hekima na upendo. Basi, kwa usafi kamili *roho inazidi kuwa na nguvu, mwanga na upendo.* Ndipo panapoonekana hasa adili hilo linavyozaa matunda. Usafi kamili unampatia sista *nguvu* na mamlaka hospitalini au magerezani, hata mara nyingi akaheshimiwa na watu wapotovu! Hasa bikira Maria ni tishio la mashetani!

Kwa usafi roho *inaangazwa*: “Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu” (Math 5:8). Kati ya wainjili, tai alikuwa na usafi kamili, na vilevile Mt. Paulo. Mwanateolojia bora, Mt. Thoma wa Akwino, alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita aliondolewa moja kwa moja vishawishi vya uzinifu aweze kuzama katika mafumbo ili awashirikishe wengine. Pengine usafi kamili unawapa watakatifu uwezo upitao maumbile wa kuona kwa namna fulani uzuri wa Mungu na ulinganifu wa sifa zake zinazoonekana kupingana; hata pasipo elimu, wanaandika maneno yasiyosahaulika.

Hatimaye, usafi kamili unaitia roho *upendo* kwa Mungu na kwa jirani ambao ni mara mia kweli na unatuza kwa ziada sadaka zote unazozidai. Katika moyo safi upendo unazidi kuwa mtamu na wa nguvu. Mbali na mabubujiko ya mapenzi ya juujuu, unainuka juu ya hisi na kuwa mwali hai katika utashi. Chini ya Roho Mtakatifu, moyo unaungana na ule wa Mwokozi ili kuchota ndani mwake nguvu kubwa zaidi na zaidi na uhai mpya daima. Upendo huo unaonjesha uzima wa milele.

Roho iliyowekwa wakfu kwa Mungu, ikiwa aminifu moja kwa moja, inastahili kuitwa bibi arusi wa Kristo, kwa kuwa upendo unaishirikisha huzuni na furaha za Yesu, kazi yake kwa ajili ya watu na ushindi wake. Kwenye kilele cha mpando huo kuna arusi ya roho na Mungu wake. Ni muungano usiovunjika unaomgeuza mtu ndani ya Mungu hata anaweza kusema, “Mpendwa wangu ni wangu, na mimi ni wake” (Wim 2:16). Ni uelewano wa ndani unaofikia hatua ya kufunua mawazo ya siri zaidi: bibi arusi wa Kristo anayahisi mambo mengi kabla ya wakati. Ni ushirika kamili wa mawazo, mapenzi, matakwa, sadaka na matendo kwa wokovu wa watu: ushuhuda wake ni komunyo ya kila siku ikizidi kuwa motomoto (upande wa utashi, hata kama si upande wa hisi).

Upendo safi na wa nguvu hivyo ni chanzo cha *ubaba* au *umama wa Kiroho.* Kama vile Yesu alivyowaambia mitume, “Enyi watoto wadogo…” (Yoh 13:33), nao waliwaandikia wanafunzi wao, “Watoto wangu wadogo…” (1Yoh 2:1). “Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu!” (Gal 4:19). “Ni nani aliye dhaifu, nisiwe dhaifu nami? Ni nani aliyekwazwa nami nisichukiwe?” (2Kor 11:29). Ndio ubaba wa Kiroho katika ukarimu, hisani na nguvu zake zote, uliofidia kwa ziada ubaba wa kimaumbile waliojinyima. Badala ya kuanzisha kaya ili kueneza uhai wa kibinadamu, walimzalia Bwana watu ambao waishi milele. Tupendezwe vilevile na umama wa Kiroho wa masista kwa watu wenye shida za kila aina; wataambiwa, “Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi” (Math 25:40). Ndivyo tunavyoona ukuu wa shauri hilo la Kiinjili. Pengine roho ya shauri

hilo iligeuza hata ubaba au umama wa kimaumbile, k.mf. Mt. Monika aliyemzaa upya mwanae Augustino kwa machozi na sala.

Katika hayo yote tunaona jinsi adili la usafi wa moyo, likieleweka na kutekelezwa sawasawa, linavyoandaa kumiminiwa sala ambapo ahadi ya kumuona Mungu inaanza kutimia. Kwa moyo safi tunaanza kumuona kwa namna fulani katika sala, katika ekaristi, katika maongozi ya maisha ambayo "katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema" (Rom 8:28), na hatimaye katika wale wanaotuzunguka, ambao pengine tunakuja kutambua kwamba wanampendeza Bwana kuliko tulivyodhani, ingawa kwa nje hawapendezi. Lakini mwanga huo unapatikana polepole tu kwa kujikana na kumpenda kwa usafi na nguvu kubwa zaidi na zaidi.

## 3.12. *UNYENYEKEVU WA WANAOENDELEA*

Tunapozungumzia maadili ya kiutu yanayohusiana zaidi na maisha ya kuungana na Mungu, tunapaswa kuzingatia unyenyekevu wa wanaoendelea unavyotakiwa kuwa. Tukimfuata Yesu kama kielelezo, umuhimu wa adili hilo na umbile lake vinaonyesha wazi umbali uliopo kati ya maadili yanayofundishwa na wanafalsafa na yale ya Injili.

Katika mapokeo yote ya Kikristo unyenyekevu umetazamwa kuwa *msingi wa maisha ya Kiroho,* ambao unatakiwa kuchimbwa kwa kina kadiri jengo linavyokusudiwa kwenda juu. Unyenyekevu unaangamiza aina zote za kiburi, lakini tendo lake maalumu na kuu si hilo, kwa kuwa Bwana Yesu na bikira Maria hawakupaswa kupinga kiburi ndani mwao, lakini waliutimiza unyenyekevu na bado wanautimiza kwa namna bora. Basi, tendo hilo la kumnyenyekea kwanza Mungu, halafu jirani ni lipi?

### UNYENYEKEVU KWA MUNGU

Tendo maalumu la unyenyekevu ni kuinama, *kujishusha* mbele ya Mungu na mbele ya yale yote yaliyo ya Mungu ndani ya kiumbe chochote. Kumnyenyekea ni kutambua kimatendo, si kinadharia tu, udogo wetu ulio wazi hata mbali na makosa; baada ya dhambi ni kutambua unyonge wetu pia.

Unyenyekevu unaungana na utiifu na ibada, ila unatofautiana navyo. Utiifu unahusu mamlaka ya Mungu na amri zake; ibada inahusu ukuu wake na heshima tunayopaswa kumpatia; kumbe unyenyekevu unakiri udogo na unyonge wetu kwa kutuinamisha ardhini na hivyo kuutukuza ukuu wa Mungu, kama malaika Mikaeli (kwa Kiyahudi, "Nani kama Mungu?"). Anayeishi Kiroho anajisikia furaha takatifu anapojishusha ili kukiri kwa matendo kuwa Mungu peke yake ni mkuu na kuwa ukuu wowote wa kibinadamu ni uongo mtupu ukilinganishwa na wa kwake.

Msingi wa unyenyekevu huo ni ukweli, hasa kwamba umbali kati ya Muumba na kiumbe hauna kiasi. Sisi ni wanyenyekevu kadiri tunavyotambua umbali huo usiopimika hata tukiwa juu namna gani. Kadiri tunavyopanda kwa Mungu, ukweli huo unazidi kuwa wazi kwetu. Hivyo aliyepanda juu zaidi ni mnyenyekevu zaidi kwa sababu ana mwanga mkubwa zaidi: bikira Maria ni mnyenyekevu kuliko watakatifu wote, tena Yesu ni mnyenyekevu kuliko Mama yake.

Tunaona unyenyekevu unavyolingana na maadili ya Kimungu tukizingatia *kweli zake za msingi* ambazo wanafalsafa wa kale hawakuzijua. Kwanza, *uumbaji kutoka utovu wa vyote,* ulio msingi wa unyenyekevu kadiri ya akili nyofu kwa kuwa unaweza kujulikana kwa juhudi za umbile letu. Pili, *fumbo la neema na la haja ya msaada wa Mungu* ili kutenda hata tendo dogo la kuletea wokovu; fumbo hilo linapita uwezo wa maumbile na kujulikana na imani tu.

Yatokanayo ni mambo manne kumhusu Muumba, kuhusu maongozi yake na kuhusu wema wake ambao ni chemchemi ya neema tena unaondolea dhambi.

Kwanza, kumhusu Muumba tunapaswa kukiri si kinadharia tu, bali *kimatendo* kuwa *sisi peke yetu si kitu:* "Maisha yangu ni kama si kitu mbele zako. Kila binadamu, ingawa amesitawi, ni ubatili" (Zab 39:5). "Nawe una nini usichokipokea?" (1Kor 4:7). Tumeumbwa kutoka utovu wa vyote kwa hiari ya Mungu, ambaye asingetudumisha tungetoweka mara. Tena, baada ya kuumbwa, ingawa tuko wengi zaidi, hakuna ongezeko lolote la ukweli, la ukamilifu, la hekima na la upendo, kwa kuwa tangu milele sifa hizo za Mungu ni kamili pasipo mipaka. Basi, tukijilinganisha na Mungu, sisi hatuko. Tungetoa yaliyo ya Mungu katika matendo yetu bora kisingebaki chochote, kwa sababu si kwamba sehemu yake moja inatoka kwetu na sehemu nyingine kwa Mungu, bali *tendo lote* ni la Mungu kama asili ya kwanza, halafu lote ni la kwetu kama asili ya pili.

Vilevile pasipo Mungu *mratibu mkuu,* pasipo maongozi yake *yanayoendesha* vyote, maisha yetu hayana dira. Tunapaswa kupokea toka kwake maongozi ya jumla ya amri zake ili kufikia uzima wa milele, na maongozi maalumu ambayo amemchagulia kila mmojawetu tangu milele na ambayo tunaonyeshwa na wakubwa wetu wanaomwakilisha, na mashauri tunayopaswa kuomba, na matukio na uvuvio wa Roho Mtakatifu. Tunapaswa kukubali nafasi aliyotupangia, hata ikiwa duni. Unyenyekevu huo una faida kwetu na kwa wengine pia. Mwokozi alikubali kwa unyenyekevu usio na kifani kushika nafasi ya mwisho, hata wakamuona Baraba kuwa bora kuliko yeye, akapokea aibu ya msalaba. Kwa hiyo katika jengo la Mungu amekuwa jiwe kuu la msingi. Ndio unyenyekevu halisi ambao unazaa ajabu na kutangaza utukufu wa Mungu hata palipofichika. Basi, tupokee maongozi maalumu anayotuelekeza, hata yakidai tujitoe sadaka ya

kuteketezwa: “Bwana huua, naye hufanya kuwa hai; hushusha hata kuzimu, tena huleta juu. Bwana hufukarisha mtu, naye hutajirisha; hushusha chini, tena huinua juu” (1Sam 2:6-7).

Halafu katika maongozi hayo hatuwezi kupiga hatua hata ndogo wala kutenda lolote la kuletea wokovu tusipopewa *neema za msaada.* Tukiri kwa furaha, “Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu watoka kwa Mungu” (2Kor 3:5). “Hawezi mtu kusema, ‘Yesu ni Bwana’, isipokuwa katika Roho Mtakatifu” (1Kor 12:3). Hasa tunahitaji neema ili kudumu waaminifu mpaka mwisho; tunapaswa kujiombea neema hiyo kwa unyenyekevu.

Unyenyekevu huo, unaotakiwa kuwemo ndani ya waadilifu wote, ulikuwa sifa ya watu wa kwanza katika utakatifu wa asili. Lakini *baada ya dhambi* tunapaswa kukiri kimatendo unyonge wetu pia: umimi, moyo finyu, ugeugeu, hasira, ndoto za mchana, usahaulifu wa mambo muhimu, kiburi, tamaa, hata kutojali utukufu wa Mungu na wokovu wa watu. Unyonge huo ni mbaya kuliko utovu wa vyote, kwa kuwa unafuja roho zetu na kuzifanya zichukize. “Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu… Nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya maovu mbele za macho yako” (Zab 51:2-4). “Ni nani awezaye kuyatambua makosa yake? Unitakase na mambo ya siri” (Zab 19:12).

Unyenyekevu haupingani na moyo mkuu, bali unaunganika nao na kukua pamoja nao kama vidole vya mkono mmoja: hatuwezi kuwa na unyenyekevu wa dhati pasipo moyo mkuu. Mkristo anatakiwa kulenga makuu yanayostahili heshima kubwa, ingawa anaona heshima si kitu; ayalenge kwa unyenyekevu na, ikiwa lazima, kwa kudhalilishwa. Azoee kukariri, “Ee Bwana, kutukuza usitutukuze sisi, bali ulitukuze jina lako” (Zab 115:1). Asiye na moyo anakataa kufanya yale ambayo anaweza na kupaswa kuyafanya, na asipotimiza wajibu mkubwa anatenda dhambi ya mauti. Kinyume chake unyenyekevu unamuinamisha mtu mbele ya Aliye Juu, ashike nafasi yake halisi ili Mungu atende ndani yake pasipo kizuio. Mnyenyekevu anajitia mikononi mwa Mungu na, ikiwa Bwana anatenda makuu kwa njia yake, hajitukuzi kuliko shoka likitumiwa na mtemakuni, wala kinubi kikichezwa na mwanamuziki bora.

**UNYENYEKEVU KWA JIRANI**

“Kila mmoja anapaswa kutambua kwamba katika yale yaliyo ya kwake tu, yeye ni duni kuliko yeyote katika yale aliyojaliwa na Mungu” (Mt. Thoma wa Akwino). Kwa kuwa kila mtu peke yake si kitu, aliyonayo ya kwake tu ni *unyonge wa makosa yake;* basi akiri kimatendo kuwa hayo ni duni kuliko yale yote ambayo mwingine yeyote amejaliwa na Mungu upande wa umbile na upande wa Kiroho.

“Mtu mnyenyekevu kweli anajiona duni kuliko wengine, si kwa matendo ya nje, bali kwa kuwa anaogopa kutenda kwa kiburi kilichofichika hata mema anayoyatenda” (Mt. Thoma wa Akwino). “Mfikirie kwamba wapo watu ambao pasipo kuonekana ni bora kuliko nyinyi, hata mkionekana waadilifu kuliko wao” (Mt. Augustino). Tukariri, ‘Hakuna dhambi iliyotendwa na mwingine nisiyoweza kuitenda mimi pia kwa udhaifu wangu: kama sijaitenda ni kwa sababu Mungu kwa huruma yake hajaacha itokee’. Tumtukuze na kumuomba, “Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu” (Zab 51:10); “Ee Bwana, utugeuze kwako, nasi tutageuka” (Mao 5:21).

Kwa kuwa upendo wake ndio asili ya mema yote, watakatifu wanajiambia, “Mtu huyu angejaliwa neema nilizozipata mimi, labda angekuwa mwaminifu kuliko mimi; na kama Mungu angeacha nitende makosa aliyoacha ayatende huyu, sasa ningekuwa mahali pake”. Ndio msingi wa unyenyekevu ambao kiburi chochote kivunjike juu yake. Unyenyekevu wa watakatifu unazidi kuwa wa dhati kadiri wanavyozidi kujua udhaifu wao mbele ya ukuu na wema wa Mungu. Tuulenge mfululizo unyenyekevu wao, lakini tusitumie maneno yao kabla hatujaamini ukweli wake; ungekuwa unyenyekevu wa bandia tu unaofanana na ule halisi kama kipande cha kioo na almasi.

Unyenyekevu kwa jirani si kuogopa watu wala kukosa moyo. Kuogopa watu ni kuogopa hukumu na hasira za waovu: hofu hiyo inasogeza mbali na Mungu. Utovu wa moyo unakwepa kazi ya lazima, na kuelekea mambo ya chini badala ya makuu yanayotupasa. Kumbe, unyenyekevu unatuinamisha mbele ya Mungu na mbele ya yaliyo yake katika jirani. Mnyenyekevu hauinamii kamwe uwezo wa waovu, tofauti na mwenye uchu wa madaraka, anayejishusha kupita kiasi ili afikie matamanio yake.

Unyenyekevu haukwepi makuu; kinyume chake unaimarisha moyo mkuu uyalenge hata kwa njia duni. Bwana ametuonyesha vizuri ajabu maadili hayo mawili yanavyotegemezana akisema (Math 20:28), “… kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumikia” (ndio unyenyekevu) “na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi” (ndiyo ari ya moyo mkuu). Mwokozi asingeweza kulenga mambo makuu zaidi wala kuyalenga kwa unyenyekevu mkubwa zaidi: alipania kutupatia uzima wa milele, lakini kupitia aibu na mateso ya msalaba. Maadili hayo yanayoonekana kupingana, yanaunganika ndani ya watakatifu pia ambao, kadiri walivyo wanyenyekevu, wana nguvu, wasijali binadamu hata wakitishwa namna gani.

Kiutekelezaji, ili tuufikie unyenyekevu kamili (ambao, tusipokuwa nao, hatuwezi kuwa na upendo kamili) tunapaswa kusimama vema kuhusu sifa na lawama. Kwanza, kuhusu sifa, *tusijisifu kamwe,* la sivyo tutajichafua tu; wanajisifu wale wanaodhani hawasifiwi vya kutosha na wengine. Halafu *tusijitafutie sifa,* la sivyo tutakuwa kiroja na kupoteza stahili za matendo mema. Hatimaye *tusifurahie sifa* tukizipata, la sivyo tutapoteza walau ua la stahili hizo.

Lakini ni lazima tupande juu zaidi kwa kusimama vema kuhusu lawama. *Tunapaswa kupokea kwa subira lawama tunazostahili,* hasa zikitoka kwa wakubwa wenye haki na wajibu wa kuzitoa: tukikunja uso tutapoteza faida ya maonyo hayo. *Pengine tunapaswa kupokea kwa subira hata lawama ambazo hatustahili au kidogo tu.* Hatimaye, kwa mfano wa watakatifu, inafaa tujiombee *upendo kwa dharau*.

Mt. Anselmi aliorodhesha vizuri vidato vya unyenyekevu: 1) kujua kwamba tunastahili dharau katika mengi; 2) kufurahia kuwa hivyo; 3) kukiri kuwa hivyo; 4) kutaka jirani asadiki hivyo; 5) kupokea kwa subira kusemwa hivyo; 6) kukubali kutendwa kama mtu anayestahili dharau; 7) kupenda kutendwa hivyo. Vidato vya mwisho vinadai kwanza sala ya kumiminiwa kuhusu unyenyekevu wa Bwana, aliyesulubiwa kwa ajili yetu, na hamu kubwa ya kufanana naye. Ni vema tulenge ukamilifu huo, lakini si wengi wanaoufikia; kabla ya hapo tuna nafasi nyingi za kukumbuka maneno ambayo Yesu ametuhimiza tumuige iwezekanavyo, "Mtu yeyote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu, na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu, na awe mtumwa wenu…" (Math 20:26-27).

## 3.13. *UNYENYEKEVU WA NENO ALIYEFANYIKA MWILI NA ULE WA KWETU UNAVYOTAKIWA KUWA*

Ni muhimu tuzingatie Bwana mwenyewe alivyotekeleza unyenyekevu ili tufuate nyayo zake, na tuone jinsi kujishusha kwake kulivyoendana na maadili ya hali ya juu.

### UNYENYEKEVU NA UKUU WA MOYO WA YESU

Mt. Paulo akitaka kuhimiza unyenyekevu aliandika juu ya ukuu usio na mipaka wa Mwokozi ili tuelewe zaidi alivyojishusha: ni jambo la ajabu jinsi alivyyounganisha hayo mawili, lakini kwa namna fulani muungano huo unatakiwa kupatikana katika ukamilifu wa Kikristo. "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu, ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba" (Fil 2:5-8).

Mwana pekee *"hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho".* Ibilisi, ambaye ni kiumbe tu, alitaka kulingana na Mungu, akakataa kimatendo utawala wake: "nitafanana na yeye Aliye juu" (Isa 14:14). Hata alipotushawishi alisema, "Mtakuwa kama Mungu" (Mwa 3:5). Lakini Yesu, aliye Mungu kweli, alijishusha kabisa: "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu… Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu" (Yoh 1:1,14). *"Alijifanya kuwa hana utukufu".* Hakupoteza umungu wake, ila alitwaa umbile letu akaanza kuishi duniani katika hali duni. Umungu ndio ukamilifu usio na mipaka wa sifa zote, kumbe ubinadamu uko chini kuliko umbile la malaika yeyote, kwa kuwa hata yule wa mwisho ni roho tu. *"Akatwaa namna ya mtumwa",* kwa kuwa binadamu, kiumbe cha Mungu, ni mtumishi wa Aliye Juu. Basi Mwana pekee wa Baba alitwaa umbile hilo ili katika Nafsi moja awe Mwana wa Mungu na Mwana wa Adamu, awe Mwana pekee aliyezaliwa tangu milele yote na mtoto mchanga pangoni, halafu mtu wa mateso aliyesulubiwa. *"Akawa ana mfano wa wanadamu… akaonekana ana umbo kama mwanadamu".* Aliamua kufanana na wadogo wake katika yote, isipokuwa dhambi; tena aliamua kuzaliwa fukara, kuteswa na njaa, kuchoka na kuishiwa nguvu, sawa nasi na zaidi tena. *"Alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba".* Mungu-Mtu alijishusha ilivyoandikwa, "Kadiri ulivyo mkuu uzidi kujinyenyekeza, nawe utapata kibali machoni pa Bwana; kwa maana rehema zake Bwana zi kuu, na siri yake ni kwa wanyenyekevu" (YbS 3:18-20). Kitambulisho cha unyenyekevu ndicho utiifu unaopinga kiburi kinachotuelekeza kutimiza matakwa yetu, kutaka kujitokeza, kuongoza wengine bila ya kuongozwa na yeyote. Basi, ili atuponye kiburi chetu, Mwana pekee wa Mungu alijifanya mtiifu hata mauti ya msalaba.

Utiifu unafanya matendo yastahili, hivi kwamba mateso yenyewe, ingawa yanaonekana kuwa ya bure, yanaweza kuzaa tele. Hilo ni mojawapo kati ya maajabu ya Mwokozi: kutukuza uchungu kwa njia ya utiifu na upendo. Utiifu usipokataa kifo wala aibu ni wa kishujaa. Basi, kifo cha Neno aliyefanyika mwili kilikuwa cha aibu kuliko vyote, ilivyotabiriwa, *"Tumhukumu auawe mauti ya aibu"* (Hek 2:20). Msalaba ulitazamwa na Warumi na Wayahudi kama adhabu ya aibu na ya kutisha waliyowekewa watumwa n.k. "Aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu" (Kumb 21:23). "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa: Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti" (Gal 3:13). Ndiyo sababu msalaba "kwa Wayahudi ni kikwazo" (1Kor 1:23): ni lazima wasadiki kuwa mti wa laana umekuwa chombo cha wokovu; na kuwa aliyepigiliwa misumari juu yake, hakulaaniwa na Mungu, bali alikusudiwa awe chemchemi ya neema zote, apendwe na kuabudiwa. *"Kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri…* Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu… Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake" (Eb 11:26; 12:2; 13:13).

Hayo yote yalifumbika tayari katika Bwana kuzaliwa "kwa ajili yetu sisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu" (Kanuni ya Imani ya Nisea-Kostantinopoli): "Ajapo ulimwenguni, asema, Dhabihu na toleo hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari… Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja - katika gombo la chuo nimeandikiwa -

niyafanye mapenzi yako, Mungu” (Eb 10:5,7). Liturujia ya Noeli inatukumbusha mfululizo mfano huo, ikikaza unyenyekevu wa kuzaliwa kwake unavyopingana na ukuu wa Mwokozi. Maria alimzaa “mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng’ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni” (Lk 2:7). Neno aliyefanyika mwili hakupata nafasi: tusilisahau hilo hasa tunapoikosa sisi pia.

## MUUNGANO WA UNYENYEKEVU NA UKUU WA KIKRISTO

Tumuige vipi Bwana wetu? Upande mmoja anatuambia tujishushe tusiweze kamwe kujinyenyekeza mno; upande mwingine anatuambia, “Ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu” (Math 5:48). Kuna watu wanaodhani kukosa unyenyekevu wakitamani muungano na Mungu ambao wanajisikia hawaustahili. Shida ipo hasa tunapopaswa kuchambua ndani mwetu unyenyekevu halisi na ule wa bandia, k.mf. tukitakiwa kushika msimamo dhidi ya wengine; pengine mwanzoni mwa mabishano tunasema kwa kutetea ukweli tu, lakini baadaye tunakuja kujibu kwa kiburi na utovu wa subira kutokana na umimi wetu kuchukizwa. Watu wanyofu wanatatua tatizo hilo kwa kutekeleza Maandiko kuhusu muungano wa hayo mawili yanayoonekana kupingana: “Yeyote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni” (Math 18:4). “Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake” (1Pet 5:6). “Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza” (Yak 4:10).

Muungano huo wa unyenyekevu wa dhati na wa ukuu upitao maumbile unajitokeza hasa kwa watakatifu. Tumsikie Mt. Paulo, “Mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake. Maana mimi ni mdogo katika mitume, nisiyestahili kuitwa mtume, kwa sababu naliliudhi Kanisa la Mungu” (1Kor 15:8-9). “Wao ni wahudumu wa Kristo? Nanena kiwazimu, mimi ni zaidi: katika tabu kuzidi sana; katika vifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi” (2Kor 11:23). Alitaja hata “maono na mafunuo ya Bwana” (2Kor 12:1) aliyojaliwa, lakini mwishoni akasema, “Makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, *Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu.* Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu” (2Kor 12:7-10).

Mt. Thoma wa Akwino alifafanua hivi, “Kama vile upendo ulivyo mzizi wa uadilifu, kiburi ndiyo asili ya kila dhambi. Ni hamu isiyoratibiwa ya ukuu unaolengwa pasipo kufanywa njia ya kumtukuza Mungu. Ndivyo tunavyosogea mbali naye: ndiyo asili ya kosa lolote, na ndiyo sababu Mungu anawapinga wenye kiburi. Basi, kwa kuwa ndani ya waadilifu umo wema unaoweza ukawafanya wapatwe na kiburi, pengine Mungu anaacha wateule wake wapatwe na ugonjwa fulani, kasoro fulani, hata dhambi ya mauti ambayo iwazuie wasitakabari, iwaaibishe kweli na kuwafanya watambue kuwa kwa nguvu zao hawawezi kusimama wala kudumu hasa. Kwa namna ya pekee mtakatifu Paulo mtume angeweza kupatwa na kiburi kwa mambo mengi: alikuwa ‘ni chombo kiteule’ cha kuenezea imani kwa mataifa (Mdo 9:15); ‘alinyakuliwa juu mpaka mbingu ya tatu… akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene’ (2Kor 12:2,4); aliteseka sana kwa ajili ya Kristo, mara nyingi alitupwa gerezani akapigwa mijeledi; alikuwa na moyo safi kwa kujaliwa ‘kwa rehema za Bwana kuwa mwaminifu’ (1Kor 7:25); alifanya ‘kazi kupita wao wote’ (1Kor 15:10), alivyosema mwenyewe; na kwa namna ya pekee alikuwa na ujuzi wa mambo ya Mungu mkubwa hivi hata uweze kumtia kiburi. Ndiyo sababu Bwana alimpa dawa ya kiburi. Ili ukuu wa maono aliyojaliwa usimfanye apatwe na kiburi, alitiwa mwiba mwilini, ugonjwa uletao aibu na kusulubu mwili ili kuponya roho… Jinsi mkosefu anavyopaswa kutetemeka, mtume mkubwa kama huyo, chombo kiteule, asipojiamini! Mara tatu alimsihi kwa nguvu Bwana amuondolee mwiba huo; mara tatu, yaani mara nyingi na kwa udumifu. Hapo akasikia maneno yafuatayo: *‘Neema yangu yakutosha’*, yenyewe itakukinga na dhambi. Uweza wa Mungu unaoonekana wazi katika udhaifu, ambao ni nafasi ya kutekeleza maadili ya unyenyekevu, subira na kujikana. Mtu akifahamu udhaifu wake anakuwa macho zaidi katika mashindano, na kwa hayo anaimarika. Basi, alisema mtakatifu Paulo, ‘nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi’, kwa sababu hivyo ninakuwa mnyenyekevu zaidi, na kupaswa kushindana ‘ili uweza wa Kristo ukae juu yangu’ na kuzaa matunda yake”.

Kinachowezesha kuoanisha unyenyekevu na moyo mkuu ni kwamba, “Tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu” (2Kor 4:7). “Kuhusu kujitathmini, daima mtu anatakiwa kuwa kama aliyefunga safari na kulenga makubwa zaidi, ‘Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la!’ (Fil 3:12)… Na daima mtu anatakiwa kujitahidi kufikia ukamilifu, ‘Nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele’ (Fil 3:13)” (Mt. Thoma wa Akwino).

Basi, kwa watakatifu unyenyekevu na moyo mkuu vinapatana: wanalenga makuu kupitia majaribu na aibu. Hata hivyo inabaki tofauti isiyopimika kati yao na Mwokozi ambaye hawezi kutenda dhambi bali ana ukuu wa kifalme. Kwa kiasi chake, ndivyo ilivyo kwa bikira Maria aliyekingiwa dhambi yoyote. Katika wimbo wake anajitokeza kwa pamoja mnyenyekevu na mkuu ajabu: “Ameutazama unyonge wa mjakazi wake. Kwa maana, tazama, tokea sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa; kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea

makuu… amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi; na wanyonge amewakweza" (Lk 1:48-49,52). Kitu hicho kinatokea tena katika maisha ya Kanisa ambapo yanatimia daima maneno yafuatayo: "Kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa" (Lk 14:11; 18:14). Katika dhuluma, Kanisa linaonekana kushindwa, kumbe linashinda; kwa unyenyekevu linalenga daima makuu mawili: utukufu wa Mungu na wokovu wa watu. Kitu cha namna hiyo kinatakiwa kumtokea kila Mkristo, hasa mtawa. Anapaswa kuwa mnyenyekevu kama mzizi uliofichika ardhini, na kulenga daima makuu, yaani imani hai zaidi, tumaini imara zaidi, upendo motomoto zaidi, muungano na Mungu ulio wa dhati na safi zaidi kila siku. Hivyo yanakuja kuoana yale yanayoonekana kupingana, kama mzizi mrefu wa mti (unaomaanisha unyenyekevu) unavyopenya zaidi na zaidi ardhini, maadamu tawi la juu (linalomaanisha upendo) linazidi kuelekea mbinguni. Polepole uzima wa Yesu unadhihirika "katika miili yetu ipatikanayo na mauti" (2Kor 4:11). Hakuna unyenyekevu halisi mbali na ule anaotujalia tukimuomba kwa moyo tufanane naye na tukikubali kufuata njia inayotufikisha huko.

## 3.14. *ROHO YA UFUKARA*

Tulivyoona, ukamilifu wa Kikristo unategemea hasa upendo, lakini tukitaka kuufikia ni lazima walau tuwe na *roho ya mashauri ya Kiinjili,* yaani tusiambatane na malimwengu. *"Muda ubakio si mwingi; basi tokea sasa wale walio na wake na wawe kama hawana; na wale waliao kama hawalii; na wale wafurahio kama hawafurahi; na wale wanunuao, kama hawana kitu. Na wale wautumiao ulimwengu huu, kama hawautumii sana; kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita"* (1Kor 7:29-31). Basi, tuongelee roho ya ufukara ambayo Bwana ametuhimiza wote tuwe nayo aliposema, "Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Math 5:3): kwa namna fulani ni wao tangu sasa, si baadaye tu.

### THAMANI YA UFUKARA WA HIARI

Thamani hiyo inawaelea hata wasio na imani wakizingatia fujo zinazotokana na tamaa ya macho, uchu wa mali, uchoyo, ubepari na usahaulifu wa njaa inayoua mafukara. "Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha" (1Tim 6:10). Ni lazima tuanze kuachana na malimwengu ili tuelewe kwamba *"kinyume cha mema ya Kiroho, malimwengu yanatenganisha watu, kwa kuwa hayawezi kuwa ya wengi kwa mkupuo moja na kikamilifu"* (Mt. Augustino). Hivyo utafutaji wake usiporatibiwa unatenganisha, wakati utafutaji wa mema ya Kiroho unaunganisha watu. Mungu tunaye kadiri tunavyomshirikisha kwa wenzetu, kumbe tukiwanyima tunakuja kumkosa.

Roho ya kutoambatana na malimwengu inahitajika pia ili tuelewe maana halisi ya haki ya kumiliki ambayo ni *haki ya kujipatia na kusimamia* vitu, ila "kuhusu kuvitumia mtu hatakiwi kuviona kama ni vyake, bali vya pamoja, awashirikishe wengine kwa urahisi katika shida zao" (Mt. Thoma wa Akwino). "Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. *Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao,* washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli" (1Tim 6:17-19).

Roho hiyo inatukumbusha kwamba katika shida kubwa fukara akiomba chakula na kukataliwa anaweza kujichukulia bila ya kutenda dhambi ya wizi. Hiyo ni kweli vilevile kuhusu nyumba na nguo za lazima. Ni amri tutoe ziada yetu ili kumsaidia mwenye shida kubwa. Turudie ufukara wa Kiinjili ili kupinga maonevu ya ubepari yanayomkatisha tamaa asiye na kazi, anayeshindwa kulisha watoto wake. "Kwa kiburi chake asiye haki mnyonge anafuatiwa kwa ukali" (Zab 10:2). Tajiri, badala ya kuwa mlimbikizaji, anapaswa kuwa *msimamizi wa riziki za Mungu* kusudi mafukara wapate mahitaji yao. Hapo haishi tena chini ya utawala wa uroho na kijicho, bali katika utawala wa Mungu. Vurugu na hatari kubwa za jamii ya leo zinatulazimisha tuzingatie na kutekeleza kweli hizo tusishikamane na vitu.

Thamani ya roho hiyo inatuelea zaidi tukikumbuka mema halisi tunayopaswa kuyatamani: "Msisumbukie maisha yenu, mle nini na mnywe nini, wala miili yenu, mvae nini. Maisha je, si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je, si bora kupita hao?… Bali *utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa.* Basi msisumbukie ya kesho, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe" (Math 6:25-26,33-34). Roho hiyo inatuelekeza tutamani zaidi mema ya milele na kutegemea *misaada ya Mungu* ili kuyafikia. Ufukara wa hiari na tumaini kwa Mungu vinaongozana: kadiri tunavyoacha kuambatana na dunia tunatamani mema ya mbinguni, na kadiri tusivyotegemea misaada ya kibinadamu tunategemea ile ya Mungu. Kwa hiyo tumaini ndiyo roho ya ufukara ambayo kila Mkristo anapaswa kuwa nayo.

"Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate" (Mk 10:21). Utekelezaji wa vitendo wa ufukara huo ni shauri, si amri; lakini kila mtu awe walau na roho ya shauri hilo: "Ukiwapenda mafukara, uende mara nyingi kati yao; ufurahi kuwaona nyumbani pako na kuwatembelea; uongee nao kwa radhi na kufurahi kuona wakikukaribia… Ukitaka kufanya zaidi, ujifanye mtumishi wa mafukara, ukienda kuwauguza wakiwa wagonjwa… ukiwahudumia kwa gharama yako… Mtakatifu Ludoviko IX mara nyingi aliwahudumia mezani mafukara

aliowategemeza, na karibu kila siku aliwakaribisha watatu mezani pake; mara nyingi alikula mabaki ya supu yao kwa upendo usio na kifani… Yatakapokupata majanga yatakayokufanya uwe fukara… moto, mafuriko, kesi… ndio wakati hasa wa kutekeleza ufukara… kwa upole na uvumilivu" (Mt. Fransisko wa Sales). Ufukara wa Kikristo unatakiwa kuwa mfurahivu, na aliyeuchagua anapaswa kuvumilia walau tabu fulani kwa upendo wa Mungu, la sivyo utawezaje kumuunganisha naye? Mt. Fransisko wa Asizi na wengineo wametuonyesha linavyoweza kutufikisha kwenye muungano wa dhati na Mungu.

**MATUNDA YA UFUKARA WA HIARI**

Yesu alichagua ufukara kwa sababu nne zinazofanya ulete mara mia zaidi kadiri ya ahadi yake: 1) asisumbukie malimwengu; 2) aonyeshe kuwa anatafuta wokovu wa watu tu; 3) ahimize kutamani mema ya milele; 4) uwezo wa Mungu wa kuokoa uonekane wazi katika utovu wa misaada ya kibinadamu.

Kwanza, *roho ya ufukara inatukomboa tusihangaikie vitu,* ambavyo hapo si tena vizuio katika kumuendea Mungu, bali vyombo vya kutendea mema. Hapo tunaweza kupiga mbio kwenye njia ya ukamilifu kwa kuwa hatulemewi na mizigo isiyo ya lazima: hatufikirii tena kukaa duniani kana kwamba ni makao ya milele, bali tunajielewa kuwa *wapitanjia* tu na tunatamani kufikia lengo kuu pasipo kuchelewa.

Pili, *ufukara wa hiari ni ishara ya kutojitafutia faida;* ishara hiyo inahitajiwa na mtume ili kila mtu amuone nia yake pekee ni kumpatia Bwana watu.

Tatu, *ufukara wa hiari unazaa katika jamii kwa namna ya ajabu:* ili tujihakikishie inatosha kutembelea nyumba za kuwahudumia maskini zinazotegemea tu misaada inayopatikana siku kwa siku; ni kama muujiza wa kudumu unaofanywa na Mungu kwa kuitikia imani ya mwanzilishi na ya wanae.

Nne, *roho ya ufukara inazaa matunda ya Kiroho ya ajabu zaidi tena:* inatufundisha subira, unyenyekevu, kutoambatana na yale yote ambayo si Mungu wala upendo wake, yaani kutoambatana na mema ya akili, mema ya moyo na mema kadhaa ya roho. *Mema ya akili* ndiyo ujuzi wetu: tunaposoma tunapaswa kukwepa udadisi, majivuno na juhudi za kibinadamu tu, ili tusome kwa kumtumikia Mungu, tukijibandua na mitazamo yetu. Hapo Bwana atatujalia mara mia hata katika hayo: yaani atatujalia ule unyofu wa hali ya juu unaohitajika kwa sala ya kumiminiwa kwa kuwa unajisahau ili kuzama katika kuzingatia ukweli. *Mema ya moyo* ndiyo mapendo yetu na yale wanayotupatia wengine huku yamejaa heshima na imani kwetu. Ili tusitumbukie maisha ya miguso tu, inatubidi tusitamani kupendwa na kuheshimiwa, bali tumtolee Mungu hata mapendo halali yawe chini ya upendo halisi, ambao utatuonyesha thamani ya urafiki mkarimu usio wa kibinadamu tu. Huo ni zawadi kubwa ambayo pengine Mungu anawajalia walioachana na yote. Hatimaye kuna *mema kadhaa ya roho* ambayo ufukara unatufundisha kutoambatana nayo, yaani faraja za kihisi. Hatutakiwi kuzitafuta zisije zikawa kizuio badala ya msaada kwa kumuendea Mungu. Wengine wanajinyima pia mema yote yanayoweza kushirikishwa kutokana na sala na stahili zao, wakimuachia bikira Maria ayatumie kwa faida ya wenye shida kubwa zaidi duniani au toharani. Kwa kufanya hivyo wanajiandaa kupokea neema kubwa ya ufukara wa Kiroho wa juu zaidi unaopatikana katika utakaso wa mwisho, ule wa usiku wa roho unaokumbusha hali ya Yesu msalabani, alipojisikia mkiwa kupita kiasi.

## 3.15. *UKUU WA UTIIFU*

Lililo kuu kati ya mashauri ya Kiinjili ni utiifu, kama vile kiburi cha maisha kilivyo vurugu kubwa kuliko tamaa za mwili na macho. Ndiyo sababu Yesu aliwaambia wenye kiburi, "Amin, nawaambia, watoza ushuru na makahaba watatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu. Kwa sababu Yohane alikuja kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini, lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini. Nanyi hata mlipoona, hamkutubu baadaye, ili kumwamini" (Math 21:31-32). Hayo tunayajua kinadharia, lakini tunayasahau kwa urahisi katika utekelezaji. Tunazingatia vurugu za wazi zinazotokana na tamaa za mwili na macho, tusitambue kuwa kosa kuu ni lile la kusema, *"Sitatumikia".* Ndilo dhambi hasa la ulimwengu "wa kisasa" unapodai kujitenga na Kanisa ili ufuate tu akili na utashi wake wenyewe: matokeo yake, unakwenda kinyume cha akili mradi usimtii Mungu. Hatimaye, kama mwana mpotevu, unajikuta katika utumishi wa kuudhalilisha ambao unasambaratisha na kuangamiza jamii.

Ugonjwa wa namna hiyo unaponyeka tu kwa kushika utiifu mnyenyekevu na wa dhati; lakini mara nyingi ukuu wa utiifu haujulikani hata katika mazingira mema. Inasahaulika kuwa nadhiri za kitawa zinainua kwa ndani maisha yote yaliyowekwa wakfu. Katika vitabu vingi nadhiri za ufukara na useja zinashika nafasi kubwa, kwa sababu kuzivunja kunatokea mara nyingi na kuzidisha dhambi hata za mauti. Kumbe utiifu unawekwa pembeni kwa sababu kwa nadra tu kuuvunja ni dhambi ya mauti. Inasahaulika thamani ya kujitoa mhanga kwa nadhiri; unasahaulika pia mpango mzima wa maisha ya kitawa kuwekwa wakfu kwa njia ya maadili ya ibada na utiifu. Hivyo kwa wengi utiifu ni nidhamu tu, utekelezaji wa nje unaodaiwa na kazi na ambao sanasana unaweza kuinuliwa kama vitendo vingine vyovyote. Ili *tuthamini kwa dhati* adili hilo, tutazingatia linatukomboa kutoka utumwa upi na linazaa matunda yapi.

**UTUMWA AMBAO UTIIFU UNATUKOMBOA NAO**

Utiifu unatukomboa kutoka utumwa wa matakwa yetu na wa maoni yetu.

Utiifu kwa Mungu na kwa wawakilishi wake (wa Kiroho na wa kidunia) unatuhakikishia ulinganifu wa matakwa yetu na yale ya Mungu. Sababu hasa ya kutii si kwamba agizo *linaonekana la kufaa*, bali kwamba limetolewa na kiongozi halali anayemwakilisha Mungu, asili ya mamlaka yote. Tukitii kwa sababu ya *kuridhika tu* na agizo, tunakosa stahili maalumu za utiifu (kama tunavyokosa zile za imani tukikubali kweli zile tu zilizo wazi, wakati sababu halisi ya kusadiki ni mamlaka ya Mungu anayetufunulia mafumbo). "Tunalotakiwa kutii ni agizo linaloonyesha matakwa ya kiongozi, liwe limetolewa wazi au la" (Mt. Thoma wa Akwino). *Hivyo utiifu unatukomboa kutoka matakwa yetu,* yaani matakwa ambayo hayalingani na yale ya Mungu, bali kwa kiburi yamepotea yakikataa kutenda inavyotakiwa.

Kwa maana hiyo matakwa yetu ndiyo sababu ya dhambi yoyote: "mkiondoa matakwa yetu hautakuwepo tena moto wa milele" (Mt. Bernardo). Ni ya hatari hasa kwa kuwa yanaweza kuharibu kila kitu. Hata matendo bora yanakuwa maovu yakifuata matakwa yetu badala ya kumtii Mungu. Bwana akiona matakwa yetu yanasababisha tendo la toba au la ibada analikataa kama yale ya Mafarisayo. Hata tusipofikia hapo, huwa tunashikilia matakwa yetu, tukijali pengine namna yetu ya kutenda jema kuliko jema lenyewe: tunataka kulitenda sisi, la sivyo tunazuia lisitendwe.

Utiifu unatakiwa kutekelezwa kwa imani, kwa kuona agizo la viongozi kuwa ni agizo la Mungu. Unapaswa kuwa wa mara moja, kuhusu jambo lolote (dogo au kubwa) na kwa viongozi halali wote (wawe wapendevu au la, wenye busara au la, watakatifu au la) mradi agizo lao halipingani na sheria ya juu. Utiifu huo unakomboa kwa sababu siku kwa siku unalinganisha matakwa yetu na yale ya Mungu na hivyo unanyosha na kuimarisha utashi wetu.

Utiifu unatukomboa pia kutoka utumwa wa *maoni yetu* yasiyo na msingi katika ukweli, yaani katika mtazamo wa Mungu. Maoni hayo yanasababisha mienendo ya pekee na ugumu wa vichwa katika utendaji. Ni maoni ya harakaharaka yatokanayo na maelekeo mabaya, umimi na kiburi. Pengine yananong'onezwa au kuthibitishwa na adui wa roho yetu. *"Kadiri mtu alivyo anaona lengo fulani kuwa linamfaa"* (Aristotle), yaani tunaona jambo kuwa jema au baya kadiri ya maelekeo ya matakwa na ya hisi zetu. Mwenye kiburi anayaona bora yale yanayomkuza, kumbe mnyenyekevu anaona kudhalilishwa kunamfaa zaidi. Mara nyingi maoni yetu yanatufikisha hata kuhukumu kinyume cha haki na upendo.

Huo ni utumwa halisi: utiifu unatukomboa ukihakikisha kwamba katika utendaji tunakubali maoni ya wakili wa Mungu aliye na haki ya kutuagiza kwa niaba yake. Agizo lenyewe linaweza likakosa busara: hapo hatudaiwi kulikubali kinadharia (labda siku za mbele kiongozi mwingine ataona tofauti), bali kuzingatia tu kwamba *limetolewa kwetu rasmi, hapa na sasa* na Mungu. Hata kama kiongozi anadanganyika, sisi tukimtii hatudanganyiki kiutendaji. Mjumbe wa maongozi ya Mungu anaweza akawa mlemavu, hata hivyo anatuletea agizo kutoka juu.

*Utekelezaji* wa shauri la utiifu unapatikana hasa utawani unapohakikisha ufishaji wa matakwa yetu: kwa hiyo ni njia ya kufikia ukamilifu mapema, kwa kuzidi kulingana na matakwa ya Mungu mpaka ndani katika vipengele vyote vya maisha ya kila siku. Lakini, ili tuufikie ukamilifu wa Kikristo, walau tunapaswa kuwa na *roho ya shauri hilo,* yaani kutoambatana na matakwa yetu. Kama vile mtoto anavyopaswa kuwatii wazazi na walezi, kila Mkristo anapaswa kuwatii wale wote wanaomwakilisha Mungu kwake upande wa roho au wa jamii. Utiifu huo ukitekelezwa kwa imani (si kwa nje, kimwili na kwa hofu tu) unaunda utashi vizuri ajabu kwa kuufanya zaidi na zaidi uwe tayari na imara chini ya ule wa Mungu. Tukumbuke mara nyingi kwamba "hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu" (Rom 13:1); hivyo tunachofanya si kumtii mwenzetu, bali mkubwa wetu na kwa njia yake kumtii Mungu.

*Ni lazima tujifunze kuyatii matukio* pia kadiri yanavyotuonyesha matakwa ya Mungu kwa kuwa hapana lolote pasipo yeye kulitaka (likiwa jema) au kuacha litokee (likiwa baya). Ili utiifu uwe kamili unatakiwa kuzingatia hata ishara hizo za matakwa ya Mungu. Kwa mfano, kufaulu vizuri na kwa haki mtihani fulani kunatuwezesha kutenda mema zaidi; ni juu yetu kutoiharibu nafasi hiyo. Kinyume chake, tukishindwa au kuugua, pengine tunaonyeshwa kuwa njia tuliyoshika si ile aliyotupangia Mungu.

Kuna matukio ambayo yana maana ya pekee na kubadili hali ya familia au muundo wa jamii. Tunapaswa kufaidika nayo kadiri iwezekanavyo, badala ya kudai irudi hali iliyofaa wakati mwingine, lakini haitakiwi tena na Mungu. *Hatuwezi kurudi nyuma katika maisha yetu wala katika historia;* mzee hawezi kurudia ujana, wala karne yetu haiwezi kuirudia ile ya XIII, ingawa inatakiwa kufaidika na mema yote ya karne za nyuma ili iandae za kesho zitawaliwe na Mungu.

Katika namna hizo zote za kuyatii yanayodhihirisha matakwa ya Mungu, yaani *utiifu wa kutimiza wajibu wa sasa hivi,* tuzingatie kielelezo cha Mwokozi *aliyekuwa "mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba"* (Fil 2:8). Ndivyo watakatifu wote walivyofurahi kuyafia matakwa yao ili kujilisha yale ya Mungu yaliyodhihirishwa na amri, mashauri na matukio.

**MATUNDA YA UTIIFU**

La kwanza ni *unyofu mkubwa wa uamuzi* unaotokana na kwamba utiifu unatushirikisha hekima ya Mungu: "Ninao ufahamu kuliko wazee, kwa kuwa nimeyashika mausia yako" (Zab 119:100). Katika nafasi ngumu, utiifu unatupa jawabu la hakika kiutendaji kwetu, *sasa na hapa.* Kama tuzo la uaminifu wake, utiifu kamili

unapata mianga ya kipaji cha shauri inayotuongoza katika mambo ya Kiroho ambayo kiongozi huenda akashindwa kuyavumbua, na ambayo busara yetu haifikii kuyaeleza ipasavyo. Kipaji hicho kinahitajiwa hasa na wale wanaotakiwa kutoa amri, ili wasifanye hivyo kibinadamu tu; ndiyo sababu tusipotii vizuri kwanza, hatutaweza kamwe kuagiza inavyotakiwa.

Kinyume cha mtazamo wa wengi, utiifu unazidisha pia *nguvu za utashi.* Mtu asipotia shaka kuwa amri fulani imetoka kwa Mungu kumpitia kiongozi halali, ana hakika kwamba inaweza kutekelezwa kwa neema yake. Mt. Augustino alisema, "Mungu haagizi kamwe yasiyowezekana, bali anapotuagiza anatuambia tuyafanye tunayoyaweza na tumuombe neema ya kufanya tusiyoyaweza". Ndiyo maana alikuwa akiomba, "Bwana, nipe unayoniagiza, halafu uniagize yoyote unayotaka". Kwa sababu hiyo, tukipaswa kufia dini, Mungu anatujalia uaminifu katika mateso, hata tukiwa watoto, wanawali au wakongwe. Utiifu unatenda miujiza nje ya nafasi hiyo pia. Tunapopewa amri kutoka kwa Mungu, *tunapewa neema ya kuweza kuitekeleza,* na tukisali ili tuwe waaminifu tutaitekeleza kwa hakika, ingawa kwa tabu.

Hatimaye utiifu, badala ya kuwa aina ya utumwa, unatia *uhuru mkubwa wa wana wa Mungu*, kama vile ufukara wa hiari unavyotia utajiri wa kweli, na vile useja mtakatifu unavyotia upendo wa dhati. "Alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru" (2Kor 3:17), kwa sababu ukweli wa Kimungu unakomboa kutoka udanganyifu. Basi, utiifu unaotia ukweli maishani, unakomboa kutoka dhana zisizo na msingi za ulimwengu, misimamo, mitindo na maelekeo yake; unakomboa kutoka mahangaiko kuhusu kuhukumiwa na watu ("watasemaje?"): tenda mema na kuacha waseme; utiifu unakomboa kutoka shaka, wasiwasi na mafadhaiko. Unayafanya maisha yawe sahili zaidi kwa kuyainua. Uhuru unaongezeka, kwa sababu unatokana na mwanga: kadiri tunavyoelewa kuwa Mungu ndiye wema mkuu, tuko huru tusifuate mivuto ya malimwengu, na tuko imara dhidi ya vitisho vya waovu. Nani aliwahi kuwa huru kuliko wafiadini ambao kwa upendo na utiifu walitoa damu yao, hata upanga na moto havikuweza kuwafanya waasi?

Ukuu wa utiifu unadokezwa na maneno yafuatayo: *Kumtumikia Mungu ni kutawala.* Ni kutawala maono yetu, roho ya ulimwengu, adui wa watu na vishawishi vyake; ni kuingia katika utawala wa Mungu na kushiriki uhuru wake kuhusu viumbe vyote; ni kujitia mikononi mwake kama chombo kilicho tayari kufanya chochote atakachotaka. Hakika utiifu unatuandaa kuzama katika mafumbo ya Mungu, kuona matakwa yake katika matukio yoyote (ya kupendeza na ya tabu), na kuelewa "ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema" (Rom 8:28).

## 3.16. *USAHILI NA UNYOFU*

Busara ya Kikristo tuliyozungumzia inatakiwa kuendana na adili lingine, yaani usahili: "iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua" (Math 10:16). Yesu alipowapeleka mitume wake kama kondoo kati ya mbwamwitu aliwahimiza wawe na busara hasa kwa waovu, wasije wakadanganywa nao, na wawe na usahili hasa kwao wenyewe na kwa Mungu: hapo yeye kwa kipaji cha shauri atawaangazia busara katika nafasi ngumu na vipingamizi vikubwa. Ndiyo sababu Mwokozi aliwatabiria mara kwamba mbele ya watesi "si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu" (Math 10:20). Pasipo usahili busara inaelekea kutumia uongo na kugeuka ujanja. *"Huyo mwenye haki, aliye mtimilifu, amekuwa ni kicheko!"* (Ayu 12:4) kwa wajanja ambao wanaona usahili wake kuwa ujinga na upumbavu tu. Pengine usahili unaendana kweli na ujinga, lakini wenyewe ni jambo bora ambalo, tukitaka kulithamini ipasavyo (pamoja na ukweli na unyofu unaodumishwa nalo), tunapaswa kuzingatia kwanza kasoro zilizo kinyume chake.

### VILEMA VILIVYO KINYUME CHA USAHILI

"*Usahili* unaitwa hivyo kwa kupingana na *undumakuwili* ambao mtu moyoni ana kitu fulani lakini kwa nje anaonyesha kingine. Hivyo usahili unahusiana na adili la ukweli… tofauti ni hii tu, kwamba ukweli unaitwa hivyo kadiri ishara zinavyolingana na kinachoashiriwa; kumbe usahili unaitwa hivyo kadiri usivyolenga mambo mbalimbali" (Mt. Thoma wa Akwino). Kwa hiyo usahili unahusiana na adili linalotia ukweli katika maneno, matendo na mwenendo, kwa kuwa unapingana na *undumakuwili* wa mtu kutaka pesa za wenzake kwa kujisingizia nia ya kuwatumikia; au kutamani utawala na heshima kwa kujisingizia nia ya kujenga nchi. Undumakuwili, unaomfanya aonyeshe sura mbalimbali kadiri ya watu anaohusiana nao, unasababisha *uongo, udanganyifu* wa kutaka kuonekana tofauti na alivyo, *unafiki* ambao mtu anaonyesha adili asilonalo, tena *majigambo* na *dhihaka* ambazo anawacheka watu ili kujikuza juu yao.

### UKWELI NA MAISHA YA KIROHO

Adili la ukweli linategemea haki na kumfanya mtu aseme na kutenda daima kadiri ya ukweli. Si kwamba tunapaswa kumuambia yeyote ukweli wote, kuropoka maneno pasipofaa kwa kudai ni ari, kumbe ni utovu wa heshima. Bali tunapaswa kukwepa *neno lolote kinyume cha ukweli* tunaloshawishiwa kulitumia katika shida, ingawa kweli kadhaa ni vema kuzificha. Kama tumedanganya, tujishtaki kwa unyofu, badala ya kujitetea kwa visingizio ambavyo polepole vinafuta uaminifu na kufanya ushuhuda wetu, unaohitajika katika jamii, usiweze kukubalika.

Pengine ni vigumu kutunza siri tuliyokabidhiwa bila ya kuongopa. Lakini mara nyingi ni kosa letu tukiulizwa maswali yasiyofaa, kwa sababu tungejikusanya na kukaa kimya zaidi tungeulizwa kwa nadra tu. Hata hivyo, ikiwa Mkristo kwa kawaida ni msikivu kwa minong'ono ya kutoka juu, katika nafasi hizo ngumu Roho Mtakatifu atamuangazia la kujibu au la kuuliza, kama alivyowafanyia Wakristo waliopelekwa mahakamani kwa ajili ya imani. Wataalamu wa maadilidini wanatakiwa kukumbuka ukweli huo muhimu, badala ya kuruhusu maneno yanayolingana na uongo wa wazi. Ni afadhali kukiri kosa la uongo kuliko kupotosha maana ya uongo ili usilaumiwe inapotakiwa. Ni muhimu tudumishe unyofu aliotufundisha Bwana, "Maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu" (Math 5:37). Aliwaambia hivyo watu waliotaka kuthibitisha ushuhuda wao kwa kula kiapo bure, wakiingia hatari ya kuapa kwa uongo; inatosha tuzoee kusema ukweli daima ili maneno yetu yaaminike.

"Watu wanaojitangaza bora kuliko walivyo wanachukiza wenzao huku wakitaka kuwapita. Kinyume chake, wasiodhihirisha mema yote yaliyomo ndani mwao wanapendeza kwa utaratibu na kiasi" (Aristotle). *Adili la ukweli linatuelekeza kunyamazia sifa zetu:* kufanya hivyo si kudhuru ukweli kwa kuwa kunyamaza si kukanusha. *"Kama ningetaka kujisifu singekuwa mpumbavu, kwa sababu nitasema kweli. Lakini najizuia, ili mtu asinihesabie zaidi ya hayo ayaonayo kwangu au kuyasikia kwangu"* (2Kor 12:6).

Tukitekeleza adili hilo kwa maneno, matendo na mwenendo wetu wote, tutatia ukweli katika maisha yetu. Hapo Mungu, aliye ukweli mkuu, atatuinamia kwa minong'ono yake inayokuwa mwanzo wa sala ya hali ya juu. Kutumia uongo ni kuupa kisogo ukweli na kuja kukosa mianga ya kipaji cha hekima. Kuishi mfululizo katika ukweli ni kujiandaa kuipokea mianga hiyo inayotufanya tupenye na kuonja ukweli wa Mungu ambao siku moja tutauona wazi.

## USAHILI WA HALI YA JUU NI MFANO WA ULE WA MUNGU

Lile tawi la ukweli linaloitwa usahili linatuandaa zaidi tena kumiminiwa sala kwa kuwa haupingani na undumakuwili tu, bali pia na changamano lolote la bure, na yale yote ambayo yanaiga mitindo au kuchafuliwa na nia ya kuonekana namna fulani (k.mf. wepesi wa kuguswa moyo unaojidai kuwa upendo).

Mtazamo wa mtoto ni *sahili,* una lengo moja tu. Kwa maana hiyo, *"Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru"* (Math 6:22). Yaani nia yetu ikiwa nyofu na sahili, maisha yetu yote yatakuwa na umoja wa ndani, ukweli, uangavu, badala ya *kugawanyika* kama yale ya wanaotaka kutumikia *mabwana wawili kwa pamoja.* Katika ulimwengu uliojaa machangamano ya bure, sura za bandia na udanganyifu wa kila aina, tunahisi kuwa adili la usahili, yaani uaminifu kamili, linarudisha mwanga wa sifa mojawapo ya Mungu.

*Usahili wa Mungu* ni ule wa Roho tupu aliye ukweli na wema mkuu. Ndani mwake hamna mifuatano ya mawazo, bali daima wazo lilelile lenye kweli zote ndani yake. *Usahili wa akili yake* ni ule wa *mtazamo safi kabisa* ambao hauchanganyikani na udanganyifu wala ujinga wowote, bali unaenea kutoka juu kwenye kweli zote usibadilike kamwe. *Usahili wa utashi wake* ni ule wa *nia safi kabisa* inayoratibu vizuri ajabu mambo yote, hata kuacha mabaya yatokee ili mema makubwa zaidi yatokane nayo. Kinachopendeza zaidi katika usahili wa Mungu ni kwamba unaunganisha sifa ambazo zinaonekana kupingana, kumbe ndani mwake ni kitu kimoja bila ya kuangamizana. Usahili huo wa ajabu unarudisha mwanga wake katika tabasamu ya mtoto na katika macho manyofu ya watakatifu, yanayoshinda busara ya ulimwengu.

Tunajidanganya tunapodhani usahili ni kusema lolote linalotujia, halafu kusema kinyume chake hali ikibadilika au mtu akiacha kutupendeza: huo ni *ugeugeu tu* unaozaa uongo. Kumbe *usahili wa watakatifu* ni ule wa hekima isiyobadilika na wa upendo safi na wa nguvu kuliko hisi za moyo. Usahili ni nia nyofu ya kumpenda Mungu ambayo ishinde mguso wowote na isisimame kujitafutia bure aina nyingi za ibada hata kusahau lengo pekee. Ndio busara bora inayolenga shabaha moja kwa moja bila ya kujishughulisha na matendo ya wengine.

Aliyekamilika ni *mtu sahili* ambaye anapima yote kwa mwanga wa Mungu (si alivyoguswa mara) na anayataka kwa ajili ya Mungu tu. Anayepima yote kwa jinsi yanavyompendeza anahangaishwa na lolote, kumbe aliye sahili anadumisha amani ya ndani kwa hekima yake na upendo wake. Tofauti na ujinga na upumbavu, usahili huo wa hali ya juu unapatana na busara ya Kikristo inayozingatia pia vipengele vidogo vya matendo yetu na matokeo yake ya mbali.

Yesu alitokeza vizuri ajabu usahili wa Mungu: ndani mwake vilipatana ukali mtakatifu wa haki dhidi ya wanafiki na huruma isiyo na mipaka kwa wale wote ambao ndiye mchungaji wao mwema. Ndani mwake vilipatana kwa usahili kujishusha hadi vilindini na kujiheshimu kwa hali ya juu. Kwa miaka thelathini aliishi kama fundi tu, akasema amekuja *kutumikia,* akawaosha mitume miguu, akapokea dharau za mateso kisha kumuomba Baba kwa usahili amuepushe. Kwa usahili huohuo alijishuhudia mbele ya Pilato kuwa ni mfalme, akamrudishia Baba roho yake akitokeza ukuu uliomfanya akida akiri, "Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu" (Math 27:54).

Usahili huo wa hali ya juu unaandaa hata wasio na elimu waelewe kwa ndani mambo ya Mungu: "Tafakarini habari za Bwana kwa moyo mwema, na kumtafuta katika unyofu wa moyo" (Hek 1:1). "Afadhali maskini aendaye katika unyofu wake" (Mith 19:1). "Watiini… si kwa utumwa wa macho, kama

wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana" (Kol 3:22). "Kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikra zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo" (2Kor 11:3). Tunapaswa kuutunza usahili huo kwa Mungu, kwa viongozi wetu, kwetu wenyewe: ndio ukweli wa maisha.

Usahili huo unawawezesha watu safi *kupenya ukuu wa Mungu*, njia za maongozi yake na mafumbo yasiyochunguzika ambayo yanawakwaza wengine. Kwa walio sahili hayo ni sahili, ingawa yanafunikwa na giza, kwa sababu *katika mambo ya Mungu* yale *yaliyo sahili zaidi* (k.mf. *Baba Yetu*) ndiyo *ya juu na ya dhati zaidi.* Tunasahau ukweli huo kwa sababu katika malimwengu ni kinyume: yakiwa mchanganyiko mkubwa wa mema na mabaya yanahitaji upambanuzi, hivyo anayetaka kuwa sahili katika hayo hayaelewi, anabaki juujuu kama mjinga. Kumbe katika mambo ya Mungu usahili unaendana na udhati na ukuu, kwa kuwa yaliyo ya juu zaidi katika Mungu na yaliyo ya dhati zaidi katika mioyo yetu ni usahili mtupu.

Nyakati hizi Bwana ametujalia Mt. Teresa wa Mtoto Yesu, kielelezo cha usahili unaozama katika mafumbo. "Badala ya kufanana na watu wale wazuri ambao tangu utotoni walitimiza aina zote za kujitesa, mimi niliridhika tu na kupinga matakwa yangu, kuzuia neno lolote la kurudishia chukizo, kutoa huduma ndogondogo pasipo kuzitia maanani, na mengine mengi ya namna hiyo… Katika njia yangu ndogo mambo yote ni ya kawaida kabisa; ni lazima yale yote ninayoyafanya, watu wadogo waweze kuyafanya vilevile … Jinsi ilivyo rahisi kumpendeza Yesu na kuvuta moyo wake kwetu! *Inatosha tumpende* pasipo kujiinamia wala kutafiti mno kasoro zetu. Hivyo, inaponitokea kuiangukia mojawapo nainuka mara. Kumuangalia Yesu na kukiri unyonge wangu unarekebisha kila kitu. Mwenyewe alijiita *'ua la uwandani'* (Wim 2:1) ili kutuonyesha tu anavyopendelea usahili". Tunaona wazi lilivyotimia ndani mwake neno alililoliandika, "Mara nyingi Bwana anaridhika kuwajalia hekima walio wadogo zaidi". Hao wanaona muungano na Mungu unadai nini ili udumu imara katika nafasi ambazo mara nyingi hazitarajiwi bali ni za tabu.

Tunapoeleza maisha ya Kiroho, ni lazima tusisitize maadili kama hilo kwa jinsi yanavyochangia namna ya kuwaza na ya kutenda. Baadaye mafundisho juu ya *sala ya kumiminiwa* yataonekana kuwa *matokeo* ya yote yaliyosemwa kuhusu ustawi wa maadili na wa vipaji saba katika watu ambao kweli wamejikana na kuambatana na Mungu karibu mfululizo.

## 3.17. *ROHO YA IMANI NA USTAWI WAKE*

Kisha kusema juu ya ustawi wa maadili ya kiutu katika hatua ya mwanga, tuzungumzie sasa ustawi wa maadili ya Kimungu kuanzia imani ili tujiandae kuelewa sala inavyotakiwa kuwa katika hatua hiyo. Basi, tuone roho ya imani ni nini, halafu inavyopaswa kustawi ndani mwetu, hatimaye ubora na uwezo wake unavyokusudiwa kuwa ili tuishi nayo daima: "Mwenye haki ataishi kwa imani" (Rom 1:17; Gal 3:11).

### ROHO YA IMANI NI NINI?

Kila mara mtu anafuata ama umbile, asipopita fikra za kibinadamu tu, ama imani, anapolenga mbinguni kwa njia ya utakatifu. Roho hizo zinazotuongoza maishani ni namna maalumu za kupima, kuona, kuhisi, kupenda, kushabikia, kutaka na kutenda. Basi, roho ya imani ni kupima yote kwa mtazamo wa juu ambao unapita maumbile na kutegemea mamlaka ya Mungu katika kujifunua, na ukweli wake katika kutushirikisha utukufu. Tunaelewa zaidi roho ya imani tukiangalia iliyo kinyume chake, yaani upofu wa roho unaozuia mtu asione mambo ya Mungu isipokuwa kidunia na kutoka nje. Hivyo Israeli haikuelewa uteuzi wake kadiri ya ukweli wa Mungu ulio wa juu kuliko ukabila au ubaguzi wowote.

Imani ina mitazamo mipana kuliko huo kutokana na usahili wake unaoshiriki hekima ya Mungu. Juu sana kuliko mifuatano ya mawazo, ni *tendo sahili* ambalo tunamsadiki Mungu anayefunua na papo hapo anajifunua. Kwa tendo hilo lipitalo maumbile tunaambatana naye pasipo udanganyifu na hivyo katika giza tunalenga kutazama mambo ya Mungu, juu kuliko hakika zote za kimaumbile. Hakika inayotokana na imani tuliyomiminiwa na Mungu, inapita hata hakika ya akili tunayoweza kujipatia kwa kuzingatia miujiza inayothibitisha ufunuo wake.

Imani ni zawadi ya Mungu: "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Ef 2:8). Ni kama hisi ya Kiroho inayotuwezesha kusikia ulinganifu wa mafumbo aliyotufumbulia, yaani kusikia sauti yake kabla hatujakaribishwa *kumuona* uso kwa uso.

"Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kujua tuliyokirimiwa na Mungu, nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni. Basi, mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni. Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu. Maana, ni nani aliyefahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo" (1Kor 2:12-16). Ili ifanye hivyo imani inasaidiwa na vipaji vya akili na hekima, lakini yenyewe ndiyo inayotufanya *tushike* Neno la Mungu pasipo udanganyifu.

Ingawa mafumbo yake ni ya giza kwetu, adili la imani ni bora kuliko ujuzi mwangavu walionao malaika

kwa umbile lao, kwa sababu imani tunayomiminiwa inalingana na uzima wa milele, kwa kuwa ndiyo mbegu yake. Malaika wenyewe walihitaji zawadi hiyo waweze kulenga hali ipitayo maumbile waliyoitiwa.

Mungu anapotujalia imani, anapenya roho yetu na kusema nayo si kwa mifuatano ya maneno, bali kwa wazo la ghafla. Imani ikifika, tunaachana na mfuatano wowote wa mawazo tuliokuwanao pamoja na sababu zake: tunaviweka chini ili imani ivikalie kama mtawala. Imani ikiangaza akili kwa mng'ao wa kweli zake, mara utashi unahisi joto la upendo wa Mungu.

**IMANI TULIYOMIMINIWA INATAKIWA KUSTAWI HADI KIFO**

Imani inatakiwa kukua kila siku. "Imani inaweza ikawa kubwa ndani ya Mkristo mmoja kuliko ndani ya mwingine, upande wa akili kutokana na hakika na imara kubwa zaidi katika kushika ufunuo, na upande wa utashi kutokana na utayari na utiifu au tumaini kubwa zaidi" kwa kuwa "imani tunayomiminiwa inalingana na zawadi ya neema, ambayo si sawa kwa wote" (Mt. Thoma wa Akwino). Bwana aliwasema wanafunzi wake kuwa "wa imani haba" (Math 6:30); kumbe alimuambia mwanamke Mkananayo, "Mama, imani yako ni kubwa!" (Math 15:28).

Imani inaweza kukua kwa *upana* na kwa *dhati au nguvu.* Inapanuka tunapozidi kujifunza yale yote Kanisa linayoyafundisha: wanateolojia wanayajua wazi, lakini si kwamba imani yao ni ya dhati na ya nguvu kadiri ilivyoenea. Kumbe tunakuta watakatifu wasiojua mengi katika hayo, lakini wanapenya mafumbo yalivyofumbuliwa na Injili kwa usahili. Mitume walimuomba Bwana imani hiyo waliposema, "Tuongezee imani" (Lk 17:5). Yesu akawaambia, "Yoyote mtakayoomba katika sala mkiamini, mtapokea" (Math 21:22). Tutayapokea hasa tukijiombea kwa udumifu yaliyo ya lazima au ya kufaa sana kwa wokovu wetu, kama vile ustawi wa maadili.

**UBORA NA UWEZO WA IMANI**

Thamani ya imani inapimwa na matatizo inayoyashinda katika majaribu: *"Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu…* yeye aliyeambiwa: Katika Isaka uzao wako utaitwa, akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu… Kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa wa simba, walizima nguvu za moto… Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizungukazunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya – watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao" (Eb 11:17-19, 33-34, 36-38). Mambo kama hayo yanatokea hata siku hizi. *"Basi na sisi pia, tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu;* ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu" (Eb 12:1-2).

"Mzingatieni Kristo aliyevumilia upinzani wa namna hiyo kutoka kwa wakosefu… Hapo *katika tabu yoyote mtaona dawa katika msalaba wa Yesu.* Humo mtakuta vielelezo vya maadili yote. Mt. Gregori Mkuu alisema tukiyakumbuka mateso ya Yesu hatutaona chochote kuwa kigumu au cha tabu tusiweze kukivumilia kwa subira na upendo" (Mt. Thoma wa Akwino). Imani ikistawi inatufanya kwa kawaida tuzidi kuhisi fumbo la Kristo; polepole hisi hiyo ipitayo maumbile inakuwa sala ya kumiminiwa yenye kupenya na kuonja, asili ya furaha na amani: "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini… Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Fil 4:4,7).

**TUISHIJE KWA ROHO YA IMANI?**

Tunapaswa kuishi hivyo kwa kupima yote kwa mwanga huo wa juu: kwanza Mungu, halafu nafsi yetu, jirani na matukio yote.

Je, kuna haja ya kusema tumzingatie Mungu kwa imani? Bila ya shaka! Kwa kuwa mara nyingi tunamzingatia kwa dhana zisizo na msingi, kwa miguso ya kibinadamu mno na kwa maono yetu, badala ya kupitia ushuhuda alioutoa juu yake mwenyewe. Pengine hata tunaposali tunajisikiliza tu kwa kumkopesha Mungu mawazo yetu yanayotokana na umimi. Tunapojiamini kipumbavu tunaelekea kudhani huruma ya Mungu ni kwa ajili yetu, na haki yake kwa watu tusioelewana nao. Kumbe tukikata tamaa tunatilia shaka kimatendo upendo wa Mungu kwetu na huruma yake kuu. Kwa imani tunamuona Mungu kupitia mafumbo ya maisha na mateso ya Mwokozi na kupitia uhai wa Kanisa linalofanywa upya na ekaristi kila siku. *Jicho la imani linasafika zaidi na zaidi* kwa ufishaji wa hisi na maono, maoni na matakwa yetu: hapo tu unakuja kuanguka polepole ule *utaji wa kiburi* unaotuzuia tusione mambo ya Mungu au tuone tu vivuli vyake na tata zake.

Tunapaswa vilevile kujitazama kwa imani. Tukijitazama kibinadamu tu, tunaona ndani mwetu sifa za umbile ambazo mara nyingi tunazizidisha. Baadaye, majaribu yakituonyesha tulivyojidanganya tunavunjika moyo kwa urahisi. Kumbe kwa imani tunakuja kujua utajiri upitao maumbile ambao Bwana ametutia katika ubatizo na kutuongezea kwa ekaristi, yaani thamani ya neema inayotia utakatifu, ya uwemo wa Utatu mtakatifu pamoja na ukuu wa wito wa Kikristo. Tunakuja kujua pia vizuio vya ustawi wa uzima huo, k.mf.

usahalifu wa mbegu ya uzima wa milele iliyopandwa ndani mwetu, na kiburi cha kipumbavu. Kwa mtazamo huo wa juu tunakuja kujua mapema kilema kinachotutawala na kivutio maalumu cha neema tulicho nacho, ambavyo cha kwanza kikomeshwe na cha pili kistawishwe.

Lakini tunayesahau zaidi kumtazama kwa imani ndiye jirani. Tunamtazama kibinadamu tu, tukiathiriwa na dhana zisizo na msingi, kiburi, wivu na vilema vingine. Kwa hiyo ndani yake tunakubali yale ambayo yanatupendeza kibinadamu, yanatufaidisha au kutukuza; kumbe tunahukumu yale ambayo yanatukinaisha, yanamfanya bora kuliko sisi na kutushusha. Dhambi ngapi za kuhukumu na kusingizia zinatokana na mtazamo huo uliofunikwa na utaji wa umimi! Tukijifunza kumtazama jirani kwa imani ni faida kubwa pande zote. Hapo tunakuja kuwaona wakubwa wetu kama wawakilishi wa Mungu, na kuwatii kwa moyo pasipo kuwasema. Tunaona kuwa wasiotupendeza wamekombolewa kwa damu ya Kristo, pengine ni viungo vya mwili wake vinavyokaribia moyo wake kuliko sisi: mara nyingi tunaishi miaka pamoja na watu safi tusitambue uzuri wa roho zao. Vilevile, tukija kuwatazama kwa imani wanaotupendeza, pengine tunavumbua wana maadili ya Kimungu kiasi cha kuzidisha na kutakasa mapendo tunayowaonea; pia kwa wema tunaona vizuio walivyonavyo kwa utawala wa Mungu na tunaweza kushauriana nao tusonge mbele katika njia yake.

Hatimaye tunapaswa kutazama kwa imani matukio yote ya maisha yetu, ya furaha na ya uchungu vilevile. Mara nyingi tunaridhika kuyaona upande wa hisi tu, au kwa akili iliyoathiriwa na dhambi. Mara chache tunayazingatia Kimungu, kwa kuona kwamba *"katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema"* (Rom 8:28): hata katika upinzani, matatizo makubwa yasiyotarajika na dhambi (tukiweza kujinyenyekesha kutokana nazo). Katika kukosewa haki na watu tunaweza kutambua haki ya Mungu ikiadhibu makosa ya siri ambayo hatulaumiwi na mtu; au tunahisi majaribu ya Kimungu, na utakaso unaokusudiwa kupatikana kwa njia ya hayo.

Hapo baadaye tutasema juu ya imani kutakaswa kwa majaribu kadhaa ya aina hiyo; kabla hatujafikia hatua hiyo tujitahidi kukua katika imani, badala ya kupima yote kibinadamu tu. Ni lazima tujinyime mianga midogo na ya bandia ili tujaliwe ile ya juu; tuache kufuata mno akili yetu ili tuone uangavu mkuu wa mafumbo ya imani na kuishi kulingana nayo. Hivyo tunaelewa kwa nini hatutakiwi kuitikia vishawishi dhidi ya imani, bali kuvikataa au kuviruka kwa kukiri imani kwa dhati zaidi; Bwana anaviruhusu kwa maendeleo yetu tu.

## 3.18. *TUMAINI KWA MUNGU NA HAKIKA YAKE*

Kisha kusema juu ya imani, tuzingatie tumaini kwa Mungu linavyotakiwa kuwa ndani ya wanaoendelea na tuelewe maana ya hakika yake. Sawa na imani, adili la kumiminiwa la tumaini ni la lazima kwa wokovu na kwa ukamilifu. Tena haitoshi tumtumainie Mungu kwa namna dhaifu na kwa kwikwi kama wengi wanavyofanya; bali tuyapende matakwa yake ambayo mara nyingi yana giza, pengine yanashangaza hata kutaka kuchukiza: tuyapende kwa utiifu wa kitoto na kusubiri msaada wa Mungu kwa tumaini imara, nyenyekevu na la kudumu.

### KASORO ZA KUEPWA

Ni lazima tuepe kasoro mbili zinazopingana: kujiamini kipumbavu na kukata tamaa. Inafaa tuzione kwanza ili tuelewe tumaini halisi ni nini na jinsi linavyoinuka juu ya hizo.

Kujiamini kuna namna mbili: ama mtu anategemea mno nguvu zake mwenyewe asiombe vya kutosha msaada wa Mungu wala kuzingatia neema inavyohitajika kwa tendo lolote la kuletea wokovu; ama mtu anatarajia kupewa na huruma ya Mungu jambo lisilowezekana kabisa, k.mf. msamaha pasipo toba halisi, au uzima wa milele pasipo juhudi.

Mara nyingi watu hao, wakipatwa na majaribu, wanatumbukia kosa lililo kinyume chake, yaani kukata tamaa, kana kwamba *jema lililo gumu kupatikana,* ambalo ndilo kusudio la tumaini, lingekuwa halifikiki. Kukata tamaa kunaweza kukazaa *uzembe katika mambo ya Kiroho,* unaotufanya tuione ngumu mno kazi ya kupata utakatifu na unaotuzuia tusijitahidi kuifanya. Hatimaye kuna hatari ya kukata tamaa kuhusu wokovu wenyewe.

Wengi wanayumbayumba hivyo wasiweze kamwe kuelewa tumaini la Kikristo na kuliishi ipasavyo.

### MFUMO HALISI WA TUMAINI LA KIKRISTO

Adili hilo linazungumziwa kidogo kuliko imani na upendo, lakini ni muhimu. Likiwa adili la kumiminiwa na Mungu *linapita maumbile,* hivyo linapita hamu ya kimaumbile ya heri na hata lile tumaini la kimaumbile kwa Mungu linaloweza kutokana na kuujua wema wake kwa akili tu.

Kwa tumaini la kumiminiwa tunalenga heri ipitayo maumbile, yaani kumpata Mungu milele, kumuona kama anavyojiona, na kumpenda kama anavyojipenda. Tena tunamlenga tukitegemea msaada aliotuahidia. Sababu ya kutumaini si juhudi zetu, bali ni Mungu anayetusaidia daima kadiri ya huruma yake, ahadi zake na uwezo wake mkuu. Sababu ya adili lolote la Kimungu haliwezi kamwe kuwa kiumbe, hata kikiwa bora, bali ni Mungu tu. Hivyo *tunataka kumpata Mungu,* lakini *kwa ajili yake*, kwa kuwa ndiye lengo kuu la tumaini ambalo tena linatakiwa kuhuishwa na upendo. Yaani kwa tumaini tunamtamani Mungu *si kwa ajili yetu* kama

tunavyotamani chakula ili kuishi, bali *kwa kujiweka chini yake.* Kwa hiyo halina kasoro yoyote: ni adili la Kimungu, ingawa la chini kuliko upendo.

Ikiwa adili la kiutu la moyo mkuu ni zuri kwa sababu linatufanya tukusudie makuu, zuri zaidi ni tumaini linalotufanya tumlenge Mungu mwenyewe tuwe naye milele. Hasa kwa sababu halitutamanishi tu kiwango cha chini cha heri ipitayo maumbile, bali uzima wa milele pasipo kupanga kiwango chochote; kinyume chake linatufanya tumuelekee Mungu kwa kasi zaidi na zaidi kutokana na kumtamani zaidi na zaidi.

**HAKIKA YA TUMAINI**

Mt. Thoma wa Akwino ametofautisha vizuri aina mbalimbali za hakika. Kwanza alikabili hoja ya kwamba *hakuna anayeweza kuwa na hakika ya kuokoka* asipojaliwa ufunuo wa pekee; na kwa kuwa huo ni wa nadra, tumaini la wengi linaonekana halina hakika. Tena ya kwamba kati ya wale wanaotumaini wengi watavunjika moyo na hatimaye kupotea. Akasisitiza kuwa tumaini lina hakika, ingawa tofauti na ile ya imani iliyomo akilini: hakika ya tumaini imo katika utashi na ina namna ya elekeo. Tumaini *linaelekea kwa hakika lengo lake* likishiriki hakika ya imani; kama vile tukipanda treni tuna hakika ya kuwa njiani na tunatumaini kufika salama, ingawa hatuna hakika ya kufika. Hakika ya tumaini si ya kufikia wokovu, bali ya kuuelekea kwa uongozi wa imani usiodanganya kadiri ya ahadi za Mungu "ambaye haagizi kamwe yasiyowezekana, bali anatuagiza tutende tunavyoweza, na tuombe tusiyoyaweza peke yetu" (Mtaguso wa Trento). Yatokanayo kwa utekelezaji ni mengi kuhusu sifa za tumaini ambazo zikue pamoja nalo.

**SIFA ZA TUMAINI LA KIKRISTO**

"Wote wanapaswa kuwa na tumaini imara kabisa kuhusu msaada wa Mungu. Watu wasipokataa neema zake, mwenyewe atatimiza kazi ya wokovu aliyoianzisha ndani mwetu, akisababisha ndani mwetu kutaka na kutenda. Lakini 'anayejidhania kuwa amesimama aangalie asianguke' (1Kor 10:12), na atimize wokovu wake 'kwa kuogopa na kutetemeka' (Fil 2:12) 'katika tabu, katika kukesha, katika kufunga' (2Kor 6:5)… Kadiri ya neno la mtume, 'Kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi' (Rom 8:13)". Kulingana na mafundisho hayo ya Mtaguso wa Trento, tumaini la Kikristo lina sifa mbili: *kufanya juhudi* ili kutojiamini kipumbavu kwa kusubiri tuzo la Mungu pasipo kufanya kazi; na *kuwa imara lisishindikane,* ili kutokata tamaa.

Linadaiwa bidii kwa sababu linalenga *jema lililo gumu kupatikana*; tunapaswa kujitahidi kwa unyenyekevu na kujikana ili tudumishe *hamu hai ya uzima wa milele*. Hamu hiyo inapozwa na tamaa za anasa na za vyeo na ni ya nadra hata kwa Wakristo wema, ingawa hakuna la kutamaniwa kuliko muungano na Mungu. Halafu tunapaswa kujitahidi ili kustahili heri ya milele. Tunahitaji neema ili kulifikia lengo, lakini tunajaliwa neema ili tuifanyie kazi kwa bidii kubwa zaidi na zaidi, si kusudi tupumzike: "Mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka" (Mk 13:13). "Hata mtu akishindana katika machezo, hapewi taji, asiposhindana kwa halali" (2Tim 2:5). Inatupasa tuondoe vizuio vya tabia mbovu, uzembe, kiburi, ugomvi, uchu wa madaraka, na tushike amri vizuri zaidi na zaidi kadiri ya wito wetu. Tumaini hilo lenye bidii pamoja na kipaji cha uchaji vinatuepusha tusijiamini kipumbavu.

Kati ya matatizo yanayoweza yakazuka hadi kifo na hadi kuingia mbinguni, tumaini linatakiwa kuwa *imara lisishindikane* wala kupungua kamwe kwa vishawishi, majaribu au makosa. Halitakiwi kushindwa na vishawishi vinavyotokana na ulimwengu, mwili na shetani: *"Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?"* (Rom 8:31). "Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" (1Kor 10:13). Tumaini halitakiwi kupungua hata kwa majaribu ambayo Bwana anatutakasa na kutufanyiza kazi kwa wokovu wa watu. Sababu ya kutumaini ni *mwenyewe aliye tayari daima kutusaidia*. Abrahamu *"aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa"* (Rom 4:18), hadi akajiandaa kumchinja mwanae Isaka aliyeahidiwa atampatia uzao mkubwa. Lengo la Mungu kutakasa tumaini ni kuliondolea vurugu za umimi, si kutufanya tuache hamu ya wokovu wetu, jambo ambalo lingekuwa sawa na kujinyima kumpenda milele Mungu kuliko vyote. Kama tungeacha kutumaini kwa lengo la kupata upendo safi zaidi, papo hapo tungeacha upendo wenyewe. Hatimaye, tumaini halitakiwi kupungua hata mbele ya makosa tuliyotenda. "Msizingatie kamwe makosa yenu yaliyopita isipokuwa kwa mwali mwangavu wa huruma isiyo na mipaka, ili kumbukumbu yake isiwakatishe tamaa, bali iwafanye mtumainie thamani isiyo na mipaka ya stahili za Mwokozi" (Mt. Katerina wa Siena). "Watu wanaweza wakadhani kwamba nina tumaini kubwa kwa Bwana kwa sababu sijawahi kutenda dhambi. Mama yangu, ukweli ni kwamba kama ningekuwa nimetenda madhambi yote yanayowezekana ningekuwa na tumaini hilohilo, ningeona wingi huo wa makosa kuwa ni tone la maji tu lililotupwa katika tanuri yenye kuwaka" (Mt. Teresa wa Mtoto Yesu). Yaani sababu ya kutumaini si juhudi zetu wala usafi wetu, bali ni huruma ya Mungu inayotusaidia.

**MATUNDA MAZURI AJABU YA TUMAINI HAI LILILOTHIBITISHWA NA MAJARIBU**

Baada ya majaribu kadhaa, tumaini likiwa limeimarika linashinda kizuio chochote: "Tunasimama ndani yake (neema); na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Wala si hivyo tu, ila *na tufurahi katika dhiki*

pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" (Rom 5:2-5). "Mtume Paulo ametuonyesha kwanza ukuu wa tumaini kwa njia ya ukuu wa jambo linalotarajiwa, halafu nguvu, ari ya tumaini. Kwa kuwa anayetumaini sana jambo fulani, kwa ajili hiyo yuko radhi kuvumilia matatizo na machungu. Basi, ishara ya kuwa tunamtumainia Kristo kwa uimara ni kwamba hatufurahii tu wazo la utukufu ujao, bali pia tabu na majaribu tunayopaswa kuvumilia. *'Imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi'* (Mdo 14:22). Mtume Yakobo alisema, *'Hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi'* (Yak 1:2-3). Kwa kuwa anayevumilia majaribu anakuwa bora, *amefaulu.* Katika kitabu cha Hekima (3:4-6) imeandikwa kuhusu waadilifu, 'Hata ikiwa - waonavyo watu - wanaadhibiwa, hata hivyo taraja lao limejaa kutokufa, wakiisha kustahimili kurudiwa kidogo watapokea wingi wa mema. Kwa kuwa Mungu amewajaribu, na kuwaona kuwa wamemstahili; kama dhahabu katika tanuru aliwajaribu, akawakubali mithili ya kafara'. Hivyo jaribu linakuza tumaini, na tumaini halidanganyi kamwe, kwa sababu Mungu hawaachi wanaomtumainia: *'Nani aliyemtumainia Bwana akaaibika?'* (YbS 2:10). Ni wazi kuwa Mungu hatakataa kujitoa kwa wale anaowapenda, ambao ameshawapa Mwanae… amewaandalia mema ya milele wale wanaompenda kuliko vyote" (Mt. Thoma wa Akwino).

Katika majaribu makubwa, tutarajie yasiyotarajika, tukimpenda Mungu kwa ajili yake mwenyewe. Hapo upendo unastawi na kuwa safi, nao unahuisha tumaini badala ya kulifuta. Majaribu hayo yanafaa kulitakasa kutoka umimi wa kutaka kujipatia ukamilifu ambao ni "wetu". Mama fulani aliyetaka *"kupata utakatifu",* baadaye akatokeza hamu yake kwa namna isiyo ya binafsi hivyo, akisema, "*Bwana, ufalme wako uzidi kufika ndani mwangu".* Hapo alifurahi kutoheshimiwa na watu, akitamani tu kuungana na Bwana. Tumaini linastawi kwa kutakaswa. *"Nakushukuru kwa moyo, Bwana wangu, kwa kuwa mambo hayaendi ninavyotaka mimi,* bali unavyotaka wewe: afadhali yaende unavyotaka wewe, kwa sababu hakuna shaka ya kwamba unavyotaka wewe ni vema kuliko ninavyotaka mimi" (Mt. Filipo Neri). *Kwa wanaompenda Mungu, yote yanachangia ustawi wao,* hata kusumbuka, kushindwa na kupingwa: hizo zote ni nafasi za kuinua moyo kwa Mungu kwa imani na tumaini. "Hata kama mtu hajisikii kuwa na tumaini hilo kwa Mungu, asiache kulitekeleza. Kutojiamini sisi na nguvu zetu kuendane na unyenyekevu na imani, ambavyo vinajaliwa kumtumainia Mungu. Kadiri tusivyo na raha tunapaswa kumtumainia yule ambaye anaona hali yetu na anaweza kutusaidia! Hakuna anayemtumainia Mungu pasipo kuchuma matunda ya tumaini lake. Mtu aendelee kutulia na kumtumainia yule anayeweza kustawisha kilichopandwa. Hatutakiwi kuacha kazi, lakini katika kuifanya tumtumainie Mungu tu kuhusu ufanisi wake" (Mt. Fransisko wa Sales).

## 3.19. *UPENDO WA KULINGANA NA MATAKWA YA MUNGU*

Sasa tuzingatie ustawi wa upendo unavyotakiwa kuwa katika hatua ya mwanga, ili tuvuke kutoka upendo wa kujitafutia faida kama kibarua hadi upendo kamili.

**DALILI ZA UPENDO USIOKAMILIKA**

Upendo kwa Mungu haujakamilika ikiwa katika kumtumikia tunashikamana na faida yetu, tunajifanya lengo na kutamani turidhike. Kinachodhihirisha zaidi upungufu huo ni kwamba tukinyimwa faraja tulizokuwa tunazipata kwa Mungu, mara huo upendo haututoshi wala haudumu, bali unafifia na kupoa zaidi na zaidi. Upungufu huohuo upo katika kumpenda jirani: tunajifanya lengo la matendo ya upendo, tunaridhika na utendaji wetu wa kibinadamu, ambamo mna kiasi kikubwa cha harakaharaka na umimi, kikifuatwa na ubaridi tusiporudishiwa shukrani.

**MFUMO WA UPENDO NA DALILI ZA USTAWI WAKE**

Dalili za ustawi wa upendo zinaelea katika mfumo wake wa kuwa *urafiki* unaotupasa tuwe nao kwa Mungu kutokana na wema wake usio na mipaka ambao unang'aa juu yetu ukituhuisha na kutuvuta kwake. Maandiko yanasema sehemu mbalimbali kuwa mwadilifu ni "rafiki wa Mungu" kama Abrahamu (Yak 2:23): hekima "huwafanya wanadamu kuwa rafiki za Mungu" (Hek 7:27); na Yesu alisema, "Ninyi nimewaita rafiki" (Yoh 15:15).

Basi, urafiki halisi una sifa tatu: kwanza ni *upendo wa kumtakia mwingine mema tunayojitakia,* tofauti na pendo tunalojitakia jema fulani, k.mf. chakula. Tunapaswa kuwatakia marafiki wetu mema yanayowafaa, na kumtakia Mungu ufalme wake uenee katika akili na nyoyo za watu. Pili, urafiki unadai wawili *wapendane,* yaani haitoshi upendo uwepo upande mmoja. Kadiri mema wanayotakiana ni bora, urafiki wao unakuwa bora. Uadilifu ndio msingi wake wasipotakiana tu mambo ya kupendeza na kuleta faida, bali uaminifu katika wajibu na maendeleo ya Kiroho. Tatu, urafiki unadai kufahamiana, *kuchanga maisha* walau kwa kubadilishana mawazo na miguso ya siri. Urafiki huo unaelekea muungano wa ndani wa mawazo, miguso, matakwa, sala, sadaka na utendaji. Sifa hizo tatu za urafiki halisi zinapatikana katika upendo unaotuunganisha na Mungu na watu ndani yake.

Kilindini mwa utashi wetu umbile linatuelekeza kumpenda Mungu, *asili ya uhai wetu,* kuliko

tunavyojipenda na tunavyopenda lolote lile, kama vile kiungo kinavyompenda mwenye nacho kuliko kinavyojipenda ili kudumisha uhai. Lakini elekeo hilo, lililopunguzwa na dhambi ya asili, lisipoponywa na neema haliwezi kutufanya tumpende *kimatendo* Mungu kuliko yote.

Juu ya hilo, katika ubatizo tumepokea upendo ambao tunamtakia Mungu, *asili ya neema,* mema yanayomfaa, yaani awatawale watu moja kwa moja, kama vile yeye anavyotutakia mema sasa na milele. Urafiki huo unategemea kuishi pamoja, kwa kuwa Mungu anatushirikisha uhai wake mwenyewe: kwa neema tumezaliwa naye na kufanana naye kama watoto na baba yao. Upendo kati yetu na Mungu unadhihirika hasa akituangazia na kutuinua tutekeleze upendo wa kumiminiwa jinsi tusivyoweza kwa neema ya msaada ya kawaida. Ni ushirika wa Kiroho ulio utangulizi wa ule wa milele. Hata kwa kiwango cha chini, unatufanya tumpende Mungu kuliko tunavyojipenda na tunavyopenda zawadi zake, walau *upande wa tathmini,* ingawa pengine hatuhisi upendo huo (k.mf. wakati wa ukavu), nao mwanzoni hauna *nguvu na ari* zinazopatikana katika waliokamilika na hasa mbinguni. Mama anahisi upendo alionao kwa mwanae aliyempakata kuliko ule alionao kwa Mungu asiyemuona; lakini akiwa Mkristo kweli anampenda kitathmini Mungu kuliko mtoto. Halafu, upendo wa tathmini ukistawi unazidi kupata nguvu (na kuitwa ari) mpaka mbinguni utashinda mapendo yetu makuu. Upendo huo hauhitaji elimu, inatosha kumjua Baba wa mbinguni kwa imani. Tukiacha kumpenda kwa dhambi yoyote ya mauti, mara tunaanza kupotea. Tunavyoona, upendo wa tathmini ni kinyume cha miguso inayoonyesha upendo isionao.

Upendo ukiwa hivyo, dalili za ustawi wake ni zipi? Kwanza ni zile za neema inayotia utakatifu: *1° kutojisikia kuwa na dhambi yoyote; 2° kutotafuta malimwengu* (anasa, mali, heshima); *3° kumfurahia Mungu* na kumfikiria, kumuabudu, kumshukuru, kumuomba msamaha, kusema naye, kumtamani. Tuongeze dalili zifuatazo: *4° kutaka kumpendeza Mungu* kuliko wale wote tunaowapenda; *5° kumpenda jirani kwa matendo* (ingawa ana kasoro kama sisi) kwa kuwa ni mtoto wa Mungu na anapendwa naye. Hapo tunampenda Mungu katika jirani, na tunampenda jirani katika Mungu. Heri anayependa hivyo, akifurahia tu kumpendeza Mungu. Akiwa mwaminifu siku moja ataonja utamu wa upendo huo na kuridhika pasipo mfano ndani ya yule aliye wema usio na mipaka.

**UPENDO WA MUNGU NA SILIKA YETU**

Je, tuliyoyasema yanawafaa hata wenye silika kali, ambao si rahisi kuhusiana nao? Tungeangukia uzushi wa Pelaji kama tungedhani upendo wa Mungu unagawiwa kadiri ya sifa na maelekeo ya umbile. Kumbe *"kila mmojawetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo"* (Ef 4:7). "Upendo upitao maumbile ambao Mungu kwa wema wake anatumiminia moyoni… unapatikana katika ncha ya juu ya roho… isiyotegemea maumbile yoyote… Hata hivyo ni kweli kwamba watu ambao kiumbile wanaelekea mapenzi, wakishatakaswa vizuri kutoka pendo kwa viumbe, wanafanya maajabu katika mapenzi matakatifu, kwa kuwa ndani mwao upendo una urahisi mkubwa wa kuenea popote. Ndiyo asili ya utamu wa kupendeza sana usiojitokeza katika wenye silika kali, chungu, ya huzunihuzuni na ambao ni vigumu kushirikiana nao. Lakini, ikiwa watu wawili, ambao kwa maumbile mmojawao anaelekea mapenzi na upole, na mwingine ukali na uchungu, wana kiwango kilekile cha upendo, bila ya shaka watampenda Mungu sawa, ingawa si kwa namna moja. Moyo mpole kiumbile utapenda kwa urahisi, upendevu na utamu mkubwa zaidi, ila si kwa imara na ukamilifu zaidi; kumbe upendo utakaoota kati ya miba na karaha ya umbile kali na kavu utakuwa wa kishujaa na mtukufu zaidi, kama vile wa kwanza ulivyo mzuri na wa kupendeza zaidi. Basi, si muhimu sana mtu kuelekea kupenda kiumbile tunaposema juu ya upendo upitao maumbile na ambao kwao tunatenda kwa namna ipitayo umbile tu. Lakini, ee Theotimo, ningependa kuwaambia watu wote: enyi watu wa kufa, mkiwa na moyo unaoelekea kupenda, mbona hamlengi upendo wa kimbingu na wa Kimungu? Ama mkiwa na moyo mkali na mgumu, enyi maskini, kwa kuwa mnakosa pendo la kiumbile, mbona hamlengi upendo upitao maumbile ambao mtajaliwa kwa upendo na yule anayewaita kitakatifu mumpende?" (Mt. Fransisko wa Sales).

**KULINGANA ZAIDI NA ZAIDI NA MATAKWA YA MUNGU YALIYO WAZI**

Upendo wa kulingana na matakwa ya Mungu ni sisi kutaka yale yote ambayo wema wake unatuonyesha una nia nayo. Unayaonyesha kwa njia ya amri, mashauri yanayolingana na wito wetu, na matukio. Ndiyo tunayoyazungumzia tukisema, Utakalo lifanyike. Basi, tuone tunavyopaswa kulingana nayo zaidi na zaidi. Kumpenda Mungu katika ustawi ni kwema, mradi tusipende ustawi sawa naye au kuliko yeye. Kwa vyovyote hicho ni kiwango cha chini, rahisi kwa wote. Kupenda matakwa ya Mungu unapokoma urahisi wa kutimiza wajibu, ni kiwango kamili zaidi, lakini tunapaswa kumuiga Yesu hata *kwa kumpenda Mungu katika mambo ya tabu na yasiyotarajiwa,* katika matatizo ya kila siku na dhiki ambazo maongozi yake yanaacha zitokee kwa ajili ya jambo jema zaidi. Hatuwezi kumpenda kweli tusipopenda dhiki hizo, si kwa zenyewe, bali kwa ajili ya mema ya Kiroho yanayotokana na uvumilivu wa kuzistahimili. Basi, kupenda mateso na machungu kwa ajili ya Mungu ndiyo kiwango cha juu cha upendo ambapo yanayotupata yanageuka kuwa mema.

Plato alisema pendo motomoto ni fukara, uchi, hoi, unahitaji daima, unalala nje mahali pagumu, kwa sababu unamfanya mtu aache vyote kwa yule anayempenda, unaondoa usingizi na kulenga muungano wa

ndani zaidi na zaidi. Hayo aliyoyasema kuhusu pendo la kimaumbile ni ya kweli zaidi kuhusu upendo wa Mungu unapochoma kwa ndani: "Hata saa hii ya sasa, tuna njaa na kiu, tu uchi, twapigwa ngumi, tena hatuna makao… Tumefanywa kama takataka za dunia" (1Kor 4:11,13). "Nani alimfikisha kwenye hali hiyo kama si upendo? Upendo ndio uliomtupa Mt. Fransisko wa Asizi uchi miguuni pa askofu wake na uliomfanya afe uchi ardhini; upendo ndio uliomfanya ombaomba maisha yake yote. Upendo ndio uliomtuma shujaa Fransisko Saveri akiwa fukara, mwenye shida, amevaa nguo zilizochanika, huko na huko kati ya Wahindi. Upendo ndio uliomfanya kadinali bora Mt. Karolo Borromeo, askofu mkuu wa Milano, afikie ufukara mkubwa hivi hata akaonekana kama mbwa nyumbani mwa bwana wake" (Mt. Fransisko wa Sales).

Upendo wa kulingana na matakwa ya Mungu ni kama moto ambao mwali wake ni mzuri na safi kadiri ulivyolishwa na kuni bora, kavu na zilizotakaswa. Kwa sababu hiyo pendo lolote lisilotokana na mateso ya Bwana ni la juujuu na la hatari. Kifo cha Yesu, tokeo kuu la upendo wake kwetu, ndiyo sababu hasa ya kumpenda. Hakuna kinachoridhisha kuliko upendo wake, kwa njia ya kuachana kikamilifu na vyote ili kuungana kwa ndani na matakwa ya Mungu.

Huo upendo wa kulingana na matakwa yake yaliyo wazi unatuwezesha kujiachilia kwa *matakwa ya Mungu yasiyo wazi bado,* ambayo yanaongoza ya kesho. Yaliyo wazi yanadai utiifu, na yasiyo wazi bado yanadai tujiachilie kwake kitoto kwa imani, tumaini na upendo. Azimio la "kushika uaminifu na kujiachilia" linaoanisha kutenda na kukubali kutendewa, likishinda utulivu wa kivivu na mahangaiko yasiyozaa kitu ya wanaojiamini bila ya kuwa na sala ya dhati. Kujiachilia kwa Mungu ndiyo njia ya kufuata; uaminifu wa kila nukta ndiyo hatua za kupigwa katika njia hiyo. Uaminifu katika mwanga wa amri unatuingiza katika fumbo lenye giza la matakwa ya Mungu kuhusu wokovu wetu.

Moyoni mwetu hatuna upendo ule wote tunaouhitaji: ndiyo sababu ni upumbavu kuutapanya ovyo kwa viumbe. Upendo wa Mungu unapoa kwa dhambi nyepesi (au kwa kuambatana nayo). Kinyume chake tendo karimu la upendo linatustahilisha ustawi wa adili hilo ambalo linayauhisha mengine yote na kufanya yastahili. Ustawi huo unatuandaa kumuona na kumpenda Mungu vizuri zaidi milele. Basi, tunachotoa ili kujipatia hazina hiyo isiyopimika tukione si kitu. Tunapompa Mungu upendo wetu, daima anatupatia wa kwake. Tena anatutangulia kwa kuwa hatuwezi kushinda umimi wetu pasipo neema yake tunayopaswa kujiombea mfululizo kama tunavyopumua.

Mungu anatamani tumpende kila siku zaidi. Hatutakiwi kamwe kusema tunampenda vya kutosha, bali tunapaswa kuendelea mfululizo katika upendo huo. Tunamuendea Mungu *kwa hatua za upendo,* yaani kwa matendo ya upendo yanayozidi kuwa makuu. Safarini tunaimba wimbo wa upendo, ule wa liturujia ulio sauti ya Bibi arusi wa Kristo. Si vibaya kutetemeka pengine mbele ya Mungu, lakini upendo unatakiwa kutawala. Tunapaswa kumcha Mungu kwa upendo wa kitoto, si kumpenda kwa hofu ya kitumwa; ndiyo sababu uchaji unaoogopa dhambi unastawi pamoja na upendo, kumbe hofu ya adhabu inazidi kupungua.

Huo upendo unastawi kwa kubeba msalaba: "Moyo wenye bidii zaidi unajilisha misalaba na mateso; kumbe waoga wanaridhishwa na mafanikio yao tu. Zaidi ya hayo *upendo safi* wa Mungu unatekelezwa kwa urahisi mkubwa katika mapingamizi kuliko katika raha, kwa sababu tabu haina lolote la kuvutia ndani mwake, isipokuwa mkono wa Mungu unaoituma… wakati mafanikio yanayo yenyewe vivutio vinavyonasa hisi" (Mt. Fransisko wa Sales). Upendo wa kulingana na matakwa ya Mungu ukistawi unafanya mateso unayojilisha yawe matamu; hapo unasonga mbele kwa hakika.

Upendo huo unastawi kila tunapofisha umimi wetu. Ili tuwe na hamu motomoto ya upendo wa Mungu tunapaswa kukomesha yale yote usiyoweza kuyahuisha. Hapo unayafanya maadili yampendeze kuliko yanavyompendeza kwa yenyewe kwa kuwa stahili ya matendo maadilifu inategemea kiwango cha upendo. Kwa hiyo, kutimiza wajibu wetu kunaweza kutakaswa hivi kwamba hata dakika moja isipotee milele. Ikiwa tuliwahi kuwa na upendo mkubwa halafu hatujatenda dhambi yoyote ya mauti, ila tumepoa kwa kuambatana na dhambi nyepesi, tunayo bado hazina hiyo, ingawa uwezo wake wa kuenea umepungua, kama ilivyo kwa mwanga katika chemni chafu. La muhimu ni kuondoa moshi upesi. Kiutekelezaji, tuone tunavyoweza kuweka mapendo yetu yoyote chini ya upendo wa Mungu: "Naweza kupinga hamu ya utajiri na tamaa za kidunia ama kwa kuvidharau vinavyostahili, ama kwa kutamani yasiyokwisha; kwa njia hiyo ya pili pendo la kihisi na la kidunia litaangamizwa na upendo wa kimbingu… Hivyo upendo wa Mungu unashika nafasi ya mapendo na maono na kuyatiisha" (Mt. Fransisko wa Sales).

Huo upendo wa kulingana na matakwa ya Mungu unafikisha kwenye upendo wa kufurahia yale yote yanayochangia utukufu wa Mungu, pamoja na wazo la kuwa hekima na heri zake hazina mwisho, la kuwa ulimwengu wote unadhihirisha wema wake, na la kuwa wateule watamtukuza milele. Tunaweza tukahisi upendo huo wa kufurahia hayo kwa uvuvio maalumu wa Mungu*,* wakati upendo wa kulingana na matakwa yake unaweza kuwepo kwa neema ya msaada ya kawaida.

## 3.20. *UPENDO WA KIDUGU, MNG'AO WA ULE WA MUNGU*

Kumpenda jirani ni tokeo la lazima na ishara ya upendo kwa Mungu: "Mtu akisema, 'Nampenda Mungu', naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo" (1Yoh 4:20). Kwenye hatua ya mwanga upendo wa kidugu ni moja kati ya dalili kuu za maendeleo yanayotakiwa kupatikana. Ni muhimu tusisitize sababu hasa ya

kuutekeleza, tusije tukauchanganya na mengineyo, k.mf. upendevu, tabia ya kijamii au urahisi wa kuruhusuruhusu lolote; urahisi huo unaonekana kufanana na upendo, lakini unatofautiana na adili hilo la kumiminiwa kwa kuwa unapuuzia imani na ukweli, kumbe upendo unavidai kama msingi wake. Ili tuwe na mtazamo sahihi tufikirie upendo wa Yesu kwetu.

**UPENDO WETU KWA MUNGU UNATAKIWA KUENEA KWA JIRANI**

Upendo wa kidugu ambao Bwana anadai tuwe nao unatofautiana na elekeo la kibinadamu la kutenda mema ili kupendeza, na lile la kuwapenda wanaotutendea mema, kuwachukia wanaotutenda mabaya na kutojali wengine wote. Pendo la kimaumbile linatufanya tumpende jirani kwa sifa njema za umbile lake na kwa misaada anayotupatia. Kumbe upendo wa Kikristo ni wa juu: "Mmesikia kwamba imenenwa: Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia: Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu wa mbinguni… Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi, mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je, nao hawafanyi yayo hayo?" (Math 5:43-46). Tunapaswa kuwapenda maadui kwa upendo uleule tulionao kwa Mungu, kwa sababu hakuna maadili mawili ya upendo, moja kwa Mungu na lingine kwa jirani, bali ni moja tu linaloelekea kwanza kwa Mungu, anayependwa kuliko yote, halafu kwetu wenyewe na kwa jirani.

Inawezekanaje kuwapenda Kimungu watu wenye kasoro kama sisi? Jibu rahisi ni kwamba anayempenda rafiki yake, anawapenda pia watoto wa rafiki na kuwatakia kila la heri kutokana na upendo kwa baba yao. Kwa ajili yake ataharakisha kuwasaidia na atakuwa tayari kuwasamehe wakimkosea. Basi, kwa kuwa watu wote *ni wana wa Mungu* kwa neema, au walau *wanaitwa kuwa hivyo,* tunapaswa kuwapenda kwa upendo upitao maumbile na kuwatakia heri ya milele kama tunavyojitakia: tunatakiwa kuelekea lengo hilo wote sawia kwa msaada wa neema na kwa kuishi upendo uleule.

Hivyo upendo ni kiungo cha ukamilifu kinachotuunganisha ipasavyo na Mungu na jirani yeyote: unatufanya tumpende Mungu ndani ya binadamu na binadamu ndani ya Mungu. Upendo huo ni wa nadra kwa kuwa wengi wanajitafutia faida hasa na kuelewa kwa urahisi zaidi usemi ufuatao: "Jeraha kwa jeraha, jicho kwa jicho, jino kwa jino" (Law 24:20). Kabla ya Yesu amri ya upendo wa kidugu ilikuwa inatekelezwa kidogo tu, hata ikampasa kuisisitiza toka hotuba ya kwanza mlimani hadi maneno yake ya buriani. Mitume wakafanya vilevile katika barua zao.

Ili tumpende Kimungu jirani yetu tunapaswa *kumtazama kwa imani* na kujiambia, "Mtu huyu, mwenye tabia tofauti na ya kwangu, *amezaliwa na Mungu* au anaitwa kuzaliwa naye na kushiriki uhai na heri ya Mungu sawa nami". Mbele ya Wakristo wasiotupendeza tujiambie, "Pamoja na yote, huyu ni kiungo cha mwili wa Kristo, pengine jirani na moyo wake; ni jiwe hai ambalo Mungu analichonga ili kuliweka mahali pake katika Yerusalemu ya mbinguni. Niwezeje kutompenda nikimpenda Mungu, Baba yetu sote? Nisipompenda, upendo wangu kwa Mungu ni uongo tu; kumbe nikimpenda ni dalili ya kuwa nampenda Mungu".

Pengine mafundisho hayo yanapingwa kwa kusema, "Je, ndiyo namna ya kumpenda mtu kweli, au ni kumpenda Mungu tu ndani ya binadamu, kama tunavyopenda almasi katika sanduku lake?" Hakika, mtu anataka kupendwa kwa ajili yake mwenyewe, lakini kwa msingi huo hawezi kupendwa Kimungu. Tena upendo haumpendi Mungu tu ndani ya binadamu, bali unampenda *mtu ndani ya Mungu na kwa ajili ya Mungu.* Unampenda kweli jinsi *anavyotakiwa kuwa,* kiungo cha milele cha mwili wa Kristo, nao unafanya yote unayoyaweza ili afike mbinguni. Unampenda vilevile jinsi *alivyo kwa neema,* na asipokuwa nayo, unapenda umbile lake, si kadiri lilivyo kisha kuanguka na kuvurugika, bali kadiri lilivyo sura ya Mungu lenye uwezo wa kupandikiziwa neema ili kuwa mfano wake.

**UFANISI WA UPENDO HUO WA KIMUNGU**

Tukimpenda jirani ndani ya Mungu na kwa ajili ya Mungu, tunampenda zaidi na kwa ukamilifu mkubwa zaidi. Hatupendi kasoro zake, ila tunazivumilia; ndani yake tunapenda yale yote yaliyo bora, yanayokusudiwa kustawi na kuchanua katika uzima wa milele. Badala ya kuwa upendo usio na matendo, unatuelekeza kumtazama jirani yeyote kwa haki, kumkubalia matakwa yake kadiri yasivyopingana na amri za Mungu, kukwepa migogoro au kuitatua mapema. Wema huo unang'aa na kutufanya tupende mfululizo si yaliyo mema kwetu tu, bali yaliyo mema kwake kwa mtazamo wa Mungu, tumtakie mema yasiyopita kamwe, hasa kumpata moja kwa moja yeye, aliye wema mkuu.

**UPANA NA UTARATIBU WA UPENDO**

Kwa hiyo, upendo wetu unatakiwa kuwaelekea bila ya mipaka wala ubaguzi *wote* duniani, toharani na mbinguni na kusimama mlangoni pa moto wa milele tu. Walaaniwa tu hatuwezi kuwapenda kwa kuwa hawawezi tena kuwa wana wa Mungu: wanamchukia milele, hawamuombi msamaha wala neema ya toba; hawana nia ya kuongoka hata chembe. Pamoja na hayo, wanafaidi huruma ya Mungu kwa kuadhibiwa kidogo kuliko wanavyostahili; jambo hilo linapendeza upendo wetu ambao kwa namna hiyo unafikia huko pia. Tusipokuwa na hakika kuhusu laana ya milele ya malaika au mtu fulani, tunadaiwa kumpenda kila mmoja.

Ili upendo uwaenee wote si lazima uwe sawa kwa wote; ustawi wake katika hatua ya mwanga unazidi

kuonyesha *utaratibu wa upendo* ambao unaheshimu na kuinua vizuri ule wa maumbile. Hivyo tunapaswa kumpenda Mungu kuliko yote, halafu roho yetu, halafu ile ya jirani, hatimaye mwili wetu ambao tuwe tayari kuutoa kwa wokovu wa roho yoyote, hasa tukiwa na majukumu kwake (k.mf. kama wachungaji wa jimbo au wa parokia). Kadiri upendo unavyostawi ndani mwetu, tunaelewa tunavyopaswa kupenda zaidi kitathmini *walio bora, karibu zaidi na Mungu,* ingawa tunaelekea kupenda zaidi kihisi *walio karibu nasi* (kwa vifungo vya damu, jamii, wito au urafiki).

Mpangilio huo tunaozidi kuutambua unatuonyesha kuwa Mungu anataka kutawala mioyo yetu, pasipo kuzuia mapendo halali ambayo upendo wake unakuja kuyahuisha, kuyainua, kuyatakasa na kuyaongezea ukarimu. *Ustawi wa upendo unafuta "usisi",* yaani tabia ya kujikuza kama kundi kwa kupuuzia wengine. "Kwa hali na ahadi siwezi kuwa wa mashirika mbalimbali, lakini kwa elekeo la upendo mimi ni wa yote… Nakiri kwa unyofu kwamba nilihuzunika sana kila nilipoona nyumba za kitawa kuoneana wivu… Je, damu iliyowapatia watawa wowote mema yote waliyonayo, si ile ya Yesu Kristo? Au ni ile ya Mt. Augustino, ya Mt. Benedikto au ya Mt. Bernardo? Mungu wangu! Dumisha imara uelewano kati ya watumishi wako… Mashirika mbalimbali ya kitawa ni miili tofauti, lakini yanatakiwa kuwa moyo mmoja, roho moja tu kama tunavyosoma kuhusu Wakristo wa kwanza" (L. wa Ballon). La sivyo tunarudia ule ufinyu wa mawazo alioulaumu Mt. Paulo, "Maana hapo mtu mmoja asemapo, 'Mimi ni wa Paulo', na mwingine, 'Mimi ni wa Apolo', je, ninyi si wanadamu? Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye" (1Kor 3:4-7). "Je, Kristo amegawanyika? Je, Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je, mlibatizwa kwa jina la Paulo?" (1Kor 1:13). "Basi, mtu yeyote asijisifie wanadamu. Kwa maana vyote ni vyenu; kwamba ni Paulo, au Apolo, au Kefa; au dunia, au uzima, au mauti; au vile vilivyopo sasa, au vile vitakavyokuwapo; *vyote ni vyenu; nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu*" (1Kor 3:21-23).

Huo utaratibu wa upendo unatakiwa uzidi kuonekana ndani ya anayeendelea: kwa namna fulani moyo wake unapaswa kupanuka kama ule wa Mungu kutokana na ustawi wa upendo ambao ni kushiriki uhai wa Mungu, upendo wa milele. Upendo huo unatakiwa kuwa si wa ndani tu, bali wa vitendo, kama vile Yesu alivyotupenda hadi kufa msalabani, na kama watakatifu wengi walivyowapenda wenzao hadi kuwapa ushahidi wa damu. Ndio upendo wa kidugu ulio uenezi wa ule wa Mungu.

**TUENDELEEJE KATIKA UPENDO HUO WA KIDUGU?**

Nafasi za kuuvunja ziko nyingi hata katika mazingira bora, kwanza kutokana na kasoro za hawa na hawa ambao hawajafikia ukamilifu hata wakiulenga. Kila mmoja wetu ni kama piramidi isiyo na kilele: mara nyingi tunamuona jirani kuwa hivyo lakini tunasahau kwamba yeye pia anatuona hivyo. Tunatazama "kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu" yetu, tusione "boriti iliyo ndani ya jicho" letu wenyewe (Math 7:3).

Hata kama kasoro zote zingekoma kabla ya kuingia mbinguni, nafasi za kubishana na kukwaruzana zingedumu kutokana na tofauti za tabia, maelekeo, akili na malezi, halafu uchovu na shetani. Huyo anapenda kufitini hasa katika mazingira bora ili azuie mema mengi yanayoweza kufanyika huko, kuliko katika yale anayoyatawala tayari kwa mawazo mapotovu yaliyoenea na mifano mibaya inayotolewa. Tunavyosoma katika Injili na katika maisha ya watakatifu, adui anasia magugu kwenye ngano bora naye anaweka lenzi katika ubunifu wa waadilifu waone chembe kuwa ni mlima.

Maongozi ya Mungu yanawaachia kwa makusudi nafasi nyingi za kujinyenyekeza na kutimiza upendo wa kidugu kati yao. Katika udhaifu ndipo neema ya Mungu inapoonyesha nguvu yake, na ndipo uadilifu wetu unapokamilika; udhaifu wetu unatunyenyekesha na ule wa wenzetu unatuzoesha. Mbinguni tu nafasi zote za kubishana zitakoma, kwa kuwa wenye heri wanaona ndani ya Mungu yale yote wanayotakiwa kuyawaza, kuyataka na kuyatenda. Hapa duniani watakatifu wenyewe wanaweza wakashindana, na kwa muda fulani hakuna aliye tayari kukubali mtazamo wa mwingine kwa sababu dhamiri inamdai ashike msimamo asiweze kuachana na wajibu wake, isipokuwa kujinyima haki tu. Kwa mfano watakatifu Karolo Borromeo na Filipo Neri hawakuelewana kuhusu kuanzisha shirika moja; hakika Bwana alitaka yaanzishwe mawili.

Kati ya matatizo mengi hivyo, upendo wa kidugu unatakiwa kustawi namna mbili: kwa kumtazama jirani kwa wema kadiri ya imani, halafu kwa kumtendea mema mbalimbali.

Kwanza *tumtazame jirani kwa imani,* si kwa macho au akili vilivyoathiriwa na umimi. Ni lazima tujikane ili kutambua uhai wa Kimungu chini ya sura duni ya wengine. Mara nyingi kinachotuchukiza kwa jirani si makosa makubwa dhidi ya Mungu, bali kasoro za silika aliyo nayo ingawa ni mwadilifu kweli. Pengine tuko tayari kuvumilia walio mbali na Mungu lakini wanapendeza kiumbile, kumbe wengine waliopiga hatua katika ukamilifu ni zoezi kubwa la subira kwetu. Basi tuamue kuwatazama wote kwa imani ili kutambua ndani mwao kile kinachompendeza Mungu na ambacho sisi pia tunapaswa kukipenda.

Kinachopingana zaidi na mtazamo huo wa wema ni *hukumu isiyo na msingi wa kutosha.* "Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa" (Math 7:1-2). Si kushuku tu, bali kuhukumu kwa kutegemea dalili ndogo; tunaona mbili na kudai ni nne, kwa sababu ya kiburi chetu. Ni dhambi ya mauti dhidi ya haki

kumhukumu jirani kwamba ametenda dhambi ya mauti, hasa kukitolewa nje kwa maneno au matendo. Kwa kuwa jirani, pamoja na haki ya kutimiza wajibu wake, anayo ile ya kuwa na sifa njema, nayo ni muhimu kuliko ile ya kumiliki vitu. Tuheshimu haki yao tukitaka ya kwetu iheshimiwe. Kwa hiyo *tutafsiri kwa wema* mkubwa iwezekanavyo mambo yasiyo na hakika. Tusipoweza kuondoa shaka, tunaweza kujihadhari naye asije akatudanganya, lakini tusitoe hukumu imara kwa dalili ndogo: mara nyingi hukumu zisizo na msingi wa kutosha ni za uongo. Tuhukumuje kwa hakika nia za mtu ambaye hatujui shaka, makosa, shida, vishawishi, hamu na majuto yake? Tuhukumuje tusipokuwa na faili za kesi?

Hata kama hukumu ni za kweli zinabaki kuwa kinyume cha haki kwa sababu tunatumia mamlaka isiyo yetu. Kanisa lenyewe *halihukumu undani* wa mtu. Zaidi tena, hukumu hizo ni kinyume cha upendo, zinatokana na ubaya katika kumtazama mtu, ingawa mara nyingi zinatamkwa chini ya kinyago cha wema. Hatufuati huruma bali umimi na kiburi, na tunamwekea sheria Roho Mtakatifu kwa kutaka njia ya kufuatwa iwe ile ya kwetu tu. Badala ya kumuona jirani kuwa ndugu, tunamuona ni mgeni au adui ambaye aondoshwe au kushushwa. Ndicho kinachozuia sala ya kumiminiwa kama ushungi unaofunika macho ya roho. Tusipofika mbali hivyo, inatutokea pengine kuhukumu undani wa mtu ili kujidai tunasoma mioyo; kumbe Mungu tu anaiona wazi. Tuangalie kwamba tunapohukumu hatutabiri kuwa baada ya kitambo tutatumbukia kosa kubwa kuliko lile tunalowalaumu wenzetu.

Uovu ukiwa wazi, Mungu hadai tusiuone, ila anatukataza tusisengenye kwa kiburi. Pengine anatuagiza, kwa msingi wa upendo, *ukosoaji wa kidugu* ambao ufanywe kwa wema, unyenyekevu, upole na busara kadiri ya Injili: "Ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu: akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru" (Math 18:15-17). Tufikirie kwanza kama utafaa na kama kuna tumaini la mtu kutubu, au kama ni lazima tumuarifu mkubwa wake. Tendo kamili ni kumhurumia mkosefu kwa kubeba kosa lake mbele ya Mungu, kama vile Bwana alivyobeba msalabani dhambi zetu zote. Je, hakutuambia, "mpendane, kama nilivyowapenda ninyi" (Yoh 15:12)?

Kisha kumtazama jirani kwa wema, tumpende kwa vitendo, kwa kuvumilia kasoro zake, kumrudishia mema kwa mabaya, kuepa kijicho, kuomba umoja wa mioyo. Tunaweza *kuvumilia* kasoro za watu tukizingatia kuwa mara nyingi kinachotusumbua kwao si dhambi ya mauti bali silika (k.mf. hasirahasira au utulivu mkubwa mno), ufinyu wa mawazo, kimbelembele n.k. Hata kama wana kosa kubwa, tusidhani tumekamilika tukiwasema kama Farisayo hekaluni. Tukumbuke Mungu haachi mabaya yatokee isipokuwa kwa ajili ya mema makubwa zaidi, tofauti na sisi tusioweza kusababisha mema isipokuwa kwa njia ya mema. Kukwazwa na maovu na kupatwa na ari chungu kulifanya marekebisho kadhaa ya utawa yasizae matunda. Tuseme ukweli kwa kiasi na wema, si kumtupia mtu usoni kwa dharau. Tunapaswa vilevile kutumia busara tusiseme juu ya makosa ya jirani bila ya sababu ya kutosha, la sivyo tunasengenya na hata kusingizia.

Injili inatufundisha pia kurudisha *mema kwa mabaya,* kwa njia ya sala, mifano mizuri na kusaidiana. Namna mojawapo ya kujipatia fadhili za Mt. Teresa wa Yesu ilikuwa kumtaabisha, kwa kuwa alifuata shauri la Bwana: "Mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia" (Math 5:40). Kwa sababu si muhimu kutetea haki zako za kidunia bali kumuokoa ndugu yako apate uzima wa milele. Kumuombea jirani wakati wa kuteseka kwa ajili yake kuna nguvu za pekee, kama kwa Yesu alipowaombea watesi wake na kwa Mt. Stefano alipopigwa mawe.

Tunapaswa pia kukwepa *kijicho,* tukifurahia sifa walizojaliwa wenzetu. "Mguu ukisema, 'Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili'; je, si wa mwili kwa sababu hiyo? Na sikio likisema, 'Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili'; je, si la mwili kwa sababu hiyo? Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio, ku wapi kunusa? Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja. Na jicho haliwezi kuuambia mkono, 'Sina haja na wewe'; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, 'Sina haja na ninyi'… bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho. Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake" (1Kor 12:15-21,25-27). Tutimize upendo hasa kwa wadogo wetu kwa kuwa ni dhaifu zaidi, na kwa wakubwa wetu waliobeba mzigo mkubwa zaidi. Tusiangalie kasoro zao: pengine mahali pao tungekuwa nazo nyingi zaidi. Kinyume chake tuwasaidie iwezekanavyo, kwa busara na kama kwa kutojitokeza.

Hatimaye tuombe *umoja wa roho na mioyo,* alivyofanya Bwana: "Utukufu ule ulionipa nimewapa wao, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja" (Yoh 17:22). Katika Kanisa la mwanzoni "jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika" (Mdo 4:32). Baadaye, lilipoenea duniani kote, halikuweza kudumisha hali hiyo kati ya viungo vyote, lakini mashirika ya kitawa na vyama vya Kikristo vinatakiwa kukumbusha huo umoja wa asili. Mahali ambapo vitu vya nje na vipindi vya sala ni vya pamoja, ni lazima uwepo umoja wa ndani, la sivyo vingekuwa uongo kwa Mungu, kwa watu na kwetu sisi. Umoja wa

mioyo unachangia kulipamba Kanisa kwa sifa angavu ya utakatifu. Ukikusanya viungo mbalimbali vya mwili wa Mwokozi unathibitisha kuwa Neno alifanyika mwili akakaa kwetu ili atuunganishe na kutupa uzima: “Wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi” (Yoh 17:23).

## 3.21. *ARI KWA UTUKUFU WA MUNGU NA KWA WOKOVU WA WATU*

Ili tuelewe upendo unavyotakiwa kuwa kwa kawaida kwenye hatua ya mwanga, ni lazima tuseme juu ya ari inayompasa hasa mtu aliyewekwa wakfu kwa Mungu. Ari kwa utukufu wake na kwa wokovu wa watu ni ari moja, ni umotomoto wa upendo uleule unaotakiwa kuwepo hata katika ukavu na majaribu ya kila aina; pengine huo umotomoto wa utashi una juhudi na stahili kadiri tusivyouhisi.

**SABABU ZA ARI HIYO**

Sababu ya kwanza ni kwamba *Mungu anastahili kupendwa kuliko yote:* amri kuu isiyo na mipaka inatudai tukue daima katika upendo. Amri hiyo ilitolewa tayari katika Agano la Kale kwa maneno yaleyale ambayo Yesu akaja kuyatumia. Manabii pia walikuwa na ari ya kuikumbusha mfululizo itimizwe na taifa la Mungu, hasa Eliya, nabii wa moto. “Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana, Mungu wa majeshi, kwa kuwa wana wa Israeli wameacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga, nami nimesalia, mimi peke yangu: nao wanitafuta roho yangu waiondoe” (1Fal 19:14). “Wivu wa nyumba yako umenila” (Zab 69:9). “Juhudi yangu imeniangamiza” (Zab 119:139). “Finehasi, baba yetu, kwa sababu alikuwa na juhudi nyingi, alipewa ahadi ya ukuhani wa milele… Eliya, kwa kuwa aliona wivu mwingi kwa ajili ya sheria, alichukuliwa juu mbinguni… Basi, ninyi, wanangu, mwe hodari, mfanye kwa kiume kwa ajili ya sheria, maana kwa hiyo mtatukuzwa” (1Mak 2:54,58,64). Ari hiyohiyo ilimfanya Yesu afukuze wafanyabiashara hekaluni na kupindua meza zao. Ari hiyohiyo inadumu hata leo katika Kanisa popote pale unapotolewa ushuhuda wa damu na katika maisha ya wengi waliowekwa wakfu kama sadaka ya kuteketezwa.

Sababu ya pili ni kwamba tunapaswa *kumuiga Bwana wetu Yesu Kristo,* aliyewaka upendo: “Nimekuja kutupa moto duniani: na ukiwa umekwishawashwa, ni nini nitakalo zaidi?” (Lk 12:49). Tangu atwae mwili alijitoa mfululizo katika maisha yaliyofichika, akituonyesha namna ya kujiandaa kwa unyenyekevu na kwa kujikana tufanye kazi za Mungu. Toka mwanzo wa utume wake akaonja uchungu uliolingana tu na upendo wake: uchungu wa upendo wenye ari unaotaka kujitoa, kumbe unakuta hali ya kutojali, kutobadilika, kutoelewa, ubaya na upinzani wenye chuki. Ari ndiyo iliyosababisha uchungu wake mbele ya dhambi za watu, na uchungu wa Maria chini ya msalaba. Maisha yake yote Yesu aliteseka moyoni, akitamani kutimiza ukombozi wetu: “Nina ubatizo unipasao kubatizwa, nami nina dhiki kama nini hata utimizwe!” (Lk 12:50). “Nimetamani sana kula Pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu” (Lk 22:15). Uchungu wake ulikoma alipokufa msalabani, lakini kiu ya wokovu wetu anayo hadi sasa: “Maana yu hai sikuzote ili awaombee” (Eb 7:25) hasa katika sadaka ya misa. “Ningependa kukuona unateswa sana na njaa ya wokovu wa watu hadi ufe kwayo, kama alivyofanya Yesu Kristo. Walau ikufanye ufie ulimwengu na kujifisha” (Mt. Katerina wa Siena).

Sababu ya tatu ni *thamani ya watu* wenye roho isiyokufa, waliokombolewa kwa damu ya Yesu Kristo. Kila mmojawao ni bora kuliko ulimwengu wote na anaitwa kufaidi uzima wa milele. Baada ya mitume, wafiadini walikuwa na ari kiasi kwamba ni thibitisho lisilopingika la utakatifu wa Kanisa. Tukiipenda nchi yetu hata kujitoa mhanga kwa ajili yake, zaidi tunapaswa kulipenda Kanisa linalotuongoza kwenda kwetu, ambako waadilifu wa mataifa yote watakusanyika pamoja milele. Vilevile tuwe na ari ya kuziombea roho za toharani.

Hatimaye sababu ya nne ni *juhudi za maadui* wa Kanisa katika kueneza fujo, upotovu na mauti. Vituondoe usingizini vita vya kishetani dhidi ya Bwana na ya mama yetu Kanisa, vita vikali kuliko vyote kwa kuwa ni vya roho, vinafikia mioyo ya watoto ili wawe waovu wasioishi kwa Mungu. Sawa na dhambi za roho, uovu wa vita hivyo hausemeki na majukumu yake ni ya kutisha. Kanisa linaona hasa madhara kwa wale wanaovipiga, na linaendelea kuwaombea Mungu awafumbue macho na kuwazuia wasifuate hata mwisho njia ya laana ya milele ambako wanavuta wengine wengi.

**ARI YETU IWE NA SIFA GANI?**

Jina lenyewe linasema kuwa ari inatakiwa iwe motomoto kwa kuwa ni mwako wa upendo. Lakini ni umotomoto wa Kiroho wenye kudumu, si ule wa kihisi ambao unatokana na silika na kujitokeza katika utendaji wa kibinadamu tu, unaolenga kujiridhisha na kujipatia sifa hata kukinaisha watu. Ili umotomoto udumu upande wa roho unatakiwa uwe na mwanga, subira, upolena usijitafutie faida.

Kwanza iwe *imeangazwa* na imani, utiifu, busara ya Kikristo na vipaji vya hekima na shauri. Mwanga wa akili hautoshi, kwa sababu kazi ya kufanywa si ya kibinadamu, bali ya Kimungu na inatakiwa kufuata njia alizotuelezeka Bwana. Umotomoto wa umbile tu, badala ya kuongoza watu kwa Mungu, polepole unaongozwa na ulimwengu na udanganyifu wake. Umotomoto huo wa wasiotulia, wavurugaji na wapendavyeo unasukumwa na matumbo, hauna busara, haujali nafasi, tena unasahau njia za lazima zipitazo

maumbile, hasa sala na toba. Kumbe, hasa katika nafasi ngumu ari inatakiwa kumuomba Roho Mtakatifu mwanga ili itimize vizuri iwezekanavyo si mambo ya ajabu bali yale ya kawaida yaliyopangwa na Kanisa na viongozi: kuadhimisha au kushiriki misa, kuwa waaminifu kwa sala inayotupasa na kwa wajibu mwingine wowote. Tusipokuwa na mwanga huo sifa zetu haziwezi kutosha, kwa kuwa pengine tunadaiwa utiifu wa kishujaa.

Halafu *iwe na subira na utamu,* iepe kukasirikia bure maovu na kukaripia ovyo, ivumilie mabaya kadhaa ili kuepa mengine makubwa zaidi na isigeuke kuwa kali na chungu. Haitakiwi kukomesha yaliyo mema kiasi kana kwamba ni mabaya, wala kuzima "utambi utokao moshi" wala kuvunja "mwanzi uliopondeka" (Math 12:20). Tukumbuke daima kuwa maongozi ya Mungu yanaacha mabaya yatokee ili yapatikane mema makubwa zaidi ambayo hatuyaoni bado, lakini yatang'aa milele.

Ili ari iwe na subira na upole*haitakiwi kujitafutia faida,* yaani kujitwalia yaliyo ya Mungu na ya watu. Baadhi wana ari kwa kazi za Mungu, lakini wanaziona kama ni za kwao: wanajifanya lengo lake bila ya kujitambua. Watakapopunguza kujiamini na kujiona wa maana, watakaponyenyekea na kutulia zaidi, Mungu atawatumia kama vyombo visivyozuia kazi yake, nao watajiachia mikononi mwake ambaye pekee anajua yanayohitajika ili kuzaa upya watu. Mara nyingi tunataka kutenda mema, lakini tunatamani mno tuyatende wenyewe na kwa namna yetu, hata tukazuia wengine wasiyafanye wala kufaulu kuliko sisi. Tusiwaonee kijicho kwa mafanikio yao, wala kushughulikia uongozi wa roho tusizokabidhiwa; tukiziondoa kwenye mvuto wa kufaa, Mungu atatudai. Pengine anatukosoa kwa njia ya majaribu yanayoumiza kiburi chetu tusitake tena kutenda kazi *yetu.* Baada ya kushinda umimi wetu, atatutumia kwa kazi *yake* ya wokovu. Hapo umotomoto wa Kiroho utakuwa mtulivu, mnyenyekevu na mpole, kama ule wa bikira Maria na wa watakatifu wengine, tena hautakuwa na la kuushinda: "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" (Rom 8:31).

Ari hiyo itekelezwe kwa namna mbalimbali za utume: *mafundisho ya Kikristo*, *matendo ya huruma* upande wa roho na wa mwili, *sala* (inayovuta neema izalishe kazi katika shamba la Bwana, hivyo ni roho ya utume wa nje, ingawa imefichika kadiri ilivyo ya dhati), na hatimaye *malipizi* (ambayo pia yamefichika; ni mwendelezo wa mateso ya Yesu katika mwili wake, ambamo kiungo kimoja kikiteseka kwa upendo, kingine kinapona; kimoja kikijikatalia matakwa yake, kingine kinaongoka na kufufuka).

Basi, katika njia ya utakatifu ari inatakiwa kuwepo, ingawa mara nyingi haipo. Ili idumu inahitaji kulishwa na sala ya dhati na kama ya kudumu katika usikivu kamili. Tuzungumzie basi, usikivu huo na sala hiyo ya wanaoendelea iliyosababisha hatua yao iitwe ya mwanga kwa kuwa roho inazidi kuangazwa na Mungu. Yale yote tuliyoyasema kuhusu ustawi wa maadili yanatuongoza kusema juu ya chemchemi za maendeleo hayo na za urafiki wa ndani na Mungu.

## 3.22. ***USIKIVU KWA ROHO MTAKATIFU***

Roho Mtakatifu, kupitia vipaji vyake tulivyovifafanua, ndiye asili ya maisha yetu ya sala na ya utendaji. "Vipaji saba *vinafungamana na upendo*; kwa hiyo, sawa na maadili ya kumiminiwa, *vinakua pamoja na upendo*, kama viungo vya mwili mmoja, au kama vidole vitano vya mkono mmoja" (Mt. Thoma wa Akwino) au kama mabawa yanayokua pamoja na ndege. Lakini marudio ya dhambi nyepesi yanavifunga, hata tukaja kupima mambo kwa aina ya upofu iliyo kinyume cha sala ya kumiminiwa.

### MIONGOZO YA ROHO MTAKATIFU

Uvuvio wake maalumu, ambao vipaji vinatuandaa kuupokea, ni tofauti na neema ya msaada ya kawaida inayotusukuma kutekeleza maadili. *Neema inayotusaidia kutenda,* ambayo tunatenda toka ndani, ni tofauti na *neema inayotenda,* ambayo tunatenda kwa kukubali tu msukumo wa Roho Mtakatifu. Katika ile ya kwanza utendaji wetu unazidi, kumbe katika ile ya pili utendaji wake ndani mwetu ndio unaozidi.

Usikivu kwa Roho Mtakatifu unafanana na ule wa mtiifu kamili anayepokea mara kwa hiari na stahili agizo la kiongozi wake, bila ya kufikiria na kuamua kwanza afanye nini. Kiongozi anatenda kwa njia yake, ila mwenyewe ana stahili za utiifu, unaozidisha nguvu zake, kwa kuwa akitii hadanganyiki wala hakataliwi neema anazohitaji atekeleze agizo.

Kwa uvuvio huo inatokea pia kwamba vipaji vinatumika pamoja na kazi ya maadili kufanyika: hapo ni kama upepo mzuri unaorahisisha kazi ngumu ya wapigakasia. Kwa mfano, uvuvio unaweza ukatukumbusha Injili wakati akili yetu inapofikiria la kufanya; kumbe pengine busara inajitambua haiwezi kutatua tatizo kubwa la dhamiri, hivyo inatuongoza kumuomba Roho Mtakatifu ambaye uvuvio wake unatufanya tuone na kutenda yanayofaa. Basi, tunapaswa kuwa wasikivu zaidi na zaidi kwake.

### MPANGILIO WA VIPAJI KUANZIA CHINI

Aina za uvuvio ni mbalimbali, tunavyoona katika orodha ya Isaya (taz. 11:2-3) ambamo vipaji vimepangwa kuanzia juu, yaani kuanzia kile cha hekima kinachoongoza vingine vyote. Wimbo huo wa zamani uliojaa utamu unafanana na noti saba za muziki zilizopangwa vizuri.

*Kipaji cha uchaji* ni cha kwanza kudhihirisha athari ya Roho Mtakatifu kwa mtu aliyeongoka. Kinafidia upungufu wa adili la kiasi na kumsaidia apambane na mivuto ya anasa na ya moyo. Uchaji huo mtakatifu ni

kinyume cha kuogopa watu, tena ni bora kuliko hofu ya kitumwa inayomsaidia mkosefu atubu kwa kuogopa adhabu za Mungu. Kipaji cha uchaji kinaogopa dhambi kuliko adhabu zake. Pengine mtu anauhisi kwa nguvu isiyoweza kusababishwa na tafakuri wala somo lolote, isipokuwa na Roho Mtakatifu ndani mwake. Mbinguni watakatifu hawaogopi tena kumchukiza Mungu, ila wanatetemeka pamoja na malaika wakiuheshimu ukuu wake; hata katika roho ya Yesu hisi hiyo ilikuwemo na bado imo. Uchaji huo, uliosababisha malipizi makubwa ya watakatifu, unahusiana na heri ya maskini ambao kwa kumcha Mungu wanabandukana na anasa na heshima za dunia.

Kwa namna fulani uchaji una elekeo hasi maana unatufanya tukwepe dhambi; lakini mtu anahitaji kumuelekea zaidi Mungu kama mwana. *Kipaji cha ibada* ndicho kinachotutia upendo wa namna hiyo kwa Baba wa mbinguni, halafu kwa Yesu, bikira Maria na watakatifu wanaotulinda. Kipaji hicho kinafidia upungufu wa adili la ibada linalompatia Mungu heshima inayotakiwa. Hakuna juhudi ya Kiroho inayodumu pasipo kipaji hicho kinachotuzuia tusiishie faraja za kihisi katika sala, bali tufaidike na huzuni na ukavu vinavyokusudiwa kutufanya wa Kiroho zaidi. “Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, ‘Aba!’ yaani, ‘Baba!’… Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa” (Rom 8:15,26). Kipaji hicho kinatuonjesha ladha ipitayo maumbile hata katika tabu za ndani; kinajitokeza hasa katika sala ya utulivu, ambamo utashi unatekwa na mvuto wa Mungu, ingawa mara nyingi akili inalazimika kupambana na mitawanyiko ya mawazo. Kwa utamu wake kinatufanya tufanane na Kristo mpole na mnyenyekevu wa moyo, na kinaleta heri ya wapole watakaorithi nchi ya walio hai.

Lakini ili tuwe na ibada imara, ambayo inakwepa udanganyifu na kutawala ubunifu na miguso, tunahitaji *kipaji* cha juu zaidi, kile *cha elimu.* Hicho kinatuandaa kupokea mwanga bora kuliko ule wa elimudunia na wa teolojia. Ni kama hisi ipitayo maumbile ambayo *tunapima vizuri mambo ya kibinadamu* kadiri yanavyoashiria yale ya Kimungu au yanavyopingana nayo. Kwa kipaji hicho baadhi wanaona hasa vitu vinavyoonekana kama alama za visivyoonekana; baadhi wanaona hasa ubatili wa viumbe na wa yote yapitayo (k.mf. vyeo na sifa), pamoja na *ubaya usio na mipaka wa dhambi ya mauti.* Kwa kuonyesha uovu huo kipaji cha elimu kinatufanya tusiogope tu dhambi, bali tutishwe nayo na kuihuzunikia sana. Kinatufahamisha pia jinsi malimwengu yasivyotokana na Mungu tu, bali na sababu zenye kasoro (katika hilo kinatofautiana na hekima). Kinaleta ujuzi halisi wa mema na mabaya, si kama Adamu na Eva waliodanganywa na Ibilisi wakapata elimu chungu ya kung’amua uasi wao na matokeo yake. Tukimfuata Roho Mtakatifu tunakuja kufanana na Mungu anayejua maovu ili kuyachukia na maadili ili kuyatimiza. Mara nyingi elimudunia inavimbisha; kinyume chake kipaji cha elimu kinaimarisha tumaini kwa kutuonyesha udhaifu wa msaada wowote wa kibinadamu na ubatili wa malimwengu, na kwa kutuhimiza tutamani kwenda mbinguni kwa kumtegemea Mungu tu. Kinahusiana na heri ya machozi ya majuto na kutupa msimamo mzuri kati ya kutegemea mema bure na kutazamia mabaya tu hata kukata tamaa. Elimu hiyo ya thamani ilikuwa nao wote waliofanya utume mkubwa, k.mf. Mt. Dominiko aliyelia mara nyingi akiona hali ya watu aliowahubiria.

Juu kuliko elimu kipo *kipaji cha nguvu,* kwa kuwa haitoshi tupambanue mema na mabaya, bali ni lazima tuepe ya kwanza na kutimiza ya pili kwa udumifu. Tunapaswa kupiga vita vikali dhidi ya mwili, ulimwengu na shetani, maadui hatari kwa uovu, ujanja na uwezo. Je, tuogope vicheko vya watu na maneno yao? Tukianguka kwa hayo tutatekwa na yule anayejitahidi kutupoteza kadiri tulivyo na wito bora. “Mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama” (Ef 6:10-13). Kipaji cha nguvu kinainua moyo wetu katika hatari na kusaidia subira yetu katika majaribu marefu. Kiliwategemeza wafiadini kikiwatia udumifu usioshindika hata watoto na mabikira. Kinahusiana na heri ya wenye njaa na kiu ya haki wanaodumisha ari takatifu kati ya vipingamizi vingi.

Lakini katika nafasi ngumu, yanapotimizwa matendo bora ya kipaji cha nguvu, tunapaswa kukwepa ushupavu wa kilokole: kwa ajili hiyo tunahitaji *kipaji* cha juu zaidi, kile *cha shauri.* Hicho kinafidia upungufu wa busara, k.mf. inaposita ikijiuliza, Ni afadhali niendelee kuvumilia au nionyeshe msimamo? Katika shida za namna hiyo tumkimbilie Roho Mtakatifu anayeishi mwetu. Kipaji hicho hakitukatazi tusiombe shauri la viongozi wa nje na wa roho, bali kinatukinga dhidi ya kufuata silika bila ya kufikiri na dhidi ya utovu wa moyo; kinatujulisha pia yale ambayo viongozi hawawezi kutuambia, hasa namna ya kulinganisha maadili yanayoonekana kupingana. Pengine Roho Mtakatifu anatuonya tusiseme neno fulani; tukienda kinyume, mara nyingi litasababisha vurugu, hasira, upotevu wa muda mwingi, mambo yaliyokuwa rahisi kuyaepa. Madogomadogo ndiyo yanayokwamisha katika njia ya ukamilifu: k.mf. zoea fulani linalozuia ukusanyaji wa mawazo, unyenyekevu au heshima kwa wengine. Vipingamizi hivyo vinaondolewa na uvuvio wa kipaji cha shauri, kinachohusiana na heri ya wenye huruma, kwa kuwa hao ni washauri hodari wanaoacha kujijali ili wainue wenye huzuni na wakosefu.

Ni lazima tupande juu zaidi ili kipaji kingine kifidie upungufu wa imani. Ni kwamba adili hilo linafikia mafumbo ya Kimungu kwa njia ya matamko ya kinadharia tu, tena mengi; tungependa yajumlishwe na moja

ambalo lituambie vizuri Mungu ni nani. Basi, *kipaji cha akili* kinatusaidia mwanga wa ndani unaotuwezesha kupenya mafumbo ya wokovu na kuhisi ukuu wake. Pasipo mwanga huo mara nyingi tunasikia mahubiri na kusoma vitabu vya dini tusielewe maana yake ya dhati. Maneno hayo tunayatunza kwa heshima katika kumbukumbu, lakini ukweli wake hautugusi, hauna mwanga zaidi, ni kama nyota ya mbali angani. Hapo maneno ya ulimwengu yanatushawishi kwa urahisi kwa kuwa hatulishwi vya kutosha na kweli hizo za Kimungu. Kinyume chake, mtu sahili aliyemsujudia Mungu ataelewa mafumbo yake, si kwa ajili ya kuyafafanua, bali kwa kuyaishi. Roho Mtakatifu ndiye anayemjalia ujuzi huo wenye kupenya na kuishi kweli za imani unaomwezesha kuchungulia uzuri mkubwa ajabu wa maneno ya Yesu. Ndiye anayemjalia kuelewa kwa ndani wito wake akimkinga na udanganyifu wowote. Kipaji hicho hakipatikani kwa kiasi kikubwa pasipo usafi mkubwa wa moyo na wa nia. Kinahusiana na heri ya wenye moyo safi, ambao kwanzia hapa duniani wanamuona Mungu kwa namna fulani katika Maandiko matakatifu, ambayo pengine yanakuja kung'aa kama kwa kupigiwa mstari wa mwanga.

Hatimaye, *kipaji cha hekima* ndicho cha juu kuliko vyote, kama vile upendo, unaohusiana nacho, ulivyo adili bora kuliko yote. Hicho kinaelekeza kupima mambo kuhusiana na Mungu, aliye asili na lengo kuu la yote, si tu teolojia inavyofanya, bali kwa *uelekevu* kwa mambo ya Mungu unaotokana na upendo. Kwa *uvuvio wake* Roho Mtakatifu anatumia uelekevu huo ili atuonyeshe uzuri, utakatifu na utimilifu mwangavu wa mafumbo ya wokovu, yanayoitikia matamanio yetu ya dhati na ya juu zaidi. Kumbe ni utovu wa hekima: kukwazwa na msalaba unaoendelea kuwepo katika maisha ya Kanisa; kutothamini vya kutosha sala, sakramenti na majaribu yanayovumiliwa kwa upendo; kujali mno elimudunia; kuchanganya upendo na urahisi wa kuruhusu maovu, au imani na msimamo mkali. Kipaji cha hekima, asili ya sala ya kumiminiwa inayoongoza utendaji, kinaonjesha wema wa Mungu na *kuudhihirisha katika matukio yoyote*, hata yaliyo machungu zaidi. Kinaonyesha uhusiano wa sababu na malengo, pamoja na mpangilio wa tunu, kwa kukumbusha kwamba si yote yanayong'aa ni dhahabu: kinyume chake, maajabu kadhaa ya neema yamefichika katika sura duni, kama ile ya Mt. Benedikto Yosefu Labre. Kinafanya watakatifu watazame kwa upendo maongozi ya Mungu wasifadhaishwe na giza lililomo, wakitambua amefichama humo. Kama vile nyuki anavyojua afyonze wapi katika maua, kipaji cha hekima kinaona wema wa Mungu katika mambo yote. Kinakumbusha kuwa "tata elfu haziundi shaka moja" (Y. H. Newman) kabla hazijatikisa msingi wenyewe wa hakika. Hivyo magumu elfu katika ufafanuzi wa Biblia hayasababishi shaka yoyote kuhusu asili ya Kimungu ya dini yetu. Basi, hekima inatia amani kubwa, yaani utulivu wa utaratibu wa mambo yaliyotazamwa upande wa Mungu. Ndiyo sababu inahusiana na heri ya wapatanishi ambao wanatunza amani hata wengine wanapofadhaika, na ambao wanaweza kuwatia amani waliovunjika moyo. Ni dalili mojawapo ya kuungana na Mungu.

Wengi, ambao waliishi katika neema inayotia utakatifu na walipokea ekaristi miaka mingi, hawaonyeshi vipaji vya Roho Mtakatifu katika mwenendo wao, bali wana uchu wa sifa, wanachukizwa na neno dogo na kuishi kibinadamu mno. Sababu ya ulegevu wao ni kwamba dhambi nyepesi, wanazozitenda mara nyingi pasipo kujali makosa hayo na maelekeo yanayotokana nayo, zinawavuta chini na kuvifunga vipaji vyao kama mabawa yaliyokunjwa. Hawako macho wapokee miangaza ya Roho Mtakatifu, hivyo inawapita tu na kuwaacha gizani. Wanaambiwa, "Ingekuwa heri leo msikie sauti yake: 'Msifanye migumu mioyo yenu'" (Zab 95:7-8).

**TUISIKIEJE SAUTI YA ROHO MTAKATIFU?**

Ili tuisikie sauti hiyo ni lazima tukusanye mawazo, tujibandue na ulimwengu na umimi, tutunze moyo na tufishe matakwa na maoni yetu. Roho yetu isipokuwa na kimya ndani mwake, au ikivurugwa na mapendo ya kibinadamu mno, haiwezi kupokea miangaza ya mlezi wa ndani. Ndiyo sababu Bwana anazifanyia kazi hisi zetu, pengine kwa dhati, kama kwa kuzisulubisha, ili hatimaye zinyamaze na kutii kikamilifu utashi uliohuishwa na upendo. Ikiwa kwa kawaida tunajifikiria tu, tutajisikiliza au tutasikiliza sauti nyingine mbovu na ya hatari zaidi inayotaka kutupotosha. Ndiyo sababu Bwana ametualika tujifie kama chembe ya ngano ardhini.

Lakini, hata tukipata kimya ndani mwetu, sauti ya Roho Mtakatifu ni ya fumbo: "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho" (Yoh 3:8). Maneno hayo yanatutaka tuwe tayari kupokea mivuto ambayo inatoka kwa Bwana na ni kama mbegu ya mambo yajayo katika maongozi yake. Ni mivuto ya kujikatalia na kusali kwa ndani, yenye thamani kubwa kuliko tunavyodhani; k.mf. kuna wasomi wanaowahi kuvutiwa na sala ya moyo, ambao peke yake huenda ikawakinga na kiburi kwa kuwapatia roho ya kitoto inayohitajika ili kuingia katika ufalme wa Mungu. Inaanza kama elekeo lisilo wazi, lakini tukidumu kwa unyenyekevu katika matakwa yake, tutakuja kutambua inatoka kwa Mungu. Mara nyingi mivuto ya kwanza inatambulisha wito: mwanga wa alfajiri unaweza ukawa mkubwa na kuongoza hija yetu ya kwenda mbinguni.

**TUJIANDAE VIPI KUWA WASIKIVU HIVYO?**

1° *Tutii kwa uaminifu matakwa ya Mungu tuliyokwishayajua* kwa njia ya amri na mashauri yanayolingana na wito wetu. Tukitumia vizuri tuliyokwishayajua, Mungu atatuzidishia ujuzi.

2° *Turudie mara nyingi azimio la kufuata matakwa yote ya Mungu.* Hivyo tutajivutia neema mpya. Tukariri maneno ya Yesu, "Chakula changu ndicho hiki: niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake" (Yoh 4:34).

3° *Tuombe mfululizo mwanga na nguvu ya Roho Mtakatifu* ili kutimiza matakwa ya Baba. Tena inafaa kujiweka wakfu kwa Roho Mtakatifu, ili tujitie mikononi mwake kwa imani. *Hasa katika nafasi ngumu na kazi mpya muhimu, tumuombe atuangaze,* tukiwa na nia nyofu ya kutimiza matakwa ya Mungu tu. Halafu, tusipojaliwa miangaza mipya, tuendelee kutenda tunavyoona vema.

Hatimaye *tuangalie kwa makini misukumo mbalimbali ya roho yetu ili kuchambua iliyo ya Mungu na isiyo yake.* Katika roho inayotii neema, kwa kawaida ile ya Mungu ni mitulivu, kumbe ile ya shetani ni ya nguvu na kusababisha vurugu na fadhaiko.

**USIKIVU KWA ROHO MTAKATIFU, UTIIFU NA BUSARA**

Waprotestanti wanataka kufuata mwanga wa binafsi kuliko Kanisa pia; kumbe usikivu kwa Roho Mtakatifu haukubali chochote kinyume cha mamlaka ya Kanisa, bali unalenga kutimiza imani na maadili mengine. Vivyo hivyo uvuvio wa Roho Mtakatifu haufuti utiifu kwa viongozi, bali unasaidia kuutekeleza, tena unatakiwa kueleweka daima kwa sharti la kwamba utiifu usiagize lingine. "Hofu pekee ni kwamba viongozi wanaweza wakafuata mno busara ya kibinadamu, na pasipo upambanuzi wakapinga miangaza ya Roho Mtakatifu kama udanganyifu na ndoto... Hata katika nafasi hiyo utiifu unatakiwa, ila Mungu atajua kurekebisha kwa wakati wake mawazo finyu ya hao wanaojiamini kipumbavu, akiwafundisha kwa uchungu wao kwamba hawatakiwi kulaumu neema zake bila ya kuzijua wala kuweza kuzitambua" (A. Lallemant).

Tusidhani usikivu kwa Roho Mtakatifu hauhitaji maamuzi ya busara wala mashauri ya watu wenye mang'amuzi. Kinyume chake, mlezi wa ndani anatuambia tuangalie vizuri yale tunayoweza kuyaona wenyewe, na tuombe shauri la watu wenye mwanga, pamoja na kumkimbilia yeye. Mt. Paulo alitumwa kwa Anania aambiwe afanye nini. Basi, usikivu huo unapatana na utiifu, busara na unyenyekevu, tena unayakamilisha.

**MATUNDA YA USIKIVU KWA ROHO MTAKATIFU**

Ukamilifu wetu wote unategemea uaminifu huo. "Wengine wanafuata ibada nyingi nzuri na kutenda mengi maadilifu; tunaweza kusema wanajitosa katika utekelezaji wa nje wa maadili. Hayo yanafaa kwa wanaoanza; lakini ni ukamilifu mkubwa zaidi sana kufuata uvuvio wa ndani wa Roho Mtakatifu na kutenda kufuatana na misukumo yake" (A. Lallemant). Tukijitakasa moyo na kuondoa yale yote yanayopingana na neema tunaweza kuufikia ukamilifu kwa nusu ya muda wake.

"Shabaha ambayo tuilenge kisha kujizoesha sana katika usafi wa moyo, ni kujiachilia tutawaliwe na kuongozwa na Roho Mtakatifu, hata mwenyewe tu awe anaongoza vipawa vyote vya nafsi yetu na hisi zetu zote, na kuratibu yote yanayotokea ndani mwetu na nje yetu, wakati sisi tunapojiachilia kabisa kwake kwa kujinyima Kiroho matakwa yetu yanayoturidhisha binafsi… Wachache wanajua kufikia neema zote walizopangiwa na Mungu, au kufidia baadaye hasara ya kuzipoteza. Walio wengi wanakosa moyo katika kujitawala na uaminifu katika kutumia vema zawadi za Mungu. Kisha kushika njia ya uadilifu, mwanzoni tunatembea gizani, lakini tukifuata neema kwa uaminifu na udumifu, kwa hakika tutafikia mwanga mkubwa kwa faida yetu na ya wengine… Pengine inatokea kwamba, kisha kupata toka kwa Mungu mwanga mzuri, mara tunajisikia kushambuliwa na ukinaifu, shaka, wasiwasi na ugumu kutoka ndani ya umbile letu lililoharibika na maono yetu yenye kupingana na uvuvio wa Mungu. Tukiupokea mwanga huo kwa utiifu kamili wa moyo, utatujaza ile amani na faraja ambayo Roho wa Mungu analeta naye daima na ambayo anawashirikisha wale wasiopinga… Ni ukweli wa imani kwamba hata uvuvio mdogo kabisa wa Mungu ni azizi na bora kuliko ulimwengu wote, kwa sababu unapita maumbile na kutokana na damu na mauti ya Mungu. Lo, upumbavu mkubwa kweli! Tunapuuzia miangaza ya Mungu kwa kuwa ni ya Kiroho na ya juu mno kuliko hisi. Hatuijali, tunapendelea vipawa vya kimaumbile, kazi za heshima, sifa za watu, starehe zetu ndogondogo na kujiridhisha binafsi. Lo, udanganyifu mkubwa mno ambao wengi wanaung'amua saa ya kufa tu! Kwa kufanya hivyo tunamnyang'anya kimatendo Roho Mtakatifu uongozi wa roho yetu; na ingawa moyo ni wa Mungu tu, tunaujaza viumbe, kwa hasara yake; hivyo badala ya kuupanua bila ya mwisho kwa uwemo wa Mungu, tunaubana upeo kwa kuuhusisha na mambo madogo yasiyo na maana. Ndicho kinachotuzuia tusifikie ukamilifu" (A. Lallemant).

Usikivu kwa Roho Mtakatifu unatuonyesha alivyo kweli *Mfariji* katika wasiwasi juu ya wokovu wetu na katika vishawishi na huzuni za maisha haya. Kwa kuwa hatuwezi kustahili kifo chema, tunahitaji uongozi, ulinzi na faraja ya Roho Mtakatifu "aliye arabuni ya urithi wetu" (Ef 1:14). Mpako wake rohoni unatuliza tabu, unaimarisha utashi dhaifu na pengine kuonjesha ladha halisi ya Kimungu katika msalaba. "Roho Mtakatifu anatufariji katika mateso ya hapa uhamishoni, tulipo mbali na Mungu, jambo linalosababisha waadilifu wawe

na huzuni isiyosemekana; kwa kuwa ndani mwao wanahisi sana utupu usiopimika uliomo na usioweza kujazwa na kiumbe chochote, ila na furaha ya Mungu tu. Muda wote ambao wametengana naye wananyong'onyea na kuteseka kama kwa kifodini chenye mateso, hata wasingeweza kuvumilia pasipo faraja ambazo Roho Mtakatifu anawajalia mara kadhaa" (A. Lallemant). Tone moja tu la utamu ambao Roho Mtakatifu anaumimina rohoni linatosha kuilevya kitakatifu.

## 3.23. *UPAMBANUZI WA ROHO*

Usikivu kwa Roho Mtakatifu unadai *tupambanue* uvuvio wake na roho nyingine mbili ambazo kwanza zinaweza zikaonekana nzuri, kumbe zinaua. Neno "upambanuzi wa roho" linaweza kumaanisha *karama* mojawapo kati ya zile alizoziongelea Mt. Paulo, inayotuwezesha kutambua mara k.mf. mtu akisema au kutenda kwa upendo halisi au kwa unafiki. Lakini linaweza pia kumaanisha upambanuzi unaotokana na *busara ya Kikristo* ikisaidiwa kutoka juu na kipaji cha shauri na neema anazojaliwa kiongozi anayewajibika. Hapa tuna maana hiyo ya pili.

Kwa neno "roho" tunamaanisha elekeo la kupima, kutaka na kutenda namna fulani. Hasa tunatofautisha roho tatu: *ile ya Mungu; ile ya kibinadamu tu* inayotegemea umbile lililoharibika, ambalo mivuto yake, utamu wake na juhudi zake za muda vinaweza kudanganya; hatimaye *ile ya Ibilisi* anayeona faida kufichama na kujifanya ni malaika wa mwanga. "Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetoka kwa Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani" (1Yoh 4:1). Kwa kawaida kila mtu anatawaliwa na roho mojawapo kati ya hizo. Waovu wanatawaliwa na shetani; watu vuguvugu wanatawaliwa na roho ya kibinadamu tu; walioanza kushika kwa bidii maisha ya Kiroho wanatawaliwa na Roho wa Mungu, lakini mara nyingi roho ya kibinadamu na ya shetani zinajiingiza, hivyo hatutakiwi kamwe kumpima mtu kwa kuzingatia matendo yake machache, bali jumla ya maisha. Hata waliokamilika Mungu anaacha wabaki na kasoro kadhaa (pengine zinaonekana tu kuwa hivyo) kusudi awatunze katika unyenyekevu na kuwapa nafasi nyingi za kutimiza maadili yanayopingana nazo. Kwa mfano, kuna watu walioendelea katika njia ya Mungu ambao kwa ugonjwa maalumu wanaelekea kukasirika; kumbe chini ya kutovumilia kwao kwa nje zinaweza kufichika subira na stahili kubwa. Basi, ni muhimu kupambanua vizuri roho ipi inatusukuma.

Kipimo kikuu kwa upambanuzi wa roho kilitolewa na Bwana: "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwamwitu wakali. *Mtawatambua kwa matunda yao.* Je, watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila *mti mwema huzaa matunda mazuri,* na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri" (Math 7:15-18).

Wenye nia mbaya hawawezi kuificha muda mrefu; itaonekana kwa namna mbalimbali: kwanza katika matendo ya dharura yasiyoacha nafasi ya kupanga udanganyifu; halafu katika tabu: "kuna rafiki wakati wa kufaa, ambaye yeye hatadumu wakati wa msiba wako" (YbS 6:8). Hivyo watu wanajionyesha walivyo wasipoweza kupata wanachotamani au kisha kukipata: k.mf. wanaofikia utawala wanakuja kujitokeza walivyo kweli.

Ikiwa undani wa utashi wetu ni mwema utazaa matunda mema. Wengine watatambua mapema kama tunasikiliza neno la Mungu ili kulitekeleza. Lakini tutazaa nini tukiridhika kumuita, "Bwana, Bwana!" tusitimize matakwa yake?

Tunaweza kutambua roho inayotusukuma kwa kuangalia matokeo yake na kuilinganisha na maadili ya Kikristo: upande mmoja unyenyekevu na kujikana, upande mwingine maadili ya Kimungu.

### DALILI ZA ROHO YA KIBINADAMU TU

Kutokana na dhambi ya asili umbile letu ni adui wa ufishaji na wa unyenyekevu: linajifanya lengo la yote na kupuuzia kimatendo maadili ya Kimungu. Hata katika sala linajitafutia faraja na kutumbukia ulafi wa roho; matatizo (au ukavu) yakianza, linaacha maisha ya Kiroho, likijisingizia eti! Busara inataka tusizidishe ugumu wa maisha na urefu wa sala (likimaanisha kutafakari kidogo kila siku). Kwa kisingizio cha utume linajiridhisha na utendaji, likizidi kujimwaga nje na kuchanganya upendo wa Kikristo na wema wa kiutu tu; yakizuka mapingamizi na majaribu, linanung'unikia msalaba na kukasirika hata kukata tamaa. Juhudi zake ni kama moto wa nyasi: hazijali utukufu wa Mungu wala wokovu wa watu. Roho ya kibinadamu tu inajumlishwa katika neno moja: umimi.

Roho hiyo imechorwa hivi, "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" (1Kor 2:14). Anapima yote kwa mtazamo wa binafsi, si wa Mungu. Polepole anapotewa na roho ya imani, tumaini na upendo; anataka kujitegemea ingawa ni udhaifu wenyewe. Ila pengine ukubwa wa uovu wake unamkumbusha neno la Yesu: "Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote" (Yoh 15:5).

### DALILI ZA ROHO YA IBILISI

Shetani kwanza anatuinua kwa kututia kiburi, halafu anatubwaga katika kuhangaika, kuvunjika moyo hata kukata tamaa. Si kila mara anatusogeza mbali na malipizi; hasa katika mazingira yanayoyaheshimu

anayahimiza yale ya nje, ili adumishe kiburi na kuharibu afya. Kumbe hahimizi ufishaji wa ndani (wa ubunifu, moyo, matakwa na maoni yetu) ingawa pengine kwa udanganyifu anatufanya tufadhaikie mambo madogo tusijali mazito wala ya hatari. Anatufanya tujithamini mno, tujipendelee, tujivune na kusali kama Farisayo hekaluni bila ya kujitambua. Mara nyingi kiburi hicho kinaendana na unyenyekevu wa bandia ambao tunajisema katika mambo kadhaa tusije tukasemwa juu ya mengine makubwa zaidi. Piu anatufanya tuchanganye unyenyekevu na hofu ya kushindwa na kudharauliwa.

Badala ya kulisha imani kwa kuzingatia Injili, anatuvuta pengine tufuate mambo ya pekee na ya ajabu yanayoweza kutokeza vipawa vyao; pengine tufikirie yasiyohusiana na wito wetu, kama vile mmisionari kuwaza ajifanye mkaapweke, na Mkartusi ajifanye mtangazaji wa Injili; pengine tena tufuate vitabu vya kisasa na kukanusha yapitayo maumbile.

Upande wa tumaini anatuchochea tujiamini kipumbavu, na kutaka utakatifu mara, bila ya kupitia hatua za lazima wala kujikana. Tukitenda dhambi anatufanya tusijivumilie bali tujikasirikie badala ya kutubu kweli.

Anastawisha umimi wetu, akiupotosha upendo kulingana na tabia na hali yetu, uwe ni upole usiopinga maovu yoyote au, kinyume chake, ari chungu ambayo inakaripia wengine badala ya kujirekebisha, inasababisha kinyongo na mafarakano badala ya amani, hata watu wakaogopa kutupinga, wakijua hatutavumilia.

Hatimaye tukija kutenda kosa tusiloweza kulificha, tunatumbukia fadhaa, hasira na kukata tamaa, ambapo shetani anatudanganya tena kwa kuzidisha ugumu wa kumrudia Mungu kama alivyotudanganya kwanza kwa kuficha hatari. Anatuunda kwa mfano wake ambaye alijiinua kwa kiburi akakata tamaa moja kwa moja. Basi, tuwe macho tukijikuta tunaguswa upande wa hisi wakati wa ibada, lakini ikimalizika tunajipendea zaidi na kukosa unyofu kwa viongozi wetu. Utovu wa unyenyekevu na wa utiifu ni dalili ya hakika ya kwamba hatuongozwi na Mungu.

**DALILI ZA ROHO WA MUNGU**

Tofauti na roho mbili tulizozieleza, Roho Mtakatifu anatuelekeza kujifisha upande wa mwili lakini kwa kiasi na utiifu, bila ya kujionyesha wala kuharibu afya. Pia anatutambulisha kuwa ufishaji huo si kitu pasipo ule wa moyo, matakwa na maoni yetu. Anatutia unyenyekevu halisi unaotuzuia tusijipendee, tusiogope kudharauliwa, tusitangaze fadhili tulizojaliwa wala kuzikanusha, tukimtukuza Mungu tu kwa hizo.

Anatuelekeza kulisha imani yetu kwa maneno sahili na ya dhati ya Injili, kwa kushika kiaminifu mapokeo na kukwepa uzushi. Anatuonyesha Bwana ndani ya viongozi, jambo ambalo linastawisha imani.

Anachochea tumaini tusijiamini kipumbavu wala kujali mno mafanikio ya kibinadamu. Anatutamanisha maji hai ya sala, akitukumbusha haja ya kuyafikia hatua kwa hatua kwenye njia ya unyenyekevu, kujikana na msalaba.

Anazidi kuwasha upendo kwa ari ya kumtukuza Mungu na kujisahau. Anaelekeza kumfikiria kabla ya yote na kumuachia atushughulikie. Anachochea upendo kwa jirani akitukumbusha kuwa ndiyo ishara kuu ya upendo kwa Mungu, na kutuzuia tusihukumu wala kukwazika bila ya sababu. Anatia ari pole inayojenga kwa sala na mifano mizuri, badala ya kuchukiza kwa maonyo yasiyofaa. Katika majaribu anatia uvumilivu, upendo kwa msalaba na kwa adui, amani ndani mwetu tena na wengine, na hata furaha ya rohoni. Tukija kuanguka kwa dharura anatukumbusha huruma ya Mungu. "Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" (Gal 5:22) pamoja na utiifu na unyenyekevu.

Kuhusu tendo maalumu, ni dalili ya kutembelewa na Mungu ikiwa hakuna sababu ya kimaumbile iliyoleta faraja ya dhati tunayojisikia ghafla. Ila tutofautishe dakika hiyo ya kwanza na zile zinazofuata ambapo mara nyingi tunawaza wenyewe pasipo uvuvio wa Mungu, na hivi tunaweza tukadanganyika.

Kwa nadra tu Roho Mtakatifu anajalia mafunuo (neema za pekee ambazo kuzitamani ni kujiamini kipumbavu), ila mara nyingi anawaangazia wenye juhudi neno la Injili. Hapo wafanye kama msanii anayefuata kipawa chake kuliko kufikiria kanuni za sanaa, akizitimiza kwa namna bora kutokana na kipawa chenyewe. Ndipo yanapokuja kupatana unyenyekevu na ari, upole na msimamo, unyofu wa njiwa na busara ya nyoka. Ndivyo Roho Mtakatifu anavyoongoza watu waaminifu hadi bandari ya milele.

## 3.24. *SADAKA YA MISA NA WANAOENDELEA*

Hatuwezi kuendelea katika maisha ya Kiroho tusipopenya kila siku zaidi kile kinachofanya sadaka ya altare iwe na thamani isiyo na mipaka. Mfiadini Mt. Yohane Fisher aliwajibu Waprotestanti, "Misa ni kama jua ambalo kila siku linaleta mwanga na joto katika maisha yote ya Kikristo".

Tunaweza kuyachimba mafundisho ya Kikatoliki juu ya sadaka ya misa ama kinadharia tu ama kimaisha, yaani kwa kujiunga nayo na kumtolea Mungu pamoja na Yesu yale yote yanayoweza yakatupata siku hiyo, hadi kufa, na hata kuingia mbinguni. Inafaa mtu anayeendelea atangulize kutoa sadaka ya uhai wake ili kujaliwa kifo chema katika neema inayotia utakatifu. Kwa kuwa maendeleo ya Kiroho yanalenga hasa tendo la mwisho la upendo hapa duniani ambalo, likiandaliwa na maisha yote na kufanywa kikamilifu, linatarajiwa kutufungulia mara milango ya mbinguni.

*Ili tupenye dhati ya misa tunapaswa kujifunza kwa Mama wa Mungu.* Baadhi ya watakatifu, hasa wale

waliojaliwa majeraha ya Yesu, waliunganika na mateso na stahili zake kwa namna ya pekee; hata hivyo muungano huo haukulingana na ule wa Maria. Kutokana na ujuzi na mang'amuzi ya dhati, Maria chini ya msalaba alipenya fumbo la ukombozi, kadiri ya imani yake na ya vipaji alivyokuwa navyo kulingana na upendo wake mkubwa.

Walio mahututi wanahimizwa kutoa sadaka ya uhai wao ili mateso ya mwisho yawe na thamani, fidia, stahili na dua. Ili tangu sasa tutoe sadaka hiyo vizuri, tunapaswa kuitoa pamoja na ile ya Mwokozi inayodumu kisakramenti altareni, na pamoja na sadaka ya Maria aliyeishiriki kwa namna bora. Ili tuelewe toleo hilo linadai nini, inafaa tukumbuke malengo manne ya sadaka: kuabudu, kufidia, kudua na kushukuru.

**KUABUDU**

Yesu msalabani alifanya kifo chake kiwe sadaka ya kuabudu, utekelezaji bora wa amri ile aliyomjibu mshawishi, "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake" (Lk 4:8). Ibada ni haki ya Mungu kutokana na ukuu wake kama Muumba, kwa kuwa mwenyewe tu yupo milele. Inatakiwa kuwa ya nje na ya ndani kwa pamoja, kuongozwa na upendo, kufanyika katika Roho na ukweli. Yesu bustanini alitoa ibada yenye thamani isiyo na mipaka aliposujudu kifudifudi akisema, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Math 26:39). Ibada hiyo ilikiri kimatendo na kwa dhati ukuu wa Mungu, Bwana wa uhai na wa kifo, ambaye "hushusha hata kuzimu, na kuinua tena" (Tob 13:2).

Ibada hiyo ilipoendelea msalabani, Maria aliishiriki kadiri ya ujazo wa neema ambao alijaliwa na ambao ukazidi kuongezeka. Mbele ya msalaba aliabudu haki ya Mungu aliyetaka kifo cha Mwanae asiye na kosa kiwe malipizi ya dhambi kwa wokovu wa milele wa watu. Tunaweza kumuabudu kwa namna nyingi, lakini hakuna iliyo bora kuliko kujiunga kila siku na sadaka ya Mwokozi. Tangu sasa ibada yetu hiyo iwe nyofu na ya dhati, kiasi cha kuongoza kweli maisha yetu na kutuandaa kwa ile itakayotupasa kuwa nayo moyoni saa ya mwisho.

**KUFIDIA**

Lengo la pili la sadaka ni *kufidia chukizo* la dhambi kwa Mungu, na *kulipa adhabu inayodaiwa na dhambi.* Bwana alilipa kupita kiasi kwa makosa yetu, kwa sababu alipotoa uhai wake kwa ajili yetu alifanya *tendo la upendo linalompendeza Mungu kuliko jinsi jumla ya dhambi zote inavyomchukiza.* Upendo wake ulikuwa mkubwa mno kuliko uovu wetu watesi wake; ulikuwa na thamani isiyopimika kwa kuwa ulitoka katika Nafsi ya Neno. Lakini, kwa vile sababu asili haifuti sababu shiriki, sadaka ya Mwokozi haifuti sadaka yetu, bali inaichochea na kuitia thamani.

Maria alitupatia kielelezo akiungana na mateso ya Mwana na kutoa fidia kwa ajili yetu hata akaitwa "mkombozi mshiriki". Alikubali kifodini cha Mwanae mpenzi ambaye alimuabudu kwa haki na kumpenda kwa hisani isiyosemeka. Shujaa kuliko Abrahamu aliyekuwa tayari kumchinja Isaka, Maria alipomtoa Mwanae kwa wokovu wetu alimuona akifa kwa mateso ya kutisha ya mwili na roho. Hakuna malaika aliyeingia kati kuisimamisha sadaka ya Maria na kumuambia, "Sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee" (Mwa 22:12). Maria aliona ilivyotimia sadaka ya Yesu, ambayo sadaka ya Isaka ilikuwa kidokezo chake tu, akateseka kwa ajili ya dhambi kadiri ya upendo wake kwa Mungu anayechukizwa nazo, kwa Mwanae aliyesulubiwa nazo, na kwa roho zetu zinazoangamizwa nazo. Kwa kuwa upendo wa Bikira ulizidi ule wa Abrahamu, maneno aliyoambiwa babu huyo yanamfaa zaidi Mama yetu: "Kwa kuwa umetenda neno hili… katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni" (Mwa 22:16-17).

Sadaka ya Yesu na Maria ilikuwa fidia ya dhambi na malipizi ya adhabu iliyodaiwa nazo. Tangu sasa tuombe saa yetu ya mwisho iwe na stahili na kufidia, tena tujaliwe neema ya kutoa sadaka hiyo kwa upendo mkubwa ambao uzidishe thamani yake. Tufurahi kulipa deni hilo kwa haki ya Mungu ili utaratibu wake urekebishwe kikamilifu ndani mwetu. Tukiungana hivyo kwa ndani na misa zote zinazoadhimishwa kila siku ulimwenguni kote, tukiungana hasa na kiini cha misa hizo, yaani sadaka iliyo hai daima moyoni mwa Kristo, tutajaliwa kuungana nazo hata saa ya mwisho. Muungano huo wa upendo na Yesu ukiwa wa ndani zaidi kila siku, fidia ya toharani itafupika, na pengine tutajaliwa kutakata tayari hapa duniani kwa kukua katika upendo, badala ya kutakaswa pasipo stahili kisha kufa.

**KUOMBA**

Yesu "siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu; na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii" (Eb 5:7-9). Tukumbuke sala yake ya kikuhani aliyoitoa kati ya karamu ya mwisho na sadaka ya msalabani, alipowaombea mitume wake hata sisi pia, "wao wamjiao Mungu kwa yeye"; sasa "yu hai sikuzote ili awaombee" (Eb 7:25), hasa katika sadaka ya misa, ambayo ndiye kuhani wake mkuu. Pamoja naye tunaombewa na bikira Maria akiitikia maombi tuliyomtolea mara nyingi.

Kufani mtu anatakiwa kuungana na misa zinazotolewa wakati huohuo akijiombea neema ya kifo chema, kutokana na thamani ya hizo na ya sala ya Kristo inayoendelea kwa njia ya hizo. Tena inafaa awaombee wale wote wanaokaribia kufa neema hiyo bora ya wateule. Ili tujiandae kuomba dua hiyo saa ya kufa, tuwaombee mara nyingi katika misa watakaokufa siku hiyohiyo, pia tuagize pengine misa ili tujaliwe kifo chema pamoja na ndugu na marafiki wanaotutia wasiwasi zaidi kuhusu wokovu wao, na wale ambao tuliwakwaza na kuwapotosha.

**KUSHUKURU**

Hatimaye kila mmoja anatakiwa kujiandaa kila siku kufanya kifo chake katika Bwana kiwe sadaka ya shukrani kwa fadhili zote alizojaliwa. Sadaka halisi itakapokoma, utimilifu wake utadumu ukiwa na ibada za wateule ambao, kwa kuungana na Yesu na Maria, wataimba na malaika wimbo wa Mtakatifu, na kumtukuza Mungu kwa shukrani. Tuitoe sadaka hiyo mara nyingi kwa kuungana na misa zinazotolewa siku hiyo, kama ingekuwa ya mwisho, ili kuitoa vema saa ya kufa kwetu, tukiwaalika Mwokozi na Mama yake waje kutuchukua na kutujalia neema kuu itakayohakikisha moja kwa moja wokovu wetu kwa tendo la mwisho la imani, tumaini na upendo.

Hayo tuliyoyasema kuhusu kutoa sadaka ya uhai wetu kwa kuungana na ile ya misa, yaeleweke kimatendo kama alivyoandika Mt. Paulo, "Ninakufa kila siku" (1Kor 15:31). Ni kupokea mapema, kwa upendo na subira, si mateso ya dakika za mwisho tu, bali yale yote ya mwili na roho ambayo Mungu ametupangia tangu milele ili kututakasa na kutufanya tuchangie wokovu wa watu. Pengine udhaifu wetu unafanya mateso hayo ya aina mbalimbali yaonekane mazito, lakini ni madogo yakilinganishwa na yale aliyoyavumilia Yesu kwa upendo mkuu. Nasi tutayapokea tukijiombea tuanze kuupenda msalaba, yaani kumpenda kweli msulubiwa, kwa kuwa tunapaswa kumrudishia upendo kwa upendo.

Turudie kusoma maneno yake kwa mwanafunzi mwaminifu katika Kumfuasa Yesu Kristo (III,47:1-3), "Mwanangu, kazi nzito uliyokubali kwa ajili yangu isikuvunje. Usipoteze moyo kutokana na mashaka. Maagano yangu yakutie nguvu na kukutuliza daima. Mimi naweza kulipa yote kupita kiasi na bila ya kipimo. Hutahangaika hapa muda mrefu mno… Siku moja tabu yote na machungu yatakoma… Kazi unayoifanya, uifanye vizuri. Lima shamba langu kwa bidii, mwenyewe nitakuwa tuzo lako. Andika, soma, imba, juta, nyamaza, sali, vumilia kiume pingamizi; inafaa kujipatia uzima wa milele kwa masumbuko hayo, na hata kwa makubwa zaidi. Siku moja amani itakuja… Laiti ungewaona watakatifu mbinguni na mataji yao ya milele, jinsi wanavyofurahi sasa katika utukufu mkuu! Kumbe, ndio waliopata dharau duniani, wakatupwa kama wasiostahili kuishi… Hungetamani siku ya furaha duniani, la; bali ungependa kuvumilia mengi kwa ajili ya Mungu; ungeona ni faida kubwa kutupwa na watu kama takataka".

Katika misa tuunganishe hivyo sadaka yetu na ya Mwokozi; tumtolee pingamizi na tabu zitakazotupata, tukifikiri zitatuletea faida kubwa, hata vizuio vikawa vyombo. *Msalaba ulikuwa ndio kizuio kikuu walichotaka kumwekea Yesu, kumbe akaufanya chombo kikuu cha wokovu.* Katika mwili wake wa fumbo, kila kiungo kikiwajibika kwa imani, vingine vyote vinafaidika. Kwa sababu hiyo, hata kitu kidogo kinakuwa kikubwa tukikifanya kwa upendo wa Mungu na wa jirani katika muungano na Yesu, kuhani wa milele.

Tuzingatie sehemu za misa zinavyolingana na *upendo unaotakata, unaoangaza na unaojitoa mhanga kwa kuungana na Mungu.* Zinaanza kwa kututia toba na majuto (Nakuungamia, Bwana Utuhurumie), ibada na shukrani (Utukufu), dua (Sala) na imani (Masomo, Nasadiki) ili tuwe tayari kumtoa Mwanakondoo wa Mungu, halafu kumpokea na kushukuru. Hivyo zinatukumbusha hatua za kuinuka kwa Mungu: utakaso wa wanaoanza, mwanga wa wanaoendelea, na muungano wa waliokamilika.

## 3.25. ***KOMUNYO YA WANAOENDELEA***

Kila Komunyo inatakiwa kustawisha upendo na hivyo kutuandaa tumpokee Bwana vizuri zaidi kesho yake. Komunyo ya kwanza ni neema kubwa, lakini zile zinazofuata zinatakiwa kuzaa matunda makubwa zaidi na zaidi. Katika safari yetu ya kumuendea Mungu ongezeko la kasi linatakiwa kupatikana katika wale wanaoendelea kuliko kwa wanaoanza. Ili tuelewe Komunyo ya wanaoendelea inavyotakiwa kuwa, tukumbuke kwamba tokeo lake kuu ni kustawisha upendo, ambao ndio adili linalotakiwa kukua zaidi ndani yao, na kwamba upendo wa kidugu ndio dalili kuu ya upendo kwa Mungu. Tutaelewa zaidi kwa kuzingatia Komunyo inavyohakikisha, kwa njia ya muungano na Bwana, umoja na ustawi wa mwili wake wa fumbo.

**KARAMU TAKATIFU NA UMOJA WA MWILI WA FUMBO**

"Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" (1Kor 10:17). Mabishano yoyote yakome kwenye meza ya waamini wote. Ushirika wao katika mwili wa Kristo ndio "ishara ya umoja, kiungo cha upendo!… Bwana ametupa mwili wake na damu yake katika maumbo ya mkate na divai. Kama vile mkate unavyotokana na chembe nyingi za ngano, na divai inavyotokana na zabibu nyingi, vivyo hivyo Kanisa la Kristo linatakiwa kutokana na wingi wa waamini waliounganishwa na upendo" (Mt. Augustino). Mt. Pius X alipowaalika tena waamini kupokea ekaristi mara

nyingi na hata kila siku, alikumbusha kuwa "karamu takatifu ndiyo ishara, mzizi na chanzo cha umoja wa Kikatoliki".

Kwa msingi huo kabla hatujapokea tufikirie vizuio tunavyoweka pengine kwa muungano wa upendo na Yesu na viungo vyake. Tumuombe tuone vizuio hivyo vinavyotokana nasi, na tuwe na juhudi za kuviondoa; tena, tukiwa wazembe katika kuviondoa, tuombe aviondoe hata kwa kututia uchungu. Katika maandalizi ya Komunyo tuseme, "Nakutolea yaliyo mema ndani mwangu, ijapo ni machache na hafifu, kusudi uyatakase zaidi na kuyakamilisha… Nakutolea pia tamaa takatifu zote za watu wema… Nawaombea wote waliotaka niwakumbuke katika sala… Nakutolea pia sala zangu na sadaka ya kitubio kuwaombea hasa watu ambao walinidhuru, walinichukiza, walinidharau au kunikosea kwa namna yoyote. Vilevile nawaombea wale ambao siku moja niliwatia uchungu, niliwaudhi, niliwalemea na kuwakwaza kwa maneno au kwa matendo, kwa kujua au la, kusudi utuondolee dhambi zetu na makosa tuliyokosa. Ee Bwana, ondoa moyoni mwetu dhana zote za kudhaniana, chuki yote, hasira, ugomvi na lolote ambalo linavunja mapendano au kupunguza mapatano ya kidugu" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,9:4-6). Komunyo iliyopokewa hivyo inahakikisha maishani umoja na Mwokozi na wote aliowahuisha, ili atawale na amani yake.

**KOMUNYO NA USTAWI WA MWILI WA FUMBO**

Komunyo inatakiwa kuchangia na kuhakikisha pia ustawi wa mwili wa fumbo wa Mwokozi: "Tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa... huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo" (Ef 4:15-16). Mwokozi anajenga hivyo viungo vyake hasa katika ekaristi; kwa kupokea mkate wa uzima hao wanaufikia ukamilifu waliopangiwa na Mungu. "Kama vile ubatizo, mlango wa sakramenti, unavyosababisha ndani mwetu chanzo cha uzima wa Kiroho, ekaristi inasababisha utimilifu wake; yenyewe ni kama lengo la sakramenti nyingine ambazo zinatuandaa kuipokea… Kwa hiyo tokeo la ubatizo rohoni… linalenga lile la ekaristi" (Mt. Thoma wa Akwino), kama utoto unavyolenga ukomavu wa utu uzima. Kwa maana hiyo hamu fulani ya tokeo la ekaristi ni ya lazima kwa wokovu.

Hatuwezi kuufikia ukamilifu wa Kikristo tusipojiandaa kupokea ekaristi vizuri na kwa manufaa zaidi na zaidi. Tena si kila Mkristo tu, bali kila parokia, kila jimbo na Kanisa lote katika kila kizazi ndivyo wanavyofikia ukomavu na kuzaa kwa kueneza imani kama mbegu takatifu. Kila wakati una matatizo yake, na Mkristo anatakiwa kujipatia nguvu katika ekaristi leo kama wakati wa dhuluma. Anapaswa kuwa na njaa ya ekaristi, yaani kutamani kuunganika na Kristo kwa undani wa utashi hata ashinde vishawishi vyote akiendelea kutimiza maadili katika nafasi ngumu.

Tumuambie, "Kweli ndiwe mpenzi wangu kabisa; nimekuchagua kati ya maelfu. Roho yangu inapenda kukaa nawe siku zote za maisha yangu. Kweli ndiwe unayenituliza, kwako napata amani kuu na raha kamili; mbali nawe pana masumbuko na uchungu na tabu isiyo na mwisho… Siwezi kueleza uzuri wa tabia yako. Kusudi uwaonyeshe wadogo wema wako, umependa kuwalisha mkate mtamu mno unaotoka mbinguni" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,13:1-2).

Kwa kuupokea motomoto yanatimia maneno ya Zaburi (31:19): "Jinsi zilivyo nyingi fadhili zako ulizowawekea wakuchao!" "Ndio wanaomtambua Bwana wao kwa namna anavyomega mkate, ambao moyo wao unawaka sana wakiwa njiani pamoja na Yesu. Mara nyingi sina ibada ya nguvu namna hii, sina upendo kama huo, wala sisikii moyo kuwaka. Ee Yesu mwema, mpole, mpendevu! Nipe mimi, maskini wako, nisikie mara moja tu mwako wa moyo walau kidogo wakati ninapopokea Komunyo, ili nizidi kukusadiki kwa imara, kuutumainia wema wako, kukupenda kwa upendo kamili usiopoa, kama chakula hiki cha mbinguni kimewasha moto moyo wangu. Huruma yako ina uwezo wa kunipa neema hii ninayopupia mno. Unaweza kunijia kwa upole wako siku yoyote utakayotaka na kunitia moto moyoni" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,14:2-3).

Njaa ya ekaristi inaelezwa hivi, "Napenda kukupokea wewe, Bwana, kwa ibada kubwa sana, kwa upendo unaowaka, kwa hamu yote ya moyo wangu na kwa shauku ya nguvu, vile walivyokutamani watakatifu na watu wema wengi wakati wa kutaka Komunyo. Walikupendeza kabisa kwa usafi wa mwenendo wao na kwa bidii yao iliyokuwa kama moto usiozimika… Napenda kukutolea nafsi yangu na yote niliyo nayo kwa hiari yangu na kwa moyo mkuu. Ee Bwana Mungu wangu, uliyeniumba, uliyenikomboa, leo napenda kukupokea kwa heshima ile na ibada, na sifa na adabu, na shukrani na utaratibu na mapenzi, kwa imani na tumaini na usafi, alivyokuwa navyo Mama yako mtukufu bikira Maria alipokuchukua mimba… Nakutolea furaha za watakatifu wote, mapenzi yao makubwa, shangwe za roho zao, miangaza waliyopewa nawe… pamoja na sifa zote na fadhila zote unazosifiwa… Nataka makabila yote ya kila nchi na ya kila lugha wakusifu, watukuze jina lako takatifu na tamu kama asali, kwa shangwe kuu na kwa ibada ya upendo" (Kumfuasa Yesu Kristo IV,17:1-5). Mkristo anayepokea kwa msimamo huo anamuelekea Mungu kasi zaidi na zaidi na kuvuta wengi nyuma yake: ndivyo unavyohakikishwa ustawi wa mwili wa fumbo wa Kristo. Lakini ni lazima tupige hatua nyingine upande wa ukarimu.

**KOMUNYO YA KUJITOA**

Bwana ametuambia, "Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo" (Yoh 13:34).

Mwenyewe ametupenda hata kutufilia msalabani na kujifanya chakula chetu. Basi Mkristo anapaswa kujifunza katika ekaristi ajitoe kama Bwana alivyofanya. Yesu anayetupatia kila siku ekaristi ndiye kielelezo bora cha kujitoa kikamilifu, naye anatukumbusha kuwa "ni heri kutoa kuliko kupokea!" (Mdo 20:35), kupenda kuliko kupendwa. Anayezidi kuunganika naye kwa njia ya ekaristi, anatakiwa kuwa chakula cha wanaomzunguka, akijitoa pasipo kipimo, hata akipatwa na uchungu wa kudhaniwa vibaya, ubaridi, uovu na uonevu. "Kwa mfano wa Bwana wetu, padri anapaswa kufia mwili wake, roho yake, matakwa yake, heshima yake, familia yake na ulimwengu; anapaswa kujitoa mhanga kwa kimya, sala, kazi, malipizi, mateso na kifo. Kadiri tulivyokufa tuna uhai na kuushirikisha" (M.H. Antoni Chevrier). Yaliyosemwa hapa kuhusu padri yanamfaa kila Mkristo aliyekomaa, ambaye ajitoe mhanga mfululizo ili kuwavuta wanaomzunguka kwenye lengo la safari wanalolisahau mara nyingi. Ari hiyo ya utukufu wa Mungu na ya wokovu wa watu ndiyo itikio ambalo wote walitoe kwa amri kuu ya Mwokozi. Katika Komunyo motomoto tutachota ukarimu huo ambao unang'ariza kwa wengine zawadi tuliyoipokea na unadhihirisha matunda yake. Kazi yetu ni kuupokea tu upendo wa Mungu na kumrudishia kwa kumpenda jirani.

## 3.26. *HESHIMA YA WANAOENDELEA KWA BIKIRA MARIA*

Kisha kuzungumzia jinsi bikira Maria anavyotuathiri, tuone la kufanya kadiri ya Mt. Alois Maria wa Montfort ili tuelewe heshima ya wanaoendelea kwa Maria inavyotakiwa kuwa.

### HESHIMA HALISI KWA MARIA

Hatuzungumzii heshima ya nje tu, yenye kiburi, isiyodumu, ya kinafiki au ya kujitafutia faida, bali ile halisi ambayo ni "utashi kuwa tayari kutenda mara yanayohusu utumishi wa Mungu" (Mt. Thoma wa Akwino). Utayari huo, unaotakiwa kudumu hata hisi zikiwa kavu, unatuelekeza kumuabudu Bwana na kumpatia Mama yake heshima ya pekee anayostahili.

Wengine wanadanganyika wakidai kuufikia muungano na Mungu pasipo kumpitia mfululizo Yesu Kristo: hivyo wataufikia ujuzi wa kinadharia tu kumhusu Mungu, si ule mtamu unaoitwa hekima ambao ni wa juu, hai, wenye kung'amua njia za maongozi yake hata katika mambo madogo. Watulivu walidai eti! Ubinadamu wa Yesu ni njia ya kufaa mwanzoni tu mwa maisha ya Kiroho. Uzushi huo ni kutotambua upana usio na mipaka wa ushenga wa Mwokozi.

Uzushi mwingine ni ule wa Waprotestanti wanaotaka kumuendea Bwana pasipo Maria. Hata baadhi ya Wakatoliki hawaoni inavyofaa kumkimbilia Bikira ili kuwa wandani wa Kristo. Wanamjua Maria "kinadharia tu, kwa namna kavu, kame, isiyojali… Wanaogopa kuzidisha heshima kwake na kumchukiza Bwana wetu kwa kumstahi mno Mama yake mtakatifu… Wakisema juu ya heshima kwa Maria, si kwa kuihimiza, bali hasa kwa kuondoa matumizi yake yasiyofaa" (Mt. Alois Maria wa Montfort). Wanaonekana kudhani Maria ni kizuio kwa kuufikia muungano na Mungu, kumbe athari yake yote inalenga kutufikisha huko. Ingekuwa sawa na kusema Mt. Yohane Maria Vianney alikuwa kizuio kwa wanaparokia wake wasimuendee Mungu. Ni kukosa unyenyekevu kupuuzia washenga ambao Mungu ameujalia udhaifu wetu.

### NGAZI ZA HESHIMA HIYO

Heshima hiyo, ambayo inatakiwa kuwemo ndani ya kila Mkristo na kustawi pamoja na upendo, ngazi yake ya kwanza ni kumuomba Bikira mara kwa mara, k.mf. kusali vizuri Malaika wa Bwana.

Ngazi ya pili ni kuwa na heshima, tumaini na upendo kamili zaidi kwake, ambavyo mtu asali kila siku walau robo ya Rozari kwa kutafakari matendo ya furaha, ya mwanga, ya uchungu na ya utukufu yaliyo njia ya kufikia uzima wa milele.

Ngazi ya tatu, ambayo ndiyo inayowafaa wanaoendelea, ni kujiaminisha kwa Bwana kwa njia ya Mama yake: "Heshima hiyo ni kujiaminisha kabisa kwa Bikira mtakatifu ili kwa njia yake tuwe mali ya Yesu kabisa. Tunapaswa kumtolea: 1) mwili wetu pamoja na hisi zake zote na viungo; 2) roho yetu na vipawa vyake vyote; 3) mali yetu ya nje... ya sasa na ya kesho; 4) mema yetu ya ndani na ya Kiroho, yaani stahili zetu, maadili yetu na matendo yetu mema ya jana, ya leo na ya kesho".

Ili tuelewe vema tendo hilo tunapaswa kutofautisha katika matendo mema mambo yasiyoshirikishwa na yale yanayoweza kushirikishwa. *Yasiyoshirikishwa* ni zile stahili hasa ambazo zinatupa haki ya kustawishiwa upendo na kupata uzima wa milele. Tukizitoa kwa Bikira mtakatifu si kusudi awagawie wengine, bali atudumishie na kutuzalishia na, tukija kuzipoteza kwa dhambi ya mauti, atupatie neema ya kutubu vizuri ili turudishiwe si neema inayotia utakatifu tu bali kiwango chake tulichokuwa nacho.

*Yanayoweza kushirikishwa* ni stahili za kufaa tu na thamani ya matendo yetu mema kwa kufidia na kuombea. Stahili za kufaa hazitegemei haki bali upendo au urafiki unaotuunganisha na Mungu; kwa msingi huo tunaweza kumpatia jirani neema, kama vile mama mwema anavyowavutia wanae, kwa kuwa Mungu anajali nia na matendo yake maadilifu. Tunaweza kuwaombea majirani, wakosefu sugu, walio mahututi, marehemu n.k. Tunaweza kulipa kwa niaba ya wengine, kupokea kwa hiari adhabu za dhambi zao, kama Maria alivyofanya chini ya msalaba ili kuwavutia huruma ya Mungu. Tunaweza pia kuwapatia waliopo toharani rehema kwa kuwafungulia hazina ya stahili za Yesu na ya watakatifu ili kuharakisha ukombozi wao.

Tukimtolea Maria matatizo na tabu zetu zote, atatupatia misalaba inayolingana na nguvu tulizonazo kwa msaada wa neema, ili tuchangie wokovu wa watu.

Tumshauri nani ajiaminishe hivyo? Si wale watakaokubali kwa kufuata hisia za moyoni tu au kiburi kuhusu mambo ya Kiroho, wasielewe uzito wake, bali watu wenye juhudi: nao wajiaminishe kwanza kwa muda mfupi, halafu kwa mwaka mmoja, ili wapenywe na hiyo roho ya kujiaminisha, hadi waweze kujitoa kwa faida maisha yao yote.

Baadhi wanabisha wakisema tendo hilo ni kujinyima yote tusilipe madeni yetu, hivyo litarefusha tohara yetu. Bwana alimjalia Mt. Brigita kuelewa jinsi wazo hilo linavyotokana na umimi na linavyosahau wema wa Maria, ambaye hashindwi na yeyote katika ukarimu. Tukijinyima hivyo tutapokea mara mia. Upendo wenyewe, unaoshuhudiwa na tendo hilo, unatuondolea tayari sehemu ya tohara.

Wengine wanauliza tutafanyeje kuwaombea ndugu na marafiki kisha kumtolea Maria sala zetu zote? Jibu ni kwamba Bikira anajua wajibu wetu kwa ndugu na marafiki, na kama tungesahau kuwaombea angetukumbusha. Tena mara nyingi hatujui nani kati yao anahitaji zaidi kuombewa, kumbe Maria anajua na kutumia sala zetu kwa ajili yake. Hatimaye tunaweza kumuomba amsaidie fulani au fulani.

**MATUNDA YA HESHIMA HIYO**

Njia hiyo ya kumuendea Mungu ni *rahisi na inastahili zaidi,* kwa hiyo ni fupi, kamili na ya hakika zaidi.

Kwanza ni rahisi zaidi. “Kwa kusema ukweli tunaweza kuufikia muungano na Mungu kwa njia nyingine; lakini itakuwa kwa misalaba mingi zaidi sana na kwa vifo vya ajabuajabu na kwa matatizo mengi zaidi sana ambayo tutayashinda kwa shida kubwa zaidi. Itatupasa kupitia giza la usiku, mapambano na mafadhaiko yasiyosemekana, milima yenye magenge, misitu ya miba inayochoma na majangwa ya kutisha. Kumbe kwa njia ya Maria tunapita kwa utamu na utulivu mkubwa zaidi. Ni kweli kuwa huko vinapatikana vita vikali ambavyo tuvipige na matatizo makubwa ambayo tuyashinde, lakini huyo Mama mwema anawakaribia watumishi wake waaminifu ili kuwaangazia giza lao, kuwashauri katika wasiwasi wao, kuwategemeza katika mapambano na matatizo yao, kiasi kwamba njia hiyo ya Kibikira ya kumpata Yesu Kristo ni ya mawaridi na asali ukiilinganisha na nyingine”. Hiyo inathibitishwa na watakatifu waliofuata njia hiyo kwa namna ya pekee.

Ingawa njia hiyo ni rahisi zaidi, kwa kuwa Bikira anatutegemeza, haiachi kustahili zaidi, kwa kuwa Maria anatupatia upendo mkubwa ulio asili ya stahili. Matatizo ni nafasi ya kustahili, lakini asili ya stahili ndiyo upendo ambao tunayashinda. Maria kwa matendo rahisi alistahili kuliko wafiadini katika mateso yao yote, kwa jinsi alivyotumia upendo mwingi katika kuyatenda.

Njia ya Maria ni fupi zaidi, kwa maana tunaifuata kwa urahisi na hivyo tunakwenda kasi zaidi. Kwa muda mfupi wa kumfuata Mama wa Mungu tunasonga mbele kuliko kwa miaka ya kufuata busara yetu. Chini yake, ambaye Neno aliyefanyika mwili alimtii, tunapiga hatua za jitu.

Njia hiyo ndiyo kamili zaidi, kwa kuwa Neno alitushukia kwa njia ya Maria asipoteze chochote cha Umungu wake; basi kwa njia yake walio wadogo wanaweza kupanda vizuri kwa Aliye Juu wasiogope chochote. Mwenyewe anatakasa matendo yetu mema na kuzidisha thamani yake akiyatoa kwa Mwanae.

Hatimaye ndiyo njia ya hakika zaidi inayotunakinga dhidi ya udanganyifu wa shetani ambaye kwanza anajaribu kutupotosha kidogokidogo ili baadaye atufikishe kutenda makosa makubwa. Pia inatunakinga dhidi ya udanganyifu wa ndoto na hisia za moyoni, kwa kuwa Maria kama chombo cha neema anatuliza na kuratibu hisi zetu ili roho ipokee athari ya Bwana kwa manufaa zaidi. Tena Maria ni kiumbe kitakatifu: hivyo akizingatiwa na hisi zetu anainua roho iungane na Mungu. Anatupatia uhuru mkubwa wa ndani, na pengine tukimuomba kwa udumifu atatupatia neema ya kukombolewa mara na upotovu wa hisi unaozuia sala na muungano wa ndani na Bwana. Kila athari ya Maria inalenga kutufikisha huko, kama vile Yesu anavyotufikisha kwa Baba. Inafaa kuomba msaada wake wa pekee wakati na baada ya Komunyo, ili atushirikishe ibada yake ya dhati pamoja na upendo wake, kana kwamba tungeazima moyo wake safi tumpokee Yesu inavyotakiwa.

Kiini cha kujiaminisha kwa Yesu kwa mikono ya Maria ni kama ifuatavyo: “Ee Yesu mpendwa, unayestahili kuabudiwa, Mungu kweli na mtu kweli! Nakushukuru kwa jinsi ulivyojishusha kabisa ukitwaa namna ya mtumwa ili kunikomboa kutoka utumwa wa shetani… Nakimbilia maombezi ya Mama yako mtakatifu uliyenipa awe mtetezi wangu kwako; kwa njia hiyo natumaini utanijalia majuto na msamaha wa dhambi zangu, nipate na kutunza hekima. Nakusalimu Maria usiye na doa, malkia wa mbingu na nchi, ambaye vyote vilivyo chini ya Mungu viko chini yako. Nakusalimu, kimbilio la hakika la wakosefu, wewe ambaye huruma yako haimpungui yeyote: unitimizie hamu yangu ya kupata hekima ya Kimungu, na kwa lengo hilo pokea nadhiri na matoleo ninavyokutolea kwa unyonge wangu. Mimi, mkosefu nisiye mwaminifu narudia leo na kuthibitisha mikononi mwako ahadi za ubatizo wangu. Namkataa moja kwa moja shetani, fahari zake na mambo yake yote na kujitoa kabisa kwa Yesu Kristo, Hekima aliyefanyika mwili, ili nyuma yake nibebe msalaba wangu siku zote za maisha yangu. Basi, ili niwe mwaminifu kwake kuliko nilivyokuwa mpaka sasa, nakuteua Maria uwe Mama yangu. Nakuachia na kukukabidhi mwili wangu na roho yangu, mema yangu ya

ndani na vitu vya nje, hata thamani ya matendo yangu mema ya jana, ya leo na ya kesho… kwa hiyo uniweke miongoni mwa wale ambao unawapenda, unawafundisha, unawaongoza, unawalisha na kuwalinda. Ee Bikira mwaminifu, unifanye niwe katika yote mwanafunzi mkamilifu na mwigaji wa Hekima aliyefanyika mwili, Yesu Kristo Mwanao, hata nifikie kwa maombezi na mifano yako kwenye utimilifu wa ukomavu wake hapa duniani na wa utukufu wake mbinguni. Amina".

## 3.27. *KITABU CHA "KUMFUASA YESU KRISTO" KINAWAELEKEZA WOTE NJIA YA MAFUMBO*

"Kumfuasa Yesu Kristo" si kitabu cha teolojia, bali maisha halisi ambayo mtu aliyevutiwa na ukamilifu aliyaandika siku kwa siku kutokana na sala yake, pengine ya shida, pengine ya mwanga na utamu wa kimbingu. "Kina uzuri na nguvu ambavyo vinagusa na kutikisa na kuvutia sana mioyo dhaifu, isiyojali na hata isiyo na imani. Lakini walengwa asili si wakosefu, wala wanaoanza; kinadai wasomaji wawe wameendelea kiasi fulani katika uadilifu. Kinachotaka si kidogo, bali ni kutuinua tuzame katika mafumbo na kupata faraja za ndani za maisha ya muungano. Kwa kweli kuzama katika sala na kuungana kwa ndani na Mungu ndiko shabaha, lengo na haja ya dhati ya roho yetu, inayoweza kuona amani na pumziko ndani ya Mungu tu. Ndiyo sababu kila anayekisoma, hata akikosa kabisa ukamilifu na kukielewa kidogo tu, anaonja utamu wenye faraja asioweza kujielezea: kwa kuwa kinadokeza hiyo amani na hilo pumziko na kuelekeza roho iungane na wema mkuu" (pd. Dumas).

**"KUMFUASA YESU KRISTO" KINALENGA MAFUMBO**

*Ujuzi wa kifumbo* wa Mungu ni ule unaopatikana kwa kuzingatia mambo si kwa akili, wala kwa imani tupu, bali kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu katika sala ya kumiminiwa. "Ni ujuzi wa Mungu ambao unakaribia kuwa mang'amuzi" (Mt. Thoma wa Akwino) "Unatokana na athari ya Mungu ambayo inaifundisha roho kwa siri na kwa ukamilifu wa upendo, yenyewe isielewe hata ni kitu gani" (Mt. Yohane wa Msalaba).

"Kumfuasa Yesu Kristo" hakikomi kuhimiza unyenyekevu, kujikana na usikivu, ambavyo vinaandaa kumiminiwa sala hiyo na kuungana na Mungu: "Nimechoka kusoma na kusikia mengi mara kwa mara. Kwako napata yote ambayo nayatamani na kuyapenda. *Wataalamu wote wanyamaze;* viumbe vyote vikae kimya mbele yako. *Wewe peke yako unifundishe!* Kama mtu amezoea kujikusanya kwa ndani na kuwa mnyofu, ataelewa mambo mengi makuu pasipo shida; *kwa sababu akili yake inaangazwa na mwanga wa juu"* (I,3:1-3).

"Mtu gani ni huru kuliko asiye na tamaa duniani? Kwa hiyo ni lazima nipae juu ya viumbe vyote, na kujiachilia kabisa, niangalie mambo ya Mungu na kufahamu kwamba wewe Muumba hufanani na kiumbe chochote… Elimu ya mtu aliyejifunza kwa kazi yake ni tofauti sana na hekima ambayo mtu amepewa na Mungu katika sala. *Hekima hiyo imetoka juu; ndiyo kazi ya mwangazo wa Mungu;* ni bora sana kuliko elimu iliyopatikana kwa mtu kujisumbua akili yake. Wapo wengi wanaotamani miangazo ya roho, lakini hawapendi kujitendea yaliyopaswa kwa hali hiyo. Watu hao huzuiwa sana, kwa sababu hupenda mambo ya ajabu na kusikia utamu, bila ya kujitesa na kujikana barabara" (III,31:1-3).

Mbele Bwana anasema, "*Ndimi ninayemuelimisha mnyenyekevu kwa dakika moja tu ajue ukweli wa milele vema sana, kuliko kwa kufundishwa na mwalimu mwingine miaka kumi.* Mimi nafundisha bila ya mshindo wa maneno, bila ya kubishana kwa fujo, bila ya kutafuta sifa, bila ya kushindana. Ndimi nifundishaye kudharau malimwengu na kutupa furaha za sasa, kutaka mambo ya milele na kuyapenda, kuepa sifa za watu, kuvumilia dharau, kunitumikia mimi, kunipenda mimi peke yangu kwa moyo wote na kutotaka kitu ila mimi tu" (III,43:2). Sala ya kumiminiwa inayozungumziwa na kitabu hicho ni neema ya juu, lakini imo katika njia ya kawaida ya utakatifu; inatangazwa kuwa ya kutamaniwa kuliko yote: "Ndiyo niombayo, ndiyo nipendayo: tuungane kabisa sisi… nijifunze kuonja mambo ya mbinguni na ya milele… Ee Bwana Mungu, siku gani nitaungana nawe kabisa kama kuzama ndani mwako hata kujisahau? Wewe ndani mwangu, mimi ndani mwako; nipe tukae hivi sikuzote" (IV,13:1).

**MASHARTI, YAANI JUHUDI ZINAZODAIWA**

Kwa ajili hiyo, kitabu hicho kinadai hasa kujikana na unyenyekevu: "Ujifunze kuzivunja nia zako, ukakubali kutumikia kwa kila namna. Piga vita motomoto upate kujishinda, wala usikubali jipu la majivuno kuvimba rohoni mwako. Ujifanye mdogo na mnyenyekevu mpaka watu wote waweze kutembea juu yako wakukanyage kama takataka ya njiani" (III,13:2-3). Kujikana hivyo ni kufisha umimi ili kuwa mali ya Mungu, ni kutojifanya tena lengo la yote ili kumlenga yeye mfululizo. *"Mwanangu, ukitaka kupewa yote, ni sharti utoe yote bila ya kubakiza chochote kiwe mali yako"* (III,27:1): hapo utapata amani ya ndani.

Usafi wa moyo na nia nyofu inayomlenga Mungu tu vinamuandaa mtu kumiminiwa sala inayomfanya ajiaminishe kwake na kuungana naye: "Naomba huruma yako hata unijalie neema moja iliyo bora, yaani moyo wangu mgumu ulainike kabisa mbele yako, nijae upendo wako nisijitafutie tena kitulizo chochote kwingine" (IV,4:2). Hapo tunaelewa matokeo mazuri ajabu ya upendo wa Mungu ambao "huchukua mzigo pasipo kuona uzito, hugeuza machungu yote kuwa matamu na mazuri… huelekeza kutenda makubwa, na

kutamani makubwa zaidi… Hakuna kitamu kushinda upendo, wala chenye nguvu, wala cha ubora, wala kikubwa, wala kipendevu, wala kamili, wala kitimilifu duniani na mbinguni ila upendo tu. Upendo unatoka kwa Mungu, hauwezi kutulia isipokuwa kwa Mungu peke yake" (III,5:3). Kwa mtu aliyebandukana na yote na asiyejifanya tena lengo la chochote, muungano ndio tunda la kuzama katika wema mkuu.

Hivyo "Kumfuasa Yesu Kristo" kinaelekeza si kufanya juhudi tu, bali pia kuzama katika mafumbo, yaani kutimiza maadili ili kujaliwa muungano na Bwana. Maneno yake juu ya kuzama katika wema wa Mungu yanawafaa wote, mradi wakubali kufuata njia ya unyenyekevu, ya kujikana, ya kusali mfululizo na ya kuwa wasikivu kwa Roho Mtakatifu.

## 3.28. *SALA YA KUMIMINIWA*

Tuliyoyasema yanatuelekeza kufafanua sala ya kumiminiwa katika hatua ya mwanga.

### KUVUKIA SALA YA KUMIMINIWA KADIRI YA MT. FRANSISKO WA SALES

Tafakuri ni kazi ya akili inayotunga mawazo kadhaa ili kuchochea mapenzi kwa Mungu. Tukidumu katika njia hiyo, inakuja kuwa sala sahili ya mapenzi ambamo hatua mbalimbali za tafakuri zinaelekea kuungana. Hivyo tunainuliwa polepole hadi kuzama katika mafumbo, yaani *"kuzingatia kwa upendo, kwa usahili na kwa kudumu mambo ya Mungu":* hapo tunatazama kwa usahili sifa mojawapo ya Mungu au mwanga wake unaorudishwa na kazi yake fulani. Kwa hiyo "sala inaitwa tafakuri kabla haijatengeneza asali ya ibada: baada ya hapo inakuwa ya kumiminiwa… Kama vile nyuki wanavyofonza katika maua, vivyo hivyo sisi *tunatafakari ili kukusanya upendo wa Mungu, lakini kisha kuukusanya tunazama ndani ya Mungu na kuzingatia wema wake* kutokana na utamu ambao upendo unatuonjesha humo".

Tofauti hiyo ya kwanza inasababisha ya pili: "Tafakuri inazingatia kinaganaga na kama sehemusehemu mambo yanayoweza kutugusa moyo; kumbe sala ya kumiminiwa ni mtazamo sahili sana unaokazania kinachopendwa… Hatusimami tena juu ya kipengele hiki au hiki, bali tunafikia mtazamo wa jumla unaotulia ndani ya Mungu kwa mshangao na upendo, kama vile macho ya msanii yanavyotulia katika viumbe, au yale ya mtoto katika uso wa mama yake".

Tofauti ya tatu inatokana na hizo mbili: tafakuri inafanyika kwa uchovu, kumbe "sala ya kumiminiwa inafanyika kwa raha, maana inadai kwanza tumpate Mungu na upendo wake mtakatifu". Hata hivyo kuna saa za giza ambamo roho inasikitikia kumkosa kwa jinsi inavyomtamani, na ambamo katika jaribu inajiunga na matakwa yake.

*"Kwa kuwa sala ya kumiminiwa ndiyo lengo na shabaha ya vitendo vyote vya Kiroho, inavijumlisha vyote";* lakini *"namna hiyo ya kujikusanya* hatuisababishi kwa uamuzi wetu, kwa maana *hatuwezi kuwa nayo tunapotaka; haitegemei juhudi zetu ila Mungu anaitokeza ndani mwetu kwa neema yake takatifu anapotaka mwenyewe"*.

### MISINGI YA MAFUNDISHO HAYO KADIRI YA MT. THOMA WA AKWINO

Tendo lolote la kuzama kwa akili ni la juu kuliko mifuatano ya mawazo, *ni mtazamo sahili wa ukweli.* Lile linalozungumziwa na watakatifu *linatokana na upendo* na kuhitaji *uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu,* ambao vipaji vyake vinatuandaa kuupokea mara kama vile tanga za boti zinavyopokea msukumo wa upepo. Ndiyo sababu sala hiyo inastahili kuitwa *ya kumiminiwa,* ingawa mara nyingi inaandaliwa na somo, tafakuri na maombi. Kwa njia hizo mtu anajiandaa kupokea uvuvio wa Roho Mtakatifu, ambao pengine utakuwa na nguvu ya kutosha isihitaji tafakuri, kama vile upepo mzuri wenye nguvu za kusukuma boti unavyofanya kazi ya wapigakasia isihitajike tena.

Ili kutuonjesha mafumbo ya imani uvuvio huo maalumu unatumia mvuto wa mambo ya Kimungu unaotegemea upendo. "Ndio ukamilifu mkuu wa sala ya kumiminiwa, kwamba ukweli wa Kimungu usionekane tu, bali upendwe pia". Uvuvio huo unasababisha *tendo la kumiminiwa la upendo na la imani hai yenye kupenya na kuonja* linalotuonyesha jinsi mafumbo yaliyofunuliwa yanavyoitikia vizuri ajabu matamanio yetu ya juu na ya dhati zaidi ingawa bado yana giza kwetu. Matendo hayo ni ya kumiminiwa si kwa sababu tu yanatokana na maadili ya kumiminiwa, bali kwa sababu yanahitaji *uvuvio maalumu* wa Roho Mtakatifu, kwa kuwa hatuwezi kuyafikia kwa msaada wa neema za kawaida. Kwa mfano, tukisoma Injili, ghafla neno tulilokwishalisoma mara elfu linatuangaza na kutuvutia; au mhubiri akijitambua hawezi kusema inavyofaa juu ya mateso ya Yesu siku ya Ijumaa Kuu, kisha kuanza anapokea uvuvio unaohuisha akili yake, utashi wake na hisi zake kwa faida ya wasikilizaji.

Pengine mtazamo huo unainuka *wima* kwa Mungu, k.mf. kutoka tendo fulani au mfano wa Injili hadi kushangaa huruma ya Mungu. Pengine una *mwendo wa pia,* k.mf. kutoka mafumbo ya wokovu hadi wazo hai la dhati la uzima wa milele. Pengine tena ni mtazamo *wa mzunguko* wa wema usio na mipaka wa Mungu unaong'aa juu ya yote; ni mtazamo sahili uliojaa upendo, unaofanana na mruko wa tai juu hewani, anapokazia macho jua na uenezi wa mwanga wake.

**KUKUSANYIKA KWA KUJALIWA KADIRI YA MT. TERESA WA YESU**

Mpito kati ya sala ya kujipatia na ile ya kumiminiwa unaeleweka zaidi tukifuata maandishi ya Mt. Teresa kuhusu aina ya mwisho ya sala za kujipatia na ile ya kwanza ya sala za kumiminiwa.

Tusome alivyofafanua aina bora ya sala za kujipatia: "Inaitwa sala ya kujikusanya kwa sababu hapo *roho inakusanya vipawa vyake vyote na kujifungia ndani* pamoja na Mungu wake. Kwa njia hiyo Mwalimu wake wa Kimungu ataifundisha na kuijalia sala ya utulivu mapema kuliko kwa njia nyingine yoyote. Roho ikiwa imejificha ndani mwake inaweza kufikiria mateso, kujichorea Mwana wa Mungu na kumtolea Baba isihitaji kujichosha ikamtafute huko Kalivari, au bustanini pa mizeituni au mnarani. Watakaoweza *kujifungia* hivyo ndani ya mbingu ndogo za roho zao anamokaa Muumba wao… *watakaozoea kuzuia* macho yao, kusali mahali pasipo kitu kinachoweza kutawanya hisi za nje, wawe na hakika ya kufuata njia bora na ya kuweza kunywea chemchemi ya uhai. Hakika watasonga mbele sana kwa muda mfupi… Huko kujikusanya kama ni kwenyewe kunatambulikana kwa urahisi kwa njia ya tokeo lake fulani. Sijui namna ya kujieleza, lakini mwenye mang'amuzi hayo atanielewa vizuri. Tungesema kuwa roho, ikiona malimwengu ni upuuzi tu, inainuka ghafla na kuyaacha. Au kwamba mtu, akitaka kujihami na adui yake, anaingia ndani ya ngome. Hisi zinajikusanya mbali na vitu vya nje na kuvisogeza mbali kwa dharau sana, hata mtu bila ya kujitambua anakuja kufumba macho asivione tena na hivyo afanye mtazamo wa roho upenye zaidi. Kweli wanaofuata njia hiyo wanafumba macho karibu mfululizo wanaposali. Zoea hilo ni zuri ajabu pande zote… Tukidumu kujilazimisha muda fulani tutaona wazi faida itakayopatikana. Mara tutakapoanza kusali tutaona nyuki kuja kwenye mzinga na kuingia watengeneze asali. Hilo halina juhudi yoyote kwa sababu *roho* kama malipo ya yale iliyoyafanya kwanza *imestahili kutawala hivyo hisi kwa njia ya utashi.* Ikitoa tu ishara ya kutaka kujikusanya, hisi zinaitii na kujikusanya ndani yake… *Atakayetaka kujipatia zoea hilo, ambalo narudia kusema limo ndani ya uwezo wetu, asichoke kulifanyia kazi…* Mkijitahidi kweli mtafaulu kwa mwaka mmoja, na pengine kwa miezi sita. Je, si kidogo sana kwa faida kubwa namna hii? Tena kwa kufanya hivyo mnaweka msingi imara, na Bwana akipenda kuwainua kwenye makuu, atawakuta mko tayari, kwa kuwa mnabaki karibu naye zaidi". Ndivyo sala ya kujipatia inavyotuandaa kwa ile ya kumiminiwa.

Akafafanua hivi sala ya kwanza ya kumiminiwa: "Naona hiyo ni namna ya kukusanyika *ipitayo maumbile*. Kiini chake si kwenda gizani wala kufumba macho… Ingawa pasipo kutaka tunafumba macho na kutamani upweke. Inavyoonekana ndipo jumba la sala nililolizungumzia linapojengwa *pasipo kazi ya ufundi…* Msidhani huko kukusanyika kunapatikana kwa kazi ya akili, kwa kujitahidi kumfikiria Mungu ndani mwetu, au kwa kazi ya ubunifu, kwa kujichorea alivyo… *Si namna hiyo ya kutenda ambayo kila mmoja anaiweza,* bila ya shaka daima kwa msaada wa Mungu. Ninayoongelea ni tofauti. Pengine, hata kabla hatujaanza kumfikiria Mungu… *tunang'amua wazi kabisa utamu wa kukusanyika… Hilo halitegemei utashi wetu: linatokea tu Mungu anapotaka kutujalia neema hiyo.* Nadhani Mungu anachagua kuwajalia watu walioachana na malimwengu… Naamini pia *tukimuachia Mungu uhuru wake wa kutenda, hatazuia ukarimu wake* kwa wale anaowaita wazi kupanda juu zaidi". Asipojalia bado neema hiyo, haiwezekani "kufunga akili kwa faida kubwa kuliko hasara".

Hayo yote yanalingana na mafundisho ya Mt. Yohane wa Msalaba: "Katika *sala ya kumiminiwa* Mungu analisha na kuimarisha roho pasipo hiyo kuchangia kwa kazi au mawazo yoyote ya makusudi". Kwa hakika kazi ya maadili inatakiwa kuendelea, hata kwa matendo ya kishujaa, lakini sala inazidi kuwa sahili, na mtu anapaswa hasa kupokea kwa mikono miwili uvuvio wa Roho Mtakatifu.

"Huko kutazama gizani ndiyo teolojia ya mafumbo ambayo walimu wanaiita hekima ya siri, na ambayo kadiri ya mafundisho ya Mt. Thoma inashirikishwa kwa njia ya upendo kumiminwa rohoni". Huo utekelezaji bora wa maadili ya Kimungu na ya vipaji vinavyoendana nayo ukidumu muda fulani unaitwa *hali ya sala.* Ni hali ya kumiminiwa kwa sababu hatuwezi kuisababisha ila kujiandaa tuipokee, kwa kudumu katika sala, kubeba kila siku msalaba wetu na kuwa wasikivu kwa Roho Mtakatifu. Hapo imani hai inakuwa imani ya kupenya na mara nyingi imani ya kuonja, iweze kuishi kwa dhati mafumbo yaliyofunuliwa.

## 3.29. *UZUSHI KUHUSU SALA YA KUMIMINIWA NA KUHUSU UPENDO SAFI*

Mafundisho ya mapokeo tuliyoyaeleza yamethibitishwa na Kanisa kwa kulaani maneno kadhaa ya kizushi.

**UTULIVU WA MOLINOS**

Kadiri ya M. Molinos mtu anapaswa kunyamazisha vipawa vyake, kwa sababu *kutaka kutenda ni chukizo kwa Mungu anayetaka kutenda peke yake ndani mwetu.* Utendaji ni adui wa neema, nadhiri ya kutenda jambo ni kizuio cha ukamilifu, roho isipotenda inajiangamiza na kuirudia asili yake: hapo Mungu anatawala na kuishi ndani yake. Ndiyo njia ya Kiroho ambapo mtu hatendi kwa kumjua wala kumpenda Mungu, tena hafikirii uzima wa milele wala adhabu za motoni. Mtu hatakiwi kutamani ajue kama anampendeza Mungu au la, wala kufikiria matendo na makosa yake ili kujirekebisha; hatakiwi kutamani ukamilifu na wokovu wa milele, wala kumuomba Mungu neno maalumu; hahitaji kupambana na vishawishi, ila asivijali.

Kwa kufundisha hayo, *alifuta* kwa mkupuo mmoja *juhudi zote* na utekelezaji wa maadili ambayo ndiyo maandalizi halisi ya sala ya kumiminiwa na ya muungano na Mungu. Hivyo alipotosha maisha yote ya Kiroho.

**Mafundisho ya Kikatoliki**

1) Kuna *hali ya kutendewa* ambapo Mungu mwenyewe anatenda ndani mwetu; lakini *kwa kawaida* tunaifikia baada tu ya kutekeleza muda mrefu maadili na tafakuri.

2) Kwa kawaida tendo la sala ya kumiminiwa linadumu muda mfupi, ingawa hali ya roho inayotokana nalo inaweza ikadumu siku kadhaa.

3) Sala ya kumiminiwa, inayoendana na tendo la kumpenda Mungu, inatimiliza *maadili yote,* lakini haituruhusu tuache kuyatekeleza nje ya sala.

4) *Jambo kuu* ambalo tuzame ndani yake ni Mungu mwenyewe, lakini Yesu ndiye *la pili;* nje ya tendo la sala ya kumiminiwa tusiache kumfikiria mshenga huyo wa lazima wala kumuendea Mungu tusimpitie.

5) *Kujiachilia kitakatifu* ni njia kamili, lakini bila ya kufikia hatua ya *kutojali* wokovu wa milele; kinyume chake tunapaswa kuutamani, kuutumaini na kuuomba.

6) Katika majaribu ya Kiroho ubunifu na hisi vinaweza vikavurugika, huku sehemu ya juu ya roho ikifurahia amani; lakini utashi unapaswa daima kupinga vishawishi (walau kwa kutovizingatia au kwa kupoteza lengo) usije ukavikubali.

**Uzushi wa Molinos**

1) Kuna njia moja tu, yaani *sala ya kumiminiwa, ambayo tunaweza kujipatia* kwa neema ya kawaida tukikoma kutenda lolote. Basi tuiingie mapema iwezekanavyo.

2) Tendo la sala ya kumiminiwa linaweza kudumu miaka, hata maisha yote, usingizini pia, bila ya kuchochewa.

3) Kwa kuwa sala ya kumiminiwa ni ya kudumu, inaturuhusu tuache kutekeleza maadili (k.mf. imani, tumaini, ibada na toba); hayo yanawafaa wanaoanza tu.

4) Kumfikiria Yesu na mafumbo yake ni kasoro; kuzama katika umungu tu ni kwa lazima, tena kunatosha. Anayetumia picha au mawazo hamuabudu Mungu katika Roho na ukweli.

5) Katika hali ya sala ya kumiminiwa tunatakiwa kutojali lolote, hata utakatifu na wokovu wetu, bali tupoteze tumaini ili upendo usiwe wa kujitafutia faida.

6) Tusisumbuke kupinga vishawishi: mawazo na matendo machafu ni majaribu yaliyowapata watakatifu pia; hayana lawama kwa kuwa ni kazi ya shetani, hivyo hatutakiwi kuyaungama. Ndivyo tunavyofikia kujidharau na kuungana kwa ndani na Mungu.

## UTULIVU UPANDE

Utulivu upande uliangukia uzushi kuhusu upendo safi. Kosa lake kuu lilikuwa kufundisha kwamba, katika hali ya sala kamili ya kumiminiwa, mtu anaingia aina ya maangamizi matimilifu, ambapo yuko mbele ya Mungu akikubali matakwa yake matakatifu, asijali kuokoka wala kulaaniwa.

Hivyo wajibu wa tumaini la Kikristo ulipuuzwa, kwa kusahau kwamba kujinyima hamu ya wokovu ni sawa na kujinyima upendo wenyewe unaotuelekeza kumtukuza Mungu milele. Maagizo yake kuhusu tumaini na upendo hayapingani, bali yanaimarishana. Kwa njia ya tumaini tunatamani kumpata Mungu bila ya kumfanya chombo chetu; kwa njia ya upendo, unaohuisha tumaini usiliangamize, tunampenda Mungu kwa ajili yake, hivyo tunatamani wokovu wetu na wa wengine ili atukuzwe milele.

Makosa hayo yanajumlishwa katika manne yafuatayo (tumeyapigia mstari yaliyo ya kizushi hasa): 1) Katika maisha haya kuna *hali ya kudumu* ya upendo safi ambapo *hapana tena hamu ya wokovu wa milele.* 2) Katika majaribu ya mwisho ya maisha ya Kiroho mtu anaweza akawa na hakika *isiyoshindikana* ya kwamba anastahili kulaaniwa na Mungu, na kwa hakika hiyo *akajinyima* heri ya milele. 3) Katika hali ya upendo safi mtu *hajali ukamilifu wake wala matendo ya maadili.* 4) Wanasala hasa katika hali kadhaa wanapotewa na *mtazamo maalumu* wa kihisi na wa kimawazo kwa Yesu Kristo.

Ukweli ni kwamba: 1) Katika waliokamilika hamu ya heri inahuishwa mara nyingi na upendo, na kuna *nafasi* ambapo hawafikirii wazi wokovu wao. 2) Ikiwa mtakatifu fulani alihisi atalaaniwa, haikuwa hakika ya mawazo; tena ikiwa alijinyima wokovu wake, alifanya hivyo *kwa sharti* tu, si *moja kwa moja.* 3) Hata katika hali za juu za ukamilifu, watakatifu wanahimiza kushughulikia *maendeleo ya roho* na *maadili muhimu zaidi.* 4) Hata katika muungano unaotugeuza, watakatifu wengi walijaliwa kuuona *ubinadamu wa Mwokozi,* ila katika nafasi kadhaa mtu aliyezama ndani ya Mungu hamfikirii Yesu wazi.

## SUALA LA UPENDO SAFI

Je, upendo wetu kwa Mungu utaathiriwa na umimi daima? Je, upendo safi unawezekana? Ukiwezekana,

unahusiana vipi na pendo la nafsi yetu lililo kiini cha maelekeo ya umbile letu? Aina za udanganyifu za kuepwa zinapingana; ukweli unainuka kama kilele kati na juu ya hizo.

Ni kwamba elekeo la umbile letu la kumpenda *Mungu kama asili ya uhai wetu* limepunguzwa na dhambi (ya asili na za binafsi), lakini linadumu ndani ya utashi wetu, na adili la upendo linaliinua upya tumpende *Mungu kama asili ya neema* kuliko tunavyojipenda. Kwa hiyo, *tukipenda kiadilifu sehemu ya juu ya utu wetu, tunampenda zaidi Muumba wetu;* kumbe tusipotaka ukamilifu wetu tunasogea mbali naye.

Katika matakaso ya Kimungu upendo kwa Mungu na kwa jirani unazidi kuwa safi mpaka upendo motomoto wa ari kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa watu ushinde kabisa umimi.

**UTEKELEZAJI WA UPENDO SAFI**

Ni kujiachilia kwa maongozi ya Mungu kuhusu mambo yajayo: tendo hilo linatokana na imani, tumaini na upendo kwake ulio safi kila siku zaidi. Watulivu walidanganyika walipoondoa tumaini katika ukamilifu: kinachotakiwa tu ni kwamba liwe chini ya upendo na kuhuishwa nao, hatimaye liwe la kishujaa "kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa" (Rom 4:18). Walidanganyika pia walipoondoa katika ukamilifu juhudi za kutekeleza maadili na kushinda vishawishi. Hawakuzingatia *kujiachilia kwa matakwa ya Mungu yasiyo wazi bado* kunavyotakiwa kuendane na *utekelezaji wa matakwa ya Mungu yaliyokwishadhihirishwa na amri, mashauri na matukio.* Uaminifu wa kudumu kwa matakwa hayo yanayodhihirika nukta baada ya nukta, ndio unaotuwezesha kujiachilia kwa ukweli, tumaini na upendo kwa yale yajayo.

Tendo la upendo safi linaweza kutazamwa namna tatu: 1) kama tendo la pekee na la nadra; 2) kama tendo la kudumu; 3) kama tendo la kawaida analoliweza kila Mkristo.

1) Tendo la pekee na la nadra la upendo safi ni muungano wa ndani na wa juu na Mungu unaopatikana tu katika waliokwishatakata, ambao kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu hawafikirii tena heri yao kwa namna wazi.

2) Utekelezaji wa mfululizo wa tendo hilo la upendo safi unawezekana mbinguni tu.

3) Tendo la kawaida la upendo safi wanaloliweza Wakristo wote ni lile la kumpenda Mungu *kwa kumthamini* kuliko yote na kuelekea kumpenda *kwa dhati* kuliko yote huko mbinguni.

## 3.30. *NGAZI ZA SALA YA WANAOENDELEA*

Sasa tuzingatie ngazi za sala ya kumiminiwa kwa wanaoendelea zilizofafanuliwa na Mt. Teresa wa Yesu.

**MAENDELEO YA SALA NA YA MAADILI**

Ngazi za sala ya kumiminiwa ni zile za *ustawi wa mfululizo* wa imani, upendo na vipaji vya Roho Mtakatifu. Kwa namna fulani ustawi huo wa muungano na Mungu unadhihirika kwa hali hiyo *kuzidi kuenea* katika vipawa mbalimbali, ambavyo polepole vinavutwa na Mungu hata ikakoma mitawanyiko ya mawazo inayotokana na ubunifu usiotulia wala kuratibika. Zaidi ya hayo, *maadili kwa kawaida yanastawi kadiri sala inavyoendelea.*

Mt. Teresa ametuonyesha hayo akifananisha ngazi za sala na namna nne za kumwagilia bustani. Ya kwanza ni *kutoa maji kisimani kwa nguvu ya mikono tu;* ni mfano wa tafakuri yenye mifuatano ya mawazo inayochangia ustawi wa maadili. Ya pili ni kupandisha maji kwa *chombo cha kurahisishia uvutaji wa kamba;* ni mfano wa sala ya utulivu inayoandaliwa na kazi yetu: hapo maua ya maadili yanakaribia kuonekana. Ya tatu ni kupitisha bustanini *maji ya mto;* katika sala hiyo maadili yanapata nguvu nyingi kuliko awali na maua yake yanachanua. Ya nne ni *mvua,* mfano wa sala ya muungano ambayo Mungu anamjalia mtu pasipo huyo kuchoka: "katika sala hiyo anachota mema mengi zaidi sana na unyenyekevu wake unakua. Ndipo vinapotokea ahadi na maazimio ya kishujaa, hamu motomoto, chuki kwa ulimwengu, mtazamo wazi wa ubatili".

Mt. Yohane wa Msalaba alisema vilevile, akionyesha katika usiku wa hisi mwanzo wa sala ya kumiminiwa pamoja na hamu kubwa ya Mungu: ni *utulivu mkavu* unaoandaa ule mtamu ulioelezwa na Mt. Teresa katika makao ya nne.

**SALA YA UTULIVU**

Katika utulivu mtamu, unaoitwa pia sala ya nderemo za Kimungu (aina ya pili ya umwagiliaji), *"utashi tu umetawaliwa"* na nuru ya uhai inayodhihirisha uwemo mtamu wa Mungu ndani mwetu na wema wake. Hapo kipaji cha ibada kilichomo ndani ya utashi kinauelekeza kumpenda kitoto. Ni kama mtoto mchanga anayeonja maziwa anayopewa, au vizuri zaidi ni kama bubujiko la maji hai ambayo "yanatokana na chemchemi yenyewe, yaani Mungu… yanatiririka kutoka kina cha undani wetu kwa amani, utulivu na utamu mkuu… Maji hayo ya mbinguni yakianza kububujika kutoka chemchemi yake… mara ni kana kwamba undani wetu wote unatanuka na kupanuka. Hapo yanatujia mema ya Kiroho yasiyosemekana, na mhusika hawezi kuelewa anayoyapata wakati huo".

Lakini katika hali hiyo akili, kumbukumbu na ubunifu havijatawaliwa na kazi ya Mungu: pengine vinasaidia na kutumikia utashi, pengine vinauvuruga tu. Hapo utashi usivijali kuliko "jinsi ya kumshughulikia kichaa".

Ingawa mara nyingi huo utulivu mtamu unakatizwa na ukavu na majaribu ya usiku wa hisi, na vishawishi vinavyodai vipingwe kwa nguvu, matokeo yake ni uadilifu mkubwa zaidi, hasa upendo mkubwa zaidi kwa Mungu na amani isiyovurugika, walau katika sehemu ya juu ya roho.

Sala ya utulivu ina hatua tatu: 1) *mtu kujikuta anakusanyika,* hali ambayo ni neema ya pekee ya kufyonza matakwa ya Mungu kwa utamu na upendo; 2) *utulivu wenyewe* ambapo utashi unapatwa na Mungu ukiwa unabaki kimya au unasali kama umelewa Kiroho; 3) *usingizi wa vipawa* ambapo, utashi ukiendelea kutawaliwa na Mungu, akili inaacha kufuata mawazo na inakuja kupatwa na Mungu vilevile, ingawa kumbukumbu na ubunifu vinaendelea kutikisika.

La kufanya katika hatua hizo ni kujiachilia kwa unyenyekevu mikononi mwa Mungu. Mtu asijaribu kuingia hali hiyo, inayoweza kutokana tu na neema maalumu ya Roho Mtakatifu ambaye mara anatuelekeza kunyamaza kwa upendo, mara kububujika mapenzi kama maji ya chemchemi. Ikiwa akili na ubunifu vinatawanyika, hakuna haja ya kuhangaika au kuvifuatia; utashi uendelee kufurahia fadhili uliyojaliwa, kama nyuki katika chumba cha mzinga.

**SALA YA MUUNGANO SAHILI**

Mtu akiwa mwaminifu – si tu katika kutimiza kwa makini wajibu wowote wa kila siku, bali pia katika kusikiliza minong'ono ya Roho Mtakatifu anayezidi kudai kadiri anavyofadhili – basi kwa kawaida anainuliwa hadi ngazi ya juu inayoitwa ya "muungano sahili". Hapo kazi ya Mungu inakuwa na nguvu za kutosha *ivute vipawa vya roho* ambayo kazi yake yote inakuja kumuelekea yeye badala ya kupotea nje. Si utashi tu unatawaliwa naye, bali pia akili na kumbukumbu, hata mtu ni kama ana hakika ya uwemo wa Mungu. Ubunifu hautikisiki tena, bali unatulia; pengine ni kama umesinzia ili kuacha akili na utashi viungane na Mungu. Hapo neema ya pekee ya Roho Mtakatifu ni kama maji yanayotiririka toka mtoni.

Inatokea pia kwamba utendaji wote wa roho uende upande wake wa juu, hata kuna kusimamishwa kwa muda kwa hisi za nje, yaani *mwanzo wa kutoka nje ya nafsi* kama si kutoka kwenyewe. Ikiwa pengine mtaalamu aliyezamia somo lake hasikii anachoambiwa, zaidi tena itamtokea mtu aliyevutiwa na Mungu. Hapo anapokea maji hai ambayo yanaburudisha na kutakasa kama *mvua* toka mbinguni. "Mungu hamuachii kutoa mchango mwingine isipokuwa ule wa utashi uliotawaliwa kabisa… Jinsi ilivyo nzuri hali inayompata kisha kuzama katika ukuu wa Mungu na kuungana kabisa naye, ingawa kwa muda mfupi, kwa sababu nionavyo mimi muungano huo haufikii kamwe nusu saa!"

Mt. Teresa anasema pia hiyo sala ya muungano mara nyingi *si kamili, yaani ubunifu na kumbukumbu havisimamishwi,* bali vinavipiga vita akili na utashi: "Kwa muungano tunaouzungumzia hapa, je, ni lazima vipawa hivyo visimamishwe? Hapana. Bwana anaweza kuwatajirisha watu kwa njia mbalimbali na kuwafikishia makao hayo bila ya kuwapitisha *njia ya mkato* niliyoielekeza", yaani utamu wa kutokuwa na mitawanyiko ya mawazo, wa kutochoka na wa kusikia nderemo kwa wingi.

Matokeo ya sala ya muungano ni mtu kubadilika kama mdudu anapokuwa kipepeo. Anasikia *majuto makubwa kwa makosa yake;* anapata *ari motomoto* ya kumtumikia Mungu na kumtangaza ili apendwe; anaumia kuona wakosefu wakipotea;anahisi mateso ya Bwana yalivyokuwa. Hapo anaanza kutimiza maadili kishujaa, hasa kutii kikamilifu matakwa ya Mungu na kumpenda jirani. Pengine wafiadini walijaliwa sala hiyo katikati ya mateso yao.

Sala ya utulivu mtamu na ya muungano sahili zinapatikana kati ya matakaso ya Kimungu ya hisi na roho. Maana kwa kawaida kuna kipindi cha utulivu katika ya hayo mawili, yaani usiku wa hisi (mwanzo wa makao ya nne) na usiku wa roho (makao ya sita) tutakaouona katika sehemu ya nne tutakapoeleza muungano mkavu na muungano wa kutoka nje ya nafsi hadi kufikia muungano unaotugeuza.

Waliyoyasema walimu wa Kiroho kuhusu sala ya kumiminiwa si ya juu mno kwa mtu anayefuata njia ya unyenyekevu na kujikana, akizidi kuelewa kwamba Mungu "amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi; na wanyonge amewakweza" (Lk 1:52). Si ya juu mno kwa mtu anayeamini kwamba katika ubatizo amepokea *mbegu ya uzima wa milele,* na anayetambua haja ya kuzidi kusadiki thamani isiyo na mipaka ya ekaristi. Muhimu ni *kupokea toka kwa Mungu yale yote anayotaka kutupatia* kwa huruma yake isiyo na mipaka ili kutuvuta kwake na kutushirikisha milele uzima wake wa ndani na heri yake isiyo na mwisho.

## 3.31. *MASUALA YANAYOHUSU SALA YA KUMIMINIWA*

**SUALA KUU**

Wote wanakubali kwamba mtu yeyote anaweza *akatazama ukweli kwa usahili,* pasipo mifuatano ya mawazo, k.mf. kuuona katika viumbe wenye mchanganyiko na mabadiliko uwepo wa uhai wenyewe, ulio sahili tu, usiobadilika, ulio asili na lengo la vyote. Thibitisho zote za falsafa kuhusu uwepo wa Mungu zinalenga kilele hicho, ambacho akili inaweza kukifikia kwa nguvu zake na msaada wa kawaida wa neema.

Lakini kuhusu mtazamo sahili wa Kikristo, unaotegemea kupokea kwa imani ufunuo wa Mungu, walimu wa Kiroho wana maana gani wanapoutofautisha na tafakuri? Mbona tafakuri ya Kikristo pia inahusu kweli za

imani na yanayotokana nazo? Jibu ni kwamba, "sala hasa ni ujuzi wenye upendo kumhusu Mungu tunaomiminiwa" (Mt. Yohane wa Msalaba), ujuzi ambao haututeki daima, bali pengine unaendana na mitawanyiko ya mawazo na ukavu wa matakaso ya Kimungu. Ni tofauti na tafakuri inayotegemea mifuatano ya mawazo hata inapozidi kuwa sahili.

Kisha kutafakari tunaweza tukafikia *kumjua Mungu na kazi zake kwa usahili na upendo kama tunda la juhudi zetu zikisaidiwa na neema.* Mtazamo huohuo wanaweza kuwa nao: mwanateolojia akijumlisha aliyoyajua kwa utafiti wake; au mhubiri anayeona hotuba yake yote katika wazo kuu; au msikilizaji wake anayeshangaa umoja wa maneno yake na kufurahia mwanga wa ukweli. Huo unatokana na imani ikiendana na upendo, tena na athari wazi kidogo za vipaji vya akili, hekima na elimu; lakini usingekuwepo bila ya kazi ya kupanga vizuri mawazo ili kuonyesha yanavyolingana. Mkristo anayefikiria ukweli fulani wa imani anaweza akafikia *tafakuri sahili ya kimapenzi, aina ya sala ya kimapenzi au sala ya kujikusanya kwa makusudi,* ambapo asimame muda mfupi kutazama kwa usahili na mshangao wema wa Mungu au maongozi yake au stahili za Mwokozi; halafu akarudia mifuatano ya mawazo na mapenzi.

Kumbe toka tafakuri tunaweza tukavukia "hali ambayo Mungu anajishirikisha kwa mtu asiyetenda lolote, kama mwanga unavyomfikia mwenye macho wazi" (Mt. Yohane wa Msalaba). Sala hiyo ya kumiminiwa *si tunda la utendaji wa mtu kwa msaada wa neema, bali la uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu.* Kwa mfano, katika hotuba ya kukinaisha tu, linatajwa neno la Bwana linalokuja kumgusa na kumteka mtu fulani: hilo ni tendo la wazi la sala ya kumiminiwa, kwa sababu yeye *hawezi* kulisababisha kama anavyoweza kutekeleza imani namna ya kawaida. Tendo hilo ni la pekee, linatokana na imani yenye kupenya na pengine hata kuonja, ambamo kiongozi stadi anatambua mapema athari za vipaji vya akili na hekima. Ingawa hatuwezi kulisababisha, tunaweza *kujiandaa* kupokea *uvuvio wa Kimungu* unaolisababisha, na tunaweza kuufuata. Hivyo *tendo la upendo wa kumiminiwa* ni la hiari na lenye kustahili kutokana na usikivu kwa Roho Mtakatifu ulionalo.

Hiyo sala ya kumiminiwa inaanza mtu anapojikuta akikusanyika katika usiku wa hisi. Hali hiyo ikidumu na kujirudiarudia, mtu ameshaingia maisha ya mafumbo.

**UMBILE LA SALA YA KUMIMINIWA**

Sala ya kumiminiwa haitokani tu na maadili ya kumiminiwa, bali ni *tendo la kumiminiwa la ujuzi linaloendana na upendo wa kumiminiwa,* tusiloweza kulitenda wenyewe kwa msaada wa neema ya kawaida. Kwa baadhi unatawala upendo, kwa baadhi mwanga. "Ujuzi huo wenye giza unaitwa wa siri, na Mt. Thoma alisema *unashirikishwa na kumiminwa na upendo rohoni.* Unashirikishwa kwa siri, pasipo mchango wa utendaji wa kimaumbile wa akili wala wa vipawa vingine. Kwa kuwa hivyo *haviwezi kuupata, ila Roho Mtakatifu ndiye anayeumimina rohoni kwa fadhili,* ndiyo sababu ni wa siri kweli" (Mt. Yohane wa Msalaba). Kwa uvuvio huo toka juu imani hai inazidi kupenya na kuonja.

Basi, *tofauti* kati ya sala ya kumiminiwa na tafakuri yoyote si ya *ngazi* tu bali ya *maumbile.* Kwa kuwa tafakuri inategemea *uwezo wetu,* inatokana na utendaji wetu ukisaidiwa na neema ya kawaida; athari ya vipaji vya Roho Mtakatifu ikiwepo, siyo inayoisababisha, bali inaisaidia tu, kama kazi ya wapigakasia inavyosaidiwa na upepo wa kuwaburudisha. Kinyume chake sala ya kumiminiwa *haitegemei uwezo wetu,* bali uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu ambao si neema kubwa ya msaada, bali *unaendesha* kwa kufuata kanuni ya juu. Ndivyo vilivyo tofauti maadili ya kumiminiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu. Maadili ya kumiminiwa ni asili ya matendo tunayoweza kuyasababisha, kumbe vipaji vinatuandaa kupokea kwa mikono miwili msukumo wa Roho Mtakatifu kwa matendo ambayo *namna yake ipitayo maumbile* na itokanayo na *kanuni ya juu* inazidi utendaji wetu unaosaidiwa na neema ya kawaida.

Katika maisha ya juhudi, kabla ya takaso la Kimungu la hisi lililo mwanzo wa sala ya kumiminiwa, vipaji vya Roho Mtakatifu vinaathiri kidogo tu, na mara nyingi ni kama *vimefungwa* na ambatano fulani na dhambi nyepesi. Baadaye, katika maisha ya mafumbo vipaji vya akili na hekima vinakuja kuonekana: kwa baadhi ya watu hasa kwa namna ya kutazama ukweli, kwa baadhi kwa namna inayoelekea zaidi utendaji.

Matendo ya sala ya kumiminiwa *hayana mifuatano ya mawazo hata kidogo,* bali ni mtazamo sahili; pengine ni matulivu kiasi kwamba mhusika hayaoni, tofauti na yale anayoyakusudia. Kwa hiyo Mt. Antoni abati alisema, "sala si kamili mkaapweke akijitambua anasali". Ndio "ujinga wenye ujuzi" uliozungumzwa na walimu wa Kiroho. Matendo manyofu ya sala ya kumiminiwa hayana uvivu wowote wa hatari, bali ujuzi wa dhati wa ukweli wa Mungu. Ikiwa mtu, kisha kusali hivyo, anajikuta mnyenyekevu, mtulivu, amebandukana na yote, ana ari kwa utekelezaji wa maadili, maana yake hakupoteza muda wake.

**MAENDELEO YA SALA YA KUMIMINIWA**

Mt. Teresa alieleza maendeleo ya sala ya kumiminiwa kwa kusisitiza *uenezi* wa *utawala* wa Mungu juu ya *vipawa vya roho,* kimoja baada ya kingine, lakini alijua kuwa *tukio* la ubunifu na hisi *kusimamishwa si la msingi wala la lazima*, kwa sababu katika hali kamili kupita zote, yaani muungano unaotugeuza, mtu kwa kawaida hatoki tena nje ya nafsi yake. Hivyo *uenezi* si mamoja na *udhati,* ila ni dalili rahisi kutambulikana na kuelezwa; inafaa mradi iendane na nyingine ya ndani zaidi, yaani *matakaso ya Kimungu* yanayoonyesha

maendeleo makubwa katika kumjua na kumpenda Mungu na katika maadili mengine.

Basi sala ya kumiminiwa inaanza na takaso la Kimungu la hisi, ambalo ni uongofu wa pili katika utulivu mkavu, inaendelea na nderemo za hatua ya mwanga, inapenya zaidi wakati wa usiku wa roho katika majaribu makali dhidi ya maadili ya Kimungu, ambapo maadili hayo na unyenyekevu yanatakata na kuwa ya kishujaa kweli, hata mtu anakuwa tayari kwa muungano unaotugeuza ulio kilele cha sala ya kumiminiwa.

**MAMBO YASIYO YA LAZIMA KWA SALA YA KUMIMINIWA**

Mambo muhimu yafuatayo yanatokana na yale tuliyoyasema:

1) Sala hiyo, katika ngazi zake, haileti furaha daima: *kwa kawaida inaanza katika ukavu wa hisi* na inaweza *kudumu katika ukavu mkubwa wa roho.* Vilevile si lazima iondoe uwezo wa kupanga mawazo: ni *ya juu kuliko mifuatano ya mawazo,* lakini kwa sababu hiyohiyo *inaweza kuiongoza kutoka juu,* k.mf. wakati wa kuhubiri au kuandika.
2) Kuzama katika mafumbo kunaleta pengine *utambuzi wa uwepo wa Mungu* (ujuzi unakaribia kuwa mang'amuzi kutokana na kipaji cha hekima), pengine *kiu kubwa ya Mungu* pamoja na uchungu mwingi kwa kutoweza kumfurahia na hisi kali ya *kuwa mbali naye kimaadili* na Kiroho (hasa katika usiku wa roho, ambapo upenyaji wa kipaji cha akili unajitokeza kuliko mwonjo wa kipaji cha hekima). Katika hali hiyo ya mwisho ujuzi wa kumiminiwa na upendo wa kumiminiwa vinasababisha *uchungu mkali* kwa kuona Mungu hapendwi inavyotakiwa. Uchungu huo na kiu hiyo haviwezi kuwepo pasipo athari ya dhati ya neema: hivyo ni uwemo mchungu wa Mungu.
3) Sala ya kumiminiwa *haidai mawazo ya kumiminiwa* kama yale ya malaika, ila mwanga wa kumiminiwa, yaani mwanga maalumu wa vipaji ambavyo ni tofauti na karama zinazotolewa hasa kwa faida ya wengine (k.mf. kutabiri au kupambanua roho).
4) *Yenyewe si kumhisi moja kwa moja Mungu alivyo,* lililo jambo maalumu la heri ya milele. Kwa athari kubwa ya kipaji che hekima, uwemo wa Mungu unajulikana pasipo mifuatano ya mawazo, kwa njia ya matokeo yake, hasa *upendo wa kitoto anaotuvutia kwake* na utamu wa upendo anaouonjesha mara kadhaa.
5) *Tangu hapo maisha ya Kiroho yanatawaliwa na namna ipitayo maumbile ya vipaji vya Roho Mtakatifu,* hasa kile cha hekima kinachoviangaza vingine; utawala huo umekuwa *unajirudiarudia na ni wazi* kwa kiongozi stadi. Hata hivyo, katika usiku wa hisi kipaji cha elimu ndicho kinachotawala kikionyesha ubatili wa malimwengu; halafu katika usiku wa roho tunakuta hasa kipaji cha akili kikipenya mafumbo, pasipo kuonja ladha yake kwa kipaji cha hekima, kinachojitokeza katika ustawi wake wote wakati wa muungano unaotugeuza tu. Hatutakiwi kuichanganya hali ya kuzama katika mafumbo kwa jumla na vipindi vyake vyenye faraja, wala kuichanganya na utimilifu wake, kwa kura mara nyingi ina namna ya utulivu mkavu.

**WITO WA KUMIMINIWA SALA**

Je, wanaoishi Kiroho wanaitwa wote kwa jumla na kwa mbali kumiminiwa sala? Tunajibu "ndiyo" kwa kufuata mafundisho *juu ya vipaji vya Roho Mtakatifu* wanavyojaliwa waadilifu wote, na juu ya *matakaso ya Kimungu* yanayohitajika kufikia ukamilifu wa Kikristo unaotupasa wote kuulenga. Sababu kuu za jibu hilo ni tatu, nazo zinahusu mzizi, maendeleo na lengo la maisha ya Kiroho.

*Sababu ya kwanza: mzizi wa kumiminiwa sala ni uleule wa maisha ya Kiroho ya kawaida, yaani neema ya maadili na vipaji.* Basi, *kwa kawaida usikivu* kwa Roho Mtakatifu *kadiri ya namna ipitayo maumbile* ya vipaji *unatakiwa kuja kumtawala* mtu anayeendelea, ili ufidie upungufu wa kudumu wa namna ya kibinadamu ya maadili na ya utendaji wetu ukisaidiwa na neema za kawaida. Basi, maisha ya kuzama katika mafumbo, ambayo sifa zake maalumu ni huo *usikivu* na hiyo *namna ipitayo maumbile* ya kumiminiwa ujuzi wenye upendo, *kwa kawaida* yanajitokeza kwanza katika hatua ya mwanga, halafu hasa katika ile ya muungano.

*Sababu ya pili: katika maendeleo* ya maisha ya Kiroho *utakaso haukamiliki pasipo matakaso ya Kimungu,* ambayo yamo upande wa mafumbo*,* kwa kuwa *sala ya kumiminiwa* inaanza na takaso la Kimungu la hisi, halafu inapanda juu katika usiku wa roho. Hapo Roho Mtakatifu anatakasa unyenyekevu na maadili ya Kimungu akitokeza sababu za Kimungu za maadili hayo, yaani ukweli mkuu unaojifunua, huruma yenye enzi zote inayosaidia, na wema wa kupendeza kupita yote. Basi, matakaso hayo ni sehemu za *njia ya kawaida ya utakatifu* na yanawaondolea haja ya kupitia toharani wale wanaoyavumilia kwa moyo. "Ni lazima kupitia usiku wenye giza wa kutakaswa ili kuja kukamilika" katika muungano unaotugeuza ambapo "hakika mtu hasumbuliwi tena na shetani, ulimwengu, mwili na tamaa; hata anaweza kukariri maneno ya Wimbo ulio Bora (2:11-12), 'Kaskazi imepita, masika imekwisha, imekwenda zake; maua yatokea katika nchi'" (Mt. Yohane wa Msalaba).

*Sababu ya tatu: lengo la maisha ya Kiroho ni lilelile la maisha ya mafumbo,* yaani heri ya kumuona Mungu milele, na upendo wa kudumu unaotokana nayo. Basi, maisha ya kuzama katika mafumbo *yanasogeza karibu* zaidi na lengo hilo kuu, ni kama *utangulizi* wake, inavyothibitishwa na heri, zilizo matendo bora yatokanayo na maadili na vipaji. Hivyo maisha ya mafumbo, ambayo sifa yake maalumu ni kumiminiwa na Mungu tendo la kumjua na kumpenda, yanaonekana tena sehemu ya njia ya kawaida ya utakatifu. "Sala

takatifu ya kumiminiwa ndiyo lengo lenyewe la mazoezi yote ya Kiroho" (Mt. Fransisko wa Sales). "Ni kosa letu tu tusipoonja kamwe utamu usiosemekana wa kumiminiwa sala" (Y. Alvarez de Paz).

Mafundisho hayo yanatuelekeza kukiri kwamba wanaoishi Kiroho *wanaitwa wote kwa jumla na kwa mbali* kumiminiwa sala. "Lakini nawaungamia kuwa *wachache sana kati yetu wanajiandaa* kumuona Bwana, kuvumbua lulu azizi tunayozungumzia… Lo! Jinsi tunavyohitaji kukomesha ulegevu wowote tulionao" (Mt. Teresa wa Yesu). Wasiwasi kuhusu *wito wa binafsi na wa karibu* wa kumiminiwa sala unatokana na kwamba *"watu wengi wanakataa kuvumilia ukavu na ufishaji hata uwe mdogo namna gani,* badala ya kutenda kwa subira isiyoshindikana. Hapo Mungu haendelei kuwatakasa kwa dhati" (Mt. Yohane wa Msalaba). Hakika, si waadilifu wote wanaitwa binafsi na kwa karibu wamiminiwe sala kwa kuwa *dalili tatu* za wito huo hazipatikani ndani yao wote. Hatimaye wito unaweza kuwa *wa kutosha* na hata hivyo usizae kutokana na ulegevu wetu; kinyume chake unaweza kuwa *wa hakika* kwa kiasi mbalimbali, hata kutufikisha ama kwenye ngazi za chini ama kwenye zile za juu za sala ya kumiminiwa.

Kutokana na hayo, *hamu ya kumiminiwa sala ni halali* kwa wote, mradi wabaki wanyenyekevu na kumuachia Mungu apange wakati wa kuwajalia. Kwa mkulima ni halali kutamani na kuomba mvua itakayootesha mbegu alizozipanda, mradi ayaachie maongozi ya Mungu. Ikiwa sala yoyote inatakiwa kuwa kwa pamoja nyenyekevu, yenye tumaini na udumifu, ni hivyo pia kwa ile tunayoomba ujuzi hai na wa dhati zaidi wa mafumbo tuliyofumbuliwa: Maandiko matakatifu yana sala hiyo sehemu mbalimbali.

**UONGOZI WA ROHO KUHUSU SALA YA KUMIMINIWA**

*Kabla dalili yoyote haijaonyesha wito wa karibu wa mtu kumiminiwa sala,* tuwajulishe wote ukuu wa *roho ya imani* inayotufanya tutazame upande wa Mungu mafumbo, ibada, watu na matukio. Kwa kuwa mtazamo huo unakuwa kamili na wa kudumu kwa kumiminiwa sala tu, tunasema juu ya neema hiyo bila ya kuitaja bado, ili mtu yeyote atamani na kujiombea imani yenye kupenya na kuonja mafumbo ya wokovu. Kama tunavyofanya mtu atamani uzima wa milele kabla hajaonyesha dalili za uteule wake, inafaa atamani yale yote yaliyo sehemu za njia ya kawaida ya kuufikia uzima huo.

Ila tutofautishe nia na utekelezaji wake. Upande wa nia, lengo linatangulia njia; kumbe upande wa utekelezaji tunatakiwa kupanda taratibu toka chini hadi juu, na kukwepa haraka, la sivyo tutaharibu kila kitu, kama mtu anayetaka kupaua kabla hajaweka misingi, au kuruka kabla hajaota mabawa. Kwa hiyo ni lazima tukumbushe mfululizo masharti ya muungano halisi na Mungu: kujikusanya karibu daima, kujinyima kikamilifu, kuwa na moyo safi, unyenyekevu wa kweli, udumifu katika sala hata katika ukavu wa muda mrefu, na upendo mkubwa wa kidugu. Tukiongeza upendo kwa liturujia na kwa mafundisho ya imani tunajiandaa kweli kuitwa kwa karibu kwenye urafiki wa ndani na Mungu.

*Wito huo unapokuja kuonekana* inafaa wahusika wasome juu ya dalili zake tatu wasije wakapotoshwa na tabu na ukavu wa usiku wa hisi. Wakimiminiwa sala mara nyingi waendelee kusoma maandishi ya namna hiyo, hasa yale yanayoangalisha dhidi ya hamu ya neema za pekee (njozi, mafunuo n.k.). Wakilegea kidogo, tuwaambie mara juu ya kasoro za wanaoendelea, juu ya kupenda msalaba, juu ya haja ya kutakata kwa dhati zaidi ili kuungana kwa ndani na Mungu.

## 3.32. *YALIYO MAPYA KATIKA SALA YA KUMIMINIWA*

Kuna watu wanaodhani maelezo yetu kuhusu sala ya kumiminiwa hayatoshi kwa kuwa, eti! Hayaonyeshi vya kutosha yaliyo *mapya* katika sala hiyo, hata tofauti yake na sala ya kujipatia inaonekana kuwa ya kiwango tu, kwa sababu hiyo ya pili nayo inachangiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu ingawa si wazi. Basi, tuzingatie zaidi.

**JE, UPYA UNAONEKANA WAZI KILA MARA?**

Upya wa sala ya kumiminiwa unaonekana wazi mtu akivuka mara toka tafakuri sahili hadi *utulivu mtamu* ambapo utashi unatawaliwa na mwanga wa ndani (unaouonyesha wema wa Mungu uliomo ndani mwake kama chemchemi ya maji hai) ingawa akili na ubunifu vinaleta vurugu. Upya huo ungeonekana wazi zaidi kama akili pia ingetawaliwa, na ubunifu na kumbukumbu vingetulia inavyotokea katika sala ya muungano.

Lakini mara nyingi mtu havuki hivyo, bali mwanzo wa sala ya kumiminiwa unaendana na ukavu wa hisi wa muda mrefu, hata ukaitwa *utulivu mkavu.* Hapo upya huo hauonekani wazi, kwa kuwa athari za uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu zinaanza tu kujitokeza. Wenye juhudi wanaweza wakamiminiwa sala *wasitambue,* kwa sababu hali hiyo inakuwepo hata katika giza nene. Basi, upya huo hauonekani kila mara, tena hata ukiwa wazi kiasi, si sawa katika utulivu mkavu na katika ule mtamu.

**TUELEZEJE KUVUKA HUKO?**

Mtu akivuka hatua kwa hatua, *uvuvio maalumu unaopokewa na vipaji vya Roho Mtakatifu* unaeleza vya kutosha upya wake, mradi tuone vizuri tofauti iliyopo kati ya *namna ya kibinadamu* ya maadili (hata yale ya Kimungu) na *namna ipitayo maumbile* ya vipaji vya Roho Mtakatifu, ambavyo matendo yake yanaratibiwa moja kwa moja na *uvuvio wake maalumu.* Uvuvio huo ni *neema inayotenda* ambayo inatufanya tutende kwa

hiari *pasipo kuamua kwa mifuatano ya mawazo;* hivyo ni ya juu kuliko neema za kawaida ambazo *zinasaidia kutenda* kwa kuamua kwa mifuatano ya mawazo.

Ndiyo tofauti iliyopo kati ya vipaji na maadili yote: uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu ni kanuni ya Kimungu inayosababisha utendaji upitao maumbile. Kwa mfano, nikiona imefika saa ya kusali naenda mwenyewe (kwa neema ya kawaida inayosaidia kutenda); kumbe pengine, nikiwa nimezama katika somo gumu, ghafla napata wazo la kusali ama kwa kuelewa somo hilo ama kwa kumuombea mtu. Katika mfano wa kwanza busara ndiyo iliyoniongoza kutekeleza imani na ibada; katika ule wa pili ni uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu ulionielekeza kabla sijafikiria. Jambo hilo ni jipya, ingawa kuvuka kunafanyika pengine polepole na pengine kwa kasi au hata ghafla.

Hapa ni lazima tuzingatie vipaji si kwa jumla na kinadharia tu, bali kinaganaga na kimatendo, vilivyofafanuliwa na walimu wa Kiroho. Kipaji cha elimu ndicho chanzo cha mang'amuzi ya ubatili wa malimwengu kulingana na mambo ya Kimungu, na hasa cha ujuzi wa uzito wa dhambi ya mauti unaomfanya mtu aiogope kweli. Kusoma kwa makini vitabu vya dini na kujitafiti dhamiri kusingetosha kamwe kutia majuto ya namna hiyo yanayoonyesha uvuvio maalumu, jambo jipya kweli.

Vilevile kipaji cha ibada ndicho chanzo cha utashi *kutawaliwa* na uwemo mtamu wa Mungu katika sala ya utulivu: "Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, 'Aba!' yaani, 'Baba!' Roho mwenyewe *hushuhudia* pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Rom 8:15-16). Roho Mtakatifu anatoa ushahidi huo *kwa kututia upendo wa kitoto kwa Mungu* tusioufikia kwa msaada wa neema za kawaida. Tena kipaji cha ibada kinaeleza maneno haya: "Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa" (Rom 8:26).

Hatimaye kipaji cha hekima ndicho chanzo cha *kung'amua uwemo wa Mungu ndani mwetu* kwa kutegemea kwa pamoja uvuvio maalumu na ulinganifu wetu na mambo ya Kimungu unaotokana na upendo. Huo uvuvio *unatumia* ulinganifu huo kwa kuutekeleza (tendo la kumiminiwa la upendo) ili kutuonyesha jinsi mafumbo ya imani yanavyotimiza matamanio yetu ya juu zaidi na kuchochea mengine mapya. Hapo tendo ni *la kumiminiwa* si kwa sababu linatokana na maadili ya kumiminiwa bali kwa sababu lisingepatikana pasipo uvuvio maalumu ambao vipaji vinatuweka tayari kuupokea; linahitaji *neema inayotenda,* si ile ya kawaida tu inayosaidia kutenda.

**KUJIBU HOJA**

Kadiri ya maelezo hayo, tofauti kati ya vipaji na maadili si ya kiwango tu: mwenendo si uleule ukiwa na uvuvio maalumu au la. Tofauti hiyo ni wazi pale ambapo tendo la busara katika kuamua la kufanya linafuatwa na lingine la kipaji cha shauri lisilotegemea mifuatano ya mawazo bali uvuvio maalumu unaofanya busara yenye kusitasita isitumike tena wakati huo. Lakini pengine uvuvio huo unarahisisha tu uamuzi wa busara kwa kukumbusha neno fulani la Injili: hapo tofauti si wazi. Vivyo hivyo katika mfano wa umwagiliaji wa bustani, tofauti inajitokeza wazi mtu akivuka mara toka namna ya kwanza hadi ya nne; lakini badiliko linaweza likatokea hatua kwa hatua.

Ili kueleza sala ya kumiminiwa hakuna haja ya kudai inafanyika kwa *mawazo ya kumiminiwa* kama yale ya malaika, bali unatosha ule mwanga wa kumiminiwa unaostawi daima katika mwadilifu yeyote mwenye upendo kwa msalaba na usikivu kwa mlezi wa ndani. Kwa namna hiyo imani inazidi kupenya na kuonja.

Vilevile hakuna haja ya kudai uwepo *mwanga wa kinabii,* kwa kuwa ule wa vipaji unatosha: "Katika sala ya kumiminiwa Mungu anatazamwa kwa *mwanga wa hekima* ambao unainua roho itambue mambo ya Mungu, ingawa umungu wenyewe hauonekani moja kwa moja. Ndivyo kwa neema *Mungu anavyoonekana na mwanasala baada ya dhambi ya asili, ingawa kwa ukamilifu mpungufu kuliko katika utakatifu wa asili*" (Mt. Thoma wa Akwino). Yaliyo *mapya* katika sala ya kumiminiwa yanaelezwa vya kutosha na mafundisho ya mapokeo. Thibitisho ni kwamba *neema ya maadili na vipaji* inayotuunganisha na Mungu, *ni bora kuliko karama* zinazotuwezesha tu kujua au kupendekeza *ishara* za utendaji wake. Muungano wa ndani na Mungu aliyemo mwetu unapita ishara hizo ambazo zinaulenga tu; tena kuzijali mno kunasogeza mbali na sala ya kumiminiwa inayomfikia Mungu mwenyewe katika giza la imani.

Kwa kawaida wanaoshikilia mafundisho hayo ni wale waliomiminiwa sala, kumbe wanaoyapinga wengi wao wanakiri hawana mang'amuzi hayo, ila wanajaribu kujichorea kadiri ya masomo yao wakijiuliza kuhusu maana ya maneno ya walimu wa Kiroho, k.mf. *kumuona Mungu.* Bila ya shaka si kumuona moja kwa moja *alivyo,* bali ni *aina ya ujuzi inayofanana na mang'amuzi* kumhusu Mungu *kwa njia ya upendo wa kumiminiwa anaotuvutia kwake.* "Kuonja kwa imani" ndio tokeo maalumu la kipaji cha hekima: "Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema" (Zab 34:8). Walimu hao wametuachia mafundisho ambayo hatujaelewa kikamilifu. Ili tuweze kuyaboresha tunahitaji mang'amuzi ya juu pamoja na ujuzi wa dhati wa teolojia; lakini haitoshi tujipangie maendeleo hayo, mpaka tujaliwe: kabla ya hapo tupenye zaidi maneno yao tusiyapotoshe.

## 3.33. *ULINGANIFU NA TOFAUTI KATI YA WATAKATIFU TERESA WA YESU NA YOHANE WA MSALABA*

Tangu tusome mara ya kwanza maandishi ya watakatifu Teresa wa Yesu na Yohane wa Msalaba, ni rahisi

tutambue tofauti ambazo zimesisitizwa mara nyingi. Basi, tuone hasa asili yake.

**ASILI YA TOFAUTI HIZO**

Zinatokana na tofauti za mitazamo yao. Mt. Teresa alitegemea mang'amuzi yake binafsi, akidokeza neema za pekee alizojaliwa (njozi n.k.) asiwe makini kuzitofautisha na mambo yaliyo *ya lazima* katika "makao saba" ya jumba la Kiroho. Hivyo alitia maanani kuliko wengine matukio ya kihisi, ya nje na ya ziada yanayoweza yakaendana na sala ya kumiminiwa; vilevile alisisitiza kuzingatia ubinadamu wa Mwokozi.

Mt. Yohane wa Msalaba pia alisema kwa mang'amuzi yake binafsi na ya watu aliowaongoza, lakini hakuyataja, akijitahidi kuyachimba kiteolojia, jambo ambalo ni muhimu ili kutofautisha yaliyo ya kawaida na yaliyo ya ziada. Alieleza *sababu* za hali za sala kwa mafundisho juu ya maadili ya Kimungu na ya vipaji vinavyoendana nayo. Kwa mtazamo huo alizingatia yaliyo *ya lazima* katika safari ya kuelekea utakatifu, hasa matakaso ya Kimungu yanayohitajika kwa usafi kamili wa upendo. Hivyo hakuelekea kujali neema za pekee zinazoendana pengine na sala ya kumiminiwa, wala hakusisitiza kuzingatia ubinadamu wa Mwokozi, akilenga moja kwa moja shabaha kuu ya sala ya kumiminiwa, yaani Mungu aliyemo mwetu, ambaye tunamfikia katika giza la imani kwa njia ya ujuzi ambao anatumiminia na unafanana na mang'amuzi. Kwa kufanya hivyo amekamilisha maandishi ya Mt. Teresa na kutusaidia tuyaelewe.

**JE, KUNA MSINGI MMOJA CHINI YA TOFAUTI HIZO?**

Wengi wamethibitisha jibu la "ndiyo", kwa kuwa Mt. Teresa alijua vya kutosha mang'amuzi ya wafuasi wake aweze kuelewa na kueleza nini inatokea *kwa kawaida* kwa watu wanaopitia hayo makao saba. Tukitumia maelekezo aliyoyatoa huko na huko tunaweza kubainisha zaidi yaliyo *ya lazima* na yaliyo ya ziada.

Kimsingi watakatifu hao walielewa vilevile sala ya kumiminiwa, muungano na Mungu unaotokana nayo, na matakaso ya Kimungu yanayohitajika ili kuufikia ule kamili. Ikifaa kuonyesha tofauti zao, inafaa zaidi kuonyesha wanavyolingana na kutambua teolojia inavyoweza kusaidia katika masuala hayo magumu.

# 4. **MUUNGANO WA WALIOKAMILIKA**

## 4.1. ***KUINGIA HATUA YA MUUNGANO KUPITIA USIKU WA ROHO***

Kuhusu *kuingia* hatua ya muungano kwa kutakaswa upande wa roho tutasema kwanza juu ya haja ya kutakaswa kasoro zinazodumu katika wale walioendelea. Tutaona utakaso huo ukoje na unavyoelezwa na teolojia. Tutatoa kanuni za uongozi wa kufaa kwa wakati huo, tukionyesha matokeo ya utakaso huo na majaribu yanayoendana nao. Hivyo itakuwa rahisi zaidi baadaye kudhihirisha *hatua ya waliokamilika, uwemo wa Utatu ndani ya roho zao zilizotakata, imani, tumaini na upendo wao,* tena *ukamilifu wa Kikristo* ukoje.

Katika sehemu hii hatutazungumzia neema za pekee, ambazo pengine zinaendana au hata zinatangulia muungano, bali tutabainisha kilele cha kawaida cha maisha ya neema hapa duniani, ambacho ni ustawi kamili wa maadili na vipaji vya Roho Mtakatifu *unaozidi kutuunganisha na Mungu* mpaka uzima wa milele utimilize neema. Muungano huo ni *wa juu* na wa nadra, lakini kwa umbile lake si fadhili *ya pekee* kama karama, ambazo kwa vyovyote ni za thamani ndogo kuliko neema inayotia utakatifu.

### 4.1.1. ***HAJA YA KUTAKASWA ROHO NA UTANGULIZI WA HATUA YA MUUNGANO***

"Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na *kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa"* (Yoh 15:1-2). "Katika mzabibu wa kawaida, tawi lenye machipukizi mengi linazaa kidogo, kwa sababu utomvu unapotewa na nguvu ukienea mno katika machipukizi yaliyozidi; ndiyo sababu mkulima anayakata. Kitu cha namna hiyo kinamtokea mtu ambaye ana msimamo mzuri na kuunganika na Mungu, lakini mapendo na maisha yake yanamwagika mno nje, kwa njia mbalimbali: hapo nguvu za maisha ya Kiroho zinapungua zisizae mema mengi zaidi. Kwa hiyo Bwana, kwa mfano wa mkulima, anawatakasa watumishi wema, mara nyingi anapogolea ndani mwao yasiyo na faida ili wazae zaidi; anawatakasa kwa muda mrefu kutosha, akiwatumia tabu na kuruhusu majaribu yanayowalazimisha kuyapinga kitakatifu kwa stahili nyingi, jambo ambalo linawaimarisha zaidi kwa ajili ya uadilifu. Bwana anawatia nguvu na kuwatakasa namna hiyo wale walio safi tayari, kwa kuwa hapa duniani

hakuna aliye safi kutosha, kadiri ya maneno ya Mt. Yohane, 'Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu' (1Yoh 1:8)... Hivyo Bwana anawatakasa watumishi wake ili wazae zaidi, wastawi katika maadili na wazae matendo mema mengi zaidi kadiri walivyo safi" (Mt. Thoma wa Akwino).

Ndivyo alivyotakaswa Ayubu aliyesema, "Je, mtu hana wakati wake wa vita juu ya nchi?" (Ayu 7:1). Kwa maana hiyo mababu na walimu wa Kiroho walisema mara nyingi juu ya msalaba tunaopaswa kuubeba kila siku upande wa hisi na upande wa roho, ili polepole zitakaswe hata hisi ziitii kikamilifu roho, nayo imtii Mungu. Hayo yanafanyika hasa katika roho kutakaswa ili kuandaliwa iungane na Mungu.

**KASORO ZA WALIOENDELEA**

Inafaa tuzizingatie kwa sababu tatu: ili tuone haja na thamani ya msalaba unaotupasa kila siku; halafu tutofautishe tabu zisizo na maana tunazojipatia kipumbavu na zile zinazotutakasa; hatimaye tuelewe tutakavyohitaji kupitia toharani tusipofaidi vya kutosha misalaba ya maisha haya, kwa kuwa heri ya kumuona Mungu haiwezi kutolewa kwa mtu asiye safi kabisa.

Walioendelea, ambao wameshatakaswa hisi kwa kiasi kikubwa na wameanza kuishi Kiroho kwa kuzamia mafumbo ya imani, bado wana kasoro nyinginyingi, mfano wa kutu itakayokoma tu kwa kupatwa na moto unaotakasa. "Maana dhahabu hujaribiwa motoni, na watu wateule kalibuni mwa unyonge" (YbS 2:5).

Kwa namna fulani wanajitakia *mitawanyiko ya mawazo* wakati wa sala, *utupu wa ndani* kwa kujimwaga nje bure, *mapendo ya kibinadamu mno* kwa baadhi ya watu yanayosababisha kuwakosea wengine heshima, haki na upendo. Pengine wanatokeza *tabia kali* kwa *kukosa subira. Wakidanganywa* na shetani, baadhi wanatia maanani mno neema walizojaliwa, baadhi wanatumbukia *ari chungu* kwa jirani; hivyo bila ya kujitambua wanavimbika kwa *kiburi katika mambo ya Kiroho* na *kujiamini*, wanasogea mbali na usahili, unyenyekevu na usafi unaodaiwa na muungano wa dhati na Mungu. "Wanaweza wakawa wagumu kiasi kwamba kurudia uadilifu sahili na roho halisi ya ibada kuna shaka sana" (Mt. Yohane wa Msalaba). Basi, hatari zinazowakabili ni kubwa kuliko zile za mwanzoni.

Mbali ya kasoro hizo katika maisha ya ndani na uhusiano na Mungu, wanazo nyingine katika mafungamano na wakubwa wao, walio sawa nao na walio chini yao, ambazo zinadhuru upendo na haki na kuathiri utume na uongozi wao.

Kiburi upande wa maisha ya Kiroho na wa akili kinawafanya *washikilie mno msimamo wao,* namna yao ya kutazama, kuhisi na kutaka. Matokeo yake ni kijicho, uchu wa siri wa madaraka na hata *kuongoza kwa mabavu* (tabia yao isipoelekea kinyume, yaani *kuruhusuruhusu mno* na kuwa dhaifu mbele ya wanaowakosea wenzao). Vilevile mara nyingi hawana utayari na juhudi katika kutii, au wanatii kilaghai; wanakosa upendo kwa wivu, usengenyaji na mashindano.

Yanaweza yakazuka makosa mengi kati ya yale yanayovuruga zaidi roho. *Undani wa akili na utashi* umeathiriwa bado na kiburi, maoni na matakwa yao hata mwanga na matakwa ya Mungu visiweze kutawala bila ya kupingwa. Kasoro hizo kwa kudumu muda mrefu zinakomaa na kuharibu tabia isihusiane na Mungu kwa dhati. Matokeo ni magomvi na mafarakano mengi kati ya wale wanaotakiwa kushirikiana kwa wokovu wa watu.

Hayo yote yanadhihirisha haja ya *"sabuni kali ya usiku wa roho, ambayo isipokuwepo usafi unaodaiwa kwa kuungana na Mungu utakosekana daima"* (Mt. Yohane wa Msalaba). Hata baada ya kuvuka usiku wa hisi walioendelea ni *washamba* katika kutenda na kuhusiana na Mungu; wanamuelewa na kumzungumzia bila ya ukomavu. Ukamilifu tu, unaopatikana upande wa mafumbo, unaleta *utu uzima* ambapo roho inatenda makubwa, kwa sababu utendaji wake ni wa Kimungu kuliko wa kibinadamu.

**UNDANI WA UTASHI UNAHITAJI KUTAKASWA**

Y. Tauler alisisitiza jambo hilo kutokana na umimi ambao haujitambui lakini unadumu ndani ya utashi na kusababisha tuseme na nafsi yetu bila ya utulivu wala faida, badala ya kusema na Mungu kwa amani na kwa kutiwa uhai. Umimi huo unasababisha tujifanye lengo la yote na kuhukumu jirani (kumbe tunajitetea mno); unajitokeza hasa katika majaribu, ambapo mara tunajitafutia nje msaada na faraja: lakini si hivyo tunavyomuona Mungu. Hatujajenga vya kutosha juu ya Kristo, ndiyo sababu nyumba yetu si imara. Tumejenga juu yetu, juu ya utashi wetu, na hiyo ni sawa na kujenga juu ya mchanga.


"*Inambidi Mungu ajitwalie kabisa undani wa roho* na kushika nafasi yote, jambo ambalo linawatokea tu marafiki wake halisi. Mwenyewe alitupelekea Mwanae pekee ili maisha matakatifu ya huyo Mungu-mtu, maadili yake makuu na kamili, mifano yake, mafundisho yake na mateso yake mengi yatuinue juu yetu wenyewe, tutoke kabisa umimi wetu na *kuacha mwanga wetu mdogo hafifu uzame ndani ya nuru halisi…* 'Nuru yang'aa gizani, wala giza halikuipokea' (Yoh 1:5). Nuru hiyo wanaipokea wale tu walio *maskini wa roho* na *waliovua* vizuri umimi wao na matakwa yao binafsi. Wengi walioshika ufukara miaka 40 hawajawahi kupokea hata mwali mdogo. Kwa njia ya hisi na akili wanajua vizuri yaliyosemwa juu ya nuru hiyo wasiionje kamwe kwa ndani; kwao ni ngeni na inabaki mbali nao. Hivyo umati mnyofu wa akina yahe walipomfuata Bwana wetu, Mafarisayo, wakuu wa makuhani na walimu wa sheria, wale wote wenye utakatifu wa


kuonekana, walimpinga vikali na hatimaye wakamuua". Hiyo inaonyesha unafikisha wapi undani huo wa umimi na kiburi unaotupofusha tusione makosa yetu. Mungu ndiye ukuu wa wanyenyekevu, na njia zake za juu hazieleweki kwa kiburi chetu. Basi ni muhimu *nuru hai* ya imani na vipaji *ipenye undani wa akili yetu* hadi *mzizi wa utashi wetu.*

Ili itokee hivyo haitoshi tujue na kusadiki maneno ya Injili, ni lazima tufyonze kwa dhati roho yake. La sivyo, chini ya sura ya Kikristo, pamoja na miundo na misamiati ya Kikristo, tutadumisha ndani mwetu kitu tofauti *kinachokataa nuru ya uhai,* kama ngome unapojificha umimi usiotaka kusalimu amri Mungu atutawale moja kwa moja. Ndiyo sababu wanaojiona wameendelea vya kutosha wasitambue kasoro zao, wako hatarini kuliko umati wa watu wanaoungama ukosefu wao na kudumisha uchaji wa Mungu. "Basi, wanangu wapenzi, mtumie utendaji wenu wote wa Kiroho na wa umbile ili *hiyo nuru halisi ing'ae ndani mwenu mweze kuionja.* Kwa namna hiyo mtaweza kuirudia asili yenu, inapong'aa nuru halisi. Maumbile yatake yasitake, mtamani na kuomba neema hiyo". Hapa Y. Tauler anatofautisha ujuzi wa kawaida wa imani na yale mang'amuzi ya upendo wa Mungu waliyowekewa marafiki wake, akialika wote wayatamani ili yarekebishe undani wa roho kwa kuiangaza na kuitoa nje ya ngome ilipojificha.

Kasoro hizo zote, ambazo kwa kiasi fulani zinadumu katika akili na utashi wa walioendelea, zinahitaji utakaso ambao Mungu tu anaweza kuufanya. *"Mungu tu anaweza kutia umungu, kama vile moto tu unavyoweza kuwasha"* (Mt. Thoma wa Akwino). Kutakaswa naye kutakuwa na mateso, kama *kifo cha fumbo,* yaani maangamizi ya umimi unaopinga neema hata vikali. *Kiburi kinatakiwa kupigwa hadi kufa* kiuachie nafasi unyenyekevu halisi. Hiyo nuru ya uhai iliyoongezeka duniani hadi ujio wa Mwokozi inatakiwa kuongezeka vilevile ndani ya kila mtu hadi aingie mbinguni.

Utakaso wa Kimungu wa roho ndio *mapambano ya mwisho kati ya kiburi na unyenyekevu unaoendana na upendo.* Pande hizo mbili zinaweza kuchorwa kama miti miwili: mmoja unatokana na asili na matokeo ya mizizi saba ya dhambi, unachanua maua ya laana na kuzaa matunda ya sumu. Kinyume chake, mti wa maadili na vipaji, mzizi wake ni unyenyekevu unaozidi kupenya ardhi ili kufyonza rutuba, matawi yake ya chini ni maadili ya kiutu na vipaji vinavyohusiana nayo, matawi yake ya juu ni imani, tumaini na upendo (ambao ndio wa juu na wenye kuzaa zaidi). Imani inahusiana na kipaji cha akili, na pia cha elimu ambacho kinakamilisha tumaini kikionyesha ubatili wa malimwengu na wa misaada ya binadamu kwa lengo la Kimungu, na hivyo kutufanya tutamani uzima wa milele kwa kumtegemea Mungu. Upendo unahusiana na kipaji cha hekima kinachosababisha hasa sala ya kumiminiwa inayoleta muungano na Mungu unaokuwa kama wa kudumu pamoja na kujiachilia kwake. Ili mti huo ustawi mpaka mwisho unahitajika ushindi wa moja kwa moja dhidi ya mabaki ya kiburi ambayo walioendelea wanayo upande wa akili na wa maisha ya Kiroho. Ndiyo sababu wanahitaji kutakaswa roho ambako, kwa msaada wenye nguvu wa Roho Mtakatifu, watekeleze kishujaa maadili ya Kimungu ili kushinda vishawishi dhidi yake.




### 4.1.2. *UFAFANUZI WA UTAKASO WA KIMUNGU WA ROHO*

Bwana tu anaweza kuutakasa undani wa roho jinsi unavyohitaji. Basi, tufafanue utakaso huo tusije tukaingia hasara kwa kuuchanganya na tabu za nafsi na ukavu wa hisi. Kinachovitofautisha ni maendeleo katika kumjua na kumpenda Mungu. Tabu za nafsi hazitakasi zisipovumiliwa kwa upendo wa Mungu na kwa kujiachilia kwake. Vilevile tabu zinazotokana na utovu wa maadili (k.mf. hisi zisizoratibiwa) hazitakasi zisipopokewa kama aibisho la kufaa kwa kufidia makosa.

**GIZA AMBAMO ROHO INAHISI IMEJIKUTA**

Kama vile utakaso wa Kimungu wa hisi unavyodhihirishwa na hali ya kunyimwa faraja za kihisi tulizoambatana nazo, ule wa roho unaonekana kuwa hasa kunyimwa mianga ya awali kuhusu mafumbo ya imani. Tuliyazoea hivi kwamba urahisi wa kuyafikiria katika sala ulitusahaulisha ukuu wake usio na mipaka na kutufanya tuyaone kibinadamu mno. Basi, ili atuinue juu Bwana anakuja kutubandua toka namna hiyo ya kuwaza na kusali. "Mungu anawaondolea hao walioendelea vipawa, mapendo na hisi, upande wa roho na wa hisi; anaacha akili gizani, utashi ukavuni, uwezo wa kukumbuka bila ya kumbukumbu maalumu, na mapendo ya mtu yakipotea katika mateso, uchungu na mafadhaiko. Ndani ya mtu hamna tena hisia wala mwonjo kuhusu mema ya Kiroho yaliyomvutia hapo awali" (Mt. Yohane wa Msalaba). Huzuni inayompata hapo si ile inayoweza ikatokana na ugonjwa wa nafsi, kuvunjwa moyo na kupambana na maisha. Ni tofauti hasa kwa sababu inaendana na hamu kubwa ya Mungu na ya ukamilifu, na utafutaji wa mfululizo wa yule ambaye peke yake anaweza kulisha na kuhuisha roho.

Hapo mtu anapaswa kusonga mbele "kama kipofu, kadiri ya imani tupu ambayo ni usiku wenye giza kwa vipawa vya umbile" (Mt. Yohane wa Msalaba). Hawezi tena kuambatana kwa urahisi na ubinadamu wa Yesu, ameondolewa kama mitume walivyoondolewa alipopaa mbinguni. Miezi ya nyuma urafiki wao ulistawi siku kwa siku, hata Yesu akawa uhai wao; kumbe kawaacha wasiweze kumuona wala kusikiliza maneno yake yenye faraja. Walijisikia wakiwa hasa mbele ya matatizo ya utume waliokabidhiwa kuufanya ulimwenguni kote, kati ya uovu na udanganyifu mkubwa. Walipaswa kukumbuka maneno ya Yesu: *"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja*

*kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu"* (Yoh 16:7). "Mitume waliambatana na ubinadamu wa Kristo bila ya kuinuka vya kutosha hadi upendo wa Kiroho kwa umungu wake, wala kuwa tayari kumpokea Roho Mtakatifu… ambaye watapelekewa ili awafariji na kuwaimarisha katika tabu zao" (Mt. Thoma wa Akwino). Hilo ondoleo la uwepo wazi wa Yesu kabla hawajageuzwa siku ya Pentekoste linasaidia kuelewa hali ya giza na ukiwa tunayoizungumzia, ambapo mtu anajiona ameingia usiku halisi wa roho kwa kuondolewa mianga kama jua linapotua magharibi.

**KATIKA GIZA HILO UKUU WA MUNGU UNAFUNULIWA**

Je, katika giza hilo hakionekani chochote kile? Upande wa maumbile, jua likitoweka zinakuja kuonekana nyota zinazodhihirisha ukuu wa anga: hivyo usiku tunaona mbali kuliko mchana. Huo ni mfano wa ukweli mkubwa, kwamba roho inapoingia giza hilo haioni tena yaliyo jirani nayo, ila inazidi kuhisi ukuu na usafi usio na mipaka wa Mungu, unaopita wazo lolote tunaloweza kujitungia; kutokana na hisi hiyo inajiona wazi zaidi ilivyo nyonge.

Lakini, kabla hatujafurahia nyota za angani tunapaswa kuzoea kutembea usiku bila ya hofu na kushinda *vishawishi vikali dhidi ya imani na tumaini.* Kwa Mt. Yohane Maria Vianney teso kuu lilikuwa kujiona mbali na kipeo cha upadri, ambao katika giza la imani alizidi kutambua kilivyo kikuu, pamoja na haja za umati uliomkimbilia. Kadiri alivyoona mema mengi yaliyohitajiwa, alishindwa kuona na kufurahia yale aliyoyatenda. Teso lake kuu lilikuwa kuona dhambi na upotevu wa milele, kidogo kama Yesu kuhani na sadaka juu ya msalaba na Maria chini yake. Teso hilo linategemea kuzidi kupenya katika usiku wa imani wema mkuu wa Mungu (ambao unapuuzwa na kudharauliwa) na thamani ya uzima wa milele.

Ukuu na wema wa Mungu na unyonge wetu vinapingana kiasi cha kuangaziana ajabu. Hivyo M.H. Anjela wa Foligno aliandika, "Najiona sina jema wala adili lolote, nimejaa wingi wa vilema… rohoni mwangu naona kasoro tu… Ningependa kuwajulisha wengine kwa sauti kubwa uovu wangu… Mungu amejificha kwangu… Niwezeje kumtumainia?… Hata kama wenye hekima wote waliopo duniani na watakatifu wote wa mbinguni wangenijaza faraja zao, wasingenisaidia chochote kabla Mungu hajabadili undani wa roho yangu. Tabu hiyo ya ndani ni mbaya sana kuliko kifodini". Baada ya hapo, akikumbuka mateso ya Kristo, alitamani tabu hiyo iongezeke kwa kuwa inatakasa na kufunua vilindi vya mateso hayo. Siku chache baadaye, akiwa njiani alisikia kwa ndani maneno yafuatayo, "Binti yangu, nakupenda kuliko yeyote wa bonde hili… Fransisko alinipenda sana nikamtendea mengi; lakini mtu angenipenda kuliko Fransisko ningemtendea mema mengi zaidi… Nampenda upeo yule anayenipenda bila ya uongo… Hakuna anayeweza kujisingizia, kwa kuwa wote wanaweza kupenda; Mungu anaomba upendo tu, kwa kuwa mwenyewe anapenda bila ya uongo, naye ndiye upendo wa roho". Yesu msulubiwa akimuonyesha kidogo mateso yake akaongeza, "Tazama vema: je, ndani mwangu unakuta chochote kisicho upendo?"

Mfano mwingine wa usiku wa roho ni Mt. Paulo wa Msalaba aliyeandika, "Tabu ndogondogo za mwili au za roho ndiyo vidato vya kwanza vya ile ngazi ndefu takatifu inayopandwa na watu bora na wakarimu. Hao wanapanda hatua kwa hatua hadi kufikia kidato cha mwisho. Huko juu wanakuta uchungu safi kabisa, usiochanganyikana hata kidogo na faraja toka mbinguni wala duniani. Nao wakiwa waaminifu wasijitafutie faraja yoyote, watavuka toka huo uchungu safi hadi upendo safi wa Mungu usiochanganyikana na chochote kingine. Lakini wanaofikia hatua hiyo ni wachache sana… Wanajiona kana kwamba wameachwa na Mungu, kwamba yeye hawapendi tena, amewakasirikia… Nikiruhusiwa kusema hivi, kidogo ni kama adhabu ya kumkosa Mungu milele, ni teso ambalo uchungu wake hauna mfano. Lakini mtu akiwa mwaminifu anakusanya hazina isiyopimika! Dhoruba zinapita na kwenda zake, kumbe yeye anakaribia muungano halisi, mtamu na wa dhati na Yesu msulubiwa, ambaye anamgeuza ndani mwake na kumlinganisha naye".

Hugo wa Mt. Viktori alifananisha roho kutakaswa na Mungu na mageuzo ya ukuni mbichi ulioshikwa na moto, "Ubichi unakauka, moshi unapungua, mwali mshindi unapamba… nao hatimaye unaushirikisha ukuni umbile lake, hata ukuni mzima unakuwa mkaa wenye kuwaka. Ndivyo upendo wa Mungu unavyokua polepole rohoni; mwanzoni hisia za moyoni zinapinga na kusababisha tabu nyingi na mafadhaiko: ni moshi mzito unaotakiwa kutawanywa. Halafu upendo wa Mungu unazidi kuwaka, mwali wake unakuwa mkali zaidi… na hatimaye unapenya roho nzima. Ukweli wa Mungu unapatikana na kumezwa katika sala ya kumiminiwa: roho iliyojikana inamtafuta Mungu tu. Kwa roho yeye ni yote katika yote, nayo roho inatulia katika upendo wake na kukuta humo furaha na amani".

Y. Tauler pia alieleza kwamba Roho Mtakatifu anauondolea undani wa roho yale yote yenye umimi na kiburi bado. Anaiacha tupu ili kuiponya, halafu anaijaza pamoja na kuiongezea zaidi na zaidi uwezo wa kupokea. "Hapo inaonekana njia isiyo na mtu, iko gizani na faraghani. Kwenye njia hiyo Mungu anajitwalia tena yale yote aliyowahi kuyatoa. Hapo mtu anaachwa peke yake kabisa hata kuonekana hajui tena chochote kumhusu Mungu. Anafikia hatua ya kufadhaika asijue tena kama aliwahi kushika njia nyofu… hiyo inamtia uchungu mkubwa kiasi kwamba ulimwengu huu mpana unaonekana naye mdogo mno. Hasikii tena chochote kumhusu Mungu wake, hajui tena chochote juu yake, na mengine yote kwake ni karaha. Ni kana kwamba amebanwa na kuta mbili, mbele yake kuna upanga na nyuma yake mkuki mkali. Basi aketi na kusema, 'Nakusalimu, Mungu wangu, uchungu mkali uliojaa neema zote!'… Kwake inaonekana ni jaribu linalomtesa

kuliko moto wa milele, kama huo ungewezekana duniani. Yale yote anayoweza akaambiwa katika hali hiyo hayamfariji kama asivyoweza kufarijiwa na jiwe. Tena, jambo asilopenda kabisa ni kusikia viumbe wakisema".

Mt. Visenti wa Paulo kwa miaka minne alijaribiwa hivyo na kishawishi kikali cha mfululizo kuhusu imani hata akaandika maneno ya Nasadiki akayavaa juu ya moyo akayakandamiza mara kwa mara ili kuthibitisha kwamba hajakubali kishawishi hicho. Katika miaka 30 ya kuhudumia monasteri nimekutana walau mara 20 na usiku wa roho ulio wazi, kwa kawaida pasipo ugonjwa wowote, katika watu wenye akili timamu ambao walipaswa kuongoza jumuia au shirika na walifanya vizuri kazi yao.

Tukiona utakaso huo wa Kimungu ni nje ya njia ya kawaida ya utakatifu, sababu ni kwamba hatufikirii vya kutosha utakaso wa dhati unaohitajika ili kupata mara uzima wa milele na kumuona Mungu moja kwa moja. Pengine tukisoma walimu wa Kiroho walivyoufafanua ni kwa udadisi, si kwa hamu nyofu ya utakatifu wetu. Tungekuwa nayo, tungeona maandishi yao yanavyotufaa.

Kwa njia moja au nyingine ni lazima tupitie urojorojo huo ili mateso, unyenyekevu na upendo wa Yesu kwetu visiwe havieleweki au kueleweka kinadharia tu; pasipo ujuzi wake hai hapana upendo kwa msalaba wala kwa utakatifu halisi. Kwa mfumo wake, neema inayotia utakatifu ikistawi inazidi kutufananisha na Mungu. Kadiri ilivyo *ya Kikristo* inazidi kutufananisha na Msulubiwa hadi tuingie mbinguni.

Tunapaswa pia kutambua tofauti za watu na za neema walizonazo, tusije tukawadai kuliko uwezo wao: tuhimize kwa wengine ushujaa wa mfululizo, kwa wengine hatua ndogondogo za kulisogelea lengo. Lakini kila mmoja anapaswa kujitoa sadaka afanane na Kristo.

### 4.1.3. ***KINACHOSABABISHA ROHO KUTAKASWA***

Kisha kufafanua watumishi bora wa Mungu wanavyotakaswa roho, tueleze kiteolojia kinachosababisha hali hiyo, ambapo mambo ya Kiroho yanang'amuliwa katika giza na uchungu.

**MWANGA WA KUMIMINIWA UNAOTAKASA NA MOTO WA KIROHO**

Waadilifu wameandikwa, "Mungu amewajaribu, na kuwaona kuwa wamemstahili; kama dhahabu katika tanuru aliwajaribu, akawakubali mithili ya kafara" (Hek 3:5-6). Maandiko yanarudiarudia wazo hilo, "kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, ni moto ulao, Mungu mwenye wivu" (Kumb 4:24) dhidi ya yale yanayomzuia asitawale rohoni. Nabii aliandika, "Toka juu amepeleka moto mifupani mwangu, nao umeishinda... amenifanya kuwa mtu wa pekee, na mgonjwa mchana kutwa" (Mao 1:13); ndivyo alivyoona vizuri makosa ya Israeli, haki ya Mungu na wema wake akamtolea dua nyingi kwa wokovu wa wakosefu.

"Kwa kuwa wewe unaiwasha taa yangu; *Bwana Mungu wangu aniangazia giza langu*" (Zab 18:28). Ndivyo Roho Mtakatifu anavyoangaza kama umeme roho anayotaka kuitakasa. Pengine anatuambia, "Je, unataka kutakaswa?" Tukikubali ataanza kazi ya dhati, akitupatia ukweli wa Kimungu ili kutuondolea umimi unaotudanganya bado mara nyingi. *"Ninyi mkikaa katika neno langu*, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena *mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru*" (Yoh 8:31-32). Yaani, tukishika kimaisha neno la Kristo kwa kujirekebisha, polepole ukweli mkuu utatupenya na kutukomboa kutoka udanganyifu wa hatari zaidi, ule tunaojiambia. Hatuwezi kamwe kutamani vya kutosha mwanga huo unaotakasa; kumbe, mara nyingi tunaukwepa kwa kuogopa kukosolewa.

Mt. Yohane wa Msalaba aliufafanua hivi, "Usiku huo wenye giza ni Mungu kuiathiri roho ili kuitakasa na ujinga na kasoro za kawaida. Wanasala wanauita *sala ya kumiminiwa* na teolojia ya mafumbo, ambapo Mungu anaifundisha roho kwa siri na ukamilifu wa upendo, pasipo mchango wa mhusika, na hata pasipo huyo kuelewa hiyo sala ya kumiminiwa ni nini". Baadaye akarudia mfano wa Hugo wa Mt. Viktori, "*Mwanga wa Mungu unaoitakasa roho na kuiandaa kwa muungano kamili* unafanana na moto unaotakasa ukuni kabla haujaugeuza ndani yake. Huo moto wa kimaumbile unaanza kukausha ukuni ukiondoa ubichi wake: halafu unautia rangi nyeusi na kuufanya utoe harufu mbaya na kuutolea takataka zote… Hatimaye unaanza kuuwasha kwa nje, na joto linaugeuza kuwa moto na linaufanya ung'ae kama moto wenyewe. Ndivyo ilivyo kwa *moto wa Kimungu wa sala ya kumiminiwa.* Kabla haujasababisha muungano na mageuzo ya roho ndani ya Mungu, ni lazima aiondolee vipingamizi vyote. Anaitolea takataka zote, anaifanya nyeusi… roho inaonekana mbaya, ya kuchukiza na kutopendeza kuliko awali. Basi utakaso huo unafanyika ili kuondoa vilema vyote ambavyo roho haijaviona kwa jinsi vilivyoshikamana nayo na kuwa kitu kimoja nayo; haikujua vipo wala *haikudhani mabaya makubwa hivyo yamo ndani mwake.* Hapo inadhani unyonge wake unamfanya Mungu aichukie".

Matatizo hayo ya kufaa ni tohara halisi ya kabla ya kufa, ambapo mtu anatakaswa na moto wa Kiroho wa sala ya kumiminiwa na upendo. Ndiyo sababu "mtu anayetendewa hivyo duniani, ama anakwepa tohara ya ng'ambo ama anabaki toharani kidogo sana; saa moja ya mateso hayo katika maisha haya inafanya kazi bora kuliko saa nyingi za toharani" (Mt. Yohane wa Msalaba) kwa sababu hapa tunatakata kwa kustahili. Basi, kwa kuwa hali ya toharani ni adhabu ya kosa lililotakiwa kuepwa, *njia ya kawaida ya utakatifu* ni kutakaswa kabla ya kufa, ingawa wachache tu wanakwenda mbinguni wasipitie toharani. Watakatifu tu wanatimiza kikamilifu utaratibu wa maisha ya Kikristo.

**ATHARI YA KIPAJI CHA AKILI KATIKA UTAKASO HUO**

"Mtu anapokea namna mpya ya kutazama mambo, kwa kuwa mwanga wa neema ya Roho Mtakatifu ni tofauti na hisi, kama vile mambo ya Kimungu na yale ya kibinadamu… Hivyo basi polepole usiku huo wenye giza unambandua na namna yake ya kawaida ya kuelewa, ili umuinue kwenye namna ya Kimungu iliyo tofauti na wazo lolote la kimaumbile, kiasi kwamba anadhani kuwa anatembea nje yake mwenyewe". Fundisho hilo la Mt. Yohane wa Msalaba linaangazwa na lile la Mt. Thoma wa Akwino kuhusu kipaji cha akili kusababisha *upenyaji mpya* na *utakaso:* "Kadiri mwanga wa akili ulivyo mkubwa unapenya undani wa jambo ili kuelewa mfumo na sifa zake. Basi, mwanga wa kimaumbile wa akili yetu (hata ukiwa mkubwa namna gani) uwezo wake una mipaka usiovukika. Kwa hiyo mtu anahitaji mwanga upitao maumbile ili kupenya mbali zaidi (kwa Mungu au katika vilindi vya roho), na mwanga huo upitao maumbile ambao binadamu anajaliwa unaitwa kipaji cha akili". Ni wa juu kuliko mifuatano ya mawazo, ni chanzo cha ujuzi wa mara moja, sahili na wenye kupenya kama mwali wa jua.

Kipaji hicho kinadai iwepo kwanza imani iliyo hai kwa upendo, nacho kinaikamilisha hivi: imani hai inatufanya tushikilie mafumbo ya Mungu kwa sababu yamefunuliwa naye, lakini peke yake haiwezi kutufanya tupenye maana yake ya dhati. Upenyaji huo hautokani na masomo, bali na mwanga maalumu wa Roho Mtakatifu unaoshinda masomo kwenda juu na ndani, tena si kinadharia tu, bali kwa namna hai na kimaisha. Mwanga huo wenye kupenya tunaupokea kwa mikono miwili kwa kipaji cha akili. Hicho kwanza kinatuzuia tusichanganye *maana halisi ya Neno la Mungu* na ufafanuzi wake mdanganyifu; kinaonyesha mara *ubatili wa hoja za kupinga* kama noti mbaya inayoharibu ulinganifu wa noti zote: hapo tunatambua udanganyifu hata tusipoweza kuukanusha kiteolojia. Kipaji hichohicho kinatokeza umbali mkubwa uliopo kati ya mambo ya Kiroho na ishara zake, kati ya roho na mwili. Vilevile kinazuia tusichanganye faraja za kihisi na nderemo za Kiroho ambazo ni za juu na za hakika zaidi.

Kipaji hicho hakizuii tu udanganyifu, bali kinatufanya tupenye kwa namna hai kweli za dini zinazoeleweka (kama vile uwepo wa Mungu), na hasa mafumbo yapitayo uwezo wa akili: "Maana Roho huchunguza yote, hata *mafumbo ya Mungu"* (1Kor 2:10). Hapa duniani hakiwezi kuyaonyesha wazi, ila katika giza la imani kinaonyesha maana yake ya dhati iliyo vigumu kuieleza, ukuu wa Mungu, sifa zake, Ubaba wake kwa Neno na kwetu, ukombozi n.k.

Kipaji hicho kinatuongoza kuelewa na kutenda pia, kikitukumbusha umuhimu wa amri ya upendo, na thamani ya uzima wa milele tunaposhawishwa kukata tamaa. Kinatuzindua kuhusu mambo ya Kiroho, kinatuonyesha ukosefu wetu kuliko utafiti wowote wa dhamiri, kwa kutuangazia unyonge wetu pamoja na ukuu wa Mungu. Ndiyo sababu kinahusiana na heri ya wenye moyo safi, kwa kuwa kinatakasa akili yetu dhidi ya udanganyifu katika kuelewa na kutenda, na kinaibandua na picha za hisi.

"Hatumjui Mungu alivyo" (Mt. Thoma wa Akwino). *Umungu* haufikiwi na maumbile, kwa kuwa uko juu kuliko sifa zote zinazoweza kujulikana na kushirikiwa kimaumbile, juu ya uhai, umoja, ukweli, wema, ujuzi na upendo; unashirikishwa tu kwa namna ipitayo maumbile ya neema inayotia utakatifu. Duniani hatuwezi kuujua, ndiyo sababu wanasala waliuita *giza kuu.* "Siku moja roho yangu ilinyakuliwa, nikamuona Mungu katika uangavu mkubwa kuliko wowote niliowahi kujua… Nilimuona Mungu katika giza, na ni lazima liwe giza, kwa kuwa yuko juu mno kuliko roho, na lolote linaloweza kufikiriwa halilingani naye… *Sioni kitu ila naona yote; hakika inapatikana katika giza.* Kadiri giza lilivyo nene, wema unazidi yote. Ni fumbo lililofichika… Uweza, hekima na utashi wa Mungu, nilivyoviona vizuri ajabu siku nyingine, natambua ni kidogo kuliko hilo. Hilo ni kitu kizima, hivyo ni kama sehemu zake tu" (M.H. Anjela wa Foligno). Maana yake, sasa sioni kitu maalumu, ila naona sifa zote za Mungu zimeunganika vizuri ajabu katika ukuu wake unaozidi akili yangu.

Giza hilo ni Mungu ambaye "amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona" (1Tim 6:16). Mwanga unaotakasa wa kipaji cha akili unaonekana giza, kwa kuwa unatuingiza katika giza la juu la fumbo la Mungu, lililo kinyume cha giza la chini la mwili, tamaa, dhambi na udanganyifu.

Hivyo kipaji cha akili kinathibitisha hakika ipitayo maumbile inayotokana na imani, kikitufanya tupenye mafumbo na kukataa udanganyifu. Sala ya kumiminiwa iliyopo katika hiyo hali ya giza inatokana kwa mbali na imani hai na kwa jirani na kipaji cha akili; mara nyingi hata kile cha elimu kinachangia kwa kutuonyesha hasa unyonge wetu. Ukavu wa roho unaopatikana katika hali hiyo unaonyesha hakuna athari kubwa ya kipaji cha hekima *kinachotuonjesha* mambo ya Mungu kikituletea hivyo faraja na amani kubwa. Upenyaji wa kipaji cha akili ni tofauti na mwonjo huo. Ndiyo sababu anayezidi kupenya ukuu wa Mungu anajisikia mbali naye kutokana na unyonge wake; ila, kisha kutakaswa roho, ataonja kwa dhati uwemo wa Utatu rohoni mwake, ataujua kama kwa kuung'amua, jambo ambalo linaanza kidogo kabla ya usiku wa roho na litakamilika katika muungano unaotugeuza.

## 4.1.4. *GIZA LA MWANGA MKALI*

Tueleze zaidi kwa nini mwanga wa kipaji cha akili unaonekana giza ili tutofautishe *giza la juu* na *giza la chini,* tukiinuka mfululizo ili kupenya lile la juu, yaani ile nuru anamokaa Mungu. Hapo usiku wa roho utaonekana ni uzima wa milele unaochipuka kwa uchungu ndani mwetu. Kwa ufupi, mwanga wa kumiminiwa

unaotakasa unaonekana giza kwa sababu ya ukali wake na ukuu wa jambo unaloliangaza; nao unatutesa kwa sababu ya uchafu na udhaifu wetu, tunaoutambua zaidi kutokana na vishawishi vya wakati huo.

**MATOKEO YA MWANGA MKALI MNO**

"Hekima ya Mungu inaonekana giza kwetu kwa kuwa inapita uwezo wa kimaumbile wa akili yetu, hivyo kadiri inavyodhihirika kwetu tunaiona kama giza" (Mt. Yohane wa Msalaba), kwa sababu tunazidi kuelewa umungu unavyopita mawazo yote tunayoweza kujitungia juu yake, k.mf. uhai, ukweli, wema, ujuzi, upendo wenyewe. Ndani yake una sifa hizo kwa namna bora hivi tusiweze kuufikia. "Jua likipambazuka na rangi nyekundu… au likitua na rangi nyeupenyeupe, tunasema ni dalili ya mvua. Teotimo, jua si jekundu, wala jeusi, wala jeupe, wala la kijivu wala la kijani. Nyota hiyo haipatwi kabisa na hali hizo wala mabadiliko ya rangi, kwa kuwa rangi yake pekee ni ule mwanga wake mkali na wa kudumu… Ila sisi tunasema vile kwa sababu ndivyo linavyoonekana kwetu kadiri ya hewa mbalimbali zilizopo kati yake na sisi, zinazofanya tulione namna tofauti. Ndivyo tunavyofikiri pia kumhusu Mungu: si kadiri alivyo, bali kadiri ya matendo yake ambayo tunamtazama… Ndani ya Mungu mna ukamilifu mmoja tu ambao ndani yake zimo sifa nyingine zote njema kwa namna bora kabisa tena kuu hata roho yetu isiweze kudhani kamwe" (Mt. Fransisko wa Sales).

Nuru hiyo isiyofikiwa ndiyo giza kuu kwetu; kama vile mwanga wa jua unavyopofusha macho ya ndege wa usiku asiyeweza kuvumilia hata mwanga dhaifu wa alfajiri. Aristotle aliwahi kusema kadiri mambo ya Kimungu yalivyo maangavu ni giza kwetu, kwa kuwa yako mbali zaidi na hisi zetu, k.mf. "jua lipo" ni tamko wazi kwetu kuliko "Mungu yupo". Lakini kwa usahihi Mungu tu yupo kweli, ndiye Aliye: mwanga wa jua ukilinganishwa naye ni kivuli tu. Vilevile *muda* upitao ni wazi kwetu kuliko *umilele* usiopita wala kubadilika.

Hivyo *mambo ya Mungu yanayotuelea* (k.mf. uwepo wake) *ni yale tunayoyapata katika kioo cha viumbe vinavyoonekana* tukitumia mwanga dhaifu unaolingana na umbile letu. Kumbe ulinganifu wa dhati wa haki na huruma zisizo na mipaka pamoja na hiari kuu katika fumbo la uteule, ingawa ni mwangavu sana, kwetu ni giza nene. Ndiyo sababu mara nyingi wanaopitia usiku wa roho wanajaribiwa kuhusu fumbo hilo, wasiweze kuishia maelezo rahisi ya kibinadamu: wanahisi kwamba wangeyakubali wangeshuka badala ya kupanda. La kufanya ni kuruka kishawishi hicho kwa tendo kubwa la imani kuelekea giza la juu la *umungu na vilindi vyake,* ambamo ulinganifu huo unang'aa.

Vilevile *Utatu ulio mwanga wenyewe unaonekana giza kwetu.* Ndiyo sababu Mt. Teresa wa Yesu alisema, "Kadiri mafumbo ya imani yalivyo ya giza, najisikia kuyaheshimu, kwa kuwa najua giza hilo linatokana na mwanga mkali mno kwa akili yangu finyu". Mateso ya Yesu yaliyokuwa saa ya giza nene na ya kukwaza zaidi kwa mitume, ndiyo saa ya ushindi wake mkuu dhidi ya dhambi na shetani. "Mwali wa Kimungu wa sala ya kumiminiwa unapopenya roho, unaijaza uangavu, lakini kwa kuwa unapita umbile la roho, unaitia giza kwa maana unaiondolea hisi zake na mapendo yake ya kimaumbile ambavyo awali ilikuwa ikivitambua kwa mwanga wa kimaumbile… Hapo roho inaanza kupima vizuri zaidi sana yaliyo kweli na yaliyo uongo; inayaona mara na kuyaelewa wazi zaidi sana kuliko kabla haijaingia giza hilo" (Mt. Yohane wa Msalaba).

**MATOKEO YA MWANGA JUU YA MACHO MABOVU**

Zaidi ya hayo, mwanga wa Kimungu unaomiminwa katika usiku wa roho unaitesa kutokana na uchafu ilio nao bado. "Mwanga unachukiza macho mabovu, ingawa unayapendeza yaliyo safi" (Mt. Augustino). Inatokea hivyo hasa mwanga huo ukitakiwa kushinda pingamizi la muda mrefu la mtu asiyependa kuangaziwa kasoro zake fulanifulani (k.mf. ari chungu au kujiridhia kwa siri) kwa kuwa anataka kuziona ni maadili anavyodanganywa na umimi na shetani. "Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa" (Yoh 3:20).

Mara nyingi mtu anateseka pia kwa kuwa anashindwa kuelewa sababu ya Mungu kumjaribu vile, kwa mfano wa hakimu asiye na huruma. Kwake ni vigumu kusadiki kimaisha wema wa Mungu: hata akiambiwa ukweli huo anauona ni nadharia tu, kumbe anajisikia haja ya kuung'amua kwa faraja kidogo. "Tabu hiyo ni kali sana kwa roho iliyo chafu bado, inapomiminiwa huo mwanga unaotakasa. Kwa kuwa *usafi huo unaojiambatanisha na uchafu* ili kuumaliza, unaionyesha vizuri roho ilivyo chafu na nyonge hata ikadhani Mungu anaiwinda kama adui yake" (Mt. Yohane wa Msalaba).

**HOFU YA KUKUBALI VISHAWISHI**

Tabu hiyo ya ndani inazidishwa tena na hofu ya kukubali vishawishi vinavyojitokeza wakati huo dhidi ya imani, tumaini na upendo. Katika hali hiyo chungu, mtu anaona vizuri kwamba pengine amevipinga, lakini anahofia kuwa pengine amevikubali. Hofu hiyo inamfadhaisha kwa jinsi anavyompenda Bwana tayari, asitake kuchukiza ukuu wake wala kudharau wema wake. Ndiyo sababu, wakati kilele cha roho kina tendo la imani iliyoangazwa na kipaji cha akili, lililo *tendo sahili* la kuzamia mafumbo kwa ukavu na bila ya kujitambua, mtu anajiona kama ameachwa na Mungu. Anayejaribiwa hivyo ana *mawimbi ya kwenda na kurudi* kama roho za toharani ambazo, zikisukumwa na upendo zimuelekee Mungu, zinajisikia kurudishwa na unyonge wao. Mt. Katerina wa Genoa alisema hizo zina tabu kubwa ambayo haieleweki kwa yeyote duniani tena inaongezeka kadiri ya maendeleo ya utakaso, kwa kuwa ndani mwao hamu ya Mungu inakua; lakini hata furaha takatifu

inakua kwa sababu zinazidi kujali matakwa ya Mungu kuliko tabu yao. Yeye anang'oa mzizi wowote wa umimi hata kusababisha rohoni "tendo la mwisho la upendo ambalo anamalizia kuitakasa".

Kwa kawaida kiongozi wa Kiroho hawezi kumfariji mtu anayeteseka hivyo; akisema juu ya matokeo matukufu ya jaribu hilo, na juu ya nuru tamu atakayoikuta baada ya handaki hilo, mhusika haelewi kwa jinsi alivyozama katika mateso yake. Hawezi kufarijiwa kibinadamu ila kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu na kwa *matendo sahili* ambayo huyo anasababisha ndani yake. "Roho zinazotembea mwangani zinaimba tenzi za mwanga; kumbe zinazotembea gizani zinaimba tenzi za giza. Tuache hizo na hizo vilevile ziimbe mpaka mwisho sehemu na maneno zilivyopangiwa na Mungu. Tusiweke chochote katika vile anavyojaza mwenyewe; tuache matone yote ya hiyo nyongo ya machungu ya Kimungu yatonetone hata kulevya… *Roho tu anayetia uchungu, ndiye anayeweza kufariji.* Maji hayo mbalimbali yanabubujika toka chemchemi moja" (P. Caussade).

"Naua mimi, nahuisha mimi, nimejeruhi, tena naponya, wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu" (Kumb 32:39). "Wewe unayo mamlaka juu ya uhai na mauti, watelemsha mpaka malango ya kuzimu, na kuleta juu tena" (Hek 16:13). Ndiyo yanayotokea katika usiku wa roho, ulio *kifo cha fumbo* na unaoandaa kuingia undani wa muungano na Mungu. Aliyeondolewa umimi wote anafikia unyofu mkuu. Kinyago chochote kimeanguka; mtu hana tena chochote cha kwake, yuko tayari kumpata Mungu, walivyofanya mitume waliojieleza kuwa "kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote" (2Kor 6:10). Utupu anaouona ndani unamfanya amtamani zaidi Mungu.

**THIBITISHO**

Tuliyoyasema yanaweza kuthibitishwa namna mbalimbali. Kwanza kwa *dogma ya toharani.*

Pili kwa maneno ya Mt. Yohane wa Msalaba: *"Katika usiku wa roho Mungu anamuangaza na kumtakasa mtu kama anavyowaangaza malaika;* lakini malaika mbinguni yuko tayari kupokea mwanga huo, kumbe mtu akiwa bado mchafu hawezi kuupokea pasipo uchungu, kama vile macho mabovu yanayopokea mwanga mkali mno". Tukiupokea mwanga huo wa Mungu, kwa kawaida hatutambui kwamba anatuangaza, lakini tunaangaziwa neno fulani la Injili, na hiyo ni ishara ya kupokea neema ya mwanga.

Tatu kwa *mfano wa usiku wa kawaida* unaotusaidia kuelewa ule wa roho, ambapo *tunaona mbali kuliko wakati wa mwanga uliotangulia;* ni lazima tuondolewe mianga ya chini ili tuanze kuona ukuu wa anga la Kiroho. Mitume walipokosa kuuona tena ubinadamu wa Yesu walianza kuchungulia ukuu wa umungu wake, na siku ya Pentekoste wakaangazwa na kuimarishwa vizuri hivi hata Mt. Petro aliwahubiria waliokuwa hekaluni, "mlimwua yule *Mkuu wa uzima*, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi wake" (Mdo 3:15). Tena, kesho yake: "*hakuna wokovu katika mwingine awaye yote,* kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Mdo 4:12). Mahubiri ya namna hiyo yanatokana na kuzamia fumbo la Kristo. Ndivyo inavyotakiwa kuwa ili hotuba ziwe hai na za dhati; lakini hiyo haitokei kikamilifu kabla roho haijatakaswa. "Kabla mtu hajafikia huo ulinganifu wa juu, anatakiwa kuachana na wingi usiolingana wa aina mbili: ule wa *wingi wa vitu vya nje…* na ule wa *wingi wa mawazo yanayofuatana;* ni lazima afikie *mtazamo sahili wa ukweli*" (Mt. Thoma wa Akwino). Sadaka hiyo maradufu ya hisi na ya mifuatano ya mawazo inafanyika polepole katika sala, hata akili ifikie kupima yote *Kiroho:* "Mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu. Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo" (1Kor 2:15-16).

Y. Tauler pia alieleza hayo kwa mtu, ambaye anajaribiwa na kujiona *anasali bure,* kwamba hata hivyo anatafutwa na Mungu na akimuitikia kwa unyenyekevu na tumaini kama mwanamke Mkananayo, "yatatokea yote unayoyataka na jinsi unavyotaka, kwa kuwa Bwana anasema, *kadiri ulivyoachana na ya kwako, inakubidi uingie yaliyo yangu… Kadiri mtu anavyojikana na kutoka nje yake mwenyewe, ndivyo Mungu anavyoingia kweli ndani yake*". Neema hiyo ya kujikana ndio utekelezaji wa neno la Injili, "Amin, amin, nawaambia: Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyohiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi" (Yoh 12:24). Heri kifo kinachofuatwa na ufufuko huo wa Kiroho!

### 4.1.5. ***MAELEKEZO KWA USIKU WA ROHO***

Inafaa tutoe maelekezo kadhaa kwa uongozi wa watu wanaojikuta katika ukavu huo wa muda mrefu na wa tabu nyingi.

**KUKUBALI KWA MOYO**

Elekezo la jumla kwa uongozi wa wanaojaribiwa hivyo ni kwamba tuwatendee kwa huruma nyingi na tuwasaidie kupokea matakwa ya Mungu. Elekezo la kwanza ni kwamba *wakubali kwa moyo jaribu hilo kwa muda ule wote ambao atataka udumu, na waishi kwa kujiachilia mikononi mwake.* Kadiri watakavyokubali utakaso huo, utawahi kwisha, kwa kuwa lengo alilokusudia Mungu litafikiwa mapema zaidi. Kama ule wa toharani, kwa kawaida utakuwa mfupi kadiri ulivyo mkali, isipokuwa kama mtu atatakiwa kuteseka kwa ajili ya wakosefu, mbali ya utakaso wake binafsi.

Kuhusu kujiachilia tuepe hatari mbili zinazopingana. Utulivu wa kupita kiasi unakanusha haja ya mchango

wetu na kufikia hatua ya kudai eti! Tujinyime tumaini na hamu ya kuokoka. Kumbe hapo tunapaswa "kutarajia yasiyoweza kutarajiwa" (Rom 4:18). Kinyume cha kosa hilo ni lile la kuzidisha haja ya mchango wetu kwa kupunguza ile ya sala na kupuuzia nguvu ya dua zetu kwa jinsi Mungu anavyoongoza yote.

Tuongeze maelekezo matatu kuhusiana na maadili ya Kimungu ambayo tuyaishi hasa katika usiku wa roho, tamko la mtume linapotimia kwa namna ya pekee, "Haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani" (Rom 1:17). Usiku wa roho ni usiku wa imani kuhusu mafumbo yanayoonekana giza kadiri yalivyo ya juu kuliko hisi. "Imani inahusu yasiyoonekana" (Mt. Thoma wa Akwino). Tunayoyaona hayahitaji kushuhudiwa tuyasadiki.

**IMANI KATIKA FUMBO LA MSALABA**

Basi, katika jaribu hilo ni lazima *tusadiki kwa uthabiti yale ambayo Mungu ametuambia kuhusu manufaa makubwa ya msalaba unaotakasa* katika maisha ya Kanisa na katika yale ya Kiroho ya kila mtu. Ili imani hiyo isiwe ya nadharia tu tujisemee, *Msalaba ni wa lazima na wa kufaa kwangu.* Tusadiki kwamba ni vema kwetu kutakaswa kwa uchungu hivi, kwamba hiki ni kitambulisho kimojawapo cha watoto wa Mungu, tena kwamba utakaso huo wa dhati na mchungu unamtukuza Bwana. "Kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye" (Rom 8:17). Kama vile neema inayotia utakatifu ni kushiriki umungu na kufananishwa na Mungu, vilevile kadiri *inavyotokana na Yesu Msulubiwa na inavyotufananisha naye* inatuandaa kubeba msalaba kama yeye. Kwa maana hiyo inaongeza namna maalumu kwa neema inayotia utakatifu ya watu wa kwanza.

Hivyo tunakuja kufahamu fumbo la ukombozi kwa namna hai na ya dhati zaidi, kama kwa kuling'amua. Tunakuja kuelewa Wayahudi walivyodanganyika kumlilia Bwana, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani" (Math 27:40). Kinyume chake wangepaswa kumkiri kama akida alipomuona alivyokufa, "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu" (Mk 15:39). Siku ya Ijumaa Kuu ushindi wa Kristo dhidi ya dhambi na shetani ulikuwa mkubwa kuliko ule alioupata dhidi ya kifo kwa ufufuko wake.

Basi, msalaba ni kitambulisho cha Mkristo aliyelinganishwa na Mwokozi wake, na zifuatazo ni dalili za uteule: kuvumilia tabu kwa upendo wa Mungu; kupenda maadui bila ya kujali matusi na masingizio yao; kupenda mafukara, hasa ikiwa uchungu unasukuma kuwasaidia. Kwa hiyo, kwa mfano wa watakatifu, katika usiku wa roho tunapaswa kutazama mara nyingi mateso ya Yesu na kuomba mwanga wa kuelewa kwa dhati alivyojishusha na alivyozaa kwa njia hiyo matunda ya ukombozi yasiyohesabika.

**TUMAINI IMARA NA SALA YA KUDUMU**

Katika huo utakaso mchungu tunapaswa pia *kutumaini yale yasiyotumainika kibinadamu* na kuomba msaada wa Mungu bila ya kuchoka. Ndivyo alivyofanya Abrahamu alipojaribiwa kwa kudaiwa amchinje mwanae. Kama ilivyomtokea mwanamke Mkananayo, mwanzoni Mungu anaonekana hasikilizi; kumbe anataka kupima tunavyomtumainia; na wakati huohuo tukimuomba *anatujalia neema ya kuzidi kusali,* jambo ambalo linashuhudia tayari kuwa anataka kutusikiliza.

Tunapaswa kuomba watakatifu watuombee, hasa waliojaribiwa hivyo. Tunapaswa kusali inavyofundisha liturujia, inayozidi kudhihirisha ubora wake kwa wanaovumilia jaribu hilo. "Ee Bwana, nakuomba sana, uniokoe nafsi yangu. Bwana ni mwenye neema na haki, naam, Mungu wetu ni mwenye rehema" (Zab 116:4-5). "Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu… Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji" (Zab 23:1,4). Tukisali hivyo, tumaini litatakasika na kuimarika ndani yetu; badala ya kujinyima hamu ya wokovu tunatakiwa kumtamani Mungu kwa usafi na nguvu zaidi na zaidi. Bila ya shaka hatupaswi kumlenga kwa faida yetu kwanza, kama tunavyotamani tunda linalohitajika kulindia uhai wetu, bali tutamani kumpata akiwa ni wema mkuu ili tumtukuze milele. Hivyo sababu ya upendo inainua ile ya tumaini bila ya kuiangamiza.

**UPENDO WA KULINGANA NA MATAKWA YA MUNGU**

Hatimaye katika jaribu hilo tunahitaji kupenywa na neno la Yesu, *"Chakula changu ndicho hiki: niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake"* (Yoh 4:34). Katika tabu na machungu ya roho tunapaswa kujilisha matakwa ya Mungu ili yatawale ya kwetu na umimi wote ukome moja kwa moja. Itatokea hivyo tukikubali kwa upendo wa Mungu tutende na kuteseka yale yote anayotaka kadiri tunavyoonyeshwa na utiifu, na matukio na mwanga wa ndani wa Roho Mtakatifu.

Hivyo wakati huo tuchimbe Heri Nane na kukariri maneno ya Mt. Paulo, "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?… Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je, ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?… Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Rom 8:31,35,37-39).

Ni vema pia tumuombe Mungu upendo kwa msalaba, *hamu ya kushiriki jinsi Mwanae alivyojishusha* kadiri anavyotutakia. Tena tumuombe katika hamu hiyo tuone nguvu ya kuvumilia yoyote yanayoweza yakatokea,

tuyavumilie kwa amani na hata kwa furaha ili kuinua moyo wetu na wa wale wanaotujia.

"Kabla utashi wetu haujakumbatia aibu na sadaka za kila aina, kazi ya Mungu haikamiliki rohoni au inafanyika kidogo tu. Kuvumilia tabu ni hatua fulani, lakini haitoshi. Kwa uvumilivu tunaweza tukafikia utakatifu, lakini njia pekee ya kuinuka juu yetu ni *kuungana na kushiriki sadaka ya Yesu Kristo.* Ndiyo *nguvu yetu* na chanzo cha ule uzima wa Kimungu unaojijenga juu ya magofu ya umimi wetu… Kuimarisha utashi wetu kuhusu karaha za umbile letu ni jambo linalopatikana tu kwa sala ya kudumu isiyochoka, kwa kutojiamini kabisa na kwa kumtumainia Mungu kadiri ya uweza wake usio na mipaka" (Maria wa Kutungwa Mimba). Hapo jaribu hilo gumu tutaliona kuwa jema, au walau tutasadiki linatufaa na kututakasa. "Msalaba una usalama. Msalaba una uzima. Msalaba unakulinda na maadui wote. Msalaba unakujaza utamu wa mbinguni. Msalaba una maadili yote. Msalaba una utakatifu kamili… Hakuna mtu mwenye kufahamu moyoni mwake mateso ya Yesu kama yule aliyepata kuteseka vilevile… Mateso yanayopatikana sasa hayafanani na utukufu wa siku za mbele" (Kumfuasa Yesu Kristo II,12:2,5,10).

Utakaso huo mchungu kwa kuondoa umimi na kiburi unafanya nafasi kubwa rohoni na kututia hamu ya Mungu iliyo kubwa zaidi na zaidi. "Kama vile mtu anavyoweza kukamilishwa na wema wa Mungu tu, vivyo hivyo wema huo hauwezi kutekeleza ukamilifu wake kwa nje kuliko kwa ubinadamu wetu. Huo unahitaji sana na unaweza sana kupokea mema, nao wema una ukarimu mkubwa na elekeo kubwa la kuzawadia. Hakuna kinachoufaa ufukara kuliko utajiri mkarimu, wala hakuna kinachoupendeza utajiri mkarimu kuliko ufukara wenye kuhitaji… Kadiri fukara anavyohitaji anatamani kupokea, kama vile utupu unavyotamani kujazwa. Basi ni mkutano mtamu na wa kutamaniwa ule unaofanyika kati ya utajiri na ufukara; hata karibu isingewezekana kusema upi unafurahi zaidi: kama ni wema tajiri unapoenea na kujishirikisha, au kama ni upungufu wenye kuhitaji unapopokea. Lakini Bwana wetu amesema, 'Ni heri kutoa kuliko kupokea' (Mdo 20:35). Basi, wema wa Mungu unafurahia kutugawia neema kuliko sisi kuzipokea" (Mt. Fransisko wa Sales). Nafasi inayopatikana katika mtu aliyevuliwa umimi na kiburi inamwezesha kupokea zaidi na zaidi wingi wa upendo. Kwa maana hiyo "Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu" (Mith 3:34; Yak 4:6; 1Pet 5:5), naye anawanyenyekesha ili kuwajaza.

Hayo yote yanathibitisha kwamba, "Upendo kwa Mungu unaunganisha, kwa kuwa unainua mapendo yetu kutoka mema mengi hadi wema mkuu; ndiyo sababu maadili yanayotokana na upendo yanafungamana. Kinyume chake kujipendea kunabomoa, kunatawanya na kupotosha mapendo yanayolenga viumbe vingi na vya kupita" (Mt. Thoma wa Akwino). Upendo wa Mungu unazidi kung'arisha ndani mwetu mwanga wa akili na ule wa neema, kumbe dhambi inachafua roho na kuiondolea uangavu huo wa Kimungu. Utakaso wa roho tuliouzungumzia unauondoa uchafu uliomo ndani mwa vipawa vyetu vya juu viweze kung'aa kwa mwanga wa kweli.

### 4.1.6. *MATOKEO YA ROHO KUTAKASWA HASA UPANDE WA MAADILI YA KIMUNGU*

Kisha kueleza utakaso huo na uongozi unaohitajika, tuseme matokeo yake ni yapi ukivumiliwa kwa moyo. Ndiyo lengo la Mungu katika kuwatakasa watumishi wake, kwamba upande wa juu wa roho uinuliwe kuliko umbile lake na kuandaliwa uungane na Mungu, kama vile hisi zilivyohitaji kutiishwa chini ya roho. Kati ya matokeo hayo, mengine ni ya kubomoa, yaani kukomesha kasoro, na mengine ni ya kujenga, yaani kukamilisha maadili yaliyomo upande wa juu wa roho.

**MATOKEO YA KUBOMOA**

Matokeo hayo yanajitokeza kwa kuzidi kupunguza mitawanyiko ya mawazo, upumbavu wa roho, na haja ya kujimwaga nje na ya kufarajika. Polepole umimi unakwisha. Mtu hadanganyiki kama awali, kwa kuwa anazidi kuishi kadiri ya upande wa juu wa roho, ambamo adui hawezi kuingia ila Mungu tu. Bila ya shaka adui anazidisha vishawishi vyake, lakini mtu akikimbilia kiini chake mwenyewe anamokaa Mungu, adui hawezi kumdhuru wala kujua kinachotokea ndani mwake; sanasana anaweza kushuku, kwa sababu siri za moyo ziko nje ya uwezo wake.

Utakaso huo unafuta kasoro nyingine nyingi: zile zinazohusu mafungamano na majukumu; ukali wa silika unaoelekeza kukosa subira; kiburi cha chinichini kinachosababisha vurugu na mashindano; pia kutojali shida (pengine kubwa) za jirani anayeomba msaada. Hapo mwenye jukumu la kusimamia wengine na kujitoa kwa ukarimu anaelewa kwa dhati maneno ya Yesu: "Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. Mtu wa mshahara, wala si mchungaji, ambaye kondoo si mali yake, humwona mbwamwitu anakuja, akawaacha kondoo na kukimbia; na mbwamwitu huwakamata na kuwatawanya" (Yoh 10:11-12). Ili tufaidike na maneno hayo tumuombe Bwana atuzidishie ari halisi, ambayo ina subira na upole, si umimi, inachota uzima ndani ya Mungu ili kuushirikisha zaidi na zaidi.

Pengine yanatokea *matakaso ya pamoja* (k.mf. dhuluma) tunayopaswa kufaidika nayo. Hapo ushujaa wa maadili unakuwa wa lazima, maana tunajikuta katika haja yenye heri ya kugeuka watakatifu tusije tukapoteza roho yetu. Mara nyingi wanaoonekana wema katika hali ya amani, wanajitokeza dhaifu na waoga katika shida hizo kubwa, kumbe wengine wasiotarajiwa wanajitokeza bora. Lakini haiwezekani kamwe kuwa watakatifu pasipo kulingana na Kristo msulubiwa. *Utakatifu halisi unadai utakaso uleule katika vipindi vya*

*amani na vile vya vurugu.* Watakatifu walioishi katika vipindi vitulivu vya maisha ya Kanisa walipatwa na majaribu ya Kiroho, ambayo wasingekuwa nayo wasingefikia usafi kamili alioutaka Mungu.

Hatimaye kuna majaribu mengine yanayotudai utashi mnyofu tu, k.mf. matukio ya pekee yakitulazimisha kusimama upande wa Mungu kwa sadaka kubwa. Mzee Simeoni alisema juu ya mtoto Yesu, "Huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa" (Lk 2:34). Yaani ilimbidi Yesu, aliyekuja kuokoa wote, asababishe wengine waangukie uasi kwa kukataa kumtambua kuwa ndiye Kristo. Hivyo yalifunuliwa mawazo ya siri ya Mafarisayo ambayo kwa kiasi fulani yangefichika kama wangeishi kabla yake. Kitu cha namna hiyo kinatokea waadilifu na waovu wanapofarakana k.mf. bikira Maria akitokea. Kama B. Pascal alivyosema, kuna mwanga wa kutosha kwa wanaotaka kuona, na giza la kutosha kwa wasiotaka. Matukio hayo yanathibitisha maelezo yetu kuhusu roho kutakaswa, kwa kuwa ziara za Bwana "ni za aina tofauti: za kufariji… za kukosoa… na pengine za kuhukumu" (Mt. Thoma wa Akwino). Huenda akatutembelea ili kutufariji, kama katika maono ya Lurdi, lakini tusipofaidika anaweza akatuadhibu, na tusipofaidika tena anaweza akatuhukumu.

Hayo yanaonyesha tunavyopaswa kujitahidi tufaidike na majaribu tunayoletewa na Bwana, hasa katika kipindi kirefu cha usiku wa roho tunachozungumzia. Tukikivumilia kwa moyo, kasoro nyingi zinazozuia ustawi wetu zitang'olewa moja kwa moja: hapo umimi utauachia nafasi upendo wenye ari.

**MATOKEO YA KUJENGA YA UTAKASO HUO**

Matokeo hayo ni hasa ustawi wa kasi wa maadili yaliyomo upande wa juu wa roho (kwa namna ya pekee unyenyekevu, ibada na yale matatu ya Kimungu) ambayo *yanatakaswa kikamilifu yaache kutegemea sababu za kibinadamu* ambazo ni za ziada tu na zinafanya yatekelezwe kibinadamu mno. Kwa mfano, wengine wanahudhuria misa kila siku kwa sababu ni jambo jema, lakini pia kwa sababu ni desturi ya mazingira wanapoishi, kiasi kwamba kama desturi hiyo ingekoma, labda wangeacha kuhudhuria kila siku. Kumbe ni lazima maadili yatekelezwe zaidi na zaidi kwa upendo wa Mungu, mbali na sababu za chini. Hapo inazidi kujitokeza sababu hasa ya kila moja kati ya maadili matatu ya Kimungu: ukweli mkuu unaojifunua kama sababu ya imani, uweza usio na mipaka unaokuja kusaidia kama sababu ya tumaini, na wema mkuu unaopendeza mno kama sababu ya upendo.

Lakini kwanza kuna utakaso wa namna hiyo katika unyenyekevu. Ili kiburi chote kifukuzwe ni lazima Bwana alete uvuvio maalumu wa vipaji vya elimu na akili ambavyo anatuonyesha wazi unyonge wetu kiasi tusichoweza hata kudhani, na anatuangazia moyoni vificho vya kasoro za hatari. Ni kama mwali wa jua ambao ukipenya chumba chenye giza unaonyesha mavumbi yote ambayo yanaelea hewani lakini hayakuweza kutambulika kwanza. Kwa mwanga huo unaotakasa tunaona ndani mwetu rundu ya kasoro tusizokuwa tumezizingatia; tunaabika kiasi cha kutouvumilia.

Ndio utakaso wa ule unyenyekevu wa kununa tu ambao tunajiweka pembeni kwa sababu hatukubaliwi. Hapo unakuwa unyenyekevu halisi wa moyo unaopenda kuwa si kitu ili Mungu awe yote. Unainamia ukuu usio na mipaka wa Aliye Juu na yale yote ya kwake yaliyomo katika kila kiumbe. Hapo tunang'amua kwamba kwa nguvu zetu tu hatuwezi kutenda lolote la kustahili uzima wa milele. Tunaona ukweli wa fundisho la Kanisa kwamba hata mwanzo wa wokovu unategemea neema tu na kwamba inahitajika zawadi ya pekee ili *kudumu* mpaka mwisho. Tunakuja kuelewa kuwa neema, mbali na kuwezeshwa na ridhaa yetu, ndiyo inayosababisha ridhaa hiyo: *"ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu,* kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Fil 2:13). Katika kipindi hicho, mtu anapopambana na vishawishi vikali vya kukatisha tamaa, anahitaji kuusadiki huo *uwezo wa Kimungu* wa neema unaomuinua aliye dhaifu aweze kutekeleza amri na kugeuka.

Ndivyo unyenyekevu unavyostawi hatua kwa hatua hadi ushujaa. Unadai uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu na utakaso wa Kimungu tunaouzungumzia. Wenyewe upo katika njia ya kawaida ya kufikia utakatifu; ukamilifu wa Kikristo haupatikani bila ya unyenyekevu wa namna hiyo. Katika watakatifu wote tunaona unyenyekevu huo mkubwa unaotokana na kuzama katika kweli kuu zifuatazo: 1) *Tumeumbwa na Mungu kutoka utovu wa vyote* naye anatudumisha kwa hiari yake. 2) *Pasipo msaada wa neema yake hatuwezi kutenda lolote la kustahili wokovu.* Hapo wanafikia kutambua kuwa neema inatolewa bure na kutenda yenyewe, na kuwa bila ya neema hawawezi kusonga mbele ila kurudi nyuma tu. Unyenyekevu uliotakaswa hivyo unaimba utukufu wa Mungu kuliko nyota za angani.

Kuna utakaso wa namna hiyo kwa adili la ibada pia. Ni lazima iwepo ibada halisi, yaani utayari wa utashi katika kumtumikia Bwana, hata isipokuwepo ibada ya kihisi wala faraja za rohoni kwa miezi na miaka. Hapo uvuvio wa kipaji cha ibada unakuja kusaidia adili la ibada; unatufanya tudumu katika sala bila ya kujali ukavu mkubwa wa roho. Ibada hiyo ya dhati inazaa heri ya upole.

**UTAKASO WA IMANI**

Kama vile Bwana anavyowafundisha marafiki wake kuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo, ndivyo pia anavyotakasa imani yao. Waamini wote wanayasadiki yaliyofunuliwa na Mungu, lakini wachache tu wanayaishi mafumbo yaliyoshikwa na imani. Sanasana wengi wanazingatia kweli zinazoeleweka (k.mf.

uwepo wa Mungu na maongozi yake) na wanaishia upande wa nje na wa hisi wa ibada za Kikristo. Imani dhaifu haituwezeshi *kuishi* kweli mafumbo ya Utatu mtakatifu, umwilisho, ukombozi, ekaristi na uwemo wa Roho Mtakatifu ndani mwetu. Tunaweza tukayataja kwa moyo wa ibada, lakini kwetu ni hafifu, si hai, na kweli zake ziko mbali kama nyota: hayajawa vya kutosha *mwanga wa uzima,* msingi wa machaguo yetu na vipimo vya kawaida vya mawazo yetu.

Halafu sababu ya kusadiki mafumbo hayo ni kuwa *Mungu ameyafunua kwetu,* lakini tunaishia mno kutegemea sababu nyingine zinazotusaidia: kwanza imani iliyoenea katika mazingira yetu; halafu uwiano kati ya dogma zipitazo maumbile na kweli zinazoeleweka; hatimaye mang'amuzi ya kazi ya Mungu ndani mwetu. Kama angetuondolea ghafla sababu hizo zote za ziada na katika ukavu wa roho wa miezi na miaka tusingesikia tena faraja yake ndani yetu wala kuona ulinganifu wa mafumbo yapitayo maumbile na kweli za kimaumbile, tendo la imani lingekuwa gumu. Ndivyo ilivyo hasa *mwanga wa Mungu unaotakasa unapokuja kuyaangazia katika mafumbo hayo yale ambayo ni ya juu zaidi* na yanaonekana kutolingana na akili, kama vile haki yake upande mmoja na uteule usiostahilika upande mwingine. Tena katika jaribu hilo shetani anajitahidi *kutupotosha* kwa kutuonyesha eti! Haki ya Mungu ni kali mno. Kana kwamba walaaniwa wanaomba msamaha wasiupate, wakati kwa kweli hawauombi kamwe. Vilevile adui anajitahidi kutuonyesha kuwa ugawaji wa neema haukubaliki wala haufai. Tena kuwa Mungu mwema mwenye uweza wote asingeruhusu mabaya yote yanayotukia ulimwenguni; shetani anayazidisha ili kuleta hoja mpya. Anafanya tusikie noti mbaya ili ivuruge ulinganifu bora wa mafumbo ya imani. Akitaka tusadiki hakuna kitu kisha kufa, anajitahidi kuthibitisha udanganyifu huo wa kutisha. "Siku hizi pazia nzito na nyeusi imefunika roho yangu maskini… Hakika moja tu imeonekana kunipata: kwamba mambo yote ya Kimungu hayapo… Hiyo imenipata *nitake nisitake,* kama aina ya hakika isiyopingika ambayo sina budi kuikubali… Ni kama kubomoka kwa *imani yangu niliyoipenda sana,* ambayo kwa muda mrefu iliongoza maisha yangu… Lakini pengine wazo likanijia: kwamba *ningekubali minong'ono hiyo, ningetia shakani maneno ya Bwana wetu ambaye alikuwa mtakatifu mno asiweze kudanganya,* na hapo nikasikia kama *wajibu ulionidai* niwe mwaminifu kwake kwa heshima ya kupendana kwetu, kwa kuwa tumetoleana nafsi zetu. Hapo nikaweza kusema, Bwana, *nasadiki, nataka kusadiki, lakini zidisha imani yangu"* (Fransiska wa Yesu).

Mtu anajikuta kati ya *athari mbili zinazopingana:* ile ya mwanga wa Mungu unaomtakasa kwa kurusha akili yake katika vilindi visivyodhanika vya mafumbo kama vile angetupwa baharini bila ya kujua kuogelea; na ile ya shetani anayejitahidi kupotosha athari ya mwanga huo. Inabaki sababu moja tu ya kusadiki, yaani kwamba *Mungu amefunua hayo.* Hapo ni lazima kuomba *neema ya msaada* inayosababisha tendo la imani, neema ya kushinda na kama kuruka kishawishi badala ya kukifikiria, neema ya kuambatana na *ukweli wa Mungu uliojifunua, na mamlaka yake ya kujifunua,* juu kuliko dhana zetu finyu kuhusu ukamilifu wake. Hapo mwanasala anapokea mwanga upitao maumbile wa kipaji cha akili ambao kwa kumfunulia roho ya Neno la Mungu, unamlazimisha kuvuka herufi zake na kawaida ya kumfikiria Mungu kibinadamu. Katika huo usiku wa roho, mtu yuko katika mshangao: mwanga ni mkali mno kwa macho yake dhaifu bado. Lakini atalitoka jaribu hilo akiwa na ujuzi wa juu na imara zaidi kuhusu kweli za imani, akipita maneno ya dogma asadiki kwa dhati na kuishi mfululizo mafumbo yanayotolewa katika matamko hayo. Polepole anapata kimbilio katika yule asiyebadilika, katika ukweli mkuu, katika Neno lisiloumbwa lenye kuleta ufunuo, linalojulisha k.mf. kwamba Mungu akiacha mabaya yoyote yatokee ni kwa ajili ya mema makubwa zaidi ambayo aliyaona nasi pia tutayaona milele; pengine tunayachungulia katika usiku wa roho.

Hapo imani inaondolewa takataka yote; haiishii tena kwenye sababu za ziada za kusadiki (ambazo kwa sasa zimetoweka) wala upande wa hisi wa mafumbo ya umwilisho, ukombozi na ekaristi, bali inapenya vilindi vya ufunuo. Ndivyo imani ya mitume ilivyotakaswa katika jaribu chungu la wakati wa mateso, ambapo Yesu, ambaye watatu kati yao walimtazama mtukufu mlimani, alionekana kudhalilishwa na kuangamizwa. Bila ya kujali hayo, walitakiwa kusadiki, kama bikira Maria aliyesimama imara katika imani, kuwa ni Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili na kuwa atafufuka siku ya tatu. Hata baada ya Kupaa Bwana, walipoondolewa fursa ya kumuona Yesu mfufuka, walipaswa kuishi katika giza la imani ambayo tangu Pentekoste wakaja kuitangaza kwa hakika hadi kuifia. Watakatifu waliofuata walipitia majaribu ya aina hiyohiyo, k.mf. M.H. Henri Suso kwa miaka kumi.

Mwishoni mwa jaribu hilo, imani imezidishwa mara kadhaa. Ili kuona uangavu wa mafumbo ya Mungu, ni lazima akili iwe imetoa sadaka yake kwa kujinyima kufuata macho yake na kwa kupokea kwa unyenyekevu mwanga wa Mungu. Ndio uongofu wa tatu ambapo maadili ya Kimungu yanatekelezwa kwa namna bora kuliko awali. Bwana analima tena palepale lakini kwa ndani zaidi ili mbegu anayotia ardhini izae si kumi wala thelathini, bali hata sitini na mia (taz. Mk 4:8). Hapo mtu anaanza *kumtazama* Mungu kwa dhati zaidi, kwa namna ambayo inaelekea kuwa *ya kudumu,* na ni kama *kuongea naye mfululizo.* Hekima hiyo ndiyo "*lulu nzuri"* ambayo tuuze vyote ili kuinunua (Math 13:45).

## UTAKASO WA TUMAINI

Baada ya matokeo ya utakaso wa imani, yanaanza kujitokeza yale ya utakaso wa tumaini. Anayesadiki kuwa jambo muhimu pekee ni utakatifu na wokovu, anaweza akajiuliza kama ataweza kudumu mpaka

mwisho kati ya majaribu anamojikuta.

Tumaini ni adili la Kimungu ambalo tunamlenga Mungu kama heri yetu, tukitegemea huruma yake na uweza wake usio na mipaka unaotusaidia ili tumfikie. Shabaha kuu ya tumaini ni kumpata Mungu milele; sababu yake ni *Mungu kusaidia*, kama vile sababu ya imani ni Mungu kuwa *ukweli mkuu unaojifunua*.

Kila Mkristo mwema ana adili hilo la kumiminiwa pamoja na upendo; na anapoomba neema zinazohitajika kwa wokovu anamtumaini Mungu mwenyewe. Lakini mara nyingi tumaini linakosa ukuu wake, kwa maana tunatamani mno malimwengu kadhaa yanayoonekana kuufaa wokovu wetu, kumbe sivyo; pengine tunatamani mema ya kibinadamu yanayoweza yakatudhuru na kuzuia mema ya juu yanayotokana na sisi kujibandua na yote na kuwa wanyenyekevu. Hapo tumaini linapungukiwa msukumo lisiweze kuruka moja kwa moja kwa Mungu.

Tena mara nyingi lina takataka fulani upande wa sababu yake, kwa kuwa tunatumaini msaada wa Mungu, lakini pia tunategemea kupita kiasi sababu za chini zisizo na hakika; tunajiamini mno, pamoja na uwezo wetu, maadili yetu na misaada ya kibinadamu tunayoweza kuipata; vilevile tunakata tamaa tukishindwa au tukikosa misaada hiyo. Ikiwa Mungu, kusudi atakase tumaini letu, anatuondolea ghafla malimwengu tuliyoyatumainia pamoja na sababu hizo za chini zilizotutumainisha (k.mf. wema na misaada ya marafiki, himizo na heshima ya wakubwa); na wakati huohuo anatuonyesha udhaifu wetu kwa kiasi tusichodhani; tena akiacha yatokee maradhi, masingizio na upinzani mkali dhidi yetu: je, tutaendelea kutumaini, mbali na tumaini lolote la kibinadamu, kutokana na sababu moja tu, yaani kuwa Mungu anabaki daima msaidizi wetu asiyeshindwa, litokee lolote lile?

Ndio wakati wa kujisemea, “Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, kwa kuwa *rehema zake hazikomi”* (Mao 3:22). “Bwana amejaa huruma na neema, haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili” (Zab 103:8). “Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili” (1Kor 10:13). Yeye haruhusu kamwe tujaribiwe kupita uwezo wetu unaotegemezwa na neema yake; anatusaidia daima tupate wokovu; hatuachi kamwe kwanza; anataka kutuinua toka maanguko yetu kila tunapomlilia. “Maana milima itaondoka, na vilima vitaondolewa, bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema Bwana akurehemuye” (Isa 54:10). “Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, atanisitiri katika sitara ya hema yake, na kuniinua juu ya mwamba… Bwana, uso wako nitautafuta. Usinifiche uso wako, usijiepushe na mtumishi wako kwa hasira. Umekuwa msaada wangu, usinitupe, wala usiniache, Ee Mungu wa wokovu wangu. Baba yangu na mama yangu wameniacha, bali Bwana atanikaribisha kwake” (Zab 27:5,8-10).

Watakatifu walitumaini hivyo katika majaribu makuu. “Nilisema nguvu zangu zimenipotea, na tumaini langu kwa Bwana. Kumbuka mateso yangu, na msiba wangu, pakanga na nyongo… Ni vema mtu autarajie wokovu wa Bwana na kumngojea kwa utulivu… Kwa kuwa Bwana hatamtupa mtu hata milele. Maana ajapomhuzunisha atamrehemu, kwa kadiri ya wingi wa huruma zake. Maana moyo wake haupendi kuwatesa wanadamu, wala kuwahuzunisha” (Mao 3:18-19,26,31-33). Ndivyo Mt. Yohane Mbatizaji alivyotumaini gerezani, alipoyaona yale yote yanayopinga ujio wa ufalme wa Mungu alioutangaza. Ndivyo Mt. Yohane wa Msalaba alivyotumaini gerezani, yote yalipoonekana kuchangia maangamizi ya urekebisho wa Karmeli. Ndivyo Mt. Alfonso Maria wa Liguori alivyotumaini shirika lake lilipoonekana kukoma. Ndiyo sadaka ya Isaka ambayo Mungu anawaomba tena watumishi wake ili wafanye kazi waliyokabidhiwa si kama kazi yao, bali kama kazi yake ambaye anaweza kushinda mapingamizi yote na hakika atayashinda kama ameamua milele kazi hiyo ifanikiwe.

Hapo, juu ya sababu yoyote ya kutumaini, inazidi kujitokeza sababu halisi ya tumaini la Kikristo, yaani *Mungu aliye tayari kusaidia* kutokana na uweza wake na stahili za Yesu zisizo na mipaka. Hapo mtu anajisikia kurudia sala ya Esta, “Bwana wangu, wewe peke yako u mfalme wetu, unisaidie mimi niliye mkiwa, wala sina msaidizi mwingine ila wewe, maana hatari yangu imo mikononi mwangu… Ee Mungu, uweza wako ni juu ya yote; isikie sauti yao wasio na tumaini, utuokoe mikononi mwao wafanyao maovu, uniokoe katika hofu yangu” (Est 4:17l,y). Hapo tumaini linageuka kujiachilia kikamilifu kwa Mungu kuhusu kazi yake duniani na kuhusu wokovu wa milele.

Vilevile tunaposaidia wagonjwa mahututi tunatakiwa kuwaombea tumaini hilo la kujiachilia kikamilifu, na kadiri utashi wao unavyolingana na *matakwa ya Mungu yaliyokwishajulikana*, uko tayari kujiachilia kwa *yale yasiyojulikana bado*. Hivyo mtu anajiinua juu ya giza la dunia, udanganyifu na dhambi, ajizamishe katika giza la maisha ya ndani ya Mungu na la upendo wake kwa kila mmojawetu. Hapo si kwa nadra mtu anajaribiwa kuhusu fumbo la uteule, kama vile Mt. Katerina wa Siena ambaye shetani alimuambia, “Malipizi hayo yanasaidia nini kama hujateuliwa? Kumbe kama umeteuliwa, utaokoka bila ya hayo”. Mtakatifu akamjibu, “Kama nimeteuliwa, juhudi zako za kunipoteza zinasaidia nini? Kumbe kama sijateuliwa, kwa nini unanishughulikia hivi?” Ni kwamba uteule, kama vile maongozi yote ya Mungu, unahusu si lengo tu, bali pia njia za kulifikia. Kama vile katika maisha ya kawaida hatupati mavuno tusipopanda mbegu, katika utaratibu wa neema wokovu haupatikani pasipo sala na maadili.

Mwishoni mwa utakaso huo wa tumaini, adili hilo limeondolewa umimi uliochanganyikana nalo, pamoja na

hamu isiyoratibiwa ya faraja, nalo limekuwa imara zaidi katika usafi wake. Limekuwa *hamu motomoto ya kumpata Mungu kuliko zawadi zake;* hata hivyo yeye hajitokezi: ndipo yanapoanza kuonekana matokeo ya utakaso wa upendo.

**UTAKASO WA UPENDO**

Hasa katika adili hilo matakaso ya Kimungu yanafanana na yale ya toharani, mbali ya tofauti kubwa ya kwamba hayo ya pili hayaongezi upendo wala stahili. Kila Mkristo mwema anao upendo, ambao tunampenda Mungu kwa ajili yake mwenyewe; lakini tunampenda pia kwa sababu anatupatia faraja, tunahisi uwemo wake mwetu, na kazi tunazomfanyia zinafanikiwa na kutufurahisha. Vilevile tunampenda jirani kwa ajili ya Mungu, kwa kuwa anapendwa na Baba yetu sote; lakini tunampenda pia kwa kuwa anaitikia upendo wetu; kumbe asipoonyesha shukrani hatumpendi vya kutosha, ingawa tunapaswa kuwapenda maadui pia na kuwaombea wanaotudhulumu. Maana yake upendo wetu una takataka na hautawali vizuri uchungu au ukali kwa kukosewa adabu.

Hivyo, Bwana anapotaka mtu mwenye tumaini kubwa afikie upendo safi ambao ampende kweli kwa ajili yake mwenyewe kuliko kwa zawadi zake, anamnyima kwa miezi na miaka faraja yoyote ya Kiroho pamoja na hisi ya uwemo wake, ingawa anazidi kuungana naye na kumtendea kwa dhati. Anaonekana kumuacha kama Yesu alipolia msalabani, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Zab 22:1). Ni maneno ya Zaburi ya Kimasiya ambayo yanafuatwa na mengine ya tumaini kamili, kujiachilia na upendo, kama ilivyotokea moyoni mwa Yesu. Katika usiku huo wa roho, mtu anapojiona ameachwa na Mungu, anatimiza tendo kubwa la upendo kwa sababu moja tu tena safi, yaani kwamba Mungu mwenyewe ni wema usio na mipaka, bora mno kuliko neema zake zote, na kwamba ndiye aliyetangulia kutupenda. Hivyo, kwa mfano wa Mwanae msulubiwa, anapaswa kumrudishia upendo kwa upendo.

Mt. Teresa wa Mtoto Yesu alipitia saa hizo chungu mwishoni mwa maisha yake, alipoandika, "Mungu amependa niyakabili mateso mengi ya aina mbalimbali. Tangu niwepo duniani, nimepata kuteseka sana. Lakini ikiwa utotoni mwangu niliteseka kwa huzuni, sasa siteseki tena kwa jinsi hiyo, bali kwa furaha na amani. Sasa ninafurahi kweli kuteseka… Wakati ule wa furaha wa kipindi cha Pasaka, Yesu alinifahamisha kuwa kweli wapo watu wasio na imani; watu ambao kwa kutotumia vema neema, waliipoteza hiyo hazina ya thamani, iliyo asili ya furaha halisi pekee. Pia Yesu aliruhusu roho yangu ivamiwe na giza jeusi kabisa, hata wazo la mbingu, ambalo awali lilikuwa tamu kwangu, likawa linasababisha tu mahangaiko na mateso. Jaribu hilo limedumu si siku chache wala majuma machache, lisiondolewe mpaka saa iliyopangwa na Mungu mwenyewe, ambayo haijafika. Ningependa kuweza kueleza jinsi ninavyojisikia; lakini, lo! Ninakiri kwamba haiwezekani. Ingembidi mtu apite mwenyewe katika shimo hili la giza ili kuelewa weusi wa giza hili… Hata hivyo, Ee Bwana, huyu mwanao amefahamu mwanga wako wa Kimungu; naye sasa anawaombea hao ndugu zake msamaha. Kwa sababu yuko radhi kuula mkate huu wa huzuni, kadiri ya muda wewe utakaoutaka; wala hataki kusimama na kuacha meza hii iliyojaa uchungu ambapo maskini wakosefu watakula mpaka siku ile uliyoipanga. Je, hawezi kuomba kwa ajili yake na kwa niaba ya ndugu zake, akisema, 'Utuonee huruma, Ee Bwana, maana sisi tu maskini wakosefu! Ee Bwana utuachilie twende zetu tumetakata! Uwajalie wale wote ambao hawajaangazwa na ule mwanga wa imani, siku moja nao wauone uking'aa…' Moyo wangu unaochoshwa na giza linalouzunguka, ninapotaka kuufariji kwa kuikumbuka ile nchi angavu ninayoitamani, ndipo teso langu linapokuwa maradufu. Inaonekana kana kwamba hilo giza, likiazima sauti ya wakosefu, linanidhihaki likisema, 'Unaota tu juu ya mwanga, na juu ya nchi ya kwenu yenye manukato mazuri sana; pia unaota kuwa utakaa milele na Muumba wa maajabu hayo yote; isitoshe unasadiki kuwa siku moja utaondoka kwenye ukungu huu unaokuzunguka! Basi, endelea, endelea kuota vile, hata kufurahia kifo, ambacho, ole wako, hakitakupatia yale unayotumaini, bali tu usiku wa giza nene zaidi, usiku wa kutokuwepo kitu chochote kile…' Adui yangu anaponichokoza, ninajihami kijasiri. Nikifahamu kuwa haifai kukubali kupigana naye, namgeuzia mgongo nisikubali kumtazama usoni; bali ninamkimbilia Yesu wangu. Ninamuambia Yesu kuwa niko tayari kuimwaga damu yangu, hadi tone la mwisho, ili kuiungama imani yangu, kwamba kuna mbingu. Pia ninamuambia kuwa ninaridhika kutoionja duniani humu furaha ya hizo mbingu nzuri ili yeye awafungulie milele wale maskini wasioamini. Hivyo, licha ya kujaribiwa namna hii kwa kuondolewa faraja yangu yote, naweza kupaliza sauti nikisema, 'Umenifurahisha, Bwana, kwa kazi yako; nitashangilia kwa ajili ya matendo ya mikono yako' (Zab 92:4). Kwa sababu je, iko furaha kubwa kuliko ile ya kuteseka kwa ajili ya upendo wako? Kadiri teso lilivyo la ndani zaidi, na lisivyoonekana na macho ya watu, ndivyo linavyokufurahisha zaidi, Ee Mungu wangu! Lakini, hata kama kweli wewe usingelijua hili teso langu, jambo lisilowezekana, ningefurahi kuteseka, ikiwa kwa kuteseka ningezuia au kufidia dhambi moja ya utovu wa imani… Hivyo basi, ninapoimba juu ya furaha ya mbingu na juu ya kuishi na Mungu milele, sisikii furaha hiyo moyoni, ila tu ninayaimba yale *ninayotaka kuyasadiki.* Ni kweli kwamba pengine mshale mdogo sana wa jua hutokeza na kuliangaza giza langu; katika kitambo hicho naacha kujaribiwa. Lakini baadaye kumbukumbu ya mwali ule, badala ya kunifurahisha, inasababisha giza langu kuwa hata nene zaidi. Mama mpendwa, nilikuwa sijapata kufahamu jinsi Bwana wetu alivyo mwema na mwenye huruma kweli; maana hakuniletea jaribu hilo kabla sijaweza kulikabili. Kwa kuwa nadhani lingenijia kidogo mapema, lingenitumbukiza katika hali ya kukata tamaa.

Kumbe sasa linaniondolea kila kitu ambacho kingekuwa kiridhisho cha kimaumbile kwa hamu yangu ya mbingu".

Ndio utakaso wa pamoja wa maadili ya Kimungu, ambao kwake uliendana na malipizi kwa ajili ya wakosefu. Humo matendo ya imani, tumaini na upendo ni kama yameunganika katika kujiachilia kikamilifu kwa matakwa ya Mungu kama Yesu msalabani, "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu" (Lk 23:46). "Kadiri mtu anavyoelewa ukuu wa Mungu na kuona anavyostahili kupendwa, anazidi kuwaka upendo kwake na kuona tabu ya kutoungana naye bado" (Mt. Teresa wa Yesu). Baada ya utakaso huo wa mwisho, upendo kwa Mungu na kwa jirani umeondolewa takataka yoyote kama dhahabu iliyojaribiwa kwa moto, tena umezidishwa.

Tukisifu upendo wa mke wa baharia asiyekoma kumfikiria mumewe, ambaye tangu miezi hana habari zake na huenda akafa, bali anazidi kumpenda na kuwalea wanae wampende kana kwamba yupo; basi, hatuwezi kuacha kushangaa usafi wa upendo wa bibi arusi wa Yesu Kristo ambao utamu wake unageuka nguvu ya kuungana naye katika jaribu lolote, kwa kuwa: "Upendo una nguvu kama mauti… maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, wala mito haiwezi kuuzamisha" (Wim 8:6-7). Msalabani upendo wa Bwana, anayewaunda wafuasi kwa mfano wake, ulikuwa na nguvu kuliko mauti ya roho, dhambi na shetani na kwa ufufuko ukashinda kifo kilicho tokeo la dhambi. Katika kutakaswa na Mungu, watakatifu wanaungana na Kristo katika mateso kabla hawajalinganishwa naye katika utukufu wa milele.

**MATESO YANAYOWEZA YAKAENDANA NA KUTAKASWA KWA ROHO**

Mt. Teresa wa Yesu aliposema juu ya utakaso huo hakubainisha vizuri mateso ambayo yanaendana nao mara nyingi lakini si kwa lazima: "Mungu wangu! Jinsi zilivyo kubwa tabu za nje na za ndani ambazo mtu anapaswa kuzivumilia kabla hajaingia makao ya saba! Kwa kweli ninapozifikiria naona kwamba angewahi kuzijua, udhaifu wake wa kimaumbile ungesita kuamua hata kama angeahidiwa faida gani… Kweli katika hali hizo inaonekana yote yamepotea. Ni masingizio ya watu tunaohusiana nao… Wale walioonekana marafiki wanasaliti, tena wanang'ata kwa ukali zaidi; jambo ambalo hakika linaumiza kwa dhati. Ukiwasikia eti! Mtu huyo anadanganyika kwa namna ya pekee. Eti! Yote yanayomtukia yanatoka kwa shetani. Eti! Atapotea kama fulani au fulani… Namfahamu mtu aliyefikia hatua ya kuhofia hatapata tena padri anayekubali kumuungamisha… Mbaya zaidi ni kwamba maneno hayo, badala ya kukoma mapema, yanadumu pengine maisha yote… Na jinsi ilivyo ndogo idadi ya wanaotetea ikilinganishwa na ile ya wanaoteta wanavyotaka. Mang'amuzi ni kwamba watu wako tayari kutoa vilevile sifa na lawama, hata mtu asijali tena hizo wala hizo. Baadaye anaimarika badala ya kukata tamaa akiona anasemwa, kwa kuwa ameng'amua faida yake. Anaona kana kwamba wanaomdhulumu hawamkosei Mungu, ila mwenyewe amewaruhusu kwa faida yake. Jambo hilo linaonekana naye wazi. Hapo kwa kawaida Bwana anamtumia maradhi makubwa… Halafu niseme nini kuhusu tabu za rohoni? Ingewezekana kutoa picha yake, zile za nje zingeonekana nyepesi sana!… Teso lingine linalowapata, hasa kama waliwahi kutenda makosa, ni kwamba wanadhani Mungu ameacha wadanganyike kutokana na dhambi zao. Ni kweli kwamba wakati wa kujaliwa fadhili hawawezi kuwa na wasiwasi kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayezitenda ndani mwao. Lakini tabu yao inaanza upya kwa kuwa fadhili hizo zinapita haraka, wakati kumbukumbu ya dhambi zao inabaki, tena wenyewe wanaona ndani mwao kasoro nyingi (nani hana?). Muungamishi akiwatuliza, tabu inapungua, halafu inarudi tena. Lakini kama padri mwenyewe ndiye anayezidisha wasiwasi wao, tabu inakuwa karibu haivumiliki, hasa kama wakati huo wamo katika ukavu ambamo tunadhani hatujawahi wala hatutawahi kuwaza lolote juu ya Mungu na ambamo tukisikia anazungumziwa ni kama kusikia juu ya mtu tuliyepata habari zake muda mrefu uliopita… Bwana anamruhusu shetani amshawishi na kumfanya aamini amelaaniwa na Mungu… Katika dhoruba hiyo hawezi kupata faraja yoyote… dawa pekee ni kutumainia huruma ya Mungu, naye isipotarajiwa kwa neno moja analomuambia mtu au kwa tukio moja linalotukia anamkomboa mara na mabaya yake yote".

### 4.1.7. *HATUA YA WALIOKAMILIKA: MUUNGANO WAO NA MUNGU*

Baada ya utakaso mchungu tuliouzungumzia, kuna aina ya ufufuko na mwanzo wa maisha mapya. Ndicho walichokionja mitume siku ya Pentekoste ambapo, kisha kuondolewa ubinadamu wa Yesu, waligeuzwa kwa kuangazwa na kuimarishwa na Roho Mtakatifu wakahubiri Injili mpaka miisho ya dunia iliyojulikana wakaithibitishe kwa damu yao. Basi, tuone sifa kuu za hatua ya waliokamilika zinazoitofautisha na zile zilizotangulia. Hasa tunahitaji kuzingatia sifa za ujuzi wao juu ya Mungu na juu yao wenyewe na sifa za upendo wao.

**KUMJUA MUNGU KAMA KWA MANG'AMUZI NA KWA MFULULIZO**

Waliokamilika wanamjua Mungu kama kwa mang'amuzi si ya mara kwa mara, bali karibu ya mfululizo. Wanamuelekea si wakati wa ibada au sala tu, bali pia nje, katikati ya shughuli; hawapotewi na uwepo wake, bali wanadumisha muungano wao naye. Mtu anayejipendea, ajue asijue, anajifikiria daima na kuhusisha yote naye mwenyewe; anaongea mfululizo na nafsi yake kuhusu tamaa zake, huzuni zake na furaha zake za juujuu; maongezi hayo ya ndani hayazai kitu. Kinyume chake, aliyekamilika *anamfikiria mfululizo Mungu,*

*utukufu wake na wokovu wa watu* na kuelekeza yote huko, ajitambue asijitambue. Ndani mwake haongei tena na nafsi yake bali na Mungu, na maneno ya Injili yanamjia mara nyingi kuangazia maisha ya kila siku, matukio yoyote, ya furaha au ya huzuni. Anaimba utukufu wa Mungu na kueneza mwanga na joto la Kiroho anavyovipata mfululizo toka juu. Sababu ni kwamba hamtazami tena Mungu kama wanavyofanya wale wanaoanza, yaani kupitia vitu vinavyoonekana au mifano ya Injili, jambo ambalo haliwezi kufanyika mfululizo. *Katika kivuli cha imani anatazama wema wenyewe wa Mungu,* kwa mfano wa mwanga ambao unatuzunguka na kuangaza vyote.

Ni ujuzi wa wema mkuu unaoangaza yote; hapo mtu anaona kama kwa mang'amuzi kwamba Mungu amefanya yote, upande wa maumbile na upande wa neema, ili kuridhisha wema wake na kwamba akiacha baya litokee ni kwa kulenga jema kubwa zaidi. Kutokana na usahili wake wa hali ya juu, mtazamo huo wa Kiroho unaweza kudumu mfululizo, tena hauzuii kuona matukio yanayofuatana maishani, bali unayaona yote toka juu, kidogo kama anavyofanya Mungu, au kama mtu ambaye mlimani anaona yote yanayotokea bondeni. Mtazamo huo unaona vizuri ajabu maana ya dhati hata ya mambo madogomadogo muhimu. Hivyo unafuta kasoro zinazotokana na haraka ya kimaumbile, kujifanya lengo la yote bila ya kujitambua, na kukosa zoea la kujikusanya.

Yatokanayo ni kwamba *waliokamilika wanajifahamu* si ndani mwao tu, bali ndani ya Mungu, aliye chanzo chao na kikomo chao. Ndani mwake wanaona unyonge wao na umbali usiopimika unaowatenga na Muumba. Ni kama wanajisikia wakidumishwa na upendo wake wa hiari; wanang'amua mfululizo wanavyohitaji neema yake kwa tendo lolote la kuwaletea wokovu. Kwa makosa yao hawakati tamaa, bali wanajifunza unyenyekevu halisi. Wanajiona kwa unyofu watumishi wa bure, ambao peke yao hawawezi kitu, ila Bwana anaridhika kuwatumia atende makuu yanayoandaa uzima wa milele. Wakiona makosa ya jirani, wanafikiri hakuna dhambi ambayo wasingeweza kuitenda kama wangekuwa na urithi uleule na kuwekwa katika hali zilezile na vishawishi vilevile vya kwake. Kumbe wakiona maadili makubwa ya mwingine wanayafurahia kwa ajili ya Bwana na kwa ajili yake, wakikumbuka kwamba katika mwili wa Kristo kiungo hakiwezi kustawi viungo vingine visifaidike.

Mtazamo huo wa kumiminiwa unatokana na imani hai iliyoangazwa na kipaji cha hekima ambacho kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu kinaonyesha *hakuna linalotokea pasipo Mungu kutaka* (kama ni jema) *au pasipo Mungu kuacha litokee* (kama ni baya la lazima kwa upatikanaji wa jema kubwa zaidi). Kutokana na usahili na upana wake, mtazamo wa juu hivi unaweza kuwa karibu wa kudumu, kwa maana matukio ya kila siku yanajipanga kama mafundisho ya kimatendo toka kwa Mungu mwema, na kama utekelezaji wa Injili katika maisha ya kila mmoja. Ni Injili inayozidi kuandikwa rohoni mwa watu hadi mwisho wa nyakati. Hapo Mkristo, kwa kujua ukamilifu wa Mungu na maadili ambayo ayatekeleze, ameacha nyuma si wazo *la juujuu* tu, bali wazo *la teolojia* pia, na kufikia wazo *hai* lenye utajiri wa mang'amuzi linalomuelekeza alitekeleze kwa faida ya watu. Ni wazo hai la wema usio na mipaka, la usahili kamili na la unyenyekevu halisi unaomfanya apende kuwa si kitu ili Mungu awe yote.

**KUMPENDA MUNGU KWA ROHO YOTE**

Hivyo aliyekamilika anafikia ule urafiki wa dhati na Bwana ulio lengo la upendo. Ni kutakiana mema na *kuishi wawili pamoja katika ushirika wa Kiroho wa kudumu. Kama vile mwenye umimi akijifikiria mfululizo anajipenda vibaya katika vyote, aliyekamilika akimfikiria Mungu karibu mfululizo anampenda kwa kudumu,* si tu kwa kukwepa dhambi na kuiga maadili ya Bwana, bali "kwa kuambatana naye, kumfurahia na kutamani kifo ili kuwa naye" (Mt. Thoma wa Akwino). Hilo ni *tendo la moja kwa moja,* sahili, ambalo linageuza utashi wetu na kuwa chanzo cha matendo yaliyofikiriwa. Kwa kweli aliyekamilika anajipenda ndani ya Mungu kwa kumpenda kuliko nafsi yake, na anatamani mbingu ili kutukuza milele wema wa Mungu, asili ya mema yote, kuliko kwa heri yake binafsi. Ndio upendo safi wa Mungu na wa watu ndani mwake, ndiyo ari ya kitume, motomoto kuliko awali, lakini pia nyenyekevu, tamu, vumilivu. Aliyekamilika hainukii mara kwa mara tu kilele hicho cha roho, bali ni kana kwamba amehamia humo, amekuwa mtu wa Kiroho na wa Kimungu anayeabudu katika Roho na ukweli. Kwa hiyo anadumisha *amani* karibu mfululizo, hata katika hali za kusikitisha na zisizotarajiwa, na mara nyingi anaishirikisha hata kwa watu waliovurugika zaidi. Ndiyo sababu heri ya wenye amani inahusiana na kipaji cha hekima ambacho, pamoja na upendo, kinawatawala moja kwa moja.

Ndizo sifa za hatua hiyo: kuongea kwa ndani karibu mfululizo na Mungu anayependwa kwa usafi kuliko vyote na kwa hamu hai ya kufanya ajulikane na kupendwa.

**UWEMO WA UTATU MTAKATIFU KATIKA ROHO ILIYOTAKATA**

Mbinguni Nafsi tatu za Mungu wanaishi katika roho iliyotakata kama katika hekalu ambamo wanajulikana na kupendwa. Utatu mtakatifu unaonekana wazi ndani mwa roho hiyo unayoidumisha katika uhai na katika neema isiyoweza kupotezwa. Hivyo kila mwenye heri ni kama tabenakulo hai, kama hostia iliyogeuzwa, tena yenye ujuzi na upendo upitao maumbile. Utangulizi wa hali hiyo unapatikana duniani katika mtu

aliyekamilika aliyefikia muungano unaotugeuza tutakaouzungumzia mbele. Kwa sasa tuseme kuwa muungano huo wa dhati ni wa nadra lakini si nje ya utaratibu wa kawaida, kwa kuwa ni *mwendelezo wa uwemo wa Utatu mtakatifu ndani ya kila mwadilifu.* Uhai unaoletwa na neema inayotia utakatifu ni mbegu ya utukufu; kimsingi ni uhai uleule wa milele. Ikiwa mbinguni Utatu mtakatifu umo rohoni mwa mwenye heri ambamo unaonekana bila ya kizuio, ni lazima uwemo tayari ndani ya mwadilifu katika giza la imani, ukijulikana na kama kung'amuliwa naye kadiri alivyotakata. Kama vile roho inavyojing'amua kuwa asili ya matendo yake, inajaliwa pia *kumtambua Mungu kama asili ya matendo yapitayo maumbile* ambayo isingeweza kuyasababisha pasipo uvuvio maalumu toka juu. Kadiri mtu alivyotakata, anatofautisha ndani mwake yale yanayotokana naye kwa msaada wa kawaida wa Mungu, na yale yanayotokana na uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu.

Utambuzi huo wa uwemo wa Mungu unategemea hasa kipaji cha hekima kinachotufanya tupime mambo ya Kimungu kwa *kulingana* nayo, kwa *hisi ipitayo maumbile* inayotegemea upendo, na kwa *uvuvio wa Roho Mtakatifu* anayetumia hisi hiyo aliyotutia ili tumtambue. Hivyo tunaonja mafumbo ya wokovu na uwemo wa Mungu ndani mwetu kwa mfano wa wanafunzi wa Emau walioambiana, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia Maandiko?" (Lk 24:32). Ni ujuzi ambao *unafanana na mang'amuzi,* unapita mifuatano ya mawazo na kulingana na ule wa roho inayojifahamu kama asili ya matendo yake. Mungu, asili ya neema na ya wokovu, yumo ndani mwetu kuliko sisi wenyewe, naye *anatuvuvia* tutende mambo ya dhati tusiyoyaweza peke yetu, na ndivyo anavyojitambulisha kwetu kama chanzo cha maisha ya Kiroho.

Ujuzi huo *unafanana tu* na mang'amuzi kwa sababu mbili: 1) haumfikii Mungu moja kwa moja, inavyotokea kwa kumuona mbinguni, bali katika tendo la upendo wa kitoto analolisababisha ndani mwetu; 2) hatuwezi kutofautisha kwa hakika matendo hayo ya upendo yapitayo maumbile na miruko ya kimaumbile ya moyo inayofanana nayo: hivyo tusipojaliwa ufunuo maalumu hatuwezi kuwa na hakika ya mia kwa mia ya kwamba tuna neema inayotia utakatifu.

Uwemo wa Utatu mtakatifu unadumu hata usingizini, mpaka tunapodumu *kuwa tumeunganika* na Mungu kutokana na hali ya neema. Lakini ni wazi kuwa muungano huo wa kawaida unalenga *muungano* tunaouzungumzia sasa, hata ule wa dhati zaidi unaotugeuza.

Basi, katika roho iliyotakata inazidi kuonekana *hali ipitayo maumbile ya kufanana na Mungu.* Roho kwa umbile lake inayo tayari sura ya Mungu, kwa kuwa si mwili na inaweza kujua na kupenda. Kwa neema inayotia utakatifu, asili ya maadili ya Kimungu, inaweza pia kumjua na kumpenda Mungu kwa namna ipitayo maumbile. Kadiri neema hiyo na upendo vinavyokua vinatutenganisha na mambo ya chini na kutuunganisha na Mungu. Hatimaye mbinguni neema kamili itatuwezesha kumuona moja kwa moja anavyojiona na kumpenda anavyojipenda. Hapo hali ya kufanana naye itakamilika, upendo usioweza kupotezwa utatufananisha na Roho Mtakatifu aliye upendo-nafsi; heri ya kumuona Mungu itatufananisha na Neno ambaye akiwa uangavu wa Baba atatufananisha naye. Kutokana na hayo tunaelewa unavyotakiwa kuwa tangu hapa duniani muungano kamili ambao ni *utayari wa moja kwa moja wa kujaliwa heri ya kumuona mara baada ya kufa* bila ya kupitia toharani. Ndiyo siri ya maisha ya watakatifu. Pengine hali hiyo ipitayo maumbile ya kufanana na Mungu na Yesu inadhihirika mwilini pia.

**DALILI ZA UTATU MTAKATIFU KUWEMO KATIKA ROHO ILIYOTAKATA**

Dalili hizo zilitajwa na Mt. Thoma wa Akwino alipojiuliza kama mtu anaweza kujua ana hali ya neema. Ingawa hazimwezeshi kuwa na hakika ya imani juu ya hali hiyo, zinamwezesha kukaribia meza ya Bwana bila ya kuogopa kukufuru. Zile muhimu zaidi zinaorodheshwa kama ifuatavyo kuanzia zile za chini.

1) *Ushuhuda wa dhamiri njema* isiyojisikia kuwa na dhambi yoyote ya mauti. Ndiyo dalili ya msingi inayodaiwa na zile ambazo zinaifuata na kuithibitisha.

2) *Furaha ya kusikia Neno la Mungu,* si kwa kulisikiliza tu, bali kwa kulitekeleza.

3) *Kuonja hekima ya Mungu* hata kujisomea Injili ili kutafuta roho yake ndani ya maneno na kujilisha hata kuhusu fumbo la msalaba, ukiwa ni pamoja na ule wa kuubeba siku kwa siku.

4) *Elekeo la kuongea na Mungu kwa ndani,* na kuanza tena maongezi hayo yakikatika. "Urafiki unamuelekeza mtu atake kuongea na rafiki yake. Maongezi ya mtu na Mungu yanafanyika kwa kumkazia macho katika sala ya kumiminiwa, kadiri ya maneno ya mtume Paulo, 'Sisi wenyeji wetu uko mbinguni' (Fil 3:20). Kwa kuwa Roho Mtakatifu anatutia upendo wa Mungu anatuelekeza vilevile kumtazama. Ndiyo sababu mtume alisema pia, 'Sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho' (2Kor 3:18)" (Mt. Thoma wa Akwino). Kabla ya hayo, mwalimu huyo wa Kanisa aliandika kuwa maongezi ya ndani na Mungu ni kama ufunuo wa mawazo ya siri zaidi, kwa maana sisi hatuna cha kumficha, naye anatukumbusha maneno ya Injili yanayotuonyesha yale yote yanayotupasa dakika kwa dakika. Ndiyo matokeo ya urafiki ambao "kwa namna fulani unaunganisha mioyo miwili kuwa mmoja, hivi kwamba tunachomfunulia rafiki halisi tunaona hakijatutoka".

5) *Kumfurahia Mungu,* kwa kukubali kwa dhati matakwa yake hata katika mapingamizi. Pengine wakati

wa kuvunjika moyo tunatiwa furaha safi na ya juu inayoondoa huzuni yoyote. Hiyo ni dalili kubwa ya kutembelewa na Bwana. Yesu alipomuahidi Roho Mtakatifu alimuita Mfariji. Kwa kawaida tunamfurahia kadiri tunavyotimiza amri zake, kwa kuwa hivyo tunazidi kuwa moyo mmoja naye.

6) *Uhuru wa wana wa Mungu.* "Wana wa Mungu wanaongozwa na Roho Mtakatifu si kama watumwa, bali kama viumbe huru… Roho Mtakatifu anatufanya tutende akiongoza utashi wetu wenye hiari utake, kwa sababu anatufanya tumpende Mungu na anatuelekeza tutende kwa upendo wake, si kwa hofu kama watumwa" (Mt. Thoma wa Akwino). "Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, 'Aba!' yaani, 'Baba!'. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Rom 8:15-16). "Alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru" (2Kor 3:17), yaani ukombozi kutoka utumwa wa dhambi. "Kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi" (Rom 8:13). Ndio ukombozi halisi, yaani uhuru mtakatifu wa wana wa Mungu wanaotawala pamoja naye juu ya tamaa, juu ya roho ya ulimwengu na juu ya uovu.

7) *Kumzungumzia Mungu kama kwa kufurika toka moyoni.* Kwa namna hiyo "mahubiri yanatakiwa kutokana na ukamilifu wa kuzama katika mafumbo ya imani" (Mt. Thoma wa Akwino). Roho Mtakatifu anazidi kujitokeza kwetu kama chemchemi ya neema mpya daima, "chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele" (Yoh 4:14), chemchemi isiyokwisha ya mwanga na upendo. Ndiyo faraja yetu kati ya huzuni za hapa uhamishoni. Katika matatizo ya kimataifa ya wakati huu, linadumu tumaini kubwa, kwa kuwa mkono wa Bwana haujafupika. Tunaona alivyo mwingi wa huruma daima katika watakatifu anaozidi kuwaleta ulimwenguni. Ndio watumishi wake wakuu wenye mifano bora ya imani, tumaini na upendo, ambayo mingi tunaweza kuifuata.

Kwa msimamo huo inafaa wanaoishi Kiroho wajiweke wakfu kwa Roho Mtakatifu ili kuongozwa naye zaidi kwa kutambua na kufuata minong'ono yake, kama vile wanavyojiaminisha kwa Maria ili awaongoze kwa Mwanae, na wanavyojiweka wakfu kwa Moyo mtakatifu wa Yesu awafikishe kwa Baba yake.

## 4.1.8. ***AINA MOJAWAPO YA MAISHA MAKAMILIFU: NJIA YA UTOTO WA KIROHO***

Njia ya utoto wa Kiroho iliyofundishwa na Mt. Teresa wa Mtoto Yesu inadhihirisha utume aliopangiwa na Mungu wa kulea watu wa wakati huu. Njia hiyo inafuata sifa njema za umbile la mtoto na kulingana na mafundisho ya teolojia kuhusu neema inayotia utakatifu, maadili ya kumiminiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu. Tuzingatie basi sifa hizo za mtoto, sifa kuu za mtoto wa Mungu na tofauti zilizopo kati ya utoto wa Kiroho na ule wa kimaumbile. Hivyo tutaona mwanga mwingi kuhusu teolojia ya neema.

### SIFA ZA KIMAUMBILE ZA MTOTO

Mbali ya kasoro ndogondogo, mtoto kwa kawaida ni sahili na anafahamu udhaifu wake. Hasa kama amebatizwa na kulelewa Kikristo, unyofu unajitokeza ndani yake: anasema anavyowaza na anaeleza bila ya mizunguko anavyotaka, asiogope watu watasema nini; haigizi kwa ujanja bali anajionyesha alivyo. Halafu anafahamu udhaifu wake, kwa kuwa peke yake hawezi kitu, bali anawategemea wazazi na inampasa apokee vyote toka kwao; kujifahamu dhaifu ni aina ya unyenyekevu.

Ujuzi huo unaelekeza kutekeleza maadili ya Kimungu kwa dhati na usahili. Kwanza mtoto anaelekea kusadiki anayoambiwa na wazazi wanapomzungumzia Mungu na kumfundisha kusali. Anaelekea kuwatumainia wanapomfundisha kumtegemea Mungu kabla hajajifunza sala ya tumaini katika katekisimu na kuitumia asubuhi na jioni. Hatimaye mtoto anawapenda wazazi kwa moyo kwa kuwa anawawia vyote, na ikiwa hao ni Wakristo kweli wanaelekeza moyo huo mdogo kwa Mungu, kwa Yesu na kwa Mama yake.

Katika unyofu huo, katika ujuzi wa udhaifu wake na katika utekelezaji sahili wa maadili ya Kimungu mna kiini cha maisha ya Kiroho ya hali ya juu. Ndiyo sababu Yesu, alipotaka kuwafundisha mitume wake umuhimu wa unyenyekevu, alimuita mtoto katikati yao akasema, "Amin, nawaambia: Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Math 18:3). Nyakati hizi tumeona ulivyotimia utabiri wa Mt. Pius X, "Kutakuwa na watakatifu kati ya watoto" walioalikwa mapema kupokea ekaristi mara nyingi.

Kwa kawaida mtoto akifikia ubalehe, anapotewa na usahili wake na ujuzi wa udhaifu wake; anataka kujifanya mtu mzima kabla ya wakati, na ndani mwake vinaanza kujitokeza undumakuwili na kiburi. Akisifu maadili, si yale ya Kimungu, bali nguvu inayodhihirisha anavyoanza kukomaa, pamoja na busara fulani ambayo haitofautishi vizuri na ile ya bandia na inaweza ikawa ujanja tu wa kuficha kasoro.

Baadaye, magumu ya maisha yatamkumbusha udhaifu wake; pengine atagongana na utovu wa haki ambao utamuonyesha thamani ya adili hilo; atasikitikia masingizio na hivyo atavumbua thamani ya unyofu. Hatimaye, akiendelea kusali ataelewa maneno ya Bwana: "Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote" (Yoh 15:5), na maana ya dhati ya *Baba Yetu* itadhihirika kwake kwa namna mpya. Atarudia sala hiyo ya utoto wake akitumia pengine dakika kumi kuisali mara moja kutoka kilindi cha moyo wake: hapo atakuwa ameona tena njia yake.

## MAADILI MAKUU YA MTOTO WA MUNGU

Maadili hayo ni yale yanayokuza sifa za kimaumbile za mtoto lakini si kasoro zake, tuwe tulivyo kadiri ya neema ipitayo maumbile, si kadiri ya kasoro zetu.

Kwanza mtoto wa Mungu anatakiwa kuwa sahili na mnyofu, kukwepa unafiki na uongo asijaribu kuonekana tofauti na alivyo. "Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru" (Math 6:22). Maana yake, ikiwa mtazamo wa roho ni mnyofu, na nia ni nyofu, maisha yote yatajaa mwanga.

Mtoto wa Mungu anatakiwa kujitambua daima dhaifu na mhitaji, akikumbuka mfululizo kwamba Baba yetu ametuumba kwa hiari toka utovu wa vyote, na kwamba pasipo neema hatuwezi kufanya lolote kuelekea utakatifu na wokovu. Akikua katika unyenyekevu huo atazidi kusadiki Neno la Mungu kwa dhati, kuliko watoto wanavyosadiki maneno ya wazazi wao. Atakuwa na imani isiyoogopa watu na atakayojivunia kuwa nayo; mara nyingine imani hiyo itapenya mafumbo pasipo mifuatano ya mawazo; ataishi kulingana nayo na kuyaonja, akiyatazama kwa mshangao kama mtoto anavyomtazama machoni baba yake mpendwa. Akifuata njia hiyo, mtoto wa Mungu ataona tumaini lake likiimarika siku kwa siku na kugeuka kujiachilia katika mikono ya Baba ambayo ni kama lifti inayotuinua hadi kwake. Hatimaye, mtoto wa Mungu atampenda kila siku zaidi, kwa ajili yake mwenyewe, si kwa ajili ya fadhili zake, kama vile mtoto mwema anavyompenda mama yake kuliko mabembelezo anayompatia. Mtoto wa Mungu anampenda Baba katika majaribu kama katika furaha, naye wakati mgumu anakumbuka wajibu wa kumpenda kwa nguvu zote hata kwa roho yote na kuunganika naye mfululizo ili *kumuabudu katika Roho na ukweli.*

Jambo hilo la mwisho linathibitisha kuwa mara nyingi katika majaribu njia ya utoto inadai ushujaa, adili la nguvu pamoja na kipaji cha nguvu. Tunaliona hilo hasa mwishoni mwa maisha ya Mt. Teresa wa Mtoto Yesu, alipopitia *usiku wa roho* kwa imani ya ajabu akiwaombea wasiosadiki, kwa kujiachilia kikamilifu kwa upendo safi na wa nguvu uliomfikisha hadi muungano wa kutugeuza. Njia ya utoto ikieleweka hivyo inalinganisha maadili yanayoonekana kupingana: upole na nguvu, unyofu na busara. Katika ulimwengu uliopotoka tunahitaji *busara*, lakini pia *nguvu* hata kufia dini kama mahali pengi katika karne XX: ili tuwe nazo ni lazima tuwe na vipaji vya shauri na nguvu, ambavyo ili tuwe navyo tuzidi kuwa wanyofu na watoto mbele ya Mungu na ya Mama Maria. *Kadiri tunavyoacha kuwa watoto kwa watu, tunapaswa kuwa watoto kwa Mungu.* Kutoka kwake tu tunaweza kupata nguvu na busara tunazozihitaji katika mapambano ya nyakati hizi. Njia ya utoto ikieleweka vizuri inalinganisha pia *unyenyekevu halisi na hamu ya kuzama kwa upendo katika mafumbo ya wokovu,* ambako si karama ya pekee kama njozi na fadhili nyingine za nje ambazo hazikupatikana katika maisha ya mtakatifu huyo.

## KINACHOTOFAUTISHA UTOTO WA KIROHO NA ULE WA KIMAUMBILE

"Ndugu zangu, msiwe watoto katika akili zenu; lakini katika uovu mgeuzwe watoto wachanga, bali katika akili zenu mkawe watu wazima" (1Kor 14:20). Basi, tofauti ya kwanza kati ya aina hizo mbili za utoto ni ukomavu katika kupima mambo. Lakini ipo nyingine: kwamba upande wa maumbile, kadiri mtoto anavyokua anatakiwa kujitegemea, kwa sababu siku moja wazazi watamuacha peke yake. Kumbe upande wa neema, kadiri mtoto wa Mungu anavyokua anaelewa kuwa hataweza kamwe kujitegemea bali kumtegemea Mungu tu. Kadiri anavyokua anatakiwa kuishi kwa uvuvio maalumu wa Roho Mtakatifu, ambaye kwa vipaji vyake anafidia kasoro za maadili, hivi kwamba hatimaye mtu anatendewa na Mungu kuliko kutenda mwenyewe, na wakati uliopangwa ukifika ataingia tumboni mwa Baba ambamo ataona heri yake. Kijana akikua anawaacha wazazi ili kuanza maisha yake; kisha kufikia utu uzima hawategemei tena, bali anawategemeza. Kinyume chake mtoto wa Mungu akikua anazidi kumtegemea asitake tena kufanya chochote peke yake, pasipo miangaza na mashauri ya Baba yake. Hapo maisha yote yanakolezwa na sala: ndilo fungu bora ambalo hatanyang'anywa kamwe.

"Kubaki wadogo ni kujitambua si kitu, ni kutarajia yote toka kwa Mungu mwema, kama vile mtoto anavyotarajia yote toka kwa baba yake; ni kutohangaikia chochote, ni kutolenga faida. Hata kati ya mafukara, mpaka mtoto ni mdogo anapewa anavyovihitaji, lakini akishakua tu baba hataki tena kumlisha bure, hivyo anamuambia, 'Sasa fanya kazi, unaweza kujitegemea'. Basi, ili nisiambiwe maneno hayo, sikutaka kamwe kukua, nikijiona siwezi kujitegemea katika kupata uzima wa milele mbinguni. Hivyo nimebaki daima mdogo, asiye na kazi nyingine isipokuwa kuchuma maua ya upendo na ya sadaka nimtolee Mungu mwema ili kumpendeza. Tena kuwa mdogo ni kutoamini kuwa maadili ninayoyatekeleza ni ya kwangu, kana kwamba naweza kitu, bali ni kukiri kuwa Mungu mwema anaweka hazina hiyo ya maadili mikononi mwa mtoto wake ili aitumie atakavyohitaji, ikibaki daima mali ya Mungu mwema" (Mt. Teresa wa Mtoto Yesu). Ndivyo ulivyosema mtaguso wa Trento, "Wema wa Mungu kwetu ni mkubwa hivyo hata atake zawadi zake zitugeukie stahili zetu". Tunaweza kumtolea yale tu anayotupa; ila tunayoyapokea kama neema tunamtolea kama stahili, ibada, sala, fidia na shukrani. "Hatimaye kuwa wadogo ni kutokata tamaa kwa kasoro zetu, kwa sababu watoto wanaanguka mara nyingi, lakini ni wadogo hivi hata wasiweze kuumia sana" (Mt. Teresa wa Mtoto Yesu).

Katika mafundisho hayo, ya juu kuliko mifuatano yoyote ya mawazo ya kibinadamu, linang'aa hasa lile la

neema ambalo mababu na wanateolojia waliandika mengi juu yake, na ambalo humo limetekelezwa kwa usahili na udhati na mtu aliyekubali kuongozwa na Roho Mtakatifu hadi bandari ya wokovu. Wenye heri wanateolojia watakaoweza kuongoa watu wengi kama mtakatifu huyo alivyofanya! “Tuseme nini sisi wenye ndevu na udhaifu pamoja, tuliowaona wasichana kuingia ufalme wa mbinguni kwa upanga, wakati hasira inatushinda, kiburi kinatuvimbisha na uchu wa madaraka unatuvuruga?” (Mt. Gregori Mkuu). Hakika Mt. Teresa wa Mtoto Yesu *ametuelekeza njia nyofu inayofikisha juu sana.*

## 4.2. ***USHUJAA WA MAADILI***

Ili tuelewe vizuri hatua ya muungano tunahitaji kuzungumzia ushujaa wa maadili, hasa yale ya Kimungu ambayo ndiyo yanayotuunganisha na Mungu.

### 4.2.1. ***USHUJAA WA MAADILI KWA JUMLA***

Ushujaa wa maadili, unaodaiwa na Kanisa ili kutangaza watumishi wa Mungu kuwa wenye heri mbinguni, unaanza katika utakaso wa Kimungu wa hisi yanapopatikana matendo ya kishujaa ya usafi wa moyo na ya subira. Matendo ya kishujaa yanapatikana zaidi katika utakaso wa Kimungu wa roho unaoingiza katika hatua ya muungano, na hasa baada ya jaribu hilo. Tukimuona mtu ametoka handaki hilo la kwanza, na zaidi hilo la pili, akiwa na ushujaa wa maadili, ni dalili ya kuwa amevuka vizuri asiache njia; au, kama alitenda makosa, ameinuliwa tena na neema ya Mungu na kuletwa hadi unyenyekevu mkubwa zaidi, kwa kutojiamini na kumtegemea yeye tu.

**SIFA ZA ADILI LA KISHUJAA**

“Adili la kawaida linamkamilisha binadamu kiutu, kumbe adili la kishujaa linampatia ukamilifu upitao utu. Shujaa akiogopa penye sababu za kuogopa, ni adili; asingeogopa katika nafasi za namna hiyo angekuwa shupavu tu. Lakini asipoogopa tena kitu kwa sababu anategemea msaada wa Mungu, adili hilo linapita utu, ni la Kimungu” (Mt. Thoma wa Akwino). Juu kuliko *maadili ya raia mwema*, mtakatifu huyo alifafanua *maadili yanayotakasa:* “Ni yale ya watu wanaoelekea kufanana na Mungu. Hapo busara inadharau malimwengu yote ipende zaidi kuzama ndani ya Mungu na kuelekeza mawazo yote kwake; kiasi kinaachana na madai ya mwili kadiri umbile linavyoweza kuvumilia; nguvu inamzuia mtu asiogope kifo wala ahera; hatimaye haki inamsukuma ashike moja kwa moja njia hiyo ya Kimungu tu”. Juu ya hayo tena yapo *maadili ya roho iliyokwishatakata,* yaani yale ya watakatifu wakuu hapa duniani na ya wenye heri mbinguni: “Hapo busara ni kama inahisi mambo ya Kimungu; kiasi hakijui tena tamaa za kidunia; nguvu inasahaulisha hofu yoyote; haki inafunga na Mungu agano la milele”. Akizungumzia *Heri Nane* alisema kuwa ndiyo matendo ya juu zaidi ya maadili na ya vipaji, na kuwa tuzo lake hapa duniani ni *utangulizi fulani wa heri ya milele.*

Mafundisho kuhusu adili la kishujaa yalijumlishwa hivi na Benedikto XIV, “Masharti manne yanatakiwa kwa adili la kishujaa lililothibitishwa au lililodhihirika: 1) *jambo* linatakiwa kuwa *gumu*, la juu kuliko nguvu za kawaida za watu; 2) linatakiwa kutendwa *mara*, kama kwa urahisi; 3) tena kwa *furaha takatifu;* 4) *si kwa nadra*, bali kila inapopatikana nafasi”. Hivyo ushujaa wa maadili ni wa juu kuliko kawaida ya waadilifu. Unajitokeza mtu anapotimiza majukumu yote bila ya wasiwasi wala shuruti, hata katika nafasi ngumu zaidi.

Masharti hayo yaeleweke kuhusiana na mtu anayetekeleza adili la kishujaa: lililo *gumu* kwa mtoto wa miaka kumi ni lile lipitalo nguvu za kawaida za watoto wenye umri wake; vilevile lililo gumu kwa mzee ni tofauti na lililo gumu kwa mtu mwenye afya na nguvu. La pili, yaani *utayari* na urahisi, lieleweke upande wa juu wa roho, bila ya kukanusha ugumu upande wa chini, fumbo la Getsemane linavyothibitisha; ili sadaka ya kuteketezwa ikamilike ni lazima uwepo uchungu na ugumu mkubwa unaoshindwa mara na upendo wa kishujaa. Vilevile *furaha takatifu,* iliyo sharti la tatu, ni ile ya sadaka inayotupasa, nayo haizuii uchungu wala huzuni, bali pengine inaendana na hali ya kukaribia kulemewa ambayo inatolewa kitakatifu kwa Mungu; tena furaha ya kuteseka pamoja na Bwana inaongezeka pamoja na uchungu, ndiyo sababu ni dalili ya neema kubwa. Sharti la nne, yaani *mazoea* ya kutenda hivyo nafasi ikipatikana, linathibitisha zile zilizotangulia na linaonyesha adili la kishujaa lililokwishajaribiwa kweli.

Ushujaa wa maadili unadhihirika hasa katika kifodini, lakini hata nje ya hapo, k.mf. katika kusamehe na kupenda kwa namna ya ajabu wadhalimu. Ndivyo ilivyomtokea kwa namna ya pekee Yesu, hata kabla ya mateso yake, alivyoonyesha hasa kwa upendo wake usio na mipaka kwa ajili ya wote, upendo wa mchungaji aliyejiandaa kutoa uhai wake kwa ajili yetu.

Katika adili la kishujaa *wastani adili* ni wa juu kuliko katika adili la kawaida: sasa adili linatekelezwa pamoja na kipaji kinachohusiana nalo, na kwa kuwa linatumikia upendo tunakuta ndani yake mruko wa adili hilo la Kimungu. Halafu, kwa kuwa matendo ya kipaji yanategemea uvuvio wa Roho Mtakatifu, *Mkristo shujaa* anadumu mnyenyekevu kama *mtoto* wa Mungu anayemtazama daima Baba, tofauti na shujaa anayezingatia nguvu zake mwenyewe na kulenga makuu yatakayomtukuza, kuliko kumuacha Bwana atawale kwa dhati ndani mwake.

**USHUJAA NA ULINGANIFU WA MAADILI**

Ili tutofautishe uadilifu wa kishujaa, unaotokana na msaada mkubwa wa Mungu, na mambo yanayoonekana tu kufanana nao, tunapaswa kuzingatia masharti hayo manne lakini pia ulinganifu wa maadili. Busara, *dreva wa maadili,* inaongoza maadili ya kiutu, wakati upendo unaelekeza matendo ya maadili yote kwa Mungu na kuyafanya yastahili. Ndiyo sababu maadili yote, yakiunganika katika busara na upendo, yanakua pamoja kama vidole vitano vya mkono uleule mmoja, au kama viungo mbalimbali vya mwili mmoja. Fundisho hilo ni la msingi ili kubainisha maadili ya kishujaa, kwa sababu kutekeleza kwa pamoja maadili yanayoonekana kupingana kuna ugumu wa pekee, kwa kuwa silika ya kila mmojawetu inaelekea adili moja au lingine. Maadili ya kujipatia na ya kumiminiwa yanatakiwa kukamilisha maelekeo mema ya umbile letu na kupinga kasoro zinazoliharibu. Tunapaswa kupiga kinanda bila ya kutokeza noti zisizolingana na nyingine, tusichanganye upole na woga, wala moyo mkuu na kiburi.

Basi, tunaona umuhimu wa ulinganifu wa maadili, na ugumu wa kuyatekeleza yote karibu kwa wakati mmoja ili kudumisha ulinganifu wa maisha maadilifu. Litokanalo ni kwamba adili lolote halina kiwango cha ushujaa ikiwa mengine hayapo katika kiwango hichohicho walau *katika utayari wa roho* kuyatekelezwa nafasi ikidai hivyo. Si busara kutamka haraka kuwa mtumishi wa Mungu ana ushujaa wa adili fulani halafu kufasiri kwamba kwa sababu hiyo anayo mengine pia kwa kiwango hicho; ili tuweze kusema adili mojawapo ni la kishujaa, ni lazima tuwe tumeshapima ukuu wa mengine. Ingawa maadili, hasa ya Kimungu, yanakua pamoja, fulani anaweza kuelekea kiumbile au kimazoea adili moja au lingine; tena kuna watumishi wa Mungu ambao, kwa ajili ya utume maalumu, wanapokea neema za msaada zinazowafanya watekeleze adili moja kuliko mengine.

Mungu tu, anayeunganisha ndani mwake sifa zote kamili, anaweza kuwajalia watumishi wake waunganishe vilevile maadili yote katika mwenendo wao. Ulinganifu wa ajabu wa maadili ulionekana hasa ndani ya Bwana wakati wa mateso, ambapo tunaona upendo wa kishujaa kwa Mungu na huruma isiyopimika kwa watesi pamoja na upendo mkuu kwa ukweli na haki; unyenyekevu wa dhati na moyo mkuu wa ajabu; nguvu ya kishujaa katika kujishusha na upole mkuu. Hivyo ubinadamu wa Mwokozi ni kioo safi ambamo sifa za Mungu zinarudisha mwanga wake.

Ulinganifu wa maadili ndio unaotofautisha *mashahidi wa kweli* na watu waliovumilia mateso kwa kiburi na ushupavu katika kushikilia udanganyifu. Mashahidi wa kweli tu wanaunganisha nguvu na upole unaowafanya wawaombee watesi wao kama alivyofanya Mwokozi. Hasa ndani mwao tunakuta masharti manne ya uadilifu wa kishujaa tuliyoyafafanua. Humo tunaona kazi maalumu ya Mungu anayetegemeza watumishi wake asiache kuwajalia neema za pekee katika nafasi ngumu zaidi.

Tusisitize kuwa *ushujaa wa watoto* unapimwa kulingana na nguvu za kawaida za watoto waadilifu wa umri uleule. Ikiwa watu wazima kadhaa uadilifu wao ni mdogo, wapo watoto ambao uadilifu wao ni mkubwa. "Vinywani mwa watoto wachanga na wanyonyao umeiweka misingi ya nguvu; kwa sababu yao wanaoshindana nawe" (Zab 8:2). Yesu aliwakumbusha maneno hayo makuhani na waandishi waliochukizwa na watoto kushangilia, "Hosana, Mwana wa Daudi!" (Math 21:15). Ikiwa pengine imani ya watoto ni kielelezo kwa watu wazima, ni vilevile kuhusu tumaini lao na upendo wao. Tukisoma matendo ya kishujaa ya watoto wenye umri wa miaka kumi na miwili au chini ya hapo, na maneno mazuri ajabu ambayo baadhi yao waliyatamka kabla hawajafa, tunakuta hekima ambayo katika usahili na unyenyekevu wake ni ya juu kuliko elimu changamano ya kibinadamu. Ni kipaji cha hekima katika kiwango cha juu, kulingana na upendo wa hao watoto ambao ni wakubwa kwa ushuhuda wa kishujaa waliomtolea Mungu. Katika usafi wa mtoto aliyebatizwa Roho Mtakatifu hahitaji kutakasa mengi kabla hajamshirikisha mianga yake na nguvu zake. Bila ya shaka mna madonda ya dhambi ya asili ambayo baada ya ubatizo ni kama makovu yanayoelekea kupona; lakini hayana sumu inayotokana na makosa yaliyorudiwarudiwa kwa hiari. Mtoto akiwa mwaminifu kwa neema katika kutimiza wajibu wa umri wake, Roho Mtakatifu anamsamehe matakaso yale machungu ambayo kwa waliotenda dhambi ni ya lazima kadiri walivyopotea. Hapo mtoto anainuka hata juu.

## 4.2.2. *IMANI YA KISHUJAA INAYOZAMA KATIKA MAFUMBO*

Baada ya kuzungumzia ushujaa wa maadili kwa jumla, tuzingatie ule wa adili muhimu mojamoja ili kuelewa maisha kamili ya Kikristo yanavyofundishwa na Kanisa. Kwanza: sababu gani katika kesi za kutangaza watakatifu wapya halitafuti uthibitisho wa kuwa walimiminiwa sala? Inatosha kuona walikuwa na imani ya kishujaa, ambayo mara nyingi kati ya dalili zake yanajitokeza matunda ya sala hiyo inayowafanya waishi kwa kuongea na Mungu karibu mfululizo. Imani ya kishujaa si ile ambayo inahuishwa na upendo na kupatikana ndani ya waadilifu wote, bali ni ile ya juu ambayo sifa zake bora ni *uimara* wa kushika mafumbo yaliyojaa giza, *utayari* wa kukataa udanganyifu, na *upenyaji* unaofanya itazame yote kwa mwanga wa ufunuo wa Mungu na kuishi kwa dhati kadiri ya hayo mafumbo yaliyofumbuliwa. Uimara unatokana na imani yenyewe, kumbe utayari na upenyaji yanatokana hasa na kipaji cha akili kinachokamilisha imani. Kwa njia hiyo imani inashinda ulimwengu, tunavyoona kwa namna ya pekee nyakati za dhuluma.

**UIMARA WA KUSHIKA MAFUMBO**

Tulipozungumzia utakaso wa Kimungu wa roho tuliona uimara wa imani unavyotakiwa kuwa ili ushinde vishawishi vikali vya wakati huo. Hapo upande wa chini wa akili unayumba, lakini imani inabaki imara kileleni, tena inathibitika zaidi na zaidi na katika giza inajiinua hadi ukuu wa Mungu. Uimara huo unazidi kujidhihirisha kwa kupenda Neno la Mungu lililoandikwa, kwa kuheshimu Mapokeo yaliyotunzwa na mababu wa Kanisa, kwa kushika kikamilifu mafundisho hata madogo yanayotolewa nalo na kwa kutii maelekezo ya mchungaji mkuu anayemwakilisha Yesu Kristo. Uimara huo ni wazi hasa ndani ya wafiadini, lakini pia ndani ya wale ambao katika mabishano makuu, badala ya kuyumba, wanakana umimi wao ili kudumu moja kwa moja katika njia nyofu.

Uimara wa imani kamili unaonekana pia katika utendaji, watumishi wa Mungu wanapokabili matukio machungu na yasiyotarajiwa wasishangae njia za ajabu ambazo maongozi ya Mungu yanazifuata. "Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu, na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; naam, yeye aliyeambiwa: Katika Isaka uzao wako utaitwa, akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano" (Eb 11:17-19). Utiifu huo wa kishujaa ulitokana na imani ya kishujaa. Giza la baadhi ya njia za Mungu linatokana na mwanga mkali mno kwa macho yetu dhaifu; hivyo saa ya mateso ya Yesu ilikuwa ya giza kuliko zote ikitazamwa toka chini, kumbe ya mwanga kuliko zote ikitazamwa toka juu. "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema Bwana" (Isa 55:8). Uimara wa imani unawafanya watumishi halisi wa Mungu watambue kuwa, kadiri ya maongozi yake, lengo la majaribu ya kushangaza zaidi ni utakaso wao, wokovu wao na wa wengine wengi.

**UTAYARI WA KUKATAA UDANGANYIFU**

Imani ya kishujaa inayozama katika mafumbo, pamoja na kuwa imara, iko tayari kukataa udanganyifu, kwa maana haikatai tu mara mitazamo mipotovu ya ulimwengu inayojipamba kwa maneno ya propaganda, bali pia inatambua mara makosa yanayoonekana madogo kumbe yanaweza yakawa chanzo cha upotovu mkubwa. Tofauti ndogo katika kilele cha pembetatu inakuwa kubwa katika mistari inayotokana nacho. Utayari wa kukataa kila chanzo cha upotovu unajitokeza katika utendaji kwa namna ya kuungama dhambi, yaani si kwa mazoea tu bali kwa kuziona wazi na kwa unyofu unaoondoa kila kisingizio, kana kwamba mtu anasoma tayari kitabu cha uzima kitakachofunguliwa siku ya kifo chake.

Utayari huo wa imani kukataa udanganyifu unawatia watumishi wa Mungu huzuni nyingi wakiona watu wakipotea. Matokeo yake ni ari kubwa kwa uenezaji wa imani, ari iliyo motomoto lakini haina uchungu wala ukali, ari inayojitokeza hasa kwa ile sala yenye bidii na karibu ya kudumu inayotakiwa kuwa roho ya utume.

**UPENYAJI UNAOONYESHA YOTE KWA MWANGA WA UFUNUO**

Imani hiyo kamili inafanya mtu aone yote kwa mwanga wa Neno la Mungu na kama kwa macho yake, akizidi kuelewa yale yote yaliyofunuliwa kuhusu ukuu wa Mungu, ukamilifu wa sifa zake, Nafsi za Utatu mtakatifu, umwilisho uletao ukombozi, uhai wa Kanisa na uzima wa milele. Kwa mwanga huohuo upitao maumbile anazidi kuona ndani mwake sifa njema na kasoro vilevile, pamoja na thamani ya neema alizojaliwa. Anatazama kwa amani hata wenzake, udhaifu wao na ukarimu wao, na kupima matukio yanayofurahisha na yanayosikitisha kuhusiana na lengo la milele: upimaji huo unainuka juu ya vitu vinavyoonekana na ya mtazamo wa akili tu ili ufikie kwa namna fulani mpango wa Mungu upitao maumbile.

Kuhusu watu waliokamilika hivyo, Bwana alimuambia Mt. Katerina wa Siena, *"Hao wanaelewa kuwa mimi ndimi ukweli mtamu tena mkuu unaomgawia kila mmoja wakati, muda na mahali, faraja na tabu* kadiri anavyohitaji kwa wokovu na ukamilifu niliomuitia. Mtu angekuwa mnyenyekevu kweli angeona kwamba kila kitu kinachotoka kwangu nakitoa kwa upendo, na kwamba kwa sababu hiyo anatakiwa kupokea kwa upendo na heshima yale yote ninayomtumia… *Kwa mwanga huo mtu anapenda, kwa kuwa upendo unafuata ujuzi,* na kadiri mtu anavyojua anapenda, tena kadiri anavyopenda anajua. Upendo na ujuzi vinalishana". Mtakatifu huyo alisema wandani wa Bwana wanateseka wakiona dhambi, ambazo zinamchukiza Mungu na kuharibu watu, lakini wakati huohuo wanafurahi, kwa sababu hakuna anayeweza kuwanyang'anya upendo ulio heri yao.

Imani hiyo kamili inaelekeza kutenda si kwa sababu za kibinadamu bali daima kwa zile zipitazo maumbile. Inayatia maisha usahili wa juu unaorudisha mwanga wa usahili wa Mungu na pengine unaonekana hata katika nyuso zinazong'aa Kimungu.

**USHINDI WA IMANI YA KISHUJAA JUU YA ULIMWENGU**

"Kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu: hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?" (1Yoh 5:4-5). Ushindi huo wa imani ya kishujaa ulipatikana tayari katika Agano la Kale: "Walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga, walizungukazunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya – watu

ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao" (Eb 11:37-38).

"Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi" (Eb 12:4). Pasipo kufikia ushahidi wa damu, ushindi huo unapatikana na imani ya watakatifu wote. "Wapandao kwa machozi watavuna kwa kelele za furaha" (Zab 126:5). Ndivyo watu wanavyolinganishwa na Kristo: kwanza na maisha yake ya utotoni, halafu na maisha yake yaliyofichika, kwa kiasi fulani na maisha yake ya kitume, hatimaye na maisha yake ya uchungu kabla hawajashiriki uzima wake mtukufu mbinguni.

### 4.2.3. *TUMAINI LA KISHUJAA NA KUJIACHILIA KWA MUNGU*

Kabla Mkristo hajafikia ukamilifu, tumaini lake halina msimamo kwa maana mambo yakimuendea vema anajiamini kipumbavu, halafu juhudi zake zikishindikana anavunjika moyo. Tumaini la kishujaa, likiwa juu ya mabadiliko hayo, sifa zake ni *uimara usioshindikana* na *kujiachilia kwa Mungu* pamoja na kutimiza mfululizo wajibu wowote kwa uaminifu. Tumaini hilo linajidhihirisha pia katika matokeo yake kwa *kuinua moyo wa watu waliopo kandokando* na kwa kuchochea njaa na kiu ya haki ya Mungu.

**UIMARA USIOSHINDIKANA WA TUMAINI KAMILI**

"Wote tunapaswa kuwa na tumaini imara kabisa katika msaada wa Mungu; kwa sababu, tusipopinga neema yake, mwenyewe aliyeanzisha kazi ya wokovu ndani mwetu ataikamilisha, akitimiza ndani mwetu kutaka na kutenda" (Mtaguso wa Trento). Tulivyoona, uimara huo usioshindikana unajidhihirisha katika kutakaswa roho ambapo Bwana anaacha mtu akose msaada wowote wa viumbe kusudi amtumainie yeye tu. Hapo anapaswa kutarajia kishujaa *yasiyotarajiwa kibinadamu*. Jaribu hilo likivumiliwa vema, tumaini linazidi kuimarika na kuongezeka mara kadhaa. Halitutii hakika ya moja kwa moja kuhusu wokovu wetu binafsi (jambo linalohitaji ufunuo wa pekee), ila linafanya tuzidi kutumaini hivyo kwa *hakika ya kuelekea huko*. Kama vile kwa maongozi ya Mungu silika ya mnyama *inavyoelekea kwa hakika* lengo lake, sisi tukiongozwa na imani katika ahadi zake *tunauelekea kwa hakika* uzima wa milele.

Uimara huo unatakiwa kuwa haushindikani kutokana na sababu yake, yaani *Mungu aliye tayari daima kusaidia* alivyoahidi. Bila ya kujali tunaposhindwa, tunapopingwa, tunapoona umaskini wetu na makosa yetu, tunapaswa daima kumtumainia Mungu aliyewaahidia msaada wanaomuomba kwa unyenyekevu, tumaini na udumifu. Tuyaombe malimwengu kwa sharti, yaani kadiri yanavyoufaa wokovu wetu; kumbe neema za lazima kwa kudumisha urafiki na Mungu *tuziombe pasipo sharti*, kwa tumaini la moja kwa moja, ingawa kwa unyenyekevu. Tuombe hivyo si tu neema za lazima kwa utakatifu wetu, bali Roho Mtakatifu mwenyewe aliye paji kuu (taz. Lk 11:9-13). Yeye *anatumwa tena* kwetu tunapovuka toka kiwango fulani cha upendo hadi kingine cha juu zaidi, inavyotupasa ili tushinde majaribu yanayokusudiwa kuleta maendeleo hayo. Tumaini lililotakaswa hivyo halishindikani, kadiri ya maneno yaliyotegemeza wafiadini: "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" (Rom 8:31). Mara kadhaa Bwana aliwaambia watakatifu wake, "Utakosa msaada hapo tu mimi nitakapokosa uweza".

"Hata kama ningekuwa mkosefu mkuu kuliko wote duniani, tumaini langu kwa Mungu lisingepungua, kwa kuwa halitegemei usafi wangu, bali huruma na uweza wa Mwenyezi Mungu" (Mt. Teresa wa Mtoto Yesu). Ndiyo sababu ya kutumaini ambayo Mt. Paulo alielewa ukuu wake alipoandika, "Napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu" (2Kor 12:10); yaani naacha kujitumainia ili nimtumainie Mungu: "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Fil 4:13). Siku moja Mt. Filipo Neri alikuwa anatembea katika ua wa nyumba yake ya kitawa akilia kwa sauti kuu, "*Nimekata tamaa, nimekata tamaa"*. Wanae wa Kiroho wakamuambia kwa mshangao, "Baba, inawezekanaje, wakati wewe ulichochea mara nyingi tumaini letu?" Naye akaruka kama kawaida yake akajibu kwa furaha, "Ndiyo, upande wangu nimekata tamaa, lakini kwa neema ya Bwana wetu nina tumaini bado". Kwa njia hiyo alifaulu kushinda kishawishi kikubwa cha kukata tamaa.

**KUJIACHILIA KWA TUMAINI NA UAMINIFU WA KUDUMU**

Tumaini la kishujaa linajitokeza pia katika kujiachilia mikononi mwa maongozi ya Mungu na wema wake wenye uwezo wote. Kujiachilia kikamilifu kunaendana na uaminifu wa kudumu kwa wajibu hata mdogo wa kila nukta, kadiri ya maneno ya Bwana, *"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia"* (Lk 16:10). Ikibidi, atasaidiwa na Mungu hata kuvumilia kifodini. Yote yakionekana kuwa yameshindikana, tuungane na Mtungazaburi akisema, *"Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu…* Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji" (Zab 23:1,4). Katika nafasi ngumu zaidi aliyejaribiwa anakumbuka maneno ya Ayubu (1:21): "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa, jina la Bwana na libarikiwe!" Hapo anapaswa kukariri, "Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako" (Mith 3:5-6) *"Nimekukimbilia wewe, Bwana, nisiaibike milele"* (Zab 31:1). Mt. Teresa wa Yesu, mambo yalipoonekana kushindikana, alikuwa akisema, "Bwana, wewe unajua yote, unaweza yote na kunipenda!" Kujiachilia mikononi mwa upendo huo, na kupokea mapema toka kwake yale yote yatakayotokea, kunatuliza na kuleta ushindi dhidi ya vishawishi

vya kulalamika, "Bwana, mbona huji kunisaidia?" Tukumbuke kwamba hakuna kinachotokea kinyume cha maongozi ya Mungu, kwamba mwenyewe anatukeshea, na kwamba katika msalaba anaotutumia imefichika neema ya thamani. "Lo! Tumaini la kimbingu, linalopata kadiri linavyotarajia!" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Tumaini hilo la kishujaa linazidi kutegemea pia stahili zisizopimika za Mwokozi na thamani ya damu aliyotumwagia. Litokee lolote lile, tunapaswa kumtegemea mchungaji mwema aliyetoa uhai wake kwa ajili ya kondoo zake, na kumtegemea Mungu Baba "asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye" (Rom 8:32) sisi tunaomkimbilia? Bwana alimuambia Mt. Katerina wa Siena, "Tumaini hilo halisi na takatifu ni kamili kadiri ya kiwango cha upendo ambacho mtu anacho kwangu, na kadiri hiyohiyo *anaonja maongozi yangu"*. Mwonjo huo wa Kiroho ni wa juu kuliko faraja za kihisi, kwa kuwa aliyekamilika haamini tu maongozi hayo, bali anayatambua hata pasipotarajiwa. Anayaonja kwa kipaji cha hekima kinachotufanya tuone ndani ya Mungu mambo yote, hata matukio ya kusikitisha na yasiyotarajiwa, kikitufanya tuhisi mapema mema ya juu ambayo kwa ajili yake anaruhusu hayo ya kwanza yatukie. Bwana alimuambia tena, "Wanaonitumikia bila ya kulenga faida yao, bali wakitamani tu kunipendeza, wanaonja maongozi yangu kuliko wale ambao, kwa huduma wanayonitolea, wanatarajia kulipwa furaha wanayoiona ndani mwangu… Nawashughulikia wote, wakamilifu na wasio wakamilifu: hakuna atakayenikosa, mradi asithubutu kujitumainia". Kadiri tusivyojitafutia faida tunaonja maongozi ya Mungu, tena kadiri tunavyoyaona katika maisha yetu tunajiachilia kwake na kwa ushenga wa Kristo. Pamoja na tumaini letu kwake linakua tumaini kwa Maria ambaye chini ya msalaba alitimiza tendo la tumaini kamili kuliko yote akastahili kuitwa msaada wa Wakristo, Mama wa Msaada wa daima: kumkimbilia mara nyingi ni dalili ya uteule.

**TUMAINI LA KISHUJAA LINACHOCHEA TUMAINI LA WENGINE**

Jambo hilo linaonekana hasa katika maisha ya waanzilishi wa mashirika ya kitawa. Hao wakati ambapo hawakuwa na fedha wala misaada ya kibinadamu, miito ilichelewa kujitokeza, na walikutana na wasiwasi na upinzani tu, walimtumainia Mungu na kuinua tumaini la wanao wa kwanza waliobaki waaminifu. M.H. Raimundi wa Kapua anasimulia kuhusu Mt. Katerina kwamba, "mimi au ndugu mwingine tulipokuwa tukiogopa hatari fulani, alikuwa akisema, 'Ya nini kujihangaikia? Myaachie maongozi ya Mungu yashughulike; mnapoogopa zaidi, anawakazia macho asiache kamwe kushughulikia wokovu wenu'". Katika nafasi chungu zaidi, Bwana alimuambia, "Mwanangu, unifikirie mimi: ukinifikiria, mimi nitakufikiria daima wewe". Tumaini hilo lilimwezesha kuinua moyo wa watu kandokando yake katika utume mgumu aliokabidhiwa wa kumrudisha Papa toka Avignone hadi Roma.

Alipojitoa kwa urekebisho wa Kanisa, Bwana alimuambia, "Nyinyi mnapaswa kunitolea sadaka ya nafsi yenu na kikombe cha tabu nyingi ninazowatumia kwa namna yoyote, msichague mnavyoona muda wake wala jinsi yake wala kipimo chake, bali mvipokee ninavyowapatia. Kikombe hicho kinatakiwa kujaa, nacho kitajaa mkipokea tabu hizo zote kwa upendo, mkivumilia kasoro zote za jirani kwa subira halisi pamoja na kuchukia na kupinga dhambi… Mteseke kiume hivyo hadi kufa: kwenu itakuwa ishara ya kuwa mnanipenda. Msigeuke nyuma wala kuipa plau kisogo kwa kuogopa dhiki. Kuwa katika dhiki ndio wakati wa kufurahia… Mtakapokuwa mmeteseka nitayatia faraja majaribu yenu makali mliyoyavumilia kwa urekebisho wa Kanisa".

Bwana anategemeza tumaini la watakatifu wake kama alipomuambia Mt. Yoana wa Ark kifungoni, "*Usikatae kifodini, hatimaye utaujia ufalme wa mbinguni*". Wakizidi kutumainia msaada wake wanakariri, "Mwenyezi Mungu ana nguvu kuliko yote". Sadaka yao inawalinganisha na Mwokozi: pamoja naye wanashinda dhambi na shetani. Katika mapambano wanamuomba hamu ya *kushiriki kujishusha kwake* ambamo wakute nguvu, amani na pengine hata furaha ya kuinua moyo wa watu wanaowazunguka. Kadiri upendo unavyozidi moyoni, hofu ya mateso inapungua, kumbe hofu ya dhambi inakua pasipo kupunguza tumaini: kadiri tulivyoungana na Mungu kwa njia ya upendo na tunavyoogopa dhambi inayoweza kututenga naye, tunazidi kumtumainia yule ambaye anatupenda na kutuvuta kwake.

## 4.2.4. *UPENDO WA KISHUJAA*

Ili tuelewe upendo wa kishujaa ni nini, tunapaswa kuzingatia ulivyo kwanza kwa Mungu, halafu kwa jirani.

**UPENDO WA KISHUJAA KWA MUNGU: KULINGANA KIKAMILIFU NA MATAKWA YAKE NA KUUPENDA MSALABA**

Upendo wa kishujaa kwa Mungu unadhihirishwa kwanza na *hamu motomoto ya kumpendeza,* kwa kuwa kumpenda fulani kwa ajili yake ni kumtakia mema, kutaka yale ambayo yanamfaa na kumpendeza. Kumpenda Mungu kishujaa ni kutaka, hata katika matatizo makubwa, kwamba matakwa yake matakatifu yatimizwe na utawala wake uwaenee wote. Hamu hiyo ni upendo unaothibitishwa na matendo, kwa kulingana na matakwa ya Mungu katika kutekeleza maadili yote. Hivyo mtu anafikia uaminifu wa kudumu katika mambo madogo kama katika yale makubwa na magumu zaidi.

Upendo huo wa kishujaa unadhihirika katika utakaso wa Kimungu wa roho, tunapopaswa kumpenda kwa ajili yake pasipo faraja yoyote, katika ukavu mkubwa wa muda mrefu na vishawishi vya ukinaifu, uzembe na

ulalamishi. Bwana akionekana kutuondolea zawadi zake na kutuacha tufadhaike si kwamba amepungukiwa wema wake usio na mipaka, asistahili tena kupendwa kwa usafi. Ikiwa hapo, bila ya kujali ukavu huo, mtu anapenda kukaa peke yake na Mungu, hasa mbele ya sakramenti kuu, na maisha yake yanazidi kuwa sala ya kudumu, basi hiyo ni dalili ya upendo wa kishujaa.

*Ulinganifu wa kishujaa na matakwa ya Mungu* unadhihirika mtu anapopokea kwa upendo yale ambayo hayampendezi na yanamtia tabu, akizidi kuona ukweli wa neno hili: "Mema na mabaya, uzima na mauti, umaskini na utajiri, hayo yote yatoka kwa Bwana" (YbS 11:14). Hapo ana hakika ya dhati ya kuwa Mungu anatumia hata uovu wa binadamu ili kuwastahilisha wale wanaotaka kuishi kwa ajili yake tu. Ndivyo Ayubu alivyopokea misiba na Daudi alivyovumilia matusi ya Shimei. Katika matatizo makubwa watakatifu, pamoja na kufanya wanavyoweza, wanasema, "Yote yatatokea anavyotaka Mungu wetu mwema". Dalili hiyo inathibitishwa na kwamba, aliyejinyima hivyo matakwa yake, anaonja furaha takatifu: kwa kuyalinganisha zaidi na zaidi na yale ya Mungu anayo yale yote anayoyataka.

Mt. Bernardo alifafanua hatua za upendo wa kishujaa akisema, "Upendo wa Mungu unasababisha tumtafute bila ya kukoma; tufanye kazi mfululizo kwa ajili yake; tuvumilie majaribu yote pamoja na Kristo, bila ya kuchoka; tumuonee kiu halisi Mungu; tumkimbilie haraka; tutende kwa uhodari mtakatifu na ushujaa usioogopa; tuambatane na Mungu moja kwa moja; tuwake moto mtamu na kama kuteketea kwa ajili yake; hatimaye tuungane naye kabisa mbinguni".

Dalili kuu ya upendo wa kishujaa kwa Mungu ni *kuupenda msalaba,* ambako ndiko subira na ulinganifu na matakwa ya Mungu tulivyozungumzia vinakofikisha. Bwana alimuambia Mt. Katerina wa Siena, "Ndiyo dalili iliyoonekana ndani ya mitume walipompokea Roho Mtakatifu. Walitoka ghorofani, wakiwa wameondolewa hofu yoyote, wakatangaza neno langu na kuhubiri mafundisho ya Mwanangu pekee. Badala ya kuogopa mateso, wakawa wanayaona ni utukufu kwao… Wenye hamu ya heshima yangu, na njaa ya wokovu wa watu, *wanakimbilia meza ya msalaba mtakatifu…* Hakuna kinachoweza kulegeza mwendo wao: wala matusi, wala dhuluma, wala anasa ambazo ulimwengu unawatolea… Moyo uliogeuzwa kabisa na upendo unafurahia na kuonja lishe hiyo ya wokovu wa watu, ukiwa tayari kuvumilia yote kwa ajili yao… Ndicho kinachothibitisha bila ya shaka kwamba mtu anampenda Mungu wake kikamilifu na pasipo kujitafutia faida… Hao nawajalia neema ya kusikia kwamba sitenganiki nao kamwe". Yaani utekelezaji bora wa upendo unaendana kwa kiasi kilekile na tendo la kipaji cha hekima linalowawezesha kama kung'amua uwemo wa Mungu ndani mwao. Ndiyo maisha halisi ya kuzamia mafumbo, yanayowezekana tu kwa kuupenda msalaba, ambako tena kunawezekana tu kwa kulikazia macho fumbo la Yesu kufa kwa kutupenda. Ndiyo sababu Bwana alimuambia tena, "Mara wewe na watumishi wangu wengine mtakapojua ukweli wangu hivyo, mtakuwa tayari kuvumilia hadi kufa tabu zote, dharau, matusi ya maneno na matendo kwa utukufu na heshima ya jina langu. Ndivyo utakavyopokea na kuvumilia tabu, yaani kwa subira, shukrani na upendo".

Ndizo dalili za upendo wa kishujaa kwa Mungu: kulingana kikamilifu na matakwa yake katika majaribu, na kuupenda msalaba. Kuna dalili nyingine bado: upendo kamili kwa jirani.

### UPENDO WA KISHUJAA KWA MAJIRANI: HAMU MOTOMOTO YA WOKOVU WAO; WEMA UNAOWAENEA WOTE

Upendo unatuelekeza kumpenda jirani ndani ya Mungu na kwa ajili ya Mungu, yaani kwa sababu Mungu anampenda na kama Mungu anavyompenda. Unatufanya tutamani jirani awe wa Mungu tu na kumtukuza milele. Upendo wa kishujaa kwa jirani upo tayari tunapotawala mara vishawishi vikali vya kijicho, ugomvi na ubaguzi, na vile vya kujiamini vinavyotuelekeza kukataa msaada wa wengine baada ya kukwaruzana nao.

Upendo huo kamili unadhihirika ikiwa, kati ya matatizo makubwa, tunampenda jirani *kwa mawazo, maneno na matendo,* yaani kwa kumpima kwa wema, kusema vema juu yake, kumsaidia katika shida, kumsamehe kwa moyo na kujifanya yote kwa wote. Unadhihirika zaidi tukiwaelekea hasa walioanguka na kupotea, ili kuwainua na kuwaelekeza tena njia ya mbinguni. Sifa kuu mojawapo ya upendo wa kishujaa kwa majirani ni *hamu motomoto ya wokovu wao,* kulingana na neno la Yesu msalabani, "Naona kiu" (Yoh 19:28). Huo upendo wa kishujaa uliwafanya watakatifu kadhaa wajiuze kama watumwa ili kukomboa waliotekwa na hivyo kuondoa familia zao katika ufukara. Ari hiyo ilidhihirika ndani ya Mt. Paulo hata akasema, "Ningeweza kuomba mimi mwenyewe niharimishwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu kwa jinsi ya mwili; ambao ni Waisraeli" (Rom 9:3-4). Ari hiyo ndiyo iliyochochea utendaji wa wamisionari bora.

Dalili nyingine ya upendo wa kishujaa kwa jirani ni *wema wa kuwaenea wote* kati ya matatizo makubwa, kadiri ya neno, "Heri wapatanishi" (Math 5:9), yaani wale ambao hawadumishi amani yao tu wakati wa vurugu, bali wanawashirikisha wengine na kuwatia moyo waliovurugika zaidi. Wema unaoenea, upendo kwa jirani unaofikia hatua ya kujitoa sadaka kila siku bila ya kutambulikana, ndiyo dalili ya hakika ya uwemo wa Mungu rohoni. Pengine wema huo unaelekeza kukosoa, lakini pasipo uchungu, wala ukali, wala utovu wa subira; na kusudi ukosoe vema unatokeza ndani ya yule anayestahili kukosolewa mema aliyonayo, yaliyo kama mbegu nzuri inayotakiwa kustawishwa. Hapo anayekosolewa anatiwa moyo akijiona anaeleweka na kupendwa. Bikira Maria angetutokea kutukosoa, angetuambia juu ya kasoro zetu kwa wema mkubwa hivi hata tungekubali mara maneno yake na kuchota humo nguvu ya kusonga mbele.

Upendo huo kamili kwa jirani unatokana na muungano wa dhati na Mungu na kumfikisha jirani kwenye muungano huohuo. Kadiri mtu alivyoungana na Mungu, anamvutia wengine badala ya kujivutia tu. Ndani mwake unaelea wema wa Kimungu ambao unaenea, unavuta kwa nguvu na upole na hatimaye unashinda kizuio chochote. Upendo huo unaoshinda hivyo uovu, unawashirikisha watakatifu ushindi wa Kristo juu ya dhambi na shetani. Ni utukufu mmojawapo wa mwili wake wa fumbo; kwa njia yake unadhihirika ukuu wa uhai wa Kanisa, uzazi wake katika kila aina ya wema; ndiyo thibitisho la asili yake ya Kimungu.

### 4.2.5. *USHUJAA WA MAADILI YA KIUTU*

Kwa kuwa hatuwezi kueleza ushujaa wa kila adili la kiutu, tutaongea kwanza juu ya ushujaa wa unyenyekevu na upole; maadili hayo yanaleta sura ya Kikristo na kufungua njia ya kusema juu ya ushujaa wa maadili ya nguvu, busara, haki na yale yanayohusu mashauri ya Kiinjili.

**UNYENYEKEVU NA UPOLE WA KISHUJAA**

Unyenyekevu ni wa kishujaa unapofikia ngazi za juu zilizofafanuliwa na Mt. Anselmi, yaani si tu kutambua tunastahili dharau pande fulanifulani, bali kutaka watu wasadiki hivyo, kuvumilia waseme hivyo, kupokea dharau zao na hatimaye kupenda tutendwe hivyo, ili tulingane na Bwana aliyechagua kupatwa na aibu kuu za mateso kwa wokovu wetu.

Unyenyekevu huo unadhihirishwa na utaratibu mkubwa wa kudumu: “Kila mtu atatambulikana kwa uso wake; mwenye ufahamu atajulikana kwa sura yake popote umkutapo, nazo nguo za mtu, na finyo la kutoa meno, na mwendo wake, huonyesha mara alivyo yeye mwenyewe” (YbS 19:29-30). Uso mtulivu, mnyenyekevu, usiocheka mno, pamoja na mwendo mzito, mnyofu, usio na unafiki, vinashuhudia kuwa mtu anajisikia daima mbele ya Mungu na kuongea naye kwa ndani. Hivyo aliye mnyenyekevu na mtaratibu kweli anasema juu ya Mungu hata kwa mwenendo wake na kwa kimya chake.

Unyenyekevu wa kishujaa unaendana na kiasi hichohicho cha upole. Kwa njia ya adili hilo mtu anafikia kujitawala kikamilifu, hata kushinda ubaya kwa wema badala ya kuupinga kwa hasira. Ngazi za juu za upole ni kutofadhaishwa na matusi, kufurahia kitakatifu matokeo bora yanayotokana nayo, na hatimaye kumhurumia mtukanaji kwa matokeo mabaya yanayoweza kumpata. Ndivyo Yesu alivyolia juu ya Yerusalemu kwa kuwa ulikosa shukrani; alisikitikia maangamizi ya mji huo kuliko kifo kikatili kitakachompata.

**NGUVU YA KISHUJAA NA MOYO MKUU**

Ndani ya mtu aliyekamilika unyenyekevu na upole vinaendana na maadili ya nguvu na moyo mkuu ambayo yanaonekana kuwa kinyume chake, kumbe yanakamilishana navyo.

Nguvu ni adili la kiutu linalotuimarisha katika kulenga mema magumu tusiogope mapingamizi makubwa. Inatawala hofu yetu mbele ya hatari, kazi za kuchosha, lawama na yale yote yanayoweza kupooza juhudi za kuelekea mema; halafu inatuzuia tusisalimu amri tunapopaswa kupambana. Nguvu inaratibu pia ushupavu na uchangamfu usiofaa ambavyo vinaelekeza kutenda bila ya kujali lolote. Matendo yake makuu ni mawili: kukabili hatari na kustahimili magumu. Tunapaswa kuyavumilia kwa upendo wa Mungu, na kwa hakika ni vigumu kustahimili muda mrefu kuliko kujitosa wakati wa kuchangamka.

Nguvu inaendana na *subira* katika kuvumilia huzuni za maishani bila ya kuhangaika wala kulalamika, halafu inaendana na *ustahimilivu* unaovumilia muda mrefu, na *udumifu* katika kutenda mema ambao ni kinyume cha ukaidi katika kutenda mabaya. Adili la nguvu linahusiana pia na *moyo mkuu* unaosukuma kutenda makuu katika maadili yote, ukikwepa ulegevu pasipo kuangukia makosa ya kujiamini, kujivuna au kutaka kuringa.

Kipaji cha nguvu kinaliongezea ukamilifu wa juu zaidi na kutuandaa tupokee uvuvio wa Roho Mtakatifu ukija kututegemeza mbele ya hatari, na kuondoa hangaiko la kujisikia hatuwezi kutimiza wajibu mkubwa wala kuvumilia majaribu yanayotukabili. Kipaji hicho kinadumisha “njaa na kiu ya haki” katika hali yoyote. Ushujaa wa adili la nguvu unadhihirishwa hasa na kifodini kinachovumiliwa ili kutetea ukweli wa imani au adili fulani. Nje ya kifodini, adili la nguvu na kipaji cha nguvu, pamoja na subira na moyo mkuu vinatumika kila palipo na haja ya kutenda kishujaa au kuvumilia makubwa. Nguvu hiyo ya Kikristo inatofautiana na uvumilivu wa mwenye kiburi, kwa sababu inaendana na unyenyekevu, upole na unyofu mkubwa. Huo wa mwisho ni wa kishujaa unapopenda ukweli hata kukwepa kila undumakuwili, uongo, ulaghai, utata, ingawa unajua kutunza siri usiseme yale yote yaliyomo moyoni.

**BUSARA YA KISHUJAA**

Hiyo inazungumziwa kidogo, lakini katika nafasi ngumu busara pia inakuwa ya kishujaa. Adili hilo linahusu utekelezaji wa ukweli, yaani ukweli katika matendo. Ndiyo sababu Bwana alisema, “Iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua” (Math 10:16). Si rahisi kulinganisha kila mara maadili hayo, lakini yote mawili ni ya lazima kwa Mkristo anayetakiwa si tu kuwa *mwadilifu kamili*, bali kutenda daima kama *mwana wa Mungu,* akimtegemea kikamilifu na kuzidi kujua anavyomtegemea. Busara ya Kikristo katika

ngazi ya juu inajua wazi mema yanayompasa mtoto wa Mungu, na inaelekeza kwa imara maadili mengine yayatende kitakatifu. Wanaolenga ukamilifu wanatakiwa kulenga maadili yote kwa ngazi ya juu, jambo linalodai kiwango hichohicho cha busara walau kuhusu utakatifu wao wenyewe. Adili hilo ni la lazima zaidi kwa wale wanaopaswa kushauri na kuongoza wengine.

Tunapoiamini mno busara yetu, Mungu akitaka kututakasa anatuacha tuangukie makosa ya wazi, au tusahau au kutozingatia mambo, na matokeo yake yanatuaibisha. Baada ya takaso hilo busara inaweza ikawa ya kishujaa na kuongozana na kiwango cha juu cha kipaji cha shauri ambacho tunapokea uvuvio wa Kimungu wa kuhisi la kufanya katika nafasi ngumu.

Inatokea vile Bwana anapomfanya mtumishi wake atende namna ambazo wengi wanaona hazina busara, k.mf. Mt. Fransisko wa Asizi katika kupenda ufukara. Ndivyo walivyofanya wale wote ambao kwa uvuvio wa Mungu walikabili kazi ngumu zaidi, kama kuokoa makahaba au majambazi hata kuwafanya watawa; hapo walijikuta katika nafasi ambapo kutenda na kutotenda kulionekana vilevile kukosa busara, hata iliwapasa kumuomba Bwana uvuvio wa kipaji cha shauri, pamoja na kutulia mikononi mwake. Busara kamili haitenganiki na sala ya kudumu kwa kupata mwanga wa Mungu; vilevile inaelekeza kusikiliza mashauri mazuri ya wanaoweza kutuangazia na inadhihirisha ukomavu wa roho.

Kuhusu mambo ya pekee yapitayo maumbile, busara halisi inachukua tahadhari: haiyakanushi kimsingi, bali inayapima na kuyatolea tamko pale tu inapolazimika na baada ya kumuomba Mungu mwanga. Busara hiyo ya hali ya juu inadhihirika pia katika kupima miito ya pekee. Ushujaa wa adili hilo unadhihirika hasa katika matendo ambayo binadamu anayaona hayana busara, kumbe matokeo yake yanakuja kuonyesha yalivyokuwa na busara ya juu. Ndivyo Mwokozi alivyowatuma mitume wake kumi na wawili waongoe ulimwengu bila ya chombo chochote cha kibinadamu.

**HAKI YA KISHUJAA**

Ili tupate picha ya haki kamili tukumbuke adili hilo halikatazi tu wizi na utapeli, bali pia uongo wowote, unafiki, ulaghai, kuvunja siri, kuwakosea watu heshima kwa masingizio, masengenyo na vitendo, kuwahukumu bila ya msingi na kuwacheka kwa dharau. Mara nyingi haki yetu ina dosari tunapoitekeleza walau kiasi kwa faida yetu, k.mf. tukilipa madeni ili kukwepa pia gharama ya kesi, au tukisema ukweli kwa kuzingatia usumbufu unaoweza ukatokana na uongo. Hapo inahitaji kutakaswa kama maadili mengine yote. Haki kamili inahitajiwa na wale wanaolenga muungano wa dhati na Mungu, kwa kuwa wanatakiwa wasiwe na kosa lolote dhidi ya wenzao bali watimize wajibu wowote wa haki na upendo kwao. "Uishindanie kweli hata kufa, naye Bwana atakupigania wewe. Usiwe mwepesi wa kunena, mlegevu wa kutenda, msahaulifu. Usiwe kama simba nyumbani mwako, mwenye kutuhumu watumishi wako. Mkono wako usinyoshwe kupokea, ukarudishwa wakati wa kulipa" (YbS 4:28-31).

Mtu aliyefikia hatua ya muungano anatakiwa kutimiza kishujaa aina zote za haki, zikiwa ni pamoja na usawa. Ashike kikamilifu sheria zote za Mungu na za kibinadamu, za Kanisa na za nchi. Akipaswa kugawa mema au mizigo, afanye hivyo kadiri ya stahili za kila mmoja, asijali undugu wala urafiki. Aepe dhara lolote kwa yeyote.

Haki ya kishujaa inadhihirika hasa pale ambapo ni vigumu kuipatanisha na mapendo ya dhati: kwa mfano jaji anapotakiwa kumhukumu mwanae mwenye makosa; au mkubwa anapotakiwa kumtuma mwanae mpenzi wa Kiroho mahali pa mbali na pa hatari.

**USHUJAA WA MAADILI YA KITAWA**

*Adili la ibada* linadhihirika kuwa la kishujaa mtu anapotimiza wajibu alionao upande huo bila ya kujali upinzani mkali wa ndugu wa ukoo na wengineo. Linadhihirika vilevile katika utekelezaji wa nadhiri ya kutenda yaliyo bora, na katika uanzilishi wa familia ya kitawa kati ya matatizo makubwa ambayo kwa kawaida yanaendana nao.

*Ufukara* wa kishujaa unajinyima vyote, ukiridhika na riziki za lazima tu, ili kufanana na Bwana ambaye hakuwa na mahali pa kupumzikia. Asiyetamani chochote hakosi kitu, ni tajiri Kiroho na mwenye heri. *Usafi wa moyo* wa kishujaa unadhihirika hasa katika ubikira wa kudumu, mtu anapoishi mwilini maisha ya Kiroho tu hata akasahau vurugu zote za hisi kwa kuzoea kuzishinda. Hatimaye *utiifu* wa kishujaa unadhihirika katika kujikatalia kikamilifu matakwa ya binafsi, mtu asipofanya chochote bila ya ruhusa ya wakubwa, akiwatii wote bila ya kujali walivyo, hata wasipomuonyesha wema. Pengine anadaiwa kutii maagizo magumu, kama vile Abrahamu alivyodaiwa sadaka ya mwanae pekee. Hapo anahitaji imani kubwa ambayo imuonyeshe Mungu ndani ya wakili wake. Ni nafasi ya giza ambayo ikivukwa vizuri inaleta mwanga mkubwa, kwa kuwa Bwana anamlipa kwa ukarimu yule anayetii hivyo.

Basi, ni wazi jinsi ushujaa wa maadili ya kiutu unavyoyafanya yatumikie upendo na kuandaa muungano wa dhati na Mungu.

### 4.2.6. ***UPENDO KWA MSULUBIWA NA KWA MARIA KATIKA HATUA YA MUUNGANO***

Mt. Teresa wa Yesu aliandika hivi juu ya watu waliofikia makao ya sita, "Mnaweza mkadhani kwamba hao

wanaofurahia matamu hayo ya hali ya juu hawapaswi tena kutafakari mafumbo ya ubinadamu mtakatifu sana wa Bwana wetu Yesu Kristo, na kwamba kazi yao ni kupenda tu… Tutawezaje kusogea kwa hiari mbali na yule aliye hazina na dawa yetu pekee?… Yesu alisema kuwa *ndiye njia*. Alisema pia kuwa *ndiye mwanga* na kwamba *hakuna mtu aendaye kwa Baba ila kwa njia yake*. Na kweli wale ambao Bwana amewaingiza katika makao ya saba karibu hawatenganiki kamwe na Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa namna ya ajabu, yupo nao kiaminifu kwa ubinadamu wake na umungu wake kwa pamoja... Maisha ni marefu na tunakabiliana na tabu nyingi. Ili tuzivumilie inavyofaa tunahitaji kuzingatia jinsi kielelezo chetu Yesu Kristo, mitume na watakatifu walivyozivumilia. Urafiki wa Yesu mwema ni bora: basi tusijitenge naye wala na Mama yake mtakatifu… Narudia tena, wanangu, muangalie: njia hiyo ni ya hatari. Shetani anaweza akatufikisha hadi kupotewa na ibada kwa sakramenti kuu".

**USHINDI WA KRISTO NA UENEZI WAKE**

"Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida… Ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo" (Fil 1:21,23). Kama vile vita ndiyo maisha ya askari, na elimu ndiyo maisha ya msomi, Kristo amekuwa daima maisha ya watakatifu wote, lengo la kudumu la upendo wao na chemchemi ya nguvu zao. "Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali *sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa*; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu… Maana naliazimu nisijue neno lolote kwenu, ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa" (1Kor 1:22-24; 2:2). "Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake, aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu… Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (Ef 1:18-20; 3:17-19). Watakatifu wote waliishi hadi mwisho kwa kuzamia mateso ya Yesu msulubiwa, hasa wale waliolingana naye zaidi.

Katika hatua ya muungano zinazidi kudhihirika hazina zisizopimika za roho ya Mwokozi, za akili yake, za utashi wake na za hisi zake. Unazidi kugundulika *utakatifu wake wa asili, wa dhati, usioumbwa*, unaoundwa na Nafsi yenyewe ya Neno inayomiliki kwa ndani na moja kwa moja roho yake na mwili wake. Inazidi kueleweka thamani ya *ukamilifu wa neema, wa mwanga na wa upendo* ulioenea rohoni mwake kutokana na Neno; ukamilifu ambao ulikuwa chemchemi ya amani kuu na heri timilifu tangu duniani hapa, na kwa wakati huohuo ulisababisha ukali wa mateso ya Kristo kuhani na sadaka, kwa sababu mateso yake kwa dhambi za watu alizozibeba yalikuwa na ukuu uleule wa upendo wake kwa Baba aliyechukizwa nazo na kwetu sisi aliokuja kutukomboa.

Katika hatua ya muungano mtu anazidi kuelewa *ushindi mkuu* alioupata Kristo katika mateso yake hadi msalabani; ushindi juu ya dhambi na shetani uliodhihirika siku ya tatu kwa ushindi juu ya kifo. Ushindi huo unazidi kueleweka unavyotokana na *tendo la upendo wa Mungu-mtu* ambalo katika Nafsi ya Kimungu ya Neno lilichota *thamani yake isiyo na mipaka* kwa kutoa fidia na kutustahilia uzima wa milele. Tendo hilo "lilimpendeza Mungu kuliko yalivyomchukiza maovu yote pamoja" (Mt. Thoma wa Akwino) kwa kuwa lilitokana na Nafsi ya Mwana aliye sawa na Baba na kustahili kuliko jumla ya stahili zote za malaika na za binadamu. "Jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu" (Yoh 16:33); katika nafasi ngumu na za dhuluma ni faraja iliyoje kwetu kufikiri kwamba Msulubiwa ameshapata ushindi wa moja kwa moja na kwamba upande wetu tunapaswa tu kujitoa kwake ili atushirikishe. Duniani mapambano yanaendelea, lakini ushindi umeshapatwa na Kichwa cha mwili wa fumbo ambao sisi ni viungo vyake. Hapo ibada kwa mateso ya Mwokozi inazidi kuwa ibada kwa Kristo mtukufu.

Katika hatua ya muungano yanazidi kueleweka aliyoyasema Mt. Thoma, "Mungu anapenda zaidi yaliyo bora, kwa kuwa upendo wake ndio chemchemi ya mema yote, hivyo kiumbe kisingekuwa bora kuliko kingine kama kisingependwa zaidi na Mungu. Kwa hiyo Mungu anampenda Kristo si tu kuliko binadamu wote, bali kuliko viumbe vyote pia, kwa kuwa alimtakia mema makuu zaidi na kumkirimia jina lile lipitalo kila jina akimjalia kuwa Mungu kweli. Ubora wa Mwokozi haupunguzwi na ukweli kwamba Mungu alimtoa afe kwa wokovu wetu. Kinyume chake Yesu amekuwa hivyo mshindi mtukufu".

Kwa namna hiyo inaeleweka zaidi sababu gani Mungu aliacha itukie dhambi ya asili na matokeo yake. "Mungu haachi mabaya yatokee isipokuwa kwa ajili ya mema makubwa zaidi. Ndiyo maana mtume Paulo aliandika, *Dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi* (Rom 5:20). Nalo Kanisa linapobariki mshumaa wa Pasaka linaimba, *Lo! Kosa lenye heri, lililostahili kumpata Mwokozi mkuu kama huyo!"* (Mt. Thoma wa Akwino). Kifo cha Yesu msalabani ndio ufunuo mtukufu zaidi wa huruma na uweza wa Mungu. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee" (Yoh 3:16). Hayo yote yanazidi kuwa wazi kwa mtu aliyemiminiwa sala na yanamfanya aone pia kila siku zaidi thamani isiyopimika ya sadaka ya misa ambayo inadumisha ile ya msalabani na kutushirikisha matunda yake.

**HESHIMA KWA MARIA KATIKA HATUA YA MUUNGANO**

Ili kupenya zaidi fumbo la Kristo mtu aliyemiminiwa sala anatakiwa kumuomba Maria, inavyothibitishwa na liturujia, k.mf. katika sekwensya ya Mama wa Mateso: "Mama kwa upendo wako / Nijulishe teso lako / Nililie na wewe. / Ewe, washa moyo wangu / Kwa kumpenda Yesu Mungu, / Ili nimwelekee. / Yesu Bwana kifo chake, / Teso lake nishike, / Wazie majeraha. / Nijeruhi kama Yeye, / Msalabani unilevye, / Kwa damu ya Mwanao". Ndiyo sala ya mtu anayetamani kujua donda la upendo na kushirikishwa mafumbo ya uchungu kwa kuabudu na kufidia, kama walivyofanya Mt. Yohane na Mt. Maria Magdalena karibu na Maria huko Kalivari, na pia Mt. Petro alipomwaga machozi mengi. Machozi hayo ya majuto na ibada tungependa kuyamwaga daima kwa sababu kadiri tunavyosikitikia chukizo tulilomtendea Mungu, tunafurahia sikitiko hilo: "Aliyetubu asikitike daima pamoja na kufurahia sikitiko lake" (Mt. Augustino). Ndivyo inavyosema sekwensya hiyo pia, "Mimi nawe nimlilie, / Msulibiwa huzunie, / Maisha yangu yote. / Natamani kusimama / Msalabani nawe Mama, / Niomboleze nawe".

Tusiache chemchemi hizo zibubujike bure: kutoka madonda ya Kimungu yanatiririka yale maji hai tunayopaswa kuyanywa kwa wingi. Mt. Katerina wa Siena, aliyejaliwa mara kadhaa kunywea donda la moyo wa Yesu, hakuchoka kusisitiza thamani ya damu yake. Bwana atuinue hadi Moyo wake mtakatifu tunaposhiriki sadaka ya misa na kukaribia meza yake. Kuzama hivyo katika stahili zisizo na mipaka za Mwokozi ni sehemu ya njia ya kawaida ya utakatifu; bila ya kufanya hivyo hatuwezi kupenda msalaba, ambako kimsingi ni kumpenda motomoto Yesu msulubiwa. Ndiyo njia ya kifalme ya kuendea mbinguni.

Mtu fulani aliyejaribiwa kuliko kawaida aliandika, "Nimetegemezwa mara nyingi na neno la Kimungu la Mwokozi, 'Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu' (Yoh 16:33). Ushindi wake wa moja kwa moja, ambao unaangaza malimwengu kwa nuru ya faraja kubwa, unanitia furaha isiyosemekana. Ninapojisikia kuangamia, nikiinua macho kwa Mwalimu mwema na kumnong'onezea kwa huzuni, 'Bwana, nahitaji furaha!', basi naona ushindi wake wa fahari mwishoni mwa nyakati, na mwanga huo kutoka juu unaangaza giza nene la usiku na kuleta utulivu kati ya dhiki zozote. Ni kana kwamba kutoka pwani ningeona kupita mikondo ya maji ya kutisha. Duniani mambo yanakwenda vibaya hivi! Misingi ya ulimwengu inatikisika, lakini yeye habadiliki, anabaki daima mwema tu!" Tukimfuata hivyo hatutatembea gizani kamwe, bali tutazidi kupokea mwanga wa uzima.

## 4.3. *NAMNA NA NGAZI ZA HATUA YA MUUNGANO*

Hatuwezi kupata picha halisi ya hatua ya muungano tusipoongea juu ya namna zake mbalimbali na juu ya ngazi zake. Kwa hiyo tutazungumzia kwanza maisha kamili ya kitume kama tunda la kuzama katika mafumbo, halafu maisha ya malipizi. Hayo yatatuandaa tuelewe zaidi mafundisho ya walimu wakuu wa Kiroho kuhusu muungano unaotugeuza. Tutaona jawabu la swali: je, upendo kamili kwa Mungu unawezekana pasipo kuungana naye kifumbo?

Walimu vijana wanafundisha kuliko wanavyojua, yaani hata mengi wasiyoyajua. Wenye umri wa makamo wanafundisha yale yote wanayoyajua. Kumbe wazee wanafundisha yale yanayowafaa wasikilizaji. Tunapokabili masuala kama hayo yanayotuzidi ni lazima tufuate mfano wa hao wa mwisho. Tungehitaji kwanza kung'amua muungano huo wa hali ya juu. Kumbe tutaweza tu kuripoti kifupi tunayoyaona muhimu zaidi katika ushahidi wa watakatifu. Sisi ni kama watazamaji ambao, tukiwa bado bondeni, tunaangalia wanaopanda hadi kilele cha mlima.

### 4.3.1. *MAISHA KAMILI YA KITUME NA SALA YA KUMIMINIWA*

Haifai tuzungumzie muungano wa dhati na Mungu bila ya kusema juu ya matunda yake katika maisha kamili ya kitume yanayounganisha sala ya kumiminiwa na utendaji. Ni lazima tudumishe uwiano na umoja wa pande hizo mbili kwa kulingana iwezekanavyo na maisha ya Bwana na ya mitume wake.

**CHEMCHEMI YA JUU YA UTUME**

Katika hotuba ya Mt. Petro siku ya Pentekoste, na katika barua za Mt. Paulo, tunakuta Neno la moto likiongozwa na uvuvio wa Mungu. Mababu wa Kanisa ili wawaokoe watu waliwalisha matunda ya sala waliyomiminiwa. Kuzama kwa upendo katika mafumbo ni bora kuliko vitendo vya toba na kuliko masomo: ndiyo roho ya utume. Mtume yeyote awe anashirikisha mang'amuzi yake ya sala ya kumiminiwa ili kuwatakasa na kuwaokoa watu, kadiri ya maneno ya Mt. Thoma wa Akwino: "Kuzama katika mafumbo na kuwashirikisha wengine yaliyotazamwa hivyo".

Ili maisha hayo yadumu kuwa na umoja, sala ya kumiminiwa na utendaji haviwezi kuwemo *katika msingi wa usawa;* ni lazima kimoja kiwe chini ya kingine, la sivyo vitadhuriana na hatimaye itabidi kuchagua kimojawapo tu. Wengi, wajue wasijue, wanapotosha fundisho la mapokeo, wakisema maisha ya kitume *lengo lake kuu* ni *utendaji wa kitume,* ila yanalenga pia sala kama *chombo cha lazima* kwa ajili ya utendaji. Lakini je, kweli mitume na wamisionari watakatifu, k.mf. Mt. Fransisko Saverio, waliona kuzama kwa upendo katika mafumbo ya imani ni *chombo tu kinacholenga utendaji?* Je, kweli Mt. Yohane Maria Vianney alitazama hivyo

sala na misa? Kudhani hivyo ni kupunguza umuhimu wa muungano na Mungu, ulio chemchemi ya utume wowote. Kwa mtazamo huo, ambao pengine hautokezwi wazi, ungefikiwa uzushi wa kupindua mpangilio wa upendo kwa kusema ule kwa jirani ni wa juu kuliko ule kwa Mungu.

Kuzama katika mafumbo yake na hivyo kuungana naye hakuwezi kuwa *njia ya kulenga utendaji*, kwa sababu ni *jambo la juu zaidi*. Duniani hakuna lolote la juu kuliko kuungana na Mungu kwa sala ya kumiminiwa na upendo: "Kwa umbile lake maisha ya sala hasa yanatangulia yale ya utendaji, kwa sababu yanalenga mambo makuu na bora, halafu yanasukuma na kuongoza katika maisha ya utendaji" (Mt. Thoma wa Akwino). Utume hauna thamani kubwa usipotokana na chemchemi hiyo kama *sababu ya juu.* Tena wenyewe ni njia inayolenga muungano na Mungu tunaotaka kuwafikishia watu. Kwa hiyo tunapaswa kulenga hasa *kuzama katika mafumbo ambako kunazaa utume*.

Yesu Kristo hakuridhika na maisha ya sala tu, bali alichagua yale ambayo yanatokana na utajiri wa sala ya kumiminiwa na yanashuka kuwashirikisha watu kwa njia ya mahubiri. Uhusiano wa kuzama katika mafumbo na kutenda unafanana na ule wa umwilisho na ukombozi. Umwilisho wa Neno hauhusiani na ukombozi wetu kama njia ya chini inavyolenga shabaha ya juu, bali kama *sababu ya juu* inayoleta tokeo la chini. Tangu milele Mungu alipanga umwilisho si kwa *kulenga ukombozi* bali kwamba *uzae ukombozi.* Vivyo hivyo alipanga maisha ya kitume yawe na sala ya kumiminiwa na muungano na Mungu si kwa kulenga utendaji, bali kwamba vizae matunda katika utume.

Ni lazima utume utokane na kuzama katika mafumbo ya wokovu ili mahubiri na uongozi wa roho viwe viangavu, hai, sahili, vyenye hakika ya dhati ambayo inachoma na kuvutia mioyo. "Anayewaletea wengine neno la Mungu anatakiwa kuwaelimisha, kuivuta mioyo yao kwa Mungu na kuchochea utashi wao watekeleze sheria yake" (Mt. Thoma wa Akwino). Inatakiwa iwe hivyo ili mahubiri yasishirikishe herufi tu, bali roho ya Neno la Mungu, ya mafumbo yapitayo maumbile, ya amri na ya mashauri. Si suala la miguso ya juujuu, bali la uvuvio wa ukweli wa Mungu unaotokana na imani kubwa na upendo motomoto kwa Mungu na kwa watu.

Ili tuelewe mahubiri ya Injili yanavyotakiwa kuwa, tukumbuke kwamba sheria mpya si Maandiko kwanza, bali *sheria iliyomiminwa* rohoni, yaani neema ya Roho Mtakatifu. Ili tuishi kwa neema hiyo ilibidi tuelimishwe kwa maneno ambayo yalitamkwa na kuandikwa kuhusu mafumbo ya kusadikiwa na amri za kutekelezwa. Mahubiri ya Injili yanatakiwa kuwa roho na uzima; ili mtume asikate tamaa katika mapingamizi yote anayopambana nayo ni lazima awe na njaa na kiu ya haki ya Mungu, awe na kipaji cha nguvu aweze kudumu mpaka mwisho na kuvuta watu. Hizo njaa na kiu zinakua katika liturujia na sala ya moyo. Hasa *adhimisho la misa,* pamoja na muungano na Mungu unaopatikana humo, ndio kilele ambapo ububujike mto wa mahubiri hai ya Neno la Mungu. Ili awe "Kristo mwingine", padri anatarajiwa kuzama katika sadaka ya msalaba inayodumu kutolewa altareni. Huko kuzama kuwe roho yenyewe ya utume inayofanana na chemchemi hai daima zinazotiririsha mito mikubwa. Kifupi ni kwamba, ili tuwalete wengine kwa Mungu ni lazima kwanza tuwe tumeungana naye kwa dhati.

**MASHARTI NA MATUNDA YA UTUME**

Matunda ya utume yanatakiwa kuwa uongofu wa wasio Wakristo na wa waamini wakosefu pamoja na maendeleo ya waadilifu: kwa jumla, ni wokovu wa roho. Lakini kwa ajili hiyo Bwana hakuridhika kuhubiri ukweli, bali alikufa msalabani. Vivyo hivyo mitume hawawezi kuokoa watu kwa mahubiri tu, bila ya kuteseka kwa ajili yao. "Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; sikuzote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu" (2Kor 4:8-10). Mwenyewe, alipowaahidia mara mia wale wanaomfuata aliwatabiria dhuluma za namna hiyo (taz. Mk 10:30).

"Kama vile Bwana wetu alivyotimiza ukombozi wa ulimwengu kwa msalaba wake tu… hata watenda kazi ya Injili wanagawa tu neema za ukombozi kwa msalaba wao na kwa dhuluma zinazowatesa. Kwa hiyo hakuna cha kutumainia kutokana na huduma yao isipoendana na mapingamizi, masingizio, matusi na mateso. Baadhi wanadhani kutenda maajabu kwa sababu mahubiri yao yametungwa vizuri, wanayatoa kwa ufasaha, wanasifiwa na kupokewa vema kila mahali. Lo! Wanavyodanganyika! Njia wanazozitegemea si zile ambazo Mungu anazitumia ili kutenda makuu. Ili kuokoa ulimwengu inahitajika misalaba. Mungu anaongoza katika njia ya msalaba wale anaowatumia kuokoa watu" (A. Lallemant). Wamisionari wengi waliuawa kikatili, na damu yao ikawa mbegu ya Wakristo wapya! Uhai wa Kanisa, kama ule wa mwanzilishi wake umepitia mautini na hivyo unadumu kuwa na nguvu na kuzaa matunda yasiyoisha.

Kwamba utume unatakiwa "utokane na utimilifu wa sala ya kumiminiwa" (Mt. Thoma wa Akwino) ni uthibitisho mwingine wa kwamba, kuzama katika mafumbo kwa imani hai iliyoangazwa na vipaji vya Roho Mtakatifu ni katika njia ya kawaida ya utakatifu, hasa kwa padri anayetakiwa kuongoza watu, kuwaangaza na kuwafikisha kwenye ukamilifu.

## 4.3.2. *MAISHA YA MALIPIZI*

Kuhusu muungano wa waliokamilika na Mungu tunapaswa bado kuzungumzia walau kidogo maisha ya malipizi, ambayo ni utume unaofanyika kwa sala na sadaka ili utume wa Neno uzae matunda mengi. Bwana

wetu aliokoa ulimwengu kwa upendo wake wa kishujaa msalabani kuliko kwa mahubiri yake. Maneno yake yametuangaza na kuelekeza njia, lakini kifo chake ndicho kilichotupatia neema ya kuifuata. Maria, anayeitwa kwa haki mkombozi mshiriki na mgawaji wa neema zote, ndiye kielelezo cha wanaoishi kwa kufidia dhambi za watu. Kwa uchungu wake chini ya msalaba ametustahilia kwa msingi wa urafiki wake na Mungu yale yote ambayo Neno aliyefanyika mwili ametustahilia kwa msingi wa haki. Hivyo akawa mama wa Kiroho wa binadamu wote.

Katika misa sadaka ya Yesu haifanyiki kwa mateso mapya kama pale msalabani, ila mateso yake yanatakiwa kuendelea katika mwili wake wa fumbo, na kweli yataendelea hadi mwisho wa dunia. Kwa kuwa Yesu akizidi kuwaunganisha naye waamini anaowahuisha, anachapa ndani mwao chochote cha mafumbo ya furaha, mwanga na uchungu ya maisha yake kabla hajawashirikisha utukufu wake mbinguni. Kwa lengo hilo anawashirikisha kazi yake ya kuokoa watu, waifanye pamoja naye, kwa ajili yake na ndani mwake wakifuata njia zilezile alizozifuata mwenyewe. Kwa maana hiyo Mt. Paulo aliandika, "*Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake"* (Kol 1:24). Kwa yenyewe mateso ya Kristo hayapungukiwi kitu, kwa kuwa thamani yake haina mipaka kutokana na Nafsi ya Kimungu ya Neno; kilichopungua ni kiasi cha uenezi wake ndani mwetu. Ndio utume mkuu wa mateso unaowashirikisha watakatifu uchungu wa Mwokozi na neema ya kuitia kazi yao mhuri alioitia kazi yake msalabani.

**MAISHA YA MALIPIZI YA PADRI**

Padri anatakiwa kuwa *"Kristo mwingine"* kwa namna ya pekee. Yesu ni kuhani na kafara, naye padri hawezi kushiriki ukuhani wa Kristo asishiriki hali yake ya kuwa kafara kadiri alivyopangiwa na Mungu. Ndivyo walivyoelewa mapadri watakatifu, k.mf. Mt. Yohane Maria Vianney ambaye wakati wa kutolea mwili na damu takatifu ya Bwana alikuwa anatolea mateso yake yote kwa ajili ya waamini waliomuendea. M.H. Charles wa Foucauld, aliyeutia mhuri wa damu utume wake kati ya Waislamu, aliandika maneno yafuatayo katika daftari alilolichukua daima ndani ya mavazi yake, "Ishi kana kwamba leo ni siku yako ya kufia dini. Kadiri tunavyokosa vyote duniani, tunakikuta kitu bora zaidi ambacho dunia inaweza kutupatia, yaani msalaba".

**MAISHA YA MALIPIZI YA WANAOPASWA KUBEBA MSALABA MZITO**

Mkristo yeyote anapaswa kubeba "msalaba wake kila siku" (Lk 9:23) na kuunganisha mateso yake na sadaka ya Yesu inayozidi kutolewa altareni: anapaswa kuyatoa kwa ajili yake na ya watu anaoshughulikia wokovu wao. Kwa mfano wa Maria, Mabibi arusi wengi wa Kristo wanashiriki mateso yake na hivyo kuwa mama wa Kiroho kwa wale wote waliokombolewa na damu ya Mwanae. Maria hakutiwa rohoni alama isiyofutika ya upadri lakini "alijaliwa ukamilifu wa *roho ya kipadri*" (M. Olivier) yaani roho ya Mkombozi. Alipenya fumbo la altareni kuliko Mt. Yohane aliyeadhimisha misa mbele yake na kumkomunisha. Alistawisha utume wa Thenashara akijitoa pamoja na sadaka ya misa. Kwa mateso yake ya ndani, kama yale yaliyompata uzushi ulipoanza kujitokeza, alikuwa mama wa Kiroho wa watu kwa kiwango kisichofikirika pasipo mang'amuzi ya dhati ya utume huo uliofichika. Kwa namna hiyo aliendeleza sadaka ya Mwanae.

"Mwili wa fumbo wa Kristo hauwezi kuishi pasipo mateso, kama vile macho yetu yasivyoweza kuishi bila ya mwanga wa jua. Hapa chini kadiri mtu alivyo karibu na Mungu, yaani kadiri anavyompenda, anawekwa wakfu kwa mateso. Kwa watu waliopewa yote na Kanisa, je, si wito bora kuishi na kujitoa sadaka kwa ajili ya Mama yao?… Inahitajika subira, lakini nitaipata: Bwana wetu atanipatia… Namuambia daima: 'Namtaka mtu huyu kwa gharama ya mateso yoyote'… Hadi mwisho wa dunia Kristo atateseka katika viungo vyake, na kwa mateso hayo Kanisa, Bibi arusi wake, litazaa watakatifu… Tangu Yesu afe, sheria haijabadilika: roho zinaokolewa tu kwa kuteseka na kufa kwa ajili yao… Moyo wa Yesu uliotukuzwa milele hautateseka tena kwa sababu hauwezi kuteseka tena. Sasa ni zamu yetu… Ni heri iliyoje kwamba kuteseka ni zamu yetu, si zamu yake tena!" (Fransiska wa Yesu).

Bwana anawaambia watu wa malipizi kama sista huyo aliyeishi miaka kadiri ya kweli hizo, "Je, hujaniomba kushiriki mateso yangu? Chagua: unataka furaha ya imani isiyo na vivuli, ambayo ikupate na kukujaza matamu, au unataka giza na uchungu ili kushiriki katika kuokoa watu?" Anawaalika wachague kwa hiari tu; lakini wao, wakivutwa na nguvu isiyoshindikana, wanajichagulia uchungu na giza lote ili wengine wapewe mwanga, utakatifu na wokovu. Pengine Bwana anawaonyesha ugumu wa mioyo, na ni kana kwamba mashetani wote wanajaribu kwa kila namna kuwakatisha tamaa; kwa saa kadhaa wanapambana nao roho kwa roho ili kumfuata kwa vyovyote Mwalimu mwema mpaka mwisho. Naye anawajalia kuelewa zaidi na zaidi anavyotarajia wapende kudharauliwa na kuangamia, kama chembe ya ngano iliyomwagwa ardhini ioze ikazae kwa wingi.

Ndiyo dalili ya upendo kamili ambao "unatolewa na Roho Mtakatifu akiushirikisha utashi nguvu yake mwenyewe" (Mt. Katerina wa Siena). Bwana alimuambia mtakatifu huyo kuwa wanaotamani wokovu wa watu "hawana lengo lingine isipokuwa kuteseka na kukabili uchovu wowote kwa manufaa ya jirani, wakichukua mwilini mwao madonda ya Kristo, kwa kuwa upendo msulubiwa unaowajaa unajitokeza katika kujidharau, kufurahi kudhalilishwa, kupokea mapingamizi na mateso mengine ninayowajalia toka pande zote

na kwa namna yoyote… Hivyo wanalingana na Mwanakondoo asiye na doa, Mwanangu pekee ambaye msalabani alikuwa na heri na uchungu kwa wakati mmoja… Nani anaweza kuninyang'anya na kusogeza mbali nami watu hao, waliozama katika moto wa upendo, kwa kutokuwa na matakwa yoyote ya kwao tena na kwa kuwaka kabisa kwa ajili yangu?"

Ndio ulinganifu kamili na Yesu Kristo unaozaa na kuangaza katika maisha ya malipizi. Hata kwa wasiopokea upadri ni kushiriki hali ya kafara ya Yesu na kuungana kwa dhati na kuhani wa milele: "Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo" (1Pet 2:4-5).

**KIELELEZO CHA MT. PAULO WA MSALABA KATIKA USIKU WA ROHO KWA AJILI YA MALIPIZI**

Maandishi ya Mt. Yohane wa Msalaba yanaweza yakaleta picha ya kwamba usiku wa roho ni hasa utakaso wa binafsi kwa ajili ya muungano kamili na Mungu. Utakaso huo wa Kimungu unaoendana na kuzama katika mafumbo ni *wa lazima* ili kuondoa kasoro za walioendelea. Mwishoni giza na fadhaa vinaacha nafasi kwa mwanga wa juu na furaha ya muungano unaotugeuza na kuandaa moja kwa moja uzima wa mbinguni. Inaonekana baadaye hakuna tena haja ya kuingia handaki la namna hiyo. Kumbe maisha ya watumishi kadhaa wa Mungu yanaonyesha uwezekano wa mwendelezo fulani wa usiku wa roho hata baada ya kuingia muungano unaotugeuza. Ikitokea hivyo ni kwamba jaribio hilo halilengi hasa *utakaso* bali *malipizi*.

Mt. Yohane wa Msalaba, ingawa hakusisitiza hilo, alidokeza mara kadhaa majaribu ya ndani yaliyowapata watakatifu kwa ajili ya wakosefu. Mt. Teresa wa Yesu pia alisema juu ya ukarimu mkubwa wa walioingia makao ya saba, "Mfalme mkuu hawezi kutujalia kitu bora kuliko maisha yanayolingana na yale ya Mwanae mpenzi. Nina hakika imara kwamba neema hizo lengo lake ni kuimarisha udhaifu wetu na kutuwezesha kuvumilia mateso makubwa kwa mfano wa huyo Mwana wa Mungu. Ama hatuoni kwamba wale wote waliomkaribia zaidi Bwana wetu Yesu Kristo ni wale waliopatwa na tabu nyingi zaidi? Tuzingatie zile za Mama yake mtukufu na za mitume watakatifu".

Tusisahau kwamba mateso makubwa ya rohoni yaliyowapata Bwana na Mama yake hayakuwa kwa utakaso wao, bali kwa ukombozi wetu, na kwamba, kadiri watu wanavyoendelea mateso yao ya ndani yanafanana na yale ya Yesu na Maria. Watumishi wa Mungu wanajaribiwa kwa namna ya pekee, ama kwa sababu wanahitaji utakaso wa dhati zaidi, ama kwa sababu wanatakiwa kufuata njia zilezile za Bwana katika kushughulikia lengo kubwa la Kiroho.

Tukisoma kijuujuu kuhusu mwisho wa maisha ya Mt. Alfonso Maria wa Liguori, tutadhani alikuwa akipitia usiku wa hisi, ambao mara nyingi unaendana na vishawishi vikali dhidi ya usafi wa moyo na ya subira. Kwa mzee huyo aliyekwishatimiza miaka 80 vilikuwa vikali hivi hata mtumishi wake akajiuliza kama atarukwa na akili. Lakini tukizingatia kazi yote iliyokwishatendwa na neema rohoni mwa mtakatifu mkubwa kama huyo, tutatambua majaribu hayo yalimpata hasa kwa ajili ya wengine, na ya shirika alilolianzisha kwa mateso mengi.

Mfano wa kushtua zaidi ni ule wa Mt. Paulo wa Msalaba, mwanzilishi wa Wapasionisti, aliyeishi miaka 81. Ilitokea nini katika maisha hayo marefu yaliyowekwa wakfu kwa Mungu tangu utotoni katika ugumu wa hali ya juu? Kwenye umri wa miaka 19 alipiga hatua kubwa, hata akaita kipindi hicho kuwa cha "uongofu wake"; kilikuwa na dalili za *utakaso wa Kimungu wa hisi*. Tangu hapo maisha yake ya kuzama katika mafumbo yalipitia vipindi vitatu. Cha kwanza kilichukua miaka 12, ambapo aliinuliwa ngazi kwa ngazi hadi muungano unaotugeuza. Cha pili kilichukua miaka 45, ambapo aling'amua kwa dhati ya pekee maisha ya malipizi. Cha tatu kilichukua miaka 5, ambapo nderemo ziliongezeka kadiri alivyokaribia mwisho wa maisha yake, ingawa majaribu nayo yaliendelea.

Katika kipindi cha kwanza, baada ya usiku wa hisi na tabu zake, akiwa amejaliwa kuzama katika mafumbo, alidumu saa tatu au nne mfululizo katika sala ya moyo, jumla saa saba kwa siku. Kwenye umri wa miaka 24 alijaliwa sala ya kutoka nje ya nafsi, alipopokea mianga mikubwa kuhusu mafumbo ya imani na njozi zilizomjulisha anavyotakiwa kuanzisha shirika la malipizi. Wakati huo alijaliwa pia njozi ya Utatu mtakatifu, ya mbinguni na ya motoni, akaona kana kwamba imani imekuwa jambo wazi. Alipata *utakaso wa Kimungu wa roho* kwenye umri wa miaka 26, hasa wakati wa mfungo wa siku 40 aliposikia maneno ya kishetani dhidi ya Mungu yaliyomchoma moyo na roho. Utakaso huo ulimalizika kwa kuzama katika mateso ya Mwokozi aliyojipatia kwa njia ya upendo. Mwenyewe aliandika, "Roho ikiwa imezama yote katika upendo safi, pasipo utafiti, ila kwa imani tupu na safi kabisa inajikuta, inapompendeza Mungu aliye wema mkuu, imezama sawasawa katika bahari ya mateso ya Mwokozi" na kuona "kwamba mateso ni kazi ya upendo tu". Tangu hapo sala yake ikawa kuvaa mateso ya Yesu na kujiachilia azamishwe katika umungu wake. Kabla ya kufikia umri wa miaka 31 alijaliwa *muungano unaotugeuza* ulioendana na ishara ambazo pengine zinaudhihirisha kwa hisi (njozi na kupewa pete ya dhahabu iliyochongwa ionyeshe vyombo vya mateso).

Tunapaswa kuzingatia alivyoufikia mapema hivi muungano wa dhati na Yesu msulubiwa, na alivyotakiwa kuishi bado miaka 50 na kuanzisha shirika la malipizi, tusije tukashangaa kumuona baadaye kwa miaka 45 katika tabu kubwa za rohoni na upweke mchungu, ambapo kwa nadra tu Bwana alimjalia kupumua kidogo.

Hakunyimwa tu faraja za kihisi, bali ni kana kwamba imani, tumaini na upendo vilipatwa visimng'ae. Alidhani ameachwa na Mungu kwa hasira. Vishawishi vya kukata tamaa na huzuni vilimlemea. Hata hivyo katika jaribu hilo la muda mrefu alionyesha subira kubwa, kujiachilia kikamilifu katika mapenzi ya Mungu pamoja na wema mkubwa kwa wale waliomkaribia. Siku moja alimuambia kiongozi wake wa Kiroho, "Kama wangeniuliza muda wowote ninafikiria nini, naona ningeweza kujibu roho yangu inajihusisha na Mungu". Ilikuwa hivyo hata alipojiona hana tena imani, tumaini na upendo: "Naona haiwezekani kuacha kumfikiria Mungu, kwa kuwa roho yangu imejawa naye, nasi sote tumo ndani mwake".

Alipokuwa akipitia barabara za Roma na kulia, "*Kutoka njia ya Paulo, utuopoe, Ee Bwana",* aliweza kupumua tu upande wa Mungu. Kwa miaka 45, usiku na mchana, sala yake chungu, ya kishujaa, isiyokoma, ilimtafuta kwa ari kwa niaba ya watu aliokuwa anateseka kwa ajili yao. Hivyo alitekeleza vizuri ajabu maneno ya Mwalimu "ya kwamba *imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa"* (Lk 18:1). Basi, tuelewe uzito wa neno la Mt. Yohane wa Msalaba: "Tendo moja tu la upendo safi linaweza kulifaidisha Kanisa kuliko matendo mengi ya nje" yanayotokana na upendo mdogo zaidi.

### 4.3.3. *ROHO MTAKATIFU ANAVYOMUATHIRI ALIYEKAMILIKA*

Ili tuelewe muungano na Mungu, ni lazima tukumbuke mafundisho ya hakika na ya juu zaidi kuhusu athari ya Roho Mtakatifu kwa aliyekamilika tukimzungumzia kwanza yeye kama paji kuu, halafu yatokanayo ndani ya mtu.

**ROHO MTAKATIFU, PAJI LISILOUMBWA**

Neema inayotia utakatifu, ambayo ni zawadi iliyoumbwa, inapita tayari vipawa vyovyote vya kibinadamu (k.mf. ubunifu, akili na utashi) hata kama ni vikubwa namna gani. Neema hiyo inapita pia umbile la malaika na karama za nje (k.mf. kutenda miujiza). Zaidi tena basi, Roho Mtakatifu kama *paji lisiloumbwa* linapita kiwango chochote cha upendo na cha utukufu.

Kwanza ni paji lisiloumbwa kama tunda la mwisho na la milele la uzima wa Mungu Baba na Mwana. Baba, aliye mwema pasipo mipaka, kwa kumzaa milele Neno anamshirikisha umungu wake wote, awe Mungu aliyetoka kwa Mungu, mwanga kwa mwanga. Baba, akiwa na Mwana, anatokwa na Upendo-nafsi aliye Roho Mtakatifu. Hivyo Nafsi ya tatu ya Mungu inatokana na upendano wa Baba na Mwana; ni paji lisiloumbwa ambalo hao wawili wanatoleana, paji pekee linalotokana na uvuvio wa milele ambao unamshirikisha Roho Mtakatifu umungu wote. Roho Mtakatifu anaitwa Paji-nafsi kwa sababu, ikiwa kila zawadi inatolewa bure kwa msingi wa upendo, kitu cha kwanza tunachokitoa zawadi ni upendo ambao tunamtakia fulani mema.

Hilo paji kuu, ambalo Nafsi mbili za kwanza zinatoleana milele, limetolewa kwetu pia katika historia. Kisha kutujalia ekaristi katika karamu ya mwisho na kutumwagia damu yake azizi msalabani; kisha kutujalia neema kwa njia ya sakramenti zote, Bwana alipenda kutuvuvia *Paji kuu* akamilishe fadhili zake zote. Mwokozi alitustahilia matokeo yote ya uteule wetu: wito wa kuishi Kikristo, uongofu na utakaso, kufa katika urafiki na Mungu na utukufu wa waliokombolewa kwa damu yake; zaidi ya hayo akapenda kutujalia paji lisiloumbwa, yaani Roho Mtakatifu. Ndiye anayefariji katika huzuni za maisha, katika mahangaiko yanayoweza yakafikia hali ya mafadhaiko. Ndivyo alivyowafariji mitume walipoondolewa uwepo wa Bwana kimwili na walipokabili ugumu mkubwa wa kuanza kazi yao. Walipompokea waliangazwa, waliimarishwa, walidumishwa katika neema na kugeuzwa; hivyo chini ya uongozi wake wakawa waaminifu hadi kufia dini. Pentekoste ikafanyika upya kwa kila mmojawetu siku ya kipaimara.

**KAZI YA PAJI LISILOUMBWA NDANI MWETU**

Tumepokea kweli paji kuu na tunaweza kulifurahia kwa njia ya upendo na ya kipaji cha hekima, ambavyo unatokea ujuzi unaofanana na mang'amuzi kuhusu uwemo ndani mwetu wa Nafsi za Kimungu zisizotenganika kamwe. Inafaa tusisitize matokeo makuu ambayo tunamsifu hasa Roho Mtakatifu, ingawa yanasababishwa na Baba na Mwana pia, kama tokeo lolote la uweza wa Kimungu ambao ni wa Nafsi tatu pamoja.

*Kwanza paji lisiloumbwa linathibitisha, linadumisha na kukuza ndani mwetu zawadi iliyoumbwa ya neema inayotia utakatifu,* "maji yaliyo hai… yakibubujikia uzima wa milele" (Yoh 4:10-14). Kinyume cha maji ya birika au mtaro, maji hai hayatenganiki na chemchemi na kwa msukumo wake yanatiririkia daima bahari. Vivyo hivyo neema inayotia utakatifu haitenganiki na chemchemi ya Roho Mtakatifu: ndiye anayeidumisha ndani mwetu na kuisukuma ielekee bahari ya uzima wa milele. "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" (Rom 5:5).

Kwa hiyo pengine anampatia mtu aliyekamilika *hakika fulani kuhusu hali yake ya kuwa na neema hiyo*: "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Rom 8:16). Anatoa ushahidi huo kwa njia ya upendo wa kitoto ambao anausababisha ndani mwetu na hivyo kutufanya tumsikie kama uhai wa maisha yetu. Hata hivyo hakika hiyo ya muda si ya wazi, kwa kuwa hatuwezi kutofautisha kikamilifu huo upendo wa kitoto unaotokana na Roho Mtakatifu na tendo la kimaumbile tu la kumpenda Mungu kwa namna isiyozaa matunda.

Mwanga wa Roho Mtakatifu haufikiwi bali unaonekana giza kwetu kwa jinsi ulivyo mkali; ila uvuvio wake *unaimarisha imani yetu* na kuifanya ipenye na kunogewa. "Sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu" (1Kor 2:12). Kutokana na hayo *Roho Mtakatifu anathibitisha pia hakika ya tumaini letu,* ambayo si bado hakika ya kufikia wokovu, bali ni hakika ya kuuelekea ambayo inaongezeka kadiri tunavyokaribia mwisho wa safari. Hatimaye na hasa Roho Mtakatifu, akiwa ndiye Upendo-nafsi, *anachochea katika waliokamilika upendo wa kumiminiwa* kwa Mungu na kwa jirani ulio tofauti na mapendo mengine. Ni upendo tusioweza kuufikia kwa msaada wa neema za kawaida; unahitaji uvuvio maalumu, yaani neema inayotenda iliyo ya juu zaidi, ambapo Roho Mtakatifu anatokeza moyoni mwetu upendo huo ambao yeye ni kwa pamoja mwanzo na mwisho wake. Hatutaweza kamwe kumpenda Mungu kama anavyotupenda kwa upendo usioumbwa na wa milele; hata hivyo kati yake na sisi kuna *usawa fulani wa upendo* Roho Mtakatifu anapotokeza ndani mwetu upendo wa kumiminiwa ambao anautakasa na kuuimarisha hadi kuingia mbinguni.

Bwana alimuambia Mt. Katerina wa Siena, "Ndani ya waliokamilika Roho Mtakatifu analia machozi ya moto" hasa akiona dhambi zinazopeleka watu kwenye maangamizi; mara nyingi machozi hayo ya Kiroho yanajaliwa madhambi makubwa yasamehewe. Kwa sababu hiyohiyo anaitwa *Baba wa maskini,* hasa wa wale wanaopenda ufukara mtakatifu. "Roho Mtakatifu anamlisha mwadilifu, anamlevya kwa utamu, anamjaza utajiri usiopimika… hapo mtu anakubali huzuni zote, hakuna cha kumkatisha tamaa, hakuna cha kumtikisa: anapokea nguvu kubwa na kuanza kuonja uzima wa milele" (Mt. Katerina wa Siena). "Watakatifu wanahisi ndani mwao kama utupu usio na mipaka, ambao viumbe vyote haviwezi kuujaza na ambao unaweza kujazwa tu na hali ya kumfurahia Mungu. Walipotenganika naye wanasikitika na kuteseka kama kwa kifodini cha muda mrefu, ambacho wasingekivumilia pasipo faraja ambazo Roho Mtakatifu anawapatia mara kadhaa" (A. Lallemant).

Yeye anawatia *upendo kwa msalaba,* yaani kwa Yesu msulubiwa, kwa mateso yake, kwa kuangamia kwake kitakatifu; anawapa hamu ya kuushiriki kadiri ya maongozi ya Mungu, na katika hamu hiyo anawafanya waone amani, nguvu na pengine hata furaha. Anawalinganisha na msulubiwa, akiokoa watu kwa njia yao na ya mateso yao. Anawaelewesha thamani ya miangaza yake ya Kimungu ambayo isipopingwa inafikishia utakatifu halisi. Hapo inazidi kueleweka jinsi matokeo ya kujiweka wakfu kwake yanavyoweza kuwa makubwa. Hatimaye anaweza akawapa waliokamilika zaidi hakika fulani ya uteule wao, kwa ufunuo wa pekee au neema inayolingana nao, akiwajalia mwonjo wa uzima wa milele ambao wanang'amua neema inayotia utakatifu kama mbegu ya utukufu.

**HATIMA**

Mafundisho hayo yenye msingi wa hakika katika ufunuo yanatuinua kwa mpando wa kupendeza hadi maandishi bora kuhusu muungano mkavu halafu mtamu, ambao pengine unamtoa mtu nje ya nafsi yake, na ambao ustawi wake kamili unaitwa muungano unaotugeuza. Baada ya kusoma *taratibu za juu za ustawi wa neema inayotia utakatifu,* wa upendo na wa vipaji vya Roho Mtakatifu, maneno ya watakatifu juu ya muungano huo hayashangazi: yanaonekana matunda bora yanayoundika ndani ya ua la upendo kwa athari ya dhati zaidi na zaidi ya mlezi wa ndani anayefundisha kwa mpako wake, pasipo kelele, akivuta kwa nguvu kubwa zaidi na zaidi.

*Muungano wa fumbo ni tunda bora lakini la kawaida la uwemo wa Utatu mtakatifu ndani mwetu,* kwa kuwa Nafsi za Kimungu zinakaa ndani ya mwenye neema inayotia utakatifu kama katika hekalu ambamo zinaweza kujulikana, na pengine kweli *zinajulikana kama kwa mang'amuzi kutokana na upendo wa kumiminiwa.* Zinajitambulisha kama uhai wa maisha yetu, na huo ujuzi hai wa Nafsi tatu zilizomo mwetu pamoja na upendo huo wa kumiminiwa vinapokomaa ipasavyo vinaunda muungano halisi. Hivyo uwemo wa Utatu ndani mwetu ndio kiini ambacho maisha yote ya Kiroho yanatoka na kurudi. Ndio utimilifu wa maneno ya Mt. Yohane: *"Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake"* (1Yoh 4:16). Hayo tuliyoyasema yanaonekana ya kweli zaidi tukimzingatia si huyu au huyu, bali binadamu alivyo na hasa *neema* ya maadili na vipaji *ilivyo:* si mbegu ya muungano wa fumbo tu, bali *kwa kawaida* ni pia mbegu ya heri ya kumuona Mungu.

### 4.3.4. ***MUUNGANO MKAVU NA ULE WA KUTOKA NJE YA NAFSI***

Tutazungumzia kwanza *muungano mkavu na mchungu,* yaani usiku wa roho, halafu *muungano wa kutoka nje ya nafsi,* yaani uchumba wa Kiroho, na hatimaye katika sura ijayo *muungano unaotugeuza,* yaani arusi ya Kiroho.

**MUUNGANO MKAVU NA MCHUNGU**

Hapo Mungu anafanya mtu atamani mema makuu aliyomuandalia akimpitisha katika tabu za kutisha: "Akili huwa imepatwa na giza isiweze kuushika ukweli; inasadiki yale yote ambayo ubunifu unaichorea na shetani anaiambia. Bila ya shaka Bwana wetu anamruhusu huyo amshawishi mtu, na pengine hata kumdanganya kwamba, eti! Amelaaniwa na Mungu… Katika dhoruba hiyo mtu hawezi kupokea faraja

yoyote… Hakuna dawa nyingine isipokuwa kuitumainia huruma ya Mungu. Naye isipotarajiwa kwa neno moja analomuelekezea au kwa tukio moja linalomtokea anamkomboa kutoka mabaya yake yote. Ungedhani mawingu hayajawahi kuwepo … na mtu anamtukuza Bwana, kwa kuwa ndiye aliyempigania na kumpa ushindi. Mtu anaona wazi kabisa kwamba hajaanza kupambana mwenyewe… Hapo anatambua unyonge wake na uwezo mdogo tulionao Bwana akitunyima msaada wake. Hahitaji tena kutafakari aelewe kweli hizo" (Mt. Teresa wa Yesu). Kwa kuwa sasa anaelewa vizuri maneno ya Mwalimu: *"Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote"* (Yoh 15:5) kuhusu wokovu, na anazidi kuelekea kukubali ya kuwa neema inatenda yenyewe na kusababisha juhudi zetu, badala ya kudhani kuwa inawezeshwa na juhudi hizo ifanye kazi.

**TUFANYE NINI KATIKA JARIBU HILO?**

"Kwa kuwa tabu hizo zinatoka juu, viumbe haviwezi kufanya kitu. Mungu wetu anataka tukiri ukuu wake na unyonge wetu… Njia bora ya kufikia kuvumilia mafadhaiko hayo ni kuwajibika katika kazi za upendo na kutegemea yote kutoka huruma ya Mungu. Yeye hawaachi kamwe wanaomtumainia… Mateso ya nje yanayosababishwa na mashetani ni ya nadra zaidi… tena tabu zote wanazoweza wakasababisha ni ndogo sana ukizilinganisha na hizo nilizokwishazieleza" (Mt. Teresa wa Yesu).

Baada ya tabu za ndani ambamo mna *uwemo mchungu wa Mungu,* mtu anapata ujuzi wa ukuu wa Mungu ambao mara nyingi unasababisha atoke nje ya nafsi yake walau kiasi.

**MUUNGANO WA KUTOKA NJE YA NAFSI UNAVYOONEKANA NA ULIVYO**

Kutoka nje ya nafsi ndiko *kusimama kwa hisi za nje;* hakudai daima mwili uinuke juu kutoka ardhini. Kunajitokeza kwa *mtu kutohisi tena* walau kiasi, kwa upumuaji kulegeza mwendo na kwa joto la mwili kupungua. "Mtu anatambua kwamba joto la uhai linapungua na mwili unazidi kuwa baridi, lakini kwa utamu na raha isiyosemekana… Mwili *unaganda,* macho yanaelekea moja kwa moja jambo lisiloonekana: pengine kope zinashuka… Hali hiyo, badala ya kudhoofisha mwili, *inauongezea nguvu mpya;* inaweza ikatokea kwamba mtu ambaye kwa kawaida anashindwa kuwa amepiga magoti muda mrefu, wakati wa kutoka nje ya nafsi anabaki vile pasipo shida" (Mt. Teresa wa Yesu). Pengine kusimama kwa hisi *si kamili* na kunamruhusu mtu aseme anapata mafunuo gani ili yaandikwe. Muungano wa kutoka nje ya nafsi kwa wenyewe hausimamishi kazi zote za mwili, kama vile kupumua.

Kupotewa na utumiaji wa hisi za nje katika hali hiyo kunatokana na *roho kuvutwa na Mungu* kwa neema ya pekee ya mwanga na upendo. Mwanga mwingi unaotolewa hapo kuhusu mafumbo ya imani unasababisha mshangao na upendo mkubwa kwa Mungu. Utashi unatekwa na utendaji wa Mungu, ni kama unajeruhiwa nao, na unamuelekea kwa nguvu zote, kama vile dira inavyoelekea kaskazini. Mshangao wa akili unakua kwa upendo, na upendo unakua kwa mshangao: "kutazama uzuri kunatufanya tuupende, na upendo unatufanya tuutazame" (Mt. Fransisko wa Sales). Mtu akiwa ametekwa hivyo na mshangao na upendo kwa Mungu, anapotewa na utumiaji wa hisi zake kwa sababu utendaji wake wote unakwenda upande wake wa juu: "Roho ikifuata kabisa utendaji wa kipawa chake kimojawapo, mtu anaacha kutenda kwa kipawa kingine" (Mt. Thoma wa Akwino). Ikiwa mwanasayansi anaweza akazama katika utafiti wake kiasi asisikie tena anachoambiwa, zaidi inaweza ikamtokea mwanasala neema kubwa inapomfanya ahisi ukuu usio na mipaka wa Mungu na avutwe kuutazama kwa raha. Hali hiyo inaweza kuwa matokeo ya kawaida ya kuzama ndani ya Mungu. Tutakavyoona, kesi ya roho kutekwa ghafla na kwa nguvu ili kuinuliwa izame katika mafumbo kwa namna ya juu ni tofauti kwa sababu hapo utekaji unatangulia tendo la kuzama badala ya kulifuata.

Je, upendo unaotoka nje ya nafsi *una hiari na stahili bado?* Bila ya shaka! Hiari ya tendo la upendo, ambayo ni sharti la kustahili, inatoweka mbinguni tu, roho inapomuona Mungu uso kwa uso, inavutwa naye isiweze kumuacha, na inampenda kwa upendo wa kujiotea usio wa hiari tena: ni upendo mkuu kuliko hiari.

*Muda* wa kutoka nje ya nafsi unaweza ukawa tofautitofauti; kama ni kamili kwa kawaida kunadumu nukta chache, sanasana nusu saa: lakini zipo kesi za hisi kusimama hata siku nne na zaidi. Kwa kawaida hali hiyo inakwisha kwa *mtu kuzinduka mwenyewe* na kuanza kutumia tena hisi zake polepole tu, kana kwamba angetokea ulimwengu mwingine. *Kuzinduka kunaweza kukasababishwa na agizo la kiongozi,* liwe limetolewa kwa sauti au kwa wazo tu. *Utiifu huo* wakati wa kutoka nje ya nafsi ni moja kati ya dalili zinazothibitisha asili yake ya Kimungu, kutokana na uadilifu unaofanya utashi wa binadamu umtii Mungu hata kwa kuacha hali hiyo.

Mara nyingi hali hiyo ikiwa ya bandia ni rahisi kuipambanua na ile halisi. Mtu akitoka nje ya nafsi kwa neema hachangamki kwa namna za ajabuajabu na za kimwili tu wanavyofanya wenye ugonjwa wa nafsi, halafu wakapoa na kuishiwa nguvu. Bali roho na mwili wake wote vinaelekea jambo la Kimungu kwa utulivu mkubwa; roho inavutwa na nguvu ya fumbo itoke nje ya hisi zake, kwa kawaida kutokana na njozi iliyoipata. Mwisho wake ni kurudia hali ya kawaida kwa utulivu, likibaki tu sikitiko la kutoweka kwa njozi na furaha ya kimbingu iliyosababishwa nayo. Mtu dhaifu anaweza akazimia kutokana na ubunifu wake kuchangamka au sala kumgusa mno: hapo ni lazima tuzuie iwezekanavyo kuzimia huko kwa kuimarisha mwili kwa lishe bora zaidi. Hatimaye hali ya namna hiyo inaweza ikasababishwa na shetani: dalili zake ni kwamba mtu anaishi katika dhambi, anajisokotasokota, anasema maneno yasiyo na maana anayayosahau baadaye, anatafuta

kuonekana hivyo penye watu wengi, na hasa anapokea ujumbe unaoelekeza kutenda maovu au kutenda mema kwa lengo baya.

**TOFAUTI KATI YA KUTEKWA NA KUTOKA NJE YA NAFSI**

Kutoka nje ya nafsi ni aina ya *kuishiwa nguvu* inayotokea kwa utamu kutokana na jeraha la upendo. "Mtu anasikia amepata jeraha la kupendeza… ambalo asingependa lipone kamwe. Anamlalamikia Bwana arusi wake hata kwa nje kwa maneno ya upendo. Hawezi kujizuia kwa sababu yeye anamfanya asikie uwemo wake asijidhihirishe kwa namna anayoweza kumfurahia" (Mt. Teresa wa Yesu). Hiyo ni kama ziara fupi kabla ya muungano wa kudumu zaidi unaoitwa muungano unaotugeuza.

Kutoka nje ya nafsi kwa kuishiwa nguvu ni tofauti na kutekwa na Mungu kwa ghafla na kwa nguvu. Tukio hilo "linaiongezea kitu hali ya kutoka nje ya nafsi… kutekwa kunaiongezea aina ya kutumiwa mabavu" (Mt. Thoma wa Akwino). Mara nyingi kutekwa hivyo ndiyo kilele cha uchumba wa Kiroho; hapo mtu ni kama amelewa asiweze kushughulikia kingine isipokuwa Mungu. Kutekwa kunafuatwa na *mruko wa roho,* ambapo mtu anajiona amehamishiwa mahali pengine, pa Kimungu tu.

**MATOKEO YA MUUNGANO WA KUTOKA NJE YA NAFSI**

Huko kuvutwa ndani ya Mungu kunasababisha *utengano mkubwa na viumbe*, ambavyo ubatili wake unazidi kuonekana wazi; halafu kunasababisha *uchungu mkubwa kwa dhambi zilizotendwa* na kwa yale yote yanayosogeza mbali na Mungu. Mtu anazidi kuona *thamani ya mateso ya Mwokozi* na ya uchungu wa Maria chini ya msalaba, na katika kuzama ndani ya mafumbo hayo anachota subira ya ajabu ili avumilie majaribu ambayo Bwana anataka kumtumia tena ili achangie wokovu wa watu.

Kwa kifupi, matokeo ya muungano wa kutoka nje ya nafsi ni utakatifu mkubwa maishani. "Tukimuona mtu ambaye anatekwa katika sala… lakini hatoki nje ya nafsi yake katika maisha, yaani hana maisha bora yanayoambatana na Mungu, kwa kujinyima malimwengu na kufisha matakwa na maelekeo ya kimaumbile, kwa upole, usahili na unyenyekevu wa ndani, na hasa kwa upendo wa kudumu, unisadiki, Teotimo, kwamba kutekwa kwake ni kwa shaka na kwa hatari sana" (Mt. Fransisko wa Sales).

**UTAKASO WA UPENDO**

Baada ya muungano wa kutoka nje ya nafsi, kuna utakaso mchungu wa upendo kama maandalizi ya muungano unaotugeuza. "Mtu anajisikia kama kuchomwa kwa mshale wa moto… ndani mwake kabisa… Uchungu wa ndani ni mkali hivi kwamba hajali tena mwili… Anahisi upweke wa ajabu; hakuna kiumbe duniani kinachoweza kumfariji… yote yanamtesa. Ni kama mtu aliyeelea hewani; ardhi haimtegemezi hata kidogo, wala hawezi kujiinua juu mbinguni. Anateswa na kiu asiweze kuifikia chemchemi… Ni haki kabisa kwamba kitu cha thamani sana kilipwe sana. Mtu anaelewa thamani isiyopimika ya utakaso huo mchungu wa upendo na kujitambua hastahili kamwe kuupata… Katika kiwango hicho cha ukali, jaribu hilo linachukua muda mfupi: sanasana saa tatu au nne; la sivyo udhaifu wetu wa kimaumbile usingeweza kulistahimili… Kifodini hicho ni kichungu, lakini kinamuachia matokeo ya ajabu. Hasa kinamuondolea hofu ya tabu ambazo zinaweza zikampata, kwa kuwa anaziona si kitu akizilinganisha na mateso makali yaliyompata… Mwenyewe amejitenga na viumbe zaidi sana kwa kuelewa kwamba Muumba tu anaweza kumfariji na kumshibisha" (Mt. Teresa wa Yesu).

## 4.3.5. *MUUNGANO UNAOTUGEUZA, UTANGULIZI WA ULE WA MBINGUNI*

Sasa tunataka kusema juu ya ustawi wa uzima wa neema unaowezekana duniani katika mtu aliyevuka utakaso wa Kimungu wa roho. Akitoka hizo tabu za ndani ana ujuzi wa ukuu wa Mungu unaomfanya pengine azame ndani yake, pengine ashangilie sifa za Mungu asiweze kujizuia. "Shangwe hizo zinamzamisha katika kujisahau pamoja na viumbe vyote hata asiweze kuwaza wala kusema isipokuwa kwa kumpatia Mungu sifa zile ambazo ni kama tunda la furaha yake" (Mt. Teresa wa Yesu). Hiyo furaha takatifu, inayotegemea muungano na Mungu, inaweza kutamaniwa, wakati haifai hata kidogo kutamani njozi na mafunuo ambavyo ni fadhili za pekee zisizohusiana na ustawi wa uzima wa neema ndani mwetu. "Kwa kupokea fadhili nyingi za namna hiyo mtu hastahili ongezeko la utukufu… Kuna idadi kubwa ya watakatifu wasiojua maana ya kupokea neema hizo, kumbe wapo wengine wasio watakatifu wanaozipokea… Mara nyingi kwa fadhili moja tu ya namna hiyo Bwana anapeleka wingi wa tabu" (Mt. Teresa wa Yesu).

**NEEMA ZINAZOWEZA ZIKAENDANA NA MUUNGANO UNAOTUGEUZA**

Pengine arusi ya Kiroho inaadhimishwa kwa ishara za maana, kama vile mtu kupewa pete iliyopambwa kwa vito, ambayo baadaye anaweza akaiona mara kadhaa, au mtu kusikia nyimbo za mbinguni. Pengine ishara hizo zinazofikiwa na hisi zinaendana na *njozi ya Bwana* na *kuuona Utatu mtakatifu kwa akili.*

Mwono huo kwa njia ya wazo la kumiminiwa na ya mwanga mkuu, unawadhihirishia tofauti za Nafsi tatu na umoja wa hali yao kuliko anavyoweza kufanya mwanateolojia bora kwa maelezo yake. Hawana mwono wa moja kwa moja wa umungu, fumbo hilo halijawa wazi kwao, hawajaona kwamba asingekuwa Nafsi tatu

asingekuwa Mungu. Wanabaki katika ngazi ya imani, lakini imani yao imekuwa inapenya mafumbo, inaangaza na kunoga kwa namna ya pekee. Wanaelewa kuliko zamani kwamba Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho Mtakatifu ni Mungu, na kwamba hata hivyo Baba si Mwana wala hao si Roho Mtakatifu. Kwa namna fulani wanaanza kuona kwamba Baba katika uzazi wake usio na mipaka anamshirikisha Mwana umungu wote, na kwamba hao wanamshirikisha Roho Mtakatifu kwa uenezi kamili wa wema wa Kimungu na kwa umoja wa dhati. Katika hilo wanaona kielelezo cha ajabu cha ushirika wa ekaristi na cha muungano wa ndani wa roho na Muumba na Baba yake. Huo mwono wa kiakili wa Utatu mtakatifu si bora kama ule wa mbinguni, uangavu wake una kiasi tofauti, unapatikana kwa kwikwi, na si lazima uendane na muungano unaotugeuza ambao hapa duniani ndio mwisho wa kupanda kwa Mungu.

**MUUNGANO UNAOTUGEUZA WENYEWE**

Kwa kawaida katika hatua hiyo hali ya kutoka nje ya nafsi haipatikani tena. "Roho inapotewa na *udhaifu huo mkubwa* ambao ulikuwa unampa tabu sana asiweze kabisa kuachana nao. Labda hiyo inatokana na kwamba Bwana wetu ameiimarisha, ameipanua na kuiwezesha kufanyiwa kazi" (Mt. Teresa wa Yesu). Hivyo muungano na Mungu unakuwa karibu wa kudumu, kwa kuwa unaweza kufanyika bila ya kuzuia matumizi ya vipawa. *Hapo vipawa vya juu vinavutwa na kiini cha roho unamokaa Utatu mtakatifu.* Kwa neema hiyo mtu hawezi kutia shakani uwemo wa Nafsi za Kimungu ndani mwake wala karibu hapotewi kamwe na uhusiano nazo. "Katika matendo fulanifulani ya siri mtu anatambua kwamba Mungu ndiye anayeihuisha roho" (Mt. Teresa wa Yesu).

Mt. Yohane wa Msalaba alitoa mifano mbalimbali, "Jiwe linavutwa daima na kiini cha dunia… likifikia humo, tunaweza kusema limefikia kiini cha dhati zaidi. Basi, kiini cha roho ni Mungu; roho ikimfikia kadiri ya mfumo wake na ya nguvu zote za utendaji wake na za elekeo lake, *itakuwa imeona kiini chake cha dhati ndani ya Mungu*… itamjua, itampenda na kumfurahia kikamilifu. Kabla haijafikia kiwango hicho… inalenga daima muungano kamili zaidi… Ikifikia kiwango cha mwisho, upendo wa Mungu utakuwa umeitia jeraha katika kiini chake cha dhati zaidi, na *kwa roho hilo litakuwa mageuzo na maangazo ya nafsi yake yote*, ya uwezo na nguvu yake yote, kadiri inavyoweza kupokea, hivi kwamba inaonekana imekuwa Mungu. Hapo ni kama kioo safi na kiangavu kilichofikiwa na nuru… Ikiwa nuru hiyo ni tele zaidi, kioo kinaonekana kuchanganyikana nayo… Ni kama pale ambapo moto, baada ya kushambulia ukuni na kuukausha kwa mwali wake, hatimaye unaupenya na kuugeuza ndani mwake". Bado ni ukuni, lakini ukuni wa moto, uliopata sifa za moto. Vivyo hivyo moyo uliotakata unatoka karibu mfululizo mwali unaomuelekea Mungu.

Mt. Teresa alitumia mfano mwingine, "Ni kama maji ambayo yanamwagika kutoka mbinguni ndani ya mto na kuchanganyikana nao visiweze kupambanuliwa tena". Ulitolewa pia mfano wa mishumaa miwili ambayo miali yake inaunganika kuwa mmoja. Kuna aina ya muungano kati ya uhai wa roho na uhai wa Mungu. Undani wa hali hiyo ya juu si muujiza hata kidogo, bali ni "*hali kamili ya maisha ya Kiroho*" (Mt. Yohane wa Msalaba): ndio ustawi kamili wa neema ya maadili na vipaji.

Basi, muungano unaotugeuza ni wa dhati na kuleta amani kubwa, ambayo karibu isiweze kuvurugika, walau kwenye kilele cha vipawa vya juu. Hata hivyo inaweza ikatokea kwamba roho "ina huzuni nyingi kiasi cha kufa" (Mk 14:34), Yesu akitaka kuishirikisha tena maisha yake ya malipizi na kuileta kwenye Getsemane kwa wokovu wa wakosefu. Katika bustani hilo mwenyewe, ambaye hakuhusiana na Mungu kwa muungano unaotugeuza tu bali kwa umoja wa nafsi, hata hivyo alitaka kuonja huzuni hiyo ili sadaka yake ya kuteketezwa iwe kamili.

**UFAFANUZI WA TEOLOJIA KUHUSU HALI HIYO**

Mt. Yohane wa Msalaba aliandika kuhusu vyumba vya ndani kwamba, "Tunaweza kusema vyumba hivyo ni saba, na *vinakaliwa vyote mtu akiwa na vipaji vya Roho Mtakatifu kikamilifu,* kadiri anavyoweza kuvipokea hapa duniani… Wengi wanafikia na kuingia chumba cha kwanza, kila mmoja kadiri ya ukamilifu wa upendo alionao, lakini wachache sana wanaingia kuanzia maisha haya katika chumba cha mwisho, cha ndani zaidi; kwa sababu humo umeshafanyika muungano kamili na Mungu ambao ni desturi kuuita arusi ya Kiroho". Kwa maneno mengine, *mtu anapokuwa na ukamilifu wa kipaji cha hekima*, ambacho ndicho cha juu kati ya vyote saba alivyovipokea pamoja na neema ya utakaso, amefikia hekalu la ndani mwake unamokaa Utatu mtakatifu. Hapo muungano na Mungu unafanyika kweli na kwa namna fulani unamgeuza; ingawa kati ya kiumbe na Muumba kuna umbali usiopimika, muungano huo unafanyika kwa ujuzi unaofanana na mang'amuzi na kwa upendo wa dhati. Roho *inakuwa ya Kimungu* kwa kushirikishwa kikamilifu umungu: "Yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye" (1Kor 6:17).

Hapo muungano *unatugeuza* kwa sababu roho, bila ya kupotewa na umbile lake, inazidishiwa kwa kiasi kikubwa neema inayotia utakatifu na upendo, tena kwa sababu upendo motomoto unatugeuza katika yule ambaye tunampenda kama *mimi mwingine*, na kumtakia mema yote ya kumfaa kama tunavyojitakia. Ikiwa huyo ni Mungu, watakatifu wanamtakia awatawale kwa dhati zaidi, awe ndani mwao kuliko walivyo wenyewe, kuliko hewa ilivyo ndani ya mapafu au kuliko damu mpya ilivyo ndani ya moyo. "Kadiri roho ilivyo safi na tupu katika imani yake hai na kamili, ina wingi wa upendo wa kumiminiwa na Mungu; na *kadiri ilivyo na*

*upendo, Roho Mtakatifu anaiangaza* na kuishirikisha vipaji vyake, hivi kwamba upendo ndio sababu na njia ya ushirikishaji huo" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Furaha ya muungano wa uchumba haidumu zaidi ya nusu saa hivi, ambapo mtu anamng'amua Mungu aliyemo ndani mwake na kumkumbatia, kumbe katika arusi ya Kiroho, ambayo inafungwa hapa duniani na kutimia mbinguni, muungano wa upendo na Mungu, anayejulikana kama kwa mang'amuzi katika kiini cha roho, unakuwa *wa kudumu zaidi*. "Kati ya watu waliopo katika uchumba wa Kiroho, mmoja anapokea kuliko mwingine: mmoja kwa namna moja, mwingine kwa namna nyingine" (Mt. Yohane wa Msalaba). Vilevile katika muungano unaotugeuza kuna viwango mbalimbali hadi kile cha juu zaidi alichokifurahia bikira Maria. Katika viwango hivyo wamefikia kiini chao cha dhati kadiri ya uteule wao. Ndio utimilifu wa ombi la Yesu: "Wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi" (Yoh 17:22-23).

**MATOKEO YA MUUNGANO UNAOTUGEUZA**

Matokeo ya hali hiyo ni yale ya maadili ya Kimungu na ya vipaji vilivyostawi kikamilifu. "Nionavyo mimi, roho haiwezi kamwe kujaliwa hali hiyo pasipo kuthibitishwa moja kwa moja katika neema inayotia utakatifu" (Mt. Yohane wa Msalaba) kwa maana neema hiyo ni kushiriki utakatifu usioweza kupotewa wa wenye heri wa mbinguni kwa njia ya *ustawi mkubwa wa upendo* unaozidi kutusogeza mbali na dhambi. Ustawi huo unakamilishwa na *ulinzi wa pekee* wa Mungu, ambaye anazuia nafasi za dhambi na kuimarisha kadiri inavyohitajika hivi kwamba tangu hapo mtu anakingiwa daima dhambi ya mauti na kwa kawaida hata dhambi nyepesi ya makusudi. Mt. Teresa alisema tu kuwa mtu karibu anaondolewa usumbufu wowote unaotokana na maono, na kwamba hatendi dhambi nyepesi ya makusudi wakati wote ambapo neema ya muungano unaotugeuza inaendelea kufanya kazi, "Mtu aliyeingizwa katika makao hayo hatawaliwi tena na mabadiliko ya hisi na ubunifu; walau hayo hayawezi kumdhuru wala kumuondolea amani. Inaweza ikaonekana kwamba nataka kusema aliyefadhiliwa hivyo ana hakika kuhusu wokovu wake na hawezi kuanguka tena. Lakini wazo langu ni tofauti. Kila ninaposema kuwa yuko salama, ni lazima kuelewa hivi, kwamba yuko salama mpaka Mungu Mkuu atakapomshika mikononi mwake na mpaka mwenyewe hatamkosea". Mbele ya misimamo hiyo tofauti kidogo, labda tuseme tu kuwa hapo Roho Mtakatifu anamthibitishia mtu hakika ya tumaini ya kulenga wokovu akikuza ndani yake upendo wa kitoto.

Pengine katika hali hiyo kuna *miguso ya Kimungu* ya dhati hivi kwamba inatiwa katika undani wa roho. Mguso wa Kimungu ni tendo lipitalo maumbile linalofanyika katika utashi na akili, mle vinamotokana na undani wa roho. Mungu yumo ndani mwetu kuliko tulivyo sisi wenyewe, kwa kuwa ndiye anayetudumisha kwa tendo la kuendeleza uumbaji. Vilevile ndiye anayedumisha neema inayotia utakatifu katika undani wenyewe wa roho, na pengine anajivutia undani wa utashi na akili kwa uvuvio maalumu *unaoanzia ndani* ya vipawa hivyo.

Ni kana kwamba *Mungu anakumbatia roho,* pengine kwa nguvu kubwa kweli. Pengine katika undani wa vipawa hivyo vya juu mna *jeraha la upendo*, jeraha tamu rohoni ambalo linaweza likaendana na jeraha chungu mwilini, hasa upande wa moyo. "Kwa kawaida Mungu haujalii mwili fadhili yoyote kabla hajaijalia roho hasa, na hapo, kadiri ya ukubwa wa furaha na nguvu ya upendo unaosababishwa na jeraha la roho, ni mkubwa vilevile uchungu unaosababishwa na jeraha la mwili. Yote mawili yanakua pamoja kwa sababu watu hao, wakiwa wametakata na kuimarika ndani ya Mungu, kile kinacholeta uchungu upande wa mwili unaoelekea kufa, ni utamu na raha kwa roho iliyopata nguvu na afya" (Mt. Yohane wa Msalaba). Ni Mungu anayejeruhi roho akiivuta kwa nguvu kwake na kuitia hamu kubwa ya kumuona moja kwa moja isitengane naye kamwe. Ndio msimamo unaowezesha kupata mara heri hiyo: kwa namna yake hamu hiyo imo pia katika roho za toharani mwishoni mwa utakaso wao.

Mungu hawezi akajionyesha moja kwa moja kwa watu wasio na hamu kubwa ya kuwa naye milele. Mwenyewe anawaandaa kwa hilo kwa mguso wa Kimungu wenye *ladha ya uzima wa milele.* Miguso ya namna hiyo haipatikani pasipo kubandukana kikamilifu na malimwengu yote, lakini mmojawapo kati ya miguso hiyo unalipa juhudi zote alizofanya mtu.

"Lo! Mwali hai wa upendo, / jinsi unavyokijeruhi kwa upole / kiini cha dhati cha roho yangu! / Kwa kuwa si mchungu tena, / timiza kazi yako, ukipenda: / chana sitara ya mkutano huo mtamu" (Mt. Yohane wa Msalaba). Yaani, timiza kazi ya muungano wetu, kata uzi wa maisha ya duniani, ambao ndio kizuio cha mwisho cha kukutana na Mpenzi. Sitara hiyo inaruhusu kumchungulia Mungu, lakini inazuia muungano wa moja kwa moja. Mwali hai ndiye Roho Mtakatifu anayesababisha ndani ya mtu matendo ya upendo yanayostahili kuliko yale yote aliyoweza kuyafanya kabla yake. "Jambo la ajabu! Huo moto wa Kimungu, ambao unaweza kuangamiza ulimwengu mara elfu kwa urahisi mkubwa kuliko moto wa kawaida unavyoweza kuteketeza uzi wa kitani, hata hivyo hauangamizi wala hauteketezi. Hivyo siku ya Pentekoste huo moto wa Kiroho ulipowashukia mitume, wakawa wanawaka kwa ndani upendo mtamu wa kupanua na kufurahisha roho" (Mt. Yohane wa Msalaba).

*"Ni vema kueleza hapa sababu gani ni wachache hivi wanaofikia hiyo hali ya juu ya ukamilifu na ya muungano na Mungu*. Kwa hakika si kwa sababu Mungu anataka kuijalia idadi ndogo tu ya watu bora:

kinyume chake hamu yake ni kwamba huo ukamilifu mkuu uwe wa wote. Ila anachotafuta mara nyingi bure ni vyombo vinavyoweza kupokea ukamilifu huo. Mungu anamtumia mtu majaribu mepesi, lakini huyo anadhihirika kuwa dhaifu na kukimbia mateso kadiri anavyoweza, hataki kupokea uchungu wowote, wala kujifisha walau kidogo, tena anakosa kabisa ile subira imara anayotakiwa kuwa nayo. Hapo Mungu haendelei kuwatakasa akiwainua kutoka mavumbini kwa njia ya kuwashusha… *Watu wanatamani kuwa wakamilifu lakini hawakubali kupitishwa katika njia ya majaribu inayowaunda wakamilifu"*. Ni lazima kupitia tabu nyingi ili kufikia "maisha kamili ya Kiroho ambayo ni kumpata Mungu kwa njia ya muungano wa upendo" (Mt. Yohane wa Msalaba). Mambo ya Kiroho yaliyo matamu kweli yanatokana na msalaba na moyo wa sadaka unaofisha ndani mwetu yale yasiyoratibiwa ili upendo kwa Mungu na kwa jirani ushike nafasi ya kwanza.

"Moyo unapowaka hivyo kwa upendo wa Mungu wake, mtu anaona *taa za moto* zinazoangaza yote kutoka juu; hizo ndizo sifa za Mungu: hekima, wema, huruma, haki, maongozi, umilele, enzi kuu. Ni kama rangi za upinde wa mvua wa Kimungu ambazo zinaunganika ndani ya umungu bila ya kuangamizana, kama vile rangi saba za upinde wa mvua angani zinavyounganika katika nuru nyeupe inayozisababisha. Taa hizo zote zinaunganika katika nuru moja, katika tanuri moja, ingawa kila sifa inadumu kuwa na mwanga wake na moto wake" (Mt. Yohane wa Msalaba).

Kinachoshangaza katika watu wa namna hiyo ni *jinsi wasivyojijali na wanavyotamani kuteseka kwa mfano wa Yesu.* Wanashiriki nguvu yake na upendo wake mkuu kwa ajili ya jirani. Wanafikia kutekeleza kwa pamoja maadili yanayoonekana kupingana; wanaunganisha sala ya hali ya juu na utendaji bora unaowapasa katika malimwengu. Hivyo wamefananishwa na Kristo moja kwa moja. Maisha ya kitume au maisha ya malipizi yanafurika kutoka ukamilifu wa muungano wao na Mungu.

**KUTAMANI MUUNGANO UNAOTUGEUZA**

Je, mtu anayeonekana kuwa amevuka usiku wa roho walau kiasi, anaweza kutamani na kuomba neema ya muungano unaotugeuza? Bila ya shaka, tujue tusijue, neema hiyo ni kilele cha matamanio yetu hapa duniani; lakini inafaa tuitokeze hamu hiyo kwa namna tofauti, kwa kutamani Mungu azidi kutawala ndani mwetu nasi tufanane na Yesu kikamilifu zaidi. Mt. Teresa wa Yesu alialika wafuasi wake kuutamani muungano huo wa dhati, lakini kwa unyenyekevu mkubwa, wasitake kulazimisha: "Mkiona pingamizi lolote toka kwa Mungu, nawashauri msijaribu kwenda mbele. Mngemchukiza kiasi kwamba angewafungia mlango moja kwa moja. Yeye anapenda sana unyenyekevu. Mkijiona hamstahili kuingia hata katika makao ya tatu, mtajaliwa mapema kuingia katika yale ya tano. Mtaweza kuyazoea na *kumtumikia humo vizuri* hivi kwamba atawaruhusu muingie katika yale aliyojiwekea… Kwa kweli nyinyi hamtaweza kuingia makao yote kwa nguvu zenu, hata mkiziona ni kubwa sana: ni juu ya mwenye jumba kuwaingiza".

"Enyi mnaoota kutembea kwa utulivu na faraja kwenye njia za Kiroho, laiti mngejua ilivyo lazima mjaribiwe ili kufikia hizo hakika na faraja kwa njia ya mateso… Lo! Kama tungeelewa kwa dhati kwamba haiwezekani kufikia unene yaani vilindi vya hekima na utajiri wa Mungu pasipo kupenya unene wa aina elfu za mateso, kwa furaha na hamu kubwa ya roho! Mtu anayetamani kweli hekima, kwanza anatamani sana kuzama kabisa katika unene wa msalaba unaofikisha kwenye uzima… Wengi wanataka kufikia mwisho bila ya kupitia njia inayofikisha huko" (Mt. Yohane wa Msalaba).

**UDHATI WA MUUNGANO HUO**

Udhati wa muungano unaotugeuza unatokana na *neema inayotenda* ya hali ya juu. Tofauti na neema inayosaidia tu kutenda, ile inayotenda tokeo lake ni la kumpatia Mungu, kwa sababu hapo hatutendi, bali tunatendewa naye, ingawa kwa kukubali wenyewe, kwa sababu utashi wetu utadumu hata katika heri ya milele. "Hapo utashi wa mtu haupotei, bali unaunganika kwa nguvu na utashi wa Mungu anayempenda hivi kwamba unapenda kwa nguvu na ukamilifu ambavyo anapendwa naye… Nguvu hiyo ndiye Roho Mtakatifu, na hapo roho inageuzwa ndani yake. Mwenyewe anatolewa kwake ili kuipatia hiyo nguvu ya upendo, naye anatolea na kufidia yale iliyopungukiwa nayo" (Mt. Yohane wa Msalaba).

**USAWA WA UPENDO**

Mtu anafikia *usawa fulani* na Mungu: "Roho inatenda ndani ya Mungu na kwa njia yake yale ambayo Mungu mwenyewe anayatenda ndani ya roho na *kwa namna* anayoyatenda; utashi wa pande mbili ni kama mmoja tu, na *utendaji wa Mungu umeunganika na ule wa roho*. Tangu hapo, kwa kuwa Mungu anajitoa kwake kwa uhuru na pasipo kujitafutia faida, pia roho, iliyo na utashi huru na mkarimu kadiri ilivyounganika vema na Mungu, inampatia Mungu mwenyewe, kwa njia ya Mungu, na ndiyo zawadi halisi na kamili ya roho kwa Mungu… Hivyo roho inampatia kwa mikono miwili yale inayoyapokea toka kwake, na katika zawadi hiyo inayompatia Mungu, roho inampatia, kwa utashi wake wote ulio huru, Roho Mtakatifu aliye wake, ili kwa njia yake ajipende anavyostahili. Nayo roho inapata furaha na raha isiyopimika kwa sababu inaona kuwa inampatia Mungu kitu cha kwake kinacholingana na ukuu wa Mungu usio na mipaka" (Mt. Yohane wa Msalaba).

**HATIMA**

Ni ile ya "Wimbo wa Kiroho" wa Mt. Yohane wa Msalaba, "Enyi watu mlioumbwa kwa ajili ya vilele hivyo na mlioitwa kuvipata, mnafanya nini? Mnashughulikia nini? Mnayoyatamani ni ya chini tu, mali yenu ni umaskini mtupu! Lo! Upofu wa kusikitisha! Ingawa kuna mwanga mkubwa hivi, macho yenu hayaoni, nanyi mnabaki viziwi wakati zinaposikika sauti kubwa hivi!"

"Mwaliko huo, ambao mtakatifu wetu aliwaelekezea watu kwa jumla, unatuonyesha kuwa hakudhani makuu hayo aliyotueleza yako nje ya kawaida… Hakika kuchanua kwa mbegu ya uzima upitao maumbile, iliyo neema inayotia utakatifu ndani mwetu, kumeandaliwa kwa wote waliyo nayo" (Gabrieli wa Mt. Magdalena).

# 5. **NEEMA ZA PEKEE**

Kisha kusema juu ya hatua tatu za maisha ya Kiroho bila ya kupunguza ukuu wake, yaani kuzama katika mafumbo ya imani, sasa tunataka kufafanua neema za pekee ambazo pengine zinaendana na hali hiyo, lakini umbile lake ni tofauti.

## 5.1. ***KARAMA***

"Pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule… Kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa *neno la hekima*; na mwingine *neno la maarifa*, apendavyo Roho yeye yule; mwingine *imani* katika Roho yeye yule; na mwingine *karama za kuponya* katika Roho yule mmoja; na mwingine *matendo ya miujiza*; na mwingine *unabii*; na mwingine *kupambanua roho*; mwingine *aina za lugha*; na mwingine *tafsiri za lugha*; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimwagia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" (1Kor 12:4-11; taz. Rom 12:6-8). Mtume aliendelea kwa kuweka upendo juu kuliko karama hizo zote, "Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora. Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi" (1Kor 12:31-13:2) kwa sababu hapo utashi wangu unaelekea kinyume cha matakwa ya Mungu.

**UMBILE NA MGAWANYO WA KARAMA HIZO**

Neema inayotia utakatifu na upendo vinatuunganisha na Mungu, lengo letu kuu; kwa hiyo ni bora kuliko karama, zilizo fadhili za pekee ambazo zinalenga *hasa faida ya jirani,* tena zinamuandaa tu kuongoka, bila ya kumshirikisha uzima wa Mungu. Karama ni *ishara* tu zinazothibitisha ama ufunuo wa Mungu uliotolewa kwa wote, ama utakatifu wa mtumishi wake.

Neema inayotia utakatifu inapita maumbile kwa namna tofauti na karama. Neema inayotia utakatifu *inapita maumbile* kwa kuwa ni kushiriki uzima wa ndani wa Mungu; kwa hiyo haionekani wala haijulikani na maumbile. Kumbe hizo ishara zinazojulikana na maumbile haziyapiti kwa mfumo wake zenyewe, isipokuwa kwa namna zilivyotokea. Hivyo ufufuo wa maiti unamrudishia *kwa njia ipitayo maumbile* uhai *wa kimwili* bila ya kusababisha ndani yake uzima wa Mungu. Hivyo katika ishara hizo kinachopita maumbile ni cha nje na kidogo kuliko neema inayotolewa na ubatizo.

Katika jedwali lifuatalo tunaweza kuona karama hizo kadiri ya Mt. Thoma wa Akwino:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Neema zilizotolewa bure ili kuelimisha jirani kuhusu mambo ya imani | 1. zinajulisha kikamilifu mambo ya Mungu | | *imani* au hakika ya pekee kuhusu misimamo isiyoyumbishwa<br>*maneno ya hekima* kuhusu yatokanayo na Mungu asili ya yote<br>*maneno ya maarifa* kuhusu mifano na matokeo yanayodhihirisha sababu |
| | 2. zinathibitisha ufunuo wa Mungu | kwa matendo | *Uponyaji*<br>*matendo ya miujiza* |
| | | kwa ujuzi | *unabii*<br>*upambanuzi wa roho* |
| | 3. zinasaidia kuhubiri Neno la Mungu | | *aina za lugha*<br>*tafsiri za lugha* |

**MATUMIZI YA MAFUNDISHO HAYO**

Kwa kawaida fadhili za pekee, ambazo pengine zinaendana na sala ya kumiminiwa, zinapangwa pamoja na karama hizo. Mt. Yohane wa Msalaba akianzia misimamo ya teolojia alitofautisha vizuri *kuzama katika mafumbo kwa jumla katika giza* na namna mbalimbali za *ujuzi maalumu (mafunuo, njozi na maneno ya ndani):* "Kuhusu ujuzi wa jumla katika giza hakuna mgawanyiko, ni *kuzama katika mafumbo kwa imani: ndio lengo* ambapo tuifikishe roho; ujuzi mwingine wowote unatakiwa kulichangia kuanzia wa awali, nayo roho inatakiwa kusonga mbele daima kwa kuachana na kila mmojawapo".

Tutaeleza kwanza *mafunuo, halafu tutaona namna maalumu ambazo yanapatikana.* Tena kati ya fadhili hizo tutaeleza kwanza zile za nje zaidi, ambazo zinalenga *hasa faida ya jirani* na kuhusiana na karama. Halafu tutazingatia zile zinazolenga zaidi utakatifu wa mtu anayezipokea. Tukianzia mambo ya jumla kwenda yale maalumu, na kutoka yale ya nje kwenda yale ya ndani tutakwepa kujirudiarudia na tutaelewa zaidi kazi ya Mungu.

## 5.2. ***MAFUNUO NA NJOZI***

Mafunuo ya Kimungu yanadhihirisha kwa namna ipitayo maumbile ukweli fulani uliofichika, yakitegemea karama ya unabii. Yenyewe ni *ya hadhara* ikiwa yalitolewa na manabii wa Agano la Kale, na Kristo na mitume wake na yanapendekezwa kwa wote na Kanisa ambalo linatunza hazina hiyo katika Maandiko na katika Mapokeo. Kumbe ni *ya binafsi* yakilenga faida ya watu kadhaa tu. Mafunuo ya binafsi, hata yale muhimu, hayadai tuyashike kwa imani ya Kikatoliki, ila baadhi yake yanaweza yakavuta watu wazingatie ibada fulani ambayo kwa umbile lake inawahusu waamini wote (k.mf. ibada kwa Moyo mtakatifu wa Yesu) na Kanisa likishachunguza hoja za kutetea ibada hiyo linaweza likaihamasisha na kuiweka rasmi bila ya kudai imani kwamba ufunuo wa binafsi ulioisababisha umetoka kwa Mungu.

**TUYAONEJE MAFUNUO YA BINAFSI?**

Kwa hakika wale waliojaliwa mafunuo ya Kimungu yaliyopimwa na kutambuliwa na wenye mamlaka wanatakiwa kuinamia kwa heshima tokeo hilo la Mungu. Kanisa linapokubali mafunuo ya binafsi linataka kutamka tu kwamba hayapingani na imani na hivyo yanaweza kupendekezwa kwa waamini wayapokee kwa msingi fulani. Lakini hata katika yale yaliyokubaliwa hivyo unaweza ukajitokeza udanganyifu fulani kwa sababu watakatifu wenyewe wanaweza wakadhani kitu kilichotokea ndani mwao kimesababishwa na Roho Mtakatifu, kumbe sivyo, au wanaweza wakatafsiri vibaya ufunuo wa Kimungu, kama lilivyoeleweka vibaya neno la Yesu kuhusu urefu wa maisha ya Mt. Yohane. Uwezekano wa kudanganyika unatokana na kwamba karama ya unabii ina ngazi nyingi, kuanzia hisi tu hadi ufunuo kamili. Kama ni hisi ya kinabii tu, maana

sahihi na vilevile asili ya Kimungu ya mafunuo vinaweza vikabaki vimefichika au havieleweki; ndivyo Kayafa alivyotabiri bila ya kujitambua akisema, “Yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima” (Yoh 11:50).

Mtu aliyeangazwa kweli na Mungu kabla hajapanga la kufanya kufuatana na ufunuo huo aombe shauri la kiongozi wake au la mtu mwingine mwenye elimu na busara ambaye achunguze jambo *lenyewe* upande wa imani, wa teolojia na wa busara, hasa kwa sababu ni rahisi kudanganyika katika kutafsiri mafunuo. Dalili mojawapo ya asili ya Kimungu ya ufunuo fulani ni *unyenyekevu na usahili* ambao aliyefadhiliwa anaupokea na kumshirikisha kiongozi wake kwa maneno machache, asishikamane nao zaidi na *akimtii* kikamilifu wakili wa Kristo. Lakini kwa nadra karama ya unabii inapatikana hata katika watu wasio na sifa hizo.

Kuhusu *hamu ya mafunuo,* Mt. Yohane wa Msalaba, ambaye mara nyingi alialika wanasala watamani kwa unyenyekevu lakini pia kwa tumaini na ari kuzama katika mafumbo ya imani ili kuungana na Mungu, alilaumu kwa nguvu hamu hiyo. Alionyesha kwamba anayetamani mafunuo anampa shetani nafasi ya kumdanganya kwa udadisi huo na kwamba elekeo hilo linachafua usafi wa imani, linalemea roho, linaonyesha utovu wa unyenyekevu, linaingiza katika hatari nyingi, tena ni kumkosea heshima Yesu aliyetupatia ukamilifu wa ufunuo katika Injili. Pengine Mungu anawajalia fadhili hizo walio dhaifu bado, au wenye nguvu wanaotakiwa kutimiza utume wa pekee kati ya matatizo makubwa; lakini kuzitaka ni dhambi walau nyepesi, hata kama lengo ni jema. Zinasaidia tu zikisababisha unyenyekevu na upendo wa Mungu. Hivyo linaeleweka kosa la viongozi wasio na busara wanaowadodosa waliojaliwa njozi na mafunuo. Upotovu huo unasababisha udanganyifu, unaondoa utulivu na kusogeza mbali na unyenyekevu kutokana na *kufurahia bure njia za pekee*.

Hatimaye alisisitiza kwamba *hamu ya mafunuo inasogeza mbali na sala ya kumiminiwa,* “Inadhaniwa kwamba limetokea jambo kubwa, kwamba Mungu mwenyewe amesema: kumbe ni kitu kidogo au hakuna kitu au hata chini ya hapo. Kwa kuwa kinaweza kusaidia nini kinachokosa unyenyekevu, upendo, ufishaji, usahili mtakatifu, kimya n.k.? Kwa hiyo natamka kwamba aina hizo za udanganyifu zinazuia sana muungano na Mungu, kwa sababu mtu akizizingatia, *jambo hilo tu linatosha kumsogeza mbali sana na kilindi cha imani*… Roho Mtakatifu anaangaza akili iliyojikusanya kadiri ilivyojikusanya, na kujikusanya kikamilifu kunafanyika kwa imani… Upendo wa kumiminiwa unawiana na usafi wa roho katika imani kamili: *kadiri upendo huo ulivyo na nguvu, Roho Mtakatifu anaiangaza na kuishirikisha zawadi zake”*.

Lakini tutofautishe aina mbili za mafunuo ya binafsi:

*1) Mafunuo hasa,* yanayotufunulia siri fulani kuhusu Mungu au kazi yake, yanaweza yakaendana na udanganyifu kwa urahisi mkubwa zaidi. Bila ya shaka yeye anaweza akawafunulia watu muda uliowabakia kuishi, majaribu yatakayowapata, na mambo yatakayotokea kwa taifa au mtu fulani. Lakini shetani anaweza kuyaghushi kwa urahisi, tena kwa kuthibitisha uongo wake anatanguliza habari ambazo zinawezekana au ni nusu kweli. “Kwa jinsi yule Mwovu anavyoweza kujitwalia sura ya ukweli na kuithibitisha, karibu haiwezekani kukwepa ujanja wake tusipokataa mara” (Mt. Yohane wa Msalaba).

*2) Mafunuo upande*, yanayotufanya tuelewe zaidi kweli zipitazo maumbile zilizokwishajulikana kwa imani, yanafanana na hali ya kuzama katika mafumbo, hasa yasipoishia jambo maalumu, bali yanamhusu Mungu mwenyewe na kuchimba kwa dhati hekima, wema au uweza wake usio na mipaka. “Aina hizo za ujuzi wa juu unaotegemea upendo zinapatikana tu na mtu katika hali ya muungano na Mungu; zenyewe ndio muungano huo kwa kuwa zinatokana na fungamano maalumu la roho na umungu. Ni Mungu mwenyewe ambaye anahisiwa na kuonjwa. Bila ya shaka Mungu hahisiwi bayana na wazi kabisa kama katika utukufu, ila fungamano hilo ni hai na bora kwa ujuzi na mvuto hivi kwamba linapenya undani wa roho. Shetani hawezi kujiingiza humo na kudanganya kwa kughushi; hakuna cha kufanana nalo, hakuna cha kukaribia raha na nderemo za namna hiyo. Hizo zina ladha ya umungu na ya uzima wa milele, naye shetani hawezi kughushi mambo ya juu hivyo. Kuhusu hisi nyingine tulisema mtu aachane nazo, lakini wajibu huo unakoma mbele ya hizo zilizo matokeo ya muungano ambao tunajitahidi kufikishia roho. Yale yote tuliyowahi kuyafundisha kuhusu *kujinyima* na kujibandua kabisa *yanalenga muungano huo*, na fadhili za Kimungu zinazotokana nao ni matunda ya unyenyekevu, ya hamu ya kuteseka kwa upendo wa Mungu, kwa uvumilivu na bila ya kutarajia tuzo” (Mt. Yohane wa Msalaba).

**AINA MBALIMBALI ZA NJOZI ZIPITAZO MAUMBILE**

Mafunuo ya Kimungu yanatokea kwa namna ya njozi au ya maneno. Njozi zipitazo maumbile zinaweza kupitia hisi, ubunifu au akili.

*Njozi za kihisi au za kimwili* za Mwokozi, za Bikira na za watakatifu zinaweza zikatolewa kwa wanaoanza ili kuwabandua na malimwengu. Zikichangwa na idadi kubwa ya watu, ni dalili ya kwamba ni za nje, lakini si hakika ya kwamba zimetoka kwa Mungu. Zikiwa za mtu binafsi, ni lazima kuchunguza kwa uangalifu hali ya ndani ya mtu anayejishuhudia kuwa nazo, halafu kuendelea kwa busara kubwa. Kiongozi ataweza kutambua kama hizo ni fadhili za Mungu kwa kuzingatia zinavyolingana na mafundisho ya Kanisa na zinavyozaa matunda rohoni mwa mhusika. Huyo atapaswa kuonyesha uaminifu katika kuchuma utakatifu uliokusudiwa

na Mungu akitoa fadhili hizo.

*Njozi zinazohusisha ubunifu* zinasababishwa na Mungu au malaika katika kipawa hicho mtu akiwa ama macho ama usingizini. Mara kadhaa Mt. Yosefu alielekezwa na Mungu katika ndoto. Ingawa ni vigumu kutambua asili ya Kimungu ya ndoto, kwa kawaida tukimtafuta kwa bidii anajua kujitambulisha kwetu ama kwa hisi ya amani ya dhati ama kwa matukio yanayothibitisha ndoto. Hivyo mkosefu anaweza akaonywa katika ndoto kuhusu haja ya kuwahi kuongoka. Njozi hizo zinaweza zikapatwa na udanganyifu wa ubunifu na wa shetani. Zile zinazotoka kwa Mungu zinatambulishwa na dalili tatu: 1) tusipoweza kuzisababisha wala kuziondoa tunavyotaka, bali zinatokea ghafla na kudumu muda mfupi; 2) zikiacha rohoni amani kubwa; 3) zikizaa matunda ya uadilifu, unyenyekevu na udumifu katika kutenda mema. Njozi ya namna hiyo ikitolewa mtu akiwa macho, karibu kila mara inaendana na hali ya kutoka nje ya nafsi walau kiasi.

*Njozi zinayohusisha akili* zinaionyesha kwa hakika jambo fulani pasipo kutumia kwa wakati huo vitu vinavyofikiwa na hisi. Pengine njozi hizo *zina giza* na *si wazi,* pengine ni *angavu* na *wazi.* Zikitoka kwa Mungu zinatambulishwa na matokeo yake: amani ya ndani, furaha takatifu, unyenyekevu wa dhati, ambatano la moja kwa moja na maadili. Hata njozi bora zaidi, kwa kuwa ni za chini kuliko heri ya mbinguni, haziweki kuufikia umungu *ulivyo,* ila kwa namna fulani ya kuona kupitia mawazo ya kumiminiwa.

## 5.3. *MANENO NA MIGUSO YA KIMUNGU*

### AINA MBALIMBALI ZA MANENO YAPITAYO MAUMBILE

Maneno yapitayo maumbile ni matokeo ya wazo la Mungu yanayosikika ama katika hisi za mwili, ama katika hisi za nafsi, ama katika akili moja kwa moja.

Maneno yapitayo maumbile *yanayosikika masikioni* ni mawimbi yanayoundwa na malaika hewani. Maneno ya namna hiyo yanaweza kuwa madanganyifu sawa na njozi za kimwili, hivyo ni lazima tuyachambue kwa kanuni zilezile.

Maneno mengine yapitayo maumbile *yanahusisha ubunifu* wa mtu akiwa macho au usingizini. Yanaonekana yametoka pengine juu mbinguni, pengine ndani mwa moyo. Yanaeleweka kikamilifu ingawa hayasikiki kimwili. Hayasahauliki kwa urahisi na hasa yale yanayoleta utabiri fulani yanajichapa katika kumbukumbu. Tunayatofautisha na yale yanayotungwa na roho yetu kwa sababu hatuwezi kuyasikia tunavyotaka na kwa sababu ni maneno na matendo kwa wakati mmoja; k.mf. yakilaumu kasoro zetu, yanabadili papo hapo misimamo yetu ya ndani na kutuwezesha kukabili lolote kwa ajili ya utumishi wa Mungu: hapo ni rahisi kuyapambanua. Yakitokana na shetani, yanasababisha mabaya: mara nyingi ni rahisi kuyatambua mapema kwa sababu yanafanana na yale halisi kama kioo na almasi tu.

*Maneno yanayohusisha akili* yanasikika katika kipawa hicho moja kwa moja, bila ya kupitia hisi wala ubunifu, kama malaika wanavyoshirikishana mawazo na matakwa yao. "Ni usemi usio na maneno, ambao ndiyo lugha ya kwetu mbinguni" (Mt. Teresa wa Yesu).

### MIGUSO YA KIMUNGU

"Mara nyingi" sala ya kumiminiwa ya hali ya juu inaendana na aina nyingine ya fadhili, yaani "miguso ya Kimungu" ambayo inafanyika katika utashi na kuwa na "matokeo katika akili… inaipenyeza ndani ya Mungu kwa namna ya juu na tamu sana". Haitegemei utendaji wa roho, wala tafakuri zake, ingawa kwa njia hiyo roho inajiandaa kuipokea. Pengine ni ya dhati na ya nguvu hivi kwamba inaonekana imefanyika "katika undani wenyewe wa roho". Undani huo hauwezi kutenda, kusikia, kuhisi wala kupenda usipopitia vipawa vyake; ndiyo maana ulipewa vipawa hivyo. Katika hilo unatofautiana na Mungu ambaye peke yake katika usahili wake anatenda mwenyewe moja kwa moja asihitaji vipawa. Yeye, akiwa ndani ya roho kuliko roho yenyewe kwa sababu ndiye anayeidumisha, anaweza *kugusa* (Kiroho, si kimwili) na kusukuma toka humo undani wa vipawa hivyo hata roho itende matendo ya dhati isiyoweza kuyasababisha yenyewe. "Kukubali kwa unyenyekevu bila ya kutenda ndio msimamo unaompasa mtu; Mungu anajalia fadhili hizo kadiri ya matakwa yake, akipendelea watu wanyenyekevu waliojibandua na yote" (Mt. Yohane wa Msalaba).

## 5.4. *MADONDA MATAKATIFU NA KUDANGANYIKA*

Je, udanganyifu unaweza kusababisha mwilini madonda ya Bwana ambayo watakatifu kadhaa walijaliwa katika miguu, mikono, ubavu na paji la uso pamoja na maumivu makali yaliyokumbusha kwa namna ya pekee yale ya Yesu? Hayo yalitokea pasipo sababu ya nje na kutiririsha mara kwa mara damu isiyoharibika. Wa kwanza kujulikana ni Mt. Fransisko wa Asizi; baada yake kesi hizo ziliongezeka, lakini madonda hayo yanapatikana tu ndani ya wale wanaotoka nje ya nafsi, yakitanguliwa na kuongozana na maumivu makali ya kimwili na ya Kiroho yanayowalinganisha na Yesu msulubiwa.

### MAFUNDISHO YA MAPOKEO

A. Sempé aliandika vizuri, "Kwa umbile lake madonda halisi, yale ya watakatifu ambayo peke yake

yanazingatiwa na Kanisa, si madonda ya kawaida… maendeleo yake ni tofauti *kimsingi* na yale ya kawaida. Ili tukumbushe tu sifa zake zilizothibitishwa zaidi, tunaweza kusema madonda hayo *yanakataa matibabu yoyote na vilevile hayapatwi na uozo wowote:* hakuna tiba inayoweza kuyaponya, wala usaha unaopatikana ndani yake, ingawa mara nyingi yanakaa wazi miaka"; kumbe jeraha lolote la kawaida linasababisha usaha, hata katika hao wenye madonda matakatifu. "*Pengine madonda yanakauka ghafla kikamilifu*, kiasi kwamba ngozi ya kovu inavutika na kuwa imara kama ngozi ya jirani… ingawa inawezesha kutambua sura na ukubwa wa donda la chini yake. *Hatimaye madonda halisi yanatonatona mara kwa mara* kulingana na maadhimisho ya liturujia" au kwenye Ijumaa, pengine hata siku ambazo mhusika hakutarajia kwa kutojua mwaka huo adhimisho fulani linaangukia siku hiyo. "Je, sifa hizo si za ajabu? Hakuna kitu cha namna hiyo kinachotokea kamwe… kwa msaada wa udanganyifu katika wenye matatizo ya nafsi".

Pengine mwenye madonda matakatifu akilala chali, damu yanatiririka kutoka madonda ya miguu upande iliotiririka kutoka yale ya Kristo, kwa hiyo *kinyume cha elekeo la mvutano.* Vilevile *wingi wa damu inayotoka* haueleweki: ingawa kwa kawaida madonda matakatifu yako juujuu, mbali na mishipa mikubwa ya damu, yanabubujika kwa wingi.

Katika kueleza madonda hayo sifa hizo za pekee kisayansi zinatajwa pamoja na *nafasi za Kiroho* za tukio hilo la pekee, hasa *huruma kubwa kwa mateso ya Mwokozi.* Tuzingatie kuliko yote kwamba madonda matakatifu yanapatikana tu katika watu ambao wanatimiza *maadili kishujaa* na kupenda msalaba, wanapenya fumbo la ukombozi, mateso ya roho na ya mwili ya Kristo aliyejitoa sadaka kwa wakosefu. Ndilo jambo lisilo na uhusiano wowote na watu wenye ugonjwa wa nafsi: kwamba Msulubiwa anajichagulia watu awalinganishe naye, kwa namna inayoonekana au isiyoonekana, ili atukumbushe sisi tusiojali mateso yake makali. Kusahau jambo hilo ili kufafanua kimaumbile tu madonda hayo ni kutaka kuyazingatia mbali na sababu zake kuu. Ni kama kuzingatia kinyago upande wa ubao ambamo kimechongwa, bila ya kujali muundo wake wa sasa, lengo lake halisi na msanii aliyejiwekea lengo hilo.

Halafu, tukitaka kupima vema tendo lolote la kibinadamu, ni lazima tuzingatie kwa uangalifu nafasi zake mojamoja kadiri ya mfululizo maarufu ufuatao: *Nani, nini, wapi, kwa misaada ipi, sababu gani, namna gani na lini?* Vivyo hivyo, ili tupime vizuri maana na uzito wa tukio la pekee kama hili, ni lazima tuzingatie kwa uangalifu mambo yake yote upande wa mwili na wa roho, hasa: zile zinazohusu *lengo (sababu gani)* likionyeshwa ama mapema kwa sala au ahadi fulani, ama baadaye kwa upendo mkubwa kwa msalaba; zile zinazohusu *kitu chenyewe (nini)*, k.mf. madonda ya mwili yanasababisha pamoja na mateso makali mwilini jeraha tamu rohoni linaloweza kutokana na Mungu tu; zile zinazomhusu *mtu (nani)*, ambaye ni mnyenyekevu, mtiifu na ana upendo mkubwa; zile zinazohusu *njia (kwa misaada ipi),* ambapo hapana ujanja wala ushirikina; hatimaye zile zinazohusu *wakati na mahali (wapi na lini).* Mambo hayo yote yakilingana, tunafikia hakika fulani kuhusu asili ya Kimungu ya madonda hayo, kwamba hakuna ugonjwa unaofanya watu hao wafanane na Yesu msulubiwa.

**KUTOKA NJE YA NAFSI NA MADONDA MATAKATIFU**

Je, madonda hayo mwilini yanaweza *kusababishwa kimaumbile na huruma kubwa ipitayo maumbile* kwa mateso ya Bwana ikizidiwa na hali ya kutoka nje ya nafsi? "Upendo ni wa ajabu katika kukuza ubunifu hata ujitokeze kwa nje… Lakini kwa kweli upendo uliokuwemo ndani (ya Mt. Fransisko wa Asizi) haukuweza kutoboa mwili kwa nje. Ndiyo sababu serafi wa moto akija kusaidia alirusha miali miangavu yenye kupenya hivi hata ikasababisha kweli mwilini madonda ya nje ya Msulubiwa ambayo upendo ulikwishachapa ndani ya roho" (Mt. Fransisko wa Sales).

Wengi walikuwa na huruma kubwa ipitayo maumbile kwa mateso ya Mwokozi wasipate madonda hayo. Tunaweza kutaja watakatifu waliowahi kuzama katika mafumbo, kutoka nje ya nafsi zao na hata kuwa na jeraha la Kiroho moyoni pasipo madonda mwilini. Kati ya walioyapokea, walio wengi hawakuyatarajia wala kuyataka: Yesu mwenyewe anawapatia wale anaotaka, anapotaka na anavyotaka. Ni neema ya pekee ambayo haipo katika njia ya kawaida ya utakatifu.

**KUELEA HEWANI**

Ni tukio la mwili kuinuka juu mbali na ardhi bila ya sababu yoyote ya kueleweka, hivi kwamba unabaki hewani pasipo kutegemezwa na kitu chochote, ilivyokuwa ikimtukia Mt. Yosefu wa Copertino. Kinyume chake kuna matukio ya mwili kuwa na uzito mkubwa usio wa kawaida. Udanganyifu wa wenye matatizo ya nafsi haujawahi kusababisha mwili wao uelee hewani.

Benedikto XIV alidai kwanza tukio liwe limethibitika, ili kukwepa ujanja wowote. Halafu alionyesha kwamba tukio hilo halielezeki kisayansi kwa sababu ya elekeo la mvutano, lakini halipiti uwezo wa kuinua miili walionao malaika na shetani; kwa hiyo ni lazima kulichunguza vizuri upande wa mwili, maadili na dini lisiwe limesababishwa na ibilisi; mambo yote yakilingana tunaweza na kupaswa kuliona limesababishwa na Mungu au na malaika kwa kuijalia miili ya watakatifu utangulizi fulani wa wepesi wa miili mitukufu.

**KUANGAZA**

Pengine waliozama katika mafumbo wanapata uangavu wa pekee: mwili wao unazungukwa na nuru, hasa usoni. Tukio hilo ni la kulichunguza sawa na lile la kuelea hewani, isipoelezeka kisayansi: kama linatokea mchana au usiku; kama nuru hiyo inapita mianga mingine yote; kama tukio linadumu muda mrefu na kujirudiarudia. Pia ni lazima kulizingatia kwa makini upande wa maadili na wa dini: kama linatukia wakati wa mahubiri, wa sala, wa kutoka nje ya nafsi; kama linasababisha matokeo ya neema, k.mf. uongofu wa kudumu; kama mhusika ni mwadilifu. Ikiwa masharti hayo yote yametimia na kuthibitika, tunaweza kuliona tukio hilo la pekee kama utangulizi fulani wa uangavu wa miili mitukufu.

**KUNUKIA**

Pengine miili ya watakatifu inanukia wakiwa hai au kisha kufa. Daima waamini wameona hiyo ni ishara ya harufu nzuri ya maadili yao. Ili kuhakikisha tukio hilo linatoka kwa Mungu ni lazima tuchunguze kama harufu nzuri ni ya kudumu, kama karibu na mwili huo kuna kitu kinachoweza kuisababisha kimaumbile, na kama tukio hilo la pekee linasababisha neema fulani.

**KUFUNGA CHAKULA KWA MUDA MREFU**

Kuna watu, hasa kati ya wenye madonda matakatifu, walioishi miezi au miaka bila ya kula chochote isipokuwa ekaristi takatifu. Ni lazima tulichunguze kwanza tukio hilo kwa makini, kwa muda mrefu, pasipo nafasi katikati, kwa kutumia mashahidi wengi wenye uerevu wa kugundua udanganyifu na ujanja wowote. Ni lazima kuona kama mtu amefunga chakula chochote hata cha majimaji kwa muda mrefu na wakati huohuo anaendelea na shughuli zake. Hapo tukio halielezeki kimaumbile.

Ni vilevile kuhusu kuacha usingizi kwa muda mrefu.

Katika hayo matukio mbalimbali ya pekee, baada ya uchunguzi wa makini wa tukio lenyewe, wa nafasi zake za kimwili, za kiadili na za kidini, mwili unaonekana kutolemea roho (inavyotokea mara nyingi) bali kuwa chombo chake kinachoiacha ionyeshe uzuri wake wa ndani, uangavu wa kumiminiwa na upendo motomoto. Mara kadhaa tunapewa ishara hizo za nje ili kuonyeshwa upande wa hisi kuwa maisha kamili ya Kikristo ni utangulizi wa uzima wa milele.

## 5.5. ***TOFAUTI KATI YA MATUKIO YA KIMUNGU NA YALE YATOKANAYO NA UGONJWA***

Matukio ya pekee tuliyoyazungumzia, hasa yale yanayoendana pengine na hali ya kutoka nje ya nafsi, yamethibitishwa vizuri hivi hata wasio na imani wasiweze kuyakanusha, ingawa wanajaribu kuyafananisha na dalili fulanifulani za ugonjwa wa nafsi.

Kwa hakika watakatifu wanapatwa na maradhi kama watu wengine; suala ni kujua kama, mbali ya maradhi ya mwili, wana afya na msimamo mzuri upande wa nafsi. Utakatifu na kuzama katika mafumbo vinaweza vikaendana na maradhi ya nafsi kiasi tu, maana yale ya kudumu hayapatani na hali ya juu ya maisha ya Kiroho.

Kama walivyokwishafanya wanasaikolojia na wanateolojia wengi, tutazingatia tofauti zilizopo: 1) upande wa wahusika; 2) upande wa matukio; 3) upande wa matokeo.

**TOFAUTI UPANDE WA WAHUSIKA**

"Wagonjwa wengi wa umanyeto wana hali ya akili ya pekee inayotambulikana kwa urahisi. Tangu ututoni wenye elekeo hilo wanagundulika kwa sifa za pekee. Kwa kawaida ni wasichana wenye akili kubwa, wenye kukomaa mapema mno, wepesi kushtuka, wenye majivuno, wanaojaribu kujivutia macho ya watu, werevu katika kudanganya na kuongopa, na wanaopatwa na hofu za usiku, ndoto na majinamizi. Umanyeto ukishathibitishwa, hali ya nafsi na ya maadili ya wagonjwa hao sifa yake kuu *upande wa akili* ni *ugeugeu mkubwa mno* unaowafanya wasidumu katika lolote… hawawezi kabisa kumaliza jambo la maana. Pamoja na hayo wana elekeo la wazi la *kupinga,* la kubishana, la kuwa na mawazo ya ajabuajabu… na vilevile la *kuiga, kudanganyika na kujidanganya*. Upande wa maadili hali ni hiyohiyo: *tabia isiyotabirika*, kaidi, bunifu, geugeu kupita kiasi… undumakuwili, uongo, wepesi wa kuigiza, kudanganya na kubuni: elekeo la kutenda ghafla na wakati usiofaa maovu makubwa au matendo bora ya kushangaza; haja ya kudumu ya kujitokeza, n.k." (E. Régis). Halafu wana mawazo yasiyobanduka kwa ndani, njozi za bandia, kuchanganyikiwa na hatimaye kichaa. Hivyo tunaweza kuona ugonjwa wa nafsi unavyozidi kustawi, akili inavyozidi kushindwa kuongoza mwenendo, kumbukumbu inavyozidi kusambaratika hata kumfanya mgonjwa ajione ana pande mbili; mapema rohoni yanabaki tu mawazo machache yasiyobanduka. Pamoja na akili, utashi unapungua vilevile: miguso inakuja kutawala pamoja na ugeugeu.

Kinyume chake, akili ya wale ambao wanazama katika mafumbo na kutoka nje ya nafsi, inapanuka kwa kumjua Mungu, sifa zake na kweli za iman,i na vilevile kwa kujifahamu kwa dhati. Hao wanasema kuwa kwa

nukta chache za kuzama katika mafumbo wanajaliwa kujifunza mengi kuliko kwa kusoma vitabu vingi. Katika nafasi za namna hiyo wanapokea mwanga wa juu unaowafanya wachungulie yale yote waliyokwishayajua kama kwa muhtasari bora, hai, mwangavu, unaochochea utashi ujitahidi kutenda makuu kwa udumifu wa ajabu, bila ya kujali matatizo yasiyosemekana. Pamoja na hayo, watu hao ni wanyenyekevu na watiifu kwa matakwa ya Mungu hata katika majaribu makali. Ndani mwao tunaona fungamano na ulinganifu kati ya maadili tofauti, na juu ya yote upendo wa Mungu na wa jirani na busara vinavyowapatia amani na utulivu wa ajabu. Kinyume cha mahangaiko na ugeugeu wa wenye umanyeto, wanafanya kazi ili kutimiza jambo gumu, wakidumu kutenda mema, kujali ukweli na kutunza siri.

**TOFAUTI UPANDE WA MATUKIO**

Tofauti kati ya hali halisi ya kutoka nje ya nafsi na ile ya umanyeto ni kubwa vilevile. Ili tupate hakika ya kwamba hazifanani hata kidogo inatosha tuishuhudie hiyo ya mwisho mara moja au mbili.

*Katika matukio yaliyotokana na ugonjwa mtu anachanganyikiwa* kwa kuona mambo ambayo hayapo, au kufuata kumbukumbu au kujisimulia, kadiri ya kiwango cha ndoto. Hatua ya kwanza inafanana kidogo na tatizo la kifafa, isipokuwa kwa *kuhisi aina ya mpira* ikipanda kooni; ni hisi ya kukabwa inayosababishwa na koo kuvimba. Hatua ya pili inaleta vitendo vya fujofujo na kunyonganyonga mwili mzima. Hatua ya tatu inaleta pozi za hofu, wivu, tamaa chafu kuhusiana na taswira inayomchanganya mtu. Hatimaye huyo *anapatwa na kulia au kucheka;* ndio mwisho wa tatizo, unaofuatwa na *uchovu mkubwa.*

Kumbe, *hali halisi ya kutoka nje ya nafsi* ina utulivu wa roho iliyounganika na Mungu kwa dhati unaotokana na *neema ya kukusanyika* kwa ndani ambayo Mungu tu anaweza kujalia na inapita yale yote yanayotokana na juhudi za kujikusanya. Ni elekeo la utu mzima, roho na mwili, kwa jambo la Kimungu lililotokea katika ubunifu au katika akili. Mwisho wa hali hiyo ni kurudia ile ya kawaida kwa utulivu tu, pamoja na sikitiko la kutoona tena njozi hiyo na furaha ya Kiroho iliyotokana nayo. Tena hali hiyo, badala ya kudhoofisha mwili, inauongezea nguvu mpya.

**TOFAUTI UPANDE WA MATOKEO**

Tofauti hizo ni kubwa zaidi. Wagonjwa wa umanyeto wanaendelea kuchanganyikiwa na kuzidisha udanganyifu, uongo, unyama na uzinifu hata ugeugeu wa hisi unakuja kutawala akili na utashi moja kwa moja. Nafsi inasambaratika na fujo ya ndani inaelekea kichaa. Kinyume chake hali halisi ya kutoka nje ya nafsi ina ustawi mkubwa zaidi na zaidi wa ujuzi wa mambo ya Mungu, wa maisha ya Kiroho, wa wokovu na upotevu wa watu, pamoja na ustawi wa kudumu wa upendo kwa Mungu na wa kujitoa kwa jirani, inavyoonyeshwa na miundo ambayo wanaianzisha na mara nyingi wanaifanikisha kiasi kwamba inadumu karne na karne.

Wenye umanyeto wanatawaliwa na wazo moja tu (k.mf. lile la kujiua) kwa kupotewa na mengine yote. Kumbe wanaozama katika mafumbo wazo ambalo linatawala mengine na kuyalinganisha kikamilifu ni wazo la Mungu, la wema wake usio na mipaka kwetu, pamoja na hakika angavu na ya dhati ya kwamba inatupasa kuitikia upendo wake. Hakuna kusambaratika kwa nafsi, bali sehemu zake zinajipanga kadiri ya utaratibu wa upendo: kwanza Mungu ambaye apendwe kuliko vyote, halafu watu ambao waokolewe. Ndiyo sababu watakatifu wana kipawa cha kupanga mambo hata kibinadamu, kama walivyokiri wanasaikolojia kadhaa wasio na imani, k.mf. M. wa Montmorand, “Wana kipawa cha kupanga na cha kuongoza na wanaonekana wenye elekeo zuri upande wa uchumi. Miundo wanayoianzisha ni hai na inadumu; katika kuwaza na kuendesha mipango yao wanaonyesha busara na ushujaa”.

**KESI ZA PEKEE**

Katika maisha ya waliozama katika mafumbo tukio fulani linaweza likaleta dhana ya kuwepo umanyeto. Hapo ni lazima kuchunguza kwanza hali ya mwili na maadili ya mhusika. Kiongozi wa Kiroho anaweza (na pengine anapaswa) kushauriana na daktari. Mara nyingi uchunguzi wa makini utaleta hakika fulani, hasa ukiendana na kusali, kutojitafutia faida, na kulenga ukweli kwa nia safi.

## 5.6. *MATUKIO YA KISHETANI*

Dhuluma za shetani ni zile zote tunazoweza kuteswa naye, yaani kushawishiwa, kupatwa na kupagawa. Kuhusu hayo tukumbuke neno la teolojia linaloyaangaza yote: kwamba kazi ya shetani haivuki kamwe upande wa hisi wa roho zetu wala haiwezi kutendeka *moja kwa moja* katika akili na utashi. “Mungu tu aliweza kuelekeza akili yetu kwenye ukweli wote na utashi wetu kwenye wema wote, na hatimaye kama lengo kuu kwake mwenyewe aliye wema mkuu. Kwa hiyo yeye tu anaweza kutenda moja kwa moja katika akili yetu na utashi wetu, kadiri ya elekeo la kimaumbile ambalo mwenyewe aliliweka na analidumisha ndani ya vipawa hivyo” (Mt. Thoma wa Akwino). *Mungu tu anapenya roho.* Kwa ruhusa yake shetani anaweza akatushambulia akitenda katika ubunifu wetu, hisi zetu, vitu vya nje na mwili wetu ili kututia maovuni. Tujihadhari tusizidhishe pande mbili tofauti: ama kumhusisha shetani na yale yanayotokana na tabia mbovu ya kiburi na ya tamaa au na maradhi; ama kutokubali kamwe athari yake wala kujali yale yanayofundishwa

na Maandiko na Mapokeo matakatifu.

### KUPATWA NA SHETANI

Yeye anaweza akatenda: katika uwezo wa kuona kwa maono ya kuchukiza au ya kupendeza; katika uwezo wa kusikia kwa kusababisha kelele au kufanya yasikike maneno ya kukufuru au ya uchafu; katika uwezo wa kugusa kwa kupiga au kwa kupapasa kimapenzi. Pengine hayo hayatokei mwilini bali katika ubunifu au yanatokana na mhemuko wa mishipa ya neva.

Kazi ya moja kwa moja ya shetani katika ubunifu, kumbukumbu na maono inaweza ikasababisha taswira zisizobanduka ingawa mtu anafanya juu chini azifukuze na ambazo zinaleta hasira, chuki, pendo la hatari au fadhaiko la kukatisha tamaa. Pengine wanaodhulumiwa hivyo wanahisi kwamba ubunifu wao ni kama umefungwa na giza nene na kwamba moyo wao unalemewa na uzito unaowakandamiza. Ni utovu wa nguvu ulio tofauti na ule unaotokana na kazi ya Mungu ambaye akijalia kuzama katika mafumbo anasababisha tafakuri karibu isiwezekane. Adui yake, akitamani kwa wivu kumuiga, anajitahidi kuchepusha matokeo ya kazi hiyo, hivi kwamba katika matakaso ya Kimungu mtu anajikuta pengine kati ya utendaji wa Mungu, unaomuelekeza maisha ya Kiroho yasiyotegemea zaidi hisi, na utendaji wa adui unaomsababishia kwa namna yake utovu wa nguvu ili kumchanganya.

Ikiwa vishawishi tunavyovizungumzia ni vya ghafla, vya nguvu na vya kudumu na havielezeki kwa maradhi yoyote, inawezekana kuviona vimeathiriwa na shetani kwa namna ya pekee.

### KUPAGAWA NA SHETANI

Katika kupagawa *shetani anakaa mwilini mwa mhusika,* badala ya kutokeza tu utendaji wake toka nje inavyotukia katika kupatwa naye. Akitenda hivyo toka ndani, *hazuii tu utendaji wa hiari wa vipawa* vya mtu, bali *anasema na kutenda mwenyewe kupitia viungo vya mtu,* bila ya huyo kuweza kumzuia na kwa kawaida hata kutambua. Shetani hamkalii mtu kama roho inavyohuisha mwili wake, bali kama *mota* ambayo kupitia mwili inatenda rohoni. Anatenda moja kwa moja katika viungo vya mwili vifanye matendo ya kila aina, na kwa njia yake anatenda katika vipawa kadiri vinavyotegemea mwili kwa kutenda kazi.

Wakati wa *upeo wa hali hiyo* kwa kawaida mhusika anapotewa na hisi yoyote ya mambo yanayomtokea, kwa sababu baadaye hakumbuki lolote isipokuwa mara mojamoja. Wakati wa utulivu ni kana kwamba shetani amejiondokea, ingawa pengine yanabaki maradhi ya kudumu ambayo madaktari wanashindwa kuyatibu.

Kwa kawaida kupagawa ni *adhabu* kuliko jaribu la kutakasa, lakini katika watu waliojitoa mhanga kwa ajili ya wakosefu hali hiyo inaweza ikaendana na takaso la Kimungu la hisi au la roho.

### DALILI ZA KUPAGAWA KWELI

Ni kusema kwa lugha isiyojulikana au kumuelewa mtu anayeiongea; kuvumbua mambo ya mbali na ya siri; kuonyesha nguvu inayozidi ile ya kimaumbile ya mhusika, kulingana na umri na hali yake. Dalili hizo na nyinginezo, hasa zikipatikana nyingi kwa pamoja, zinatufanya tushuku mtu amepagawa. Kwa namna ya pekee zinashtusha ikiwa k.mf. mtu asiyejua Kilatini wala teolojia anakuja kusema Kilatini kwa ufasaha kuhusu masuala magumu ya teolojia. Dalili nyingine ya kupagawa ni mtu kukasirika na kumkufuru Mungu kwa namna ya kutisha akiguswa kwa kitu kitakatifu au akiombewa kwa sala fulani. Dalili hiyo ni wazi zaidi ikiwa anaguswa au kuombewa bila ya yeye kujua, hivi kwamba itikio hilo lisiweze kutokana na hiari yake kwa ubaya au kwa kujifanya amepagawa.

Katika umanyeto wa hali ya juu yanatokea mambo ya namna hiyo, ingawa si kiasi cha kumfanya mgonjwa atoe hoja kwa lugha asiyoijua au juu ya suala asilolielewa. Tena shetani anaweza akasababisha maradhi ya akili au matukio ya nje yanayofanana nayo; anaweza vilevile kutumia maradhi yaliyopo na kumkatisha mgonjwa tamaa.

### DAWA ZA KUPAGAWA

1) Kufanya toba na kutakasa dhamiri kwa kuungama vema. 2) Kupokea ekaristi mara nyingi kufuatana na shauri la padri mwenye busara na mwanga. Kadiri tulivyo safi na wenye toba shetani hana uwezo juu yetu, na ekaristi takatifu inatutia yule ambaye alitustahilia neema na kumshinda shetani. Hata hivyo komunyo iruhusiwe tu wakati wa utulivu. 3) Kuomba mara nyingi huruma ya Mungu kwa sala na mfungo. 4) Kukimbilia kwa tumaini jina takatifu la Yesu na kutumia kwa imani kubwa visakramenti, hasa ishara ya msalaba na maji ya baraka. 5) Hatimaye kwa ukombozi wa waliopagawa yamewekwa mazinguo kutokana na mamlaka ya kufukuza mashetani ambayo Yesu Kristo ameliachia Kanisa. Lakini mazinguo makuu yanaweza kufanywa na mapadri wale tu walioteuliwa na kupewa ruhusa maalumu na askofu wa jimbo.

### MFANO WA KUSHTUA

M.H. Maria wa Yesu Msulubiwa alipatwa na majaribu ambayo ni kati ya yale makubwa zaidi yanayoweza yakaendana na matakaso ya Kimungu: *"Ni vita vya wazi kati ya roho mbili… Mungu kadiri na jinsi*

*anavyomvuta mtu anamruhusu shetani atende dhidi yake kwa namna hiyo…* Pengine shetani anamtisha sana mtu: duniani hapa hapana teso la kufanana na hilo. Roho inaishirikisha roho hofu yake" (Mt. Yohane wa Msalaba).

# HATIMA

## MHIMILI NA UMOJA WA MAISHA YA KIROHO

Teolojia ya maisha ya Kiroho ni utekelezaji wa teolojia ya dogma na ya maadili katika kuongoza roho kuelekea muungano na Mungu ulio wa dhati zaidi na zaidi. Inategemea mafundisho kuhusu maadili ya Kikristo na vipaji vya Roho Mtakatifu, halafu inachimba taratibu na masharti ya maendeleo yake kwa lengo la kufikia ukamilifu wa Kikristo.

Kweli za msingi tulizozitafakari kwa muda mrefu ni hai na za dhati zaidi kwetu hata tukazama ndani yake. Mmojawapo ni kwamba imani, tumaini na upendo ndio mhimili wa maisha ya Kiroho. Kutotambua ukweli huo ni kosa kubwa linalothibitisha kuwa mtu haelewi Ukristo. Lakini umuhimu wake katika maisha ya Kiroho unategemea msimamo kuhusu tofauti iliyopo kati ya upande wa juhudi na upande wa mafumbo. Neno juhudi linamaanisha utekelezaji wa ufishaji, ibada na maadili: upande huo maisha ya Kiroho yanaongoza watu kupambana na dhambi na kuendelea katika uadilifu. Kumbe upande wa pili unahusu mafumbo, yaani muungano wa dhati wa roho na Mungu, matukio ya muda yanayoweza yakaendana na ngazi za muungano huo (k.mf. kutoka nje ya nafsi) na hatimaye neema za pekee (k.mf. mafunuo ya binafsi). Upande wa juhudi unatokeza hasa namna ya kibinadamu ya maadili ya Kikristo, kumbe upande wa mafumbo mara nyingi unatawaliwa wazi na namna ya Kimungu ya vipaji vya Roho Mtakatifu (ambavyo waadilifu wote wanavyo). Katika mtazamo huo, uliosahauliwa na wengi kati ya karne XVII na XX, tunaona umoja wa maisha ya Kiroho katika hatua zake tatu zilizoainishwa na mapokeo.

Inatosha kusoma vitabu vya Mt. Fransisko wa Sales kuhusu maisha ya Kiroho upande wa juhudi ili kuhakikisha alivyoyawekea mhimili wa maadili ya Kimungu. Humo alisema ufishaji wa ndani na wa nje ni njia kubwa ya kujivutia fadhili toka mbinguni, mradi ufanyike kwa upendo. Kwake malipizi makali siyo bora, kwa

kuwa ufishaji wa kawaida, ambao kila siku unapata nafasi bila ya kuzitafuta, unazaa matunda mengi zaidi na kulinganisha matakwa yetu na yale ya Mungu. Alisema ufishaji bila ya sala ni kama mwili usio na roho, na sala bila ya ufishaji ni kama roho isiyo na mwili. Alieleza ustawi wa maadili ya Kimungu si tu kinadharia bali kiutekelezaji.

Teolojia hiyo safi kuhusu juhudi, badala ya kuishia mawaidha yanayosahau ukuu wa maadili ya Kimungu, inahuishwa nayo daima na kuelekeza maisha ya juu zaidi. Hatupotoshi maisha ya Kiroho tunapoonyesha maadili ya kiutu yanavyotakiwa kutumikia imani, tumaini na upendo. Vilevile hatuyapotoshi wala hatuzidishi nafasi ya vipaji vya Roho Mtakatifu dhidi ya maadili ya Kimungu, tunapofundisha ustawi wa imani, tumaini na upendo unavyotakiwa kuwa katika hatua ya mwanga, wala tunapokumbusha maadili hayo matatu yanavyotakaswa katika usiku wa roho, wala tunapoonyesha ushujaa wa maadili hayo katika hatua ya muungano. Hatupunguzi hata kidogo nafasi ya imani tunapofafanua ngazi zake za juu kwa kusema juu ya namna ya Kimungu ya vipaji vinavyotufanya tupenye na kuonja mafumbo tuliyofunuliwa. "Sala ya kumiminiwa ni tendo ambalo kimsingi linatokana na imani hai na kwa namna yake ya Kimungu linatokana na vipaji vya hekima na akili" (Gaetano na Yosefu wa Roho Mtakatifu). Hatuwezi kuwaza tendo la vipaji hivyo lisilotokana na imani kama mzizi wake. Maadili ya Kimungu yanabaki bora kuliko vipaji, ingawa yanakamilishwa navyo, kama vile mti ulivyo bora kuliko matunda yake, lakini ukiwa nayo ni kamili kuliko usipokuwa nayo.

Mwanateolojia anapaswa kukwepa aina yoyote ya kujidai, ambayo haivumiliki ndani mwake kuliko ndani ya wengine, inaweza kuyaondolea maisha yake ya Kiroho msukumo wowote na kuyafanya yakose neema kubwa, na hata kumzuia asielewe vema watu wa sala. Anapaswa kukumbuka utaalamu aliojipatia kwa kutumia vema akili ni wa chini kuliko kipaji cha kumiminiwa cha hekima ambacho kinapima yote kwa kufuata uvuvio wa Roho Mtakatifu na kwa kulingana na mambo ya Mungu. Mt. Thoma wa Akwino alikuwa na kiwango cha juu cha aina hizo mbili za ujuzi, ambazo ukuu wa ule wa pili ulikuwa ukimzuia asijivunie wa kwanza, hata mwishoni mwa maisha yake alikuwa kama amezama ndani ya Mungu kwa sala ya kumiminiwa akawa anashindwa kuagiza makarani waandike nini. D. Banyez, aliyewahi kumuongoza Mt. Teresa wa Yesu, alisema inawafaa wanateolojia, kisha kutumia miaka katika masomo, wawasiliane na watu wenye maisha ya Kiroho, kwa sababu wasipofanya juhudi za kudumu wala kuwa na maisha ya sala ya dhati, hawawezi kutambua utajiri wa Kiroho wa masomo wanayoyafafanua. Wanaishia kwenye ganda wasifikie kiini chake: tena wako katika hatari ya kuzingatia historia au mantiki tu wakizungumzia kwa mtazamo wa chini mafumbo makuu ya Kimungu. Roho ya teolojia ina uhai mdogo kadiri tunavyoishia hapo badala ya kujiweka tayari "kuelewa mafumbo kwa faida kubwa" (Mtaguso wa I wa Vatikano) kwa mtazamo wa juu unaotawaliwa na vipaji vya akili na hekima.

Hayo yote yanathibitisha kwamba mhimili wa maisha ya Kiroho ni maadili ya Kimungu, ambayo ni bora kuliko vipaji, lakini yanakamilishwa navyo. Kwa mfumo wake imani inapita maumbile isiweze kukosa, lakini ni kamili zaidi inapopenya na kuonja mafumbo yote kwa uvuvio wa vipaji vya akili na hekima.

## HERI YA KUMUONA MUNGU NA UTANGULIZI WAKE WA KAWAIDA

Kama Mungu angetuumba katika hali ya kimaumbile tu, tukiwa na mwili wa kufa na roho isiyokufa lakini haina uhai wa Kimungu wa neema, lengo letu kuu na heri yetu vingekuwa vilevile kumjua Mungu na kumpenda kuliko vyote, kwa sababu akili yetu imeumbwa ili kujua ya kweli na hasa ukweli mkuu, na utashi wetu umeumbwa ili kupenda mema na hasa wema mkuu. Tungeumbwa hivyo, tuzo kuu la uadilifu lingekuwa kumjua na kumpenda Mungu, ila tungemjua kama *kwa nje* tu, kadiri sifa zake zinavyoonekana katika viumbe; tungemjua kwa hakika kuliko wanafalsafa bora wa zamani, tena pasipo mchanganyiko wa udanganyifu, lakini bado kwa ujuzi *wa kinadharia* kupitia vitu na mawazo yenye mipaka. Tungemjua kama asili kuu ya roho na ya miili yote, na kuorodhesha sifa zake zisizo na mipaka tulivyozijua kwa kuzingatia viumbe. Mawazo yetu juu ya sifa zake yangebaki vipande tu vya picha visivyoweza kuonyesha kikamilifu sura yake inavyopendeza. Ujuzi huo ungetuachia giza nene, hasa juu ya ulinganifu wa dhati wa sifa za Mungu. Tungepaswa kusema, Lo! Kama tungeweza *kumuona* Mungu, aliye chemchemi ya ukweli na wema wote, anayesababisha uhai wa viumbe vyote, wa akili na utashi pia.

Kumbe huruma isiyo na mipaka ya Mungu imetuitia uhai upitao maumbile ambao ukamilifu wake unaitwa si uzima ujao tu bali *uzima wa milele*. *"Uzima wa milele ndio huu: wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (Yoh 17:3). "Wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule *tutaona uso kwa uso*; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule *nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana"* (1Kor 13:12). *"Tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo*" (1Yoh 3:2). Kanisa limetamka rasmi kwamba fundisho hilo lililofunuliwa linatakiwa kueleweka ni *kuona umungu moja kwa moja,* pasipo kupitia ujuzi wa kiumbe chochote. Kwa maneno mengine, upande wa akili yetu, iliyoimarishwa Kimungu na mwanga wa utukufu, tutamuona Mungu vizuri kuliko tunavyoona kwa macho ya mwili watu tunaoongea nao, kwa sababu tutamuona wazi ndani mwetu. Hapa duniani sanasana tunamjua Mungu asivyo, kwamba hana mwili, habadiliki wala hana mipaka; lakini hapo *tutamuona alivyo* katika

umungu wake, katika udhati wake usio na mipaka, katika *maisha yake ya ndani* yanayochangwa na Nafsi tatu na ambayo neema *inatushirikisha,* kwa sababu itatuwezesha kumuona moja kwa moja kama anavyojiona, kumpenda kama anavyojipenda, kuishi milele kwa uhai wake.

*Kati yake na sisi hakutakuwa hata na wazo moja*, kwa kuwa wazo la kimaumbile haliwezi kumuonyesha Mungu wala ukweli wake usio na mipaka wala upendo wake usio na mwisho. Hatutaweza kuufafanua mtazamo huo kwa neno lolote, hata la ndani tu, kama tunavyozama kuona tamasha la ajabu lisilosemeka. Huo mtazamo wa moja kwa moja unapita wazo lolote tunaloweza kuwa nalo kuhusu sifa za Mungu. Tunaitwa tukaone *sifa hizo zote zisizo na mipaka zikilinganika kwa dhati na kuunganika katika ukuu wa umungu.* Tutaona jinsi *huruma* yenye hisani kuu na *haki* isiyopindika hata kidogo zinavyotokana na *upendo* uleule mmoja, mkarimu pasipo mipaka na mtakatifu pasipo mipaka, ule upendo wa milele wa wema mkuu ambao unaelekea kwa dhati kuenea (ndiyo asili ya huruma) lakini pia unastahili kupendwa kuliko vyote (ndiyo asili ya haki). Tutaona jinsi huruma na haki zinavyounganika katika matendo yote ya Mungu, jinsi upendo wa milele unavyolingana na *wema mkuu* unaopendwa milele, jinsi *hekima* ya Kimungu inavyolingana na *ukweli mkuu* unaojulikana milele, tena jinsi sifa hizo zote zilivyo kitu kimoja na uhai wenyewe wa Yule Aliye.

Tutaona pia *utajiri usio na mipaka* wa umungu unaojitokeza katika Nafsi tatu, uzazi wa milele wa Neno ambaye "ni mng'ao wa utukufu" wa Baba na "chapa ya nafsi yake" (Eb 1:3), na uvuvio usiosemeka wa Roho Mtakatifu aliye ukamilifu wa upendo wa Baba na Mwana unaowaunganisha milele katika kujitoa kabisa. Wema mkuu kwa mfumo wake unaelekea kuenea katika maisha ya ndani ya Mungu na kwa hiari unaeneza nje utajiri wake kwa kuumba na kwa kutuinua sisi bure hadi uzima wa neema. "Wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi" (Rom 8:29). Tangu milele Mungu anaye Mwana pekee anayemshirikisha umungu wote awe Mungu toka kwa Mungu, mwanga kwa mwanga; naye anataka kuwa na wana wa kambo anaowajalia neema inayotia utakatifu washiriki hali yake; kutokana na neema hiyo vipawa vyao vya juu vipokee mwanga wa utukufu na upendo usioweza kupotea. Tutazama pia kuona moja kwa moja muungano wa dhati usiovunjika wa Nafsi ya Neno na utu wa Mwokozi: wakati huohuo tutaona uangavu wote wa uzazi wa Kimungu wa Maria na wa ushenga wake mshiriki, thamani ya wokovu wa watu na utajiri usiopimika wa uzima wa milele wa wateule.

Hakuna anayeweza kufafanua heri itakayosababishwa na mtazamo huo wa moja kwa moja ambao utakuwa kama muungano wa kuyeyusha pamoja roho yetu na umungu, muungano unaotugeuza pasipo kikomo, ushirika wa dhati na kamili usioweza kupunguzwa na lolote. Upendo wa Mungu utakaosababishwa na mtazamo huo utakuwa na nguvu na usafi kiasi kwamba hakuna la kuweza kuupunguza; utakuwa unajibubujikia tu, si wa hiari tena, kwa kuwa utakuwa juu ya hiari, ukivutwa tu na Wema mkuu. Kwa upendo huo tutafurahi hasa kwamba Mungu ni Mungu, mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, mwenye haki na huruma zisizo na mipaka; tutaabudu maongozi yake yote yaliyolenga kudhihirisha wema wake, na tutajiweka moja kwa moja chini yake. Tutaingia katika heri yake mwenyewe, kadiri ya neno la Mwokozi: *"Ingia katika furaha ya Bwana wako"* (Math 25:21,23).

Ikiwa neema inayotutia utakatifu ndiyo mbegu ya uzima wa milele, yatokanayo ni yapi? Kwanza ni kwamba neema hiyo ya maadili na vipaji ni *bora* kuliko karama. Kama tulivyoona, kujaliwa kuzama katika mafumbo ya imani chanzo chake si hizo neema za pekee, bali ni neema ya maadili na vipaji ambayo wote wanaipokea katika ubatizo. Mtazamo huo wa kumiminiwa ni tendo la imani iliyohuishwa na upendo na iliyoangazwa na vipaji vya akili na hekima; kwa hiyo, *kwa umbile lake si fadhili ya pekee* (kama karama) bali ni sehemu ya njia ya kawaida ya utakatifu.

Ukweli huo unathibitishwa zaidi tukizingatia kwamba *neema inayotia utakatifu,* kwa kuwa *inalenga uzima wa milele kwa umbile lake,* inalenga pia *utangulizi wa moja kwa moja wa heri ya kumuona Mungu.* Utangulizi huo ndio utekelezaji bora wa imani hai iliyoangazwa na vipaji vya akili na hekima, yaani kujaliwa kuzama katika wema wa Mungu na katika uangavu wake, pamoja na upendo kamili na hamu hai ya heri ya kumuona. Hapa duniani ukamilifu wa hamu hiyo unapatikana tu katika muungano unaotugeuza. Kwa hiyo muungano huo hauko *nje* ya njia ya kawaida ya utakatifu; ndio jema ambalo Mkristo alitamani kwa moyo wake wote: kumpata Mungu milele. Ili kufikia huko, awe na ile imani ya dhati zaidi na zaidi, lile tumaini imara zaidi na zaidi na ule upendo wa Mungu ulio safi na wa nguvu zaidi na zaidi, ambavyo vinapatikana hasa katika muungano huo. Hivyo muungano unaotugeuza unadhihirika kuwa utangulizi wa moja kwa moja wa heri ya kumuona Mungu kwa roho nyenyekevu zilizotakata kikamilifu. Ni lazima kuwe na *uwiano fulani kati ya nguvu ya hamu na tuzo jema lililotamaniwa;* basi tuzo hilo halina mipaka, hivyo hatuwezi kamwe kulitamani mno. Wala haifai litolewe kwa roho isiyolitamani bado kwa nguvu. Inalitamani kadiri ilivyotakata, na ikiwa wakati wa kufa hamu yake haijawa na nguvu iliyotakiwa, inahitaji utakaso mwingine: ule wa toharani.

Utayari huo wa kuingia mbinguni mara baada ya kifo unadai *utakaso kamili* unaofanana na ule wa roho ambazo zinakaribia kutoka toharani na zina hamu hai ya Mungu. Kwa kawaida duniani utakaso huo kamili unapatikana tu katika wale waliostahimili *matakaso ya Kimungu ya hisi na roho*. Hoja hiyo inathibitisha yale yote tuliyoyasema na inadhihirisha jinsi matakaso hayo yalivyo sehemu ya njia ya kawaida ya utakatifu, kama ulivyo muungano wa dhati na Mungu ambao yanaandaa kuufikia. Inatuonyesha pia utakatifu upi

unatajwa tunaposema “njia ya kawaida ya utakatifu”: ni ule unaowezesha kuingia mbinguni mara baada ya kufa.

Bila ya shaka, ili tuelewe maana na uzito wa fundisho hilo, tunapaswa kuzingatia watu si tu *jinsi walivyo*, bali *jinsi wanavyopaswa kuwa.* Ni kazi ya teolojia ya maisha ya Kiroho kuwakumbusha mfululizo wanavyopaswa kuwa ili kupita hali waliyonayo. Mt. Paulo alipenda kusema, “Dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana” (2Kor 4:17). Naye ametuwasha hamu ya utukufu huo akitukumbusha tumeshajaliwa “arabuni ya Roho” (2Kor 5:5), yaani amana na mwonjo wa uzima wa milele. *“Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake”* (Yoh 14:21). Kristo anajidhihirisha kwa siri kwa mwamini hasa akifikia heri za juu zaidi kati ya zile nane ambazo ni utekelezaji bora wa maadili na vipaji. Humo mna *“mwanzo fulani usiokamilika wa heri ya milele tangu maisha haya katika watakatifu”* (Mt. Thoma wa Akwino). Matunda ya stahili yanaanza kuonekana tayari hapa duniani, nayo yana ladha ya uzima wa milele, ni mwonjo wa awali wa raha ya wateule.

## NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI KWA MAFUNGO MATATU YA SIKU SITA SITA

### A. KUHUSU MAENDELEO YA KIROHO

1. Lengo kuu la maisha yetu yote: heri ya mbinguni, uk. 356-359. Uzima wa neema ni mwanzo wa ule wa milele, 11-15.
2. Dhambi, mizizi yake na matokeo yake, 103-108; kilema tawala, 108-112; uzembe, 132-135.
3. Upendo wa Kristo unaotukomboa, 36-40; 201-204; 318-320.
4. Upendo kwa Mungu, 221-225; 312-313.
5. Upendo kwa jirani, 225-230; 314.
6. Ufishaji, 96-103.
7. Unyenyekevu, 197-204.
8. Ufukara, 204-207.
9. Usafi wa moyo, 194-197.
10. Utiifu mtakatifu, 207-210.
11. Msalaba na matakaso kwa jumla, 174-181.
12. Sala ya kuomba na Sala ya Kanisa, 147-152.
13. Sala ya moyo, 152-156.
14. Usikivu kwa Roho Mtakatifu, 233-242.
15. Heshima kwa Maria, 248-251.
16. Namna ya kuishi Misa kwa dhati, 242-245.
17. Komunyo takatifu, 245-248.
18. Ari kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa watu, 231-233.

### B. KUHUSU MUUNDO WA KIROHO

1. Maisha ya Kiroho, maongezi ya ndani na Mungu, 16-20.
2. Maadili ya Kimungu, 20-22. Imani, 213-217.
3. Tumaini na hakika yake, 217-221.
4. Upendo, 221-230.
5. Maadili ya kiutu, 22-24. Busara na maisha ya Kiroho, 186-188.
6. Aina mbalimbali za haki, 189-191.
7. Nguvu na subira, 191-194.
8. Usafi wa moyo, 194-197.
9. Unyenyekevu, 197-204.
10. Neema za msaada na aina zake mbalimbali, 28-32.
11. Uwemo wa Utatu Mtakatifu ndani mwetu, 32-36.
12. Vipaji vya Roho Mtakatifu na usikivu kwake, 24-28; 233-242.
13. Kristo mkombozi anavyoathiri Mwili wake wa fumbo, 36-40.
14. Msaada wa Maria, mgawaji wa neema, 40-43.
15. Ustawi wa uzima wa neema kwa njia ya stahili, sala na sakramenti, 44-48.
16. Sakramenti ya kitubio, 135-139.
17. Kushiriki Misa, chemchemi ya utakatifu, 139-142; 242-245.
18. Komunyo takatifu, 142-147; 245-248.

### C. KUHUSU UKAMILIFU WA KIKRISTO

1. Umbile halisi la ukamilifu wa Kikristo, 48-55.
2. Ukuu wa ukamilifu wa Kikristo na heri nane, 55-59.
3. Ukamilifu wa Kikristo na amri ya upendo, 67-70.
4. Ukamilifu wa Kikristo na mashauri ya Kiinjili, 70-73.
5. Wajibu wa pekee wa padri na wa mtawa wa kulenga ukamilifu, 73-77.
6. Hatua tatu za maisha ya Kiroho, 78-85.
7. Hatua ya wanaoanza, 93-96.
8. Utakaso wa hisi na wa ubunifu, 114-117.
9. Utakaso wa akili na wa utashi, 120-128.

10. Wachelewaji, 159-162.
11. Hatua ya wanaoendelea, 182-186.
12. Upambanuzi wa roho, 239-242.
13. Sadaka ya Misa na wanaoendelea, 242-245.
14. Komunyo ya wanaoendelea, 245-248.
15. Kitabu cha “Kumfuasa Yesu Kristo” kinawaelekeza wote njia ya mafumbo, 251-253.
16. Misalaba ya hisi na ya roho, 174-181.
17. Hatua ya waliokamilika, 296-301.
18. Heri ya kumuona Mungu na utangulizi wake wa kawaida, 356-359.